# MISINGI YA BIBLIA

Bible Basics: Kiswahili
KITABU CHENYE MAFUNZO
KINACHOFUNUA FURAHA NA
AMANI KWA UKRISTO ULIO WA KWELI

DUNCAN HEASTER
Carelinks, PO Box 152 Menai NSW 2234 AUSTRALIA
www.carelinks.net

## DIBAJI

Watu wote ambao wamekubali kuwa Mungu yupo, na kwamba Biblia ni ufunuo wake kwa mwanadamu, Kwa kusema kweli wanahitaji wao wenyewe watafute ujumbe wamsingi uliomo katika Biblia. Wengi wanao jiita ni 'Wakristo' wanazembea kwenye kazi hii, kwani, husoma mistari michache toka Agano Jipya siku za Jumapili wengine huwa na Biblia mahali fulani majumbani mwao ambamo kamwe haifunguliwi, Kwa uwazi hawaoni na kukumbuka habari nyingi zilizo kwa wingi katika Biblia. Ajabu ndogo ni kwamba kwa tabia hii dhidi ya Mungu kwa neno lake la kwanza , Kumekuwepo na mtafaruku mno usiotegemewa katika maisha na mioyo ya wengi

Kwa upande mwingine, wapo wale ambao wana malezi kidogo ya kikristo ambao huamua kujaribu kuufikiria ujumbe wa Biblia, lakini wanakuta kwamba kila mtu wanae mkaribia hujaribu kuwapa furushi lilojaa tele mafunzo ya elimu ya mwanadamu inayodumisha mapokeo ya imani kwenye dini ya Kikristo isiyoleta sifa ya maneno ya Biblia.

Ni lengo la kitabu 'Misingi ya Biblia' kuchambua ujumbe wa Biblia kwa makini kwa njia ya taratibu. Kimepangwa kusomwa moja kwa moja kama kitabu , au kwa shauri la pili kinaweza kutumika kama kuandikiana masomo ya kumfunza mtu mwingine . Majibu ya maswali yaliyomo mwishoni mwa kila somo yaweza kutumwa kwa kufuata anuani utakayo pewa chini , Kisha majibu yako yatapelekwa kwa mfunzi wako ambae wakati huo ataweza kuwasiliana nawe kwa kadri unavyosonga mbele na masomo hayo. Inafahamika ya kwamba wasomaji wengine watakuwa wenye soni kutokana na wazo la kujibu maswali , lakini badala yake watauliza maswali yahusuyo maeneo ambayo hawajayaelewa au hawakubaliani na tafsiri iliyotolewa hapa . Basi, ikiwa kutumiana barua huku kunaelekezwa kufuata anuani hiyo hapo chini, Majibu yako unaweza kupewa.

Ni nia ya mbuni kitabu ya kwamba ujumbe wa msingi wa Biblia hudhihirika wazi . Ingawa hivyo, daima yatakuwepo mafungu mengine ya maneno au habari ambayo inaweza kuonekana kijuu juu kutofautiana na jambo zima la maandiko. Baadhi ya haya, pamoja na maelekezo mengine ya Injili yanaweza kuwavutia wasomaji wengine pekee , yamejadiliwa katika sehemu iitwayo 'Acha kwa kitambo habari inayoandikwa' itawezekana kuelewa ujumbe wa msingi wa Biblia pasipo kusoma sehemu ya tumeacha kwa kitambo yaliyoandikwa, lakini inatazamiwa kuwa wanafunzi wengi watasoma yote. Kwa ujumbe tafsiri iliyotumika katika masomo haya ni kutoka Union Version - Biblia ya kiswahili. Lakini kukiwepo kutokueleweka vizuri katika tafsiri, basi tuna nukuu kuto tolea lingine la Biblia . Lipo toleo lingine la Biblia iitwayo ya kisasa hii ni kwa ajiri ya kuelewesha vema somo - hii ni 'Biblia Habari Njema .' kwa Kiswahili.

Wapo watu wengi ambao inabidi kuwashukuru kwa msaada wao katika kukitengeneza kitabu hiki, hasa nawiwa na Clive Rivers kwa uhodari mfululizo wa kutoa picha na wale waliofafanua juu ya maandiko lakini, kuwiwa kwangu kikubwa kupo kwa mamia ya watu walio Africa, West Indies, Ufilipino na Ulaya Mashariki na wenye maswali ya upekuzi na kiu ya kujua ukweli wamenishurutisha kuona hata mwisho kwenye misingi hii ya Biblia mara kwa mara. Ubora wake na nguvu pekee vinaongezeka na kwa kutazama kutoka kona nyingi tofati tofauti. Kwenye mkusanyiko wa taxi, kwenye magari makubwa yaliyo wazi, kwenye vyumba vya mkutano tulivu hadi kwenye hoteli zenye roshani zisizo na raha shauri ya joto na vijijini. Masuala haya yamejadiliwa, kubishaniwa na wanafunzi wengine wameonyesha shauku katika Biblia kutoka kwenye nyendo zote za maisha. Ndugu zangu wakristadelfiani ambao nilibahatika kufanya nao katika kazi hii wamekuwa ndio chanzo cha msaada na kunitia moyo. Sehemu muhimu nyingi zinazoitwa Kuacha kwa kitambo kile kinachozungumuziwa katika kitabu hiki mara nyingi karatasi zilichanwa katikati yetu kwenye vyumba vya hoteli, baada ya balaza lenye majadiliano makali na kundi la wanafunzi wanaopokea masomo. Ushirika na urafiki unaokuja kwa kufungamana pamoja katika mafunzo haya ya msingi iliyo ya Biblia ya

kweli ni hakika hauna kifani katika maarifa ya mwanadamu. Basi kwa yote hayo "Wafanyakazi wenzangu katika ufalme wa Mungu" nataja sifa nikitumaini kwamba watakuta kitabu hiki ni msaada katika kazi kubwa ya kuchapisha Injili ya kweli "kwa mataifa yote."

Kushika ukweli halisi wa injili kama ulivyofundishwa katika kurasa za Biblia kutabadilisha kila sehemu za maisha yetu, kuwaongoza wanaume na wanawake na ulimwengu zaidi, hasa kutoa utukufu wa Mungu kama alivyokusudia , pande zote mbili sasa na hata milele. Kila mtu anayepata ukweli anakuwa amepata 'Lulu ya thamani kubwa' atajua mawazo ya Yeremia kwa ajili yake mwenyewe.

"Maneno yako yalionekana, nami nikayala ; na maneno yako yalikuwa furaha kwangu, na shangwe ya moyo wangu" (Yer. 15:16). Ili kufaulu katika suala hili, hakikisha unaomba msaada wa Mungu uelewe neno kabla ya kushughulika na masomo haya . "Basi sasa nawaweka katika mikono ya Mungu , na kwa neno la neema yake, ambalo laweza kuwajenga na kuwapa urithi pamoja nao wote waliotakaswa" (Matendo 20:32).

*Duncan Heaster dh@heaster.org*

## VIFUPISHO VILIVYOTUMIKA KATIKA MASOMO HAYA KWA VITABU VYA BIBLIA

Mwa. - Mwanzo Yer. - Yeremia Rum. - Warumi
Kut. - Kutoka Eze. - Ezekieli 1 Kor. - 1 Wakorintho
Law. - Walawi Dan .- Danieli 2 Kor. - 2 Wakorintho
Hes - Hesabu Hos .- Hosea Efe. - Waefeso
Kum.- Kumbukumbu la Torati Amo. - Amos Flp .- Wafilipi
Yos. - Yoshua Mik .- Mika Kol .- Wakolosai
Amu. - Waamuzi Nah .- Nahumu 1 The. - 1 Wathesalonike
1 Sam.- 1 Samueli Hab .- Habakuki 2 The. - 2 Wathesalonike
2 Sam. -2 Samueli Sef .- Sefania 1 Tim .- 1 Timotheo
1 Nya .- 1 Mambo ya nyakati Hag .- Hagai 2 Tim. - 2 Timetheo
2 Nya .- 2 Mambo ya nyakati Zek .- Zekaria Tit. - Tito
Neh. - Nehemia Mal. - Malaki Ebr . - Waebrania
Zab. - Zaburi Mt. - Mathayo 1 Pet. - 1 Petro
Mit. - Mithali Mk. - Marko 2 Pet. - 2 Petro
Muh. - Mhubiri Lk. - Luka 1 Yoh.- 1 Yohana
Isa .- Isaya Yn. - Yohana 2 Yoh.- 2 Yohana
Ufu. - Ufunuo

Maswali yaliyo mwisho mwa kila somo ni ya aina mbili: Uchaguzi wenye sehemu nyingi (ambapo inakupasa uchague jibu moja kati ya majibu yaliyoorodheshwa ikiwa ni jibu sahihi kwa swali lililoulizwa.) Na maswali ya kawaida yanayohitaji sentensi chache kwa majibu. Andika majibu yako kwenye kipande cha karatasi tofauti , Usisahau kuandika jina lako na Anuani inayosomeka kwa uwazi. Tuma majibu yako kwa anuani hii hapa chini

**Bible Basics, P.O.Box 3034, South Croydon SURREY CR2 0ZA ENGLAND**
**Email: info@carelinks.net**

# MISINGI YA BIBLIA

**Sehemu ya 1:**

**"Mambo yanayohusu ufalme wa Mungu"**

**SOMO LA 1 :Mungu**

1.1 Uwepo wa Mungu
1.2 Nafsi yake Mungu
1.3 Jina la Mungu na tabia ya sifa yake
1.4 Malaika
Tumeacha Kitambo sehemu ya 1: 'Mungu ni roho'
Tumeacha Kitambo sehemu ya 2: 'Matumizi ya jina la Mungu'
Tumeacha Kitambo sehemu ya 3: 'Ufunuo wa Mungu'

**SOMO LA 2: Roho Ya Mungu**

2.1 Ufafanuzi
2.2 Maongozi ya Mungu
2.3 Vipawa vya roho Mtakatifu
2.4 Kurudishwa kwa vipawa
2.5 Biblia ni Mamlaka pekee
Tumeacha kitambo tulichoandika sehemu ya 4 : "Roho Mtakatifu ni mtu ?
Tumeacha kitambo sehemu ya 5 : "Mtindo wa kuita kitu kana kwamba ni mtu"
Tumeacha kitambo sehemu ya 6 : "Mafundisho ya Kelvin
Tumeacha kitambo sehemu ya 7 : "Nanyi mtapokea Roho mtakatifu"

Tumeacha kitambo sehemu ya 8 : “ Na ishara hizi zitafuata“

**SOMO LA 3: Ahadi za Mungu**

3.1 Dibaji
3.2 Ahadi katika Edeni
3.3 Ahadi kwa Nuhu
3.4 Ahadi kwa Abrahamu
3.5 Ahadi kwa Daudi

Tumeacha kitambo sehemu ya 9: Kuharibiwa kwa mbingu na Nchi

Tumeacha kitambo sehemu ya 10: Madai ya Uisraeli wa visiwa vya Uingereza.

**SOMO LA 4: Mungu na mauti**

4.1 Binadamu
4.2 Nafsi au Roho
4.3 Roho ya Mtu
4.4 Mauti ni Kutokuwa na Fahamu Kabisa
4.5 Ufufuo
4.6 Hukumu
4.7 Mahali pa kupewa thawabu : Mbinguni au Duniani ?
4.8 Uwajibikaji mbele za Mungu
4.9 Kuzimu

Tumeacha kitambo sehemu ya 11: Purgatory

Tumeacha kitambo sehemu ya 12: Roho na mafunzo ya kuwa huingia kwenye mwili mwingine

Tumeacha kitambo sehemu ya 13: Kwa mwili upi tunafufuliwa

Tumeacha kitambo sehemu ya 14: Kunyakuliwa

**SOMO LA 5: Ufalme wa Mungu**

5.1 Kuelezea wazi kabisa Kuhusu Ufalme
5.2 Kwa Sasa Ufalme Haujasimikwa
5.3 Ufalme wa Mungu uliopita
5.4 Ufalme wa Mungu wakati ujao
5.5 Miaka Elfu
Tumeacha kitambo sehemu ya 15: Ufalme wenyewe
Tumeacha kitambo sehemu ya 16: Maelezo mafupi ya Historia ya Israeli

**SOMO LA 6: Mungu na Ubaya**

6.1 Mungu na Ubaya
6.2 Ibilisi na Shetani
6.3 Mapepo
Tumeacha kitambo sehemu ya 17: Uchawi
Tumeacha kitambo sehemu ya 18: Edeni palitokea nini ?
Tumeacha kitambo sehemu ya 19: Lusifa
Tumeacha kitambo sehemu ya 20: Majaribu ya Yesu
Tumeacha kitambo sehemu ya 21: Vita Mbinguni

**Sehemu ya 2:**

**“Mambo yanayohusu……Jina la Yesu Kristo” ( Matendo 8: 12)**

**SOMO LA 7: Mwanzo wa Yesu**

7.1 Unabii unaomhusu Yesu kwenye Agano la Kale
7.2 Kuzaliwa na Bikira

7.3 Nafasi ya Kristo katika Mpango wa Mungu
7.4 “Hapo mwanzo kulikuwako neno”
Tumeacha kitambo sehemu ya 22: Yesu wa Historia
Tumeacha kitambo sehemu ya 23: Nimeshuka kutoka Mbinguni
Tumeacha kitambo sehemu ya 24: Je ? Yesu aliumba Dunia
Tumeacha kitambo sehemu ya 25: “ Kabla ya Ibrahimu, Nalikuwepo”
Tumeacha kitambo sehemu ya 26: Melkizedeki

**SOMO LA 8: Asili ya Yesu**

8.1 Dibaji
8.2 Tofauti zilizopo kati ya Mungu na Yesu
8.3 Asili ya Yesu
8.4 Ubinadamu wa Yesu
8.5 Uhusiano wa Mungu na Yesu
Tumeacha kitambo sehemu ya 27: “Akiwa Yuna na namna ya Mungu”

**SOMO LA 9: Kazi ya Yesu**

9.1 Ushindi wa Yesu
9.2 Damu ya Yesu
9.3 Kutoa Dhabihu Kwa Ajili Yetu Na Kwa Ajili YaNafsi Yake Mwenyewe
9.4 Yesu ni mwakilishi wetu
9.5 Yesu na Torati na Musa
9.6 Sabato
Tumeacha kitambo sehemu ya 28: Sanamu ndogo ya Yesu Msalabani

Tumeacha kitambo sehemu ya 29: Je? Yesu alizaliwa December 25?

**SOMO LA 10 : Kubatizwa Katika Jina La Yesu**

10.1 Maana Muhimu Sana Ya Ubatizo
10.2 Tubatizwe jinsi gani ?
10.3 Maana ya Ubatizo
10.4 Ubatizo na Wokovu
Tumeacha kitambo sehemu ya 30: Kubatizwa tena
Tumeacha kitambo sehemu ya 31: Kiwango cha elimu itakiwayo kabla ya kubatizwa
Tumeacha kitambo sehemu ya 32: Mnyang'anyi Msalabani
Tumeacha kitambo sehemu ya 33: Mfano wa huduma ya Ubatizo

**SOMO LA 11 : Maisha Katika Kristo**

11.1 Dibaji
11.2 Utakatifu
11.3 Maisha ya kikristo yenye Matendo
11.4 Ndoa
11.5 Ushirika

**MWISHONI MWA KITABU 1:** Maelezo Mafupi Ya Msingi Wa Mafunzo Ya Biblia
**MWISHONI MWA KITABU 2:** Tabia Yetu Kujifunza Biblia
**MWISHONI MWA KITABU 3:** Kristo Amekaribia Kurudi.
**MWISHONI MWA KITABU 4:** Haki ya Mungu

# SOMO LA 1
# MUNGU

## 1.1 Uwepo wa Mungu

"Mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kuwa yeye yupo na kwamba huwapa dhawabu wale wamtafutao" ( Ebr 11:6). Lengo la masomo haya ni kuwasaidia wale wanomwendea Mungu, wakiisha mwamini "Kwamba yupo"; kwa sababu hii hatutajitia kwenye ushahidi usiothibitisha imani ya kuwa Mungu hayuko.katika kupima muundo wa miili yetu (Zab 139:14) Ushahidi wa kielelezo katika ua, Kukazia macho juu kwenye anga pana wakati wa usiku kukiwa wazi bila mawingu, haya na mengine yasiyohesabika, Mawazo ya kangaliifu juu ya maisha, hakika yanafanya imani ya kutosadiki kuwa Mungu hayupo iwe ni ya kushangaza. Kusadiki kuwa Mungu hayuko hakika inahitajika imani zaidi kuliko kuamini yupo,pasipokuwepo Mungu mpangilio haupo, Kusudi au kutoa maelezo ya asili ya Ulimwenguni basi hii itafikiriwa katika maisha ya mtu asiyeamini kuwa Mungu yupo. Tukikumbuka hili, siyo ajabu kuwa watu wengi wanakiri kwa kiwango fulani cha kumwamini kuwa Mungu yupo hata katika jamii ambayo vitu vya mwili ni Mungu anayeshinda maisha ya watu.

Lakini ipo tofauti pana kati ya kuwa na fikra isiyodhahiri ya kwamba ipo nguvu ya juu, na hasa kweli kuwa na uhakika kwa kile ambacho Mungu anampa mtu anayemtumikia kwa ***Uaminifu. Waebrania 11:6*** jambo hili tunasoma;

> ***"Yatupasa tuamini kuwa (Mungu )yupo na Kwamba huwapa thawabu wale wamtafutao kwa bidii"***

Maelezo mengi ya biblia ni historia ya watu wa Mungu Israeli; mara kwa mara neno limetolewa kwamba kukubali kwao kuwa Mungu yupo hakukulingana na imani zao kwa ahadi zake.Waliambiwa na mkubwa kiongozi wao Musa'Kwa hiyo ujue…….Ukaweke moyoni mwako, ya kuwa BWANA ndiye Mungu katika mbingu juu, na katika nchi chini, hapana mwingine. Basi, zishike sheria zake, na amri zake (Kum. 4:39:40).

Neno hili hili limetolewa - ufahamu wetu katikati yetu ya kuwa Mungu yupo hakumaanishi kwamba tunakubalika mbele za Mungu bila kufikiri.Ikiwa bila mchezo tunakubali kwamba kwa kweli tunaye Muumba,'Kwa sababu hiyo tuzishike sheria na amri zake' Ni shabaha ya mfululizo huu wa masomo kuelezea amri hizi jinsi zilivyo na namna ya kuzishika. Tunapochungunza maandiko kwa kufanya hivi, tutakuta kwamba imani yetu kuwa Mungu yupo inatiwa nguvu.

'Imani chanzo chake ni kusikia, na kusikia huja kwa neno la Mungu' (Rum 10:17). Vile vile,(Isaya 43:9-12) yaonyesha namna ya kufahamu unabii wa Mungu kuhusu wakati ujao - Unabii unatufanya tujue'kuwa mimi ndiye' (Isa. 43:13)- yaani hilo jina la Mungu, 'Mimi niko ambaye NIKO' kwa ukamilifu ni kweli (Kut. 3:14.) Mtume Paulo alifika kwenye mji unaoitwa Beroya, eneo hili kwa sasa liko kaskazini mwa Uyunani ( Ugiriki) kama kawaida,

akahubiri injili (Habari njema) ya Mungu; lakini badala ya watu kusikia neno la Paulo alilokuwa anasema, tunasoma kwamba, " Walilipokea kwa kusikia neno (la Mungu, sio la Paulo) kwa uelekevu wa moyo, wakayachunguza maandiko kila siku, waone kwamba mambo hayo ndivyo yalivyo. Basi watu wengi miongoni mwao wakaamini ( mdo 17:11,12)

Imani yao ilikuja kwa kuwa mioyo yao ilikuwa wazi, sawa sawa (' Kila siku') na kwa utaratibu wa ('mambo hayo') waliyachunguza katika Biblia, Basi kupata imani ya kweli haikuwa Mungu aliwafanya wawe nayo ghafla kwa aina fulani ya upasuaji wa moyo wa kiroho, pasipo kujihusisha na neno la Mungu. Ni jinsi gani basi watu wa Ulimwengu wanaweza kufuata kwa moyo pigano juu ya maovu la Bill Graham au uamsho wa mikutano ya wapentekoste kisha wanahama tena kama'Waamini' ? Ni muda gani wameendelea katika masuala haya wakiwa wanachunguza maandiko kila siku ? Kwa kweli kukosekana huku kwa imani ambayo msingi wake upo kwenye Biblia bila shaka kunaonyesha utupu wa'Waongofu' hawa na kujikuta baadae kwa wanayopata Wakristo, na ni kwa sababu gani wengi wanaondoka kutoka kwenye Ushirika wa Madhehebu ya wa-Injilisti.

Masomo haya lengo lake ni kukupa mjengo wa utaratibu wako mwenyewe kuchunguza maandiko, ili kwamba nawe pia uweze basi kuamini muunganiko kati ya kusikia Injili ya kweli na kuwa na imani ya kweli mara nyingi kumejitokeza wazi katika taarifa ya kuhubiri injili.

- "Wakorintho wengi waliposikia waliamini wakabatizwa" (mdo 18:8)
- Watu wasikie neno la Injili, waamini ( mdo 15:7)
- Ndivyo tuhubirivyo, na ndivyo mlivyoamini'(1 Kor. 15:11)

• ‘Mbegu’ Kwenye mfano wa mpanzi ni neno la Mungu (Luka 8:11) wakati katika huo wa mti wa haradali ni imani ( Luka 17:6) kwa kuona kwamba imani huja kutokana na kupokea'Neno kwa imani’ ( Rum 10:8) “Maneno ya imani, na mafundisho mazuri” ( 1Tim 4:6), katika moyo ambao upo wazi kumwamini Mungu na neno lake (Gal 2:2, Ebr 4:2)

• Mtume Yohana anaisema taarifa iliyoandikwa ya maisha ya Bwana kuwa anasema' kweli ( Yaani ukweli) ili nanyi mpate kusadiki’ ( Yohana 19:35).Basi neno la Mungu limeitwa ‘Kweli’(Yoh:17:17) ili mpate kuamini.

## 1.2 Nafsi yake Mungu

Ni mwenye enzi, Mungu aliyeandikwa katika Biblia na kwamba ni kweli, mtu wa kugusika, naye yupo katika umbo. Vilevile ni mafunzo ya kwanza ya Ukristo kuwa Yesu ni mwana wa Mungu. Ikiwa Mungu hana umbo , basi haiwezekani yeye kuwa na mwana ambaye alikuwa ni 'Chapa ya nafsi yake' (Ebr 1:3) Tena inakuwa vigumu kuendeleza maisha ya uhusiano wake na mungu ikiwa Mungu ni wazo lililo kwenye akili zetu, Mkusanyiko wa roho mahali popote juu katika anga lisilo na kitu. Ni huzuni kusikia kwamba dini za watu wengi zina wazo lisilo la kweli lisilotambulika kuhusu Mungu. Yeye akiwa mkubwa mno kuliko sisi, inaeleweka ya kwamba imani ya watu wengi imeweka kikwazo kwenye ahadi dhahiri kuwa mwishowe tutamwona Mungu. Israeli walikosa imani ya kumwona Mungu alivyo (Yoh. 5:37) ni dhahiri ana umbo halisi, Imani hii huja kutokana na kumjua Mungu kwa kuamini neno lake

Heri walio safi wa moyo, Maana watamwona Mungu (Math 5:8)

Na watumwa wake (Mungu) watamtumikia, nao watamwona uso wake, na jina lake(Jina la Mungu ) litakuwa katika vipaji vya nyuso zao (Uf 22:3-4)

Tumaini hili la ajabu kama kweli tunaliamini litaonyesha matokeo ya matendo kwenye maisha yetu:

- Tafuteni kwa bidii kuwa na amani na watu wote na huo utakatifu, ambao hakuna mtu atakaye mwona Bwana asipokuwa nao (Ebr 12:14)
- Tusiape, kwa kuwa aapaye kwa mbingu, Huapa kwa kiti cha Mungu na kwa yeye na kwa yeye aketiye juu yake ( Math 23:22) hii itakuwa haina maana ikiwa Mungu sio mtu mwenye mwili.
- Tutamwona kama alivyo (akidhihirika katika kristo ) na kila mwenye matumaini haya katika yeye hujitakasa, kama yeye alivyo mtakatifu (1 Yoh 3:2,3)

Katika maisha yetu haya kumfahamu Mungu wetu wa mbinguni, hakujakamilika sana. Tunaweza kutazama mbele, kupitia giza linalotatanisha la maisha haya hadi mwisho wa kukutana naye. Kumwona kwa macho yetu hapana shaka kutakuwa sawa na kumfahamu kwa akili zaidi. Kutoka vina vya masumbufu ya mwanadamu. Ayubu aliweza kufurahia uhusiano wake wote na Mungu ambao utimilifu wake atauona mwisho wa siku.

Na baada ya ngozi yangu kuharibiwa hivi (Yaani katika mauti),Lakini pasipokuwana mwili wangu (Yaani pasipo mwili unaoharibika ) nitamwona Mungu;Nami nitamwona mimi nafsi yangu,na macho yangu yatamtazama, wala si mwingine (Ayubu

19:26,27). Mtume Paulo aliyatazamia maisha mengine yasiyo machungu yasiyo na msukosuko: “Maana wakati wa sasa tunaona kwa kioo kwa jinsi ya fumbo; Wakati ule tutaona uso kwa uso” ( 1Kor 13:12)

## USHAHIDI WA AGANO LA KALE

Ahadi hizi zilizo katika Agano Jipya zimejengwa juu kwenye ushahidi wa mambo yake makubwa ya Agano la kale, Kuwa ni Mungu aliye na mwili. Ushahidi hauwezi kukaza zaidi lakini ni mwanzo wa kukubali hali ya Mungu kama tunataka kuwa na ufahamu wa kweli yoyote kuhusu dini ambayo msingi wake upo kwenye Biblia. Agano la Kale lina mazungumuzo ya Mungu kuwa ni mtu na mtu uhusiano wa mtu na mtu pamoja Mungu, ambao Agano la Kale na Jipya linausema ni wa pekee kwa tumaini la Ukristo wa kweli. Yafuatayo ni majadiliano ya nguvu kwa ajili yake, Mungu aliye na mwili.

“Mungu akasema, Na tufanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu” (Mwa. 1:26) Hivyo mtu amefanywa kwa mfano na sura ya Mungu, Kama ilivyodhihirika kupitia Malaika. Yakobo 3:9 anasema … Wanadamu waliofanywa kwa mfano wa Mungu. Maneno haya hayatumiki kutaja mfano wa akili ya mwanadamu, kwa kuwa hali ya fikra zetu zipo mbali kabisa toka zake Mungu na katika njia nyingi kwa kikubwa zimepingana na haki yake.”Maana mawazo yangu si mawazo yenu, wala njia zenu si njia zangu, asema Bwana. Kwa maana kama vile mbingu zilivyo juu sana kuliko nchi, kadhalika njia zangu zi juu sana kuliko njia zenu, na mawazo yangu kuliko mawazo yenu” ( Isa 55:8 - 9 ). Kwa hiyo mfano na sura, tunavyoshirikiana naye Mungu, inabidi uwe ni mfano wa mwili- Lakini yeye hana wa dhambi.

Popote Malaika walipoonekana duniani wamesemwa kuwa wana umbo la watu, kwa mfano, Abrahamu aliwakaribisha malaika bila kujua, akizania kuwa walikuwa watu wa kawaida. Sisi jinsi tulivyoumbwa kwa mfano wa Mungu kwa kweli maana yake ni kwamba tunaweza kufahamu jambo lingine kuhusu mtu halisi, ndivyo tulivyo, lakini tunafanana. Basi, Mungu tunaye mshabihi siyo mtu mwingine asiyedhahiri ambaye hatuwezi kumfikiria.

“Wao wenyewe Malaika wanafanana na Mungu. Hivyo Mungu aliweza kumsema Musa, “Kwake nitanena mdomo kwa mdomo, maana wazi wazi wala si kwa mafumbo. Na umbo la Bwana yeye ataliona” (Hesabu 12:8) Haya yalikuwa yanamtaja Musa, akifunzwa na Malaika aliye kuwa na jina la Bwana (Kut. 23:20:21) Ikiwa Malaika alikuwa na umbo la Bwana, Inaonyesha kuwa Mungu amefanana na Malaika Yaani - Kimwili ana umbo la Mwanadamu. “BWANA alisema na Musa uso kwa uso kama vile mtu asemavyo na rafiki yake. (Kut. 33:11: Kum. 34:10 ). Bwana alijidhihirisha katika Malaika wake, ambaye uso na kinywa alifanana na Bwana mwenyewe.

“Kwa maana yeye anatujua umbo letu, (Zab. 103:14).Ana tutaka yeye, tumfikirie kuwa ni mtu, Baba ambaye tunaweza kuunganishwa naye.Huyu ataelezwa kwa ushahidi mwingi wa mikono ya Mungu, Viganja,Macho n.k. Ikiwa Mungu alikuwa ni furushi la Nafsi mahali fulani katika mbingu, ambazo inabidi ziwe Mungu, ni wazo letu kama tukitaka utu wake; basi ushahidi huu unatupotosha kukuza kusudi lolote.

“Maelezo ya sehemu ya makao ya Mungu, Wazi wazi yanaonyesha kwamba “Mungu” ana mahali pake; “Mungu yuko Mbinguni”( Mhubiri 5:2);Maana ametazama toka patakatifu pake pa juu, toka mbinguni BWANA ameiangalia nchi (Zab 102:19,20);

“Usikie huko mbinguni, Makao yako” (1Fal. 8:39). Lakini kwa kupambanua zaidi kuliko hivi tunasoma kwamba Mungu ana “Kiti cha Enzi” (2 Nya. 9:8, Zab 11:4; Isa. 6:1,66:1).Lugha kama hii ni ngumu kuitumia nafsi isiyo wazi kabisa, inayokaa katika milki ya Kimbingu. Mungu amesemwa kuwa “Ameshuka kuja chini” wakati mwenyewe anapojidhihirisha. Hapa panadokeza makao ya Mungu yaliyo mbinguni. Inakuwa vigumu kueleza wazo la udhihirisho wa Mungu bila kukubali hali ya umbo la Mungu. Isaya 45 ina ushahidi tele wa Mungu kujihusisha kwake katika mambo ya watu wake: “Mimi ni BWANA, wala hapana mwingine ….., mimi ni BWANA anayetenda haya yote …., Mimi, BWANA nimeiumba Ole wake ashindanaye na Muumba wake … Mimi, naam, mikono yangu mimi, imezitanda mbingu …, niangalieni mimi mkaokolewe, enyi ncha zote za dunia. mstari hasa kweli huu wa mwisho unaonyesha uwepo wake Mungu - Anawataka watu wamwangalie yeye, Kuwaza uwepo wake halisi pamoja na jicho la imani.

Mungu amejifunua kwetu akiwa ni mwenye kusamehe anayesema, maneno kwa watu. Hata hivyo msamaha na usemi unaweza tu kutoka kwa mtu: ni matendo ya akili, Hivyo Daudi alikuwa ni mtu aliyeupendeza moyo wa Mungu (1 Sam 13: 14), inaonyesha kwamba Mungu ana moyo, unaoweza kunakiliwa kwa kiwango kidogo na mtu, ingawa mwanadamu wa mwili haupendezi moyo wa Mungu. Mafungu ya maneno kama BWANA akaghairi kwa kuwa amemfanya mwanadamu duniani akahuzunika moyo (Mwa. 6:6), hufunua hisia ya Mungu, mwenye ufahamu kuliko kuwa kishindo cha roho ya kuwazika katika hewa. Hapa tunasaidiwa tukubali jinsi kwa kweli tunaweza pande zote mbili kumpendeza na kutokumpendeza, Kama mtoto anavyoweza kwa baba wa mwili.

## IKIWA MUNGU SI MTU MMOJA

Kama Mungu si wa kweli, mmoja mwenye kuwepo, Basi wazo la kupenda mambo ya roho ni vigumu kushikana nayo. ikiwa Mungu ni mwenye haki kabisa lakini si mtu mwenye umbo, basi kwa kweli hatuwezi kuiwazia haki yake ilivyodhihirika kwa watu. Pande zote mbili, Ukristo uliokenguka na wayahudi wana wazo la kwamba haki ya Mungu inaingia katika maisha ya watu kwa njia ya

'Roho Mtakatifu' Asiyedhahiri ambaye kwa namna isiyoeleweka tunafanywa mfano kwenye akili ya Mungu, na kukubalika kwake. Kwa maneno mengine, mara tukitambua ya kwa mba yupo mtu mwenyewe aitwaye Mungu, basi tunaweza kurekebisha tabia yetu kufuata atakavyo, Kwa msaada wake utokao kwenye ushawishi wa neno lake na kwa kuleta sifa inayoonyesha tabia ya Mungu katika utu wetu.

Lengo la Mungu ni kujidhihirisha mwenyewe katika mkutano wa watu waliotukuzwa. Jina la kumbukumbu yake, YEHOVA ELOI, linamaanisha hivi ( Atakaye kuwa kwa wenye nguvu ni tafsiri iliyo karibu sahihi.) ikiwa Mungu si mtu mwenye umbo, basi thawabu ya waaminifu katika ufalme wa Mungu ujao duniani inaonyesha ya kwamba watakuwa nayo wazi tena dhahiri wakiwepo katika mwili, Ingawa hawatakuwa katika udhaifu wa mwili wa Mwanadamu tena. Ayubu alitamani' Siku ya mwisho' atakapofunguliwa na mwili wake ( Ayubu 19:25:27); Abrahamu itabidi awe mmojawapo wa wale wengi wa hao walalao katika mavumbi ya nchi ambao wataamka…… Kwa uzima wa Milele wa nchi ya Kanani (Dan. 12:2) hivyo basi ataweza kupata ahadi ya urithi wa milele wa nchi ya kanaani, Sehemu inayoonekana katika dunia hii

(Mwa. 17:8.) " Na wataua wake watashangilia….. waimbe kwa sauti kuu vitandani mwao….. ili kufanya kisasi juu ya

mataifa (Zab 132: 16; 149: 5,7) Kushindwa kwa watu wote wa pande mbili, Wayahudi na watu wa mataifa,

Kutambua mafungu ya maneno kama haya vyema, kwa ukubwa wa maneno yenyewe Kuletwa ahadi za kuonekana kwa Abrahamu, kumeongoza watu kwenye imani potovu la' Nafsi haifi' ya kwamba Mwanadamu halisi anakuwepo hai akifa. Wazo hili halina msaada wa Biblia kabisa. Mungu hapatikani na mauti, Mtu mwenye utukufu, analifanya lengo lake, ili kwamba wanaume na wanawake waweze kuitwa na kuishi katika ufalme wake ujao kwenye dunia hii, Kushiriki sifa, zilizoelezwa katika umbo la mwili.

Waaminifu wameahidi wa kwamba watarithi mwili wa Mungu (2 Pet. 1:4) Ikiwa Mungu si mtu mmoja, basi hii ina maana tutaishi milele kwa roho zisizo na mwili. Lakini hili si fundisho la Biblia. Tutapewa mwili kama ule wa Yesu. (Flp. 3:21), Nasi tunajua kwamba tutakuwa na mwili halisi kwenye ufalme mwili utakaokuwa na mikono macho na masikio (Zek. 13:6, Isa. 11:3 ), mafunzo ya Mungu kuwa ni Mmoja, kwa sababu hii yanasimulia Injili ya Ufalme.

Itakuwa wazi kwamba hakutaweza kuwa na wazo la kujua Ibada, dini au uhusiano mmoja na Mungu mpaka itambulike kuwa Mungu ni mtu mmoja, na kwamba kwa mwili sisi ni mfano wake. Ingawa ni mfano usio kamili sana unahitajika kuukuza kufuata mfano wa akili yake, Hivyo basi, tutaweza kupata utimilifu wa mfano wake unaoonekana katika ufalme wa Mungu. Maana nyingi zaidi na faraja tunaweza kupata kutoka mafunzo ya maneno ambayo yanamtaja Mungu kuwa ni Baba aliye na upendo, akiturudi kama Baba afanyavyo kwa mwanae (mfano. Kum. 8:5). Katika maneno yenyewe ya mateso ya Kristo tunasoma

kwamba,'Lakini BWANA aliriidhika kumchubua' (Isa. 53:10 ),Ingawa "Alimlilia Mungu" aliisikia sauti yangu…….. Kilio changu kikaingia masikioni mwake (Zab.18:6). Ahadi ya Mungu kwa Daudi kuhusu mzao atakaye kuwa ni mwana wa Mungu ilitakiwa azaliwe kwa Muujiza kwa Mwanadamu; Ikiwa Mungu hakuwa ni mtu mmoja, asingekuwa na mwana huyo.

Kumfahamu Mungu kwa usahihi ni ufunguo unaofungua maneno mengi mengine ya muhimu katika mafundisho ya Biblia. Lakini kama uongo mmoja huongoza kwenye uongo mwingine, Hivyo dhana potovu juu ya mungu inaficha utaratibu wa kweli ambao maandiko yanatoa. Kama umepata kuona kuwa hii sehemu inadhibitisha, au hata ikiwa ni ndogo, basi, swali linakuja. Je? Unamjua Mungu kweli?. Sasa tutachunguza maandiko ya Biblia zaidi kuhusu yeye.

### 1.3 Jina La Mungu Na Tabia Ya Sifa Yake

Ikiwa Mungu yupo, inafaa kufikiri kuwa atakuwa amevumbua njia nyingine ya kutuambia habari zinazo mhusu yeye mwenyewe. Tunaamini ya kwamba Biblia ni ufunuo wa Mungu kumjulisha Mwanadamu, na humo ndani ya kitabu tunaona kudhihirika tabia ya sifa ya Mungu. Hii ndio sababu Neno la Mungu linasemwa kuwa ni'Mbegu' yake (1 Petro 1:23) Kwa kuwa kama likigeuza hali ya mioyo yetu, kiumbe mpya anaumbwa ndani yetu ambaye ana sifa za Mungu (Yakobo. 1:18, 2Kor. 5:17). Kwa hiyo sisi wenyewe tunapotumia zaidi neno la Mungu na kuchukua masomo sisi wenyewe, ndivyo zaidi tutafanana mfano wa mwana wake ( Rum, 8:29) ambaye kwa tabia ya sifa alikuwa mfano kamili wa Mungu (Kol. 1:15).Kwa hii imelala thamani ya kusoma sehemu za historia ya Biblia, Zimejaa kadhia ya masomo jinsi Mungu

alivyojishughulisha na watu pamoja na matifa, Daima akionyesha msingi ule ule wa sifa.

Katika Kiebrania jina la mtu mara nyingi lilileta tabia ya sifa zao au taarifa zinazowahusu. Mifano mingine iliyowazi:

- 'Yesu''Mwokozi' Kwa kuwa atawaokoa watu wake kutoka dhambi zao' (Math. 1:21)
- 'Abrahamu''Baba wa mkutano mkubwa' Maana nimekufanya kuwa baba wa mataifa mengi'(Mwa. 17:5)
- 'Hawa (Eva)'Uhai' Kwa kuwa alikuwa mama wa wenye uhai wote (Mwa. 3:20)
- 'Simeoni''Kusikia' Kwa kuwa bwana amesikia kwamba nalichukiwa, kwa sababu amenipa mwana huyu (Mwa. 29: 33).

Katika Yeremia 48:17, kuwajua watu wa Moabu ni sawa sawa na kufahamu jina la moabu.Mara nyingi zaburi zinamlinganisha Mungu mwenyewe na jina lake, neno lake na matendo (Zab. 103:1, 105:1, 106:1,2,12,13.) Kwa sababu hii itegemewe kwamba majina ya Mungu na heshima vitatupatia habari nyingi kuhusu yeye mwenyewe, kwa kuwa yapo maelekeo mengi ya tabia ya sifa na kusudi kwa kweli ana jina zaidi ya moja.Somo lenye kueleza jambo moja moja la jina Mungu linafaa baada ya Ubatizo; kufahamu zaidi sifa na tabia ya Mungu kumeelezwa katika jina lake, ni jambo lingine ambalo liendelee wakati wa maisha yetu yote katika Bwana. Linalofuata sana kwa hilo, mengi ni Utangulizi.

Musa alipotaka aelimishwe kwa undani kuhusu Mungu ili imani yake iimalike wakati wa kipindi kisicho sahaulika sana cha maisha yake. Malaika,'Alitangaza jina la BWANA: BWANA,BWANA Mungu, Mwingi wa huruma, Mwenye fadhili, Si mwepesi wa hasira, Mwingi wa rehema na kweli, Mwenye kuwaonea huruma watu elfu elfu, Mwenye kusamehe uovu na

makosa na dhambi; Wala si mwenye kumhesabia mtu mwovu kuwa hana hatia,' (Kut. 34:5-7)

Huu ni ushahidi ulio wazi wa kwamba majina ya Mungu yanaweka sifa zake.Tendo la kuwa nazo ni uhakika kuwa ni mtu mmoja, si busara kufikiri ya kwamba fungu la roho laweza kuwa na dalili na sifa ya tabia hizi ambazo vile vile zaweza kuendelezwa ndani yetu wanadamu.

Mungu amechagua hasa jina moja ambalo amependa ajulikane na kukumbukwa na watu wake, ni kwa ufupi, maelezo mafupi, ya kusudi lake kwa watu.

Israeli walikuwa watumwa Misri, Walihitajika kukumbushwa lengo la Mungu kwao. Musa aliambiwa awaambie Jina la Mungu, ili kwamba hili liwasaidie kuwaletea kusudi la kuondoka Misri na kuanza safari kuelekea nchi ya Ahadi (1Kor. 10:1) Nasi pia tunahitajika kuelewa mambo ya msingi yahusuyo jina la Mungu kabla ya kubatizwa na kuanza safari yetu ya kuelekea Ufalme wa Mungu. Mungu aliwaambia Israeli kuwa Jina lake alikuwa YAHWEH-YAHU (Zab 89:8 uv); Maana yake"Mimi niko ambaye NIKO" au limetafsiriwa kwa usahihi zaidi,'Nitakuwa ambaye Nitakuwa'(Kut 3:13-15) Jina hili, kidogo likapanuka wakati ule:" Tena Mungu akamwambia ( Ikiwa ni nyongeza) Musa, Hivi ndivyo utawaambia wana wa Israel, BWANA (Yahweh) Mungu wa Babu zenu, Mungu wa Abrahamu, Mungu wa Isaka, Mungu wa Yakobo, ….Hili ni Jina langu Milele, la kumbukumbu yangu kwa vizazi vyote. (Kut. 3:15). Kwa sababu hiyo jina kamili la Mungu ni "BWANA Mungu"

Zaidi Agano la kale liliandikwa kwa Kiebrania na tafsiri ya Kiswahili ni lazima kutukia visivyo sawa sawa wakati ujapo wa kutafsiri maneno ya Kiebrania hasa neno "Mungu" mengi ya

maelezo moja moja yakosekana - Tafsiri yetu ya Kiswahili imetoka kwenye Kiingereza. Moja ya maneno yanayotumiwa na Kiebrania limetafsiriwa'Mungu' ni Elohim (ELOI) maana yake'Wenye Nguvu' Kumbukumbu ya jina la Mungu, jina ambalo anatutaka tumkumbuke, kwa sababu hiyo.

## YAHWEH ELOHIM - YAHU ELOI

***Maana yake***

## ATAKAYEDHIHIRIKA KATIKA KUNDI LA WENYE NGUVU.

Kwa hiyo ni kusudi la Mungu kuidhihirisha tabia ya sifa yake, Umuhimu wake katika kundi kubwa la watu. Kwa kulitii neno lake tunaweza kukuza sifa zingine za Mungu ndani yetu wenyewe sasa, hivyo basi kadri ya busara sana. Mungu alijifunua mwenyewe kwa waamini wa kweli katika maisha haya.lakini jina lake Mungu ni la Unabii wa wakati ujao hapo dunia itakapo jaa watu watakao kuwa sawa naye, pande mbili kwa tabia na mwili (2Petr 1:4). Ikiwa tunataka kuungana na lengo la shabaha ya Mungu na kuwa kama Mungu bila hata kufa tena, kuishi milele katika uadilifu wote uliokamilika, basi yatupasa sisi wenyewe tujiunge na jina lake.

Namna ya kufanya hivi ni kubatizwa katika jina, yaani la Yahweh Elohim (Math. 28:19). Hili linatufanya tuwe watoto ('Uzao') wa Abrahamu (Gal,. 3:27-29) uliohaidiwa kurithi milele nchi (Mwa. 17:8; Rum. 4:13) Kundi la wenye nguvu (Elohim - Eloi) ambao unabii wa jina la Mungu utatimilika. Limeelezwa zaidi kwa habari katika somo la 3.4.

### 1.4 Malaika

Yote ambayo tumeyapima sana katika somo hili yanaletwa pamoja kwenye tafakari ya Malaika:

- Viumbe walio na mwili
- Huchukua jina la Mungu
- Wao ni njia ambayo roho wa Mungu anatenda kazi ya kutimiza mapenzi yake
- Wanapatana tabia na kusudi lake
- Na kwa hiyo wanamdhihirisha yeye.

Tumetaja kwenye somo la 1.3 ya kwamba moja kati ya maneno yanayotumika zaidi katika Kiebrania lililotafsiriwa “Mungu” ni' Eloi’ ambalo hasa maana yake ' Wenye nguvu’ hawa,'Wenye nguvu’ ambao huchukua jina la Mungu wanapotokea wana weza kuitwa 'Mungu’ kwakushirikiana kwao pamoja na naye karibu. Hawa viumbe wanaitwa Malaika.

Taarifa ya uumbaji wa ulimwengu katika mwanzo 1 inatuambia ya kwamba Mungu alitamka amri halisi kuhusu Uumbaji'Ikiwa hivyo’ walikuwa ni Malaika waliotimiza amri hizo:

“Enyi Malaika zake, mliohodari mtendao neno lake, mkiisikiliza sauti ya neno lake (Zab. 103:20).

Kwa sababu hii busara husadiki kuwa tunaposoma 'Mungu’ akiumba ulimwengu, kazi hii kweli ilifanywa na Malaika. (Ayubu 38:4-7) anadokeza vile vile namna hii. Sasa ni wakati mzuri kuelezea kwa kifupi matukio ya uumbaji kama yalivyoandikwa

Mwanzo 1:

Siku ya Kwanza‘ Mungu akasema, Na iwe nuru, Ikawa’ (Mstari 3)

Siku ya Pili 'Mungu akasema, Na iwe anga katikati ya maji, likayatenga maji na maji.Mungu akalifanya anga ,akayatenga yale maji yaliyo juu ya anga na yale yaliyo chini ya anga: Ikawa hivyo’ (Mstari 6,7)

Siku ya Tatu ‘Mungu akasema, Maji yaliyo chini ya mbingu na yakusanyike mahali pamoja, (akifanya Bahari na Bahari kuu) ili pakavu paonekane; Ikawa hivyo’ (Mstari wa 9)

Siku ya Nne ‘Mungu akasema, Na iwe mianga katika anga la mbingu… Ikawa hivyo’ (Mstari 14:15)

Siku ya Tano ‘Mungu akasema, Maji na yajae kwawingi na kitu kiendacho chenye uhai …. ndege waruke juu ya nchi ….. Mungu akaumba kila kiumbe chenye uhai (Mstari wa 20:21), Ikawa hivyo.

Siku ya Sita ‘Mungu akasema, Nchi na izae kiumbe haikwa jinsi zake…. Mnyama wa kufugwa,nacho kitaambaacho …. Ikawa hivyo (Mstari 24)

Siku hiyo hiyo ya sita mtu aliumbwa. Mungu akasema, na tufanye mtu kwa mfano wetu, na kwa sura yetu (Mwa 1:26). Tuliwahi kutoa maelezo juu ya mstari huu katika somo la 1.2. Kwa muda uliopo, tunataka kujua hapa ya kwamba.'Mungu’ sio tu anatajwa Mungumwenyewe katika utu'Na tufanye mtu’ inaonyesha kuwa Mungu anatajwa mtu zaidi ya mmojaNeno la Kiebrania linalotafsiriwa hapa'Mungu’ ni Elohim (Eloi), Maana yake'Wenye nguvu’ Ukiwa ni ushahidi unaotaja Malaika. Ukweli ni kwamba

Malaika walituumba sisi kwa mfano wao maana yake ni kuwa wana sura ya mwili ule ule kama tulio nao. Kwa sababu hiyo ni wa kweli, wa kugusika, viumbe wenye mwili, wakishiriki mwili ule ule kama wa Mungu.

'Mwili' Kwa maana hii unatajwa kwa msingi jinsi mtu mwingine alivyo kwa sababu ya muundo wa mwili wao. Katika Biblia ipo "Miili" ya aina mbili katika maana halisi ya neno haiwezekani kwa wakati huo huo kuwa miili hii ya aina mbili.

Mwili wa Mungu ('Mwili wa Uungu')

Hauwezi kutenda dhambi (Mkamilifu) Rum 9:14,6:23; Zab. 90:2, Math 5:48,Yak 1:13)Haupatikani na Mauti ( 1Timotheo 6:16)

Una nguvu tele na uweza ( Isaya 40:28)

Huu ndio mwili wa Mungu na Malaika na ambao alipewa Yesu baada ya kufufuliwa (Matendo 13:34; Ufunuo 1:18; Ebr. 1:3) Huu ndio mwili ambao tumeahaidiwa kupewa (Luka 20:35,36; Isa. 40:28,31)

Mwili wa mwanadamu

Hujaribiwa na kutenda dhambi ( Yak 1:13-15 )kwa nia mbaya ya asili (Yer 17:9; Marko 7:21-23) Huangamia mautini, Yaani unapatwa na kifo ( Rum. 5:12,17; 1Kor 15:22) Una kikomo cha nguvu, sehemu mbili, kwa mwili (Isa. 40:30) na kwa akili ( Yer 10:23)

Huu ni mwili ambao watu wote, wema na wabaya, kwa sasa wanao mwisho wa mwili huo ni kifo (Rum 6:23). Ulikuwa ni mwili ambao Yesu alikuwa nao wakati wa maisha yake ya mwili

unaokufa hapa duniani (Ebr. 2:14-18,Rum. 8:3 Yoh 2:25, Marko 10:18)

**MATENDO YA KUONEKANA NA MALAIKA**

Malaika wakiwa na mwili wa Uungu, inabidi wawe hawana dhambi na kwa sababu hiyo hawawezi kufa kwa kuona kwamba dhambi huleta mauti (Rum. 6:23). Inapasa wawe na umbo halisi na mwili wa kuwepo mauti "Na yaletwe basi maji kidogo ukanawe miguu, mkapumzike chini ya mti huu"(Mwanzo 18:4)

Wawili kati ya hao Malaika wakati ule walikwenda kwa lutu katika mji wa Sodoma. Tena, walitambuliwa kuwa ni watu na lutu pamoja na watu wa Sodoma.'Basi, wale malaika Wawili wakaja Sodomaa jioni aliowakaribisha wakae kwake usiku. Lakini watu wa Sodoma wakaja kwenye nyumba yake, wakiuliza kwa namna ya kutisha,'Wawapi wale watu waliokuja kwako usiku huu ?' Lutu akawasihi,' Watu hawa msiwatende neno' Taarifa ya maandiko ya Mungu pia inawaita ni'Watu', Wale watu ( Malaika ) wakanyoosha mikono yao, wakamwokoa Lutu, Basi wale watu wakamwambia Lutu … BWANA ametutuma tuuharibu Sodoma (Mwanzo 19: 1,5,8,10,12,13).

Ufafanuzi wa Agano jipya juu ya matukio haya yanadhibitisha kwamba Malaika wanafanana na umbile la watu. "Msisahau kuwafadhili wageni; Maana kwa njia hii wengine (Kwa mfano Lutu na Abrahamu ) waliwakaribisha Malaika pasipo kujua (Ebr 13:2)

Yakobo alishindana usiku kucha na mtu mmoja ( Mwa 32:24) ambaye baadae tumeambiwa kuwa alikuwa Malaika (Hosea 12:4)

Watu wawili wakasimama karibu nao, wenye nguo nyeupe walikuwepo kwenye ufufuo (Luka 24:4) na wakati wa kupaa (Mat. 1:10) Yesu, kwa uhakika hawa walikuwa ni Malaika. Ona vidokezo vya'Kipimo cha Kibinadamu, maana yake cha Malaika' (Uf 21:17).

## MALAIKA HAWATENDI DHAMBI

Malaika wakiwa na mwili wa Uungu, hawawezi kufa, kwa sababu dhambi huleta mauti, Basi wao hawawezi kutenda dhambi. Maneno ya asili katika lugha ya Kiyunani na Kiebrania yaliyotafsiriwa'Malaika' maana yake ni mjumbe; Malaika ni wajumbe au watumishi wa Mungu, Watiifu kwake, Kwa hiyo hawafikiriwi wao kuwa ni wenye dhambi. Kwa hivyo neno la Kiyunani'Agelos' lililotafsiriwa'Malaika' vile vile limetafsiriwa'Wajumbe' Wanaposemwa wanadamu kwa mfano Yohana mbatizaji, (Math 11:10) na wajumbe wake (Luk. 7:25) wajumbe wa Yesu (Luk. 9:52) na watu walioupeleleza mji wa Yeriko (Yak. 2:25). Kwa kweli inawezekana kwamba'Malaika' katika maana ya wajumbe wanadamu wanaweza kutenda dhambi.

Mafungu ya maneno yafuatayo ni wazi kwamba Malaika wote ( Sio tu baadhi yao) kwa umbile ni watiifu kwa Mungu, na hivyo hawawezi kutenda dhambi.

'BWANA ameweka kiti chake cha Enzi mbinguni Na Ufalme wake unavitawala vitu vyote (Yaani haiwezekani kuwepo uasi juu ya Mungu mbinguni)Mhimidini BWANA, Enyi Malaika zake, Ninyi mlio hodari, mtendao neno lake, Mkisikiliza sauti ya neno lake Mhimidini BWANA, enyi majeshi yake Yote; Ninyi watumishi wake mfanyao mapenzi yake (Zab. 103:19-21)

“Msifuni, enyi Malaika wake wote …. Majeshi yake yote ( Zab 148: 2 ) Je ! hao wote si roho (Malaika ) watumikao, wakitumwa kuwahudumia wale watakaourithi wokovu ? ( Ebra. 1: 13,14 )

Kurudiwa kwa neno'Wote’ linaonyesha ya kwamba Malaika hawajagawanyika katika makundi mawili, kundi moja zuri na jingine lenye dhambi. umuhimu wa kufahamu vema umbile la malaika ni kwamba thawabu ya waaminifu ni kushiriki mwili wao. “Wale wahesabiwao kuwa wamestahili…. Hawaoi wala hawaolewi … wala hawawezi kufa tena. kwa sababu huwa sawa sawa na Malaika (Luk 20:35, 36).

Hili ni neno la muhimu kulishika. Malaika hawawezi kufa'Maana hatwai asili ya Malaika (Kwa kuwa tangu asili hawajatenda dhambi). Ila atwaa asili ya mzao wa Abrahamu - ‚sababu ya dhambi’ (Ebr 2:16) Ikiwa Malaika waweza kufanya dhambi, Basi wale ambao watakuwa wamestahili thawabu ya Kristo atakapo kuja bado wataweza kutenda dhambi pia, Na kwa kuwa dhambi huleta mauti (Rum 6:23) kwa sababu hiyo hawataweza kuwa na uzima wa milele, kama tukiwa na uwezekano wa kutenda dhambi ni kufanya ahadi ya Mungu ya uzima wa milele haina maana, kwa kufahamu kuwa thawabu yetu ni kushiriki mwili ule wa Malaika. Ushuhuda wa'Malaika (Luk. 20:35,36) unaonyesha kwamba hakuna aina ya Malaika wema na wenye dhambi; ipo aina moja ya Malaika tu.

Ikiwa Malaika waweza kutenda dhambi, Basi Mungu ameachwa hana nguvu za kutenda tendo la haki katika maisha yetu na mambo ya ulimwengu, kwa kufahamu kuwa ameeleza kwamba anafanya matendo yake kwa njia ya Malaika zake( Zab 103:19-21) Wamefanywa kwa'Roho wa Mungu katika maana ya

kwamba anatimiza yote kwa nguvu zake. Akitenda kazi katika Malaika (Zab 104:4). Kwamba wanamwasi Mungu haiwezekani. Mkristo amwombe kila siku, Mungu ili ufalme uje duniani, ili mapenzi yake yafanyike kama sasa yanavyofanyika mbinguni (Math 6:10) Ikiwa Malaika wa Mungu iliwapasa washindane na Malaika wenye dhambi huko mbinguni, basi, kwa utimilifu mapenzi yake hayakuweza kufanyika huko, na kwa sababu hiyo hali hiyo hiyo itapatikana kwenye ufalme wa Mungu ujao. Kutumia maisha ya milele kwenye ulimwengu ambao utakuwa ni uwanja wa vita kati ya dhambi na utii, kwa shida hayo sio matazamio ya kutia moyo, lakini hilo, kwa kweli, sio ndiyo suala lenyewe.

## MALAIKA NA WATU WANAOAMINI

Ipo sababu nzuri ya kuamini kuwa kila mwamini wa kweli ana Malaika pengine mmoja maalumu-wa kuwasaidia katika maisha yao:-

'Malaika wa BWANA hufanya kituo, akiwazungukia na kuwaokoa wamchao' (Zab 34:7)

Mmojawapo wa wadogo hawa waniaminio (Yaani wafuasi dhaifu- Zek, 13:7 Mat 26:31)…Malaika wao mbinguni siku zote huutazama uso wa Baba yangu' (Mat. 18:6,10)

Wakristo wa kwanza ni wazi waliamini kwamba Petro alikuwa na Malaika mlinzi (Matendo 12:14,15).

Watu wa Israeli walipita katika bahari ya Shamu, waliongozwa na malaika kwenye jangwa kuelekea nchi ya Ahadi. Kutembea kupitia katika bahari ya shamu maana yake ni Ubatizo wetu katika maji (1Kor 10:1), Hivyo nasi vile vile ina maana tusadiki kuwa baadae tunaongozwa na kusaidiwa na Malaika

tunaposafiri katika jangwa la maisha kuel;ekea nchi ya ufalme wa Mungu.

Ikiwa Malaika wana weza kuwa waovu katika maana ya kuwa wenye dhambi, basi Ahadi hizi za Malaika kuongoza na kushawishi katika maisha yetu zinakuwa laana badala ya Baraka.

- Basi tufahamu ya kuwa Malaika ni Viumbe………
- Wenye mwili ulio sawa na Mungu na huonekana kwa mwili
- Ambao hawawezi kutenda dhambi
- Daima hufuata amri za Mungu
- Wao ni njia ambayo Mungu katika Roho nguvu hunena na
- kutenda kazi (Zab. 104:4)

LAKINI..?

Makanisa mengi ya'Kikiristo' yana wazo la kwamba Malaika wanaweza kutenda dhambi, na kwamba Malaika wenye dhambi sasa hivi wapo na wao wanahusika na dhambi pamoja na matatizo yaliyopo hapa Duniani. Tutajadili zaidi vya kutosha juu ya kutofahamu vema jambo hili kwenye somo la 6. Kwa sasa tutatengeneza vipengele vifuatavyo:-

Inawezekana kwamba uumbaji ulikuwepo uliotutangulia sisi wa kweli, yaani huo ulioandikwa katika Mwanzo 1. Pia inaweza kusadikika ya kwamba Malaika waliopo walikuja kuwa na fahamu za'Wema na Ubaya' (Mwa. 3:5) walipo kuwa katika hali kama hii tuliyonayo katika maisha haya.

Ya kwamba viumbe wengine walioishi kwa kipindi kile walitenda dhambi hatujakatazwa kufikiri; lakini yote haya ni mawazo ambayo mioyo ya watu hupenda kujishughulisha. Biblia yatuambia kile ambacho tunakihitaji kujua kuhusiana na hali iliyopo, ambayo ni kwamba hawapo Malaika watenda dhambi, Malaika wote ni watiifu kwa Mungu kabisa.

Hawawezi kuwepo viumbe wenye dhambi mbinguni, kwa kufahamu kuwa Mungu'ana macho safi na hawezi kuangalia uovu' (Ab. 1:3) katika maelezo haya, Zaburi 5:4,5 yatuambia:-

'Mtu mwovu hatakaa kwako. wajivunao hawatasimama mbele za macho yako' yaani makao ya mbinguni. Jambo la kwamba ulikuwepo Uasi juu ya Mungu mbinguni na Malaika watenda dhambi ni wazo linalopingana kabisa na maneno yaliyotolewa.

Neno la kiyunani lililotafsiriwa'Malaika' maana yake'Mjumbe' linataja wanadamu, kama tulivyoonyeshwa'Wajumbe' wanadamu hawa wanaweza kwa kweli kufanya dhambi.

Ya kwamba upo uovu, viumbe wenye dhambi ambao juu yao mwelekeo wa maisha yote yasiyofaa wanaweza kutupiwa lawama kwa kawaida ni moja ya Imani zaidi iliyoshikiliwa katika Upagani.Kwa njia hiyo hiyo mambo yanayohusu Krismas yameingia kwenye kile kinachodhaniwa ni'Ukristo' Basi, vile vile Ukristo una fikra hizo za Kipagani

Yapo mafungu ya maneno ya Bibilia yaliyojaa tele ambayo yanaweza kutoeleweka kusaidia wazo hili la Malaika wenye dhambi kwa sasa wapo. Haya yamepimwa katika 'Kumsaka Shetani' yanapatikana kwa wachapishaji - Mafungu haya ya maneno hayawezi kuruhusiwa kupingana na mafunzo tele ya Biblia kwa kutofautiana na haya yaliyokwisha tolewa.

**Tumeacha Kitambo sehemu ya 1:'Mungu ni roho' (Yohana 4:24)**

Katika somo la pili tunafafanua kwa utaratibu zaidi jinsi Roho wa Mungu alivyo. Tunaweza kutoa maelezo kwa ufupi sababu zilizoonyeshwa hapo kwa kusema kwamba roho wa /ya Mungu ni nguvu au pumzi yake ambayo kwa hiyo nafsi yake mwenyewe, Utu wake na tabia, vimedhihirika kwa mwanadamu kwa njia ya matendo yake ambavyo Roho huyo anatimiza.Hivyo'Mungu ni Roho' kama katika Yohana 4:24 atafsiriwe vema kwa kuwa Roho yake ndiyo inafanya utu wake.

Mungu amesemwa kuwa yumo katika vitu vingi, kwa mfano:-

'Mungu wetu ni moto ulao' (Ebr. 12:29)
'Mungu ni Nuru' (1 Yoh. 1:5)
'Mungu ni Pendo (1 Yoh.4:8)
'Neno (Kiyunani'Lagos' - Mpango, Lengo,Kusudi, wazo) alikuwa Mungu' (Yoh 1:1)

Hivyo,'Mungu' ni sifa yake. Ni kosa lililo wazi kuleta sababu za kupinga kwamba sifa za upendo wa Mungu ni za kuwazika, kwa kuwa tunasoma kwamba 'Mungu ni pendo' tunaweza kumwita mtu mwingine Mwema wenyewe; lakini hii haina maana kwamba haupo bila mwili ni namna ya kuwepo yeye ndiko kunatudhihirishia wema kwetu.

Roho ikiwa ni nguvu ya Mungu, mara nyingi tunasoma Mungu akiituma au akiiongoza roho yake kutimiliza mabo yake kwa kupatana na mapenzi yake na tabia ya sifa yake. Hata ameelezewa kuwa anaumba roho (Yaani Upepo UV). Kusema kwamba Mungu

na roho yake katika maana safi iliyo halisi ni msemo ule ule kwa namna nyingine - katika maana inakuwa Uwepo wa Mungu.

Mifano ya Mungu akiiongoza Roho yake ni mingi, inaonyesha mtengano wa Mungu na Roho yake:-

> 'Yeye (Mungu) aliyetia kati yao Roho yake mtakatifu'(Is. 63:11)
> 'Nitatia Roho yangu (Mungu) juu yake (Yesu )' ( Math.12:18)
> 'Baba huwapa Roho mtakatifu' (Luk. 11:13)
> 'Roho akishuka kama hua toka Mbinguni' (Yoh. 1:32)
> 'Nitawamwagia watu wote Roho yangu' (Matendo. 2:17).

Kwa kweli ushahidi juu ya 'Roho wa Mungu' ni uhakika wa kutosha kuwa Roho sio Mungu mwenyewe. Tofauti hizi kati ya Mungu na Roho ni shida nyingine ilio kwa wale wanao amini kuwa Mungu ana Nafsi'Tatu' ambazo Mungu amelingana na Yesu na Roho Mtakatifu. Jambo hili kama lingekuwa la kweli, na kama Mungu amedhaniwa kuwa sio mtu, basi halikadharika hata Yesu naye sio mtu halisi.

Kwa umuhimu sana, Mungu asiye mtu hata sala kuelekea kwake inakuwa haina maana, kwenye alama ambayo sala ni mazungumuzo kati ya fahamu zetu na wazo la Mungu ambalo lipo katika akili zetu. Daima tunakumbushwa kwamba tunamwomba Mungu ambaye ana Umbo makao yake yapo Mbinguni (Mhu. 5:2; Math. 6:9,5:16, 1Fal. 8:30) na kwamba Yesu sasa yuko mkono wa kuume huko ili kutoa maombi yetu mbele zake (1Pet. 3:21, Ebr. 9:24).

Ikiwa Mungu si mtu binafsi, maneno haya yametolewa bila kuwa na maana. Bali, Mungu akieleweka kuwa ni wa kweli, Baba mwenye upendo, Sala ya kumwomba inakuwa ya kweli, Jambo

lililowazi na dhahiri - hasa tukizungumza na mtu mwingine ambaye tunamwamini ana mapenzi sana na anaweza kujibu.

**Tumeacha Kitambo sehemu ya 2:'Matumizi ya jina la Mungu'**

Tumefahamu kwamba Jina la Mungu na hilo la mwanae Yesu yana maana ya kina sana. Tunaposema 'Mungu' tunagusa juu ya kila mwelekeo wa kusudi lake la Ajabu la upendo na kweli. Ya kwamba Jina la Mungu litumike bure kama upole usio na maana au kwa maelezo ya kukasirisha, ni moja ya mambo ambayo mtu hufanya na kumnena vibaya zaidi Muumba wake. Kwa sababu hii kila mtu anayetaka kumpendeza Mungu na kumheshimu atafanya kila jitihada kutotumia vibaya Jina la Mungu kirahisi- rahisi. Katika jamii ulimwenguni pote kufuru hii imekuwa sehemu ya kawaida kwa Lugha za siku hizi; Kukatisha ile iliyokuwa ni tabia ya mazoea haita kuwa kazi rahisi. Sala ya kweli ya kuomba msaada wa Mungu hakika itasikika. Wale ambao wapo ndani ya shughuli yetu ya kuwaongoza na kuwavuta, Mf. Watoto, pia watakumbushwa hatari ya kukufuru:"Maana BWANA hatamhesabia kuwa hana hatia alitajaye jina lake bure (Kum. 5:11)

Kwa upande mwingine wapo wale wanaosisitiza kwamba tusipotumia maneno ya Kiebrania Yahweh au Yehova (Njia tofauti ya kutamka neno lile lile) Tunapozungumuza kuhusu Mungu, wakati huo tunakuwa tumepotea sana. Miongoni mwao zaidi ya hawa ni Chama cha mlinzi, wanasisitiza kuwa Mkristo asipojiita mwenyewe ni'Shahidi wa Yehova' Basi hana uhusiano na Mungu.

Kwa kufanya hivi, watu hawa wanatumia jina takatifu la Mungu na la ajabu kuchochea aina fulani ya mfumo wa Imani wa

kuelimisha kiroho, ambapo wanawadharau watu wengine tu kwa matamshi au matumizi ya neno moja. Hii sio kusema kuwa ni vibaya kutumia Jina la Mungu; Hasa kweli linafaa kutumika kwenye Sala zetu wenyewe mara tukibatizwa kwa usahihi katika Jina lake. Ingawa hivyo, Agano Jipya halitupatii ishara yoyote kuwa hili ni lazima au inatakiwa na Mungu. Aliongoza kuandika Agano Jipya hivyo basi liliandikwa kwa Kiyunani (Kigriki) likitumika neno moja la'Mungu' -'theos' likiwa na maana "Mtu mkubwa".

Hakuna tofauti iliyofanywa ndani yake kati ya'Mungu' na 'Yahweh' wala haipo amri yoyote dhahiri inayohusiana kwa waamini wakiwa ni jumuiya wajiiteje.Petro anamsema mwamini kuwa ni " Mkristo" kuliko kumwita ni'Mtu wa Yehova' au jambo lingine kama hili (1 Petro 4:16) kutilia mkazo zaidi katika matumizi ya Jina la 'Yehova' kunapelekea kupunguza thamani ya kazi na Nafsi ya BWANA'Yesu' kwa njia hii ambayo wakristo wengi wa kiinjili wanatia msukumo zaidi kwenye jina na kazi ya Yesu huku wakiacha kuangalia nafsi ya nguvu zaidi iliyo ya Mungu.

Majina mengine ambayo jumuia ya waaminiao ya wakristo wa kwanza waliyojiita wenyewe, hayatii ndani jina la Yehova:-

'Jamii ya Israeli' (Ef. 2:12)
'Mkutano mkuu na kanisa la wazaliwa wa kwanza' (Ebr. 12:23)
'Kanisa lake Mungu' (Matendo 20:28)
'Kanisa la Mungu aliye hai, Nguzo na Msingi wa kweli' (1 Timotheo 3:15)
'Nyumba ya Mungu' ( 1 Timotheo 3:15)

Tunapopita, ujue kuwa waamini hawakujiita wenyewe'Wakristo'. Neno hili maana yake lilikuwa la kuvunja heshima, hawa watu wa Kristo walibezwa na maadui zao.

**Tumeacha Kitambo sehemu ya 3: 'Ufunuo wa Mungu'**

Kinachufuata sio rahisi kukishika chote wakati tunaposoma kwanza,lakini umuhimu wa jambo tunalolizungumzia litakuwa dhahiri kadri masomo yake yanavyosonga mbele. Tunajumuisha kwenye maana hii ili uliache somo hili lote Msingi wa Biblia ukisha pimwa wenye ufunuo kuhusu Mungu mwenyewe.

Jina la Mungu laweza kuchukuliwa na yeyote ambaye amemchagua kujifunua au kujidhihirisha yeye mwenyewe. Hivyo watu na Malaika sawa sawa na Yesu huweza kuchukua jina la Mungu. Hili ni jambo la muhimu ambalo linatufunulia mengi ya Biblia. Hata mwana anaweza kuchukua jina la Baba; ana mambo mamoja na Baba yake, anaweza kuwa na jina lile lile la kwanza-lakini si mmoja na kuwa mtu yeye yule kama Baba. Kwa njia hiyo hiyo mwakilishi wa kundi anaweza kusema kwa niaba ya kundi, anaweza kumpigia mtu wa kwenye shughuli na kusema, Haloo ! hapa ni wakulima, Si Bw. Wakulima, bali anachukua jina lao kwa kuwa anafanya kazi kwa niaba yao. Basi hiyo hata kwa Yesu ilikuwa hivyo.

## MALAIKA HUCHUKUA JINA LA MUNGU

Tumeambiwa katika Kutoka 23:20,21 ya kwamba Mungu aliwaambia watu wa Israeli kuwa Malaika atawatangulia mbele yao;'Jina langu limo ndani yake', waliambiwa. Jina lake Mungu ni'Yahweh'. Basi, Malaika huchukua jina la Yahweh, na hivi

anaweza kuitwa Yahweh, au BWANA kwa herufi kubwa neno BWANA linatokana na Yahweh, katika Biblia UV ya Kiswahili ni sehemu moja tu Zaburi 89:8 utakuta neno

YAHU = YAHWEH. Tumeambiwa kuwa katika kutoka 33:20 Mtu hataniona uso akaishi; lakini katika Kutoka 33:11 tunasoma kwamba "BWANA"(Yahweh) alinena na Musa uso kwa uso, kama mtu anaposema na rafiki yake - Yaani kirafiki. Hakuwa ni BWANA, Yahweh mwenyewe alikuwepo, aliyenena na Musa uso kwa uso, Kwa kuwa hakuna mtu anayeweza kumwona Mungu yeye mwenyewe. Alikuwa ni Malaika aliyechukua jina la Mungu ndiye aliye fanya hivyo, na tunasoma habari za BWANA akisema uso kwa uso na Musa wakati hasa ni Malaika aliyefanya hivyo (Mdo. 7:30-33).

Ipo mifano mingine mingi ya maneno' Mungu' na BWANA ikitaja Malaika wakiwa Mungu mwenyewe. Mfano mmoja ulio wazi ni Mwa. 1: 26 "Mungu (Malaika) akisema, na tufanye mtu kwa mfano wetu"

## WATU NA JINA LA MUNGU

Moja ya maneno ambayo yanayosaidia sana katika kuelezea yote haya ni katika Yohana 10:34-36. Hapa Wayahudi walifanya kosa ambalo wengi wanaoitwa'Wakristo' wanafanya leo. Walidhani kuwa Yesu alikuwa anasema kuwa yeye ni Mungu mwenyewe. Yesu alisahihisha kwa kusema "Haija andikwa katika sheria yenu, nimesema Ninyi ni Mungu ? Ikiwa aliwaita Miungu ….. inakuwaje mimi …." Mnaniambia ninakufuru, kwa sababu nalisema, Mimi ni mwana wa Mungu ? Yesu kwa kweli alikuwa anasema 'Katika Agano la Kale watu waliitwa Miungu; mimi nasema ni mwana wa Mungu, basi imekuwaje mnaudhika sana?

Yesu kwa kweli alikuwa ananukuu toka Zab 82 mahali ambapo waamuzi wa Israeli waliitwa'Miungu'.

Kama ilivyoonekana, Jina kamili la Mungu katika Kiebrania ni 'Yahweh Elohim' likiwa na maana, Nitadhihirika katika kundi la wenye nguvu. Waamini wa kweli ni wale wengi wenye nguvu katika maana ndogo ya maisha haya nao watakuwa na nguvu tele kwenye Ufalme. Kwa mlinganisho huu wote umeonyeshwa kwa Isa. 64:4 na 1 Kor.2:9.

"Watu hawakusikia, wala kufahamu kwa masikio, wala jicho halikumwona Mungu, ila wewe, atendaye mambo kwa ajili yake amngojaye" Paulo ananukuu mstari huu katika 1 Kor.2:9-10: Imeandikwa, Jicho halikuyaona, wala sikio halikuyasikia wala hayakuingia katika moyo wa mwanadamu, mambo ambayo Mungu amewaandalia wampendao. Lakini Mungu ametufunulia sisi kwa Roho. Fungu la maneno katika Isa. 64:4 linasema hakuna hata mmoja isipokuwa Mungu anaweza kufahamu mambo aliyowaandalia waamini; Lakini 1Kor. 2:10 mstari unasema kwamba mambo hayo yamefunuliwa kwetu, hivyo katika maana sisi ni "Mungu": sio Mungu mwenyewe katika utu, bali ufunuo wa Mungu kwa matokeo kuwa tumebatizwa katika jina lake na kujua Ukweli.

## YESU NA JINA LA MUNGU

Sio jambo la kushangaza kwamba Yesu, Ikiwa ni mwana wa Mungu na ufunuo wake mkuu kwa watu, Pia naye atachukua jina la Mungu. Aliweza kusema "Nimekuja katika jina la Baba yangu" (Yoh.5:43). Kwa utii wake, Yesu alipaa kwenda mbinguni, naye Mungu akampa jina lipitalo majina - Jina la Yahweh, la Mungu mwenyewe

(Fil. 2:9).basi hii ndiyo sababu tunasoma Yesu anasema katika Uf 3:12 "Nami nitaandika juu yake (Mwamini) Jina la Mungu wangu……na jina langu mwenyewe, lile jpya"Kumbuka Yesu alitoa kitabu cha Ufunuo miaka mingi baada ya kupaa kwenda mbinguni na akiisha kupewa jina la Mungu, kama ilivyoelezwa katika Wafilipi 2:9.

Hivyo anaweza kuliita jina la Mungu "Jina langu Jipya"; Jina ambalo hivi karibuni alipewa. Sasa tunaweza kuelewa vema Isaya 9:6, mahali ambapo kuhusu yeye tumeambiwa "Jina lake (Ujue kuwa) utaitwa, Mshauri wa Ajabu, Mungu mwenye nguvu, Baba wa milele, …." Huu ni Unabii wa kwamba Yesu atachukua majina yote ya Mungu ya kwamba atakuwa ni ufunuo wote wa Mungu kwetu.Na ndivyo kwa maana hii aliitwa "Emmanueli" maana yake 'Mungu ni pamoja nasi' ingawa yeye hakuwa Mungu.

**Somo La Kwanza : Maswali**

1.Ni nini kitakachotusaidia zaidi kuamini Mungu ?

a) Kwenda Kanisani
b) Maombi na Kusoma Biblia
c) Kuzungumuza na Wakristo
d) Kutazama maumbile.

2. Yapi ya haya yafuatayo ni ufafanuzi sahihi zaidi wa Mungu ?

a) Ni wazo tu katika mioyo yetu
b) Kipande cha Roho katika Hewa
c) Mungu Hayupo
d) Mtu halisi wa Umbo

3. Je ? Mungu ni
a) Ummoja
b) Utatu
c) Miungu wengi katika mmoja
d) Haiwezekani kufafanua kwa njia ya yoyote

4. Jina la Mungu' Yahweh Elohim' lina maana gani ?
a) Yeye atakaye kuwa
b) Atakayedhihirika katika kundi la wenye nguvu
c) Mkuu
d) Nguvu

5. neno'Malaika lina maana gani ?
a) Kama mtu
b) Aliyefunikwa na Mabawa
c) Mjumbe
d) Msaidizi

6. Je ? Malaika anaweza kutenda Dhambi ?

7. Ni kitu gani kinacho kudhihirishia kuwa Mungu yupo ?

# *SOMO LA 2*

# ROHO YA MUNGU

### 2.1 Roho ya Mungu: Ufafanuzi

Mungu akiwa ni mtu halisi (ieleweke kuwa tunaposoma mtu hatuna maana kuwa ni Mwanadamu) kwa sababu hiyo anayo mawazo na hisia, basi itegemewe kuwa atakuwa na namna nyingine ya kushirikiana mawazo na nia yake pamoja nasi, watoto wake na kwa kutenda kazi katika maisha yetu kwa mfano ambao una tabia ya sifa yake.Mungu anafanya mambo yote haya kwa 'Roho' yake kama tunataka kumjua Mungu na kuwa na uhusiano wenye matendo pamoja naye, tunahitaji kufahamu jinsi hii " Roho ya Mungu" na namna inavyotenda kazi.

Sio vyepesi kafafanua neno 'Roho' hasa lina maana gani, ikiwa uliwahi kwenda kwenye sherehe fulani, tuseme harusi, unaweza kutoa maelezo ya jinsi mambo yalivyokwenda 'Watu waliohudhuria walikuwa na Roho nzuri' Kwa msemo huu tunaelewa Kuwa una maana kwamba watu walikuwa wakarimu, wenye tabia nzuri n.k. mambo yote hayo yanafanywa na neno 'Roho' iliyokuwepo pale. Hali kadharika Roho ya Mungu kwa njia nyingine inafanya muhutasari wa kila jambo linalo muhusu yeye. Neno la Kiebrania lililotafsiriwa "Roho" kwa lugha yetu katika Agano la Kale kwa uwazi kabisa limefafanuliwa Kuwa ni

“Pumzi” au “nguvu”; kwa hivi roho ya Mungu ni 'Pumzi’ yake, Nafsi ya Mungu kabisa, ikieleza mawazo yake. Tutatoa mifano ya neno 'Roho’ lilivyotumika kuhusu mawazo ya mtu mwingine au mapenzi katika somo la 4.3. Ni dhahiri kwamba Roho sio tu inataja tupu nguvu ya Mungu ni kutoka Warumi 15:19 “Nguvu ya Roho ya Mungu”

Ni mafundisho ya Biblia yaliyo ya kawaida ya kwamba jinsi mtu afikirivyo anajieleza katika matendo yake (Mithali. 23:7, Mathayo. 12:34); mawazo kidogo ya matendo yetu wenyewe, yanadhibitisha jambo hili. Tunafikiria kitu fulani na kisha tunakitenda. “Roho” yetu au nia inaweza kuonyesha juu ya ukweli kwamba tunaumwa njaa na tunahaja na chakula. Tunaona ndizi zimo jikoni, hivyo nia ya'Roho’ wakati huo inabadilika na kuwa tendo. Tunanyoosha mkono na kuchukua ndizi, tunamenya na kula. mfano huu rahisi unaonyesha kwa sababu gani neno'Roho’ lina maana mbili zote Pumzi au Nia, na vile vile Nguvu.Roho yetu ya nafsi yetu, yanatajwa mawazo yetu na hivyo pia matendo tunayofanya ya kuonyesha mawazo hayo au mapenzi yaliyo ndani yetu. Kwa kadri ya utukufu zaidi, Roho ya Mungu ipo hivyo hivyo, ni nguvu inayoonyesha nafsi ya utu wake, mapenzi na kusudi. Mungu anafikiri na hivyo anatenda mambo. “………Kama vile nilivyoazimia (Yaani nilivyofikiria), ndivyo itakavyokuwa, na kama nilivyokusudia, ndivyo itakavyotokea”.

## NGUVU ZA MUNGU

Mafungu mengi ya maneno yanaonyesha Roho ya Mungu na nguvu zake. Kwa kuumba Ulimwengu,’ Roho ya Mungu ikatulia juu ya uso wa maji. Mungu akasema, iwe Nuru:'ikawa nuru’ (Mwa.1:2,3)

Roho ya Mungu ilikuwa ni nguvu / uweza ambao vitu vyote, kama Nuru viliumbwa.'Hizo mbingu hupambwa kwa Roho yake, mkono wake umemchoma nyoka aendaye mbio' (Ayubu. 26:13).'Kwa neno la bwana mbingu zilifanyika: na jeshi lake kwa pumzi ya kinywa chake' (Zab. 33:6). Basi, Roho ya Mungu ni maelezo ya:-

**Pumzi yake**
**Neno lake**
**Mkono wake**

Kwa hiyo ni kwa nguvu zake anafanya vitu vyote. Waumini huzaliwa mara ya pili kwa mapenzi yake (Yoh. 1:13). Ambayo ni Roho yake (Yoh. 3:3-5). Mapenzi yake yanafanya kazi kwa Roho. Akiunena uumbaji wote wa asili, tunasoma "Waipeleka Roho yako, wanaumbwa: nawe (kwa Roho yako) waufanya upya uso wa nchi" (Zab.104:30). Hii Roho / Nguvu vile vile inavihifadhi hai vitu vyote, sawa sawa na kuumbwa kwao. Ni rahisi kudhani kwamba maisha haya yamepatikana kwa bahati bila kuingizwa Roho ya Mungu. Ayubu, mtu aliyechoshwa na maisha haya, alikumbushwa na Nabii mwingine: "(Mungu) akajikusanyia Roho yake na pumzi zake; wenye mwili wote wataangamia pamoja, nao wanadamu watarejea Kuwa mavumbi"(Ayubu. 34:14,15).Alipoondoka katika bonde la mfano mmoja wa huzuni, Daudi alimwomba Mungu aendelee kumtegemeza na Roho hii, yaani, kuhifadhi uhai wake (Zab. 51:12).

Tutaona katika somo la 4.3 Roho ambayo tumepewa sisi sote na viumbe inayohifadhi uhai wetu. Ndani yetu tuna "Pumzi ya Roho ya uhai" (Mwa. 7:22) tuliyopewa na Mungu wakati wa kuzaliwa (Zab. 104:30; Mwanzo. 2:7). Hivi inamfanya awe ni Mungu wa Roho za wenye mwili wote. (Hes. 27:16; linganisha

Ebra. 12:9). Kwa Kuwa  Mungu ni mwenye nguvu ya uhai unaohifadhi viumbe vyote, Roho yake ipo kila mahali. Daudi alitambua kwamba kwa Roho yake Mungu  daima alikuwa naye popote pale alipokwenda, na kwa Roho/ Nguvu aliweza kujua kila kona ya moyo wa Daudi unavyofikiri. Hivyo, Roho ya Mungu ndio inamfanya awe kila mahali, ingawa yeye mwenyewe  makao yake ni mbinguni.

"Wewe wajua kuketi kwangu na  kuondoka kwangu; umefahamu wazo langu tokea mbali..…Niende wapi nijiepushe na Roho yako?  Niende wapi niukimbie uso wako ? Nikikaa pande za mwisho wa bahari; huko nako mkono wako wa kiume utanishika (Yaani, kwa Roho)"  (Zab.139:2,7,9,10).

Jambo hili likifahamika vema linatudhihirishia Mungu  kuwa Mungu ni mwenye nguvu sana, Nafsi itendayo kazi, watu wengi wamepevuka wakiwa hawajui vema'Kusadiki kwa Mungu', katika mioyo yao Mungu amekuwa na wazo tu akilini  akiwa ni sanduku jeusi kumjua Mungu wa kweli  na uwepo wake  kabisa akituzunguka pande  zote kwa roho yake, kunaweza kubadili sana wazo letu la uhai.

Tumezungukwa na  Roho yake,kila siku tunashuhudia matendo yake, yanayotufunulia Mungu alivyo. Kwa yote haya, Daudi alipata faraja  kikamilifu nia yake ilipobadilika:"Maarifa hayo ni ya Ajabu; yanishinda mimi" (Zab. 139:6) Lakini majukumu huja na maarifa haya; inatubidi tufahamu kwamba matendo na mawazo yetu yapo wazi kwenye  mtazamo wa Mungu. kama tunapima hali yetu mbele zake, hasa tukifikiria juu ya Ubatizo, tunahitaji kukumbuka hii moyoni. Maneno makuu ya Mungu kwa Yeremia yanatumika kwetu pia. Je! mtu yeyote aweza kujificha mahala pa siri, nisimwone? asema Bwana. Je! mbingu na nchi hazikujawa (Kwa Roho) nami (Yer.23:24)

## ROHO MTAKATIFU

Tumeona ya kwamba Roho mtakatifu ni wazo pana kufahamu; ni nia na mwelekeo wake, pia ni nguvu inayoweka mawazo yake yafanye kazi. “Maana (Mtu) aonavyo nafsini mwake ndivyo alivyo - yaani, jinsi mtu anavyowaza moyoni ndivyo alivyo, (Mithali 23:7); hivyo basi, ndivyo Mungu mawazo yake yalivyo, kwa maana hiyo ndivyo ilivyo Roho yake (Yohana 4:24). Ingawa hii haina maana ya kwamba Mungu si yake mwenyewe (Tazama tumeacha kitambo tulichoandika sehemu ya 1). Kutusaidia kuelewa upana huu wa roho ya Mungu, mara nyingine tunasoma'Roho wake Mtakatifu’.

Neno “Roho Mtakatifu” linapatikana karibu kila sehemu katika Agano Jipya peke yake. Biblia ya kiswahili maneno Roho ya Bwana na'Roho Mtakatifu’ yametumika wazi. Hili ni sawa na mafungu ya maneno'Roho ya Mungu’ au Roho ya Bwana. Hili lipo dhahiri katika maneno kama ya Matendo 2, yanatoa taarifa ya kumwagiwa mitume Roho Mtakatifu siku ya Pentekoste. Petro alisema kwamba Unabii wa Yoel ulikuwa unatimia, ambapo imesemwa nitawamwagia'Roho yangu’ (Mdo. 2:17). Tena, katika

Luk. 4:1 tunasoma habari ya kwamba Yesu “akiwa amejaa Roho Mtakatifu alirudi toka Yordani; baadae kwenye sura hiyo hiyo Yesu akasema Unabii wa Isaya 61 unatimia. “Roho ya Bwana Mungu i juu yangu”katika masuala yote mawili (na katika mengi mengine) Roho Mtakatifu amelinganishwa na neno lililo katika Agano la Kale “Roho ya Mungu”.

Fahamu vile vile ni jinsi gani Roho Mtakatifu alivyo sambamba na nguvu za Mungu kwenye mafungu ya maneno yafuatayo:-

“Roho Mtakatifu atakujilia juu yako (Mariamu), na nguvu zake aliye juu zitakufunika kama kivuli” (Luk. 1:35)

“Nguvu za Roho Mtakatifu ……. Kwa nguvu za ishara na maajabu, katika nguvu za Roho Mtakatifu” (Rum. 15:13-19)

“(Kuhubiri) Injili yetu kumekuja …… katika nguvu, na katika Roho Mtakatifu” (1 Thes. 1:5)

“Ahadi ya Roho Mtakatifu kwa wafuasi ilisemwa kuvikwa uwezo toka juu” (Luk. 24:49).

Yesu mwenyewe “alitiwa mafuta ya Roho Mtakatifu, na nguvu” (Mdo. 10:38).

Paulo aliweza kutoa mahubiri yake kwa kuonyesha nguvu za Mungu za bila kukanushwa.

“Neno langu na kuhubiri kwangu …….Kwa dalili za Roho na nguvu” (1 Kor.2:4)

## 2.2 Maongozi ya Mungu

Roho ya Mungu tumeifafanua ya kwamba ni Uweza wake, Mawazo, Maelekeo au tabia ambayo anaifunua kwa matendo yanayofanywa na Roho yake. Tulitaja katika sehemu iliyotangulia jinsi gani Roho ya Mungu ilionekana kazini katika uumbaji: “ Hizi mbingu hupambwa kwa Roho yake” (Ayubu. 26:13) -Roho ya Mungu ikatua juu ya uso wa maji kuleta viumbe vilivyopo (Mwa. 1:2). Hata hivyo tunasoma kwamba'Kwa neno la Bwana mbingu zilifanyika, na jeshi lake lote . (Zab. 33:6). Kama ilivyoonyeshwa mfano wa taarifa iliyo katika mwanzo ya Kuwa 'Mungu alisema’ vitu viliumbwa, vikatokea. Kwa hiyo, Roho ya Mungu imeonyeshwa sana kabisa neno lake - kadri maneno yetu

yanavyoonyesha mawazo yetu ya ndani na matakwa - yetu halisi kwa usahihi kabisa. Kwa busara Yesu alisema'Kinywa cha mtu huyanena yaujazayo moyo wake' (Mathayo. 12:34) Basi, kama tunataka kutawala maneno yetu, kabla ya yote yatupasa tugeuze mawazo yetu. Hivyo neno la Mungu, ni wazo la Roho yake au mawazo. Hii ni baraka ya kwamba katika Biblia tuna maneno ya Mungu yameandikwa ili tuweze kuifahamu Roho ya Mungu au nia yake. Mungu alifanya muujiza huu kwa kueleza Roho yake katika maneno yaliyoandikwa kwa njia ya KUVUVIWA. Neno hili msingi wake umezunguka neno'Roho'

## KUVUVIWA -KUONGOZWA NA ROHO

"Roho" inamaanisha "Pumzi" au kupumua, "Kuvuviwa" maana yake ni " Kupuliziwa Pumzi". Hapa pana maana ya kwamba maneno ambayo watu waliandika "Wakivuviwa" toka Mungu yalikuwa ni maneno ya Roho ya Mungu. Paulo alimtia moyo Timotheo kwamba asijione kuwa mzoefu wa Biblia hata asahau ukweli kwamba ni maneno ya Roho wa Mungu, na kwa sababu hiyo tumepewa yote ambayo twahitaji ili kwamba tuwe na elimu ya kweli katika kumjua Mungu:-

"tangu utoto umeyajua maandiko matakatifu, ambayo yanaweza kukuhekimisha hata upate wokovu kwa imani iliyo katika KristoYesu.Kila andiko lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza na kwa kuwaadibisha katika haki, ili mtu wa Mungu awe kamili; amekamilishwa apate kutenda kila jambo jema (2 Tim. 3:15 -17)

Ikiwa kuvuviwa na maandiko kunaweza kutoa elimu ya jumla, basi haipo haja ya kuwa na 'Nuru ya ndani' nyingine ya

kutuonyesha ukweli juu ya Mungu. Lakini ni mara ngapi watu husema mawazo yao wenyewe na ujuzi kuwa ndio chanzo cha wao kumjua Mungu ! ikiwa linakubalika neno lenye kuvuviwa na Mungu kikamilifu linatosha kumwandaa mtu katika maisha ya Ukristo, hakuna haja ya nguvu nyingine ya haki katika maisha yetu. Kama ipo hii haja, basi neno la Mungu halijatuandaa kikamilifu, kama Paulo alivyotuahidi Kuwa litafanya hivyo. Kushika Bibilia mikononi mwetu na kuamini kwamba Biblia ni neno la Roho ya Mungu huchukua imani nyingine kabisa. Israeli walivutwa kusikiliza kile ambacho Mungu katika neno lake, kama ilivyo kwa "Wakristo" wengi siku hizi. Sisi sote tunahitaji kwa uangalifu kuwaza katika Waebrania 4:2:-

"Sisi nasi tumehubiriwa habari njema vile vile kama hao (Israeli walipokuwa jangwani):Lakini neno lile lililosikiwa halikuwafaa hao, kwa sababu halikuchanganyika na imanindani yao walisikia.

Badala ya kusimama katika imani timilifu iliyo kwenye nguvu za Roho / neno la Mungu lililosikiwa, Kiroho ni rahisi kuvutwa na kuchukua njia ya mkato. Kwa kudhani kwamba nguvu ya haki hutujia ghafla juu yetu itakayo tufanya tubadilike mbele za Mungu, kuliko kujua inabidi kupata uchungu wa kuyaleta maisha yetu kutii neno laMungu, kwa hiyo kuruhusu roho ya Mungu ivute mioyo yetu kwa kweli.

Kutopenda kufahamu mno nguvu kubwa za kiroho zilizo ndani ya neno la Mungu matokeo yake'Wakristo'wamediliki kuhoji ikiwa maandiko yote tele yameandikwa kwa uongozi wa roho ya Mungu. Wamedokeza kwamba mengi sana tuyasomayo ndani ya Biblia yameandikwa na watu wenye busara zamani kwa mawazo

yao tu. Lakini kwa matokeo, Petro anakomesha mawazo ya maneno ya jinsi hii:-

"Nasi tuna lile neno la Unabii lililo imara zaidi, ambalo mkiliangalia kama taa….Mkijua neno hili kwanza, (Kuwa muhimu) ya kwamba hakuna Unabii katika maandiko upatao kutafsiriwa kama apendavyo mtu fulani tu. Maana unabii haukuletwa popote kwa mapenzi ya mwanadamu; Bali wanadamu walinena yaliyotoka kwa Mungu, wakiongozwa na Roho Mtakatifu (2Petro. 1:19 -21 UV)

"Zaidi ya yote" yatupasa tuamini kwamba Biblia imeandikwa kwa uongozi wa Mungu.kwa sababu hii tumeifanya kuwa mlango wa msingi mmoja katika mapatano ya maneno yanayoelezea mashauri ya Imani ya Kristadelfiani (Christadelphlan statement of faith)

## WAANDISHI WA BIBLIA

Kwa hiyo, ni muhimu kabisa kuwa na imani thabiti ya kuwa maandiko yamekuja kwa kuvuviwa na Mungu;bila kuzuiwa na mtu, Waandishi wa Biblia walivuviwa na Roho, kwa sababu hii waliyoandika hayakuwa yao wenyewe. Kwa kuwa neno ndio kweli (Yoh.17:17) linakaripia na kuadibisha (2 Tim.3:16 -17), kwa watu wengi, sio ajabu kuona kwamba neno haliwaelimishi - maana ukweli unauma.Nabii Yeremia alisumbuka sana kutokana na upinzani alioupata kwa sababu ya kusema maneno yaliyovuviwa na Mungu, basi aliamua asiyaandike wala kutangaza maneno aliyopewa. Lakini basi kuandika neno la Mungu ni zao la mapenzi ya Mungu kuliko matakwa ya mwanadamu,'Akaongozwa na Roho ya Mungu' kwa hiyo akawa hana uchaguzi wa jambo hili.'Umenihadaa, Nami nimehadaika……Nami nikasema

sitamtaja wala sitasema tena kwa jina lake, basi ndipo moyoni mwangu kumekuwamo kama moto uwakao, uliofungwa ndani ya mifupa yangu, Nami nimechoka kwa kustahimili, wala siwezi kujizuia'. (Yer. 20:7,9).

Vivyo hivyo, Balaamu alipotaka kuwalaani Israeli, Roho ya Mungu ikamfanya awabariki badala yake (Hes. 24:1 -13; Kum.23:5)

idadi ya kushangaza ya watu ambao Mungu aliwaongoza kutamka neno lake, walipita kwenye vipindi vya kutopenda kufanya hivyo. Orodha ni ya kuvutia:-

***Musa (Kut. 4:10)***
***Ezekieli (Ezek. 3:14)***
***Yona (Yon. 1:2,3)***
***Paulo (Mdo. 18:9)***
***Timotheo (1 Tim. 4:6 -14)***
***Balaamu (Hes. 22:24)***

Yote hayo yanatudhibitishia tulichojifunza katika 2 Pet. 1:19 -21 ya kwamba neno la Mungu si wazo la watu binafsi, bali ni sababu ya watu kuvuviwa kuandika yaliyofunuliwa kwao. Nabii Amosi alinena "Bwana Mungu amesema, ni nani awezaye neno ila kutabiri ?" (Amosi 3:8) kwa kitambo, Musa alipoteza akili yake mwenyewe, Kule kuvuviwa kwake na Mungu kulikuwa na nguvu sana: "Maagizo hayo yote Bwana alimwambia Musa……" (Hes. 15:22, 23); maneno haya yalisemwa na Musa hasa (mstari wa 17)

Ushahidi mwingine wa maendeleo haya ni kwamba waandishi wa Biblia hawakutambua kikamilifu mambo waliyokuwa wanaandika. walitafuta maana ya tafsiri sahihi -'Wakafunuliwa

kuwa si kwa ajili yao wenyewe, bali kwa ajili yenu walihudumu katika mambo hayo' waliyoandika (1Petro. 1: 9-12) maneno waliyoandika hasa, hayakuwa ni tafsiri yao wenyewe, bali hayo waliyochunguza. Yafuatayo yanatoa mifano iliyodhahiri:-

***Daniel (Dan. 12:8 -10)***
***Zakaria (Zak. 4:4 -13)***
***Petro (Matendo 10:17)***

Kama watu hawa walivuviwa kwa sehemu tu, basi hatuna njia ya kulifikia neno la kweli au Roho ya Mungu.Ikiwa hakika lile waliloandika lilikuwa neno la Mungu, basi, kwa hiyo iliwabidi waingiliwe kikamilifu na Roho ya Mungu wakati wa kipindi cha kuvuviwa pengine neno la Mungu lisingekuwa limehakikishwa. Kufahamu kwamba neno la Mungu ni la kale kabisa, linatupatia zaidi kusudi la kusoma na kutii.'neno lako limesafika sana, kwa hiyo mtumishi wako amelipenda' (Zab. 119:140)

Kwa hiyo, vitabu vya Biblia ni kazi yake Mungu kwa njia ya Roho yake, kuliko Kuwa na vitabu vya watu.Ukweli wa jambo hili umeonyeshwa kwa kupima jinsi Agano jipya linavyoshuhudia maandishi ya Agano la Kale:-

-Math. 2:5 panasemwa ni jinsi gani 'yaliandikwa na manabii' Mungu alikuwa anaandika kwa kupitia kwao.

- 'Roho Mtakatifu alivyonena kwa kinywa cha Daudi….' (Mdo. 1:16)

-Hivi ndivyo petro alivyonukuu toka Zaburi: linganisha na (Ebra. 3:7)

-'Roho Mtakatifu alinena vema kwa kinywa cha Nabii Isaya' (mdo. 28:25

- ndivyo alinukuu Paulo katika Isaya (Luk 3:4) anasema kama ilivyoandikwa katika chuo cha maneno ya nabii Isaya kuliko kusema, Kitabu cha Isaya tu.

Kwa hiyo wanadamu waliobuni vitabu vya Biblia hawakuwa muhimu kulingana na Wakristo wa kwanza, Ukweli ni kwamba maneno yao yalivuviwa na Roho ya Mungu na ndiyo iliyokuwa ya maana.

Tutamalizia sehemu hii kwa orodha ya mistari inayoonyesha Kuwa Roho ya Mungu imefunuliwa kwetu ndani ya neno lake lililoandikwa:-

-Yesu alisema wazi wazi,'Maneno hayo niliyowaambia... Ni Roho' (Yoh. 6:63);Alisema ni ya kuvuviwa toka kwa Mungu. (Yoh. 17:8, 14:10).

-Tumesemwa ya Kuwa tumezaliwa mara ya Pili pande mbili kwa Roho (Yoh. 3:3-5) na kwa neno la Mungu (1Pet. 1:23)

-'Tazama nitawamwagia Roho yangu, na kuwajulisheni maneno yangu' (Mith. 1:23)yanatia pamoja kufahamu neno la Mungu kweli na tendo la Roho yake juu yetu kusoma kitabu bila kuelewa yaliyoandikwa hakuna faida, kwa kuwa Roho / nia ya Mungu huwa hatujafunuliwa.

Kuna usawa kati ya Roho ya Mungu na neno lake katika mafungu ya maneno: " Roho yangu iliyo juu yako, na maneno yangu niliyoyatia kinywani mwako …." (Isaya 59:21)'Kwa ajili ya neno lako, na kwa moyo wako mwenyewe (Roho)' (2 Sam. 7:21); 'Nami nitatia Roho yangu ndani yenu (katika mioyo yenu, tazama maneno yenyewe)…;

Nitatia sheria yangu ndani yao …… na katika mioyo yao nitaiandika' (Ezek. 36:27, Yer.31:33).

**UWEZA WA NENO LA MUNGU**

Roho ya mungu haishuhudii nia yake / madaraka peke, bali pia ni nguvu ambayo yaelezea mawazo hayo, ya kuwa neno /Roho yake sio tu ni taarifa yake; vile vile kuna nguvu inayofanya kazi katika neno hilo

Kuufahamu ukweli uweza huo kutatufanya tuwe na shauku kuutumia; mawazo yoyote ya kutuzuia kusonga mbele yaliyo pamoja na kufanya hivyo yatashindwa kwa elimu yetu na kutii neno la Mungu kutatupatia nguvu tunazohitaji kusonga mbele kutoka mambo madogo ya maisha haya, kuelekea kwenye wokovu. Kutokana na mengi yaliyompata, Paulo aliandika:-

" Siionei haya Injili (Neno) ya kristo: maana ni uweza wa Mungu uletao wokovu" (Rum.1:16)

Luka 1:37 ameandika jambo lile lile " Hakuna neno (Roho) lisilowezekana kwa Mungu".

Kwa hiyo, kujifunza Biblia na kuyaelewa kuyatumia katika maisha yetu ni mwendo unaoendelea. Hauhusiani kabisa na bila kuwa mwema , kujaribu kufundisha elimu ya kibinadamu na vile vile Ukristo wa makanisa mengi wa kujisikia vema, ambako maneno machache yananukuliwa kifupi, lakini hakuna juhudi imefanywa ili kufahamu au kuyatumia. "Neno la Mungu li hai, tena lina nguvu" 'Kwa amri (Neno) la Uweza (wa Mungu)' (Ebr. 4:12; 1:3).'Neno la ujumbe wa Mungu ….. litendalo kazi pia ndani

yenu ninyi mnaoamini' (1Thes. 2:13). Kwa neno, Mungu anafanya kazi katika mioyo ya waumini wa kweli, kila saa ya siku.

Ujumbe -Msingi wa Injili unaojifunza basi ni uweza kweli wa Mungu; kama ukiuruhusu kweli kufanya hivyo, Injili inaweza kufanya kazi katika maisha yako na kukubadili; uwe mtoto wa Mungu, ukionyesha Roho / nia ya Mungu kwa kiwango fulani katika maisha haya, ukiandaliwa katika badiliko la kupata mwili wa kiroho wa Mungu Kristo atakaporudi (2Pet. 1:4). Mahubiri ya Paulo yalikuwa katika "Kuonyesha dalili ya Roho na nguvu" (1Kor. 2:4).

Tumezungukwa na hao wenye imani nusu katika Biblia kuwa ni Neno la Mungu, mbali na madai ya kumtumikia Kristo. Kwa mfano mmoja wanadai wanamwamini Mungu, Lakini wanashindwa kufahamu kwamba yeye anaishi kweli. Kwa kukana kabisa kuwa maandiko yamevuviwa, na ukuu wake juu ya mwazo na nia zetu, wanakana nguvu za Mungu. Maneno ya 2 Tim 3:5 yanatujia akilini:'Wenye mfano wa utauwa, lakini wanakana nguvu zake' yaani, nguvu za neno la Injili

Msimamo wa imani yetu unadhihakiwa na ulimwengu ('Je ! unaamini kama hivyo, Unaamini ?'), ndivyo Paulo na kundi lake la wahubiri: "Kuhubiri neno la msalaba kwao wanapotea ni upuuzi, bali sisi kwetu tunaookolewa ni nguvu ya Mungu" (1Kor.1:18) Tukikumbuka haya yote, hatuwezi kila mmoja kushika Biblia mikononi mwetu na kipimo kikumbwa cha kuiheshimu, kuisoma na shauku zaidi ya kufahamu na kutii. ?.

## MWENENDO WA WATU WA MUNGU KATIKA NENO LAKE

Kusoma haraka taarifa za Biblia zaonyesha kwamba waandishi wa Biblia sio tu walitambua kwamba walivuviwa, bali waliwaona waandishi wengine wa Biblia kuwa wanaongozwa na Mungu. Bwana Yesu alikuwa ni bora zaidi katika jambo hili. Yesu aliponukuu toka Zaburi na Daudi, alianza maneno "Daudi katika Roho ……" (Math. 22:43), akionyesha kutambua kwake ukweli wa kwamba maneno ya Daudi yalivuviwa. Vile vile aliyasema," Maandishi" ya Musa (Yoh. 5:45-47), kwa kuonyesha kwamba alimwamini Musa kuwa aliandika vitabu vitano. (Pentateuch). Wakristo waitwao watafuta makosawakuu katika Biblia wamekuwa na shaka ikiwa Musa aliweza kuandika, lakini ni dhahiri mwenendo wa Kristo unapingana na njia zao. Aliyaita maandishi ya Musa kuwa ni 'amri ya Mungu' (Marko. 7:8,9)Kundi hilo hilo la wenye mashaka wasioamini wanadai kwamba mengi yaliyo kwenye Agano la Kale ni hadithi, Yesu alisema Malikia wa sheba ukiwa ni ukweli unaofahamika kihistoria (Math. 12:42); hakusema, 'kuwa ni hadithi inayoendelea juu ya Malikia wa sheba ….'

Mwenendo wa Mitume ulikuwa wa hali moja na wa Bwana wao. Umeandikwa kifupi na Petro aliyesema ya kwamba uzoefu wake mwenyewe kusikia maneno ya Kristo kwa masikio yake mwenyewe alipatwa na'Lile neno la Unabii lililo imara zaidi'

(2Pet. 1:19 -21). Petro aliamini kwamba nyaraka za Paulo yalikuwa ni'Maandiko' zaidi kama'Maandiko mengine' msemo ambao kwa kawaida umetumika juu ya Agano la kale maandishi yake. Hivyo, Petro aliona nyaraka za Paulo kuwa ni zenye mamlaka kama Agano la Kale.

Yapo mengi ambayo yametajwa katika matendo, Nyaraka na ufunuo katika Injili (kwa mfano, linganisha (Mdo 13:51, Math.

10:14) yakionyesha sio tu kwamba yote yalivuviwa na Roho yeye yule, bali kwamba taarifa za Injili ziliandikwa kwa uongozi wa Mungu na waandishi wa Agano Jipya. Paulo katika (1 Tim. 5:18 ) ananukuu sehemu mbili Kum.25:4 (katika Agano la Kale) na Luka 10:7 kuwa ni'Andiko'. Paulo alifanya kazi nzito ya maana kwamba ujumbe wake ulitoka kwa Kristo, sio kwake mwenyewe (Gal. 1:11 -12; 1 Kor. 2:13; 11:23; 15:3) kazi yake ilitambuliwa na mitume wengine, hivyo Yakobo 4:5 ananukuu maneno ya Paulo kwa Gal. 5:17 kuwa ni "Andiko"

Mungu 'amesema' nasi kwa Kristo; kwa hiyo hatuna haja na Ufunuo mwingine zaidi (Ebr. 1:2). Yaweza kuonekana kuwa Biblia inataja maandishi mengine yaliyovuviwa yasiyopatikana sasa. (k.m. kitabu cha Yasheri, maandishi ya Nathani, Paulo kwa Wakorintho na waraka wa tatu wa Yohana unadokeza kwamba Yohana aliandika barua ambayo haikutunzwa katika kanisa ambalo Diotrefe alikataa kutii). Ni kwa sababu gani maandishi haya hayakutunzwa kwa ajili yetu ? Ni dhahiri, kwa kuwa mambo yenyewe hayakuwa yanatuhusu sisi.

Mara nyingine imedaiwa kwamba pole pole vitabu vya Agano Jipya vikakubalika kuwa vilivuviwa, Lakini ni hakika kwamba Mitume waliona maandishi ya kila mwingine kuwa yalivuviwa haikosi huku ni kudhibitisha uongo. Ilikuwepo miujiza ya kipawa cha Roho ili kupima ikiwa nyaraka na maneno yaliyodaiwa kuvuviwa kuwa kweli yalikuwa hivyo (1Kor. 14:37, 1Yoh. 4:1, Uf. 2:2). Hii ina maana kwamba nyaraka zilizovuviwa mara moja zilifahamika kuwa zimeandikwa kwa uongozi wa Mungu. Kama ulikuwepo uchaguzi wowote wa Mwanadamu asiyeongozwa kwa yale yaliyoingia katika Biblia yetu, ndipo kitabu kisingekuwa na Mamlaka.

## 2.3 Vipawa Vya Roho Mtakatifu

Kwa nyakati mbalimbali Mungu alipo shughulika na watu, alituma watumie nguvu zake ('Roho Mtakatifu') hao watu. Lakini, nguvu hii haikuwa katika namna ya " Hundi isiyo ya maandishi" kama ilivyokuwa, kuwawezesha kutenda walivyotaka siku zote kutumia Roho huyu Mtakatifu ilikuwa ni kwa kusudi maalumu. Kazi ilipotimizwa vizuri, kipawa cha Roho Mtakatifu kiliondolewa. Yatupasa tukumbuke kwamba Roho ya Mungu hutenda kazi kwa njia ambayo inapelekea mbele kusudi lake lililo moyoni mwake. Mara nyingi lengo lake linaacha muhula mfupi wa mateso katika maisha ya watu ili kuleta karibu kusudi lake la muda mrefu (tazama somo la 6.1) hivyo hatumainiwi huyo Roho Mtakatifu kutumika kutuliza uchungu wa maisha haya katika mwanadamu. Chochote kitulizo hiki kinamalizwa, kitakuwa kwa ajili ya kusudi la hali ya juu kinachoelezea hali ya Mungu kwetu.

Msimamo wa Ukristo wa walio wengi umeonekana kwa namna tofauti kabisa katika Roho Mtakatifu siku hizi; fikira zimetolewa kama kumwamini Kristo kuna thamani fulani kwa sababu ya faida ya mwili, k.m. kuponywa wagonjwa, ambayo Roho Mtakatifu amedhaniwa atatoa uponyaji. Huu utaeleza ni kwa sababu gani nchi zenye vurugu ya vita kama Uganda wamejitokeza watu wanaodai wana vipawa vya Roho ya kuponya na kihistoria mara nyingi kadhia ya jinsi hii ni matukio yanayojitokeza wakati ule ule wanadamu wanapokuwa na shida kubwa. Hii ndani yake yenyewe yanaonyesha madai ya kuwa na Roho katika hali ya mashaka mengine; Ikiwa mtu anatafuta jambo la kumpatia maarifa hayo yaliyo bora kuliko mambo ya

mwanadamu yalivyo, ni rahisi kudai limepatikana jambo lingine linalojaza hesabu.

'Wakristo' wengi siku hizi wanadai wana vipawa vya Roho ya kutenda miujiza, lakini wanapo ulizwa kuhusu nini hasa madhumni yao, wanadokeza maana isiyotumainiwa. Mungu ametoa Roho yake bila kutengwa kwa kutimiza jambo moja hasa, malengo yaliyo ainishwa. Kwa sababu hii wale ambao walikuwa na vipwa vya Roho walijua hasa watavitumia kwa jambo gani. Basi hawakufaulu tu kwa sehemu katika kufanikiwa kwao walipovitumia. Hii hutofautiana na kushindwa kwingi na matibabu nusu yaliyo na wale wanaodai kuwa na vipawa vya kuponya leo.

Mifano yote ifuatayo inaonyesha sababu dhahiri na mambo yaliyokuwa nyuma ya kupewa vipawa vya Roho. Hapakuwepo hata kidogo masuala haya yoyote yanayozungumziwa kuwa pamoja na vipawa, wala hawakuwepo wenye vipawa walioweza kuvitumia kiasi kama walivyoona inafaa. Kwa sababu tunazungumzia Roho ya Mungu, haidhaniwi kwamba watu waliongoza matumizi yake, kwa kuwa walipewa ili kufahamu matakwa fulani ya Mungu kwa namna yake maalumu, kuliko hivyo vya watu walivyotumia hivyo kwa kitambo (Linganisha Isaya 40:13)

-Mwanzoni katika historia ya Israeli, waliagizwa watengeneze hema lenye madoido, ('Maskani') ambalo ndani yake kutakuwa na madhabahu na vitu vitakatifu vingine vitaweza kutunzwa; maelezo yalitolewa jinsi ya kufanya vitu vyote vilivyokuwa vya lazima kwa ajili ya kumwabudu Mungu. Kutimiza hii kazi,Mungu aliwapa watu fulani Roho yake 'Walijazwa Roho ya Hekima ili waweze kushona mavazi ya Haruni …..' (Kut. 28:3)

-Mmoja wa watu hawa, Bezaleli, “Alijazwa Roho ya Mungu, katika hekima na Maarifa, na ujuzi wa kazi ya kila aina ….. kuwa fundi wa dhahabu, na …. Kukata vito kwa kutiwa mahali …. Na kufanya kazi ya ustadi iwayo yote” (Kut. 31: 3 -5).

Kitabu cha Hesabu 11:14 -17 kinatupatia habari ya jinsi baadhi ya Roho /nguvu aliyopewa Musa ilichukuliwa toka kwake wakapewa wazee wa Israeli, kwa kusudi la kuwawezesha kuamua kwa usahihi manung’uniko ya watu na kumpunguzia mzigo Musa. Kabla ya kifo chake, kipawa cha Roho kiliamishwa kutoka kwake akapewa Yoshua ili kwamba, naye vile vile, aweze kuwaongoza watu wa Mungu kwa Uzuri (Kut. 34:9)

Tangu wakati ule watu wa Israeli walipoingia nchi yao hadi kupata mfalme wao wa kwanza (Sauli) waliongozwa na watu walioitwa waamuzi. Wakati wa kipindi hiki watu walionewa na adui zao, lakini kitabu cha waamuzi kimetupatia taarifa jinsi Roho ya Mungu ilivyowajilia baadhi ya waamuzi, kwa muujiza wawaokoe Israeli toka kwa wavamizi wao Othiniel (Amu. 3:10), Gideoni (Amu. 6:34) na Yefta (Amu. 11:29) hawa wanaonyesha mifano hii:-

Mwamuzi mwingine, Samsoni, alipewa Roho ya kumuua Simba (Amu. 14:5,6); kuua watu 30 (Amu. 14:19) na kukata kamba alizofungwa (Amu. 15:14). Huyu'Roho Mtakatifu’ Hakuwa na Samsoni siku zote alimjilia kutimiza mambo dhahiri na kisha aliondolewa.

Mungu alipokuwa na ujumbe maalum na watu wake, Roho ilimwongoza mtu mmoja miongoni mwao kunena neno la Mungu. Ujumbe ulipokwisha, kipawa cha Roho ya kutamka kwa niaba ya

Mungu kiliondolewa mara moja, matamshi ya mtu yanakuwa ni yake mwenyewe tena sio ya Mungu. Moja ya mifano mingi:-

"Roho ya Mungu ikamjia Zekaria ……naye akawaambia (Watu), Mungu asema hivi, kwa nini ninyi kuzihalifu amri za Bwana….? (2 Nyak. 24:20)

Mifano mingine tazama 2 Nyak. 15: 1,2 na Luk. 4:18,19.

Kutokana na jambo hili, inakuwa bayana kwamba kupokea kipawa cha kutumia Roho ya Mungu kwa kusudi maalumu haikuwa

Ni uhakika wa wokovu
Ni jambo lililodumu katika maisha yote ya mtu
Ni nguvu ya Roho iliyojificha ndani yao
Ni jambo fulani linalopatikana kwa mtu kusikia furaha moyoni mwake

Inabidi kusema kwamba kumekuwa na sababu nyingi zisizodhahiri kuhusu vipawa vya Roho mtakatifu. Watu wanadai hupokea Roho Mtakatifu, na katika kumbi nyingi za Injili mhubiri hupunga mikono ya 'Kupokea vipawa vya Roho' mbele ya wale wanaoona 'Wanampokea Yesu' lakini swali inabidi liulizwe, Vipawa gani ? yaonekana kwamba watu hawajui hasa ni kipawa gani wanacho. Samsoni alipewa kipawa cha Roho kuua Simba (Amu. 14:5,6); alipomwona mnyama akiunguruma alijua hasa ni Roho gani aliyopewa na kwa sababu gani. Moyoni mwake hakuwa na shaka yoyote. Hii ni tofauti ngumu kwa wale ambao siku hizi wanadai wamempokea Roho Mtakatifu, huku hawawezi kufanya tendo lolote lililodhahiri, wala kujua ni vipawa gani walivyodhani wanavyo.

Bila shaka hakuna njia nyingine bali kumalizia kwamba watu wa jinsi hii waliwahi kuwa na mkazo wa mawazo mioyoni yaliyounganika na Ukristo, na mzunguko uliofuata katika mwenendo wa maisha yao wakiwa wameachwa na fikira ngeni za upya ndani yao wenyewe. Wakijua hivi, wameshika maneno ya Biblia juu ya vipawa vya Roho Mtakatifu, wakimalizia kwa kusema "Hivi inanibidi kuona mambo yakitendeka ! naye mchungaji wao walio na furaha huwapapasa kichwani na kusema,'Ni sawa hasa !

Bwana asifiwe ! akitumia mambo haya kuwa ni 'Ushahidi' anapojaribu kuwadhibitishia wengine wampokee Roho Mtakatifu. Chanzo cha dhihaka hii hutokana na kukosa kuielewa Biblia tangu mwanzo wa elimu aliyokuwa nayo mtu kabla ya 'Kuongoka' kwao wanakodhania.Tunaposhindana na udanganyifu wa mawazo yetu wenyewe (Yer. 17:9), yatupasa tutunze nyayo zetu juu ya mwamba ulio Imara ya mambo ya Biblia. Hakuna humu kinachohitajika wazi zaidi kuliko kujifunza ni jinsi gani Roho ya Mungu hufanya kazi. sote tunapenda kuwaza Kuwa nguvu za Mungu zatenda kazi nasi katika maisha yetu. Lakini ni jinsi gani na kwa sababu gani anafanya hivyo ? Je ! tuna vipawa kweli vya Roho kama watu walio katika taarifa za Biblia ? kama kweli tunataka kumjua Mungu na Kuwa na uhusuiano ulio hai naye, tutatambua umuhimu unaofaa kuelewa mambo haya.

## SABABU ZA KUWA NA VIPAWA KATIKA KARNE YA KWANZA

Tunapokumbuka mambo makuu tuliyojifunza tayari kuhusu vipawa vya Roho ya Mungu, sasa tunageukia taarifa iliyomo katika Agano Jipya juu ya vipawa vya Roho vilivyokuwa na kanisa la Kwanza (Yaani, vikundi vya waumini walioishi kwenye kizazi kilichokuwapo baada ya kipindi cha Yesu.)

Kristo agizo lake la mwisho, kwa mitume lilikuwa kwenda ulimwenguni pote kuhubiri Injili (Marko.16:15,16). Walilitekeleza agizo hili, na neno la kifo chake Kristo na ufufuo katika ujumbe wao ndio ulikuwa wa Kwanza. Lakini kumbuka kwamba wakati ule halikuwapo Agano Jipya kama tunavyolijua. Kama walivyosimama maeneo ya sokoni na katika masinagogi wakinena kuhusu mtu huyu Yesu wa Nazareti, masimulizi yao yangeonekana ya ovyo -Juu ya seremala toka Israeli aliyekuwa mkamilifu, aliyekufa kisha kufufuliwa kwa utimilifu barabara Agano la kale lilivyotabiri, ambaye sasa alikuwa anawataka wabatizwe na kufuata mfano wake. Katika siku hizo, watu wengine tena walikuwa wanajaribu kuwajenga wafuuasi wa dhehebu. Ikabidi iwepo njia nyingine ya kuwathibitishia ulimwengu kwamba ujumbe ulio hubiriwa na Wakristo ulitoka kwa Mungu mwenyewe, wala si kutoka kwenye elimu ya kikundi cha wavuvi waliotoka Kaskazini mwa Israeli.

Katika siku zetu tunavutwa na taarifa za Aganao Jipya juu ya kazi na mafunzo ya Yesu ili tuhakikishe kwamba ujumbe wetu unatoka kwa Mungu; Lakini katika siku hizo, kabla halijaandikwa na kupatikana, wahubiri walikubaliwa kutumia uweza wa Mungu - Roho wake Mtakatifu ili kutokeza ukweli wa kile walichokuwa wanasema. Hii ilikuwa ni sababu bayana ya kutumia vipawa mbele ya macho ya Ulimwengu; kukosekana Agano Jipya lililoandikwa pia kulifanya iwe shida kwa makundi mapya ya waumini kupevuka katika Imani. Matatizo yaliyojitokeza mengi ya utendaji kati yao yasingelikuwa na ufumbuzi ulio wazi, kwa wao mwongozo ungelikuwa mdogo katika kukua ndani ya imani iliyo kwa Kristo. Basi, kwa sababu hizi, Vipawa vya Roho Mtakatifu vikapatikana ili waumini wa kwanza waongozwe katika ujumbe ulioandikwa kwa uongozi wa Mungu, mpaka taarifa ya Agano

Jipya juu ya ujumbe huu na mafundisho ya Yesu yalipoweza kuandikwa na kusambazwa.

Kama ilivyokuwa, sababu hizi za kugawiwa Roho Mtakatifu kwa wingi ilikuwa dhahiri:-

-"(Yesu) alipopaa kwenda (Mbinguni) ….. akawapa wanadamu vipawa (vya Roho) ….Kwa kusudi la kuwakamilisha watakatifu, hata kazi ya huduma (ya kuhubiri) itendeke, hata mwili wa Kristo ujengwe" yaani waumini (Efe. 4:8,12).

-Basi Paulo aliwaandikia waumini waliokuwa Rumi, 'Natamani sana kuwaona, nipate kuwapa karama ya Rohoni', (Kipawa cha Roho) ili mfanywe imara (Rum. 1:11).

Kuhusu kutumia vipawa kwa kudhibitisha mahubiri ya Injili, tunasoma:-

- "Injili yetu haikuwafikia kwa maneno tu, bali na katika nguvu, na katika Roho Mtakatifu na uthibitifu mwingi" kwa miujiza iliyotendeka (2 Thes. 1:5 linganisha 1:5,6)

-Paulo aliweza kutaja "Neno alilolitenda Kristo kwa kazi yangu, mataifa wapate kutii, kwa neno au kwa tendo (la miujiza) kwa nguvu za ishara na maajabu, katika nguvu za Roho Mtakatifu" (Rum. 15: 18,19)

-Kuhusu wanaohubiri Injili, tunasoma, "Mungu naye akishuhudia pamoja nao kwa ishara na ajabu na nguvu za namna nyingi na kwa mgawanyo ya Roho Mtakatifu" (Waebrania 2:4)

-Kampeni ya kuhubiri Injili kule Kipro ilionyesha maajabu, hata ikawa "Liwali alipoyaona yaliyotendeka, akaamini, akiyastajabia mafundisho ya Bwana (Mdo. 13:12).

Maajabu yalimwongoza aheshimu kwa kweli mafunzo aliyoelimishwa. Vile vile pande za Ikonio, "Bwana … alilishuhudia neno la neema yake, akawajalia ishara na maajabu yatendeke kwa mikono yao" (Mdo. 14:3)

Yote haya yameelezwa kwa kifupi juu ya utii wa mitume kufuatia yale waliyoambiwa wahubiri: “ Wakatoka na kuhubiri kila mahali, Bwana akitenda kazi pamoja nao, na kulidhibitisha neno kwa ishara zilizoambatana nalo” (Marko. 16:20).

**MAMBO DHAHIRI KATIKA NYAKATI ZA NAMNA YAKE MAALUM.**

Kwa hiyo, hivi vipawa vya Roho vilitolewa ili kufanya mambo dhahiri katika nyakati za namna maalumu .hivi laonyesha kosa la kudai kwamba Kuwa na kipawa cha Roho ni maisha yote ya mtu. Mitume, akiwemo Petro, “Walijazwa na Roho Mtakatifu siku ya Pentekosti, baada ya Yesu kupaa (Mdo. 2:4) kwa hiyo waliweza kunena kwa Lugha ngeni ili kuanzisha kuhubiri Injili ya Kikristo kwa kuitangaza kwa watu. Wenye mamlaka walipojaribu kuwatia nguvuni, “Petro akajaa Roho Mtakatifu” akaweza kuwajibu na kuwadhibitishia …. (Mdo. 4:8). walipoachiwa toka gerezani wakaweza kuendelea kuhubiri kwa usaidizi wa vipawa -“Wote wakajazwa Roho Mtakatifu, wakasema neno la Mungu kwa Ujasili” (Mdo. 4:31)

Msomaji mwangalifu ataona kwamba taarifa haisemi kwamba'Tayari walikuwa wamejaa Roho’ Walijazwa na Roho Mtakatifu kufanya mambo halisi, lakini ilibidi wajazwe tena ili kutimiza jambo lingine katika mpango wa Mungu. Paulo vile vile “Alijazwa Roho Mtakatifu” alipobatizwa, lakini miaka mingine baadae “alijazwa tena Roho Mtakatifu” ili kumwadibu mtu mwovu kwa kumpiga upofu (Matendo. 9: 17; 13:9)

Katika kusema vipawa vya miujiza, Paulo aliandika kwamba waumini wa kwanza walipata “ Kadri ya kipimo cha kipawa chake Kristo” (Efe.4:7). Neno la Kiyunani 'Kadri ya kipimo’ maana

yake “Sehemu ndogo au Kiasi”. Yesu peke yake ndiye aliyekuwa na vipawa bila kipimo, yaani alikuwa na uhuru wote wa kutumia kama alivyotaka (Yoh. 3:34). Sasa tutafafanua hivyo vipawa vya Roho vinavyoonekana kutajwa zaidi walikuwa navyo katika karne ya kwanza.

## VIPAWA VYA ROHO KATIKA KARNE YA KWANZA

### UNABII

Neno la Kiyunani'Nabii’ maana yake ni mtu anayetabiri neno la Mungu kwa mambo yaliyombele kabla jambo halijatokea - Basi ni kusema kwamba ni mtu aliyevuviwa kunena maneno ya Mungu, ambayo katika vipindi yalikuwa yanatabiri matukio ya wakati ujao (tazama 2 Pet. 1:19 -21). Hivyo,'Manabii’ - hao walio na kipawa cha kutoa unabii 'Walitoka Yelusalemu kwenda Antioki. Akasimama mmoja wao aliyeitwa Agobo, naye alionyesha ishara kwa Roho ya Kuwa itakuwepo njaa kubwa ulimwenguni pote: ilitokea katika siku za Klaudio Kaisari. Ndipo wanafunzi, kila mtu kwa kadri ya uwezo wake waliamua kutuma msaada kwa ndugu’ (Mdo. 11: 27 -29). Aina hii ya Unabii dhahiri, wa hali ya juu. Ambao ulikuwa wazi na ukamilifu ulikuwa kwa miaka michache, unakosekana kabisa miongoni mwao ambao sasa wanadai wana kipawa cha unabii; kweli, ni hakika mno kuwa katika kanisa la kwanza hiki kipawa kilikuwemo kati yao kwa kweli, hata walitoa muda wao na pesa ili kukabiliana na shida iliyokuwa imetabiriwa. Mifano michache ya jambo la aina hii yaweza kupatikana makanisa yaitwayo leo'Yaliyojazwa Roho’.

### UPONYAJI

Kwa Kuwa mitume walikuwa wanahubiri habari njema (Injili) ya ufalme ujao wa Mungu wenye ukamilifu duniani,

walifaa wauthibitishe ujumbe wao kwa kuonyesha miujiza ambayo ilionjesha kwa sehemu kipindi hicho kitakachokuwa, hapo “Macho ya vipofu yatakapofumbuliwa na masikio ya viziwi yatapozibuliwa. Ndipo kilema ataruka ….” (Isaya 35: 5- 6). Zaidi kuhusu hali ya mambo kwenye ufalme wa Mungu tazama somo la 5. Ufalme wa Mungu utakaposimikwa duniani, ahadi za jinsi hii kama hizi hazitatimia kwa nusu kipimo, wala ufalme kutokuwa halisi hapa au sivyo. Kwa hivyo uthibitisho wa Mungu kwa huo ujumbe waufalme ulikuwa katika nguvu, wazi wazi usioweza kukanushwa; kwa hoja hii mingi ya miujiza ya uponyaji iliyofanywa na waumini wa kwanza ilikuwa machoni pa watu wote waweze kuona.

Mfano mashuhuri unapatikana pale Petro alipomponya mwombaji kilema aliyewekwa kila asubuhi penye mlango wa hekalu katika Matendo 3:2 tunasoma kuwa walimuweka kila siku - hivyo alizoeleka sana machoni pa watu. Akiisha ponywa kwa karama ya Roho iliyotumiwa na Petro, “Akaondoka upesi akasimama, akaanza kwenda, akaingia ndani ya Hekalu pamoja nao akaenda kuruka ruka … watu wote wakamwona akienda, akimsifu Mungu. Wakatambua ya Kuwa yeye ndiye alikuwa akiketi na kuomba sadaka kwenye mlango mzuri wa Hekalu; Basi, alipokuwa akiwashika Petro ….. watu wakamkusanyikia mbio katika tao … wakishangaa sana” (Matendo ya Mitume 3: 7 -11)

Ndipo Petro akaanza mara moja kusema kwa sauti kuhusu ufufuo wa Kristo. Wakiwa hawana la kuuliza, na wanapouona ushuhuda usiopingika mbele ya macho yao katika namna ya mwombaji aliyeponywa, tunaweza Kuwa na hakika ya kwamba waliyaelewa maneno ya Petro Kuwa yametoka kwa Mungu. Mlangoni mwa Hekalu “Saa ya Kusali” (Mdo. 3:1) Watu walikuwa wamesongamana, kama kwenye duka watu wanavyosongamana.

Ilikuwa ni mahala kama hapo, Mungu alichagua kudhibitisha mahubiri ya neno lake kwa Muujiza huu uliodhahiri. Vivyo hivyo katika matendo 5:12 tunasoma ya kwamba “Kwa mikono ya mitume zikafanyika ishara na maajabu mengi katika watu”. Kadhia zifanywazo na wapentekosti wanaoponya na wengineo huzunguka mambo yaliyotokea pembeni mwa makanisa, kuliko njiani palipo wazi ili watu waone, na katika mkusanyiko wa'Waumini’ walio katika hali ya Roho ya kutazamia'Ishara’itokee, kuliko mbele ya watu wote wenye mioyo migumu.

Acha isemwe hii nafasi kwamba mwandishi wa sasa amekuwa na ujuzi mkubwa wa kujadili matukio haya na wanaodai siku hizi wamekuwa na Roho. Vile vile kwa kushuhudia kadhia nyingi za walio na Roho. Lakini 'Ushuhuda wangu mwenyewe’ wa kuona uponyaji mwingi ni ambao hauko dhahiri, na katika tiba nzuri sana kwa sehemu, haitakiwi kuwa katika mwendo wa kuzidi kutia maelezo; Mshirika yeyote wa makanisa haya mwaminifu atakubali kwamba mengi ya haya yanaendelea. Kwa nafasi nyingi nimezungumza na rafiki zangu wapentekoste wazuri, “Sio kwamba sipendi kuamini kuwa unaweza kuwa na uweza huu mkubwa. Lakini Mungu katika nyakati zote ni bayana ameonyesha ni nani aliye na nguvu zake na nani hana; hivyo si vibaya kwangu kukuuliza hali ya mafundisho yako, ambayo kwa sasa siwezi kwa kuwa hayawezi kupatana na maandiko” Kamwe hujawa bayana 'Kufafanua Roho na Nguvu’ kwa kunieleza mimi.

Kwa namna nyingine kabisa na kwa kufikiri kwangu, Wayahudi wenye msimamo mkali wa karne ya kwanza walifunga mioyo yao katika uwezekano wa kwamba wakristo walikuwa na vipawa vya kufanya miujiza ya Roho ya Mungu. Lakini hata hivyo iliwabidi wakubali, “Mtu huyu anafanya Ishara nyingi” (Yoh. 11: 47) na “Ishara mashuhuri imefanywa nao … ni dhahiri kwa watu

wote wakaao Yerusalemu; wala hatuwezi kuikana" (Mdo. 4:16). Vivyo hivyo wale waliosikia mitume wakinena kwa lugha' Walishikwa na fadhaa" (Mdo. 2:6). Wapentekoste waongeao bila busara siku hizi hawafanyi hivyo. Ukweli ni kwamba watu wameweka katika hali inayofaa sana kwa 'Wapentekosti' wa sasa na kuweza kukana kwamba kwa kweli wanatimiza miujiza, hapana shaka ni hatua ya maana kwa mjadala huu. kama ishara moja tu imekuwa ni habari kuu Yerusalemu pote, Je ! si haki kutoa shauri la kwamba ikiwa muujiza wa kweli ulifanywa Uingereza au bustani iliyo Nairobi, wakati huo kungekuwa na kutambua ya kwamba vipawa vyenye miujiza ya Roho ya Mungu vipo leo ? Badala yake, Wapentekosti wanangojea ulimwengu ushikilie aina zifuatazo za 'Ushahidi' kuwa ndio sababu zao za kuamini :-

-(Hatimaye) kuponywa vidonda vya tumbo; njia ya kupona imedhaniwa ilianza baada ya mkutano wa maombi.

-Sehemu za mwili zilizolemaa kunyooka.

-Macho au Masikio yakipona, ingawa mara nyingi hali hurudi kama awali.

-Kuondolewa misiba mwilini.

Katika mifano hii inabidi kujumlisha kwa kusema kuwa magari ya kubebea wagonjwa yaliwachukua wagonjwa toka Hospitali hadi kituo cha Krusedi ya uponyaji cha T.O Osborn kilicho Nairobi, nchini Kenya; Madereva walikabiliwa na mashaka ikiwa wakae au warudi, walisalia - vile vile wagonjwa hawakupata ahueni yoyote.

Hata hivyo changamoto inataka watu waje kwenye mikutano hii kama matangazo yasemavyo:-" Njooni mtarajie Muujiza" kwa matakwa ya Roho ya binadamu namna zote hatua imepangwa

inayotoa shauri yenyewe kama mfano huu. Hakuna mahala popote katika Agano Jipya panapodokeza kidogo mambo haya mengi ya matakwa ya Roho ya binadamu yenye lugha laini iliyohitajika kabla ya kutokea Muujiza au ishara. Ni dhahiri kwamba baadhi ya wale walioponywa katika karne ya kwanza hawakuwa na imani - k.m. mtu mmoja hakumjua Yesu alikuwa ni nani (Yoh. 5: 13; 9:36) .

Mfano mmoja wa Roho ya kuhoji -hoji unatimizwa na akili iliyopotoka na maombi yanayorudiwa mara ya pili, Sauti za ngoma na mziki wenye sauti. hapawezi kuwa na shaka kama ya busara yoyote kumjua Mungu - na jambo lolote lingine - kwa yote hayo yapo nje ya maana. mwandishi ameweza kukumbuka alivyohudhuria mikutano kadhaa katika sehemu mbali mbali, kila wakati alijisikia kuumwa kichwa kutokana na bidii ya kuendelea kuwa na busara iliyo sawa sawa, Ufahamu wa Biblia kwa kukabili jaribu la kutaka kupotezwa na mlio wa Ngoma na kupiga makofi. Kama yote hayo yanaonekana kuwa ya lazima kutangulia kabla ya kufanywa “Ishara” ya Wapentekosti basi ni ushahidi wa kutosha kwamba 'Uponyaji’ ni matokeo ya hangaiko la moyo na kutengenezwa Roho ya mwanadamu, kuliko shughuli moja kwa moja ya Roho ya Mungu. Kwa namna nyingine kabisa, Petro aliweza kutumia karama ya kweli ya ishara kwa kuponya watu walipolala katika njia kuu (Mdo. 5:15); Kutumia Paulo karama zenye miujiza mwenyewe alishuhudiwa na mtumishi wa Serikali asiyeamini (Mdo. 13: 12,13), vile vile na wapagani walioishi katika mji wa Listra (Mdo. 14: 8 - 13). Kama zilivyotakiwa kwa kusudi kabisa na hali ya karama za Roho, mambo ya uponyaji yalifanywa hadharani, na kwa njia yoyote hakukuwa na dalili ya kusita na maelezo mengine yoyote ila kukubali ya kwamba hapa kuna nguvu za Mungu zinazoonyeshwa dhahirii na watumishi wake.

Tokeo moja ambalo Kristo alionyesha uponyaji wa miujiza lilikuwa jinsi hii “Wakastaajabu wote (Yaani walioona), wakamtukuza Mungu, wakisema, Namna hii hatujapata kuona kamwe” (Marko. 2:12).

**LUGHA**

Mitume, baadhi yao walikuwa ni wavuvi wasiotengenezwa vizuri (k.m. Kielimu), walipata agizo kubwa la kwenda ulimwenguni pote, wakahubiri Injili (Marko. 16: 15, 16).Labda wazo lao la kwanza hasa lilikuwa,‘Lakini sijui kusema lugha nyingine !’ kwa wao halikuwa suala la 'Sikujifunza vizuri lugha nilipokuwa shuleni’ maana hawakuwa na shule. Juu yao wote imeandikwa ya Kuwa ni'Watu wasio na elimu, na wasio na maarifa’ (Mdo. 4:13) lilipokuja jambo la aina hiyo. hata kwa wahubiri walioelimika zaidi (k.m Paulo), Lugha ilikuwa bado ni kikwazo kikubwa kushindana. walipofanyika waongofu, tegemezi walilohitaji Kuwa nalo ni juu ya kila mmoja kwa kujengana (Agano Jipya lilipokuwa bado halijaandikwa) maana yake ilikuwa kwamba kutokuelewana lugha na kila mmoja lilikuwa ni tatizo kubwa.

Katika kushinda hili, wakapewa karama ya kunena katika lugha ngeni (‘Ndimi’) na kuweza kuzifahamu. Ni bayana kuna upinzani kabisa kati ya mtazamo huu wa 'Ndimi’ na huu wa Wakristo wengi waliozaliwa mara ya pili, wanaoeleza matamshi yao yenye furaha katika sauti zisizotambulika Kuwa ni ndimi. Mtafaruku huu unaweza kuondolewa kwa kuonyesha kwamba Biblia inaposema “Ndimi” ni'lugha ngeni’.

Siku ya Pentekosti, ambayo ni sikukuu ya Wayahudi, mapema baada ya kupaa juu mbinguni Kristo, mitume " Wote walijazwa Roho Mtakatifu, wakaanza kunena lugha nyingine ….. Makutano wakakutanika (Mara nyingine karama ikaonyeshwa !). wakiwa wameshikwa na furaha, kwa Kuwa kila mmoja aliwasikia akinena kwa lugha yake. Wakashangaa wote, wakastaajabu na kuambiana, Tazama, hawa watu wasemao si wagalilaya hao ? Waparthi, Wamedi … tunawasikia hawa wakisema kwa lugha zetu … wakashangaa wote"(Matendo ya mitume 2: 4-12) Haielekei ya kwamba huu mkazo maradufu wa mshangao wa watu na kustaajabu kwao ulikuwa wa lazima ikiwa walisikia mambo yasiyo na maana tu yakinenwa na hao wenye kadhia ya Kuwa na karama siku hizi.; yanayozuka katika maneno madogo ya uchokozi au kutopendelea, kuliko mshangao na uthibitisho unaotokana na kufahamu maneno yaliyonenwa, yaliyoshuhudiwa katika matendo 2.

Katika matendo ya mitume 2: 4-11 lugha zilizoandikwa zipo bayana na sehemu nyingine ya maandiko ya Agano Jipya; maneno "Watu wa kila Taifa na Lugha" yametumika mara tano katika Ufunuo kwa kusema watu wote walio kwenye sayari -dunia hii (Uf. 7: 9, 10:11, 11:9, 13:7, 17:15).Neno la Kiyunani' Ulimi'linatokea katika toleo la Kiyunani la Agano la Kale (Liitwalo'Septuagint') na maana ya lugha (tazama mwa. 10:5, Kum. 28:49, Dan. 1:4) - katika Biblia yetu ya Kiswahili Kum. 28:49 ni sawa na Kiyunani.

1 Kor. 14 ni orodha ya maagizo yahusuyo kutumia kipawa cha Ulimi; mstari. 21 unanukuu Isaya 28:11 kuhusu ni jinsi gani kipawa hiki kitatumika kwa kushuhudia juu ya Wayahudi:'Katika sheria imeandikwa, kwa midomo (Ulimi) ya watu wageni na kwa lugha nyingine atasema na watu hawa' Kwa awali Isaya 28:11

inataja wavamizi wa Israeli wakisema na wayahudi kwa lugha ("Ndimi") ambazo hawakuzifahamu. Usawa uliopo kati ya 'Ulimi' na 'Midomo' unaonyesha ya kwamba 'Ndimi' zilikuwa ni lugha ngeni. vipo vionyesho vingi vingine katika 1 Kor. 14 vya kwamba "ndimi ni lugha ngeni. Sura hii ni hukumu ya Paulo iliyovuviwa yenyewe kuhusu matumizi mabaya ya karama yaliyokuwa yanafanywa katika kanisa la kwanza, kama hivi, yanatoa namna nyingi juu ya ufahamu wa karama za Ulimi na Unabii. Sasa tutajaribu kutoa jumla ya fafanuzi chache juu yake. Aya ya 37 ni mstari wa kufungua:-

"Mtu akijiona Kuwa ni nabii , au mtu wa Rohoni, ayatambue hayo ninayowaandikia ya kwamba ni maagizo ya Bwana"

Ikiwa mtu awaye yote anadai Kuwa na karama ya Roho, yampasa akubali kwamba maagizo yanayotangulia juu ya kutumia karama ni kwa kuvuviwa na Mungu. Awaye yote ambaye anaasi hizo amri leo basi ni dhahiri wanakubali kwamba wanaona inafaa kudharau maneno yaliyoandikwa kwa Uongozi wa Mungu.

**Aya ya 11 -17:-**

"Basi nisipoijua maana ya ile sauti nitakuwa kama mjinga kwake yeye anenaye, naye anenaye atakuwa mjinga kwangu.

Vivyo hivyo nanyi, kwa kuwa mnatamani sana kuwa watu wenye karama za Rohoni, takeni kwamba mzidi sana kuwa nazo ili kulijenga kanisa.

Kwa sababu hiyo yeye anenaye kwa lugha na aombe apewe kutafsiri

Maana nikiomba kwa lugha, Roho yangu huomba, lakini akili zangu hazina matunda.

Imekuwaje basi, Nitaomba kwa Roho, tena nitaomba kwa akili pia, nitaimba kwa Roho, tena nitaimba kwa akili pia.

Kwa maana wewe ukibariki kwa Roho, yeye aketiye mahali pa mjinga ataitikiaje, Amina, baada ya kushukuru kwako, akiwa hajui usemalo.

Maana ni kweli, wewe washukuruu vema,bali yule mwingine hajengwi.

Basi kunena kwa lugha ambayo wale walio katika ibada hawaelewi haina maana. “Kusema bila maana nzuri” hakufai, maana ni jinsi gani yaweza kusemwa “Amina” ya ukweli mwishoni mwa 'Sala' iliyoundwa kwa kupayuka -payuka kusikoweza kufahamika ? kumbuka kwamba “Amina” maana yake “Iwe hivyo’ yaani, nakubali kabisa na kilichosemwa katika sala hii. kunena lugha isiyoeleweka mbele za ndugu zako haiwajengi, asema Paulo.

Ninaukumbuka ugawaji vitabu vidogo nje ya ya mkutano wa kufukuza maovu uliofanywa na Billy Graham,wakiombwa watu warudi tena katika Ukristo ambao msingi wake ni katika Biblia. Mwanamke aliyeshikwa na msisimko akajaribu kunivuta kwa maneno yake ya kwamba mafundisho yangu ya Kristadelfiani 'Yaliongozwa na Ibilisi’ kwa kupayuka katika 'lugha’ kwa muda wa dakika 10. Kwa namna yoyote sikuweza 'kujengwa’ na hiyo, kwa kweli jambo hili ndilo hasa lile Paulo aliagiza lisifanywe kabisa.

**Aya ya 18:-**

“Namshukuru Mungu ya Kuwa nanena kwa lugha zaidi ya ninyi nyote”

Kwa sababu ya kusafiri kwake katika maeneo mbali mbali kumhubiri, Kristo, Paulo alihitaji karama ya lugha ('Ulimi') zaidi kuliko wote.

**Mstari wa 19:-**

"Lakini katika Kanisa napenda kunena maneno matano kwa akili zangu nipate kuwafundisha wengine, zaidi ya kunena maneno kumi elfu kumi kwa lugha". Hivi ni wazi kabisa. Mimi nitafanya vema kumhubiri Kristo kwa sentensi chache zilizo katika lugha ya Kiswahili kuliko mimi kuhubiri masaa mengi kwa lugha ngeni - au kuongea maneno yasiyofahamika vema.

**Mstari wa 22:-**

"Basi, hizi lugha ni ishara, si kwao waaminio bali kwao wasioamini, lakini kuhutubu si kwa ajili yao wasioamini bali kwao waaminio". Kwa hiyo matumizi ya lugha yalitakiwa yatumike zaidi katika kwenda nje kuhubiri Injili. Lakini wote wenye kadhia ya kunena kwa 'Lugha' watoka miongoni mwa makundi ya 'Waaminio' au (Kwa kuonekana) kwa mmoja wao anayepata wakati akiwa peke yake. Upo ukosefu sugu kwa mifano ya watu hawa ya kuweza kunena kimaajabu kwa lugha ngeni ili kueneza Injili. Mwanzoni mwa miaka ya 1990

ulifunguka mlango mpana katika kuhubiri Injili ya Kristo pande za Ulaya Mashariki, Lakini makanisa (yanayojiita) ya 'Kiinjili' ilibidi yagawe vitabu vyao vilivyo na lugha ya Kiingereza kwa sababu ya vizuizi vya lugha ! kwa kweli karama ya kunena kwa lugha mpya ingetumika ikiwa walikuwa nayo ? naye Mwinjilisti wa mikutano mikubwa Reinhardt Seiber, huku akiwa na kadhia ya kuwa na Roho kwa ajabu bado ilimbidi aseme na makutano kwa kumtumia mkalimani pande za Kampala, Uganda.

**Aya ya 23:-**

"Haya ! Ikiwa kanisa lote limekusanyika pamoja, na wote wanene kwa lugha, kisha ikawa wameingia watu wajinga au wasioamini, Je ! hawatasema ya kwamba mna wazimu ?" . Hili ndilo jambo hasa limetokea. Waislamu na wapagani pamoja wamedhihaki mwenedo wao wa ovyo (Upuuzi) wa hao wanaodai wanacho kipawa cha ulimi Afrika Magharibi pote. Hata mkristo aliye sawa akilini akitega sikio kuzunguka kona ya mkutano wa Wapentekoste atadhania ya kuwa washirika walikuwa na wazimu.

**Aya ya 27:-**

"Ikiwa mtu akinena kwa lugha, wanene wawili au watatu, si zaidi, tena zamu kwa zamu, naye mtu mmoja atafsiri". Watu wawili watatu ndio waliohitajika kunena wakati wa Ibada. Haielekei kwamba walikuwepo wenye lugha zaidi ya tatu tofauti zilizosemwa na wasikilizaji wowote. Ibada itakosa mshikamano wote muda mfupi ikiwa kila sentensi ya msemaji ikibidi itafsiriwe zaidi ya mara dufu. Ikiwa karama ya lugha imekuwepo kwenye mkutano uliofanyika katikati ya jiji la Dar -es -Salaam, wamehudhuria watu wanaoongea Kiswahili, na wengine ni Waingereza na Wajerumani wakiwa ni watalii waliohudhuria,

Wanenaji wanaweza kuanza :-

Mtumishi: Habari za jioni.
Lugha ya msemaji wa kwanza: Bon Soir (Kifaransa)
Lugha ya msemaji wa pili: Guten abend (Kijerumani)

Lakini kwa kawaida wanapaswa kunena " Kwa zamu", anaanza mmoja baadaye afuate mwingine. Utatokea mtafaruku kwao wakinena kwa wakati huo huo; lakini kwa sababu ya msimamo uliopo unaochochewa na mawazo ya 'Kunena kwa Lugha', tukio linakutwa katika vichwa vya watu wengi wakati

huo huo. Tumegundua kwamba mara mtu mmoja akianza, wengine nao upesi wanavutwa kufanya hivyo hivyo.

Karama ya Lugha mara nyingi ingetumika pamoja na hiyo ya kutoa Unabii, ili kwamba ujumbe uliovuviwa kutoka kwa Mungu utabiriwe (kwa kutumia kipawa cha kutoa Unabii) mfano wa kutumia jinsi hii vipawa viwili unaweza kupatikana katika

Mdo. 19:6. Lakini, ikiwa kwenye mkutano mjini Dar -es-Salaam ukihudhuriwa na watu wa Tanzania na wafaransa wengi wageni, msemaji akinena kwa kifaransa, watu wanaoongea kiswahili waliopo'Hawajengwi'. Kwa hiyo kipawa cha kutafsiri ulimi

(au Lugha) kingekuwepo, ili kwamba kila mmoja aweze kufahamu, kama -katika mfano wetu siku hizi, katika kutafsiri toka kifaransa kwenda kiswahili au Kifaransa kwenda kiingereza. Vivyo hivyo ikiwa swali limeulizwa na mtu anayeongea kifaransa, mnenaji hawezi kumwelewa bila msaada, hata kama alikuwa na karama ya kunena kwa kifaransa pasipo mwenyewe kukielewa. Kwa sababu hiyo kipawa cha kutafsiri kitakuwepo kusaidia suala hili.Bila kuwepo mtu mwenye kipawa cha kutafsiri kinapohitajika, kipawa cha ulimi hakitatumika:" …….. mmoja na afasiri. lakini asipokuwepo mwenye kutafsiri na anyamaze katika Kanisa (1 Kor. 14:27,28). Jambo la hakika ni kwamba watu wengi siku hizi walio na kadhia ya kuwa na Karama ya'Ulimi' wananena kwa 'lugha' ambazo haziwezi kueleweka na yeyote, na bila mwenye kutafsiri, ni hakika suala la uasi kwa maagizo haya.

**Mstari wa 32, 33 :-**

"Na Roho za manabii huwatii manabii. Kwa maana Mungu si Mungu wa machafuko, bali wa amani, Vile vile kama ilivyo katika makanisa yote ya Watakatifu."

Kwa hiyo tendo la kuwa na karama za Roho Mtakatifu lisitiwe pamoja na ujuzi anaomchukua mtu nje ya mambo ya ufahamu wa kawaida; Roho huwa chini ya uongozi wa mtumiaji, kuliko lazimisho linalo wachukua upande mwingine ili kwamba watende bila kujua mara nyingi kwa makosa imedaiwa kwamba mashetani au 'Roho wachafu' huwamiliki'Wasiookoka' (tazama somo la 6.3), Bali ni kwamba Roho Mtakatifu wanajazwa waaminio. Lakini nguvu za Roho zilizotajwa katika 1 Kor. 14:32 zilikuwa chini yake mwenye kuiongoza kwenye kusudi la namna yake maalum; haikuwa shurutisho hai la wema ikipambana na nguvu ya uovu iliyo ndani ya mwili wa mwanadamu. Isitoshe awali tumeonyesha ya kwamba nguvu hizi za Roho Mtakatifu ziliwajia mitume wakati fulani ili kufanya mambo ya namna yake maalum, si kuwa nazo daima.

Ombi kwa wenye Kuwa na karama watumie kwa namna inayofaa upendo na amani ya Mungu na kuchukia machafuko (aya ya 33) Laonekana limeangukia kwenye masikio ya viziwi katika makanisa ya wa -Pentekosti wa siku hizi.

**Aya ya 34: -**

"Wanawake wanyamaze katika kanisa, maana hawana ruhusa kunena bali watii kama vile inenavyo torati nayo." Katika fungu hili la kutumia karama za Roho, hakujawekwa kukatazwa ya kwamba wanawake wasitumie karama wakati wa ibada ya kanisa. kutoangalia hili kwa upana linatarajiwa ikiwa jambo lililopo la kunena kwa 'Machafuko ya kupayuka' laweza kuelezewa kwa maneno ya kuchochewa mawazo likipita toka kwa mtu mmoja hadi mwingine katika mkusanyiko wao. Wanawake, Watoto - na yeyote anayekuwapo kwa hiyari - anaweza kuambukizwa na msimamo wa jinsi hii, kwa hiyo wanafanya matamshi ya kusikia furaha moyoni, yanayoishia kuwa kama ni 'lugha'.

Wanawake wajitokezao kwa kusemwa 'Wananena kwa lugha' na 'kutoa Unabii' katika makanisa ya sasa hawapatani na agizo lililo wazi la aya hii. Maneno ya Upuuzi, ambayo ni mabaya yatokayo kwa watu ya kwamba Paulo alikuwa mchukia wanawake yamezimwa kwa aya chache baadaye: “Mtu akijiona kuwa ni nabii au mtu wa Rohoni, na ayatambue haya ninayowaandikia ya kwamba ni maagizo yatokayo kwa Bwana” (1Kor. 14:37) siyo ya kutoka kwa Paulo mwenyewe.

Awaye yote aaminiye Biblia kuwa imevuviwa, basi, inambidi akubali kwa maagizo haya yaliyo katika 1 Kor. 14 si ya kufanyia mchezo bayana wa kuyabeza; kufanya hivyo kunaashiria kutokuwa na imani ya kutosha katika maandiko kwamba yameandikwa kwa uongozi wa Mungu pekee - au maneno yenyewe yajieleze kwamba huyu mtu hana karama ya Roho, kwa kuwa mtu mwingine asiye na karama atakana kwamba maagizo yaliyo katika 1 Kor. 14 ni maagizo ya Bwana yaliyo kwa ajili yetu.

Kuwanza kwa akili timamu maneno haya yatuambia, yanaharibu sana. katika mwangaza huu, ni vipi uweze kusalia Kuwa mshirika wa kanisa hili,au kupenda kufanya ibada nao.

Maneno yakiwa chini ya kitabu kwa sehemu hii, ni yenye maana sana ya kwamba hayo madhehebu yenye kadhia ya kunena kwa lugha yamedhibitishwa kisayansi Kuwa na huzuni upesi kulinganishwa na watu walio katika malezi mengine. Keith Meador, Profesa wa magonjwa ya moyo katika chuo kikuu cha Vanderbilt, Marekani, alianza uchunguzi mkubwa kujifunza kuchanganua uhusiano uliopo kati ya huzuni iliyo moyoni na malezi yaliyo katika dini. Aligundua kwamba “ Idadi kubwa ya

wenye huzuni ….. miongoni mwa Wakristo wa madhehebu ya Kipentekosti ilikuwa 5.4% kulinganishwa na 1.7 % kwa uchunguzi wa kundi zima" matokeo ya kazi hii yameandikwa katika kitabu cha mambo ya kila siku, 'Hospital and Community Psychiatry, Des, 1992.'

Maandishi ya kuvutia katika ukurasa, yaliyofikiwa kwenye dhana hiyo hiyo baada ya kuchunguza sana, yalitokea katika jarida lingine liitwalo *International Herald Tribune*, la Feb. 11, 1993; na kichwa cha habari yenyewe: "Wapentekosti wapo orodha ya juu wanapokuja na huzuni" Ni kwa sababu gani wapo kwenye hali hii ? kwa kweli inabidi wawiane na uhakika wa kwamba 'Ujuzi unaojipatia' wa tendo la Kuwa na Roho, ambao wapentekosti (na wengineo) wenye kadhia hii, si lolote zaidi ya Kuwa wanauchungu sana wa m ioyo yao dhidi ya mazoea.

## 2.4 Kurudishwa kwa vipawa

Vipawa vyenye miujiza ya Roho ya Mungu vitatumika tena na waumini ili kwamba ulimwengu huu wa sasa ubadilishwe uwe Ufalme wa Mungu, Kristo atakaporudi. Basi vipawa vimetajwa Kuwa ni 'Nguvu za zamani (Zama) zijazo' (Ebr. 6:4, 5); naye Yoeli 2: 26 -29 umwagaji mkubwa wa karama baada ya toba ya Israeli. Uhakika sana wa kwamba vipawa hivi watapewa waaminio Kristo akirudi ni ushuhuda wa kutosha ya kwamba kwa sasa vipawa watu hawana - Kwa kuwa Mkristo awaye yote mwenye macho yaliyo wazi pande zote mbili Maandiko na matukio ya ulimwengu, ni hakika kurudi kwa Bwana inabidi kuwa amekaribia sana (tazama yaliyo mwisho wa kitabu cha 3).

Upo Unabii dhahiri wa Biblia kama katika maana fulani kwa kipindi cha kati ya karne ya kwanza, vipawa vilipokuwepo, na kuja mara ya pili ilibidi vipawa vya Roho viondolewe:-

“ ……Ukiwepo Unabii utabatilika; zikiwapo lugha, zitakoma; yakiwepo maarifa, yatabatilika. kwa maana tunafahamu kwa sehemu (yaani, nusu); na tunafanya Unabii kwa sehemu; lakini ijapo ile iliyokamili,iliyo kwa sehemu itabatilika (yaani, kuondolewa)”. 1 Kor. 13:8 -10 - Karama za Roho zilikuwa za muda tu.

Karama za Roho walizokuwa nazo katika karne ya kwanza ilibidi ziondolewe 'Ilipokuja ile iliyokamili’ Hii si kuja mara ya pili Kristo, kwa Kuwa kipindi hicho karama za Roho zitatolewa tena. Neno la Kiyunani lililotafsiriwa'Kamili’ maana yake hasa ni kile ambacho kimetimilika au Kizima; akimaanishi kwa lazima Kuwa ni kitu kingine kisicho na dhambi.

Hiki kitu kizima kitaingia mahali palipo na maarifa yaliyo kwa sehemu ambayo Wakristo wa kwanza walikuwa nayo kama tokeo la Kuwa na kipawa cha kutoa Unabii. Kumbuka kwamba kutoa unabii kilikuwa ni kipawa cha kutabili maneno yenye kuvuviwa na Mungu ; ni taarifa iliyoandikwa ya maneno haya yanayoifanya Kuwa Biblia.

Kwenye karne ya kwanza, Muumini wa kawaida alijua sehemu ndogo tu ya Agano Jipya kama tunavyolijua. Alisikia maneno mengine ya Unabii toka kwa wazee wa kanisa lake juu ya matukio mbali mbali ya matendo ; aliweza kujua vema juu ya maisha ya Yesu, na aliweza kusikia vema barua moja au mbili za Paulo zikisomwa kwa sauti. Lakini mara taarifa ilipoandikwa ya maneno ya Unabii na kuweza kutimilika na kugawanywa, hapakuwepo na

haja ya kipawa cha kutoa Unabii kiendelee wawe nacho. kile ambacho kilikuwa kamili, kwa sababu hiyo kilichoingia mahali pa huduma ya karama ya Roho, basi likawa ni Agano Jipya lililotimilika:-

"Kila andiko lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki, ili mtu wa Mungu awe kamili (ametimilika)" 2 Tim. 3:16 -17.

Kile ambacho kinafanywa kuwa kamili, au kutimilika, ni'Maandiko yote'; hivyo mara'Maandiko yote' yalipovuviwa na kuandika, " Kile ambacho kilikuwa kamili" kikawa kimekuja, nazo karama zenye miujiza zikaondolewa.

Waefeso 4: 8 -14 yaweka sasa wazi kikamilifu sawia fumbo lisiloeleweka vema:-"(Yesu) alipopaa juu (katika mbingu), ….akawapa wanadamu vipawa (vya Roho) ….. kusudi mwili wa Kristo ujengwe: hata na sisi sote tutakapoufikia umoja wa imani (yaani, Imani moja), na kumfahamu sana mwana wa Mungu, hata Kuwa mtu mkamilifu …. Ili tusiwe tena watoto wachanga, tukitupwa huku na huku, na kuchukuliwa na kila upepo wa elimu".

Vipawa vya karne ya kwanza vilitolewa hadi mtu alifikia kukamilika au apevuke, (yaani, akomae) nao waraka wa 2 Tm. 3:16- 17 unasema ya Kuwa " Hadi mtu wa Mungu awe kamili" kwa kufahamu mwongozo wa 'Maandiko yote' Tena, Kol. 1:28 unatufundisha ya kwamba 'Ukamilifu' huja kwa kuitikia katika Neno la Mungu. Mara maandiko yote yakishikwa. Hakuna udhuru kweli wowote tena wa kukatizwa na wingi wa mafundisho yatolewayo na makanisa mbali mbali. Ipo biblia moja tu, na Kuwa

"Neno lako ndiyo kweli" (Yoh. 17:17), kwa kujifunza katika kurasa zake tunaweza kufikia "Umoja wa imani", imani moja ambayo Efe. 4:13 inaizungumzia. kwa hiyo wakristo wa kweli

wamefikia kuishika hiyo imani moja; kwa maana hiyo wametimilika (wamekuwa'Kamili') kwa kutokana na 'kile ambacho ni kamili' au kimetimilika, Neno la Mungu lote - lililoandikwa.

Kwa kupita, tazama ni jinsi gani Efe. 4:14 unalinganisha kuwa chini ya utumishi wenye karama za miujiza, na utoto kiroho; na kwa maneno yenyewe ya kutoa unabii, namna karama zenye miujiza zilipoondolewa. 1 Kor. 13:11 unasema hayo hayo. Kufanya makelele haya kuhusu kuwa na karama za roho, basi si ishara ya kukomaa kiroho. Kusonga mbele kila msomaji wa maneno haya kufanye sasa kuelekea kufahamu kwa kina neno la Mungu lililoandikwa. Na kufurahia utimilifu wa msingi wa ufunuo wa Mungu mwenyewe ndani yake kwetu, kwa kuitikia neno katika Utii wa kunyenyekea.

## KADHIA ZILIZOPO ZENYE KUWA NA ROHO

Hatimae, hesabu ya maana nyingine inabidi ifanywe kuhusu kadhia zilizorudiwa za hao wadhaniao wana vipawa vyenye miujiza sasa:-

-"Wanenao kwa lugha" siku hizi wanaelekea kurudia rudia maneno yale yale mafupi zaidi na zaidi tena, k.m. "lala, lala, lala, shama, shama. Yesu, Yesu ……" huu sio mpangilio uliojumuika na maneno ya lugha yoyote; mtu akimsikia mwingine akinena katika lugha ngeni, mara kwa mara inawezekana ya Kuwa wanaongelea jambo fulani kwa mfano mzuri wa matamshi ambao watu hutumia, ingawa hatuwezi kuyaelewa maneno hayo. Lakini wanenao lugha siku hizi hawaangalii jambo hili, uhakika ni kwamba lugha wanenayo haijengi kanisa, ambapo hiyo ilikuwa shabaha ya kutolewa karama kwenye karne ya kwanza.

-Wapentekosti wengine wanatoa kadhia ya kwamba kunena katika lugha ni ishara ya Kuwa 'Wameokoka'na kwa sababu hii kila mwongofu wa kweli hii ishara itafuatana naye. Kadhia hii inagongana na ugumu wa maelezo kuhusu makanisa ya kwanza ulikuwa mwili, ambapo wale wanaomiliki karama tofauti - tofauti walikuwa kama viuongo mbali mbali. si kila mtu alikuwa mkono au mguu, na vivyo hivyo si kila mmoja alishika kipawa kimoja chochote, k.m Lugha. 1Kor.12:17, 27 -30 mistari hii yote inabainisha wazo hili:-

"Kama mwili wote ukiwa jicho, kuwapi kusikia ? kama mwili mzima ni sikio kuwapi kunusa ? …. Basi mmekuwa mwili wa Kristo, na viungo kila kimoja peke yake. Na Mungu amewaweka wengine katika kanisa , wa kwanza Mitume, wa pili Manabii, wa tatu Waalimu, kisha Miujiza, kisha karama ya kuponya wagonjwa, na masaidiano, na maongozi, na aina za Lugha. Je! wote ni Mitume ? wote ni Manabii.? Wote wana karama za kuponya wagonjwa ? wote wanena katika lugha ? wote wafasiri.

Awali, maana hiyo hiyo imeonyeshwa katika mlango huo:-

"Maana mtu mmoja kwa Roho apewa neno la hekima; na mwingine neno la maarifa, apendavyo Roho yeye yule; mwingine imani katika Roho yule yule; na mwingine karama za kuponya katika Roho yule yule mmoja; na mwingine matendo ya miujiza; na mwingine Unabii; na mwingine kupambanua Roho; mwingine aina za lugha; mwingine tafsiri za lugha; lakini kazi hizi zote huzitenda Roho huyo mmoja yeye yule, akimgawia kila mtu peke yake kama apendavyo yeye. Maana kama mwili ni mmoja, nao una viungo vingi, na mwili mmoja; vivyo hivyo na Kristo" (1Kor. 12: 8 -12)

Mkazo wa jinsi hii hauwezi kutoangaliwa:-

Shida nyingine kwa ubishi wa Mpentekosti ni kwamba Filipo aliwaongoa watu wengi katika mji wa Samaria - yaani, walibatizwa katika maji baada ya kuelewa Injili, lakini hawakupokea karama za Roho; kwa Kuwa baada ya hivi, Petro na Yohana waliwaendea " ….. Waliposhuka, wakawaombea wampokee Roho Mtakatifu …. Ndipo wakaweka mikono yao juu yao, nao waka mpokea Roho Mtakatifu …..Simoni aliona Kuwa watu wanapewa vipawa vya Roho Mtakatifu kwa kuwekewa mikono yao mitume" (mdo. 8: 4 - 18). inawezekana kwamba kupewa vipawa vya Roho ilikuwa ni kuwekewa mikono juu yao tu, tendo ambalo Wapentekosti hawalifanyi mara nyingi siku hizi.

Wapentekosti wengine wanasema kwamba kunena kwa lugha si ushahidi wa kuwa umeokoka. Huu ni ukweli unaojitokeza kuwa ipo tofauti kubwa ya mafundisho kati ya wenye kadhia ya kushika vipawa. Baadhi ya watu wa 'Kiroho' huamini kwamba ufalme wa Mungu utakuwa duniani, ambapo wengine wanasema utakuwa mbinguni. Wakatoliki 'wa Kiroho' wanasema kwamba Roho Mtakatifu anawaambia wamwabudu Bikira Maria na Papa, wakati wapentekoste wengine 'wa Roho' wanasema ya kwamba wao huongozwa na Roho Mtakatifu anayewaamuru wamkane Papa, wamwone kuwa yeye ni mnyama na mpinga Kristo, wanapinga mafundisho ya Katoliki. Hata hivyo Yesu alisema pasipo shaka kwamba wale walio na msaidizi, " ambaye ni Roho Mtakatifu" wataongozwa 'kwenye kweli yote' ….tena siku ile (hamtahitaji) kuuliza neno lolote …..Msaidizi …..atawafundisha mambo yote, na kuwakumbusha yote niliyowaambia" (Yoh. 16: 13,23; 14: 26).

Usingekuwepo Mgawanyiko wowote katika mafundisho ya msingi miongoni mwao wenye kuwa na msaidizi - uhakika ni kwamba upo, unaonyesha kwamba wale wanodai wanaye

hawamchukui kwa kusema kweli. Udhaifu umeonekana kwa baadhi ya hao wasemao ya kuwa wenye msaidizi, Katika Biblia ili kuthibitisha imani zao lakini wanaonekana kwamba hawajaongozwa katika kweli yote na maarifa kabisa ya msaidizi.

-Umuhimu mkubwa uliofuatana na baadhi kwa kunena katika lugha haupo sawa na taarifa za Biblia. Orodha ya vipawa katika Waefeso 4:11 haitaji, orodha kama hii inatokea chini katika 1 Kor.12: 28 -30. kwa kweli, zipo nafasi tatu pekee zilizoandikwa katika Agano Jipya mahali ambapo kipawa kilitumika (mdo. 2:4; 10:46; 19:6).

Madai ya kunena katika lugha na kufanya miujiza kulikotimizwa na Wakristo wa roho siku hizi inabidi yapimwe karibu na taarifa yenye maana ambayo tumeiandika katika somo hili kuhusiana na kazi ya Roho Mtakatifu. Kutengeneza maana yenye msingi ni kwamba lolote ambalo watu hawa wamelitimiza, haliwezi kuwa ni tokeo la wao kuwa na Roho Mtakatifu. Yeyote aletaye sababu za kusaidia mashauri ya kuwa wanamiliki karama za Roho, anayo kazi kubwa ya kufanya ili kujibu maneno ya Biblia tuliyotoa.

Ingawa hiyo ni sababu yenye maana katika kutazamia baadhi ya maelezo ya sababu gani uzushi wa kuponya kwa sehemu na kunena kwa'Lugha' (Kwa mtindo wa kunena kwa kupayuka - payuka) hutokea.

Imefahamika kwamba wanadamu hutumia sehemu ndogo ya nguvu ya ubongo wao - chini ya 1%, kulingana na makadirio mengine. Tena, akili (Moyo) imetambuliwa kuwa inaweza karibu kutawala viungo vya mwili; hivyo kwa nguvu zao za mwili hivyo huamini kuwa moto hauwezi kuunguza, Wahindu wametembea juu

ya moto nyayo zao zikiwa wazi bila kuungua. kwa vipindi vya kuchochewa, upo uwezekano wetu kutumia asilimia kubwa ya uwezo wa ubongo wetu kuliko kawaida, na kwa sababu hiyo kuwa na uwezo ya kutimiza matokeo ya viungo juu ya mwili wetu unapokuwa nje ya matendo ya kawaida. Hivyo, kwa kuchochewa na mapigano, askari anaweza kutojua kabisa kuwa mkono wake umekatika mpaka muda wa baadae.

Imani ya dini kuwa katika hali ya moto na msisimko unaoamshwa na nyimbo fulani, na mvuto wa kiongozi wa kiroho, inawezekana kabisa mambo yaliyo nje ya miliki ya kawaida kwa mwanadamu yatatokea.'Miujiza' iliyodaiwa kufanywa na'Wakristo' wa leo ni ya mpango mmoja isiyofuata utaratibu kama ya majaribio ya dini nyingine; Vivyo hivyo hata dini ya waabudu uchawi imejaribu mambo hayo hayo ya kunena kwa kupayuka - payuka, Waislamu vile vile wanaweza kutumik a kama 'Ishara' za mpango wa namna hii na hizo zilizodaiwa na Ukristo wa sasa. Lakini maana nzima ya karama za Roho zilizomilikiwa katika karne ya kwanza ilikuwa kuonyesha bayana ukuu wa Ukristo wa kweli juu ya dini nyingine zote. Uhakika ni kwamba 'Miujiza' ya Ukristo wa siku hizi upo kwa mpangilio wa namna moja na dini nyingine, yaonyesha kwamba karama za Roho Mtakatifu zilizokuwa katika karne ya kwanza kwa sasa hazishikwi na watu.

Taarifa nyingine zenye maana katika eneo hili zimetolewa katika Upentekosti wa Williamu Campbell (Makanisa ya Kristo, mwaka 1967). Anaonyesha ya kwamba dini nyingi za kipagani zina jambo hili hili la kunena 'Lugha'. Hivyo katika sehemu ya Kawaii, makuhani wa Mungu Oro wamewaza kuwa anafunua nia yake kwa sauti isiyosikika ambayo inatafsiriwa na makuhani wengine. Jambo hilo hilo hutokea katika mikutano ya Pentekosti.

Ushindi unaoendelezwa na Uislam juu ya Ukristo katika sehemu nyingi za Afrika kwa kweli usingeonekana kama 'Ukristo' wa watu wengi ulikuwa unafanya miujiza ya kweli kwa utaratibu na kwa nguvu zenye kuthibitisha za wale waliokuwa karne ya kwanza. Kwa kweli wale wenye kuwa na'Msaidizi' wa kipawa cha Roho Mtakatifu watafanya, naam, "Kazi kubwa" kuliko alizofanya Yesu (Yoh. 14: 12,16). Udhuru wa kwamba Wakristo wanaweza kufanya miujiza ya namna hii kama walikuwa na imani zaidi, hapa wanakumbana na shida kubwa. Aidha wakiwa na karama zenye miujiza ya msaidizi, au wakiwa hawana, na kama wanadai kwamba wanafanya - " Kazi kubwa kuliko hizi atafanya" (Yoh. 14:12) - si'Utaweza kufanya' !

### 2.5 Biblia ni Mamlaka pekee

Toka kile ambacho tumeona mpaka hapa katika somo hili, Roho ya Mungu inataja nia na kusudi lake, na nguvu ambazo anaweka vitu hivyo katika kutenda kazi. Tumetoa mkazo wa kwamba Roho hiyo kwa maelezo ya kwamba imefunuliwa kwetu katika kurasa za neno la Mungu. Matatizo mengi ya Ukristo wakati ule yote yameshuka katika kosa la kuhuzunisha kufahamu hili. Kwa kuwa ni vigumu kusadiki kuwa huu uwezo mkubwa umewekwa katika kitabu kimoja, sehemu zake zinazotuwia vigumu kuzielewa, ni kuvutwa kuona ya kwamba kuna namna ingine ya ufunuo wa Mungu kwa watu, kuliko Biblia. Kwa sababu ya hatia kubwa ya mwili wa mwanadamu (Yer. 17:9) unapata usafi kweli wa neno la Mungu (Yoh. 17:17) hivi huwa vigumu kuvumilia, wengi wameshindwa katika jaribu hili kwa kudai au kutaka namna nyingine ya ufunuo unaovutia zaidi katika nia ya mwili .

Yote haya yanatokeza haja ya kufahamu ukubwa wa Biblia kuwa ni neno la Mungu, na kuchunguza kurasa zake kwa kupata ujumbe wa kweli. Swali, “Biblia moja, Makanisa mengi - ni kwa nini ?” kwa upana limejibiwa linapofahamika ni jinsi gani kila kanisa lina, kwa kiwango fulani, limedai namna nyingine ya ufunuo wa Roho ya Mungu, yaani, mapenzi yake, mafunzo na fikira, kwa nyongeza katika huo wa Biblia.

Kama unataka kupata kanisa moja la kweli, imani moja ya kweli na ubatizo mmoja wa kweli (Efe. 4:4 -6), wito unapasa kukujia kwa sauti kubwa na dhahiri - “Rudi katika Biblia !”

Tumeacha kitambo tulichoandika sehemu ya 4:
Je ! Roho Mtakatifu ni Mtu?

Somo la 2.1 na 2.2 yametoa ushahidi mkubwa wa kwamba Roho ya Mungu unatajwa uweza wake, unaotoa “Nia” yake katika kila njia pana. Kwa sababu ya namna Roho ya Mungu itendavyo kazi vivi hivi ni kioo sahihi cha nafsi na utu wa Mungu, baadhi ya watu wameleta ubishi na kusema ya kwamba Roho ya Mungu ni mtu ambaye pia ni Mungu. Kusoma tena kwa makini sehemu zilizotangulia zitaonyesha ya kwamba Roho ya Mungu ni akili na uweza wake; kama hivyo ndivyo, basi hakuna mfano wa kwamba nia - akili au nguvu yaweza kuwa mtu. Umeme ni nishati - nguvu isiyoonekana ambayo inatoa matokeo kwa mtu anayeutumia, lakini umeme hauwezi kuitwa ni mtu, Roho ya Mungu ina upendo wake, kama sehemu ya tabia yake, na tena unatajwa uweza wake, lakini hautajwi kuwa ni mtu aliyejitenga toka kwake.

Ni makosa ya kuonekana wazi kama shauri hili lilivyokosewa (la Roho Kuwa ni mtu) na kuonekana, ni dhana iliyoaminiwa na 'Wakristo’ walio wengi, kwa kuwa wanasadiki mafundisho ya

'Utatu'. Kwa maana hii imesemwa kuwa wapo Miungu watatu ambao kwa njia isiyoeleweka vile vile kuwa ni yule yule Mungu Baba, Roho Mtakatifu na Yesu. Watu hao hao wametoa kadhia kuwa Mungu si mtu, lakini wanasema ya kwamba Roho Mtakatifu ni mtu; hapa maneno yanaachana kabisa. Tena, Roho Mtakatifu atafanywa kuwa ni Baba ya Yesu.

Kuna sababu nzuri ya kuamini ya kwamba'Utatu' kimsingi lilikuwa ni wazo la kipagani lililoingizwa katika Ukristo - basi hili neno halitoki katika Biblia. Wakiisha kubali dhana hii ya kuwa Mungu ana nafsi tatu, ndipo Wakristo wamelazimika kufikia wazo lisilo kweli na gumu kueleweka la kwamba uweza / Roho ya Mungu ni mtu, aliye Mungu tena, ingawa si Mungu. Wanapokabiliwa na maneno yaliyo mbali na akili kwa maono yao, njia ya kukwepa watu wengi zaidi ni kwa watu hawa kudai kwamba Mungu ni siri, nasi tukubali mambo haya kwa imani pasipo kutaka maelezo yenye maana ya akili.

Kwa maana hii ni kushindwa kutazama ushahidi ulio katika Agano Jipya katika Siri ya Mungu kuwa imefunuliwa ndani ya neno na kazi ya Kristo:-

"Kwa maana ndugu zangu sipendi msiijue siri hii" (Rum. 11:25).

"Kwa kuhubiri kwake Yesu ……. Na ufunuo wa ile siri" (Rum. 16:25)

"Akiisha kutujulisha siri ya mapenzi yake" (Efe. 1: 9; 3:3).

"Angalia, nawaambia ninyi siri ….." (1 Kor. 15:51).

Mahubiri ya Paulo yalikuwa "Katika kujulisha ile siri ya Injili" (Efe. 6:19; Kol. 4:3).

“Siri ile ……. Sasa imefunuliwa kwa watakatifu” (Kol. 1: 26, 27).

Kwa mkazo huu wote - ni kwamba - ni kule si sasa kuna siri yoyote iliyofungamana na mafundisho makubwa, atakuwepo tu mtu mwingine aliye gizani ambaye atadai kwamba kuna siri. Na mtu huyu hana wasi wasi wa kwamba Biblia inaita jina badala ya “Babeli” utaratibu wa dini ya upotovu ulioelezewa katika ufunuo, ni 'Siri’ (Uf. 17:5) ? kidokezo dhahiri ni kwamba utaratibu huu unatangaza ya kuwa imani zake ni siri; lakini waumini wa kweli wanafahamu siri ya mwanamke huyo (Uf. 17:7).

Fikira hizi zisizo dhahiri, kwa kweli zimetarajiwa toka kwao wawekao fahamu zao kwa Mungu juu ya mawazo ya vitu kama akutanavyo mwanadamu, au shughuli zisizo wazi, zisizoeleweka za nguvu nyingine kiroho juu ya fikira zao. kama kweli tunatarajiwa kweli kuwa wanyenyekevu katika fundisho la Neno la Mungu , kinachofuata tena tunatakiwa kutumia nguvu za kufikiri na akili ya kupata elimu ili kwamba tuvumbue ujumbe wake.

Mhubiri awaye yote wa Injili ambaye taarifa zake zimo katika Biblia, hakukimbilia kamwe kusema,'Hii ni siri sana, hamwezi kuanza kuielewa’ badala yake, tunawasoma wakiwasihi watu kutumia akili nao wavutwe na wazo litokalo katika Maandiko.

Katika kuhubiri kwake aina ya Injili kubwa ambayo tunaiona katika masomo haya, Paulo “ alihojiana nao kwa njia ya Maandiko, akayafunua na kuwaeleza ya kwamba ilimpasa Kristo kuteswa, na kufufuka katika wafu” (Mdo. 17:2,3). Huu ulikuwa ni utaratibu wenye muundo wa kufikiri maneno ya Biblia wastani wake ulio bora; fungu hili la maneno linatangulia taarifa “Paulo, kama ilivyokuwa desturi yake …… alihojiana nao ……. “ Basi,

huu ulikuwa ni mtindo wa kawaida yake (tazama tena Mdo. 18:19). Kwa kupatana na huu, kipindi cha kampeni kubwa pale Korintho, Paulo "alitoa hoja zake katika Sinagogi kila sabato, akijaribu kuwavuta Wayahudi ……. (Lakini) walipopingana ….." (Mdo. 18:4-6). Wale walioongoka walienda njia ya ushawishi wa maneno ya Paulo ambayo msingi wake umo ndani ya Biblia; hapa hayakuwa 'Maono ya Yesu ndani ya chumba changu'; 'hisia zilinijia zisizoelezeka', 'Nilikutana na Bwana jioni moja'.

Elewa vile vile, ya kwamba habari iliyovuviwa inatoa ombi la maneno yenye akili na busara, kwa kuonyesha kwamba "Walipingana wenyewe" vivyo hivyo kule Antiokia, Paulo na Barnaba "walisema nao (neno), wakawatia moyo ….." (Mdo. 13:43). Eneo lao lililofuata la kusita lilikuwa ni Ikonio, mahali ambapo "Walinena kundi kubwa …. Waliamini " (Mdo. 14:1).

Baadaye kidogo aliposimama kutetea maisha yake, maneno yale yale yenye utukufu na busarra yaliendelea katika kuvuviwa tumaini imara la Paulo kwa sababu ya kipindi kijacho: "Alitoa hoja zake katika habari ya haki, na kuwa na kiasi, na hukumu itakayokuja" na udhahiri huu unaopenya hata mwenye kubeza, hakimu wake "alihofu" (Matendo ya mitume 24:25).

Kwa kuwa kuongoka kwetu kunakuwa juu ya msingi huu wa njia ya kutumia akili, tunaweza kutoa maelezo yenye busara ya Biblia na tumaini letu na mafundisho:-

" kuwa tayari siku zote kumjibu kila mtu awaulizae habari za tumaini lililo ndani yenu"(1Petro. 3:15).

Kusema katika sauti yenye busara juu ya matukio ya mtu mwenyewe si kutoa hoja ya tumaini la Injili. Utegemezi

unaoendelea juu ya ushuhuda wenyewe kama njia ya kuhubiri Wakaristo wengi wa Kiinjili, ukosefu wa 'hoja ya jibu la kutumia' unajitokeza kwa 'tumaini' lao. Maelezo yote yamezuka miongoni mwa Wakristo hawa kwa'kuwawezesha katika kushiriki yale Bwana aliyofanya katika maisha yangu' n.k. Hizi hadithi fupi za maisha ya mtu zatofautiana vikali na maneno ya Paulo, "Hatujihubiri wenyewe, bali Kristo (2Kor. 4:5) - na kama toka mtu aliyekuwa na uhusiano binafsi na Yesu" zaidi kuliko wengi.

Maneno ya kutumia akili, maana ya jinsi ya kuongoka kwetu kibiblia yaweke mfano mzuri wa uhusiano wetu mpana na Mungu katika siku zetu zilizobaki. Mifano yetu, kama siku zote, ni ya Wakristo wa kwanza waliyotumia kwa "Kutoa Hoja" katika kutatua matatizo yao ya mambo ya kutoa mashauri (Mdo. 6:2).Nyaraka za Agano Jipya tena zinawasadikisha wasomaji wao wafahamu kutumia akili ya maneno ya Biblia. Basi, "Kwa akili ya kufahamu" jinsi makuhani wakuu walivyokuwa chini ya torati ya Musa, tunaweza kuelewa habari moja moja kuhusu kazi ya Kristo (Ebra. 5:3) akiisha unena upendo wa Mungu unaozidi katika Kristo, Paulo anatoa sababu ya kwamba ndiyo "Ibada yenu yenye maana (Kutuumia akili) sisi wenyewe kujitoa kabisa kwake katika kuitikia (Rum.12:1). Basi kuitikia kwetu katika maneno ya Biblia ni kumoja na kutumia 'akili' yetu kunakopatikana toka katika neno la Mungu.

Katika mwangaza wa yote haya, yatakuwa dhahiri kwamba si busara kudai ya kuwa roho ya Mungu ni nafsi peke yake ambayo si Mungu lakini wakati huo huo ni Mungu - na kwa kukabili wazo hili kwa kusema kwamba jambo hili lote ni lenye siri na kwamba kutumia akili si muhimu, kwa maneno ya Biblia halikubaliki. kama hatuwezi kuchukua maneno toka Maandiko, basi kujifundisha kote Biblia ni bure, hakuna haja ya kuwa na Biblia,

ambayo inaweza kupimwa kama maneno yanayofikiriwa kuwa kweli matamu tu au neno la kitabu kinachovutia. hiki kitabu pia kinaonekana kuwa juu ya makabati ya Wakristo wengi.

Ingawa hivyo, katika tumaini lao, baadhi ya wanaosadiki kuwa Roho ya Mungu ni mtu wanajaribu kutoa sababu za Biblia. Mafungu ya maneno yaliyonukuliwa ni yale ambayo yanataja roho wa Mungu kwa msemo wa peke yake, kama "Mfariji -Msaidizi" katika Yoh. 14:16, au ushahidi wa kuwa roho "alihuzunishwa".

Tumeonyesha kwa kuandika bayana katika somo la 4.3 kuwa "Roho ya Mwanadamu yaweza kuchukizwa (Mdo. 17:16), kufadhaika (Mwa.41:8) au kushangilia (Luka. 10:21). "Roho" yake, yaani, nafsi yake hasa, akili na kusudi lake, vinavyozusha matendo yake, kwa hiyo husemwa kuwa ni mtu tofauti, lakini bila shaka, si hivyo hasa, Vile vile, Roho ya/wa Mungu, yaweza kusemwa kwa jinsi hiyo hiyo.

Tena inabidi ieleweke ya kwamba mara nyingi Biblia imetumia msemo kutaja kitu au jambo kama ni mtu inaposema mambo ya kuwazika, kama. Hekima imetajwa kana kwamba ni mtu katika kitabu cha Mithali 9:1. Hivi ni kwa kutuonyesha mtu gani aliye na hekima anavyofanana katika kutenda matendo;'Hekima' haiwezi kuwepo isipokuwa ndani ya akili ya mtu, ndivyo shauri hili la kuita kitu kana kwamba ni mtu limetumika. Maelezo zaidi juu ya hili, tazama tumeacha kitambo …… sehemu ya 5,

"Jambo la kuita kitu kama mtu".

**Tumeacha kitambo sehemu ya 5: Kawaida ya kuita kitu kana kwamba ni Mtu**

Wengine itakuwa vigumu kufahamu maelezo ya kawaida yanayomtaja Ibilisi kuwa ni kiumbe au mtu, kwa sababu Ibilisi ametajwa mara nyingi katika Biblia kana kwamba ni mtu, labda maelezo haya yanawachanganya watu wengine. Haya kwa urahisi yameelezwa kwa kuonya kuwa ni sura za Biblia zilizotambulika za kwamba kitu kisicho na uhai kama Hekima, Mali, Dhambi, na Kanisa vyote hivi vinatajwa kana kwamba ni mtu, lakini katika suala la Ibilisi pekee baadhi ya nadharia za kuwazika tu zimetungwa kuzunguka pande zote. Mifano ifuatayo itaeleza kiini:-

**HEKIMA IMEITWA KAMA MTU**

"Heri mtu yule aonaye hekima, na mtu yule apataye ufahamu. Maana biashara yake ni bora kuliko biashara ya fedha, na faida yake ni nyingi kuliko dhahabu safi. Yeye anathamani kuliko marijani, wala vyote uvitamanivyo havilingani naye" (Mithali 3:13 -15). "Hekima ameijenga nyumba yake, amezichonga nguzo zake saba" (Mith. 9:1)

Mafungu haya ya maneno, kwa kweli sura zilizobaki ambamo yanaonekana, yanaonyesha ya kwamba hekima imeitwa kana kwamba ni mtu kama mwanamke katika Biblia ya kiingereza, bali kwa sababu hii, hakuna mtu anayewaza ya kuwa hekima ni mwanamke halisi mzuri anayetembea akizunguka pande zote za dunia; wote wanajua kwamba ni tabia ya kutamanika sana ambayo watu wote walijaribu kujipatia.

## MALI IMEITWA KANA KWAMBA NI MTU.

"Hakuna mtu awezaye kutumikia mabwana wawili: kwa maana atamchukia huyu na kumpenda huyu; ama atashikamana na huyu, na kumdharau huyu. Hamwezi kumtumikia Mungu na Mali" (Mith. 6:24). Hapa tunasoma Mali imefananishwa na Bwana. Watu wengi wanajitahidi mno kupa ta mali na kwa njia hii anakuwa ni Bwana wao. Yesu anatuambia hapa ya kwamba hatuwezi kufanya hivyo na halafu kumtumikia Mungu inavyostahili wakati huo huo. Fundisho ni jepesi lenye maana, lakini hakuna mtu awaye yote anayekubali toka hili ya kwamba mali ni mtu aliye na jina.

## DHAMBI IMETAJWA KAMA NI MTU

"…… kila atendaye dhambi ni mtumwa wa dhambi" (Yoh. 8:34). " Dhambi imetawala katika mauti" (Rum. 5:21). "Hamjui ya kuwa kwake yeye ambaye mnajitoa nafsi zenu kuwa watumwa wake katika kumtii, mmekuwa watumwa wake yule mnayemtii, kwamba ni utumishi wa dhambi uletao mauti, au kwamba ni utumishi wa utii uletao haki" (Rum. 6:16)

Kama ilivyo katika suala la Mali, dhambi imelinganishwa hapa na Bwana, nao wale watendao dhambi ni watumwa wake. Si usomaji mzuri kwa fungu la maneno linalothibitisha kwa kukubali ya kwamba Paulo anafundisha ya kuwa dhambi ni mtu.

## ROHO IMEITWA KANA KWAMBA NI MTU FULANI

"Lakini yeye atakapokuja, huyo Roho wa kweli, atawaongoza awatie kwenye kweli yote: kwa maana hatanena kwa shauri lake mwenyewe …" (Yoh. 16:13).

Hapa, Yesu aliwaambia mwanafunzi wake ya kwamba watapokea nguvu za Roho Mtakatifu, nalo jambo hili lilitimia kwenye siku ya Pentekoste, kama lilivyoandikwa katika matendo 2:3 -4, mahali ambapo pamesemwa ya kuwa "Kukawatokea ndimi zilizogawanyika, kama ndimi za moto, uliowakalia kila mmoja wao. Wote wakajazwa "Roho Mtakatifu" kwamba mamlaka yao itakuwa kwa Mungu. Roho Mtakatifu hakuwa mtu fulani bali ilikuwa ni nguvu, na Yesu alipokuwa anainena alitumia tamshi lake'Yeye'.

**MAUTI IMEITWA KAMA MTU**

"Tazama, farasi ya rangi ya kijivu jivu, na yeye aliyempanda jina lake ni Mauti" (Ufunuo. 6:8)

**TAIFA LA ISRAELI LIMEITWA KANA KWAMBA MTU**

"Mara ya pili nitakujenga, nawe utajengwa, Ee bikira wa Israeli mara ya pili utapambwa kwa matari yako ……" (Yer. 31:4).'Hakika nimesikia Efraimu, akijililia hivi; umeniadhibu nami nikaadhibika, kama ndama asiyeizolea nira; unigeuze, nami nitageuzwa; kwa maana wewe u Bwana, Mungu wangu' (Yer. 31:18). Fungu lenyewe la maneno haya linafunua dhahiri ya kwamba nabii hamtaji bikira halisi au Efraimu akiwa ni mtu, bali ni taifa la Israeli, ambalo katika mfano huu limetajwa kana kwamba ni mtu.

**WAAMINIO KATIKA KRISTO WAMEITWA KANA KWAMBA NI MTU MMOJA**

“Hata na sisi sote tutakapoufikia umoja wa imani na kumfahamu sana mwana wa Mungu, hata kuwa'Mtu’ mkamilifu, hata kufika kwenye cheo cha kimo cha utimilifu wa Kristo” (Ef. 4:13).”Upo mwili mmoja” (Ef. 4:4) “Ninyi mmekuwa mwili wa Kristo, na viungo kila kimoja peke yake” (1Kor. 12:27). “……Kristo ni kichwa cha Kanisa: naye ni mwokozi wa mwili” (Ef. 5:23). “Naye (Kristo ndiye kichwa cha mwili; ….. sasa anayafurahia mateso niliyo nayo kwa ajili yenu, tena nayatimiliza katika mwili wangu yale yaliyopungua ya mateso ya Kristo, kwa ajili ya mwili wake,yaani, Kanisa lake” (Ko.. 1:18,24). “Nimewaposea mume mmoja, ili nimletee Kristo bikira safi” (2 Kor. 11:2) “ …..harusi ya mwana kondoo imekuja, na mkewe amejiweka tayari” (Uf. 19:7)

Ni bayana haya hizi zote zataja jamii ya watu waliokuwa waumini wa kweli wa Kristo, mara nyingine wametajwa ya kuwa ni'Kanisa’ Ingawa hili halipaswi kujumuishwa na makanisa yoyote ya kiorthodox yaliyopo siku hizi, ambayo ni muda mrefu yamekoma kuwa ni ya waumini wa kweli kwa Kristo.

Waumini wa kweli, yaani, wanaoshika na kuamini mafundisho ya kweli yaliyofundishwa katika Biblia, mara nyingine wametajwa kuwa ni “Bikira safi” wakionyesha usafi wa maisha wanayoendea'Kama mwili’ mfano unaofaa kwa kuwa kiasi kama mwili wa asili ulivyo na viungo vingi, vivyo kanisa la kweli lina majukumu mengi na kufanya kazi mbali mbali. Kanisa linaposhuhudiwa kuwa ni “Mwili”, hakuna mtu anayekosea maana ya mtu mmoja mmoja, wala watafanya kosa juu ya Ibilisi au shetani maana ya upuuzi kuwa ni mtu asiye na desturi ya kawaida au malaika aliyetupwa, wanawake hawakupata mawazo mabaya toka katika makanisa yaliyopotoka kwa siku zilizopita.

Yametengenezwa katika “Ufalme wa wakristo Umepotoka” (Christeridom Astray) na Robert Roberts.

***Tumeacha kitambo sehemu ya 6: Mambo ya kelvini***

Miaka mia chache iliyopita, Kelvini alifundisha wazo la kwamba uteuzi ulikuwepo katika maisha yetu hapo kabla, hivyo basi uchaguzi wa kufanya tupendavyo kwa hiyari hauna juhudi juu ya wokovu wetu; aidha tulikwishachaguliwa kabla ili tupate wokovu au kukataliwa. wazo hili tena limeweka sura mpya katika mashauri mengine siku hizi:

kama hakuna maana kufanya bidii kubwa ya kujifunza Biblia au dini, kwa sababu kama tunaokolewa basi tutakuwa namna yoyote.

Ya kama yupo kiumbe aitwaye Ibilisi atulazimishaye kutenda dhambi na kuleta matata katika maisha yetu bila kujali mapenzi yetu. Wazo hili lisilo la kweli limejadiliwa katika somo la 6.

Ya kama hakuna haja kuomba matunzo ya Mungu katika hali ya maisha yetu, kama kulindwa wakati wa safari, kwa kuwa namna yoyote kila jambo lilikwisha pangwa. Walimwengu wana msemo, mara nyingi limesikika kwa bahati katika vyumba vya kuondokea wasafiri uwanja wa ndege,'Kama namba yako itatokea, itatokea tu’.

Makanisa ya kiinjili yanafundisha ya kwamba kwa muumini haiwezekani au kufahamu Biblia bila Roho Mtakatifu kutusaidia tuelewe.

Zipo sababu nyingi kamili za Biblia za kukataa hii aina ya elimu : -

Wazo lote la kumtii Mungu linafanywa kuwa ni upuuzi. tunaendelea kuambiwa siku zote katika Biblia kwamba yatupasa kutunza amri za Mungu, na kwa kufanya hivyo tunaweza kumpendeza au kutompendeza. Jambo hili lenye maagizo halina maana ikiwa Mungu anatulazimisha tumtii. Kristo anatoa wokovu kwa "Watu wote wanaomtii"
(Ebra. 5:9).

***Waebrania 11*** yaonyesha kwamba Mungu anapoingilia katikati ya maisha yetu na hatimaye kutupatia wokovu kumehusisha na imani yetu. Mifano mingi ya Biblia kuomba wokovu wa Mungu shida haiwi na maana kama kila jambo lilikwisha pangwa kabisa. Vivyo hivyo wazo la wokovu likiwa ni toleo la imani yetu kwa Kristo haliwi na maana tena.

Ubatizo ni sharti la wokovu (Marko. 16:16; Yoh. 3:3 -5). Hili wenye imani ya Kelvini wamekana. lakini, wokovu umewezekana kwa sababu ya kazi ya Kristo (2Tim.1:10), si kupitia wazo la kuwazika la kuchaguliwa kabla ya wakati . yatupasa sisi wenyewe kwa ufahamu tuchague kujiunga naye, mpango tunaofanya kwa kubatizwa. Mafungu ya maneno katika warumi 6:15 -17 yanatunena tunavyobadili mabwana katika Ubatizo, toka maisha ya dhambi hadi kuwa mtu wa kutii. "Kwake yeye ambaye mnajitoa nafsi zenu kuwa watumwa wake katika kumtii, mmekuwa watumwa wake yeye mnayemtii". Lugha hii ya kujitoa mtu mwenyewe ni dhahiri inadokeza mapenzi ya hiari kama yalipopingana na kwisha chaguliwa kusiko na sharti. Kujitoa ni kwa kutii katika moyo mafunzo ya Injili (Rum. 6:17).

Hakuna maana kwa Mungu kutoa neno lake, kama namna yoyote tulikwisha chaguliwa. tena hakuna maana ya kuhubiri; lakini Biblia, pande zote mbili katika amri na kuandika mifano ya

hii, inaonyesha kwamba ni kwa kuhubiri neno hata wanaume na wanawake kufika katika wokovu. "…..Neno la wokovu huu" (Mdo. 13:26) inabidi lipelekwe kwa watu.

Tutahukumiwa sawa sawa na matendo yetu (Uf. 22:12). Kwa nini, kama kutenda kwetu matendo tupendayo si muhimu katika kulingana na wokovu ? Paulo alisema ya kwamba Wayahudi wamejihukumu wao wenyewe kuwa hawastahili uzima wa milele kwa kulikataa neno la Mungu (Mdo. 13:46). Walikuwa wanajihukumu wenyewe - Mungu hakuwazuia. kama tukisema ya kwamba Mungu amewachagua watu wengine tangu mwanzo kupata wokovu na wengine wahukumiwe, basi kwa matokeo Mungu anawashurutisha watu kuwa watenda dhambi, kwa jinsi hiyo hiyo kama alivyotaka kuwalazimisha watu kuwa wenye haki. Kwa sababu ya dhambi ya Adamu "Mauti imewafikia watu wote, maana wote wametenda dhambi" (Rum. 5:12). ndiyo maana watu hufa, ikiwa ni adhabu kwa ajili ya dhambi kwa maana nyingine katika kipindi kabla ya dhambi ya Adamu.

1 Kor. 10 na mafungu mengi mengine ya maneno yameshika mfano wa waliokuwa zamani waliwahi kuwa na uhusiano na Mungu, lakini wakati ule wakaanguka, yakiwa maonyo kwa waumini. Uhakika ni kwamba upo uwezekano wa kuanguka toka hali ya neema (Gal. 5:4) maana yake ni kwamba hapawezi kuwepo 'aliyewahi kuokolewa siku zote akiwa ameokolewa' utaratibu wa wokovu kama unavyotakiwa na wenye imani ya Kelvini. Tukiendelea tu kushika mafundisho ya kweli tutaweza kuokolewa (1 Tim. 4:16).

Ni dhahiri Yesu alifundisha ya kwamba kuelewa neno la Mungu kunategemea hatua fulani iliyo juu ya bidii yetu kufanya tupendavyo. "Asomaye, na afahamu" (Mathayo. 24:15). Hivi

tunajiruhusu wenyewe kufahamu neno - hatulazimishwi. kati ya hivi upo usawa wa maneno yaliyorudiwa mara nyingi na Yesu ya kuwa "Aliye na masikio yenye kusikia ……. Na asikie" au afahamu. Kwa sababu hii kuwa na masikio yanayosikia, kumelinganishwa na kusoma neno la Mungu. Kwa kuwa Roho ya Mungu kwa ukuu sana imedhihirika katika neno lake kwa upana ambao Yesu aliweza kusema kwamba maneno yake yenye kuvuviwa na Mungu ni "Roho" (Yoh. 6:63) haiwezekani kwamba roho ya Mungu itatenda kazi juu ya mwanadamu, bila neno lake, ili kumshurutisha mwanadamu kuwa mtii katika neno.

"Yeyote atakaye" na "ayatwae maji ya uzima bure" (Uf.22:17), kwa kuitikia neno la uzima lipatikanalo katika Injili. Kwa kweli, hapa, ni kupenda kutenda atakavyo mtu kuliko kuchaguliwa tangu mwanzo bila kufikiri haja yetu binafsi kupata wokovu. vivyo hivyo matendo 2:21 "Na itakuwa kila (awaye yote) atakayeliitia jina la Bwana ataokolewa" kwa kubatizwa katika jina hilo.

***Tumeacha kitambo sehemu ya 7 : "Nanyi mtapokea Roho mtakatifu"***

Petro alihutubia mkutano mkubwa siku ya Pentekoste, akamalizia kwa ombi lililo katika aya ya 38 kutubu, kubatizwa na kupokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Huku kutajwa kipawa cha Roho ya Mungu kupo katika maneno yenyewe ya mitume wakiisha tumia karama hizo za kunena katika lugha katika mkutano, kunaelezea ya kwamba kufanya hivyo walikuwa wanatimiza unabii wa Yoeli unaohusu kupewa karama za kufanya miujiza (Mdo. 2:16 -20).kwa sababu hiyo inafaa kukubali kuwa ni kweli kwamba Petro alikuwa anaahidi karama za Roho kwa ule

mkusanyiko wa Wayahudi waliokuwa wanamsikiliza. Mkutano ulikuwa ni wa Wayahudi, si watu wa Mataifa (Mdo. 2:5).Unabii wa Yoeli kupewa karama ulihusika hapo kwanza na Wayahudi pekee. Basi, Petro ana maana hii kwao: "Ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu" (Mdo. 2:39), labda ilikuwa yataja unabii wa Yoeli ya kwamba Wayahudi watapewa Roho na watoto wao (Mdo. 2:17 linganisha Yoeli 2: 28 -32). Panaweza kuwa na kidokezo hapa cha kwamba ahadi ya karama hizi zenye miujiza ilikuwa kwa vizazi vile viwili pekee - waliokuwa wanamsikiliza Petro, na watoto wao.

Tumeonyesha ya kwamba mwishoni mwa karne ya Kwanza (Yaani, karibu miaka 70 baada ya hotuba ya Petro) vipawa vilifikia mwisho. Jambo hili tena limethibitishwa na taarifa za kihistoria. Pia kipindi cha vizazi hivyo vipawa vya Roho vilipatikana kwa watu wa Mataifa: "Na kwa watu wote walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie" (Mdo. 2:39). Fahamu jinsi watu wa mataifa wanavyoelezewa ya kuwa "walio mbali" katika Waefeso 2: 14 -17.

Walakini, kuna sababu nzuri ya kuamini kwamba lililotokea katika Mdo. 2 ulikuwa ni utimizo mdogo tu wa hayo maneno ya Yoeli 2. Utimilizo mkubwa utakuwa hapo Israeli akiisha vamiwa na Jeshi kisha nalo likiisha haribiwa (Yoeli. 2:27), "Hata itakuwa, baada ya hayo ya kwamba nitamimina Roho yangu juu yao wote wenye mwili ….." (2:28). Si hata hayo masharti yakionekana tutaweza kutafuta utimizo wowote mwingine wa maneno ya Yoeli, mbali toka utimilizo huo mdogo ulionekana siku ya Pentekoste kama ulivyoelezewa katika matendo ya mitume 2.

Ahadi ya kupokea kipawa cha Roho baada ya ubatizo, bado kinaweza kusomwa na ushahidi mwingine kwetu leo. Kuna roho

moja, lakini yaweza kuthihirika kwa njia mbali mbali (1 Kor. 12:4-7; Efe. 4:4).Katika karne ya kwanza hii ilikuwa katika vipawa vya miujiza; sasa kama vimeondolewa ni halali kabisa katika kuona utimilizo wa hiki “Kipawa cha Roho” kwa namna nyingine kilivyoahidiwa. “Kipawa cha Roho Mtakatifu”chaweza kutajwa 'Kipawa ambacho ni Roho Mtakatifu’, au katika kipawa ambacho Roho Mtakatifu anakisema yaani - kipawa cha msamaha wa wokovu ambao Roho -Neno lenye kuvuviwa la Mungu liliahidiwa. Ipo mifano mingi mingine ya matumizi haya ya neno “ ya, cha, na wa” (yenye kufahamika kuwili, katika ustadi) “Maarifa ya Mungu” (kol. 1:10) yaweza kuwa na maana maarifa ambayo Mungu anayo. Au maarifa juu ya Mungu. “Upendo wa Mungu” na “Upendo wa Kristo”

(1 Yoh. 4:9; 3:17; 2Kor. 5:14) ina maana upendo ambao Mungu na Yesu wamekuwa nao kwetu, au upendo ambao tunao kwao. “Neno la Mungu” laweza kuwa na maana neno kumhusu Mungu. Au neno ambalo limetokea kwa Mungu. Kipawa “cha” Roho Mtakatifu basi chaweza kutajwa kipawa ambacho Roho Mtakatifu anawezesha mambo na kuzungumzia sawa na kipawa ambacho kina nguvu za Roho Mtakatifu.

**KIPAWA CHA ROHO : MSAMAHA**

Rum. 5:16 na 6:23 inaeleza wokovu kuwa “Kipawa” - ikivuta mlinganisho na “Kipawa” cha Roho katika mdo. 2:38.Yaonekana kabisa kuwa matendo 2:39 unanukuu toka Yoeli 2:32 kuhusu wokovu kana kwamba hivi ndivyo kipawa cha Roho kilivyonukuliwa. Petro alitaja kipawa kilichokuwa kimeahidiwa kwa wale “Walio mbali” anataja katika kusema kwa Isaya 57:19: “Amani (ya Mungu kwa kusamehewa) kwake yeye aliye mbali”. Waefeso 2:8 aya hii inaeleza kipawa hiki kuwa ni wokovu, na kusema kwamba “katika Roho mmoja (Kipawa hiki) sisi sote

tumepata njia ya kumkaribia Baba" (2:18). hiki kimefanywa thabiti kwa uhakika kwamba Efe. 2:13 -17 tena kinatajwa kwa kusema katika Isaya 57:19: "Ninyi mliokuwa mbali hapo kwanza mmekuwa karibu kwa damu yake Kristo. Kwa maana yeye ndiye amani yetu …..akaja akahubiri amani kwenu ninyi mliokuwa mbali" Isaya 30:1 unawalaumu Wayahudi kwa kuutafuta msamaha kwa njia yao wenyewe kuliko toka kipawa cha Roho ya Mungu:'Wajifunikao kwa kifuniko (upatananisho) lakini si cha Roho yangu, wapate kuongeza (Badala ya kutoa) dhambi juu ya dhambi" Isaya 44:3 unaeleza msamaha wa siku hizi kwa Israeli kwa maneno haya: "Kwa maana nitamimina maji …… na vijito vya maji juu ya mahali pakavu (ukavu kiroho - Isa. 53:2): nitamwaga Roho yangu juu ya wazao wako, na baraka yangu juu yao utakaowazaa" Baraka ya uzao wa Ibrahimu ni kwa kusamehewa kwao kwa njia ya Kristo (Mdo. 3: 25, 26) msamaha uliopo hapa ni sawa na kumwagiwa Roho juu ya Wayahudi.Huu msemo wazi wa Yoeli 2, na matendo 2. Gal. 3:4 unaweka yote haya katika maneno mengi sana; ili kwamba baraka ya Ibrahimu (Msamaha) uwafikie mataifa katika Yesu Kristo, tupate kupokea ahadi ya Roho" Basi 1 Kor. 6:11 unanena kuoshwa dhambi zetu "Kwa Roho ya Mungu wetu" Upo usawa kwa warumi kati ya sisi kupokea "neema …..upatanisho …. Roho" (1:5; 5:11; 8:15), na kuonyesha muungano kati ya kipawa ("Neema") ya Roho na msamaha unaotuongoza hata kupata upatanisho. Ni vigumu kuelezea zaidi ni kiasi gani Agano Jipya linategemea msemo na mtungo wa maneno ya Agano la Kale, hasa kwa mtazamo wa kwanza wa Wayahudi na ushawishi uliokuwa na nyaraka. Mara kwa mara katika vitabu vitano vya kwanza katika Biblia (Pentateuch) na Yoshua Mungu anaahidi kuwapa nchi watu wake - "nchi akupayo Bwana Mungu wako uimiliki" ni maneno ya kawaida. Kifani cha nchi iliyochini ya Agano Jipya ni Wokovu; basi ni kipawa cha Mungu ambacho sasa ni mtazamo, na kuwa

pamoja na msamaha wa dhambi. Gal. 3: 2,5 linganisha na 3:8 -12, inasawazisha kupokea roho na. Kupokea baraka za Ibrahimu za wokovu na msamaha. “Ahadi ya Roho”(Gal. 3:14) imesemwa katika maneno yenyewe ya ahadi kwa Ibrahimu.

Petro aliwataka wayahudi watubu kabla ya kuweza kupokea kipawa; hiki kilihusisha sala ya mtu binafsi. hapo yaonekana kusadiki ya kwamba kipawa cha Roho ni namna ya kuelezea sala iliyojibiwa. Kupewa “Vitu vyema wale waombao” katika sala ni mamoja kama kupewa (kipawa) cha Roho Mtakatifu (Math. 7:11; linganisha Luk. 11:13).Wafilipi 1:19 unasawazisha “Kuomba kwenu ni kuruzukiwa Roho wa Yesu Kristo”. Vile vile, 1 Yoh. 3:34 tunasoma ya kwamba tunapewa Roho kama toleo la kutii kwetu amri; aya ya 22 inasema kwamba kutii amri hizo kunapelekea kujibiwa maombi yetu. Basi, ujasiri wetu ni kwa sababu maombi yetu yamesikiwa (1Yoh. 5:14) na tena kuwa na Roho (1 Yoh. 3: 21, 24; 4: 13), elewa maelezo haya yanalingana

Neno'Kujifunza’ kwa neno la kiyunani ni'Charis’, mara nyingi limetafsiriwa “Neema” litaonyesha kwamba mara nyingi limetumika kwa muunganiko na kipawa cha Roho.

“Kwa (kipawa) cha neema ya Bwana Yesu Kristo tutaokoka” (Mdo.15:11). Lakini wazo la'neema’ mara nyingi limegawanyika na ombi lililojibiwa (kama kutoka 3: 12; 34:9; Hesabu 32: 5; Zab. 84:11; 2Kor. 12:9; Ebr. 4:16; Yakobo. 4:6 na mstari wa 3). Zakaria 12:10 unasema siku ya mwisho kumwagiwa “Roho ya neema na kuomba” wayahudi. Huu unaelezea kwa ufupi tunachodokeza - kuwa sala (“Maombi”) yanaleta kipawa cha Roho katika maana ya msamaha, na huku kupewa Roho kwa kujibu maombi kumeonyeshwa katika namna ya toba ya kiyahudi ya karne ya kwanza na siku za mwisho. kwa maneno hayo hayo

yenyewe ayasemayo Paulo, “Karama na mwito wa Mungu” kufikia toba na msamaha (Rum. 11 29).

## MSAIDIZI

Kukaribia huko huko kunaweza kutumika katika ahadi ya msaidizi katika milango ya Yohana 14: na 16. Kimsingi huyu alitajwa ni nguvu zenye miujiza walizopewa wafuasi, ambao waliahidiwa hapo kwanza, pia ahadi inaweza kutuhusu nasi katika maana isiyo na miujiza. Karama zilikuwa kwa “Kuwakumbusha mambo yote, niliyowaambia”

(Yoh. 14:26), kwa kuthubutu kuwezesha kuandika taarifa za Injili.

Neno “kuwakumbusha” lenyewe lawekea mipaka jambo lenye miujiza ya ahadi ya msaidizi kwa wafuasi, walioishi na Yesu wakati wa utumishi wake. Waliweza kuwa na maneno ya Yesu tu yaliyorudi katika kumbukumbu zao na msaidizi. Lugha ya ahadi ya'Msaidizi' inatumika pia katika uwezo wa Biblia iliyokamilika. Kwa sababu hiyo tunaweza kumalizia ya kuwa hizi na ahadi nyingine za Roho zilitumika katika mfano wa miujiza kwenye karne ya kwanza, lakini sasa yatuhusu sisi katika ufunuo wa Roho kwa njia ya neno la Mungu lililoandikwa katika Biblia. Bila shaka, ni kweli kwamba Roho ya Mungu ilidhihirika katika neno lililoandikwa zamani, lakini hili ulikuwa ni ufunuo wa sehemu ukilinganishwa na utimilizo (“Ukamilifu”) ambao sasa tunao katika neno la Mungu lililokamilika (1 Kor.13:9 -13). kwa sababu hii ni kwamba haujakuwepo ufunuo wowote mwingine ulioandikwa toka kwa Mungu baada ya kuondolewa karama mara Agano Jipya lilipokamilika. Kadhia za kitabu cha Wamormoni na vingine kama hivi vilivyochapishwa, vinadokeza kwamba Biblia si ufunuo uliotimilika - kutokuwepo karama za roho leo

kunathibitisha ni hivyo. Kama tunataka kuutumia utimizo wote wa Mungu katika ufunuo wake ulio katika Biblia, yatupasa tutumie kila sehemu yake, sehemu zote mbili Agano la Kale na Agano Jipya, wakati huo tu mtu wa Mungu anaweza kuanza kuwa kamili kama ukamilifu wa Mungu, uliodhihirika katika neno.

**Tumeacha kitambo sehemu ya 8 : " Na ishara hizi zitafuata" (Marko 16:17).**

Neno hili limekazwa, ya kwamba kila mtu aaaminiye kweli atapokea karama zenye miujiza. Lakini hili linathibitisha mno - "Watashika nyoka; hata wakinywa kitu cha kufisha, hakitawadhuru kabisa; wataweka mikono juu ya wagonjwa, nao watapona" (Marko 16:18). Hii si ahadi ya mambo ambayo kinadharia yaweza kutokea ikiwa aaminiye alikuwa na imani ya kutosha; hizi zilikuwa ahadi za uhakika kwa udhahiri kitakachofanywa na Waaminio. Ishara hizi zilipofanywa kwa uwazi, ahadi ya mstari huu haiwezi kutuhusu sisi kwa wakati uliopo. Unaweza kukumbuka jinsi Paulo aliweza kumshika nyoka mwenye sumu bila kugongwa (Mdo. 28: 3 -7), uthibitisho wa mahubiri yake ukatokea ya kuwa yametoka kwa Mungu.

Wakristo wa madhehebu yaitwayo yote ya kiroho waliodai kuwa na karama kipindi cha wakati uliopita miaka mia moja iliyopita, haukuwepo ushuhuda wenye ukweli wa nguvu hizi kutendwa. Kila aaminiye asipoweza kuonyesha ishara za ukubwa huu, ahadi hii haitahusu leo. Hii inatuacha na dhana tuliyoileta toka kwenye uchunguzi wetu kwa Biblia ifundishayo kuhusu Roho: hizi karama zenye miujiza zilikuwa na wakristo wa kwanza katika karne ya kwanza, lakini zilikoma kushikwa baada ya Agano Jipya maandiko yake kukamilika.

Aya ya mwisho kwa Marko 16 inadokeza kuwa miujiza "itafuatana" na hao walioamini kwa madhumni maalum ya kuthibitisha neno la Injili lililosemwa "Ishara zitafuatana na hao waaminio …….. wakaenda na kuhubiri kila mahali, Bwana akitenda kazi pamoja nao, na kuthibitisha neno kwa ishara zilizofuatana nalo"

(Marko 16:17,20). Mara neno lililotamkwa likaandikwa kwa ukamilifu, kama tulivyonalo sasa katika Agano Jipya, hapakuwa na haja ya Ishara za Miujiza kuwafuata wale walioamini.

**Maelezo yaliyoandikwa chini ya Ukurasa :**

Siku hizi yameenea mno madai ya kuwa na karama za Roho ya kwamba katika mwaka 1989 mijadala miwili ya halaiki ilifanyika kati ya mchungaji wa dhehebu la kiroho, Yohana Liliekas, na Wakristadelfiani wawili; Bwana John Allfree na mwandishi wa sasa. Mwendo ulikuwa: "Je ! karama zenye miujiza ya Roho Mtakatifu wanayo watu leo?" Mwaliko ulitumwa kwenye makanisa mengi ya U.K; ukatokea mkutano wa watu walioungana zaidi ya watu 1000. Inastahili kusadiki ya kwamba' Ushuhuda' mzuri sana wenyekuwa na karama ungeonyeshwa. Nakala ya Habri inapatikana toka kwa :

**CHRISTADELPHIAN ADVANCEMENT TRUST PO Box 3034 South Croydon SURREY CR2 0ZA ENGLAND**

**Somo la 2 : Maswali**

1.Kati ya haya yafuatayo ni maneno gani yana maana ya 'Roho' ?

a) Nguvu b) Takatifu
c) Pumzi d) Mavumbi

2. Roho Mtakatifu ni nini ?

a) Mtu b)Nguvu
c)Uweza wa Mungu d)Sehemu ya Utatu.

3. Biblia iliandikwa kwa jinsi gani ?

a) Watu waliandika mawazo yao wenyewe
b) Watu waliandika Mungu alikuwa na mawazo gani
c) Watu walivuviwa na Roho ya Mungu
d) Baadhi ya sehemu walivuviwa, sehemu nyingine hapana.

4. Ni sababu zipi zifuatazo zilitolewa zenye karama ya miujiza ya Roho ?

a) Kusaidia tendo la kuhubiri Injili
b) Kuendeleza kanisa la kwanza
c) Kuwashurutisha watu wawe wenye haki
d) Kuwaokoa mitume toka katika shida zao wenyewe.

5. Kutoka wapi tunakoweza kujifunza kweli ya Mungu ?

a) Kwa sehemu katika Biblia, kwa sehemu toka fikira zetu wenyewe
b) Toka Roho Mtakatifu akituambia jambo moja moja mbali ya kusoma Biblia
c) Toka katika Biblia pekee
d) Toka kwa watumishi / Makuhani wa dini

6. Taja baadhi ya karama za Roho zilizokuwepo karne ya Kwanza.

7. Ni lini ziliondolewa ? Je ! yawezekana kuwa nazo sasa ?

8. Ni jinsi gani Roho Mtakatifu anaweza kufanya kazi katika maisha yetu leo ?

# *SOMO LA 3*

# AHADI ZA MUNGU

## 3.1 Ahadi za Mungu : Dibaji

Kwenye hatua hii ya masomo yetu tumefikia kufahamu upana wa Mungu ulivyo na jinsi anavyofanya kazi kwa kufanya hivyo tumepanga idadi ya makosa yahusuyo mambo haya. Sasa tunataka kuangalia kwa uhakika zaidi mambo ambayo Mungu "amewaahidi wampendao" (Yakobo 1:12; 2:5) kwa kushika amri zake (Yah. 14:15)

Ahadi za Mungu katika Agano la kale zinatumaini la Kikristo ndani yake. Akijitetea hukumuni, Paulo alizungumzia thawabu ijayo iliyomfanya awe tayari kupoteza vitu vyote: "Na sasa nasimama hapa nihukumiwe kwa ajili ya tumaini la ahadi ya baba zetu …….. nami ninashitakiwa na Wayahudi kwa ajili ya tumaini hilo" (mdo. 26:6,7). alitumia muda mwingi wa maisha yake kuhubiri "Habari njema (Injili), jinsi Mungu alivyofanya ahadi kwa mababa, Mungu amewatimizia …… kwa kumfufua Yesu" (mdo. 13:32,33). Paulo alieleza kuwa kuamini hizo ahadi kulitoa tumaini la ufufuo toka wafu (mdo. 26:6 -8 na 23:8). Kufahamu kuja kwa pili yesu kwa hukumu na ufalme wa Mungu ujao (Mdo. 24:25; 28:20, 31).

Ahadi zote hizi zinadhamisha hadithi ya kuwa Agano la kale ni historia tu iliyotembea ya Israel isiyousema uzima wa milele. Mungu hakuamua ghafla miaka 2000 iliyopita kuwa atatupatia uzima wa milele kwa njia ya Yesu. Ni kwamaba kusudi lilikuwa naye tangu mwanzo. “Katika tumaini la uzima wa milele, ambako Mungu asiyeweza kusema uongo, aliuahidi kabla ya ulimwengu kuanza;akalifunua neno lake kwa majira yake katika ule ujumbe kwa kuhubiri” (Tito 1:2,3). “Ule uzima wa milele, uliokuwa na Baba, ukadhihirika kwetu”(1 Yoh. 1:2)

Kwa kuwa kusudi la Mungu la kuwapa watu wake uzima wa milele lilikuwa naye tangu mwanzo , haikuwa na maana kuwa angebakia kimya kuhusu huo wakati wa miaka 4000 ya kujishughulisha na watu taarifa iliyo katika Agano la Kale. Kwa kweli, Agano la kale limejaa ahadi na unabii ambazo kila moja inatoa maelekezo ya tumaini hili ambalo Mungu amewatayarishia watu wake.

Ni kwa sababu hii ya kuwa kutambua ahadi za Mungu kwa mababa wa Wayahudi ni za muhimu kwa wokovu wetu: zaidi hapa Paulo aliwakumbusha waaminio katika Efeso ya kwamba kabla ya kujua mambo haya, “hawa kuwa na Kristo wakiwa wamefarakana na jamii ya Israeli, wageni wasio wa ahadi ile, mlikuwa hamna tumaini, hamna Mungu duniani” (Efe. 2:12) - ingawa pasipo shaka walidhani ya kuwa imani yao ya awali ya kipagani iliwapa tumaini lingine na maarifa ya kumjua Mungu. lakini hili ni jambo la kufikiria sana kutokujua ahadi za Mungu katika Agano la kale -kwa ukweli “ni kutokuwa na tumaini,na pasipo na Mungu duniani’. Kumbuka jinsi Paulo alivyofafanua tumainai la Kikristo kuwa ni “tumaini la ahadi zilizofanywa na Mungu kwa baba wa Wayahudi” (Mdo. 26:6).

Ni ukweli wa kusikitisha kuwa makanisa machache yanaweka mkazo juu ya sehemu hizi Agano la kale ambazo wanatakiwa. "Ukristo" Ukristo umeharibika tabia na kuwa dini ambayo msingi wake ni Agano Jipya - ingawa hata wakati huo wanaelekea kutumia mistari michache ya kutoka hilo.Yesu ameweka kwa uwazi mkazo unaozunguka njia sahihi:

"Wasipowasikia Musa (yaani, Vitabu vya kwanza vitano vya Biblia alivyoandika) na mnabii, hawatashawishiwa hata mtu akifufuka katika wafu" (Luka. 16:31).

Nia ya mwili inaweza kufikiri kuwa kuamini kwamba Yesu alifufuliwa yatosha (Luka. 16:30), Lakini Yesu alisema ya kuwa pasipo kuelewa vema Agano la Kale, hii haitawezekana kabisa.

Kukata tamaa kwa Wanafunzi baada ya kusulubishwa kulifuatishwa na Yesu kwa kutoangalia kwao kwa makini kwenye Agano la Kale.

"Akawaambia, Enyi msiofahamu, wenye mioyo mizito ya kuamini yote (kwa usahihi) waliyoyasema manabii: Je? Haikumpasa Kristo kupata mateso haya na kuingia katika utukufu wake ? Akaanza kutoka Musa na manabii wote, akawaeleza katika maandiko yote mambo yaliyomhusu yeye mwenyewe" (Luka. 24:25 -27).

Ona mkazo wake juu ya namna Agano lote la kale lilivyomsema yeye. sio kwamba Wanafunzi hawakuwahi kulisoma au kusikia maneno ya Agano la Kale, bali hayo maneno hawakuyaelewa Vizuri, na kwa sababu hii hawakuweza kuyaamini kwa kweli. hivyo kuelewa kwa usahihi neno la Mungu, kuliko kusoma tu, ni muhimu kukuza imani ya kweli. Wayahudi walikuwa washupavu kwa kusoma agano lao la kale (mdo. 15:21), Lakini hawakuelewa mistari yake iliyataja mambo ya Yesu na Injili yake, kwa kweli hawakuamini, na hivyo Yesu akawaambia:-

“Kama mungalimwamini Musa, mungeniamini mimi; kwa sababu yeye aliandika habari zangu. lakini msipoyaamini maandiko yake, mtayaamini wapi maneno yangu? (Yoh. 5:46,47).

Mbali ya kusoma Biblia yao, hawakuwa wanaona ujumbe wa kweli kumhusu Yesu, ingawa walipenda kudhani walikuwa wamehakikishiwa wokovu. Yesu ilimbidi kuwaambia.

“Mwayachunguza maandiko.(Yaani, kwa uzuri -mdo. 17:11); kwa sababu mnadhani kwa ujasiri kwamba ninyi mna uzima wa milele ndani yake: na hayo ndiyo yaliyonishuhudia” (Yoh. 5:39)

Na ndivyo inaweza kuwa na watu wengi walio na elimu ya habari ndogo ya maneno ya maana ya matukio baadhi na mafundisho ya Agano la Kale: ni marifa tu ambayo yamechukua kwa kubahatisha. ujumbe wa ajabu wa Kikristo na Injili ya ufalme wa Mungu bado unawaepuka. ni lengo la somo hili kukutwaa toka nafasi hiyo kwa kukueleza maana ya kweli ya ahadi kubwa za Agano la Kale:-

- ***Katika bustani ya Edeni***
- ***Kwa Nuhu***
- ***Kwa Abrahamu***
- ***Kwa Daudi***

Habari zake zinapatikana katika vitabu vya kwanza vitano vya Biblia (Mwanzo - Kumbukumbu la Torati) vilivyoandika na Musa na katika manabii walio kwenye Agano la Kale. Yote yalishikamana na Injili ya Kikristo inapatikana humu. Paulo alieleza kuwa mahubiri yake ya Injili hii - akasema “Sisemi neno ila yale ambayo manabii na Musa waliyasema, kwamba yatakuwa; ya kwamba Kristo hana budi kuteswa na ya kwamba yeye kwanza kwa kufufuliwa katika wafu atatanganza habari za nuru kwa watu wake na kwa watu wa mataifa” (Mdo. 26:22,23), na

katika siku zake za mwisho wimbo ulibakia ule ule: "Yeye (Paulo) akawaeleza kwa taratibu na kumshuhudia ufalme wa Mungu ….. kwa maneno ya sheria ya Musa na ya manabii, tangu Asubuhi hata Jioni" (mdo. 28:23)

Tumaini la Paulo, hilo kuu la Kikristo, liwe tumaini linalotuchochea nasi pia; kama ilivyokuwa nuru yenye utukufu mwishoni mwa tundu la maisha yake, vivyo liwe ni tumaini kubwa kwa kila Mkristo. likiwasha kwa kichocheo hiki, sasa tunaweza "Kuyachunguza Maandiko".

## 3.2 Ahadi Katika Edeni

Kisa cha kutia huruma cha kuanguka mtu kimetajwa mwanzo sura ya 3. Nyoka alilaaniwa kwa kunukuu vibaya neno la Mungu na kumjaribu Eva kirahisi. kwa kutokutii kwao mwanaume na mwanamke waliadhibiwa. lakini mwanga wa tumaini unaingia ndani ya picha hii yenye giza Mungu alipowaambia Nyoka: -

"Nami nitaweka Uadui (kuchukua upinzani) kati yako na huyo mwanamke, na kati ya uzao wako na uzao wake: huo (Uzao wa mwanamke) utakuponda kichwa na wewe utamponda kisigino" (Mwanzo. 3:15).

Huu mstari kwa kirefu umeongeza nguvu; tunahitajika kupambanua kwa makini mambo mbali mbali yaliyohusishwa. "Uzao maana yake mwana au mtoto, lakini vile vile unaweza kutaja watu waliojumuika na "Uzao" mmoja. Tutaona baadae ya kuwa "Uzao" wa Abrahamu alikuwa ni Yesu (Gal.3:16), lakini ni kwamba kama tukiwa "Ndani" ya Yesu kwa njia ya Ubatizo, Basi vile vile tumekuwa na uzao (Gal. 3:27 -29). Hili neno "Uzao"

pia linatajwa jambo la mbegu (1 Pet. 1:23); hivyo uzao wa kweli utakuwa na tabia ya sifa ya Baba yake.

Uzao wa Nyoka inabidi basi utajwe ule ulio na jamii ya kufanana na Nyoka:-

- Unaharibu maana ya neno la Mungu
- Unadanganya
- Unawaongoza wengine katika kutenda dhambi.

Tutaona katika somo la 6 kuwa hayupo mtu halisi anayefanya hivi, bali ndani yetu sisi upo.

- "utu wetu wa kale " wa mwili (Rum.6:6)
- "Mwanadamu wa tabia ya asili" (1 Kor.2:14)
- "Utu wa zamani, unaoharibika (Unaooza) kwa kuzifuata tamaa zenye kudanganya" (Efe. 4:22).
- "Utu wa kale pamoja na matendo yake" (Kol.3:9).

Huu utu wa dhambi ulio ndani yetu ni "Ibilisi" wa kwenye Biblia, uzao wa nyoka. Uzao wa mwanamke ulikuwa uwe ni mmoja dhahiri - "utamponda (uzao wa nyoka) kisigino" (Mwa.3:15) huyu mtu alikuwa daima akiuponda uzao wa nyoka, yaani dhambi -"Utakuponda kichwa". Kumpiga nyoka kwenye kichwa ni pigo la mauti kwa kuwa ubongo wake umo kichwani mwakeMtu pekee anayefaa heshima ya kuwa uzao wa mwanamke inampasa awe ni Bwana Yesu:

"Yesu Kristo, ambaye (kwa msalaba) ameondoa mauti (na hivyo ni nguvu ya dhambi - Rum.6:23) na kuufunua uzima na kutoharibika kwa ile Injili" (2 Tim. 1:10).

“Mungu kwa kumtuma mwanae mwenyewe katika mfano wa mwili ulio wa dhambi, aliihukumu dhambi katika mwili” yaani Ibilisi wa Biblia, Uzao wa nyoka (Rum. 8:3)

Yesu “alidhihirishwa ili aziondoe dhambi zetu” (1Yoh. 3:5).

“Nawe utamwita jina lake Yesu (maana yake 'Mwokozi’): maana yeye ndiye atakayewaokoa watu wake na dhambi zao” (Math.1:21).

Yesu mwenyewe “alizaliwa na mwanamke” (Gal. 4:4) akiwa ni mwana wa Mariamu, Ingawa Mungu alikuwa ni Baba yake. Hivi kwa maana hii, pia, alikuwa ni uzao wa mwanamke, ingawa alitolewa na Mungu kwa namna ambayo hakuna mtu amewahi kutokea wa jinsi hiyo. huu uzao wa mwanamke uliumizwa kidogo na dhambi, uzao wa nyoka - “Utakuponda kisigino” (Mwa. 3:25). Nyoka akiuma kisigino kwa kawaida ni kuumia kwa muda, kukilinganishwa na siku zote kumponda nyoka kichwani. Mifano mingi ya misemo ina asili ya Biblia: “Mponde Kichwani” (Yaani kukikomesha kitu kabisa) labda msingi wake ni kwenye unabii huu wa Yesu akimponda Yesu kwenye Kichwa.

Kuihukumu dhambi, uzao wa nyoka, kwanza ilikuwa kwa dhabihu ya Kristo msalabani - fahamu jinsi mistari ilivyonukuliwa inavyousema ushahidi wa Kristo juu ya dhambi kwa wakati uliopita. maumivu ya muda kwenye kisigino aliyoyapata yesu, basi, kinatajwa kifo chake kwa siku tatu. Ufufuo wake ulithibitisha kuwa maumivu yalikuwa ni ya muda tu, ukilinganisha na pigo la mauti aliloipa dhambi. inavutia ya kwamba hakuna taarifa ya historia ya Biblia inayoonyesha ya kwamba watu wa kusulubiwa walipigiliwa misumari visigino vyao kwenye gogo la mti. Hivyo Yesu “alichubuliwa kisigino” kwa kifo chake. Isaya 53: 4 -5 yaeleza kristo “alichubuliwa” na Mungu kwa kifo chake msalabani. Hii ni wazi inataja unabii wa Mwa.3:15 kuwa Kristo

alipondwa na uzao wa nyoka. Walakini mwishowe Mungu alitenda haki kwa mabaya aliyokabiliwa nayo Kristo, amesema hapa kuwa anamchubua (Isaya 53:10) kwa ajili ya kutawala nguvu ya mabaya yaliyomchubua mwanae. Hivyo pia Mungu anatenda kazi kwa mabaya kila anayoyapata mtoto wake.

**PIGANO LA LEO**

Lakini swali linaweza kuwa limezuka akilini mwako: "Ikiwa Yesu amebatilisha dhambi na mauti (uzao wa nyoka) ni kwa nini mambo hayo bado yapo leo ?" Jibu ni kwamba msalabani Yesu aliangamiza nguvu ya dhambi ndani ya nafsi yake mwenyewe: Unabii wa Mwa. 3:15 ni wa kwanza kumhusu Yesu kupingana na dhambi. Sasa hii inamaanisha ya kwamba kwa kuwa ametualika kuushiriki ushindi wake, hatimaye, nasi pia, tunaweza kushinda dhambi na mauti.

Wale ambao hawajaalikwa kuushiriki ushindi wake , au wanaokataa anapowapa, bila shaka, bado watapata dhambi na mauti. Ingawa dhambi na mauti vinawapata waamini wa kweli, kwa kuunganika kwao na uzao wa mwanamke kwa njia ya ubatizo katika Kristo (Gal. 3:27 -29) wanaweza kusamehewa dhambi zao na kwa hiyo hatimaye wataokolewa toka kwenye mauti, ambayo ni matokeo ya dhambi. Hivyo kwa kuangalia mbele"alibatilisha mauti" msalabani (2Tim.1:10), ingawa sivyo mpaka kusudi la Mungu kwa dunia liwe limekamilika mwishoni mwa baada ya miaka ya elfu hapo watu watakapo koma kufa - mauti hayatashuhudiwa tena juu ya dunia: "maana sharti amiliki yeye (kwa sehemu ya kwanza ya ufalme wa Mungu) hata awawekee maadui wake wote chini ya miguu yake. Adui wa mwisho atakayebatilishwa ni mauti" (1 Kor 15:25,26).

Kaama "ukibatizwa katika Kristo" basi ahadi kumhusu Yesu, kama zile za mwanzo 3:15, zinakuwa zetu wenyewe; haziwi tena sehemu za kuvutia tu za Biblia, ni unabii na ahadi zilizofanywa kwetu moja kwa moja ! kama uzao wa mwanamke nasi pia, tutapata ushindi wa dhambi juu yetu kwa muhula mfupi. Bwana asiporudi wakati wetu tukiwa hai, nasi pia tutapondwa kisigino kama Yesu, ni kwamba nasi pia tutakufa. Lakini kama kweli tu uzao wa mwanamke , wakati huo hilo "Jeraha" litakuwa ni la kitambo tu. waliobatizwa vema katika kristo kwa kuzamishwa ndani ya maji, wanaunganika wenyewe na mauti yake na ufufuo - kunakoashiria kwa kutoka katika maji (Ona Rum. 6:3 -5).

Kama tukiwa ni uzao wa mwanamke , basi maisha yetu yatarudisha mfano wa maneno ya Mwa 3:15 - daima kutakuwepo na akili ya kupigana ("Uadui") ndani yetu, kati ya haki na uovu. Paulo mtume kubwa ameeleza karibu ugonvi wa akilini katika kupingana kati ya dhambi na moyo wake halisi ambao ulichafuka ndani yake (Rum. 7:14 -25).

Baada ya kubatizwa katika Kristo, pigano hili na dhambi ambalo ni tabia ya kawaida ndani yetu litaongezeka na kuendelea kufanya hivyo siku zetu zote. Kwa akili ni vigumu kwa sababu nguvu ya dhambi ni kubwa. lakini kwa maana nyingine sivyo, kwa kuwa tumo ndani ya Kristo, ambaye tayari amepigana na kulishinda pigano. Fahamu jinsi waaminio walivyosemwa wao ni mwanamke katika Waefeso 5:23 -32, kana kwamba kwa kuwa uzao wa mwanamke vile vile tu mwanamke.

Kwa jinsi hiyo hiyo kama uzao wa mwanamke unamaanisha wawili Yesu na hao wanaojaribiwa kuwa na tabia ya kuwa na sifa yake, basi uzao wa nyoka unasemwa sehemu mbili dhambi ("Ibilisi"wa kwenye Biblia) na hao ambao kwa hiari wanaonyesha

tabia ya dhambi na nyoka.Watu hawa hawatojari au hawatatoa maana nzuri ya neno la Mungu , ambalo mwishowe litawapeleka katika aibu ya dhambi na kutengwa na Mungu, Jambo lililotokea kwa Adamu na Hawa. Kwa kuwa Wayahudi walikuwa watu hasa walomuua Yesu -Yaani waliuponda uzao wa mwanamke kwenye kisigino - itegemewe ya kuwa walikuwa ni mifano mkubwa wa uzao wa nyoka. Hii imethibitishwa na Yohana mbatizaji na Yesu:

"Hata alipowaona wengi (Yohana) miongoni mwa mafarisayo na masadukayo (kundi la Wayahudi waliomhukumu Yesu) wakiujia ubatizo wake, aliwaambia enyi uzao wa nyoka ,(Yaani wanaume na wanawake wameumbwa na) Nyoka nani aliyewaonya ninyi kuikimbia hasira itakayokuja ?" (Math. 3:7)

"Basi Yesu akijua mawazo yao (Mafarisayo), akawaambia ….. Enyi wazao wa nyoka , mwawezaje kunena mema , mkiwa wabaya ?" (Math.12:25,34).

Ulimwengu - hata ulimwengu wa dini - una tabia hizi hizi za nyoka. waliobatizwa tu katika Kristo hao tu wameunganika na uzao wa mwanamke; wengine wote, wana viwango vinavyopishana, vya mbegu za nyoka. Jinsi Yesu alivyowatendea watu ambao walikuwa mbegu ya nyoka inabidi uwe ni mfano wetu: -

Aliwahubiri kwa roho na upendo na ipasavyo kweli, lakini
Njia zao na fikira havikumvuta, na
Aliwaonyesha tabia ya upendo ulio na Mungu kwa njia aliyoishi.

Lakini kwa yote hayo walimchukia. Bidii yake mwenyewe kuwa mtiifu kwa Mungu kuliwafanya kuwa na wivu. Hata jumla zake (Yoh. 7:5; Marko. 3:21) na marafiki wa karibu (Yoh. 6:66)

waliweka vikwazo na wengine wakamwacha na kwenda zao. Paulo alipata jambo hilo hilo alipowalilia waliowahi kusimama pamoja naye katika makubwa na madogo: "Je ! nimekuwa adui wenu kwa sababu nawambia yaliyo ya kweli ?" (Gal. 4:14 -16).

Kamwe ukweli sio wa wote; kuujua na kuishi kwa huo kama inavyopaswa siku zote huleta aina nyingine ya matatizo kwetu, hata kusababisha maudhi: "kama vile yule aliyezaliwa kwa mwili alivyomuudhi yule aliyezaliwa kwa roho (Kwa elimu ya kweli ya neno la Mungu -1 Petro.1:23), ndivyo ilivyo na sas" (Gal. 4:29).

Ikiwa kwa kweli tumeunganika na kristo yatupasa kuonja mateso yake mengine, hivyo basi tutaweza pia kushiriki katika thawabu yake yenye utukufu. tena Paulo anatuwekea mfano usio na kifani kwa hili:-

"Ni neno la kuaminiwa: kwa maana , kama tukifa pamoja naye, tutaishi pamoja naye pia (kristo); kama tukistahimili, tutamiliki pamoja naye; (2 Tim. 10 -12).

"Ikiwa waliniudhi mimi (Yesu), watawaudhi nanyi pia ……Mambo yote haya watawatendea kwa ajili ya jina langu" (Yoh. 15:20,21)

Yaani, kwa sababu tumebatizwa kwa jina la Yesu (Mdo 2:38;8:16).

Kukubaliwa na mistari kama hii, inajaribu kuleta sababu, "kama huko ndiko kuungana na Yesu, Uzao wa mwanamke, yahusika mambo yote, nisingependa hata kidogo" Lakini bila shaka hatutategemea kuingia jambo lolote ambalo hatuwezi kwa maana ya kushindana nalo. Wakati wa kujitoa nafsi ni dhahiri unatakiwa ili kutuunga wenyewe kabisa na Kristo, Sisi kuungana naye tutasababisha thawabu hii yenye utukufu "Kwani mateso ya sasa hayawezi kulingana na utukufu utakaodhihirika kwetu" Na hata sasa dhabihu yake inawezesha maombi yetu tusaidiwe katika

masumbufu ya maisha kuwa hasa yenye nguvu kwa Mungu. Na nyongeza kwa hili yafuatayo ni matumaini yenye utukufu, kwa uzito yameelekezwa katika Biblia nyingi za Kristadelfiani:-

"Mungu ni mwaminifu, ambaye hatawaacha mjaribiwe kupita mwezavyo; lakini pamoja na hilo jaribu atafanya na mlango wa kutokea, ili mweze kustahimili" (1Kor. 10:13)

"hata (mambo) nimewaambieni mpatekuwa na amani ndani yengu. Ulimwernguni mnayo dhiki; lakini jipeni moyo; mimi nimeushinnda ulimwengu" (Yoh. 16:33)

"basi, tuseme nini juu ya (mambo) hayo ? Mungu akiwepo upande wetu, ni nani aliye juu yetu ?" (Rum. 8:31).

### 3.3 Ahadi Kwa Nuhu

Maendeleo ya historia ya mwanadamu yalipokwenda mbele baada ya kipindi cha Adamu na Eva, mwanadamu akaongezeka na kuwa mwovu sana, mambo yalifikia hatua ambayo ustarabu wa uadilifu ukaharibika mno ambapo Mungu akaamua kuuharibu utaratibu wa mambo, Isipokuwa nuhu na familia yake (Mwa. 6:5-8).Akaambiwa atengeneze safina ambayo ndani yake yeye na wanyama wote miongoni mwa waliochaguliwa wataishi kipindi cha wakati hapo ulimwengu utakapokuwa unaangamia kwa gharika. kwa kupita, ipo sababu kubwa ya kisayansi ya kuamini kwamba mafuriko haya makubwa yalitokea kweli, mbali ya taarifa za wazi za maandiko ! Fahamu kuwa dunia (Yaani, hii sayari halisi) haikuharibiwa, wanadamu waovu waliosimamishwa juu yake tu."Wakafa wote wenye mwili waendao juu ya nchi" (Mwa. 7:21).Yesu (Math. 24:34) na Petro (2Petr.3:6 -12) Wote wawili waliielewa hukumu ya ulimwengu wa Nuhu una mfano mmoja na itakayotokea Kristo atakapokuja mara ya pili. Maovu

mengi mno ya mwanadamu katika kipindi cha Nuhu yanalingana na ya ulimwengu wa leo, ambao hu karibu kuadhibiwa Kristo atakaporudi.

Kwa sababu ya udhalimu wa dhambi ya mwanadamu na orodha ya mambo ya kuiharibu sayari hii yenyewe ambayo imeanza, imetokea imani, hata miongoni mwa wakristo, ya kuwa dunia hii itaangamizwa. Wazo hili ni wazi linaonyesha kutokufahamu kabisa ujumbe wa Msingi wa Biblia - wa kwamba Mungu ni mwenye uweza anayejihusisha na mambo ya sayari hii, Na ya kuwa mapema Yesu Kristo atarejea kuusimamisha ufalme wa Mungu hapa duniani.Ikiwa mwanadamu ameruhusiwa kuiharibu sayari hii basi ahadi hizi haziwezi kutungwa barabara. Ushahidi wa maana kuwa ufalme wa Mungu utakuwa duniani unapatikana katika somo la 4 -7 na somo la 5. Wakati ule ule ufuatao utakuwa ni uthibitisho wa kutosha kuwa dunia na utaratibu wa sayari hautaharibiwa: -

- “Kama dunia aliyoiweka imara milele” (Zab. 78:69);
- “Nayo dunia hudumu daima”
- “……jua na mwezi……nyota…..mbingu amevithibitisha hata milele na milele, ametoa amri wala haitapita” (Zab.148:3 -6).
- “Dunia itajawa na kumjua BWANA, kama vile maji yanavyoifunika bahari” (Isaya.11:9)
- (Hesabu 14:21) - Vigumu, ikiwa Mungu ataiacha dunia yenyewe iharibiwe. Ahadi hii bado kutimizwa.
- “BWANA aliyeziumba mbingu asema hivi; Yeye ni Mungu; ndiye aliyeiumba dunia na kuifanya; ndiye aliyeifanya imara, hakuiumba ukiwa; aliiumba ili ikaliwe na watu “ (Isaya 45:18). Ikiwa Mungu aliiumba dunia tu aione yaharibiwa, basi kazi yake ilikuwa haifai.

Bali nyuma kabisa katika Mwanzo Mungu aliyahahidi yote haya kwa Nuhu. kama alivyoanza kuishi tena katika ulimwengu ulioumbwa na gharika, labda Nuhu alihofu ya kuwa kutaweza kuwepo maangamizi mengine ya jumla. Popote ilipoanza kunyesha mvua baada ya gharika, Wazo hili lilibidi limjie akilini mwake. Na hivyo Mungu akafanya Agano (mfululizo wa Ahadi) kuwa jambo hili halitatokea kamwe mara ya pili:-

"Mimi, tazama, nalithibitisha Agano langu nanyi; …… na agano langu nitalithibitisha nanyi, wala kila chenye mwili hakitafutwa tena kwa maji ya gharika; …….(Ona mkazo wa "MIMI" - ajabu ya Mungu akichagua kufanya ahadi na mtu mfu !); Mwa.9: 9-12).

Agano hili lilithibitishwa na upinde wa mvua: -

"Hata itakuwa nikitanda mawingu (ya mvua) juu ya nchi, upinde utaonekana winguni: nami nitalikumbuka agano langu …… kati yangu nanyi ….. Agano la milele lililoko kati ya Mungu na kila kiumbe hai katika wote wenye mwili kilicho katika nchi ……Hii ndiyo ishara (Upinde wa mvua) ya agano" (Mwa 9:13 - 17).

Kwa sababu ni Agano la milele kati ya Mungu na watu na wanyama wa dunia, kinachofuata ni kwamba dunia ilipasa watu na wanyama waishi milele humu. Huu wenyewe ni uthibitisho kuwa ufalme wa Mungu utakuwa kwenye dunia hii kuliko kusema mbinguni. Ahadi hii kwa Nuhu ni msingi wa Injili ya ufalme ; inaonyesha jinsi macho ya Mungu yanalenga kwenye dunia hii , na jinsi alivyo na kusudi nayo. hata katika hasira anakumbuka rehema (Heb. 3:2), na huu ndio upendo wake ambao hata viumbe wanyama wake anawajali (1 Kor. 9:9; Yona 4:11).

### 3.4 Ahadi Kwa Abrahamu

Injili aliyoifundisha Yesu na Mitume kwa msingi haikuwa tofauti na alivyoielewa Abrahamu. Mungu, katika maandiko,"Alimhubiri Abrahamu Injili nzima" (Gal. 3:8) Ahadi hizi ni za maana sana hata Petro alizianza na kumaliza kutangaza hadharani habari njema akiwatajia hizo (mdo. 3:13,25). Kama tunaweza kuelewa alichofunza Abrahamu, ndipo tutakuwa na picha ya msingi kabisa ya Injili ya Kikristo. kuna ishara zingine ambazo zinaonyesha kuwa "Injili" sio jambo fulani ambalo lilianza barabara kwenye kipindi cha Yesu:-

"Tunawahubiri habari njema (Injili) ya ahadi ile waliyopewa mababa, ya kwamba Mungu amewatimizia watoto wetu ahadi hiyo" (Mdo. 13:32,33).

"Injili ya Mungu, ambayo Mungu amekwisha kuiahidi kwa kinywa cha manabii wake (Yaani,Abrahamu,Mwa.20:7) katika Maandiko matakatifu" (Rum. 1:1 -2).

"Maana kwa ajili hiyo hata hao waliokufa walihubiriwa Injili" (1Pet. 4:6) - yaani waamini ambao waliishi na kufa kabla ya karne ya kwanza.

"Maana ni kweli , sisi nasi tumehubiriwa Injili vile vile kama hao" (Ebra 4:2) - Yaani, Israel walipokuwa jangwani

Ahadi zilizofanywa kwa abrahamu zina mambo mawili ya msingi :

1. Mambo yanayohusu uzao wa Abrahamu (mtoto maalamu) na
2. Mambo yanayohusu nchi aliyoahidiwa Abrahamu.

Ahadi hizi zimefafanuliwa katika Agano Jipya, na, kuendelea na utaratibu wetu kuifanya Biblia ijieleze yenyewe , tutaunganisha mafunzo ya sehemu mbili za maagano ili tupate picha kamili aya Agano lililofanywa kwa Abrahamu.

Abrahamu awali aliishi Uri, mji wenye ustawi ambao sasa ni Iraki. Watafiti wa mabo ya kale wa siku hizi wanadhihirisha ustaarabu wa hali ya juu ambao ulifikiwa na wakati wa Abrahamu. ulikuwepo utaratibu wa mabenki, utumishi wa Serikali na utaratibu wa kutawala. Akijua hakuna tofauti, Abrahamu aliishia katika mji huu, kama tunavyomjua mtu wa ulimwengu. Lakini ndipo mwaliko wa Mungu ulio wa ajabu ukinijia -ayaache hayo maisha ya walimwengu na kuanza safari kuelekea nchi ya ahadi. Wapi kabisa na kwa ukamilifu haikufanywa dhahiri barabara. Akaambiwa yote, mwishowe ikawa ni safari ya maili 1,500.Nchi ilikuwa ni Kanani -Israeli ya sasa.

Mara kwa mara wakati wa uhai wake, Mungu alimtokea Abrahamu na akarudia na akapanua ahadi zake kwake. Hizi ahadi ndizo msingi wa Injili ya Kristo, basi kama tu wakristo wa kweli mwaliko huo huo unatujia kama ulivyofanywa kwa Abrahamu, ili kuyaacha mambo ya muda mfupi ya maisha haya, na kwenda mbele kwenye maisha ya Imani, Ahadi za Mungu zikichukuliwa kwa kuzithamini, kuishi kwa kufuata neno lake. tunaweza kuwaza vema ni jinsi gani Abrahamu alitafakari juu ya Ahadi alipokuwa anasafiri.”Kwa imani Abrahamu alipoitwa aliitika, atoke aende mahali atakapopapata kuwa urithi; alitii, akatoka asijue aendako” (Ebra. 11:8).

Tunapoona kwa mara ya kwanza ahadi za Mungu , Nasi vile vile tunaweza kujiona kwamba hatujui hasa ni nchi gani ya ahadi ya ufalme wa Mungu itakavyokuwa. Bali imani yetu katika neno la Mungu iwe hivi ila nasi pia tuwe ni wenye bidii kutii.

Abrahamu hakuwa mtu wa kuzunguka asiyetaka kukosa mahali bila jambo jema moyoni kama kutengemea kubahatisha hizi ahadi. Alitoka kwenye maisha ya ulimwengu ambayo, kwa maneno makubwa yana mambo mengi yaliyo na hali iliyo sawa na yetu wenyewe. Maamuzi yenye sehemu nyingi yanayoumiza aliyakabili yalikuwa na sura moja kwa hayo yaliyotupasa kuyakabiri tunapofikiri ikiwa tukubali na kutenda kazi ahadi za Mungu toka mojawapo ya watu wafanyao mambo mageni, kuangaliwa kwa mzaha katika jicho toka kwa majirani ("amepata dini") …. Mambo haya yalikwisha julikana kwa Abrahamu. azimio ambalo abrahamu alilihitaji hata kufika katikati nalo lote lilibidi kuwa kubwa mno. Jambo pekee lililotoa azimio hilo pote pote katika miaka ya safari yake ndefu lilikuwa ni neno la ahadi. Ilimbidi kujikumbusha maneno hayo na kila siku akayatafakari hasa yalikuwa na maana gani kwake.

Kwa kuonyesha imani kama hii na kuitenda kazi, tunaweza kuwa na heshima ijayo hiyo kama Abrahamu - kuitwa marafiki wa Mungu (Isaya 41:8), kupata maarifa ya Mungu (Mwa. 18:17) na kuwa na tumaini imara la uzima wa milele katika Ufalme. tena tunasisitiza ya kuwa Injili ya Kikristo msingi wake ni ahadi hizi kwa Abrahamu. Kuuamini kwa kweli ujumbe wa Kikiristo, nasi pia, yatupasa kwa uthabiti kujua ahadi zilizofanywa kwa Abrahamu. Bila hizo imani yetu sio imani. Kwa macho yenye bidii basi tusome na kusoma tena mazungumzo yaliyoandikwa baina ya Mungu na Abrahamu.

## NCHI

1) "Toka wewe katika nchi yako …… uende mpaka nchi ambayo nitakuonyesha" (Mwa. 12:1)

2) Abrahamu “akaendelea kusafiri ….. mpaka Betheli (ndani katikati ya Israeli).BWANA akamwambia Abrahamu ….. Inua sasa macho yako, ukatazame toka hapo ulipo, upande wa kaskazini na wa kusini na wa mashariki na wa magharibi, maana hii nchi yote uionayo, nitakupa wewe na uzao wako hata milele ….. katembee katika nchi hii katika mapana yake, na marefu yake, maana nitakupa wewe nchi hiyo” (Mwa. 13: 3, 15: 18).

3) “Siku ile BWANA akafanya agano na Abrahamu, akasema , uzao wako nimewapa nchi hii, kutoka mto wa Misri mpaka huu mto mkubwa, mto Frati” (Mwa 15:18).

4) “Nami nitakupa wewe na uzao wako baada yako nchi hii unayoikaa ugeni, nchi yote ya Kaanani, kuwa miliki ya milele” (Mwa 17:8).

5) “Ahadi ile ya kwamba (Abrahamu) atakuwa mrithi wa ulimwengu” (Rum. 4:13).

Hapa tunaona ufunuo wa kuendelea mbele kwa Abrahamu: -

1) “Ipo nchi ambayo ningependa hata uende huko”

2) “Sasa umefika katika eneo. Wewe na watoto wako mtaishi hapa milele” Elewa jinsi ya ahadi hii ya uzima wa milele ilivyoandikwa Pasi na uzuri wa kudanganya au mkazo; mwanadamu angeianzisha hapana shaka ingefanywa kuwa nyepesi.

3) Eneo la nchi ya ahadi lilifafanuliwa na kuwekwa wazi zaidi:

4) Abrahamu hakutarajia kupata ahadi katika maisha haya - alikuwa awe ni “mgeni” katika nchi, ingawa baadae ataishi milele

humo. kidokezo cha hii ni kuwa atakufa na kisha baadae kufufuliwa na kumwezesha kupata ahadi hii.

5) Paulo, akiongozwa na Roho kuandika, ni dhahiri aliona Ahadi kwa Abrahamu kuwa na maana ulimwengu wote ni urithi wake.

Maandiko yanaacha nia yake ili kutukumbusha ya kuwa Abrahamu hakupata kuona utimilifu wa ahadi katika zama za uhai wake:-

"Kwa imani alikaa ugenini katika ile nchi ya ahadi, kama nchi isiyo yake (Panadokeza namna ya maisha ya muda) akikaa katika hema" (Ebra. 11:9).

Aliishi kama mgeni katika nchi, labda pamoja na akili hiyo hiyo kutoonwa kwa kukosa usalama wa kutokutembea ambako mkimbizi anaona. alikuwa anaishi kwa shida na uzao wake katika nchi yake mwenyewe. Pamoja na watoto wake Isaka na Yakobo, (ambao ahadi zilirudiwa kwao), "alikufa katika imani" asijapata ahadi , lakini akiisha kuziona tokea mbali na kuzishangilia, na kukiri kwamba walikuwa wageni na wasafiri juu ya nchi" (Ebra. 11:13). ona hatua nne: -

- Akizijua ahadi - kama tunavyofanya katika somo hili
- Akiisha "Sadikishwa nazo" - kama zilichukua maendeleo ya ushawishi kwa Abrahamu, ni kiasi gani zaidi na sisi ?.
- Kuzikubali kwa moyo - kwa kubatizwa katika Kristo (Gal. 3:27 -29).
- Kukiri mbele ya ulimwengu kwa mwendo wetu wa maisha kuwa ulimwengu huu sio nyumbani kwetu hasa, bali tunaishi kwa kutumainia enzi ijayo duniani.

Abrahamu amekuwa shujaa wetu mkuu wa mfano kama tunafahamu mambo haya. mwisho wa kutambuliwa utimilifu wa ahadi ulikuja wakati wa baadae kwa mzee aliyechoka kwa mke aliyekufa; kwa kweli ilimbidi anunue kiwanja cha nchi ya ahadi kwa ajili ya kuzika (Mdo. 7:16). Hakika Mungu "hakumpa urithi ndani yake hata kiasi cha kuweka mguu: Lakini akaahidi kwamba atampa, iwe miliki yake, na ya uzao wake baadae alipokuwa hana mtoto" (mdo. 7:5). uzao wa Abrahamu uliopo sasa unaweza kuona kutopatana wanaponunua au kukodi miliki - duniani ambayo iliahidiwa kwao kuwa yao, urithi wa milele !.

Lakini Mungu anatunza ahadi zake. Itabidi ije siku hapo Abrahamu na wote ambao ahadi zilifanywa kwao watazawadiwa. Waebrania 11: 13, 39,40 neno limekazwa sana: -

"Hawa wote wakafa katika imani, wasijazipokea zile ahadi; Mungu alikuwa ametangulia kutuwekea sisi kitu kilicho bora, ili wao wasikamilishwe pasipo sisi".

Kwa hiyo Waaminifu wote watapewa thawabu kwenye kilele hicho hicho cha muda, yaani kwenye kiti cha hukumu siku ya mwisho (2 Tim. 4:1,8; math. 25:31 -34; 1 Petro 5:4). Kinachofuata ni yeye kuwako ili kuamuliwa, Abrahamu alikuwa na wengine waliozijua ahadi hizo itabidi wafufuliwe kabla ya hukumu. ikiwa sasa hawajazipokea ahadi ya kwamba watafanyiwa hivyo tu baada ya ufufuo wao na hukumu (yaani kuamuliwa na mwamuzi) Kristo atakaporudi, halipo shauri la pili bali kufahamu kuwa walio sawa na abrahamu kwa imani hivi sasa wamelala wakiwa hawana fahamu, wakisubiri Kristo arudi; Lakini vioo vilivyotiwa picha katika makanisa ya Ulaya yote imejulikana ya kuwa Abrahamu sasa yuko mbinguni, akipata thawabu kwa ajili ya maisha ya imani Maelfu ya watu kwa miaka mamia wameweka picha hizo za

zamani, kwa dini wakikubali mawazo kama haya. Je ? utakuwa na ujasiri wenye misingi katika Biblia kuondika haraka nje ya hiyo jamii ?

**Uzao (Mbegu)**

Kama tulivyoelezwa katika somo la 3:2, ahadi ya uzao kwanza wamhusu Yesu na, Pili, kwa wale walio katika "Kristo" na kwa sababu hiyo nao vile vile wanahesabiwa kuwa ni uzao wa Abrahamu:-

1) "Nitakufanya wewe kuwa taifa kubwa, na kukubariki ….. na katika wewe jamaa zote za dunia watabarikiwa" (Mwa. 12:23)

2) "Na uzao wako nitaufanya uwe kama mavumbi ya nchi: hata mtu akiweza kuyahesabu mavumbi ya nchi, Uzao wako nao utahesabika ….. Maana nchi hii yote uionayo, nitakupa wewe na uzao wako hata milele" (Mwa. 13:15,16).

3) "Tazama sasa mbinguni , hesabu nyota, kama ukiweza kuzihesabu …… Ndivyo utakavyokuwa uzao wako ….. Uzao wako nimewapa nchi hii (Mwa. 15:5,8)

4) "Nami nitakupa ……. na uzao wako baada yako …… nchi ya Kanaani, kuwa miliki ya milele; nami nitakuwa Mungu wao" (Mwa. 17:8)

5) "Na katika kuzidisha nitazidisha uzao wako kama nyota za mbinguni, na kama mchnga uliopo pwani; na uzao wako utamiliki mlango wa adui zao; na katika uzao wako mataifa yote ya dunia watajibarikia" (Mwa. 22:17,18).

Tena, Abrahamu kufahamu "uzao" kwa kuendelea mbele kulipanuka: -

1) Kwanza aliambiwa barabara ya kwamba kwa njia nyingine atakuwa na hesabu ya ajabu ya watoto, na kwa njia ya "uzao" wake dunia yote itabarikiwa.

2) Baadaye aliambiwa ya kwamba atakuwa na uzao ambao utakuja kujumuisha watu wengi. Watu hawa watapata uzima wa milele, pamoja naye, katika nchi ambayo aliwahi kuifika, yaani Kaanani.

3) Aliambiwa kuwa uzao wake utakuwa mwingi kama nyota za angani. Hii ahadi inaweza kuwa imedokezwa kwamba atakuwa na watoto wengi wa Kiroho (Nyota za mbinguni wengi sawa na wa mwili (kama "mavumbi ya nchi").

4) Ahadi zilizotangulia zilitia mkazo wa nyongeza ya uhakika kuwa watu wengi watakao kuja kuwa sehemu ya uzao watakuwa na uhusiano wao na Mungu.

5) Uzao utakuwa na ushindi juu ya adui yake.

Fahamu kuwa uzao utaleta "Baraka" zipatikane kwa watu walio juu ya uso wa dunia yote.Katika Biblia jambo la baraka mara nyingi limeungwa na kusamehewa dhambi. Isitoshe, huu ni mbaraka mkubwa zaidi wa kupenda Mungu unaoweza kuhitajika. Kwa hiyo tunasoma mabo kama "Heri (amebarikiwa) aliyesamehewa dhambi" (Zab. 32:1); "Kikombe kile cha baraka" (1Kor. 10:16), kinasema kikombe cha divai ambacho kinawakilisha damu ya Kristo kwa hicho msamaha unawezekana.

Mtoto pekee wa Abrahamu aliyeleta msamaha wa dhambi za ulimwengu, kwa kweli ni yesu, na ufafanuzi wa Agano Jipya juu ya Ahadi zilizofanywa kwa Abrahamu unatoa msaada madhubuti :
-

“(Mungu) hasemi, kwa wazao, kana kwamba ni wengi, (yaani kwa wingi), bali kana kwamba ni mmoja, (katika mmoja), kwa mzao wako” yaani, Kristo (Gal. 3:16)

“….ambayo Mungu aliagana na baba zetu, akimwambia Abrahamu katika uzao kabila zote za ulimwengu zitabarikiwa. Mungu akiisha kumfufua mtumishi wake Yesu, alimtuma kwenu ninyi kwanza, ili kuwabariki kwa kuwaepusha kila mmoja wenu na maovu yake” (Mdo. 3:25.26).

Ona hapa jinsi Petro anavyonukuu na kuifasiri Mwa. 22:18: -

**Uzao = Yesu**
**Baraka = Msamaha wa dhambi.**

Ahadi ya kuwa Yesu, uzao, atakuwa mshindi juu ya ahadi zake sasa inafaa zaidi kwa uzuri kuwa mahali ikiwa hii inasomwa kwa kutaja ushindi wake juu ya dhambi - Adui mkubwa zaidi wa watu wa Mungu, na kwa sababu hiyo naye Yesu, Pia.

**KUJIUNGA NA UZAO**

Kwa sasa itakuwa dhahiri kuwa mambo ya awali yaliyo ya msingi wa Injili ya Kristo ilieleweka kwa Abrahamu. lakini ahadi hizi muhimu zilikuwa kwa ajili ya Abrahamu na uzao wake, Yesu. Ni vipi ? kuhusu mtu yeyote mwingine ?. Hata walio wa ukoo wa mwili wa Abrahamu wao wenyewe kuwa hivyo hakuta mfanya mtu yeyote kuushiriki huo uzao mmoja maalum (Yoh. 8:39;Rum. 9:7). kwa njia nyingine yatupasa tuwe moyoni wa shirika wa Yesu, hivyo basi ahadi za mzao zitashirikishwa nasi vile vile. Hii ni kwa njia ya ubatizo katika Kristo (Rum. 6:3 -5); mara nyingi tunasoma ubatizo katika jina lake (Mdo. 2:38; 8:16; 10:48; 19:5). Wagalatia 3:27 -29 isingeweza kuweka maana yoyote iliyowazi:-

“Maana ninyi nyote (yaani mlio wengi tu) mliobatizwa katika Kristo mmemvaa Kristo. hapana Myahudi wala Myunani (wa mataifa), hapana mtumwa wala huru, hapana mume wala mke; maana ninyi nyote mmekuwa mmoja (kwa kuwa) katika Kristo Yesu kwa ubatizo. na kama ninyi ni wa Kristo (kwa nia ya ubatizo katika jina lake), basi, mmekuwa uzao wa Abrahamu, na warithi sawa sawa na Ahadi”.

Ahadi ya uzima wa milele duniani, kwa kupokea 'baraka’ ya msamaha kwa njia ya Yesu. Ni kwa kubatizwa katika Kristo, uzao, ambaye tunashirikishwa ahadi zilizofanywa kwake ; na hivyo Rum 8:17 inatuita sisi “Warithio pamoja na Kristo”.

Kumbuka kuwa baraka ilikuwa inakuja juu ya watu wote toka pande zote za dunia , kupitia kwenye uzao; na uzao utakuja kuwa ni kundi la watu walioenea duniani pote, kama mchanga ulio kwenye ukingo wa bahari na nyota za mbinguni. kinachofuata ni kwamba hiki kinatokana na kupokea kwao kwanza baraka hivyo wanaweza kuwa uzao. Kwa hiyo uzao mbegu (moja) “Zitasimulia habari za Bwana kwa kizazi kitakachokuja” (yaani watu wengi ; Zaburi 22:30). Tunaweza kueleza kwa ufupi kuachwa ahadi mbili zilizotolewa kwa Abrahamu : -

**1) NCHI**

Abrahamu na uzao wake, Yesu, na wale walio ndani yake watairithi nchi ya Kaanani na kupanuka dunia yote, na kuishi humo milele. katika maisha haya hii ahadi hawakuipata, bali watapokea siku ya mwisho, Yesu atakaporudi.

**2) UZAO**

Kwanza kabisa huyu alikuwa ni Yesu. kwa njia yake dhambi ("Maadui") za watu ushindi utapatikana, hivyo basi mibaraka ya msamaha itafanywa ipatikane ulimwenguni pote.

Kwa kubatizwa katika jina la Yesu tunakuwa sehemu ya uzao. Izi hizi njia mbili zinatokea katika mahubiri ya Agano Jipya, na sio ya kushangaza ni mara nyingi yameandikwa ya kwamba watu waliposikia wakiishafundishwa, wakati huo wakabatizwa. huu ulikuwa, na ndivyo ulivyo, mwendo ambao hizi ahadi zinaweza kufanywa kwetu. Tunaweza kuelewa ni kwa sababu gani, Mzee alipokabili kifo, Paulo aliweza kuainisha tumaini lake kuwa ni "tumaini la Israeli' (mdo. 28:20): tumaini la kweli la mkristo ni tumaini la kwanza la Myahudi. Ufafanuzi wa Kristo ni kuwa "Wokovu watoka kwa wayahudi" (Yoh. 4:22) pia inabidi kutaja haja ya kuwa Myahudi wa Kiroho, hivyo basi tunaweza kufaidika kutoka kwenye ahadi za wokovu kwa njia ya Kristo ambazo ziliahidiwa kwa mababa wa Wayahudi.

***Tunasoma ya kwamba Wakristo wa kwanza Walihubiri :-***

1) "Mambo yanayohusu ufalme wa Mungu na
2) Jina la Yesu Kristo" (Mdo.8:12).

Haya yalikuwa ndiyo mambo mawili hasa aliyoelezwa Abrahamu mwanzoni mwa vichwa vidogo tofauti vya habari:-

1) Ahadi zinazohusu nchi na
2) Ahadi kuhusu uzao.

Angalia unapopita neno "Mambo" (yapo katika uwingi) yanayohusu Ufalme wa Yesu. yameelezewa kwa kifupi kuwa "akawahubiri Kristo" (Mdo. 8:5,12). yote hii mara nyingi

imechukuliwa kuwa na maana "Yesu anakupenda ! sema bara bara unaamini alikufa kwa ajili yako nawe ni mtu uliyeokolewa !" Lakini fungu la maneno machache "Kristo" ni dhahiri linaelezea kwa ufupi mafunzo ya hesabu ya mambo kumhusu yeye na ufalme ujao. Habari njema kuhusu ufalme huu ambazo zilihubiriwa kwa Abrahamu zilihusika sehemu kubwa katika mahubiri ya kwanza ya Injili .

Katika mji wa Korintho, Paulo, "Kwa muda wa miezi mitatu, akihojiana na watu na kuwavuta katika mambo ya ufalme wa Mungu" (Mdo. 19:8); Katika efeso alikwenda huko na huko "Akihubiri ufalme wa Mungu" (Mdo. 20:25), na kazi yake kabla ya kufa kule Rumi ilikuwa ni ile ile "Akawaeleza kwa taratibu na kuushuhudia ufalme wa Mungu, akiwaonya mambo yake Yesu, kwa maneno ya sheria ya Musa na ya manabii" (mdo. 28: 23, 31). kama kuwepo mazungumuzo mengi mno ya karibu yanayoonyeshwa ya kwamba ujumbe wa msingi wa Injili kuhusu ufalme wa Yesu hayakuwa tu ni mambo ya kusema "Mwamini Yesu" ufunuo wa Mungu kwa Abrahamu ulieleza jambo moja moja zaidi kuliko hivyo, na mambo yaliyoahidiwa ndio msingi wa Injili ya mkristo wa kweli.

Tumeonyesha ya kuwa kubatizwa katika Jina la Yesu kunatufanya kuwa sehemu ya uzao na kwa sababu hii tunaweza kurithi ahadi (Gala. 3:27 -29), lakini ubatizo pekee hautoshi kutuwezesha kupata wokovu ulioahidiwa. yatupasa kubakia ndani ya uzao , katika Kristo, ikiwa tunataka kupokea ahadi zilizofanywa kwa uzao. Kwa hiyo ubatizo ni mwanzo unaostahili; tumeingia kwenye mbio ambazo zinahitajika wakati huo kukimbia. usisahau kwamba kuhusiana na uzao wa Abrahamu hauna maana kwamba tunakubalika mbele za Mungu. Waisraeli ni uzao wa Abrahamu kwa namna nyingine, Lakini hii haina maana kwamba

wanaweza kuokolewa bila kubatizwa na kufuatisha maisha yao kwa Kristo na mfano wa Abrahamu; (Rum. 9: 7, 8; 4: 13,14). Yesu aliwaambia Wayahudi, "najua ya kuwa ninyi ni uzao wa Abrahamu ; Lakini mnatafuta kuniua ….. kama mngekuwa watoto wa Abrahamu, mngezitenda kazi zake Abrahamu" (Yohana. 8:37,39), ambaye aliishi maisha ya kumwamini Mungu na Kristo, Uzao ulioahidiwa (Yoh. 6:29).

"Uzao" inabidi uwe na sifa za babu yake ikiwa tunataka kuwa uzao wa Abrahamu wa kweli basi yatupasa sio tubatizwe tu bali tuwe na imani hasa katika ahadi za Mungu, kama aliyokuwa nayo barabara kwa hiyo ameitwa "baba yao wote wanaoamini ….. ambao wanafuata vile vile nyanyo za imani hiyo ya baba yetu Abrahamu, aliyokuwa nayo" (Rum. 4:11,12) " Fahamuni basi, wale walio wa imani, hao ndio wana wa Abrahamu" (Gal 3:7).

Imani ya kweli inabidi ijionyeshe yenyewe kwa aina nyingine ya matendo kama sivyo, mbele za Mungu, sio Imani (Yakobo.2:17). Tumeonyesha wazi imani yetu katika ahadi hizi ya kuwa tumejifunza na kubatizwa kwanza, hivyo zinatuhusu sisi wenyewe (Gal 3:27 -29).Basi, unaziamini kweli ahadi za Mungu ?. Hili ni swali yatupasa hasa tujiulize katika maisha yetu yote.

## AGANO LA KALE NA JIPYA

Itakuwa ni dhahiri kwa sasa kuwa ahadi kwa Abrahamu zinaeleza kwa ufupi Injili ya Kristo. Mkondo mwingine wa mkuu wa ahadi alizoahidi Mungu ulikuwa kwa Wayahudi katika maneno ya sheria ya Musa hizi alisema kuwa kama walikuwa watii kwenye sheria hii, basi wangebarikiwa katika maisha haya (Kum. 28). Haikuwepo moja kwa moja ahadi ya uzima wa milele katika huu mfululizo wa ahadi, au "agano". Hivyo tunaona kuwa kumekuwepo "Maagano" mawili yaliyofanywa:-

1) Kwa Abrahamu na uzao wake , umeahidiwa msamaha na uzima wa milele katika ufalme wa Mungu Kristo ajapo. Ahadi hii pia iliahidiwa katika Edeni na kwa Daudi.

2) Kwa Wayahudi kwenye kipindi cha Musa, wao waliahidiwa amani na furaha katika maisha haya ya sasa kama wangetii sheria ambazo Mungu alimpa Musa.

Mungu alimwahidi Abrahamu msamaha na uzima wa milele katika ufalme, lakini huu utawezekana tu kwa dhabihu ya Yesu. Kwa sababu hii tunsoma kuwa kifo cha Kristo msalabani kilithibitisha alichoahidiwa Abrahamu (Gal. 3:17; Rum 15:8; Dan. 9:27; 2Kor.1:20), hivyo damu yake imeitwa "Damu ya Agano Jipya" (Math. 26:28) Tulikumbuke hili kama Yesu alivyotuambia mara kwa mara tutwae kikombe cha divai, akiashiria mambo yake kutukumbusha mambo haya (Ona 1Kor. 11:25): "Kikombe hiki ni patano (Agano) Jipya katika damu yangu" (Luka. 22:20). Hakuna maana katika "kuumega mkate" kumkumbuka Yesu na kazi yake ila tukifahamu mambo haya.

Dhabihu ya Yesu imefanya msamaha wa dhambi na uzima wa milele katika Ufalme wa Mungu uwezekane. basi akafanya ahadi imara kwa Abrahamu; Yesu amekuwa mdhamini wa Agano lililo bora zaidi (Ebra. 7:22). Waebrania 10:9 yamsema Yesu "Aondoa la kwanza (Agano), ili kusudi alisimamishe la pili" hii inaonyesha ya kwamba Yesu alipothibitisha ahadi zilizofanywa kwa Abrahamu, aliliondoa Agano lingine, hilo lilikuwa ni agano lililotolewa kwa mkono wa Musa. mistari ambayo imenukuliwa kumhusu Yesu inaimarisha Agano Jipya kwa kufa kwake, inadokeza ya kuwa lilikuwepo agano la kale aliloondoa (Webra. 8:13).

Hii ina maana ya kwamba ingawa agano la kuhusu Kristo lilifanywa kwanza, halikuanza kutumika kamili mpaka alipokufa, kwa sababu hii limeitwa Agano "Jipya". Lengo la Agano la "Kale" lililofanyika na Musa lilikuwa likionyesha mbele kwenye kazi ya Yesu , na kuupa mkazo umuhimu wa kuamini ahadi kuhusu Kristo

(Gal. 3:19,21). Kwa kinyume, kumwamini Kristo kunathibitisha ukweli wa sheria aliyopewa Musa (Rum.3:31). Ya kupendeza kwa kuwa ya zamani, Paulo anaielezea kwa maneno machache: "Torati imekuwa (Mwalimu) kiongozi kutuleta kwa Kristo, ili tuhesabiwe haki kwa imani" (Gal. 3:24). Ni kusudi hili hata torati iliyokuja kwa mkono wa Musa imehifadhiwa, na bado inatusaidia kujifundisha.

Kwanza unaposema mambo haya sio mepesi kuyaelewa; tunaweza kueleza kwa maneno machache kama ifuatavyo: -

Ahadi za kumhusu kristo zilifanywa kwa Abrahamu - Agano Jipya.

Ahadi kwa Israeli zilijumuisha torati aliyopewa Musa - Agano la Kale.

Kifo cha Kristo. Agano la Kale likaisha (Kol. 2:14 -17) Agano Jipya likaanza kutumika.

Ni kwa sababu hii mambo kama kutoa fungu la kumi,kutonza sabato n.k, ambayo yalikuwa ya Agano la Kale , siyo ya lazima siku hizi - ona somo la 9.5. Agano Jipya litakujafanywa kwa Waisraeli wa kuzaliwa watakapotubu na kumkubali Kristo. (Yer. 31:31,32 ; Rum. 9:26,27; Ezek. 16:62; 37:26), Ingawa, kwa kweli Myahudi yeyote afanyaye hivyo na kubatizwa katika jina la Yesu, anaweza kwa mara moja kuingia kwa Agano Jipya (ambalo halimtofautishi Myahudi /mtu wa mataifa -Gal 3: 27 -29).

Hakika kufahamu mambo haya kunatufanya tutambue ukweli wa ahadi za Mungu. Wenye mashaka juu ya mafundisho ya dini walilaumu isivyo haki wahubiri wa Kristo wa kwanza kwa kutotoa ujumbe wa kweli. Paulo alijibu kwa kusema kwamba kufa kwake Kristo ni uthibitisho wa ahadi za Mungu, tumaini walilosema halikuwa jambo la kugusa na kisha kwenda, bali lilikuwa ni toleo la uhakika kabisa: - “Lakini kama Mungu alivyomwaminifu, neno letu (la kuhubiri) kwenu halikuwa ndiyo na siyo. Maana mwana wa Mungu, Kristo Yesu, aliyehubiriwa katikati yenu na sisi, ….. hakuwa ndiyo na siyo, bali katika yeye ni ndiyo. Maana ahadi zote za Mungu zilizopo katika yeye ni ndiyo, tena katika yeye ni, Amini” (2 Kor.1:17 -20). Kwa kweli huu mwenendo haufanyi kazi wa,'Vyema’, nadhani kunaweza kuwa na ukweli fulani katika hayo yote …….” ?.

## 3.5 Ahadi Kwa Daudi

Daudi, kama Abrahamu na wengine wengi wapokeaji wa ahadi za Mungu, hawakuwa na maisha rahisi. Alikuwa ni kijana mdogo wa mwisho katika jamaa kubwa ambaye, katika Israeli 1000 K.K., ilimaanisha kuchunga kondoo na kukimbia safari fupi za kupeleka ujumbe au kitu kwa ndugu zake wakubwa wapendao kidogo kuwa na mamlaka (1 Samweli sura ya 15 hadi 17). Katika kipindi hiki alijifunza kufika kumwamini Mungu ambaye watu wachache tangu wakati ule walimkaribia.

Siku ikafika hapo Israeli walipokabiliwa na shindano la mwisho toka kwa majirani zao wenye kuanzisha ugonvi , Wafilisti; walitakiwa wapeleke mmoja k ati yao apigane na jitu kubwa - Goliati ; Mfilisti aliyekuwa wa kwanza kujitokeza akifahamu

kuwa yeyote atakayeshinda atamiliki juu ya upande unopoteza pigano. Kwa msaada wa Mungu Daudi akamshinda Goliati kwa kutumia kombeo, lililompatia umaarufu mkubwa kuliko mfalme wao (Sauli). “Wivu ni mkali kama ahera (Kaburi)” (Wimbo ulio bora 8:6). maneno yaliyothibitisha kuwa kweli kwa mateso aliyopata Daudi toka kwa Sauli kwa miaka 20 iliyofuata akimwinda kama panya huko na huko jangwani kusini mwa Israeli.

Hatimae Daudi akawa mfalme, na kuonyesha shukrani zake kwa upendo wa Mungu wake katika maisha yake nyikani, akaazimia kujenga hekalu la Mungu. Jibu toka kwa Mungu likawa mwanae Daudi, Suleimani akawa ndiye atakayejenga hekalu na ya kuwa Mungu alitaka kumjengea nyumba Daudi (2 Sam. 7:4 -13). Ndipo yakafuata maelezo ya ahadi yanayorudia na mambo mengi aliyoambiwa Abrahamu, ambapo pia yalijaa katika maelezo mengine:-

“Nawe siku zako zitakapotimia, ukalala na baba zako, nitainua mzao nyuma yako, atakayetoka viunoni mwako, naye atakuwa mwanangu. Akitenda

maovu, nitamwadhibu kwa fimbo ya binadamu na kwa mapigo ya mwanadamu, lakini fadhili zangu hazitamwondoka, kama vile nilivyomwaondolea Sauli, niliyemwandoa mbele yako. Na nyumba yako, na ufalme wako,vitadhibitishwa milele mbele yako: nacho kiti chako kitafanywa imara milele” (mstari wa 12 - 16).

Toka masomo yetu yaliyotangulia tulitazama “Mzao” kuwa ni Yesu. Maelezo yake kuwa ni mwana wa Mungu (2 Samweli 7:4) yanathibitisha hivi, kama yafanyavyo mengine yanayomtaja katika sehemu zingine za Biblia :-

"Mimi ….. shina la mzao wa Daudi", Yesu alisema (Uf. 22:16).

"(Yesu), aliyezaliwa katika ukoo wa Daudi kwa jinsi ya mwili" (Rum. 1:3)

"Katika uzao wake mtu huyo (Daudi) Mungu amewaletea Israeli Mwokozi, yaana Yesu, kama alivyoahidi" (Mdo. 13:23).

"Malaika alimwambia Bikra Mariamu kuhusu mwanae Yesu: "Bwana Mungu atampa kiti cha enzi cha Daudi Baba yake (babu) yake …… ufalme wake hautakuwa na mwisho"(Luka. 1:32,33) Hii ni ahadi inayotumika kwa mzao wa Daudi, katika 2 Sam.7:13, kwa Yesu.

Pamoja na uthabiti wa mzao amejulikana kuwa ni Yesu, idadi ya maelezo sasa yamekuwa ni yenye
maana : -

**1) MZAO.**

"Mzao wako …… atakayetoka viunoni mwako …… nitakuwa Baba yake, naye atakuwa mwanangu" " ……Wazao wa mwili wako nitawaweka katika kiti chako cha enzi" (2 Sam 7:12,14 ; Zab. 132: 10,11). Yesu, mzao, hasa alitoka kwa jinsi ya mwili kwa watoto wa Daudi, bali Mungu akiwa ni Baba yake. Jambo hili linawezekana tu kwa kuzaliwa na Bikira kama alivyoelezwa katika Agano Jipya; Mama yake Yesu alikuwa Mariamu, aliyetoka katika ukoo wa Daudi (Luka.1:32), lakini hakuwa na Baba mwanadamu. Mungu alifanya muujiza katika tumbo la Mariamu kwa njia ya Roho Mtakatifu ili kumzaa Yesu, basi Malaika alitoa ufafanuzi "Kwa sababu hiyo hicho kitakachozaliwa kitaitwa kitakatifu, Mwana wa Mungu' (Luk. 1:35). "Kuzaliwa na

Bikira" ilikuwa ndiyo njia pekee ya Ahadi hii aliyoahidiwa Daudi kuweza kutimia vema.

**2) NYUMBA.**

"Yeye ndiye atakayejenga nyumba kwa jina langu" (2 Sam. 7:13) inaonyesha kuwa Yesu atajenga Hekalu la Mungu - mwili halisi na la Kiroho. Ezekieli 40 -48 ni sura zinazoeleza jinsi Milenia (Miaka 1000 ya kwanza ya ufalme wa Mungu baada ya Yesu kurudi Duniani) hekalu litajengwa Yerusalemu. 'Nyumba' ya Mungu ni mahali anapopenda kuishi, na Isaya 66: 1,2 tunaambiwa kuwa alikuja kuishi katika mioyo ya watu walio wanyenyekevu wa neno lake. Basi Yesu anajenga Hekalu la kiroho ili Mungu akae ndani, linaloundwa na waamini wa kweli. Maelezo yanamsema Yesu kuwa jiwe la msingi wa hekalu la Mungu ( 1 Pet. 2:4 -8) na wakristo ni mawe ya hekalu (1 Pet. 2:5) yanayopangwa sasa katika nafasi.

**3) KITI CHA ENZI**

"Nacho kiti cha enzi cha ufalme wake (Kristo) nitakifanya imara milele ….. nyumba yako (Daudi) na ufalme wako ….. kiti chako kitafanywa imara milele (2 Sam.7: 13,16 ; Isaya 9: 6,7)". Basi ufalme wa Kristo utakuwa juu ya ufalme wa Daudi wa Israeli; ina maana kwamba ufalme wa Mungu unaokuja utaanzisha tena ufalme wa Israeli - ona somo la 5.3 zaidi kuhusu huu. kwa kutimiza ahadi hii, Kristo itambidi atawale "kiti cha enzi" cha Paulo, au mahali pa utawala. huu utawala wenyewe ulikuwa Yerusalemu. Huu ni ushahidi mwingine wa kuwa ufalme itabidi uanzishwe hapa duniani ili kutimiza ahadi hizi.

**4) UFALME**

“Nyumba yako na ufalme wako vitathibitishwa imara milele mbele yako” (2 Sam.7:16 mstari unadokeza ya kuwa Daudi atashuhudia kuanzishwa kwa ufalme wa milele wa Kristo. kwa hiyo ahadi hii haikuwa ya moja kwa moja, hata atakapofufuliwa Kristo atakaporudi ndipo ataweza kuona kwa macho yake mwenyewe ufalme ukisimamishwa ulimwenguni pote, na Yesu akiwa anatawala tokea Yerusalemu.

Mambo haya aliyoahidiwa Daudi ni ya muhimu kabisa kufahamu. kwa furaha Daudi aliyasema mambo haya kuwa ni “Agano la milele …..maana ni wokovu wangu wote, na shauku yangu yote” (2 Sam. 23:5). mambo haya yanataja wokovu wetu pia; Kuyafurahia kuwa shauku yetu yote. Hivyo tena maana imeyafanya haya mafunzo kuwa muhimu. Ni jambo liletalo huzuni kama Wakristo kufunza mafundisho yanayopingana kabisa na ukweli huu wa ajabu :-

- Ikiwa Yesu mwenyewe “aliwahi kuwepo kabla” yaani alikuwepo kabla ya kuzaliwa, basi hizi ahadi hazina maana hata Yesu awe “Mzao” wa Daudi, au kuwa mtoto.

- Ikiwa Ufalme utakuwa mbinguni , basi Yesu hawezi tena kuanzisha ufalme wa Daudi wa Israeli, wala kuweza kutawala toka kwenye 'Kiti cha enzi’ cha daudi au mahali pa utawala. Mambo haya hasa yenyewe yalikuwa Duniani, na hivyo tena kuyaanzisha tena inabidi iwe ni mahali pale pale.

**YALITIMIA KWA SULEMANI ?**

Mwana halisi wa Daudi, Suleimani, alitimiza sehemu ya ahadi alizoahidiwa Daudi. Akajenga hekalu halisi la Mungu (1 Fal. 5 -8), akawa na ufalme uliostawi sana. Mataifa toka pande zote yalituma wawakilishi wa kutoa heshima kwa Sulemani

(1 Fal. 10), na kukawa na baraka kubwa za kiroho kutokana na kutumia hekalu. kwa hiyo utawala wa Sulemani ulilenga kwa kuonyesha mbele kwenye utimilifu mkubwa zaidi wa ahadi alizoahidiwa Daudi utakaoonekana katika ufalme wa Kristo.

Wengine wamedai kwamba ahadi kwa Daudi zilitimia kabisa kwa Sulemani, lakini hii inakanushwa na yafuatayo: -

- Ushahidi mwingi wa Agano Jipya unaonyesha kuwa 'Mzao' ni Kristo, siyo Sulemani.

- Daudi anaonekana akiunga ahadi alizo ahidiwa na zile zilizofanywa kwa Abrahamu. (1 Nyakati.17:27 Mwa. 22:17,18:).

- Ufalme wa'Mzao' hautakuwa na mwisho - wa Sulemani ulikuwa na mwisho.

- Daudi alitambua kuwa ahadi zilikuwa zinahusu uzima wa milele, ambapo zinapinga kabisa kutaja yeyote wa jamaa yake ya karibu: "sivyo ilivyo nyumba yangu mbele za BWANA; lakini amefanya nami Agano la milele" (2 Sam. 23:5).

- Mzao wa Daudi ni masihi, Mwokozi wa watu toka dhambi

(Isaya 9:6,7; 22:22; Yer. 33:5,6,15; Yoh. 7:42). bali Sulemani alimwacha Mungu baadaye (1 Fal. 11: 1 -3' Neh. 13:26) kwa sababu ya kuoana na walio nje ya tumaini la Israeli.

***Tumeacha kitambo sehemu ya 9: Kuharibiwa kwa Mbingu na Nchi (Ufu. 21:1; 2Pet. 3: 6 -12).***

Lengo la Mungu likiwa ni kusimamisha ufalme wake hapa duniani (Ona somo la 5), haidhaniwi kuwa ataiharibu hii sayari yenyewe, na somo la 3.3 limeonyesha ya kuwa kwa uthabiti amehahidi kutofanya jambo hili. Mstari uliopo hapo juu kuangamiza mbingu na nchi inabidi uchukuliwe kwa mfano.

Fungu la maneno kutoka Petro laonyesha mfano mmoja kati ya hukumu iliyopita duniani wakati wa Nuhu na itakavyotokea kwenye “Siku ya Bwana” wakati ujao. “Dunia ile ilivyokuwepo wakati ule, iligharikishwa na maji, ikaangamia, Bali mbingu na nchi, zilizopo sasa …… zimewekwa akiba kwa moto zikilindwa hata siku ya hukumu” (2 Pet. 3:6,7).

Petro anaonyesha tofauti kati ya maji yakiwa ni wakala wa kuangamiza kwenye kipindi cha Nuhu, na moto utakaotumika atakapokuja mara ya pili.'Mbingu na nchi’ za kipindi cha Nuhu zenyewe hazikuharibiwa - wenye miili wote’ wenye dhambi waliharibiwa (Mwa. 7:21; 6: 5, 12).'Mbingu na nchi’ kwa sababu hii unatajwa utaratibu wa mambo au muungano wa watu. Wale wasiofahamu hili fungu la maneno wanaelekea kusahau kuharibiwa kwa 'Mbingu’ zinazosemwa karibu. hii haiwezi kuchukuliwa ilivyo - ni mahali ambapo ni makao ya Mungu (Zab. 123: 1), mahali ambapo hakuna wenye dhambi (Hab. 1: 13; Zab. 65: 4, 5), ni ambazo hutangaza utukufu wa Mungu (Zab. 19:1).Kama zinataja jambo lingine katika mfano, basi inabidi nayo 'nchi’.

Mafungu yafuatayo ya maneno yanaonyesha jinsi'Mbingu na nchi’ katika sehemu zingine za Biblia hazitafsiriwi jinsi zilivyo, bali zinataja kidogo mfumo wa mambo ya dunia.

• “Naliangalia nchi, na tazama ilikuwa ukiwa, haina watu; naliziangalia mbingu, nazo hazina nuru ….. maana BWANA asema hivi, Nchi yote (ya Israeli) itakuwa ukiwa …… Kwa ajili ya hayo nchi itaomboleza na mbingu zitakuwa nyeusi” (Yer. 4:23 - 28). Hizi ni hukumu kuja juu ya 'Mbingu na nchi’ za watu wa Israeli ambazo (si mbingu na dunia halisi) zitaomboleza.

• Hapo kwanza Musa aliwatangazia Waisraeli wote “Sikilizeni, enyi mbingu, nami nitanena; na nchi isikie maneno ya kinywa changu” (Kum. 32:1). mkazo umetiwa wa kuwa palikuwepo aina mbili za watu ambao alizungumza nao:

1) “Wazee wote wa kabila zenu”na
2) “Kusanyiko lote la wana wa Israelli” (Kum. 31: 28,30).Wakati ule wazee walilinganishwa na 'Mbingu’ na watu wa kawaida na 'Nchi’.

• Isaya alianza unabii wake kwa jinsi hii: “Sikieni, enyi mbingu, tega sikio Ee nchi ……. Lisikieni neno la BWANA, enyi waamuzi ……tegeni masikio msikie sheria ya Mungu wetu” (Isa. 1: 2,10). Tena ipo mistari sambamba kati ya mbingu na viongozi; na kati ya nchi na watu.

• Ataziita mbingu zilizo juu, na nchi pia awahukumu watu wake” Israeli (Zab. 50:4) huu wajisema wenyewe.

• “Nami nitatikisa mataifa yote … nitazitikisa mbingu na dunia” (Hagai 2:7,21) vile vile.

• “Maana upanga wangu umekunywa na kushiba mbinguni: tazama utashukia Edomu, … upanga wa BWANA umeshiba damu … maana BWANA …. machinjo makubwa katika nchi ya Edomu”

(Isa. 34:5,6) hapa'Mbingu' zimelinganishwa na Edomu; Unabii uliotangulia kama jeshi lote la mbingu litafumliwa' (Isa. 34:4) kwa hiyo inatajwa Edomu kufumuliwa.

- Mbingu na nchi zilizotajwa zikifumuliwa au kunyauka katika Isaya 13 wanatajwa watu wa Babeli. katika mfululizo wa taarifa kuhusu Babeli tunasoma ya kuwa Mungu'atazitetemesha mbingu, na dunia itatikiswa itoke katika mahali pake ….. itakuwa kama vile paa aliyetikiswa ….. kila mtu atageukia watu wake, nao watakimbia, kila mtu aende nchi yake mwenyewe" (Isa. 13:13,14). Kuondoka kwa mbingu na nchi kumewekwa sawa na huko kwa watu, Ebra. 9:26 yasema "Mwisho wa dunia" ukiwa unatokea katika karne ya kwanza B.K - katika maana ya kuwa ulimwengu wa Wayahudi ulikuwa unaisha wakati ule.Katika fikira yote haya yakishikwa kwa uthabiti, itegemewe kuwa mistari ya agano Jipya inayotaja mbingu mpya na nchi atakaporudi Kristo itataja utaratibu mpya wa mambo utakaoonekana hapo ufalme wa Mungu ukisimamishwa.

Uchunguzi wa karibu kwa 2 Pet. 3 unathibitisha hivi. tukiisha eleza namna'mbingu na nchi' za sasa zitakavyoisha, mstari wa 13 unaendelea: "Lakini kama ilivyo ahadi yake, mnatazamia mbingu mpya na nchi mpya, ambayo haki yakaa ndani yake" Huku ni kunukuu ahadi ya Mungu iliyo katika Isaya 65:17: "Maana tazama, mimi naumba mbingu mpya na nchi mpya". Mistari inayoendelea katika Isaya 65 yaeleza utaratibu huu mpya kuwa ni hali timilifu hapa duniani:

"Tazama, naumba Yerusalemu iwe shangwe.. Hawatajenga, akakaa mtu mwingine …..mtoto atakufa mwenye umri wa miaka mia (yaani, maisha ya kuishi yatarefushwa) …. Mbwa mwitu na mwanakondoo watalisha pamoja" (Isaya 65: 18 -25).

Baraka zote hizi ni dhahiri zinahusu jambo la ufalme ujao wa Mungu duniani -'Mbingu na nchi mpya zitakazo ingia mahali pa hizi zilizopo zilizosimama kwa huzuni.

***Tumeacha kitambo sehemu ya 10: Madai ya'Uisraeli wa Visiwa vya Uingereza'***

Wazo limetangulizwa mbele na mtu kama H.W. Armstrong katika 'Ukweli dhahiri' wa muungano wa ahadi alizoahidiwa Abrahamu zimetimilika kwa Waingereza na watu wa Amerika, ambao, imedaiwa ni wa kabila la Efraimu na Manase. Washirika wa Uisraeli wa Uingereza wanaamini kwamba Wafalme na malkia wa Uingereza wametokea kwa Wayahudi walianza na mfalme Daudi ili kuhakikisha nadharia zao wameweza kusema kwamba Wayahudi wamekataliwa kuwa watu wa Mugnu na watu wa Uingereza wamechaguliwa badala yao.

Ikiwa tafakari ya somo la 3 limefuatwa, itakuwa dhahiri uwa kwa Biblia madai haya hayana ukweli wowote, yafuatayo ni machache kati ya alama nyingi zanyongeza zinazoweza kufanywa: -

• Watu wote sawa sawa wapo chini ya laana ya dhambi (Rum.3: 23), na kwa hiyo kristo alikufa ili kuwezesha watu watokao mataifa yote wawe na nafsi ya wokovu. malezi ya taifa lolote tutokako siyo ya muhimu kama tumebatizwa katika Kristo na kuwa sehemu ya Israeli kiroho (Gal. 3:27 -29). tumeamriwa kuhubiri Injili kwa mataifa yote. na kubatiza aaminiye (Marko. 16:15,16); hivyo Israeli mpya inakuwa na watu watokao mataifa yote, siyo Uingereza tu.

• Ni shida kuthibitisha asili ya watu wa Uingereza na Amerika; wao ni watu mchanganyiko toka sehemu nyingi za ulimwengu. kwa sababu tu mtu kazaliwa kwenye nchi hizo hakuna maana ya kuwa wao ni watu walio teuliwa na Mungu.

• Uisraeli wa Uingereza unadaiwa kwamba baraka alizoahidiwa uzao wa Abrahamu zimetimizwa kwa watu wa Uingereza, bila kujali utii wao kwa Mungu. Hili ni jambo linalopingana na baraka za Mungu ni katika hali ya utii. sura zote za Law. 26 na Kum. 28 zaeleza baraka zitakazokuja juu ya Israeli kama wangetii neno lake, na laana itakayokuja kama hawatii. kudai kuwa Mungu ameipa Uingereza baraka hizi bila kujali utii wao kwa neno lake , na mara nyingi mbele yao huwa wepesi kuliasi, kwa kweli ni kufanya jeuri kwenye maneno ambayo Mungu anatoa baraka hizi.

• Kidokezo cha kuwa Mungu amewatupilia mbali watu wake wa Israeli na badala yao amewaweka Waingereza kinaruka kwenye uso wa fungu la maneno kama Rum. 11: 1, 2: “Je ! Mungu amewasukumia mbali watu wake ? hasha !. Kwa kuwa mimi (Paulo) ni Mwisraeli, mmoja wa wazo wa Abrahamu, ….. Mungu hakuwa sukumia mbali watu wake aliowajua”.

• Ufalme wa Mungu ulikuwa ni ufalme wa Israeli zamani (2 Nyak.9:8). ulipinduliwa kwa kutotii, Lakini ufalme utarudishwa tena (Ezek. 21: 25 -27).Ufalme utarudi Yerusalemu (Mika. 4:8) Yesu atakapo tawala juu ya kiti cha Enzi cha Daudi (Luka. 1:32). Watu wa Israeli wa sasa ambao wametawanyika watakusanywa tena toka sehemu mbali mbali za dunia walikotawanyika: “Nitawatwaa wana wa Israeli toka kati ya mataifa walikokwenda na kuwaleta kwenye nchi yao wenyewe. nitawafanya kuwa taifa moja katika nchi yao, juu ya milima ya Israeli” (Ezek. 37: 21,22). Unabii huu umetimia kwa namna Wayahudi asili walivyorudi

nchini kwao; utimilifu kamili utakuwa katika ufalme, kurudi kwa Israeli waliopo kwenye nchi yao kunaonyesha itabidi kuja mapema huu ufalme.

Maelezo chini ya ktabu: Wale ambao hasa wamependezwa katika habari hii wanaweza kupata kitabu cha bure, 'Uisraeli wa Uingereza Umepimwa', kinapatikana kwa wachapishaji.

**Somo La 3 : Maswali**

1. Ni ipi kati ya ahadi za Mungu inayotabiri kujitahidi daima kushindana kati ya dhambi na haki ?.

a) Ahadi kwa Nuhu
b) Ahadi katika Edeni
c) Ahadi kwa Daudi
d) Ahadi kwa Abrahamu

2. Zipi kati ya taarifa zifuatazo ni za kweli kuhusu Ahadi katika Edeni ?

a) Mzao wa nyoka ni lusifa
b) Kristo na wenye haki ni uzao wa mwanamke
c) Uzao wa nyoka kwa muda ulipondwa na Kristo
d) Uzao wa Mwanamke ulichubuliwa kwa kifo cha Kristo

3. Uzao wa Abrahamu utaishi wapi milele ?

a) Mbinguni
b) Katika mji wa Yerusalemu
c) Duniani
d) Wengine mbinguni wengine duniani

4. Kati ya yafuatayo yapi aliahidiwa Daudi ?
a) Kwamba mtoto wako mkubwa atatawala milele
b) Kwamba 'Mzao' wake utakuwa na ufalme mbinguni
c) Mzao huyo atakuwa Mwana wa Mungu
d) Mzao huyo, Yesu, aliishi mbinguni kabla ya kuzaliwa

5. Tunawezaje kuwa uzao wa Abrahamu ?

6. Je ! dunia itaharibiwa ?

7. Ahadi za Mungu zinathibitishaje jibu lako kwa swali la 6 ?

8. Eleza Ahadi ya Edeni katika Mwanzo 3:15.

# *SOMO LA 4*

# MUNGU NA MAUTI

## 4:1 Binadamu

Watu wengi wanaonekana kutumia muda mdogo kufikiria kuhusu mauti; au kuhusu desturi zao wenyewe, ambazo ni sababu kubwa za mauti. Kukosa hivi kujihoji nafsi kunaongoza kukosa maarifa ya mwenyewe, na kwa sababu hii watu huchukuliwa kufuata maisha, Wakifanya maamuzi yao kulingana na wanavyoamriwa na haja ya mwili wao.Kupo kukataa ingawa kwa ukubwa kumefichwa - kuchukuliwa ukweli wa kwamba uhai ni mfupi mno hata watu wote pia hali ya mwisho ya mauti itakuwa juu yetu.'Uzima wenu ni nini ? Maana ninyi ni mvuke uonekanao kwa kitambo, kisha hutoweka' “Kwa kuwa hatuna budi kufa, nasi tu kama maji yaliyomwagika chini, yasiyoweza kuzoleka tena” “Asubuhi huwa kama majani yameayo: asubuhi yachipuka (Ujana wetu ) na kumea, jioni yakatika na kukauka” (Yakobo 4:14; 2 Sam.14:4; Zab. 90: 5,6). Musa kweli mtu wa kuhubiri, alitambua hili, alimwomba Mungu: “Basi, tufundishe - tujulishe kuzihesabu siku zetu, ili tujipatie moyo wa hekima” (Zab. 90:12). Basi, kwa mtazamo wa ufupi wa maisha, tendo la kupata hekima ya kweli tutalipa kipaumbele.

Kuvutika kwa mtu na Mauti kwa hali ya mwisho ni kwa namna nyingi. Mila nyingine zimejaribu kufanya mauti na maziko ni sehemu ya maisha, hupunguza maana ya msiba na kuwa hali ya mwisho. Hao wengi wachukuao jina la "Kristo" Wamedhani, kuwa mtu anayo'Roho - nafsi isiyokufa' au kitu fulani kinachoishi milele ndani yake kinachopona mauti; kinaendelea kuishi sehemu nyingine zaidi na jambo liletalo huzuni kwa mwanadamu, itegemewe ya kwamba moyo wa mtu umezoezwa sana kupunguza mgongano wa akili yake; kwa hiyo shabaha yote ya nadharia potovu imetokea kuhusu mauti na desturi hasa za mtu. Kama siku zote, hizi inabidi zipimwe dhidi ya Biblia ili kupata ukweli kuhusu hili jambo muhimu la kuzungumuziwa. Ikumbukwe kuwa uongo kabisa wa kwanza ulioandikwa ndani ya Biblia ni ule wa nyoka katika bustani ya Edeni. Tofauti na taarifa kamili ya Mungu kuwa mtu "hakika atakufa" kama akitenda dhambi (Mwa. 2:17). nyoka alidai, "Hakika ninyi hamtakufa" (Mwa. 3:4). Uongo huu unajaribu kukana hali ya kufikia mwisho kwa kufa kabisa hivi imekuwa ni desturi ya dini zote potovu, ni dhahiri hasa kwa eneo hili, fundisho moja la uongo laongoza lingine, lingine na lingine. kwa kinyume, neno moja la kweli laongoza lingine, kama lilivyoonyeshwa na 1 Kor. 15:13 -17. Hapa Paulo anaruka toka ukweli mmoja hadi mwingine (angalia "Kama ….Kama …. Kama….").

Kuelewa desturi zetu kweli, tunatakiwa kuona Biblia yasemaje kuhusu Uumbaji wa mtu. Taarifa imo katika lugha ya wazi, ambayo, ikichukuliwa kama ilivyo, hatuwi na mashaka hasa kuhusiana na mwili ulivyo (tazama kitambo kinachozungumziwa sehemu ya 18 kuhusu maneno yalivyo katika kitabu cha Mwanzo). "BWANA Mungu akafanya mtu kwa mavumbi ya ardhi …. Katika hiyo (ardhi) ulitwaliwa (Wewe Adamu) kwa maana u mavumbi wewe nawe mavunbini utarudi" (Mwa. 2:7; 3:19). Hapa

hakuna kidokezo kabisa kuwa mtu yeyote amerithi kitu kisicho kufa; hakuna sehemu iliyo ndani yake inayoendelea kuwa hai baada ya kufa.

Upo mkazo wa Biblia ulioonyeshwa juu ya ukweli kwamba mtu kwa ukubwa ametokana na mavumbi tu: "Sisi tu Udongo" (Isa. 64:8); "Mtu wa kwanza atoka katika nchi, ni wa udongo" (1Kor. 15:47); Mtu msingi wake ni katika mavumbi" (Ayu. 4:19); "mtu hurejea tena kuwa mavumbi" (Ayu. 34:14,15). Abrahamu alikiri kwamba alikuwa "ni mavumbi na majivu tu" (Mwa. 18:27).Mara baada ya kuvunja amri ya Mungu pale Edeni, Mungu akamfukuza huyo mtu ….. asije akanyoosha mkono wake, akatwaa matunda ya mti wa uzima , akala, akaishi milele" (Mwa. 3:24,22). ikiwa mtu alikuwa na kitu kisichokufa kwa kawaida ndani yake, hii amri isingekuwa ya lazima kumzuia.

**SHARTI LA KUTOKUFA.**

Ujumbe wa Injili uliorudiwa usiobadilika ni kuwa mtu anaweza kuiona njia na kupata uzima wa milele na kutokufa kwa kupitia kazi ya Kristo. Huu ukiwa ni mfano pekee wa kutokufa ambao Biblia yausema, jambo linalofuatia kama kuteseka huku mtu akiwa na fahamu kwa kutenda mabaya Biblia haisemi lolote kuhusu hili. njia peke ya kupata kutokufa ni kwa kutii amri za Mungu, na wale ambao wanatii hizo watatumia maisha ya kutokufa wakiwa na hali ya ukamilifu - thawabu ya kuwa mwenye haki. Mafungu yafuatayo ya maneno ni ushuhuda wa kutosha wa kuwa huku kutokufa ni sharti, na si jambo fulani analo mtu wa kawaida: -

- "Kristo amefunua uzima na kutokufa (Kutoharibika)kwa ile Injili" (2 tim. 1:10; 1Yoh. 1:12).
- "Msipokula mwili wake mwana wa Adamu na kuinywa damu yake, hamna uzima ndani yenu (Yaani mliourithi ndani

yenu). Aulaye mwili wangu na kuinywa damu yangu anao uzima wa milel; nami nitamfufa siku ya mwisho" na kumpa huu "Uzima wa milele" (Yoh. 6:53,54). Fikira za Kristo katika sura ya 6 ya Yohana yote ni kwamba yeye ni chakula -"Mkate wa Uzima", ni kwa usahihi pekee wa kumkubali tumaini lolote laweza kuwepo la kutokufa (Yoh. 6:47,50, 51,57, 58).

- "Mungu ametupa sisi (Waaminio) uzima wa milele, na uzima huu umo katika mwanawe" (1 Yoh. 5:11). haliwezi kuwepo tumaini la kutoharibika kwa wale wasio'Katika Kristo'. Ni kwa Kristo pekee kutoharibika kumewezekana.

- Yeye ni "Mkuu wa uzima ( wa milele)" (Mdo. 3:15) - "(Mkuu) sababu ya wokovu wa milele kwa wote wanaomtii" (Ebra. 5:9). Basi kutokufa kwa watu kulianzishwa na kazi ya Kristo.

- Mwamini wa kweli anatafuta kutoharibika, atapewa thawabu ya kipawa cha uzima wa milele - jambo lingine kwa kawaida asilonalo (Rum. 2:7; 6:23; Yoh. 10:28). Mwili wetu wa kufa, inabidi uvae kutoharibika Kristo atakaporudi (1Kor. 15:53); hivyo kutokufa ni jambo lingine lililoahidiwa, kwa sasa halipo (1 Yoh. 2: 25).

- Mungu pekee ana asili ya kutoharibika (1 Tim. 6:16).

### 4.2 Nafsi Au Roho

Kwa mwangaza unaosonga mbele inabidi kutofikiri kuwa mtu anayo'Nafsi au Roho isiyokufa' au kitu chochote kisichokufa ndani yake cha kawaida. Tutajaribu kutengeneza vizuri chafuko linalozunguka neno'Nafsi':

Maneno ya Kiebrania na Kiyunani ambayo yametafsiriwa'nafsi' katika Biblia

('Nephesh' na'Psuche' moja moja) pia yametafsiriwa kwa namna zifuatazo: -

**Mwili Pumzi**
**Kiumbe moyo**
**Akili mtu**
**Yeye mwenyewe**

Kwa sababu hii'Nafsi' inaitwa mtu, mwili au mwenyewe. Neno mashuhuri'Okoa Roho zetu' maana yake'Tuokoe katika mauti'. Kwa hiyo nafsi au Roho ni'wewe' au mambo yote yanayomfanya kuitwa mtu. Inaeleweka, basi, ya tafsiri tulizo nazo Afrika ya Mashariki (U.V) inatumia neno'nafsi' mara nyingi badala ya neno'Wewe' au'Mtu'. Katika Biblia ya kiswahili cha kisasa neno linalotumika ni kiumbe hai. Wanyama aliowaumba Mungu wameitwa ni viumbe wenye uhai viendavyo ….. kila kiumbe chenye uhai (Mwa. 1:20, 21).

Neno la Kiebrania lililotafsiriwa "Kiumbe" hapa ni'Nephesh', pia limetafsiriwa'nafsi'; kwa mfano katika Mwa. 2: 7; "…….. naye mtu akawa nafsi hai". Hivyo mtu ni'nafsi' kama nao wanyama ni'nafsi'. tofauti pekee iliyopo kati ya Wanadamu na Wanyama ni huo ubora wa akili waliyonayo; ameumbwa kwa mfano wa mwili wa Mungu (Mwa. 1:26). ona somo la 1:2, na watu wengine wameitwa kumjua Mungu kwa Injili ambamo ndani yake tumaini la kutokufa limefunuliwa kwao (2 Tim. 1: 10). Kwa habari ya asili ya desturi yetu na kawaida ya kufa kwetu, haipo tofauti kati ya Mwanadamu na Wanyama: -

“Linalowatokea wanadamu huwatokea na wanyama; jambo moja lawatokea (elewa limekaziwa mara dufu): anavyokufa huyu ndivyoanavyokufa huyu ….. wala mwanadamu hana kitu cha kumpita mnyama ….. wote (yaani wanadamu na wanyama) huenda mahali pamoja (Kaburini); wote hutoka katika mavumbi; na hata mavumbini hurudi tena” (Mhu. 3: 19,20). Mwandishi wa kitabu cha mhubiri aliyevuviwa aliomba ya kwamba Mungu awasaidie waufahamu huu ukweli mgumu, “ ya kuwa (wanadamu) wao wenyewe wanafanana na wanyama” (Mhu. 3:18). Kwa hiyo inategemewa ya kuwa watu wengi itawawia vigumu kuukubali ukweli huu; Kwa kweli utakuwa ni wa kuweza kufedhehesha kutambua kuwa sisi na wanyama ni sawa sawa, tukiishi kutokana na akili hizo hizo za kujilinda wenyewe, kuishi na kupona mbali na kifo kuwepo, na kuendelea kuzaana. Biblia zote za aina mbili yaani U.V na Biblia - Habari njema - B H.N. hii tafsiri ya mhubiri 3:8 inasema kwamba Mungu anamjaribu mwanadamu kwa kumfanya aone kuwa yeye ni mnyama tu. Yaani wale wanaojinyenyekeza mno ili kuwa watu wake wa kweli wanatueleza ukweli huu, bali wale ambao sio watashindwa'jaribu' hili. Elimu ya mwanadamu - wazo la kwamba watu wapo katika ukuu na thamani - kwa utulivu imeeneza ulimwenguni pote kwa karne hii ya ishirini. Ni kazi ya kufaa kusafisha fikira zetu kwa mvuto wa Elimu ya mwanadamu. maneno yaliyo dhahiri ya zaburi 39:5 yanasaidia: “Kila mwanadamu, ingawa amestawi ni ubatili” Njia ya mwanadamu haimo katika nafsi yake kuelekeza hatua zake si katika uwezo wa mwanadamu” (Yer. 10:23).

Moja zaidi ya mambo ya msingi tunayoyajua ni kwamba miili ya wanadamu wote - kwa kweli, vyote “Viumbe hai” hatimae hufa. Basi,'Nafsi' au Roho, inakufa; ni kinyume kabisa na kitu kingine kisichokufa. Haishangazi kuwa karibu theluthi ya matumizi yote ya maneno yaliyotafsiriwa'nafsi' katika Biblia yameunganika na kifo

na kuunganika kwa nafsi. ukweli kabisa wa neno Roho, nafsi umetumika kwa namna hii ukionyesha kwamba hakiwezi kuwa kitu fulani kisichoharibika na kisichokufa: -

- "Roho, nafsi itendayo dhambi, itakufa" (Ezek. 18:4)
- Mungu anaweza kuiua Roho (Math. 10:28). Mistari mingine ya Roho kuangamia ni (Ezek. 22: 27; Mith. 6: 32; Law. 23:30).
- Wote wenye kuvuta'Pumzi' wakaangamia kwa makali ya upanga waliokuwa katika Hazori (Yosh. 11:11; 10:30 -39). …….kila Roho yenye uhai ikafa" (Uf. 16:3; Zab. 78:50).
- Kutengwa kwa nafsi kunaweza kuleta maana ikieleweka kuwa Roho inakufa (Mith. 18: 7; 22:25; au kuchagua kunyongwa Ayubu 7:15).
- "Hakuna anayeweza kuhuisha nafsi yake" (Zab.22:29)
- Kristo "alimwaga nafsi yake hata kufa" hivyo basi'nafsi' yake au uhai, ulifanywa dhabihu kwa dhambi (Isa. 53:10, 12)

Ikiwa'nafsi au Roho' anatajwa mtu au mwili kuliko cheche fulani isiyokufa ndani yetu imeonyeshwa kwa mistari mingi ambamo neno hili linatokea. Mifano mingine iliyowazi wazi ni: -

- "Damu ya Roho" (Yer. 2:34)

- "Ee nafsi yangu ….vyote vilivyo ndani yangu ……. Ee nafsi yangu umhimidi BWANA …..aushibisha mema uzee wako" (Zab. 103: 1, 2, 5)
- "Kwa kuwa mtu atakaye kuiponya nafsi yake ataiangamiza; bali atakayeiangamiza nafsi (Uhai) kwa ajili yangu …. Ataisalimisha" (Marko. 8:35).

Huu ni ushahidi wa kutosha wa nafsi hakitajwi kitu chochote cha kiroho ndani ya mtu; hapa,'nafsi' (Kiyunani'psuche') ina maana uhai wa mwili wa mtu tu, ndivyo lilivyotafsiriwa hapa

- Hesabu 21:4 mstari unaonyesha kwamba kundi la watu laweza kuwa na nafsi - "Moyo" mmoja. Basi moyo hauwezi kutaja cheche binafsi isiyokufa ndani ya kila mmoja wetu.

### 4.3 Roho ya Mtu

Kuna chafuko lisilo la heri katika fikira za watu wengi kati ya nafsi na roho. Hili limesumbua kwa ukweli kwamba katika lugha zingine na tafsiri za Biblia, maneno ya Kiingereza'nafsi' na'roho' yanafanana.'Nafsi' kwa ukubwa yanatajwa yote yanayofanywa na mtu wakati mwingine yaweza kutaja roho vile vile. Ingawa hivyo, kwa kawaida kuna tofauti katika maana kati ya'nafsi' na'Roho' kama yalivyotumika katika Biblia; nafsi na Roho zaweza'kugawanyika' (Ebra. 4: 12).

Kiebrania na Kiyunani maneno'Roho' ('Ruach na'Pneuma' mbali mbali) vile vile yametafsiriwa kwa namna ifuatavyo: -

**Uhai** **Roho**
**Akili** **Upepo**
**Pumzi**

Tumejifunza jambo la'Roho' katika somo la 2.1. Mungu anatumia roho yake kutunza viumbe vya asili, na mwanadamu amejumuika. Roho ya Mungu iliyo ndani ya mwanadamu kwa sababu hii ni nguvu ya uhai iliyo ndani yake "mwili bila roho umekufa" (Yakobo 2:26). Mungu akampulizia katika (Pua ya Adamu) Pumzi (Roho) ya uhai; mtu akawa nafsi hai (Kiumbe)

(Mwa. 2:7)" Ayubu anaisema'roho ya Mungu' kuwa' Roho ya Mungu i katika pua yangu' (Ayubu. 27:3;Isaya 2:22). Roho ya uhai iliyo ndani yetu tunapewa tukizaliwa, nayo tunakuwa nayo mwili unapokuwa hai. Roho ya Mungu ikiondolewa toka kitu chochote, mara moja inapotea - roho ya nguvu ya uhai. Mungu "akijikusanyia roho yake na pumzi zake; wenye mwili wote wataangamia pamoja, nao wanadamu watarejea tena kuwa mavumbi. Ikiwa una ufahamu, sikia neno hili" (Ayubu. 34:14 -16). Sentensi ya Mwisho inadokeza tena ya kuwa mwanadamu anakuta hii inaweka wazi umbile lake halisi kuwa vigumu kupatana.

Mungu anapotwaa roho yake toka kwetu tunapokufa. Sio mwili pekee unaokufa, bali fahamu zetu zote zinakoma. Daudi alipofahamu jambo hili lilimfanya amwamini Mungu kuliko viumbe kama Binadamu. Zaburi.146:3 -5 ni kukabiri ugumu kwa madai ya wanadamu: "Msiwatumainie wakuu, wala binadamu ambaye hakuna wokovu kwake, Pumzi yake (roho) hutoka, hurudia udongo wake, Siku hiyo mawazo yake yapotea (Maana amefanywa kwa udongo) Heri ambaye Mungu wa Yakobo ni msaada wake".

Wakati wa kufa, "Mavumbi hurudia nchi kama yalivyokuwa; nayo roho humrudia Mungu aliyeitoa" (Mhubiri 12: 7). Tumeonyesha awali kuwa Mungu yupo kila mahali kwa njia ya roho yake. kwa maana hii " Mungu ni Roho" (Yoh. 4:24). Tunapokufa'tunavuta pumzi ya mwisho' katika maana kwamba roho ya Mungu iliyondani mwetu imeondoka. kama roho inavuta katika roho ya Mungu inayotuzunguka pande zote; basi wakati wa kufa "roho itamrudia Mungu" Kwa sababu roho ya Mungu hutegemeza viumbe vyote, mfuatano huu wa kufa huwatokea wanyama wote. Watu na wanyama wana roho ile ile, au nguvu ya kuwa hai, ndani yao.'Kwa maana linalowatukia; anavyokufa huyu

ndivyo anavyokufa huyu; naam, wote wanayo pumzi moja (Yaani, ile ile) roho ya Pumzi; wala mwandamu hana kitu cha kumpita mnyama" ( mhubiri 3: 19).

Mwandishi anaendelea kusema kwamba hakuna tofauti ya kuona kati ya roho za watu na wanyama zinakwenda wapi (Mhubiri 3: 21). Maelezo haya ya watu na wanyama kuwa na roho moja na kufa kifo kimoja, yanaelekea kurudi kutaja maelezo jinsi wote wanadamu na wanyama, waliokuwa na roho ya uhai toka kwa Mungu (Mwa. 2:7;7:15), waliharibiwa na kifo kile kile wakati wa gharika: "wakafa wote wenye mwili waendao juu ya nchi, na ndege, na wanyama wa kufugwa, na kila mnyama wa mwitu, na kila kitambaacho chenye kutambaa juu ya nchi, na kila mwandamu; kila kitu chenye pumzi ya uhai puani mwake kikafa ……kila kilicho hai kikafutiliwa mbali" (Mwa. 7:21 -23).Ona kwa kupita jinsi Zaburi ya 90:5 inavyolinganishwa mauti na gharika. Taarifa iliyo katika Mwanzo 7 kwa udhahiri inaonyesha hivyo kwa maneno ya msingi, watu wapo katika aina hiyo hiyo ni "wote wenye mwili ……..kila kilicho hai". Hii ni kwa sababu ya kuwa na roho moja ya uhai ndani yake kama wengine.

### 4.4 Mauti ni Kutokuwa na Fahamu Kabisa

Kutoka kile tulichojifunza mpaka hapo kuhusu nafsi na roho, kinachofuata ni kwamba muda mtu anapokuwa amekufa hawi na fahamu kabisa. Wakati matendo ya wale wanaopashwa kwa Mungu yatakumbukwa naye (Malaki 3:16; Uf. 20:12; Ebra. 6:10), Katika Biblia hakuna kinachodokezwa kuwa tunazo fahamu zozote mautini. Ni vigumu kubishana na shuhuda wazi zifuatazo kuhusu hili:-

• “Pumzi ya (mtu) humtoka, naye hurudi katika udongo wake; siku hiyo mawazo yake yapotea” (Zaburi 146: 4).

• “Wafu hawajui neno lolote, …. Mapenzi yao, na machukio yao, na husuda yao, imepotea yote pamoja” (Mhubiri 9:5,6). Hakuna “hekima huko kuzimu” (Mhu. 9:10) - hakuna kufikiri na kwa hiyo hakuna fahamu.

• Ayubu anasema kwamba mautini, atakuwa'Kana kwamba hakuwahi kuwepo’ (Ayu. 10:18); aliona mauti kuwa ni usahaulifu, kutokuwa na fahamu na kukosa kuwepo kabisa tuliokuwa nao kabla ya sisi kuzaliwa.

• Watu wanakufa kama wanyama (Mhu. 3:8); ikiwa mtu anakuwa na fahamu akiwa amepona kifo na kuishi mahali fulani, lakini yote mawili, maandiko na sayansi vipo kimya kuhusu hili.

• Mungu “anatukumbuka kuwa ni mavumbi. Mwanadamu siku zote si kama majani; kama ua la kondeni ndivyo asitawivyo …. Haliko; na mahala pekee hapatalijua tena” (Zab. 103:14 -16).

Mautini hakika ni kutokuwa na fahamu, hata kwa wenye haki, yameonyeshwa maombi yaliyorudiwa ya watumishi wa Mungu waruhusiwe maisha yao yaweze kurefushwa, kwa sababu walijua kwamba baada ya kufa hawataweza kumsifu na kumtukuza Mungu, kwa kuwa mautini ni kutokuwa na fahamu. Hezekia (Isaya 38:17 -19) na Daudi (Zaburi 6:4,5; 30:9; 39:13; 115:17) wao ni mfano huu mzuri. mauti yamerudiwa kwa kutaja kuwa ni kulala au kupumzika, wote wawili kwa wenye haki na waovu (Ayu. 3:11, 13:17; Dan 1.12:13). Ushahidi wa kutosha umetolewa kwa ajili yetu unaosema wazi ya kwamba wazo la watu wengi kuwa wenye haki wanakwenda kwenye hali ya furaha na kupewa thawabu mbinguni moja kwa moja mara baada ya kufa, peke yake haupatikanai katika Biblia. Funzo la mauti na umbo la binadamu kweli linatoa amani kubwa ya maana. Baada ya hali yote ya magonjwa na maumivu ya maisha ya binadamu, Kaburini ni

mahala pa usahaulifu kabisa. kwa wale ambao hawajui matakwa ya Mungu, usahaulifu huu utadumu milele. Sababu kuu ya huzuni hii na uhai wa kwanza hautarudi tena; matumaini yasiyofaa na hofu ya asili ya nia ya mwanadamu havitatambulika au kuogofya.

Kwa kusoma Biblia, kuna utaratibu kweli wa kuivumbua; lakini, kwa bahati mbaya, pia upo utaratibu wenye kosa katika dini aliyojitungia mtu, kutokana na kutoiangalia Biblia. Jitihada za binadamu kurahisisha kilele cha mauti imepelekea aamini ya kwamba ana'nafsi /roho isiyokufa' Mara ikikubalika kuwa kitu hiki kisichokufa kimo ndani ya binadamu, inakuwa ni lazima kudhani kwamba inabidi kiende mahali fulani baada ya kufa. hii imepelekea ya kwamba mautini inabidi ziwepo ajali fulani tofauti kati ya wenye haki na wabaya. kutengeneza wazo hili, imesemwa kuwa inabidi kuwepo sehemu ya'roho nzuri zisizokufa' huenda toharani - mbinguni na sehemu nyingine kwa ajili ya'roho mbaya zisizokufa' kwenda sehemu hiyo imeitwa kuzimu. Awali tumeonyesha kuwa'nafsi au roho' isiyokufa kwa Biblia haiwezekani. Mawazo mengine potovu yaliyo ndani ya watu wengi jinsi wanavyofikiri sasa yatachambuliwa: -

1. Kama thawabu ya maisha yetu inatolewa mautini kwa namna ya'roho yetu isiyokufa' kugawiwa mahala fulani.
2. Kama mtengano kati ya wenye haki na wabaya hutokea wakati wa kufa.
3. Kama thawabu ya wenye haki ni kwenda mbinguni (Toharani ) sehemu ya amani.
4. Kama ikiwa kila mmoja ana'roho isiyokufa', basi kila mtu inambidi kwenda aidha mbinguni au kuzimu.
5. Kama'roho' za waovu zitakwenda mahala pa kuadhibiwa panapoitwa kuzimu. (sehemu ya mateso).

Shabaha ya uchambuzi wetu sio tu tunakanusha; kwa kupima alama hizi kwa maelezo ya moja baada ya nyingine, tunaamini ya kwamba tutaeleza mambo mengi ya Biblia katika ukweli ambao ni sehemu ya picha ya kweli kuhusiana na desturi ya binadamu.

### 4. 5 Ufufuo

Biblia imekaza kuwa thawabu ya wenye haki itakuwa kwenye ufufuo, Kristo atakapo kuja (1 Thes. 4:16).Ufufuo wa wafu wanaopasiwa (ona somo la 4.8) Litakuwa jambo la kwanza atakalofanya Kristo; hili litafuatiwa na hukumu. ikiwa'Roho' ilikwenda mbinguni wakati wa kufa kusingekuwa na haja ya ufufuo. Paulo alisema ya kwamba ikiwa ufufuo haupo, basi juhudi yote ya kumtii Mungu haina maana (1Kor. 15:32). kweli asingefikiria kama hivi ikiwa aliamini kuwa atapewa thawabu pia na'roho' yake ikienda mbinguni wakati wa kufa ? Kidokezo ni kwamba aliamini ufufuo wa mwili kuwa ni namna pekee ya thawabu. Kristo ametutia moyo tuwe na mategemeo ya kwamba kupewa thawabu waaminifu walio hai sasa itakuwa wakati wa "Ufufuo" ( Luk. 14:14).

Maana inabidi tena ituingie sana akilini ya kwamba Biblia haifundishi namna yoyote ya kuwepo mbali na kuwa na umbo la mwili - hili linatumika kwa Mungu, Kristo, Malaika na watu. Kristo atakaporudi "ataubadili mwili wetu mbaya, upate kufanana na mwili wake wa utukufu" (Flp. 3:20,21). Ikiwa sasa ana umbo lenye mwili halisi, mwili umetiwa nguvu na roho kuliko damu, hivyo tutashiriki thawabu hii. Kwenye hukumu tutapewa thawabu kwa jinsi tulivyoishi maisha haya katika umbo la mwili

(2 Kor. 5:10). Wale walioishi maisha ya mwilini - yaani kufuata mwili unavyotaka watabaki na mwili wa sasa unaokufa,

ambao wakati huo utaoza ukirudi mavumbini; wakati wale ambao katika maisha yao wamejaribu kuishinda nia ya mwili kwa hiyo ya Roho " Katika Roho atavuna uzima wa milele" (Gal. 6:8) kwa umbo la mwili

uliojazwa Roho.

Upo ushahidi mkubwa wa kuwa thawabu ya wenye haki itakuwa katika umbo la mwili. Mara huu ukifahamika, maana kuu ya ufufuo itakuwa wazi. Ni dhahiri mwili wetu wa sasa unakoma kuishi tukifa; ikiwa tunaweza kupata tu uzima wa milele na kutokufa katika umbo la mwili, kinachofuata ni kwamba mauti ni hali ya kutokuwa na fahamu. mpaka kipindi hiki cha mwili ukiumbwa tena na kisha kupewa mwili wa Mungu.

1 Wakorintho 15 yote inazungumzia kwa kutoa maelezo ya ufufuo; siku zote italipa usomaji wa makini. 1Kor. 15;35 -44 yaeleza jinsi mbegu inavyopandwa na kisha inatoka ardhini ili kupewa mwili wa Mungu, Basi wafu vile vile watafufuka na kupewa thawabu ya mwili. Kama Kristo alivyotoka kaburini na mwili wake wa kufa ukabadilishwa hata kuwa usiokufa, hivyo mwamini wa kweli atashiriki thawabu yake (Flp. 3:21). kwa kubatizwa tunajiunga sisi wenyewe na kifo cha Kristo na ufufuo, tukionyesha imani yetu kwamba nasi, pia, tutashiriki thawabu aliyoipokea kwa kufufuka kwake (Rum.6: 3 -5). Kwa kuyashiriki mateso yake sasa, pia tutashiriki thawabu yake "Tutachukuwa katika mwili (Sasa) kuuawa kwake Yesu, ili uzima wa Yesu nao udhihirishwe katika miili yetu" (2Kor. 4:10). "Yeye aliyemfufua Kristo katika wafu ataihuisha na miili yenu ya kufa kwa roho wake" (Rum. 8:11). Basi kwa tumaini hili "tunasubiri ukombozi wa mwili wetu" (Rum.8:23), kwa mwili huo ukiisha fanywa usife.

Tumaini hili la mwili halisi la kupewa thawabu lilieleweka na watu wa mungu tangu nyakati za kwanza. Abrahamu aliahidiwa

kwamba, yeye binafsi atarithi nchi ya Kanaani milele, hakika kama alivyotembea juu ya nchi ndani yake (Mwa. 13:17; tazama somo la 3.4.). Imani yake kwa hizo ahadi ilimwezesha aamini kuwa mwili wake kwa namna nyingine, tarehe zijazo, atafufuliwa na kufanywa asife, hivyo hii itawezekana.

Ni dhahiri Ayubu alieleza fahamu zake jinsi, mbali ya mwili wake kuliwa na funza kaburini kwa umbo la mwili atapokea thawabu yake: "mteteaji (Mkombozi) wangu yu hai ….. hatimae atasimama juu ya nchi na baada ya ngozi yangu kuharibiwa hivi lakini pasipo kuwa na mwili wangu nitamwona Mungu (nitamwona Mungu kwa macho yangu mwenyewe au katika mwili huu -B.H.N) nami nitamwona mimi nafsi yangu, na macho yangu yatamtazama, wala si mwingine, Ingawa mtima wangu unazimia ndani yangu" (Ayu.19:25 -27). Tumaini la Isaya lilikuwa hili hili. "Maiti yangu itafufuka ….." (Isa. 26: 19).

Maneno haya kabisa yapatikana katika kifo cha Lazaro, rafiki yake Yesu. Badala ya kumfariji dada mtu kwa kusema kwamba roho yake imekwenda mbinguni, Bwana Yesu alisema siku ya ufufuo: "Ndugu yako atafufuka". Jibu la haraka toka kwa dada yake Lazaro, Martha laonyesha ni kiasi gani hili lilieleweka na Wakristo wa kwanza: "Martha akamwabia, Najua ya kwamba atafufuka katika ufufuo siku ya mwisho"(Yoh. 11:23,24). Kama Ayubu, hakufahamu kuwa mauti ndio njia peke ya kwenda kwenye furaha mbinguni, bali, badala yake alitazama mbele kwenye ufufuo "Siku ya mwisho ("Hatimaye" ya Ayubu). Bwana ameahidi: "Kila aliyesikia na kujifunza kwa Baba …. Nami nitamfufua siku ya Mwisho" (Yoh. 6:44,45).

## 4.6 Hukumu

Biblia hufunza kuhusu hukumu ni moja ya mambo makuu ya msingi wa imani moja, ambayo inabidi yaeleweke wazi kabla ya kubatizwa (Mdo. 24:25; Ebra. 6:2). Mara nyingi Maandiko yanataja'Siku ya hukumu' (kwa mfano, 2 Pet. 2:9; 3: 7; 1Yoh. 4: 17; Yuda.6) kipindi ambacho wale waliopewa maarifa na Mungu watapokea thawabu zao. Wote hao itawapasa "kusimama mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo" (Rum. 14:10); sisi sote "kudhihirishwa mbele ya kiti cha hukumu ya Kristo" (2 Kor. 5:10) ili kupokea thawabu ya maisha yetu katika umbo la mwili.Maono ya Danieli kuhusu kuja kwa mara ya pili Kristo, yamejumuisha moja ya kiti cha hukumu kwa mfano wa kiti cha enzi (Dan. 7: 9 - 14). Mahubiri ya mifano yanasaidia kidogo kuongeza maelezo zaidi. Hayo ya talanta yamefananishwa na kurudi kwa Bwana, awaitaye watumishi wake na kuhesabu kadri ya jinsi walivyotumia vema pesa alizowapa (Math. 25: 14 -29).Mfano wa wavuvi umelinganishwa na mwito wa Injili kwa nyavu za kuvulia, zikikusanya kila aina ya watu; ndipo watu wakaketi (Kuweka hukumu) nao wakagawa samaki wazuri na wabaya (Math. 13: 47 - 49). Tafsiri ipo wazi: "Mwisho wa ulimwengu malaika watatokea, nao watawatenga kati ya wabaya na wenye haki".

Mpaka hapo kutokana na tulichoona, ni vizuri kusadiki kwamba baada ya Bwana, akiisha rudi na kufufua kutakuwepo kukusanyika wote walioitwa na Injili kwenda mahali fulani kwa muda wa namna maalum, watakapokutana na Kristo. Hesabu itabidi wapewe, naye ataonyesha ikiwa wanakubalika au la kupokea thawabu ya kuingia katika ufalme. Ni katika maana hii tu wenye haki wanapokea thawabu yao. Yote haya yanaungwa pamoja na mahubiri ya mifano wa kondoo na mbuzi: "Mwana wa Adamu atakuja katika utukufu, na Malaika wote watakatifu

pamoja naye, ndipo ataketi kwenye kiti cha utukufu wake (Kiti cha enzi cha Daudi -Yerusalemu,Luka. 1: 32,33): na mbele yake watakusanyika mataifa yote (yaani - watu wa kutoka mataifa yote, Math. 28:19): naye atawagawa kama mchungaji anavyowagawa kondoo na mbuzi. Atawaweka kondoo mkono wake wa kuume, na mbuzi mkono wake wa kushoto. Kisha mfalme atawaambia wale walioko mkono wake wa kuume, Njooni, mliobarikiwa na Baba yangu, urithini ufalme mliowekewa tayari (Math. 25:31 -34).

Kurithi Ufalme wa Mungu, kupokea ahadi za Abrahamu kuhusu ufalme, ni thawabu ya wenye haki. Lakini hii itakuwa tu baada ya hukumu, itakuwa Kristo ajapo, Kwa hiyo haiwezekani kupokea thawabu iliyoahidiwa ya mwili usiopatikana na mauti kabla Kristo hajarudi; kwa sababu hii inatubidi kusema kuwa tangu wakati wa kifo hadi ufufuo, mwamini hana ufahamu unaoishi kabisa, kwa kuwa hauwezi kuishi kwa namna yoyote bila kuwa na mwili.

Ni neno la awali la Biblia kwamba Kristo akirudi, ndipo thawabu itatolewa - na sio kabla: -

- "Mchungaji mkuu (Yesu) atakapodhihirishwa, mtaipokea taji ya utukufu" (1Pet. 5: 4; 1:13).
- "Kristo Yesu atakayewahukumu walio hai na waliokufa, kwa kufunuliwa kwake na kwa ufalme wake ….. taji ya haki, ambayo Bwana, mhukumu mwenye haki, atanipa siku ile" (2Tim. 4:1;8).
- Masihi atakapokuja siku ya mwisho, "wengi wa hao walalao katika mavumbi ya nchi (Mwa. 3:19) wataamka, wengine wapate uzima wa milele, na wengine aibu na kudharauliwa" (Dan 12:2).
- Kristo atakapokuja katika hukumu, waliomo makaburini …. Watatoka; wale waliofanya mema kwa ufufuo wa uzima, na wale waliotenda mabaya kwa ufufuo wa hukumu" (Yoh. 5:25 -29).

• “Tazama, (mimi Yesu) naja upesi; na ujira wangu u pamoja nami, kumlipa kila mtu kama kazi yake ilivyo” (Uf. 22:12). Hatuendi mbinguni kupokea ujira - Kristo anatuletea toka Mbinguni.

Ujira upo pamoja naye Yesu kutuletea unadokezwa kwamba tumetayarishiwa mbinguni, lakini tutaletewa duniani ajapo mara ya pili;'Urithi” wetu wa nchi aliyoahidiwa Abrahamu kwa maana hii “Umetunzwa mbinguni kwa ajili yenu, Nanyi mnalindwa na nguvu za Mungu kwa njia ya Imani hata mpate wokovu ulio tayari kufunuliwa wakati wa mwisho” Kristo ajapo.(1Pet. 1:4,5) Kufahamu hili kunatuwezesha kufasiri kwa usahihi lisiloeleweka mno fungu la maneno yaliyo katika Yohana 14:2,3: “Maana (mimi Yesu) naenda kuwaandalia mahali. Basi mimi nikienda kuwaandalia mahali (tuzo “ imetunzwa mbinguni”), nitakuja tena niwakaribishe kwangu ili nilipo mimi nanyi mwepo” Yesu anasema kila mahali kuwa atakuja tena kutupa tuzo zetu (Ufu. 22:12), tumeona kwamba hizi zitatolewa kwenye kiti chake cha hukumu. Atatawala juu ya kiti cha enzi cha Daudi Yerusalemu'milele’ (Luk. 1:32,33). Maisha ya milele atayatumia hapa duniani, ni mahala atakapokuwa katika ufalme wa Mungu duniani - hapo tutakuwepo nasi pia. Ahadi ya “Kuwakaribisha kwangu” inaweza basi kusomwa kuwa ni maelezo ya sisi kukubaliwa naye kwenye hukumu. Fungu la maneno machache ya Kiyunani katika sentensi “niwakaribishe kwangu”, vile vile linatokea katika Math. 1:20 kuhusu Yusufu “kumchukua kwake” Mariamu kuwa mkewe. Basi halihitaji kwa ulazima kuondoka kwa mwili kuelekea kwa Yesu.

Kama tuzo itatolewa tu kwenye hukumu Kristo atakaporudi, kinachofuatia ni kwamba wenye haki na waovu wanakwenda kwenye sehemu moja wanapokufa yaani Kaburini hakuna tofauti inayofanywa kati yao katika mauti yao.

Kwa jambo hili yafuuatayo ni ushahidi wa hakika: -

- Yonathani alikuwa mwenye haki,Sauli mwovu,Lakini “Mautini hawakutengwa”
(2 Sam. 1:23).
- Sauli, Yonathani na Samweli wote walikwenda sehemu moja walipokufa (1 Sam. 28:19).
- Abrahamu mwenye haki “ akakusanyika kwa watu wake” au wazee, alipofariki; walikuwa ni waabudu sanamu (Mwa. 25:8; Yoshua.24:2)
- Aliye na busara kiroho na mpumbavu wanapata kifo kimoja (Mhub. 2: 15. 16).

Hii yote ni tofauti dhahiri kwa madai ya'Ukristo’ wa watu wengi. Mafundisho yao kuwa wenye haki mara akifa anakwenda mbinguni yanaharibu haja ya ufufuo na hukumu. Lakini tumeona ya kuwa haya ni matukio ya muhimu katika mpango wa wokovu wa Mungu,hivyo katika ujumbe wa Injili wazo la wengi kuwa mwenye haki mmoja anakufa na kupewa tuzo ya kwenda mbinguni, akifuatiwa siku nyingine, mwezi unaofuata, mwaka unaofuata, na wengine.

Wazo hili linapingana vikali na mafunzo ya Biblia ya kuwa wenye haki wote watapewa thawabu pamoja: -

- Kondoo wanatengwa kwenye hukumu, mmoja mmoja.mara hukumu ikiisha, Kristo atawaambia kondoo wote waliokusanyika mkono wake wa kuume,
- “Njoni, mliobarikiwa na baba yangu, urithini ufalme mliowekewa tayari” (Math.25:34). Hivyo kondoo wote wanarithi ufalme wakati mmoja (1 Kor. 15:52).

- Kwenye'mavuno' ya Kristo akirudi na kufanya hukumu, wote waliofanya kazi ya injili'Watafurahi pamoja' (Yoh. 4:35,36; Math. 13:39).
- Ufunuo 11:8 hufafanua "Wakati wafu watakapohukumiwa" hapa Mungu'atakapowapa thawabu watumwa wake ….Watakatifu …. Nao wanaolicha jina lako' - yaani waamini wote pamoja.
- Waebrania 11 ni sura inayoorodhesha watu wengi wenye haki walio katika Agano la Kale mstari wa 13 unasema: "Wote hawa walikufa katika imani, bila kupokea ahadi, alizoahidiwa Abrahamu kuhusu wokovu wa kuingia ufalme wa Mungu (Ebra. 11:8 -12). kinachofuata ni kwamba kwenye kifo chao, watu hawa,mmoja mmoja hawakwenda mbinguni kupokea thawabu. Sababu hizi zimetolewa katika mstari 39,40: Wote'hawakupokea ahadi: Kwa kuwa Mungu alikuwa ametangulia kutuwekea sisi kitu kilicho bora, ili wao wasikamilishwe pasipo sisi". Kuchelewesha kuwapa thawabu yao waliyoahidiwa sababu ilikuwa ni mpango wa Mungu wa kwamba waaminifu wote "Wakamilishwe" pamoja, kwa wakati mmoja. Tendo hili litafanyika kwenye hukumu, Kristo akirudi.

## 4.7 Mahali pa Kupewa Thawabu: Mbinguni au Duniani ?

Mbali na sababu zilizo juu, yeyote anayekuwa mbinguni sio duniani ndipo patakuwa mahala pa ufalme wa Mungu, Yaani pa tuzo iliyoahidiwa, inahitajika pia kueleza kutokana na vipengele vifuatavyo:-

- 'Sala ya Bwana' inaomba ufalme wa Mungu uje (yaani, kuomba Kristo arudi), ili mapenzi ya Mungu yatimizwe duniani kama mbinguni (Math. 6:10). Kwa hiyo tunaomba ufalme wa Mungu uje duniani. Ni huzuni kwa watu maelfu wanaomba maneno haya kila siku bila kufikiri wakati bado wanaamini kuwa

ufalme wa Mungu tayari sasa umewekwa imara mbinguni, na kuwa dunia itaharibiwa.

- "Heri wenye upole; maana hao watairithi nchi" (Math. 5:5) - Sio'…… maana nafsi, roho zao zitakwenda mbinguni'. Huu unataja katika kusema Zaburi 37, yote inakaza kusema ya kwamba thawabu ya mwisho ya wenye haki itakuwa duniani. Katika hii hii halisi ambayo waovu walifurahi ukuu wao wa muda, Wenye haki watapewa zawadi ya uzima wa milele, na kumiliki nchi ambayo waovu walitawala (Zab. 37:34, 35).'Wenye upole watairithi nchi ….. maana waliobarikiwa na yeye watairithi nchi …… wenye haki watairithi nchi, nao watakaa humo milele" (Zab. 37:11, 22,29). kuishi katika nchi/ nchi ya ya ahadi milele maana yake ni kwamba uzima wa milele kuwa mbinguni hauwezekani.
- "Daudi, ……. Alifariki akazikwa …. Daudi hakupanda kwenda mbinguni" (Mdo. 2:29,34). Badala yake, Petro alielezwa kwamba tumaini lake lilikuwa ni ufufuo toka wafu Kristo akirudi (Mdo. 2: 22 -36).
- Dunia ni uwanja wa shughuli za Mungu kwa watu: "Mbingu ni mbingu za Bwana, bali nchi amewapa wanadamu" (Zab. 115:16).
- Ufunuo 5:9,10 yataja maono ya wenye haki kile watakachosema watakapo kubaliwa kwenye kiti cha hukumu: "(Kristo) umetufanya kuwa wafalme na makuhani kwa Mungu wetu. nasi tutamiliki juu ya nchi". Hii picha ya kutawala katika ufalme wa Mungu duniani inaondowa kabisa wazo lisilo dhahiri ya kwamba tutafurahi'furaha kamili' mahala fulani mbinguni.
- Unabii wa Danieli sura ya 2 na 7 zinatoa maelezo ya mambo ya mfululizo wa nguvu za utawala, ambazo mwishowe zitaingiliwa na ufalme wa Mungu Kristo akirudi. Mamlaka ya ufalme huu itakuwa "chini ya mbingu zote" nao utajaa "dunia yote" (Dan.7: 27; 2:35,44).Huu ufalme usio na mwisho "watapewa

watu, Watakatifu wake aliye juu" (Dan. 7:27); thawabu yao basi ni uzima wa milele katika ufalme huu utakao wekwa duniani, chini ya mbingu.

### 4.8 Uwajibikaji Mbele Za Mungu

Kwa kawaida ikiwa binadamu ana'nafsi isiyokufa' analazimika kuwa na maisha ya kuishi miele mahali pengine - aidha mahali pa kupewa thawabu au mahali pa kuadhibiwa. Hapa panadokezwa kwamba kila mtu ana wajibu mbele za Mungu. Kwa utofauti; tumeonyeshwa jinsi Biblia inavyofunza kuwa binadamu amefanana na wanyama, ndani yake hana kitu kisichokufa. Lakini, watu wengine wametoa tumaini la uzima wa milele katika ufalme wa Mungu. Na iwe dhahiri kuwa sio kila mtu aliyewahi kuishi atafufuliwa; kama wanyama, binadamu anaishi na kisha kufa, na kuoza katika mavumbi. Lakini kwa kuwa hukumu itawekwa na wengine wakisha hukumiwa, wengine kuzawadiwa uzima wa milele, inatubidi tusema kwamba watakuwepo aina ya watu ambao watafufuliwa ili wahukumiwe na kupewa tuzo .

Mtu ikiwa atafufuliwa au la hutegemea ikiwa anapasiwa na hukumu msingi wa hukumu yetu utakuwa vipi maarifa yetu yameitikia neno la Mungu. Kristo alieleza: -"Yeye anikataae mimi, asiyeyakubali maneno yangu anaye amhukumuye; neno hilo nililolinena ndilo litakalo mhukumu siku ya mwisho" (Yoh.12:48).Wale ambao hawajafahamu au kuelewa neno la Kristo, na hivyo hakuwa na nafasi ya kumkubali au kumkataa, hawatahesabiwa kwa hukumu. "Kwa kuwa wote waliokosa pasipo wenye sheria (ya Mungu) watapotea pasipo sheria; na wote waliokosa, wenye sheria, watahukumiwa kwa sheria (Kwa kuwa walielewa)" (Rum. 2:12). Hivyo wale ambao hawajajua matakwa ya Mungu wataangamia kama wanyama; wakati wote kwa kujua

wanavunja sheria ya Mungu wanahitajika kuhukumiwa, na kwa sababu hii watafufuliwa ili waikabili hukumu.

Mbele za Mungu "Dhambi haihesabiwi isipokuwa sheria" Dhambi ni kuvunja sheria ya (Mungu)"; " kutambua dhambi huja kwa njia ya sheria" ( Rum. 5:13; 1 Yoh. 3:4; Rum 3:20). Pasipo kujua sheria za Mungu kama zilivyofunuliwa katika neno la Mungu, "Dhambi haihesabiwi" kwa mtu, kwa sababu hii hawahukumiwi au kufufuliwa. Wale wasiojua au kuelewa neno la Mungu basi watabakia wamekufa, kama watakavyokuwa wanyama na mimea, kwa Kuwait wana nafasi moja. "Mwanadamu ….. iwapo hana akili, amefanana na wanyama wapoteao" (Zab. 49:20). "Kama kondoo wanawekwa kwenda kuzimu" (Zab. 49:14).

Ni kujua njia za Mungu ndiko kunatufanya tuwajibike mbele zake kwa ajili ya matendo yetu na kwa sababu hii ni lazima kufufuliwa na kutokea kwenye kiti cha hukumu. Basi ifahamike kwamba sio peke yao wenye haki au waliobatizwa watakaofufuliwa, bali wote walio na wajibu kwa Mungu kwa sababu ya wao kumjua. Hili ni neno la maandiko lililorudiwa mara nyingi: -

- Yohana 15:22 unaonyesha ya kwamba kujua neno kunaleta uwajibikaji: "Kama mimi (Yesu) nisingelikuja na kusema nao, wasingelikuwa na dhambi: Lakini sasa hawana udhuru kwa dhambi yao" Warumi 1:20 -21 vile vile yasema kwamba kumjua Mungu kunawafanya watu "wasiwe na udhuru".

- "Basi kila aliyesikia na kujifunza kwa Baba …..Nami (Kristo) nitamfufua siku ya mwisho" (Yoh. 6:44,45).

- Mungu tu "amejifanya haoni" matendo ya wale wasiojua kabisa njia zake.Wale wanaojua njia zake, anawaona na kutegemea kuitikia (Mdo. 17:30).

- Na mtumwa yule aliyejua mapenzi ya Bwana wake, asijiweke tayari; wala kuyatenda mapenzi yake,atapigwa sana.Naye asiyejua naye amefanya yastahiliyo mapigo, atapigwa kidogo (Yaani kwa kubaki mfu). Maana kila aliyepewa vingi, kwake huyo vitatakwa vingi, naye waliyemweka amana vitu vingi, kwake huyo watataka na zaidi" (Luk. 12:47,48) - Basi ni kiasi gani zaidi ?

- "Basi yeye ajuaye kutenda mema, wala hayatendi, kwake huyo ni dhambi" (Yak. 4:17).

- Wajibu wa Israeli mahususi kwa Mungu ndio ulikuwa unaeleza ufunuo wake kwao kuhusu Yeye mwenyewe (Amosi. 3:2 ).

- Sababu ya fundisho hili la uwajibikaji, "Ingekuwa heri kwao (wanaorudi na kugeuka toka kumfuata Mungu) wasingeliijua njia ya haki na, kuliko kuijua, kisha kuiacha ile amri takatifu waliyopewa" (2 Pet.2:21). Mafungu mengine ya maneno ni pamoja na: Yoh. 9:19; 1 Tim. 1:13;Hosea 4:14; K/Torati 1:39.

Kumjua Mungu kunatufanya kufika kwenye kiti cha hukumu, kinachofuata ni kwamba wale wasio na elimu hii hawatafufuliwa, kwa kuwa hawahitajiki kuhukumiwa, na huko kukosa kwao elimu kunawafanya wawe "kama wanyama wanaopotea" (Zab.49:20). Zipo ishara kubwa zinazoonyesha kwamba sio wote waliokuwa hai watafufliwa:-

Watu wa zamani wa taifa la Babeli "Hawatafufuka" baada ya kufa kwao kwa sababu walikuwa hawamjui Mungu wa kweli (Yer.51: 39; Isa. 43: 17).

Isaya mwenyewe alijipa moyo: "Ee BWANA, Mungu wetu wa (Israeli), mabwana wengine zaidi ya wewe wametumiliki (Yaani, Wafilisti na Wakaldayo) …..Wao wamekufa, hawataishi (tena); Wamekwisha kufariki hawatafufuka; ……… na kuupoteza ukumbusho wao umepotea" (Isa. 26: 13,14). Ona mkazo mara tatu hapa juu ya kutofufuliwa kwao: Hawataishi (tena) …… hawatafufuka na kupoteza ukumbushop wao" kwa utofauti, Israeli alikuwa na "Wafu wako (Israeli) wataishi, miili yao itafufuka (B.H.N)" (Isa. 26:19).

Akizungumzia kuhusu watu wa Mungu -Israeli, tumeambiwa ya kwamba Kristo atakaporudi, "wengi wa hao waliolala katika mavumbi ya nchi wataamka, wengine kwa uzima wa milele, wengine kwa aibu na kudharauliwa milele" (Dan. 12:2). Hivyo "Wengi" bali sio wote, Wayahudi watakaofufuliwa, kwa ajili ya wajibu wao kwa Mungu wakiwa ni watu wake walioteuliwa. kati yao wasiomjua Mungu wao wa kweli'watalala, wasiamke tena' kwa kuwa hawana uwezo kupata "Neno la Mungu" (Amosi 8:12, 14).

**SASA TUMEJIFUNZA KWAMBA: -**

**1. Kujua neno la Mungu kunafanya kuwajibika kwake.**
**2. Wanaowajibika ndio tu watafufuliwa na kuhukumiwa.**
**3. Wasiomjua Mungu wa Kweli kwa Sababu hii watabakia na hali yao ya kufa kama wanyama.**

Vidokezo vya maneno haya vinafanya pigo baya kwa kiburi cha mwanadamu kwa kile ambacho kwa kawaida tunapenda kuamini: mamilioni ya watu,pande mbili, sasa na katika historia nzima, ambao hawaijui Injili ya kweli; kwa ugumu wa akili mbaya, ambao hawawezi kuelewa ujumbe wa Biblia; watoto wadogo na wachanga ambao wamekufa kabla ya kuwa watu wakubwa vya kutosha kuifahamu Injili; makundi yote hayo yanaangukia ndani ya aina ya wale ambao hawana elimu ya kweli juu ya Mungu, na kwa hiyo hawawajibiki kwake.

Hii ina maana kwamba hawatafufuliwa, bila kuangalia nafsi ya kiroho ya wazazi wao. Hiii huenda kinyume na chembe ya kufuata mambo ya binadamu na haja zetu zote za mwili na mawazo; Lakini unyenyekevu wa kweli kuhusu neno la Mungu kwa ukweli wa mwisho,ukiwekwa pamoja na unyenyekevu wa wazo linalostahili kwa umbo letu wenyewe, litatufanya tukubali ukweli huu. upimaji ulionyooka wa ukweli anaopata mwanadamu, hata bila ya mwongozo wa Andiko, pia tumaiani la maisha yajayo haliwezi kuwapo kwa makundi yaliyotajwa hapo juu.

Hoja yetu kwa njia za Mungu katika mambo haa ni nje mno ya amri: “Lakini, ewe binadamu, U nani hata uthubutu kumhoji Mungu ?” (Rum. 9:20 - B.H.N.). Tunaweza kukubali bila kufahamu, lakini kamwe haitupasi kumshitaki Mungu kwa udhalimu au kutokuwa na haki. Kidokezo cha kwamba Mungu anaweza kuwa katika njia yoyote ya kutopenda au katika kosa kunaendeleza mtazamo wa kuogofya kwa mwenyezi Mungu, Baba na Muumba anayewatendea viumbe wake bila akili na njia isiyo haki. Taarifa ya mfalme Daudi ya kupotewa na mtoto wake katika kuisoma inasaidia; 2 Sam. 12: 15 -24 habari imetolewa jinsi Daudi alivyoomba kwa bidii kwa ajili ya mtoto wakati akiwa hai, lakini akakubali mwisho wa kifo chake kuwa kilikuwa kitokee tu: “Mtoto alipokuwa hai, nalifunga, nikalia: kwa maana nalisema, Ni

nani ajuaye kwamba Bwana atanihurumia, mtoto apate kuishi ?. Lakini sasa amekufa nifungie nini ? Je ! naweza kumrudisha tena ? ….. Hatanirudia mimi”. Naye Daudi akamfariji mkewe, mapema iwezekanavyo akawa na mtoto mwingine.

Hatimae, inabidi isemwe ya kwamba watu wengi, kwa kushika jambo hili la wajibu kwa Mungu, wanaona kuwa hawana haja kupata elimu yoyote ya kumjua zaidi kwa kadhia wanakuwa na wajibu kwake na hukumu. lakini kwa kiwango kingine yaelekea kwamba watu hawa ni tayari wana wajibu kwa Mungu, wao kufahamu elimu ya neno la Mungu lililowafanya wajue ukweli kwamba Mungu anafanya kazi katika maisha, akiwapa uhusiano wa kweli pamoja naye. Inabidi ikumbukwe ya kwamba “Mungu Ni Pendo”, naye “Hapendi mtu yeyote apotee”, na akamtoa mwanae wa pekee, ili yeyote amwaminie asipotee, bali awe na uzima wa milele” (1 Yoh. 4:8;2 Pet. 3:9; Yn. 3:16).

Heshima hii na haki ya mtu isiyoepukika inaleta majukumu ya kujibu. Lakini haya hayajakusudiwa kuwa mazito sana au ya kututaabisha; Kama kweli tunampenda Mungu, tutafahamu ya kwamba yeye katupatia wokovu sio tuzo inayofanywa bila kufikiri kwa ajili ya matendo fulani, bali kwa upande wake ni nia ya upendo kufanya yote awezayo kwa ajili ya watoto wake, kuwapa uzima wa milele na furaha, kwa kufahamu tabia na sifa ya ajabu.

Tunapokubali na kusikia wito wa Mungu kwa njia ya neno lake, tutatambua ya kwamba tunapotembea katika kusanyiko, Mungu anatuangalia kwa nguvu maalumu, kwa shauku akitafuta nguvu za kuvutika kwetu kwenye upendo wake, kuliko kutusubiri kufikia majukumu yetu. Jicho hilo la upendo kamwe haliwi mbali nasi; wala hatuwezi kusahau wala kutangua maarifa yetu kwake ili kuufurahisha mwili, kuwa huru na wajibu kwa Mungu. Badala

yake, tuweze kujifurahisha kwa tendo maalum la kuwa karibu na Mungu na hivyo tuamini ukuu wa pendo lake, tunapotafuta kumjua zaidi kuliko kidogo. Upendo wetu njia za Mungu na nia ya kuzijua, vivi hivi basi tuweze kwa usahihi zaidi kumuigiza, kuwe muhimu kuliko woga wetu kwa utakatifu wake mkuu.

## 4.9 Kuzimu

Wazo la kuzimu kwa watu wengi ni mahala pa adhabu kwa'roho zisizopatwa na kifo' za wabaya moja kwa moja baada ya kufa, au mahala pa kuteswa wale ambao watakataliwa. Ni tendo letu la kusadikisha kwamba Biblia inafundisha kuwa kuzimu ni kaburi, mahali watu wote wanakwenda wakifa.

Ni neno lisilotumika sana katika misemo ya watu, awali katika Kiebrania neno'Sheol' limetafsiriwa'hell' kwa kiingereza. kwa hiyo Biblia ya kiswahili ilipoandikwa tafsiri toka kiingereza neno liliandikwa'Kuzimu' likiwa na maana'mahala pa kuzika wafu' Leo watu wametoa habari zinazotofautiana na Biblia inavyoelezea kuhusu neno kuzimu. Biblia yetu ya kiswahili hapa Afrika Mashariki ni U.V ikiwa na maana kuwa ni tafsiri tofauti -tofauti toka Biblia mbali mbali za kiingereza ambazo ni K.J.V, R.S.V, R V n.k sasa hivi Biblia zilizopo kwa kiswahili ni U.V na Biblia habari njema kiswahili cha kisasa kwa kifupi (B.H.N) mifano michache ambayo katika Biblia hili neno'Kuzimu' limetafsiriwa'kaburi' linafanya wazo la watu wengi kutofaa kuhusu kuzimu kuwa ni mahala pa ziwa la moto na kuteswa wabaya ni: -

"E e BWANA, …….. wasio haki wanyamaze kuzimu" (Zab. 31:17).

"Bali BWANA ataikomboa nafsi yangu, atanitoa mikononi mwa kuzimu - Kaburi (Zab. 49:15) yaani nafsi ya Daudi au mwili atafufuliwa toka kaburini, au kuzimu'.

Imani ya kuwa kuzimu ni sehemu ya kuadhibiwa wabaya mahala ambapo hawawezi kuepuka haiwezi kupatana na hii; mtu mwenye haki anaweza kwenda kuzimu (Kaburini) na kutoka tena. Hosea 13:14 anathibitisha hivi: "Nitawakomboa (watu wa Mungu) na nguvu za kaburi (kuzimu); nitawaokoa na mauti" mstari huu umenukuliwa katika 1 Kor. 15: 55 unahusu ufufuo Kristo akirudi. vivyo hivyo katika maono ya ufufuo wa pili (ona somo la 5. 5) "mauti na kuzimu zikawatoa wafu waliokuwemo ndani yake" (Uf. 20:13). Tazama mfano kati ya mauti yaani, Kaburi, na kuzimu (pia ona zaburi 6:5).Maneno ya hana katika 1 Sam. 2:6 yapo wazi kabisa: "BWANA huua naye hufanya kuwa hai (Kwa njia ya ufufuo): hushusha hata kuzimuni (kaburini), tena huleta juu".Kwa kuwa'kuzimu' ni kaburi itegemewe kwamba wenye haki wataokolewa kutoka hilo kwa njia ya kufufuliwa kwao kupata uzima wa milele. Hivi inawezekana kabisa kuingia'Kuzimu' au kaburini, na baadae kuliacha kwa njia ya ufufuo. Mfano mkubwa ni huo wa Yesu, ambaye roho yake haikuachwa kuzimu, wala mwili wake haukupata kuoza' (mdo. 2:31).wa sababu alifufuliwa. Angalia usambamba kati ya'roho' ya Kristo na'mwili' wake. kama mwili wake "haukuachwa kuzimu" ni kudokezwa kuwa alikuwako huko kwa kipindi, yaani, siku tatu ambazo mwili wake ulikuwamo kaburini. Kama Kristo alikwenda'kuzimu' uwe ushahidi wa kutosha kwamba sio sehemu wanako kwenda wabaya.

Watu wote wabaya na wazuri wanakwenda'Kuzimu' yaani kaburini. Hivyo Yesu "Wakamfanyia kaburi pamoja na wabaya" (Isa. 53:9) kwa kufuatana na mstari huu, ipo mifano mingine mingi ya watu wenye haki kwenda kuzimu, yaani kaburini. Yakobo

alisema ya kwamba "nitamshukia mwanangu, nikisikitika, hata kuzimu (kaburini) …. Akamlilia" Yusufu (Mwa. 37:35).

Ni moja ya mambo ya awali ya Mungu ya kuwa adhabu kwa ajili ya dhambi ni mauti (Rum 6:23;8:13;Yakobo 1:15). Hapa kwanza tumeonyesha mauti ni hali ya kutokuwa na fahamu kabisa. Dhambi husababisha kuangamia kabisa, sio kuteswa milele (math. 21:41;22:7; Marko. 12:9; Yakobo 4:12), hakika kama watu walivyoangamia kwa gharika (Luk. 17: 27, 29), Kama waisraeli walivyokufa jangwani (1 Kor. 10:10). katika sehemu zote hizi watenda dhambi walikufa kuliko waliteswa milele. Basi haiwezekani kwamba wabaya wanaadhibiwa wakiwa na fahamu kwa mateso na kuona.

Vile vile tumeona kuwa Mungu hahesabu dhambi - au kutuweka katika taarifa ikiwa hatujui neno lake (Rum 5:13). Walio katika nafasi hii watasalia wakiwa wafu. Walio kwisha jua matwaka ya Mungu watafufuliwa na kuhukumiwa Kristo akirudi. Ikiwa wabaya adhabu wanayopata itakuwa ni kifo, kwa sababu hii ni hukumu kwa ajili ya dhambi. Kwa sababu hii baada ya kuja mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo, wataadhibiwa na kisha kufa tena, kubaki katika kifo milele. Hii itakuwa ni'Mauti ya pili' iliyosemwa katika ufu. 2:11; 20:6. Watu hawa walikuwa wamekufa mara ya kwanza, kifo cha kutokuwa na ufahamu kabisa. Watafufuliwa na kuhukumiwa Kristo akirudi, na kisha kuadhibiwa na mauti ya pili, ambayo, kama mauti yao ya kwanza, hawatakuwa na ufahamu kabisa. Hii itadumu milele.

Ni katika maana hii ya kuwa adhabu kwa ajili ya dhambi ni ya'milele', katika hiyo haitakuwa na mwisho mauti yao. Kubaki wafu milele ni adhabu isiyo na mwisho. Mfano wa Biblia kutumia aina hii ya maelezo yanapatikana katika K/Torati 11:4. Huu

unaeleza Mungu akiwaangamiza mara moja Jeshi la Farao katika Bahari ya shamu milele, maangamizi yanayoendelea ni kama hasa jeshi hili halikurudia tena kuwasumbua Israeli, "alivyowafunikiza na maji ya Bahari ya Shamu …….. alivyowaangamiza BWANA hata hivi leo".

Hata katika nyakati za awali za Agano la Kale waamini walielewa kwamba kutakuwa na ufufuo siku ya mwisho, ambapo waovu wanaowajibika watarudi kaburini. Ayu. 21:30,32 yupo wazi sana: "Kwamba mwovu …… na kuongozwa nje (Yaani kufufuliwa) katika siku ya Adhabu ….. pamoja na hayo atachukuliwa (kwenda) kaburini". Moja ya mifano ya mahubiri kuhusu kurudi kwa Kristo na hukumu inazungumzia wabaya'Kuchinjwa' mbele yake (Luk. 19: 27). Mfano huu ni shida kufaa katika wazo la wabaya wanaishi milele katika hali ya kuwa na fahamu daima wakipokea mateso. Kwa vyovyote hii itakuwa ni adhabu isiyo na maana - mateso ya milele kwa matendo ya miaka 70. Mungu haoni raha kuwaadhibu watu wabaya; basi inategemewa kuwa hatawapa adhabu isiyo na mwisho. (Ezek. 18:23, 32; 33:11; 2 Pet. 3:9).

Ufalme wa Kikristo ulioiacha imani mara nyingi unajumuisha'kuzimu' na wazo la moto na mateso. wazo hili hutofautiana vikali na mafunzo ya Biblia kuhusu kuzimu (kaburi). "Kama kondooo wamewekwa kwenda kuzimu (kaburini); na mauti itawachunga" (Zab. 49:14) inadokeza ya kuwa kaburi ni mahala pa usahaulifu kwenye utulivu. Mbali ya roho ya Kristo, au mwili kuwa kuzimu kwa siku tatu, haukuachwa uoze (Mdo. 2:31) isingewezekana kama kuzimu ni mahala pa moto.

Ezek. 32: 26- 30 inatoa picha ya mashujaa wa vita wa mataifa yaliyowazunguka, wanalala kwa amani katika makaburi

yao: “Mashujaa wao ….. walioanguka (katika vita) walioshuka kuzimu pamoja na silaha zao za vita: ambazo wameweka panga chini ya vichwa vyao ….. wamelala ….. pamoja nao washukao shimoni”Hapa tunatajiwa desturi za mashujaa kuzikwa na silaha zao na kukilaza kichwa cha maiti juu ya upanga wake. Lakini haya ni kueleza'Kuzimu’ - kaburi. Hawa watu mashujaa bado wanalala kuzimu (yaani, kaburini) ni shida kusaidia wazo la kuwa kuzimu ni sehemu ya moto.

Vitu vya mwili (kwa mfano, mapanga) kwenda sehemu moja “kuzimu” kama watu, ikionyesha kwamba kuzimu sio uwanja wa mateso ya kiroho. Hivyo Petro alimwambia mtu mwovu, “Fedha yako na ipotele mbali pamoja nawe (mdo. 8:20) Taarifa ya yaliyompata Yona yanapinga hili. Akiisha mezwa hai na samaki mkubwa, “Yona akamwomba BWANA, Mungu wake, katika tumbo la yule samaki akisema, Nalimlilia Bwana …. Katika tumbo la kuzimu naliomba” (Yona. 2:1,2).'Tumbo la kuzimu’ hili ni sambamba na hilo la nyangumi. Tumbo la nyangumi kweli palikuwa ni'mahala pa uficho’ ambayo ndiyo maana ya neno msingi'Kuzimu’ lililotafsiriwa'kaburi’ Ni wazi haikuwa ni sehemu ya moto, Yona alitoka nje ya “tumbo la kuzimu” hapo nyangumi alipomtapika. Jambo hili lililenga mbele kwenye ufufuo wa Kristo toka'kuzimu’ (kaburini) - ona Mathayo 12:40.

## MOTO ULIOELEZWA KWA MANENO YA MFANO

Walakini, Biblia mara nyingi inatumia mfano wa moto wa milele ili kuonyesha hasira ya Mungu kwa dhambi, ambayo itasababisha kuharibiwa kabisa mtenda dhambi kaburini. Sodoma iliadhibiwa na “moto wa milele” (Yuda. 7), yaani iliadhibiwa na kuangamizwa kwa sababu ya uovu wa wakazi. Leo mji umo katika maangamizi, umezama chini ya maji ya bahari ya chunvi,

haumo kwa namna yoyote katika moto sasa, ambao ni wa muhimu tukitaka kuelewa'Moto wa Milele' katika hali halisi. Vivyo hivyo Yerusalemu ilitishiwa na moto wa milele wa hasira ya Mungu, kwa ajili ya dhambi ya Israeli: "Kama hamtaki ….. basi nitawasha moto mlangoni mwake nao utaziteketeza nyumba za enzi za Yerusalemu, wala hautazima" (Yeremia 17:27). Yerusalemu ukiwa umetabiriwa kuwa mji mkuu wa ufalme ujao (Isa. 2:2 -4; zab. 48: 2), Mungu hakuwa na maana sisi tusome jinsi mstari ulivyo. majumba ya Yerusalemu yaliteketezwa hadi chini kwa moto (2 Fal. 25:9), Lakini moto ule haukuendelea milele.

Kama hivi, Mungu aliiadhibu nchi ya Edomu kwa moto ambao "Hautazimwa mchana wala usiku; moshi wake utapaa milele: tangu kizazi hadi kizazi itakuwa ukiwa; ….. bundi na kunguru watakaa huko ….. miiba itamea majumbani mwake " (Isa. 34:9 - 15) Kwa kuwa wanyama na mimea walikuwa wawepo katika nchi iliyoharibiwa ya Edomu, Lugha ya moto wa milele inabidi iwe ni kutaja hasira ya Mungu na kuteketezwa kabisa sehemu yake, kuliko kuelewa kwa maneno halisi.

Mafungu ya maneno ya Kiebrania na kiyunani yaliyotafsiriwa "milele" maana yake iliyo halisi ni "muda mrefu" Wakati mwingine huu unatajwa wakati halisi usio na mwisho kwa kuwa mkubwa, kwa mfano muda wa ufalme, lakini sio daima. Mara kwa mara hasira ya Mungu kwa dhambi ya Yerusalemu na Israeli imefananishwa na moto: "Hasira yangu na ghadhabu yangu zitamwagwa juu ya mahali hapa (Yerusalemu) …… nayo itateketea, isizimike" (Yer. 7:20; mifano mingine inajumuisha omb. 4:11 na 2 Fal. 22:17).

Moto pia umeunganika na hukumu ya Mungu kwa dhambi, hasa Kristo akirudi: "kwa maana, angalieni, siku ile inakuja,

inawaka kama tanuru; na watu wote wenye kiburi na watendao uovu, watakuwa makapi, na siku ile inayokuja itawateketeza" (Malaki. 4:1). wakati makapi au hata mwili wa binadamu, ukiungua kwa moto, unakuwa vumbi. haiwezekani kwa kitu chochote, hasa mwili wa binadamu kuungua milele. Lugha ya'moto wa milele' basi hauwezi kutajwa kuwa mateso halisi ya milele. Moto hauwezi kudumu milele kama hauna cha kuunguza. ifahamike ya kuwa'Kuzimu' nayo'inatupwa katika ziwa la moto (Ufu. 20:14). Hii inaonyesha ya kuwa kuzimu si mahala pamoja kama'Ziwa la moto' hili linamaanisha maangamizo kamili. kwa namna ya mfano wa kitabu cha ufunuo, tumeambiwa ya kwamba kaburi litaharibiwa kabisa, kwa sababu mwishoni mwa Millenia (Miaka elfu) mauti haitakuwepo tena.

**JEHANAMU**

Katika Agano Jipya yapo maneno mawili ya Kiyunani yaliyotafsiriwa "hell" - kuzimu - Kiyunani'Hades' ni maana moja na neno la Kiebrania'Sheol'. Hivyo kwa Kiebrania'shoel', kiyunani'Hades', kiingereza'hell' ndipo tukapata neno letu kwa kiswahili'Kuzimu' ambalo tumelijadili awali'Gehanamu' ni jina la shimo panapomwagwa taka ambalo lilikuwa nje ya Yerusalemu, mahala uchafu wa kutoka mjini uliunguzwa.. Shimo hili la taka taka ni mfano mmoja na mingi ya miji inayoendelea siku hizi (k.m. mlima wa moshi, ulio nje ya manila nchini Ufilipino.) likiwa ni jina maalumu la mahali - likaachwa bila kulifasiri kwa jina'Gehanamu' kuliko kutafsiri kuwa'Kuzimu''Gehanamu' ni Kiaramu sawa na Kiebrania "Ge -ben -Hinnon'. Hili lilikuwa karibu na Yerusalemu (Yoshua. 15:8). Na katika kipindi cha Kristo likawa ni dampo la taka za mji. Miili ya wahalifu waliokufa ilitupwa kwenye moto uliokuwa unawaka siku zote humo, hivyo Gehanamu ukawa ni mfano wa kuangamizwa kabisa na kukataliwa.

Tena, maana inabidi ieleweke ya kuwa kilichotupwa kwenye moto huu hakikusalia humo milele - miili ilioza na kuwa vumbi. “Mungu wetu (atakuwa) moto ulao” (Ebra. 12:29) siku ya hukumu; moto wa hasira yake kwa dhambi itawala watenda dhambi kwa kuangamia kuliko kuwaacha wameunguzwa huku bado wakiwa hai. Wakati wa hukumu za Mungu zilizopita kwa watu wake wa Israeli kwa mkono wa Wakaldayo, Gehanamu ilijawa na miili ya waliokufa ya watenda dhambi kati ya watu wake Mungu (Yer. 7:32,33).

Kwa jinsi ya uhodari Bwana Yesu aliyaweka yote mambo haya pamoja ya Agano la Kale kwa kulitumia hili neno'Gehanamu’. mara nyingi alisema ya kuwa wale wanaokataliwa kwenye kiti cha hukumu akirudi watatupwa Gehanamu (Yaani'kuzimu’), katika moto usiozimika; ambako funza wake hawafi (Marko. 9: 43, 44) Gehanamu iliweza kufikirishwa katika akili ya Wayahudi mambo ya kukataliwa na kuharibiwa mwili, tumeona kuwa moto wa milele ni neno lililotumika kwa namna ya kawaida linaloonyesha hasira ya Mungu juu ya dhambi, na kuwaangamiza wabaya kwa mauti.

Katika kutaja “ambamo funza hawafi”, ni dhahiri sehemu ya msemo usiotumika kwa namna ya kawaida ikiwa ni mamoja na kuangamiza kabisa - haidhaniwi kuwa kunaweza kuwepo funza halisi ambao hawatakufa. Ukweli ni kwamba Gehanamu palikuwa ni sehemu ya adhabu zilizopita kwa wabaya miongoni mwa watu wa Mungu, Zaidi ya hayo Kristo anaonyesha namna ijayo kutumia mfano huu wa Gehanamu.

*Tumeacha kitambo sehemu ya 11: Purgatory*

## TOHARANI - MAHALI AMBAPO ROHO ZA WALIOHAKI HUISHI

**Purgatory: Mahala pa ahera pa kusafisha dhambi ndogo.**

Kanisa la katoliki la Roma linafundisha ya kuwa roho za watu wa Mungu zaweza kwenda mahala paitwapo'Purgatory (toharani) baada ya kufa, ambapo ni nyumba iliyopo katikati ya'Mbinguni' na'kuzimu'. wanafundisha kuwa ni mahali pa kutakasia ambapo roho itaona maumivu kwa muda kidogo kabla ya kufaa kupata wokovu mbinguni. Maombi, kuwasha mshumaa na kutoa fedha kwenye kanisa mtu na rafiki zake imedhaniwa huweza kupunguza muda ambao roho inaweza kupata machungu katika'Purgatory' (Toharani) kosa kubwa la mawazo haya linawekwa kutokana na ifuatavyo:-

- Biblia ipo kimya kuhusiana na uwepo wa sehemu hii.

- Tumeonyesha kuwa roho /nafsi unatajwa mwili wetu, sio kitu fulani kisichokufa ndani yetu, na ya kuwa'Kuzimu' ni kaburi sio mahala pa kuadhibiwa.

- Wenye haki kamwe hawajaahidiwa wokovu mbinguni. kupewa wokovu itakuwa kwenye kiti cha hukumu cha Kristo akirudi, sio wakati mwingine baada ya kufa hapo idhaniwapo kuondoka katika'Purgatory' (Toharani) (Math. 25:31 -34; Ufu.22:12).

- Wote wenye haki wapokea tuzo kwa wakati mmoja, sio kila mtu hupata wokovu kwenye nyakati tofauti (Ebra. 11:39,40;2 Tim. 4:8).

- Kinachofuatiwa na kifo ni ukimya kabisa wa kutokuwa na fahamu, sio shughuli zilizodokezwa kwa mafundisho ya Purgatory. (Toharani).

- Tunatakaswa dhambi zetu kwa njia ya Ubatizo katika Kristo na kuendelea katika imani thabiti kwa kufanya matendo yake wakati wa maisha yetu ya sasa, sio kupitia kipindi kingine kuteswa baada ya kufa. tunaambiwa'Jisafisheni, mkatoe ile chachu ya kale' ya dhambi katika maisha yetu (1 Kor. 5:7); tujitakase toka katika matendo yetu ya dhambi (2 Tim. 2:21; Ebra. 9:14).

Basi muda wetu wa kujisafisha ni sasa, katika maisha haya, sio mahala pa kutakasa ('Purgatory') (Toharani) ambayo tunaingia baada ya kufa. Wakati uliokubalika ndio sasa …… Siku ya wokovu ndio sasa" (2 Kor. 6:2). Tunapo mtii Mungu kwa ubatizo na kuendeleza tabia ya kiroho katika Maisha haya tutaongozwa kupata wokovu wetu (Gal. 6:8) - sio kutumia muda katika'Purgatory' (Toharani).

- Juhudi ya wengine kutuokoa kwa kuwasha mishumaa na michango mingine ya pesa kwa kanisa la katoliki, haita geuza wokovu wetu kabisa. " Hao wanaozitumainia mali zao …… hakuna mtu waezaye kumkomboa ndugu yake, wala kumpa Mungu fidia kwa ajili yake ….. ili aishi siku zote asilione kaburi" (Zab. 49: 6-9).

***Tumeacha kitambo sehemu ya 12: Roho na mafunzo ya kuwa huingia kwenye mwili mwingine***

Imani ya kuwa Binadamu anaendelea kuishi katika umbo la mtu mwingine au la mnyama akiwa ana roho yake, likuwa ni moja ya njia ya zamani ambazo binadamu alijaribu kujisadikisha mwenyewe kuwa kifo hakikuwa ndio mwisho kilipotokea. Tumeeleza kuwa roho ya binadamu inatajwa pumzi /nguvu ya kuwa hai iliyo ndani yake, ambayo humrudia mungu anapokufa (Mhubiri 12:7). Hii ina maana kwamba roho yake haihami na kuzunguka ikiwa ni'Mzuka', wala ipo huru kuwa na mtu mwingine au mnyama hivyo basi utu wa mtu unaendelea katika wao. Kila mmoja tutahukumiwa kwa matendo yetu wenyewe (2Kor. 5:10). Ikiwa sifa na tunayotenda ni tabia inayotenda kazi ya mtu mwingine aliyepita, basi hili wazo la Mungu kuhukumu na kutupa tuzo kulingana na kazi zetu (uf. 22:12) halina maana.

Mtu anapokufa roho humrudia Mungu, fahamu zote zinakoma. Jaribio lolote la kukutana na wafu basi linaonyesha kutofahamu mno fundisho kubwa la Biblia kuhusu hili (tazama Isa. 8:19,20).Biblia ipo wazi kabisa kuwa watu hawazirudii nyumba zao za kwanza au miji kwa namna yoyote baada ya kufa; hakuna kitu kama'roho' au'kizuka' kurudia mahali hapa mtu akiwa amekufa: " (Binadamu) ataangamia milele kama mavi yake mwenyewe: hao waliomwona watasema yupo wapi ? ….. hataonekana. Jicho lililomwona halitamwona tena; wala mahali pake (nyumba /mji) hapata mtazama tena" Ayubu. 7:9,10 ni kama huu: "Huyo ashukaye kuzimuni ….. hatarudi tena nyumbani kwake, wala mahali pake hapatamjua tena" Kukubali hili kwa unyenyekevu litatuongoza kubadilisha madai yote kuwa tumeona'mizuka' ya watu waliokufa, wakirudi nyumba zao za

zamani. mambo haya inabidi yawe ni udanganyifu wa mawazo ya kuwaza mambo asiyoona.

***Tumeacha kitambo sehemu ya 13: Kwa mwili upi tunafufuliwa***

Tumeonyesha kwamba uzima wa milele na kubadilika kuwa na mwili wa Uungu utatolewa na kupewa waaminifu baada ya hukumu. Kwanza Kristo atawafufua walio na wajibu kwake; na kisha kuwahukumu baada ya kuwa wamekusanyika kwake kwa kuwa mwili usiokufa watapewa kwenye hukumu, kinachofuata ni kwamba wote waliofufuliwa kwanza wanakuwa na mwili unaokufa. kama wamefufuliwa wakiwa na miili isiyokufa, basi hakuna sababu ya kiti cha hukumu ambako thawabu zitatolewa.

Tunaingia ufalme wa Mungu moja kwa moja baada ya kiti cha hukumu (Math. 25:34); basi waaminifu hawawi katika ufalme wa Mungu kabla ya hukumu. "Nyama na damu haziwezi kurithi ufalme wa Mungu (basi) …. Lakini sote tutabadilika …. Maana sharti huu uharibikao uvae kutoharibika, nao huu wa kufa uvae kutokufa" (1Kor. 15: 50,51, 53). kifuatacho ni kuwa badiliko hili la mwili, toka kufa hadi kutokufa, linatolewa kwenye kiti cha hukumu, kwa kuwa ndipo tunaingia ufalme.

Walakini, mtume Paulo mvuviwa mara nyingi anataja "Ufufuo" katika maana ya "kufufuliwa uhai" - ufufuo wa wenye haki kisha watapata uzima wa milele baada ya hukumu. kwa kweli alifahamu "kuwa kutakuwa na ufufuo wa wafu, wenye haki na wasio na haki" (Mdo. 24: 15).alikuwa anajua ya kwamba wenye wajibu "Watatoka (makaburini); Waliofanya mema, kwa ufufuo wa kupewa uzima; na walio fanya mabaya, kwa ufufuo wa hukumu" (Yoh. 5:29).

Kwa njia ya kufaa, Paulo anaonekana mara nyingi alikuwa akitaja'Kurudishiwa uhai' anapozungumzia “ufufuo”. wenye haki wanatoka makaburini mwao “kwa ufufuo wa uzima “ baada ya kutoka mavumbini watahukumiwa na kisha kupewa uzima wa milele. Huu mlolongo mzima ni “kurudi kwenye uhai” ipo tofauti yao, “ kutoka nje” ya kaburi, na “ufufuo wa uzima” Paulo anataja juhudi yake ya kuishi maisha ya Kikristo, “ili nipate kwa njia yoyote kuifikia kiama ya wafu - yaani ufufuo wa wafu” (Fl. 3:11). Kwa sababu alikuwa na wajibu atafufuliwa atoe hesabu kwenye hukumu kwa vyovyote; alifanya bidii “ili afike kwenye ufufuo inabidi kuwa na maana kuwa “ufufuo” anaoutaja hapa ni “kurudishwa uhai”.

Mifano mingine ya “ufufuo” ikiwa na maana ya “kurudi kwa uhai” (Luk. 14:14) pamoja na Luka 20: 35; Yn. 11:24; 1 kor. 15:21, 42; Ebra. 11:35; uf. 20:6. katika Zab. 17:15 Daudi anazungumzia kupokea thawabu yake mara “akiamshwa”. Alikuwa na mtazamo ule ule wa kufufuka, ingawa alijua kutakuwa na hukumu. kutumia fungu hili la maneno “ufufuo” kama hili katika 1 kor. 15 linasaidia kuelezea 1 Kor. 15:52 - “ wafu watafufuliwa wasiwe na uharibifu” Fungu la maneno “wafu” linastahili kuangaliwa mara nyingine (na hasa katika 1 Kor. 15) linataja wafu wenye haki, ambao watafufuliwa kuupokea uzima wa milele kwenye hukumu: 1 Kor. 15:13,21, 35,42; 1 Thes. 4: 16; Flp.. 3:11; Uf. 14: 13: 20: 5, 6 1 The 4: 16,17 imeorodhesha orodha ya matukio yanayounganishwa kurudi kwa Kristo.

1. **Kristo kwa kuonekana amerudi**
2. **Wafu wamefufuliwa**
3. **Wanao wajibu ambao wapo hai wakati huo watanyakuliwa kwenda kwenye hukumu.**

Kupewa uzima wa milele ni baada ya kukusanywa huku pamoja (Math. 25: 31 - 34; 13: 41 -43); kwa hiyo kutokufa hakutolewi wakati wa kufufuka, kwa kuwa hii inatangulia kukusanyika pamoja. tumeonyesha ya kwamba wote wenye haki watapewa thawabu kwa wakati ule ule (Math. 25:34; Ebra. 11:39 - 40). hii haiwezekani ikiwa kutokufa wanapewa wakati wa kufufuka, kwa sababu baada ya ufufuo hufuata kukusanywa pamoja walio hai wenye jambo la kujibu.

Walakini, ijulikane kuwa wazo letu la wakati ni la kibinadamu sana; Mungu hafungwi nao kabisa. inawezekana kwenda mbali zaidi katika kujaribu kutimiza kuandika tarehe dhahiri ya matukio yatakayotokea karibu na wakati wa kurudi Kristo. Kufufuka na kubadilishwa kwetu na kupata kutoharibika kwenye kiti cha hukumu kumeelezewa kuwa kunatokea “Kwa dakika moja, kufumba na kufumbua jicho” (1Kor. 15:51,53).Kwa ulazima, muda utakwenda na mzunguko tofauti wakati wa kurudi Kristo, hasa kwa watakao hukumiwa. ni jambo kuu la Biblia kuwa kila atakaye paswa kujibu kwenye hukumu watatoa hakimu ya maisha yao mbele ya kiti cha hukumu, kutakuwepo kiwango fulani cha majadiliano na mwamuzi - hakimu wao, Bwana Yesu Kristo (Math. 25:44 n.k; mhub. 3:17; 12:14; Luk. 12:2, 3; 19:23;Ezek. 18: 21, 22; 1Tim 5:24, 25; Rum. 14: 11,12). Tumepewa idadi kubwa ya mambo ya kujibu, inatupasa tusadiki kuwa maana ya muda utazuiwa au kwa uwingi utabanwa ili sote tuhukumiwe haraka, lakini pia mmoja mmoja. kwa sababu muda utabanwa kwenye hatua hii ili kwamba mlolongo mzima wa hukumu na ufufuo utokee “ Kwa dakika, kufumba na kufumbua jicho” inaeleweka kwamba ufufuo mara nyingine uliosemwa ni njia ambayo wenye haki watapewa uzima wa milele.

Ingawa hivyo hii ni kwa sababu ya kasi tutakayohamishwa toka kaburini hata kwenye kiti cha hukumu, na kisha, kwa neema ya Mungu, kupewa kutoharibika. ukweli bado umesalia toka mistari tuliyojadili awali, kuwa Biblia inafunza kwamba uzima wa milele utatolewa kwenye kiti cha hukumu sio kwenye ufufuo. Kwa sababu hii 1 Thes. 4:17 husemwa wenye haki wataitwa kwenda kwenye hukumu kwa mlio wa parapanda, wakati 1 Kor. 15:52 unazungumzia parapanda hiyo hiyo ikiwa imeunganishwa na wao kupewa kutokufa. Hii pia yaeleza ni kwa nini Paulo aliufikiria ufufuo ni ule ule wa kukubalika mbele ya kiti cha hukumu (k.m Flp. 1:23).

***Tumeacha kitambo sehemu ya 14: Kunyakuliwa***

Kuna imani iliyoenea pote miongoni mwa makanisa ya "kiinjili ya kuwa wenye haki'Watanyakuliwa' kwenda juu mbinguni Kristo akirudi. Hii imani mara nyingi imeungwa na wazo la kuwa s dunia wakati huo itateketea kwa moto. Tumeona katika kitambo tulichokuwa tunaandika sehemu ya 9 kwamba haiwezekani. Tumeonyesha pia katika somo la 4. 7 sehemu ya kupewa thawabu ni hapa duniani, sio mbinguni. Makosa ya imani hizi msingi wake upo kuzunguka tafsiri inayokosewa ya 1 Thes. 4:16, 17; "Bwana mwenyewe atashuka toka mbinguni ….. nao waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza; kisha sisi tulio hai, tuliosalia, tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu, ili tumlaki Bwana hewani; na hivyo tutakuwa na Bwana milele.

Mbali toka hatari dhahiri ya kuweka imani kubwa hii juu ya fungu moja tu la maandiko, ijulikane kuwa hapa hakuna palipotajwa wenye haki kunyakuliwa kwenda mbinguni. Kristo anashuka toka mbinguni kabla ya wakristo kukutana naye. Kristo atamiliki milele juu ya kiti cha enzi cha Daudi katika mji wa

Yerusalemu,tutakuwa pamoja naye, hapa duniani, kwa hiyo haiwezekani kwamba tutaishi milele pamoja naye tumening'inia kati kati ya hewa.'Hewa' imeenea kilomita chache juu ya uso wa dunia. maana yake ni kuwa hapatajwi mbinguni makao ya Mungu.

Fungu la maneno katika sentensi ya Kiyunani lililotafsiriwa "kunyakua" hasa maana yake kukamata upesi ili kutenga; halilengi mwelekeo wowote ulio wazi. Katika Biblia ya Kiyunani Agano la Kale linatokea katika Law. 6:4 na K/Torati 28: 31 (Septugint) kuelezea'kutengana na' au kupokonya mali kwa nguvu, hivyo ni kunyakua kama mkoba wa mtu kwa nguvu. Vile vile neno hili limetokea katika matendo ya Mituma 8: 39: "Roho wa Bwana akamnyakua Filipo, yule towashi asimwone tena ……. Lakini Filipo akaonekana katika Azoto" Hapa taarifa inaelezea jinsi Filipo alivyosafirishwa kwa muujiza toka sehemu moja ya dunia kwenda sehemu nyingine.

Kristo ajapo, wale wanaopaswa kujibu mbele zake watakusanywa pamoja sehemu ya hukumu; hawataachwa wafanye safari peke yao. inawezekana njia ya kusafirishwa sisi hadi sehemu hiyo hasa itakuwa kupitia hewani.

Yesu alisema ya kuwa "Siku ambayo mwana wa Adamu atakayofunuliwa ….. watu wawili watakuwa kondeni; mmoja atwaliwa mwingine ataachwa" (Luk. 17:30,36). Hapa tumepewa picha ile ile ya kuhamishwa ghafla. Wanafunzi kwa bidii waliuliza, "Wapi, Bwana ? Naye akawaambia, Ulipo mzoga, ndipo watakapokutanika tai" (Luk. 17: 37). Kama tai arukavyo kwa akili yake kupitia hewani na kisha kutua juu ya nchi ulipo mzoga, basi wanaopaswa kwenda kutoa hesabu wataletwa hadi sehemu watakayokutana na Bwana wao kwa hukumu.

Yatupasa tena tutie mkazo ya mafunzo ya hukumu mbele ya kiti cha Kristo; wanaowajibika yawapasa kwanza kufika hapo, kabla wenye haki miongoni mwao kupewa tuzo. kusoma kijuu juu 1Thes. 4:16,17 kunaweza kutupeleka kusema kuwa wote wanaopaswa na hiyo hukumu watanyakuliwa hewani, na kusalia huko na Kristo milele. Badala yake, tunajua ya kuwa walio na wajibu watakusanywa sehemu ya hukumu, yawezekana kwa kusafirishwa kupitia hewani, na kisha kupokea thawabu zao.

**Somo La 4: Maswali**

1. Ni nini kinatokea baada ya kufa ?
a) Roho inakwenda mbinguni
b) Tunakuwa hatuna fahamu
c) Roho inatunzwa mahali fulani hata siku ya hukumu
d) Roho mbaya zinakwenda kuzimu na nzuri kwenda mbinguni.
2. Nafsi ni kitu gani ?
a) Sehemu isiyokufa ya utu wetu
b) Ni neno lenye maana "Mwili, Mtu,kiumbe"
c) Ni maana moja na roho
d) Kitu fulani kinachokwenda mbinguni au kuzimu baada ya kufa.
3. Roho ya binadamu ni nini ?
4. Kwa kifupi elezea mwili wa binadamu
5. Andika orodha ya mistari miwli inayothibitisha kuwa mauti ni hali ya kutokuwa na fahamu
6. Unajua kitu gani kuhusu kiti cha hukumu cha Kristo
7. Ni nani watakao fufuliwa na kuhukumiwa
8. Kuzimu ni nini ?

9. Gehanamu ni nini ?

# *SOMO LA 5*

# UFALME WA MUNGU

## 5.1 Kuelezea wazi kabisa Kuhusu Ufalme

Masomo yetu yaliyotangulia yameonyesha kuwa ni kusudi la Mungu kuwapa tuzo watu wake waaminifu kwa uzima wa milele Kristo akirudi. Uzima huu wa milele utatumiwa duniani; Ahadi za Mungu zilizorudiwa kuhusu hii kamwe haidokezi kuwa waaminifu watakwenda mbinguni."Injili ( habari njema) ya ufalme wa Mungu"(Math. 4:23) ilihubiriwa kwa Abrahamu kwa namna ya ahadi za Mungu kuhusu uzima wa milele duniani (Gal. 3:8) Kwa hiyo"Ufalme wa Mungu utakuwa wakati baada ya Kristo kurudi ndipo hizi ahadi zitatimizwa. Wakati Mungu ni mfalme wa Mwisho juu ya viumbe vyote vya sasa, amempa binadamu hiari ya kufanya apendavyo kutawala ulimwengu na maisha yake mwenyewe kama atakavyo. hivyo kwa sasa ulimwengu umekuwa ni "Ufalme wa mwanadamu" (Dan. 4:17).

Kristo akirudi,"ufalme wa dunia hii utakuwa ufalme wa Bwana wetu, na Kristo wake naye atamiliki hata milele na milele"(uf. 11:15) Ndipo mapenzi ya Mungu na nia itatimizwa wazi wazi na kufanywa katika dunia hii. Basi, Yesu ametuamuru tuombe;"Ufalme wako uje (ili) mapenzi yatimizwe hapa duniani kama (sasa) yanavyotimizwa huko mbinguni"(Math. 6:10). Kwa sababu hii fungu la maneno "Ufalme wa Mungu"limebadilishana na "Ufalme wa mbinguni"(Math 13:11; Marko.4:11). kumbuka kuwa hatusomi'Ufalme katika mbingu'; ni ufalme wa mbinguni ambao utawekwa na Kristo duniani akirudi kama malaika wanavyotii kwa ukamilifu mapenzi ya Mungu (Zab. 103: 19 -21), ndivyo itakavyokuwa kwenye ufalme ujao wa Mungu, dunia itakapo kaliwa na wenye haki pekee, ambao wakati huo watakuwa "Sawa na Malaika" (Luk. 20:36) .

Kuingia Ufalme wa Mungu Kristo akirudi basi ni mwisho wa matokeo ya juhudi yetu yote ya Ukristo wa maisha haya (Math. 25: 34; Mdo. 14: 22); kama hivi; ni muhimu kuelewa kwa usahihi. Filipo akihubiri habari za "Kristo"imefafanuliwa akifundisha "Mambo yanayohusu Ufalme wa Mungu na jina la Yesu Kristo (Mdo 8:5,12). Mafungu ya maneno juu ya mafungu ya maneno yanatukumbusha jinsi ufalme wa Mungu ulikuwa ni mzigo mkubwa wa mahubiri ya Paulo (Mdo. 19: 8; 20:25; 28:23, 31). Kwa hiyo ni wenye maana kuu muhimu kuwa tunaelewa vya kutosha fundisho la ufalme wa Mungu, kwa kuwa ni sehemu ya muhimu kwa ujumbe wa Injili"Imetupasa kuingia katika ufalme wa Mungu kwa njia ya dhiki nyingi"(Mdo. 14:22); ni nuru mwishoni mwa shimo la kupita chini ya maisha haya, na kwa hiyo kusudi la kutengeneza dhabihu ambayo maisha ya kweli ya Kristo imo.

Nebukadneza , Mfalme wa Babeli, akataka kujua mambo ya ulimwengu ujao (ona Dan. 2). Alipewa ndoto ya sanamu kubwa ya

mtu, ameundwa kwa vyuma tofauti. Danieli alitoa tafsiri ya kichwa cha dhahabu kuonyesha mfalme wa Babeli (Dan. 2:38). baada yake yalikuja madola yaliyofuatana katika eneo karibu na Israeli na kumalizika na hali ambayo "Kama vidole vya zile nyayo vilikuwa nusu chuma na nusu udongo, kadhalika ufalme ule utakuwa nusu yake una nguvu na nusu yake umevunjika"
(Dan. 2:42).

Uwiano wa nguvu uliopo katika ulimwengu umegawanyika kati ya mataifa mengi, mengine ni yenye nguvu na mengine ni dhaifu. ndipo Danieli aliona jiwe dogo likiipiga sanamu kwenye nyayo, likahiaribu, nalo likakua na kuwa mlima mkubwa uliojaa dunia nzima (Dan 2: 34,35). Hili jiwe lina maana Yesu u (Math. 21:42; Mdo.4:11; Ef. 2:20; 1Pet. 2:4 -8)."Mlima" atakao ufanya uwe juu ya dunia yote ni ufalme usio na mwisho wa Mungu, utakao wekwa atakapo kuja mara ya pili.Unabii huu ni ushahidi Kuwait ufalme utakuwa duniani, sio mbinguni.

Kama ufalme utasimamishwa tu katika kweli kabisa Kristo akirudi ni msemo wa mafungu mengine.Paulo anasema Yesu akihukumu walio hai na wafu "atakapofunuliwa na ufalme wake" (2Tim. 4:1). Mika 4:1 anachukua wazo la ufalme wa Mungu kuwa kama mlima mkubwa; "Lakini itakuwa katika siku za Mwisho, ya kwamba mlima wa nyumba ya Bwana utawekwa imara juu ya mlima, nao utainuliwa juu"; Kisha hapo yanafuata maelezo jinsi huu ufalme utakavyokuwa Duniani (Mika. 4:1 -4). Mungu atampa Yesu kiti cha enzi cha Daudi kilichokuwa Yerusalemu:"Atamiliki ……. Hata milele, na ufalme wake hautakuwa na mwisho"(Luk. 1:32,33). Hii inawezesha maana yakini ambayo Yesu anaanza kutawala kiti cha enzi cha Daudi, na ufalme unaanza. Huu utakuwa Yesu akirudi."Ufalme wake hautakuwa na mwisho"imeunganika na Danieli 2: 44: "Mungu wa mbinguni

atausimamisha  ufalme ambao hautaharibiwa kamwe:  hautaachwa kwa watu wengine" Uf. 11:15 imetumika  Lugha kama hii ikielezea jinsi akirudi mara ya pili,"Falme za ulimwengu zinakuwa falme za Bwana wetu na za Kristo wake, naye atamiliki milele na hata milele"Tena, inabidi uwepo wakati dhahiri hapo ufalme wa Kristo na utawala unapoanza duniani; huu utakuwa akirudi .

## 5.2 Kwa Sasa Ufalme Haujasimikwa

Kwa upana kuna wazo  limeshikwa ya kuwa ufalme wa Mungu sasa upo kwa ukamilifu, ukiwa unawaamini waliopo - 'Kanisa'. Wakati katika matumaini waamini wa kweli 'Wameokolewa' na kupewa  nafasi za kuweza kuwa  katika ufalme, Hapawezi kuwepo shaka  kuwa sasa hatuwezi kikamilifu kuwamo katika ufalme, kwa  kuwa  Kristo bado hajarudi kuusimika.

Hakuwa dhahiri kutokana na kile tulichojifunza mpaka  hapo "yakuwa nyama na damu haviwezi kuurithi ufalme wa Mungu"(1Kor. 15:50). Sisi"tu warithi wa ufalme  ambao ameuahidi kwa hao wampendao" (Yakobo 2:5), kwa kuwa ubatizo unatufanya  tuwe warithi wa Ahadi alizoahidiwa  Abrahamu -ahadi zenye msingi wa Injili ya ufalme (Math. 4:23;  Gal. 3:8,27 -29). kwa hiyo ni kawaida kuja katikati ya kurithi ufalme Kristo akirudi, wakati ahadi alizoahidiwa  Abrahamu zitakapotimizwa  (Math. 25:34; 1Kor. 6:9,10; 15,50; Gal. 5:21; Efe. 5:5).Matumizi kabisa ya Lugha  ya urithi ujao yaonyeshwa ya kwamba  ufalme  sio miliki ya waamini waliopo sasa .

Yesu akawaambia mfano wa kuwasahihisha  wale waliodhani "kuwa Ufalme wa Mungu"utaonekana mara. Basi aliwaambia, mtu mmoja , kabaila, alisafiri kwenda nchi ya mbali,  ili ajipatie ufalme

na kurudi"Na wakati ule ule aliwaacha watumwa wake wakiwa na majukumu fulani ya kufanya. Ikawa aliporudi, ameupata ufalme wake , aliamuru waitwe wale watumwa"akafanya uamuzi nao (Luka. 19:11 -27).

Kabaila ni Kristo aliyekwenda "nchi ya mbali" ya mbinguni kuupokea ufalme, ambao anarudi nao wakati wa hukumu, Yaani kuja mara ya pili. Kwa hiyo haiwezekani kuwa "Watumwa"wawe na ufalme hivi sasa, kipindi ambacho Bwana wao hayupo.

Yafuatayo yanatoa ushahidi huu zaidi:-

- “ufalme wangu sio wa (wakati) ulimwengu huu”, Yesu amesema wazi (Yoh. 18:36). Ingawa hivyo, hata wakati alipoweza kusema ,"Mimi ni mfalme"(Yoh. 18:37), alikuwa ana maana ya kuwa 'Ufalme’ wa Kristo uliopo hana maana kuwa ufalme wake kwa sasa umesimikwa. Hata waaminifu wa Karne ya kwanza wamesema kuwa WANAUTAZAMIA "Ufalme wa Mungu"(Mark. 15:43).

- Kristo aliwaambia wafuasi wake kuwa hatakunywa kabisa tangu sasa uzao huo wa mzabibu, "Hata siku ile nitakapokunywa mpya pamoja nanyi katika ufalme wa Baba yangu"(Math. 26:29). Hii ni wazi inadokeza kwamba ufalme utakuwa wakati ujao, ndivyo watu walivyoelewa mahubiri ya Kristo ya"habari njema (Yaani, tangazo lililosogezwa mbele) ya ufalme wa Mungu"(Luk. 8:1)"Heri yule atakayekula mkate katika ufalme (wakati ujao) wa Mungu”,lilikuwa elezo lao (Luk. 14:15).

- Luka.22:29,30 yaendeleza msemo huu ,"Nami nawawekea ninyi ufalme: mpate kula na kunywa mezani pangu katika ufalme wangu”.

- Yesu alieleza ishara zitakazo ashiria kuja kwake mara ya pili, na kumalizia kwa habari."Ninyi kadharika, mwonapo mambo haya yanaanza kutokea, tambueni ya kwamba ufalme wa Mungu U karibu"(Luk. 21:31). Hii haina maana kama ufalme kwa sasa umekuwepo kabla ya kuja mara ya pili.

- "Imetupasa kuingia katika ufalme wa Mungu kwa njia ya dhiki nyingi"(mdo. 14: 22). sio ajabu mwamini anayeteseka anaomba kwa bidii ufalme uje (Math 6:10).

- Mungu "amewaita ninyi ili mwingie katika ufalme wake"(1Thes. 2:12); kwa kuitikia tutake kuingia ufalme huo kwa maisha ya kiroho sasa (Math. 6:33)

**UFALME WA MUNGU UMO NDANI YENU ?**

Mbali ya mkazo huu wote mkubwa kidogo, 'Wakristo' wengi wa orthodox huchagua kuweka imani yao kuwa sasa ufalme umo mioyoni mwa waumini , juu ya fungu moja la maneno: "Ufalme wa Mungu umo (mioyoni) ndani yenu"(Lk. 17: 21). Hii kwa usahihi zaidi imetafsiriwa"Ufalme wa Mungu umo mioyoni mwenu (katika Biblia ya Kiingereza ya A. V). Biblia ya kiswahili cha kisasa - B.H.N - mstari umeandikwa"Ufalme wa Mungu umo kati yenu". Mstari unaonyesha ya kuwa Yesu alikuwa akizungumza na Mafarisayo (mst. 20); neno"Yenu"basi alikuwa akiwataja wao. Kwa hakika hawakuwa ni waamini wa Kristo - Ufalme wa Mungu haukuwekwa mioyoni mwao.Wayahudi walikuwa wakijionyesha kwa watu kuwa walikuwa na juhudi ya kumtazamia masihi.

Kwa fungu hili la maneno,"Ufalme wa Mungu" laonyesha kuwa ni jina la masihi, wakiona atakuwa mfalme wa wafalme. Hivi

Yesu alipoingia Yerusalemu , watu walishangilia,"Ndiye mbarikiwa (masihi) ajaye kwa jina la Bwana: umebarikiwa na ufalme ujao, wa Baba yetu Daudi"(Marko. 11:9,10). Hii inasawazisha masihi na 'Ufalme' Naye Yohana mbatizaji alihubiri kuwa "Ufalme wa Mungu umekaribia. Maana huyu ndiye (Yesu) aliyenenwa na Nabii". (Math. 3: 2,3). Kwa fungu letu la maneno lililokatika Luka 17: 20 -24, Yesu alijibu swali lao lililohusu lini 'Ufalme wako utakapokuja' kwa kusema kuhusu kuja kwa "Mwana wa Adamu".

Maana ya Yesu ilikuwa kwamba Wayahudi walikuwa wanajionyesha sana kuwa walikuwa wakimtazamia masihi aje , wakitegemea atadhihirika katika nguvu, wakashindwa kutambua kwamba masihi -"Ufalme wa Mungu"- tayari ulikuwa kati yao katika mtu mpole Yesu. Hivyo akawaonya:"ufalme wa Mungu (masihi) hauji kwa kujionyesha …….. tazama, Ufalme wa Mungu uko kati yenu" (Luk. 17: 20,21).

### 5.3 Ufalme wa Mungu uliopita

Ufalme wa Mungu ujao ni thawabu ya waaminio, Ikiwa hii , ni kusudi lao kuishi maisha ya kujitoa kuiga mfano wa Kristo - jambo fulani linalohusishwa maumivu ya muhula mfupi pamoja na kutokuwa na faraja. kwa hiyo inategemewa kuwa siku zao zote zitatumiwa na nia kubwa inayoongezeka kushukuru na kuelewa ajabu za enzi ijayo. Itakuwa ni nyongeza ya jitihada zao zote kiroho, na azimio kamili kwa Mungu ambaye wamependa akiwa ni Baba yao.

Maandiko yamejaa tele na maelezo jinsi ufalme utakavyokuwa, na utakuta ni kazi ya muda ya maisha kuvumbua

baadhi yake. Njia moja inayoweza kutuletea kuelewa mambo mengine makuu ya msingi ya ufalme huu ujao ni kukubali kuwa ufalme wa Mungu uliwahi kuwepo zamani kwa namna ya taifa la Israeli. Ufalme huu utaanzishwa tena Kristo akirudi. Mengi ya Biblia yanatupatia habari kuhusu taifa la Israeli, ili tuelewe kwa maelezo marefu, jinsi ufalme wa Mungu ujao utakavyotengenezwa. Mara nyingi Mungu amejieleza kuwa Yeye ni "Mfalme wa Israeli" (Isa. 44: 6 ml. Isa. 41: 27; 43: 15; Zab.48:2; 89:18; 149:2); kinachofuata ni kwamba watu wa Israeli walikuwa ni ufalme wake, walianza kuwa ufalme wa Mungu kwa kuingia katika Agano naye chini ya mlima Sinai, muda mfupi walipotoka Misri kwa kupitia Bahari ya Shamu.

Kwa kuitikia kwa hiari yao kutunza Agano hili, watakuwa "Kwa (Mungu) ufalme …… na taifa takatifu"(Kut. 19:5,6). Hivyo,"Israeli alipotoka Misri …. Israeli (alikuwa) miliki yake" au ufalme (Zab. 114:1,2).Baada ya kuingia katika mkataba huu, Israeli akasafiri kupitia jangwa la Sinai na akaja kuweka makao katika nchi ya Ahadi -Kanaani. Mungu akiwa ni mfalme wao, mambo yao yaliamliwa na"Waamuzi"(K.m Gideon na Samsoni) sio wafalme. Hawa waamuzi hawakuwa wafalme, bali waliongozwa na wasimamizi wa Mungu wakiwa magavana wa sehemu moja ya nchi sio kutawala nchi yote. Mara nyingi waliinuliwa na Mungu kwa dhumni maalumu. k.m kuongoza wana - Israeli kutubu na kuwaokoa toka maadui wao. Wana Israeli walipomwuliza mwamuzi Gideoni ili awe mfalme wao, aliwajibu,"Mimi sitatawala juu yenu …. Yeye Bwana atatawala juu yenu" (Amosi 8:23).

Mwamuzi wa mwisho alikuwa Samweli . Katika kipindi chake wana - Israeli waliomba wawe na mfalme binadamu ili wawe kama mataifa mengine yanayozunguka (Sam.8: 5, 6). Katikati ya historia nzima, watu wa kweli wa Mungu wamejaribu kupima kidogo sana

ukaribu na uhusiano wao kwa Mungu, na kutoa dhabihu hii kwa sura yenye mfano mmoja na ulimwengu uliowazunguka. Majaribu haya ni makali zaidi ulimwengu huu wetu uliopo . Mungu alisikitika kwa Samweli:"Wamenikataa mimi, ili nisiwe mfalme juu yao"(1Sam. 8:7). Ingawa hivyo, Mungu aliwapa Wafalme, wakaanza na kuwa na Sauli mbaya, Baada yake akafuata Daudi mwenye haki, mstari mzima wa ufalme umeshuka toka kwake. Wafalme wenye nia ya roho zaidi walitambua kuwa Israeli bado walikuwa ni ufalme wa Mungu hata kama walimkataa kuwa mfalme. Kwa sababu hii waligundua kwamba walikuwa watawala juu ya Israeli kwa niaba ya Mungu sio kwa Haki yao.

Tunapolielewa jambo hili linatuwezesha kutafakari maelezo ya Suleimani, mwana wa Daudi, alipotawala juu ya "Kiti cha enzi cha Mungu, kuwa mfalme wake Bwana, Mungu wako" (2 M/Nyak. 9: 8; 1 M/nyak. 28:5; 29:23). Utawala wa Suleimani wa amani na ustawi ulionyesha mbele (au ulikuwa ni 'mfano' wa) Ufalme ujao wa Mungu. Hii ndio sababu imetiwa mkazo kwamba akawa mfalme juu ya Israeli badala ya Mungu, Kama Yesu naye atakavyoketi juu ya kiti cha enzi cha Mungu akiwa mfalme wa Israeli kwa ajili ya Mungu (Mat 27: 37, 42; Yn. 1:49; 12:13 ).

Wengi wa wafalme wenye haki walioorodheshwa kwenye Agano la Kale walifurahia tawala zilizokuwa ni mfano wa ufalme ujao wa Kristo. Hivyo kama Suleimani alivyojenga hekalu la Mugnu Yerusalemu, basi pia, Kristo atafanya hivyo katika ufalme ujao (ona Ezek. 40 -48). Kama Ezekia na Suleimani walivyopokea kodi na vipawa toka mataifa yaliyowazunguka. (1Fal.10: 1-4; 2 Fal. 20: 12). na kuona nchi ya Israeli ikibarikiwa kwa rutuba ya kushangaza na ustawi (1Fal. 10: 5-15; Isa. 37: 30), hivyo katika ufalme wa Kristo utakaokuwa wa ulimwengu wote mambo hayo hayo yataonekana kwa kipimo chenye mapana zaidi.

**NDOA**

Mbali na Suleimani kuanza vyema, wakati bado kabisa akingali kijana alifanya makosa ya mintarafu ya ndoa ambayo kwa kuyaendekeza yalinyonya nguvu zake za kiroho alipozeeka. "Mfalme Suleimani akawapenda wanawake wengi wageni …… wanawake wa moabu, na wa Waamoni, na Waedomi …. Na wa mataifa Bwana alivyowaambia wana wa Israeli, Msiingie kwao, wala wasiingie kwenu: kwa kuwa hakika watageuza mioyo yenu kuifuata miungu yao. Suleimani akaambatana nao kwa kuwapenda …. Wake zake wakamgeuza moyo wake. maana ikawa Suleimani alipokuwa mzee, Wake zake wakamgeuza moyo wake, afuate miungu mingine, wala moyo wake haukuwa mkamilifu kwa Bwana, ….. Suleimani akafanya yaliyo mabaya machoni pa Bwana,wala hakumfuata Bwana akamghadhibikia Suleimani …. Kwa hiyo Bwana akamwambia …. Hakika nitaurarua ufalme usiwe wako" (1Fal. 11: 1 -11).

Kuteleza na kuiacha imani Suleimani kulidumu maisha . Uhusiano wake na wanawake ambao hawakushiriki maarifa yake kwa Mungu wa Israeli kulimwongoza kuwa na uhusiano wa kuielekea miungu yao ya uongo. Upendo wake kwa wake zake ilimaanisha hakuona tena miungu hii inamkengeusha kiroho toka kwa Mungu wa kweli ambapo ndivyo ilikuwa. Kadri muda ulivyosonga mbele , moyo wake haukumwabudu tena Mungu wa Israeli."Moyo wake haukutimilika"yaani, dhamira yake haikumchoma tena kuabudu miungu inayodanganya. kukosa moyo wake wote kujitoa kwa Mungu wa kweli "ukawa ni uovu machoni pa Bwana"ikasababisha Mungu kuvunja uhusiano na Suleimani. Israeli waliambiwa mara kwa mara wasioane na wanawake wa mataifa yanayowazunguka (Kut. 34: 12 -16; Yoshua. 23: 12, 13; K/Torati 7:3).

Kwa kubatizwa katika Kristo kiroho tunakuwa Israeli, kama hatujaoa, tuoe tu ndani ya Israeli kiroho,"Katika Bwana" (1Kor. 7:39) - yaani, mwamini mwingine aliyebatizwa 'Katika Kristo' Ikiwa tayari tumeoa wakati tunabatizwa, tusitengane na wake zetu; uhusiano wetu wa ndoa unatakaswa kwa sababu ya imani yetu (1Kor. 7: 12 -14). Kwa kufahamu, kuchagua kuoa wale ambao hawamjui Mungu wa kweli, kwa muda mrefu, watatuongoza kwenye ukengeufu wetu. Solomoni ni dhahiri alishindwa kukubali onyo la nguvu za Mungu kuhusu wanawake hawa:"Hakika wataugeuza moyo wako"(1Fal. 11: 2; Kut. 34: 16). Usawa pekee wa ajabu wa kujiweza na nguvu ya mawazo ya toba inaweza kutufanya tusihesabiwe na amri hii .

Awali tumeonyesha jinsi huo Ukristo wa orthodox haukubali msingi wa Wayahudi ambao ni tumaini la mkristo; hawamjui Mungu wa kweli wa Israeli. Kuoana na watu hawa wasiomjua Mungu kutatupeleka pole pole kutofautiana na utukufu wenye kweli ya mafunzo ambayo ni msingi wa wokovu wetu. Kwa sababu hii Isaka na Yakobo walikwenda umbali wa ajabu kuoa wanawake ambao waliishika imani ya kweili vema, Isaka akasubiri mpaka alipofikia umri wa miaka 40 ili kupata mke anayefaa (Mwa. 24: 3, 4; 28: 1). Sababu iliyoleta huzuni kwa Ezra na Nehemia waliposikia ya kuwa Wayahudi wengine walioa wasio wayahudi zaidi inaonyesha ukubwa wa toleo hili (Ezra. 9:12; Nehemia 10: 29, 30).Tumeleta jambo hili kwenye hatua hii ili kusaidia kufikiri kwa kuangalia; ndoa imejadiliwa kwa maelezo zaidi katika somo la 11.4.

**HUKUMU YA MUNGU**

Yakiwa ni matokeo ya kukengeuka Suleimani, Ufalme wa Israeli ukagawanyika na kuwa falme mbili; mwanae Suleimani,Rehoboamu, akatawala juu ya kabila ya Yuda,

Benjamini na nusu ya kabila la Manase, wakati Yeroboamu akatawala juu ya kabila zingine kumi. Huu ufalme wa kabila kumi uliitwa Isrraeli,au Efraimu, ambapo makabila mawili yaliitwa Yuda. Watu wote wa kabila hizi kwa sehemu kubwa walifuata mfano mbaya wa Suleimani - walidai kumwamini Mungu wa kweli, wakati huo huo wakiendelea kuziabudu sanamu za mataifa waliowazunguka. Mara kwa mara Mungu aliwasihi, kwa njia ya manabii, ili watubu, bali haikufaa. Kwa sababu hii akawaadhibu kwa kuwatoa kwenda nje ya ufalme wa Israeli waingie nchi za adui zao. Hii ilikuwa kwa waashuri na wakaldayo wakiihusuru Israeli na kutwaa mateka. "Miaka mingi (Mungu) akachukuliana nao, nawe ukawashuhudia kwa roho yako (neno) kwa vinywa vya manabii wako: (bali) wao wasitake kusikiliza; kwa hiyo ukawatia katika mikono ya watu wa nchi (zilizowazunguka)"Nehemia 9:30.

Kabila kumi, ufalme wa Israeli, haukuwa na wafalme wazuri hata kidogo. Yeroboam, Ahazi, Yehoahazi n.k wote wameandikwa taarifa zao katika kitabu cha wafalme wakiwa ni waabuduo sanamu. Mfalme wao alikuwa Hoshea, kipindi cha utawala wake Israeli walipopigwa na waashuri, nao kabila kumi wakachukuliwa utumwani (2 Fal. 17). kutokana na hii hawakurudi kamwe .

Ufalme wa Yuda wenye kabila mbili ulikuwa na baadhi ya wafalme wazuri (k.m Hezekia na Yosia), ingawa walio wengi walikuwa waovu. Kwa ajili ya watu kurudia -rudia kutenda dhambi, Mungu akaupindua ufalme wa Yuda katika kipindi cha utawala wa mfalme wao wa mwisho, Sedekia. Hsii ilitokana na wao kuvamiwa na wakaldayo , waliowachukua kwenda utumwani Babeli (2 Fal. 25) Walibakia Babeli kwa miaka 70, Wengine wakarudi baadae Israeli chini ya uongozi wa Ezra na Nehemia. hawakuwa tena na mfalme wao, walipokuja tawaliwa na wakaldayo, wayunani na warumi. Yesu alizaliwa wakati wa

kipindi cha utawala wa Warumi. Kwa sababu ya Israeli kumkataa Yesu, Waroma wakawavamia mwaka 70 B.K na kuwatawanya ulimwenguni pote. Ni miaka 100 tu iliyopita walianza kurudi, hii ni ishara inaonya kurudi kwa Kristo

{ Ona kilichotiwa mwishoni mwa kitabu sehemu ya 3 }
{ nyongeza iliyotiwa mwishoni mwa kitabu}.

Ezekieli 21: 25 -27 mistari hii ilitabiri mwisho wa ufalme huu wa Mungu kama ulivyoonekana katika taifa la Israeli: "Na wewe, Ewe mtu mwovu, uliyetiwa jeraha kiasi cha kuwa , Mkuu wa Israeli (yaani, Sedekia), ambayo siku yako imekuja ….. Bwana MUNGU asema hivi; Kiondoe kilemba, ivue taji; (yaani Sedekia atakoma kuwa mfalme) haya hayatakuwa tena kama yalivyo; …… Nitakipindua, hiki nacho Nitakipindua, Nitakipindua, hakitakuwa tena, hata atakapokuja yeye ambaye ni haki yake; nami nitampa"Maneno baada ya maneno kwa manabii wanaohuzunikia kukomeshwa kwa ufalme wa Mungu (Hos.10: 3; Omb. 5:16; Yer. 14:12; Dan. 8: 12 -14).

'Kupindua' mara tatu iliyo katika Ezekiel 21: 25 -27 unatajwa uvamizi uliofanywa mara tatu na Nebukadneza, mfalme wa Babeli. Mwanafunzi anayekesha ataona katika mistari hii mfano mwingine wa jinsi ufalme wa Mungu na mfalme wake anaweza kutendwa sawa; Kuangushwa kwa Sedekia ulikuwa huo ufalme wa Mungu (ona sehemu ya 5:2). Hivyo ufalme wa Mungu kama ulivyokuwa katika taifa la Israeli ulifika mwisho: "….. na kuukomesha ufalme wa nyumba ya Israeli"(Hos. 1:4), "Hiki nacho hakitakuwa tena , hata …."Inaleta kidokezo kwamba ufalme utaanza tena hapo"atakapokuja ambaye ni haki yake; naye (Mungu) atampa". Mungu atampa (Yesu) kiti cha enzi cha Daudi Baba yake ….. na ufalme wake hautakuwa na mwisho"(Luk. 1: 32, 33) -

Kristo akirudi. Basi, hii ni hapo ahadi ya kurudishwa ufalme itakapotimizwa.

**KUTENGENEZWA KWA ISRAELI**

Lipo jambo kubwa lililoandikwa katika Agano la Kale lote na manabii la kurudishwa ufalme wa Mungu akirudi masihi.Wafuasi wa Kristo walielewa vema hili:"Basi walipokutanika, wakamuuliza, wakisema, Bwana, wakati huu ndipo unapowarudishia Israeli ufalme ?"yaani, 'Unabii wa Ezekieli 21:27 utatimia sasa ?' Yesu alijibu kwa kusema kuwa muda hasa wa yeye kuja mara ya pili hawata ujua, Ingawa malaika haraka baadaye waliwahakikishia kuwa atarudi wakati fulani (Matendo. 1: 6 -11).

Kutengenezwa ufalme wa Mungu / Israeli kutakuwa basi akirudi mara ya pili. Hivi Petro alihubiri ya kuwa Mungu atamtuma "Yesu Kristo …….. ambaye ilimpasa kupokewa mbinguni (yaani, asalie kule) hata zije zamani za kufanywa upya vitu vyote, zilizonenwa na Mungu kwa kinywa cha manabii wake watakatifu"(mdo. 3:20,12). Kuja mara ya pili kutafanya uanzishwe tena ufalme wa Mungu kama kutengeneza tena ufalme wa Israeli wa zamani.

Kwa kweli kutengeneza tena ufalme wa Mungu ni msemo wa"Manabii wote watakatifu wa (Mungu)":-

- "Kiti cha enzi kitafanywa imara kwa rehema: na mmoja (Yesu) ataketi juu yake katika kweli, katika hema ya Daudi (akija mara ya pili - Luk. 32,33), akifanya hukumu …… mwepesi wa kutenda haki"(Isa. 16:5).
- "Siku hiyo nitainua tena masikani ya Daudi yaliyoanguka (yaani, kiti cha enzi cha Daudi kilichosemwa na Luk.1: 32,33), na kuziba mahala palipobomoka; nami nitayainua magofu yake, na

kuyajenga kama siku za kale"(Amosi. 9:11 . Fungu la mwisho la maneno ni Lugha iliyowazi ya kutengeneza tena.

• “Watoto (Israeli) wao nao watakuwa kama zamani, na kusanyiko lao litathibitika mbele zangu" (Yer. 30:20) .

• “Bwana atachagua Yerusalemu tena"(Ezek. 2:12), atafanya mji mkuu kwa ufalme wake wa ulimwengu wote (Zab. 48:2; Isa. 2:2 -4).

• “Nami nitawarudisha wafungwa wa Yuda na wafungwa wa Israeli, na kuwajenga kama kwanza ……. Itasikika tena sauti ya furaha na sauti ya shangwe ……. Kwa kuwa nitawarudisha wafungwa wa nchi kama kwanza ….. katika mahali hapa (Yerusalemu) ….. yatakuwepo makao ya wachungaji …. Makundi ya kondoo yatapita"(Yerusalemu 33: 7 -13).

Kurudi kwa Kristo kuanzisha huu ufalme kwa kweli ni "tumaini la Israeli”, ambalo yatupasa tujihusishe kwa kubatizwa.

## 5.4 Ufalme wa Mungu kwa Wakati Ujao

Sehemu ya 1 na 3 ya somo hili zimetoa habari kiasi cha kutosha kuhusu jinsi huu ufalme utakavyokuwa. Tumeona kuwa Abrahamu aliahidiwa kwamba kwa njia ya mzao wake watu toka maeneo yote ya ulimwengu watabarikiwa; Rum.4: 13 inapanua suala hili kuwa na maana ya kuwa Dunia yote itakaliwa na hao watu ambao wamo'Katika’ Uzao wa Abrahamu, yaani Kristo. Unabii ulio katika sanamu ya Dan. 2 waeleza Kristo atakavyorudi kama jiwe dogo, na kisha pole pole ufalme utapanuka na kuwa wa ulimwengu wote (Zab.72:8). Hii inamaana ya kwamba ufalme wa Mungu hautakuwa eneo la Yerusalemu pekee au katika nchi ya Israeli , kama wengine wanavyosema, kama maeneo haya hakika yatakuwa maeneo yake makuu. Wanaomfuata Kristo katika maeneo haya watakuwa"Wafalme na makuhani; tutatawala

dunia"(Uf. 5:10). Tutakuwa wasimamizi juu ya makazi ya watu ya ukubwa mbali mbali na idadi; mmoja atakuwa juu ya miji kumi, na mwingine juu ya mitano (Luk. 19:17). Kristo atashiriki utawala wake pamoja nasi (uf. 2:27; 2 Tim 2:12)."Mfalme (Yesu) atamiliki kwa haki, na wakuu (Waaminio) wake watatawala kwa hukumu" (Isa. 32:1; Zab. 45: 16).

Kristo atamiliki milele katika kiti cha enzi cha Daudi kitakachokuwa kimewekwa tena (Luk. 1: 32, 33), yaani, atakuwa na mahali pa Daudi na cheo cha utawala, kilichokuwa Yerusalemu. Ikiwa Kristo atamiliki tokea Yerusalmeu, Huu utakuwa ni mji mkuu wa ufalme ujao. ni kwenye eneo hili ambapo hekalu litajengwa (Ezek. 40 -48). Wakati watu watamtukuza Mungu sehemu mbali mbali za ulimwengu wote (Malaki. 1:11), Hekalu hili litakuwa kitovu cha ibada walimwengu. Mataifa"watakwea mwaka baada ya mwaka ili kumwabudu mfalme, Bwana wa majeshi, na k ushika sikukuu ya vibanda"kuzunguka hekalu katika mji wa Yerusalemu (Zekaria 14:16). Hii hija ya mwaka kwenda Yerusalemu pia imetabiriwa kwa Isa. 2: 2,3) "Katika siku za mwisho, mlima wa nyumba ya Bwana (Ufalme- Dan.2:35,44) wa nyumba ya Bwana (Hekalu) utawekwa imara juu ya mlima (yaani, ufalme wa Mungu na hekalu vitawekwa juu ya falme zetu) ….. na mataifa yote watauendea makundi makundi Na mataifa wengi watakwenda na kusema, Njooni twendeni juu mlimani kwa Bwana, nyumbani kwa Mungu wa Yakobo; naye atafundisha njia zake, ….. maana katika Sayuni itatoka sheria, na neno la Bwana katika Yerusalemu" Hii inaonekana kuwa picha ya siku za kwanza za ufalme, watu walipotangaza maarifa ya miliki ya Kristo kwa wengine, na watu wanakwenda juu "Mlimani"wenye ufalme wa Mungu, ambao utaene taratibu ulimwenguni pote. Hapa tuna picha ya shauku ya kweli katika ibada ya dini .

Moja ya mambo makubwa yaletayo huzuni kwa mwanadamu wa siku zetu ni kwamba watu'humwbudu' Mungu kwa siasa, kwa makundi kukaa pamoja , kwa mazoea au kwa hangaiko la moyo, kuliko juu ya msingi wa ufahamu wa kweli kwake akiwa ni Baba yao na muumba. Katika Ufalme kutakuwepo shauku ulimwenguni pote ya kujifunza njia za Mungu; watu watakuwa na nia ya kusudi sana kusafiri toka miisho yote ya Dunia kwenda Yerusalemu ili kupata elimu ya Mungu zaidi. Badala ya chafuko na utaratibu wa kuhusiana na binadamu usio na haki na utawala wa haki, kutakuwa na kanuni moja ya sheria"Sheria na neno la Bwana"Vitatamkwa na Kristo toka Yerusalemu."Mataifa yote yatakwenda makundi makundi"kwenye vipindi vya mafunzo haya, yanadokeza kuwa hii nia ya watu wote kutafuta elimu ya kweli juu ya Mungu itapunguza mabishano yaliyozaliwa nayo kati ya mataifa, kama yafanyavyo kati ya mtu na mmoja mmoja wanaojitoa wenyewe kujipatia elimu kama hii katika maisha haya.

Namna hii ya mataifa kufurika katika mji wa Yerusalemu ni moja na picha inayoonyesha katika Isa. 60: 5, ambapo Wayahudi "Wanakwenda pamoja"na watu wa mataifa (wasio wayahudi) kumwabudu Mungu katika mji wa Yerusalemu. Habari hii inaungana kikamilifu na unabii ulio katika Zekaria. 8: 20 -23: -

“Itatokea halafu ya kwamba watakuja mataifa na wenyeji wa miji mingi; wenyeji wa mji huu watauendea mji huu, wakisema, Haya ! twendeni zetu kwa haraka (Zek. 14: 16 mwaka kwa mwaka) tuombe fadhili za Bwana , na kumtafuta Bwana wa majeshi; mimi nami nitakwenda. Naam, watu wa kabila nyingi na mataifa hodari watakuja Yerusalemu kumtafuta Bwana ….. watu kumi, wa Lugha zote za mataifa, wataushika upindo wa nguo yake yeye aliye Myahudi; Naam, wataushika wakisema, tutakwenda

pamoja nanyi, kwa maana tumesikia kwamba Mungu yu pamoja nanyi"

Hii inaumba picha ya watu wa Uyahudi kufanywa"Kichwa na sio mkia" wa mataifa, kwa ajili ya kutubu kwao na utiifu (K/Torati 28:13);Mpango wa Mungu kwa Wayahudi wa wokovu wakati huo utakubalika na kila mtu. Kutokujua huku miongoni mwa Wakristo wa wakati ule ule basi utafikia mwisho mara moja. Wakati huo watu kwa shauku watajadili mambo haya. Kwa kusudi kwamba waweze kuwaambia wayahudi,"tumesikia ya kwamba Mungu yu pamoja nanyi". Mazungumzo yatakuwa mambo ya kiroho wakati huo, kuliko mizuka inayojaa fikira za ulimwengu uliopo.

Kutolewa sharti kubwa kwa utauwa, halishangazi kuwa Kristo "atafanya hukumu katika mataifa mengi, ….Nao watafua panga zao ziwe majembe, na mikuki yao iwe minundu: Taifa halitainua upanga juu ya taifa jingine, wala hawatajifunza vita tena kamwe"(Isa. 2:4).

Mamlaka kamili ya Kristo na haki kabisa ya ushupavu wake katika mabishano utasababisha mataifa kwa hiari kubadili zana za kijeshi na kuwa vyombo vya kilimo na kuacha mafundisho yote ya kijeshi. "Siku zake yeye, mtu mwenye haki atasitawi" (Zab. 72:7). Kwa kiroho wakati huo atakuwa na hali ya juu, na heshima watapewa walio na sifa ya upendo wa Mungu, huruma na haki. Ni tofauti na wakati uliopo wa kuwa juu wenye kiburi, wenye kujidai na wachoyo wenye tamaa ya kuwa maarufu.

Hiari ya kufua"Mapanga kuwa majembe"itakuwa sana sehemu kubwa ya mabadiliko kwa kilimo kitakachokuja duniani, kwa toleo la dhambi ya Adamu, ardhi ililaaniwa kwa ajili yake (Mwa. 3: 17 - 19), pamoja na matokeo ya jitihada kubwa inatakiwa kwa sasa ili

kupata chakula. Katika ufalme wa Mungu"utakuwepo wingi wa nafaka katika ardhi juu ya milima - yaani sehemu kame; na matunda yake yatawaya -waya kama (mazao) Lebanoni"(Zab. 72:16)."Alimaye atamfikilia avunae,naye akanyagae zabibu atamfikilia apandae mbegu; nayo milima itadondoza divai tamu"(Amosi. 9:13), ndivyo ardhi itakuza hali ya uzaaji, na kupunguza laana iliyotamkwa Edeni juu ya ardhi

Bidii hii kubwa kwa kilimo itahusisha watu wengi. Unabii na ufalme unatoa fikira ya kuwa watu watarejea kujitosheleza, kwa mtindo wa maisha ya kulima: -

“Wataketi kila mtu chini ya mzabibu wake, chini ya mtini wake; wala hakuna mtu atakayewatia hofu" (Mika. 4:4)

Huku kujitosheleza kutashinda matumizi mabaya yaliyo ndani ya mfumo wowote wa ajira ya kazi kwa ajili ya kupata pesa. Kutumia maisha yote kufanya kazi ya kuwafanya watu wengine watajirike wakati huo itakuwa ni jambo lililopita.

“Watajenga nyumba, na kukaa ndani yake; watapanda mizabibu na kula matunda yake. Hawatajenga, akakaa mtu mwingine ndani yake; hawatapanda, akala mtu mwingine …. Wateule wangu wataifurahia kazi ya mikono yao muda wa siku nyingi. Hawatajitaabisha kwa kazi bure ……"(Isa. 65: 21 -23).

Isaya 35: 1 -7 ina unabii usio na kifani jinsi nchi kame itakavyobadilika, ikisababisha kuwa katika hali ya shangwe na kufurahisha karibu ikitiririka toka kwenye nchi, kwa sababu ya kuwa na raha na zaidi maisha ya kiroho kwa wale watendaji : "Nyika …. Pata furahi ….. jangwa litashangilia na kuchanua maua kama waridi. Litachanua … na kufurahi , naam, kwa shangwe na

kuimba …….. maana katika nyika maji yatabubujika, na vijito jangwani. Na mchanga ung'aao mfano wa maji utakuwa ziwa la maji na nchi yenye kiu itakuwa chemi chemi za maji". Hata tendo la asili la kushambuliana kati ya wanyama litaondolewa:"mbwa mwitu na mwana kondoo watalisha pamoja", na watoto wataweza kucheza na nyoka (Isa. 65:25; 11: 6 - 8).

Kwa njia hiyo hiyo Laana iliyowekwa juu ya wanyama kwa ukubwa itapunguzwa, Hivyo na tokeo lililowekwa juu ya wanadamu nalo pia litapunguka.Ufu. 20: 2,3 inasema hivi kwa lugha ya ishara ya Ibilisi ( dhambi na matokeo yake) "Kufungwa"au kuzuiwa, kwa kipindi cha millenia yaani miaka elfu. Maisha ya kuishi yataongezeka, hivyo basi mtu akifa mwenye miaka 100, atadhaniwa bali kuwa ni mtoto (Isa. 65:20) Wanawake watapata uchungu mdogo wakati wa kujifungua mtoto (mst. 23). "Ndipo macho ya vipofu yatafumbuliwa, na viziwi masikio yao yatazibuliwa. Mtu aliye kilema ataruka -ruka kama ndama, na ulimi wake aliye bubu utaimba" (Isa. 35: 5,6). Hii itakuwa kwa sababu ya kuwepo vipawa vya Roho (Ebra. 6:5).

Ufalme waMungu kwa nguvu hauwezi kukaziwa mno kama kuonekana kama kisiwa chenye joto jingi peponi, ambacho watu wenye haki watafurahia kwa namna hii watu wanavyofurahia kuota jua baada ya kuogelea katikati ya kujivunia maumbile. Kusudi la msingi wa Ufalme wa Mungu ni kutoa utukufu kwa Mungu, hata dunia itajawa na utukufu wake"Kama maji yaifunikavyo bahari" (Habakuki 2:14). Hii ni shabaha aliyokuwa nayo Mungu tangu asili:"Kama niishivyo, dunia nzima itajaa utukufu wa Bwana" (Hes. 14: 21). Utukufu kwa Mungu maana yake ni kwamba wakaazi wa dunia watatoa shukrani, Sifa na mfano ulio kiini cha tabia yake; kwa kuwa ulimwengu utakuwa katika hali hii, Mungu atafanya nayo dunia inayoonekana itoe utukufu pia. Hivyo"Wapole

watairithi nchi (Katika ufalme wa Mungu) Watajifurahisha kwa wingi wa amani (ya kiroho)" (Zaburi 37:11), kuliko kufurahia maisha ya starehe. Hao"Walio na njaa na kiu ya haki …. Watashibishwa" (Math.5:6).

Wazo tu la kuwa na uzima wa milele katika ufalme mara nyingi limetumika kama 'kuwavuta kuwapa zawadi' ya kuwashawishi watu kwenye mapenzi ya Ukristo. Ingawa hivyo, wakati huu wa kuwa nalo sisi, karibu ni la kufuata kama matokeo kwa sababu yetu ya kweli kuwamo katika ufalme ambao ni kwa kumtukuza Mungu. Ni kwa muda gani litasalia nasi baada ya sisi kubatizwa, ufahamu wetu kwa hili daima utakua. Kwa maandishi, kuishi miaka kumi tu kwa furaha ya utimilifu kabisa na dhamiri njema na Mungu lngekuwa bora kuliko maisha haya ya shida. kama hali hii yenye utukufu itadumu mielele akili peke yake inapanuka mno, na kuchukuliwa kupita upeo wa fahamu ya mwanadamu.

Hataitazamwapo kidogo zaidi kwa maneno ya kimwili, kuwa katika ufalme wa Mungu kuwe ni kusudi kuu letu kudharau faida za ulimwengu na kujikusanyia vitu vya mwilini. Badala ya kuwaza mno u karibu wa wakati ujao Yesu alishauri,"Utafuteni kwanza ufalme wa Mungu, na haki yake; na haya yote mtazidishiwa"(math. 6:30 -34) Kila kitu ambacho sasa tunaweza kufikiri na kujitahidi hakilinganishwi na utimilifu wa mwisho wa kuwamo katika ufalme wa Mungu.

Tunatakiwa kutafuta "haki (ya Mungu)", yaani kujaribu kukuza upendo wa tabia ya Mungu, ambayo maana yake ni kwamba tunataka kuwa katika Ufalme wa Mungu kwa sababu haki itatukuzwa humo, kwa sababu tunataka kwa uadilifu tuwe kamili

kabisa kuliko tu kwa sababu sisi wenyewe' tunataka kuepuka mauti na kuishi maisha ya raha milele.

Tumaini la Injili lote pia mara nyingi limeonyeshwa kwa njia ambayo inatazamisha ubinafsi wa mwanadamu. Ni dhahiri kusudi letu la kuwamo kwenye ufalme wa Mungu kwa ukubwa linahitilafiana toka siku hadi siku. Tunachodokeza hapa ni wazo la ukamilifu; kipaumbele chetu ni

kujifunza injili na kuonyesha kuwa tunaitii kwa ubatizo kutokana na wazo lenye upendo wa kumtii Mungu. Kuthamini kwetu tumaini ambalo Mungu anatoa, na sababu zetu hasa za kutosha kuamo katika Ufalme, zitakua na kukomaa baada ya ubatizo wetu.

### 5.5 Miaka Elfu - Kikwi

Kwa kipengele hiki cha somo letu la maisha katika ufalme, msomaji mwenye kuwaza kwanza atauliza, 'Picha hii yote ya ufalme wa Mungu, Je ! haionekani kuwa ni ya mwanadamu ?' watu katika ufalme watakuwa bado wanazaa watoto (Isa. 65: 23) na hata kufa (Isa. 65:20). Bado watu hawa watakaidi kile Kristo atakachokalisha - yaani ufalme (Isa.2:4) na bado watahitajika kufanya kazi ya kulima ili waishi, ingawa kazi hii itakuwa ya raha sana kuliko wakati uliopo. Haya yote yanaonekana kuwa kilio cha mbali toka ahadi za kwamba watu wenye haki watapata uzima wa milele, na mwili wa Uungu, kufanywa sawa na malaika, wasiooa na kuzaa (Luk. 20: 35,36). Jibu lipo katika ukweli kwamba sehemu ya kwanza ya ufalme wa Mungu itadumu kwa miaka 1000 -'Kikwi' (ona Uf. 20: 2-7). Kipindi hiki cha kikwi kutakuwapo makundi ya watu aina mbili duniani: -

1. Watakatifu - ni sisi hao tuliomfuata Kristo inavyokubalika katika maisha, ambao watakuwa wamepewa uzima wa milele

kwenye kiti cha hukumu, Elewa:'Mtakatifu' maana yake mtu 'aliyeitwa atoke' anatajwa mwamini yeyote wa kweli.

2. Watu wa kawaida wanaopatwa na mauti ambao hawakuijua Injili Kristo anaporudi - yaani hawakuwa na la kusema mbele ya kiti cha hukumu.

Kristo atakapokuja , watu wawili watakuwa kondeni, mmoja atwaliwa (kwenda mbele ya hukumu) na mmoja aachwa (Luk. 17: 36); hao wanao"achwa" watakuwa katika hili kundi la pili.

Wakiisha pata mwili wa Mungu mbele ya kiti cha hukumu, watakatifu hawataweza kufa au kuzaa watoto. Maelezo ya watu kupata vitu katika ufalme basi inabidi iwe ni kwa kundi la pili - hao walio hai Kristo anaporejea, Lakini hawakujua matakwa ya Mungu.Thawabu ya watu wenye haki ni kuwa "Wafalme na Makuhani: na kumiliki nchi"(Uf. 5:10). Wafalme inabidi wawatawale watu wengine; hao watu ambao walikuwa hawajui Injili wakati wa kuja mara ya pili wataachwa wawe hai, ili wamilikiwe. kwa njia ya kuwamo "ndani ya Kristo"tutashiriki thawabu yake - ambayo ni kuwa mfalme wa ulimwengu: "Na yeye ashindaye ….. nitampa mamlaka juu ya mataifa: naye atawachunga kwa fimbo ya chuma.. kama mimi nami nilivyopokea kwa Baba yangu" (Uf. 2: 26,27).

Kristo na mahubiri yake ya mfano wa fedha sasa unaingia mahala - watumwa waaminifu walipewa zawadi ya kutawala miji kumi au mitano katika ufalme (Luk. 19: 12 -19). Maarifa ya njia za Mungu hayataenea haraka Kristo akisemwa kuwa ni mfalme mjini Yerusalemu; Watu watasafiri kwenda Yerusalemu kwa ajili ya kujipatia elimu kuhusu Mungu ( Isa. 2: 2,3). kumbuka,pia, mlima uliotajwa katika Dan. 2: 35, 44 (maana yake ufalme wa Mungu)

pole pole unaenea juu ya dunia. Litakuwa ni jukumu la watakatifu kueneza maarifa ya Mungu na kwa hiyo ufalme wake. Israeli ulipokuwa ni ufalme wa Mungu awali, jukumu la makuhani lilikuwa ni kufunza watu wapate kumjua Mungu ( Malaki 2:5 -7). kwa kusudi hili waliwekwa katika miji mbali mbali ya Israeli yote. Utakapowekwa tena ufalme wa Mungu wenye utukufu zaidi, watakatifu wataingia mahali pa kazi ya makuhani (Uf. 5:10).

**Kristo akija Leo:**

1. Wafu wanaotakiwa kutoa habari watafufuliwa, pamoja na watu walio hai, watachukuliwa kwenda mbele ya kiti cha hukumu .

2. Wawajibikaji wabaya wataadhibiwa kwa mauti, na wenye haki watapewa uzima wa milele. Hukumu pia itatolewa kwa mataifa yanayo mpinga Kristo .

3. Watu wenye haki wakati huo watawatawala watu ambao wakati huo watakuwa hai, Lakini ambao hawawajibiki kwa Mungu sivyo; Watafundishwa Injili wao wakiwa ni "Wafalme na Makuhani"(Uf. 5:10)

4. Ufalme utadumu kwa miaka 1000. Wakati wa kipindi hiki watu wote wenye kupatwa na mauti wataisikia injili na kwa hiyo kuwa na wajibu kwa Mungu. Watu hawa wataishi kwa muda mrefu zaidi kwa maisha ya furaha .

5. Mwisho wa Kikwi kutatokea uasi juu ya Kristo na watakatifu, Uasi huo Mungu atauweka chini (Uf. 20: 8,9).

6. Mwisho wa miaka 1000, wote waliokufa wakati wa kipindi hicho watafufuliwa na kuhukumiwa ( Uf. 20: 5,11 -15 ).

7. Wabaya miongoni mwao wataharibiwa, na watu wenye haki wataungana nasi kuwa na uzima wa milele.

Kusudi la Mungu kwa dunia wakati huo litakamilika. Itajawa na watu wenye haki wasiokufa. Jina la Mungu 'Yahweh Elohim' - Hili jina katika kiswahili limeandikwa YAHU ELOI (lina maana'Yeye atakayedhihirika katika kundi la wenye nguvu') wakati huo litatimia. Dhambi na mauti havitaonekana tena duniani; ahadi ya kwmba uzao wa nyoka utaharibiwa kabisa kwa kupondwa kichwa, wakati itatimia kwa ukamilifu (Mwa. 3:15). Wakati wa Kikwi Kristo yampasa amiliki "hata awaweke maadui wake wote chini ya miguu yake. Adui wa mwisho atakayeondoshwa ni mauti ….. Basi , vitu vyote vikiisha kutiishwa chini yake (Mungu) aliyemtiishia vitu vyote, ili kwamba Mungu awe yote katika wote" (1 Kor. 15: 25 -28).

Hapo ndipo"Mwisho, (Kristo) atakapompa Mungu Baba ufalme wake"(1Kor. 15:24) Kitakachofuata kwa kipindi hiki Mungu atakapokuwa"yote katika wote" hatujaambiwa; yote tunayojua ni kuwa kutakuwa na uzima wa milele, mwili wa Uungu, na kuishi kwa kumtukuza na kumpendeza Mungu. Ni ufedhuli kuuliza zaidi hali ya baada ya Kikwi itakuwaje.

Kufahamu "Injli ya ufalme wa Mungu" ni muhimu kwa wokovu wa kila msomaji wa maneno haya. Tunakuomba usome tena somo hili kisha utazame mafungu ya maneno yaliyonukuliwa.

Mungu anatutaka tuwemo katika ufalme wake. Kusudi lake lote lilipangwa kwa ajili yetu kuwa na sehemu ya kweli , kuliko kueleza tu, uweza wake wa uumbaji. Ubatizo unatuhusisha na

ahadi zinazohusu ufalme huu. Ni shida kuamini kwamba ubatizo, unaofuatiwa na miaka michache ya kunyenyekea kumtii Mungu na neno lake, kunaweza kutupatia kuingia kwenye enzi zenye utukufu huo. Lakini imani yetu kwa upendo mpana wa Mungu inatakiwa iwe thabiti. Matatizo yetu yoyote ya muda mfupi, hakika hatuna sababu za kupinga mwito wa Injili .

“Mungu akiwapos upande wetu, nani aliye juu yetu ?"(Rum. 8:31 ).
“Mateso ya wakati huu wa sasa si kitu kama utukufu ule utakaofunuliwa kwetu" (Rum. 8:18).
“Dhiki yetu nyepesi, iliyo ya muda kitambo tu, yatufanyia utukufu wa milele uzidio kuwa mwingi"(2 Kor. 4:17).

***Tumeacha kitambo sehemu ya 15: Ufalme wenyewe***

Maelezo yenyewe kabisa ya ufalme yanayopatikana katika manabii wa Agano la Kale mara nyingi wameyakejeli wanatheologia na washirika wengi wa madhehebu. Imedaiwa kwamba Lugha ni ya mifano ya maeneo mengine ya kupewa dhawabu kuliko duniani, kwa kuwa sayari hii yaelekea kuchomwa moto.

Kwa kujibu hili, inabidi ieleweke kwamba kanuni ya kufundisha somo la Biblia ni kuwa siku zote tuichukulie Biblia ilivyoandikwa isipokuwa ikiwepo sababu nzuri ya kuweka tafsiri ya kiroho. Mathalani, mstari wa kwanza wa kitabu cha ufunuo unatujulisha ya kuwa maono kwa upana yameandikwa kwa ishara - Lakini sio katika Biblia ya kiswahili, Huu mstari haujaandikwa kama ni kwa ishara ila Biblia ya kiingereza ya K.J.V (Uf. 1:1), huu unaweza kutuongoza kwa mtazamo wetu. Pia ipo maana moja

nzuri na ya kuwa kweli kwa kutumia Lugha ambayo inaweza kuonyesha ikiwa au hapana maneno yasisomwe kwa ishara. Hivyo tunaposoma dunia inalewa -lewa kama mlevi (Isa. 24: 20), Kutokana na kuonekana wazi aina ya lugha iliyotumika hiyo tunakusudia kuisoma kimfano. Kwa utofauti, Lugha iliyotumika kuelezea ufalme ujao ni rahisi sana kufahamu kwa maneno halisi; hakuna fununu kwamba tusome mfano.

Inaonekana kwamba kwa ajili ya watu kutoweza kuipata imani ya kutosha kuamini kwamba muda huu kwa kweli utakuja hapa duniani, wamevumbua nadharia zinazoelezea mbali. Uchaguzi wao wa kiroho, au ufalme ambao upo mbinguni, si dhahiri na unakosa maelezo, kwa hiyo ni kidogo kuamini, na imani kidogo aidha inatakiwa au kutumainishwa. Kama kweli maelezo ya watu walemavu wataponywa au nyika zitafanywa kuwa na rutuba , ni mifano ya ishara tu, basi swali hili inabidi kwa namna yake maalum na kwa kusadikika lijibiwe: Ishara za kitu gani ? Mafungu haya ya maneno yanaelezea ufalme wa Mungu. ikiwa hatuna uhakika hasa Ishara ni za nini, basi hatuijui Injili ('habari njema’) kuhusu ufalme wa Mungu, na kwa hiyo hatuwezi kuwa na tumaini lolote ndani yake.

Juu ya hayo, itakuwa wazi kabisa toka ushahidi wote ulioonyeshwa mpaka hapa, ya kwamba Mungu analo kusudi la milele na wanadamu juu ya dunia hii. Haitaangamizwa sayari ambayo alimwahidi Abrahamu na uzao wake milele. Kwa hiyo tunangoja hapo kuwa maelezo halisi yaliyomo ndani ya Biblia ya ufalme unaokuja juu ya dunia.

Mafungu ya maneno yafuatayo yanathibitisha hili: -

- “Yeye ni Mungu aliyeiumba dunia na kuifanya; ndiye aliyeifanya imara; hakuiumba (ya bure) ukiwa, aliiumba ili ikaliwe na watu" (Isa. 45:18). kuumbwa kwa dunia kungekuwa hakufai ikiwa Mungu ataiharibu; bali, ni namna nyingine, kwani kusudi la Mungu ni kuwa ikaliwe na watu wasioharibika.

- “Dunia hudumu daima" (Muhubiri 1: 4).

- “Amevithibitisha (mpangilio wa asili wa sayari zote kulizunguka jua ) hata milele na milele: Ametoa amri wala haitapita" (Zab. 148:6).

Muda wa Kikwi kwa miaka 1000, kama ilivyoandikwa katika Uf. 20:4, ikubalike kwa maneno yalivyo, ili kuoanisha na maneno mengine katika manabii kuhusu kawaida ya kipindi hiki. Hata katika ufunuo, sio kila tarakimu ipasayo ichukuliwe kimfano. Ushahidi mwingi ndani yake kwa“theluthi" ni mifano iliyo wazi. Kwa maana zaidi Kikwi imeelezewa katika Waebrania 4: 4-9 kuwa ni siku ya sabato ya kupumzika. Kwa Mungu "siku ni sawa na miaka elfu" (2Pet. 3:8).Baada ya 'Siku’ sita za miaka elfu katika mpango wa Mungu na dunia, itafika'Siku’ ya sabato ya Kikwi.

Kulingana na kalenda ya Biblia ya uumbaji, miaka 6000 (yaani,'Siku’ 6) toka uumbaji tunafikishwa 2000 B.K (yaani - uumbaji ulikuwa karibu 4000 K.K.). Hapa panaweza kuwa na maana kwamba mwanzo wa Kikwi itakuwa karibu na 2000 B.K. Kwetu sote, muda umefika upeo. Tukiwa tunakabiliwa na matumaini ya Kristo kurejea mapema, twahitajika tutumie kila nafasi inayowezekana katika maisha haya mafupi kujiweka tayari kwa ujio wake.

*Tumeacha kitambo sehemu ya 16: Maelezo mafupi ya Historia ya Israeli*

**ABRAHAMU** aliitwa atoke Uru ya Wakaldayo; Myahudi wa kwanza. Mungu akafanya ahadi naye kuhusu nchi ya Kanaani, na uzao wake. Alikufa asijazipokea hizi ahadi.

**ISAKA.** Abrahamu alijiweka tayari kumtoa mwanae awe dhabihu. Kwa sababu Abrahamu alikuwa mwaminifu, Mungu akathibitisha ahadi zake kwa Abrahamu kwa kiapo. Hiari ya Isaka kufa kwa kumtii baba yake alichomwamuru ni mfano wa Kristo. Ahadi zilirudiwa kwa Isaka (Mwa. 26: 3-5).

**YAKOBO** alikuwa mwana wa Isaka. Ahadi zilirudiwa kwake pia . Alikuwa na wana 12 - Reubeni alikuwa mwana mkubwa, Benjamini alikuwa kitinda mimba. Lawi alikuwa ni mmoja ambaye makuhani walizaliwa naye. Yusufu alipendwa mno.

**YUSUFU.** Akiwa kijana aliota ndoto mbili zilizoonyesha picha kuwa yeye ni mtawala juu ya ndugu zake.Wakamwonea wivu, wakamuuza kama mtumwa katika nchi ya Misri. Huko akawa mtawala, akapanga kukusanya nafaka za kutumia wakati wa miaka saba ya njaa iliyoikumba nchi, wakati wa kipindi hiki, Yakobo na wanawe wakaja kuishi na Yusûsfu katika nchi ya Misri. Wao na watoto wao wakaishi sehemu ya Gosheni, sehemu ya Misri. Farao aliyekuja baadae akawatesa watu wa Israeli, kwa kuwafanya watumwa.

**MUSA** akazaliwa wakati huu; akiwa mtoto mchanga alifichwa katika kikapu, na kisha kukutwa na binti wa Farao na akafanywa kuwa wake wakati akiwa kijana, akamuua Mmisri

aliyekuwa anampiga mwisraeli. Ndipo Musa akakimbilia Midani, ambako alifanya kazi ya kulisha wanyama kwa miaka 40 kwa Yethro.Ndipo Mungu akamtokea katika kijiti kilichokuwa kinawaka moto. Akaambiwa aende kwa Farao na kutaka ukombozi wa Israeli. Alifanya ishara za miujiza ili kuthibitisha kuwa ametumwa na Mungu. Walakini Farao hakuwafungua Israeli waondoke, basi mapigo kumi yalitumwa juu ya Misri, yaani Vyura, giza, Mvua ya mawe, na mwishowe kuua kila mzaliwa wa kwanza mwanaume. Israeli ilibidi wachinje mwana kondoo na kunyunyiza damu juu ya milango yao. Hii ilionyesha tukio moja mbele jinsi damu ya Yesu inavyoweza kutuokoa toka mauti. Siku kuu hii ilikuja julikana kuwa Pasaka .

**KUTOKA.** Hatimaye Israeli waliachwa waondoke Misri - walisafiri huku wakiongozwa na malaika wa Mungu katika nguzo ya wingu wakati wa mchana, na nguzo ya moto wakati wa usiku. Jeshi la Farao lilifuata nyuma yao mpaka Bahari ya shamu. Kwa miujiza maji yaligawanyika ili watu wapite, kisha maji yalirudi mahali pake na kuua wamisri. Ndipo wakasafiri kupita jangwani kuelekea nchi ya ahadi ya Kanaani. Mungu aliwapa maji ya kunywa toka kwenye mwamba, na mkate kwa namna ya mana walipewa kila asubuhi. Walipofika mlima Sinai, Mungu akawapa amri kumi na sheria ya Musa. Wakati huo wakawa ni ufalme wa Mungu. Wakaamriwa kufanya hema maalum, waliita hema ya kukutania ambapo Mungu aliabudiwa. Walipewa kuhani mkuu na makuhani ambao wanaweza kutoa dhabihu kwa Mungu. Asili yote ya hiyo masikani na ukuhani vililenga mbele kwa ujio wa Yesu.

**NCHI YA AHADI** hatimaye waliisogelea, Wapeleezi 12 walitumwa, kumi kati yao walirudi wakisema ni vigumu kuimiliki nchi ya Kanaani. Wapelelezi wengine wawili Yoshua na Kalebu, walisema ukweli - kwamba nchi wataitamalaki, ikiwa wanaamini

ahadi za Mungu. Kwa sababu watu walishiriki mwenendo wa wapelelezi kumi, Israeli ikabidi wazunguke jangwani kwa miaka 40 hata wale wote waliokuwa na umri wa miaka 20 na zaidi walipotoka Misri walipokufa.

**YOSHUA** alimfuata Musa kuongoza wana Israeli kuingia nchi ya Kanaani mji wa kwanza kutawaliwa ulikuwa Yeriko, ambao Rahabu aliishi, kisha Ai. Mara walipowekwa katika nchi, waliongozwa kwa vipindi vya WAAMUZI, ingawa Mungu alikuwa mfalme wao wa kweli. Hawa ni pamoja na watu kama Gideoni, Yefta na Samsoni. Wote waliwakomboa Israeli toka mikononi mwa adui zao, walipotubu kumkosea Mungu.

Historia ya Israeli ina mifano iliyojaa tele ya Israeli kutokumtii Mungu wakaadhibiwa na uvamizi wa Mataifa yaliyo kando kando, wakitubu dhambi zao Mungu aliwaokoa - na kisha wakaendelea kutenda dhambi tena. Mwamuzi wa mwisho alikuwa ni Samweli. Katika kipindi chake, watu wa Israeli walimkataa Mungu kuwa mfalme wao walipoomba wapewe mfalme mwanadamu, kama mataifa yaliyowazunguka.

**WAFALME.** Mfalme wao wa kwanza aliitwa Sauli ambaye ingawa alianza vema, aligeuka kuwa mtu mbaya, aliasi amri za Mungu, na kumtesa Daudi. Baada ya kifo chake, Daudi akawa mfalme aliyefuata, alikuwa mtu bora wa Israeli. Mungu akafanya ahadi kubwa kwake. Baada yake akaja mwanae Suleimani ambaye baada ya kuanza vizuri aliiacha imani ya kweli kwa sababu ya kuoa wanawake wageni wengi toka mataifa yaliyowazunguka. Baada yake ufalme uligawanyika sehemu mbili - Kabila kumi wakafanywa ufalme wa Israeli, ulianza chini ya Yeroboamu; kabila zingine mbili, Yuda na Benjamini, zikaunda ufalme wa Yuda, ulianza chini ya Rehoboamu, mwana wa Suleimani.

Ufalme wa Israeli (kabila kumi ) haukuwa na mfalme yeyote mzuri. Daima walikuwa ni waasi juu ya Mungu. Alitumia manabii wengi kuwasihi watubu, bali hawakutaka.Kwa hiyo Waashuru wakawahusuru, na kuwatwaa kwenda utumwani. Walitawanyika ulimwenguni pote.

Ufalme wa Yuda (kabila Mbili) ulikuwa na wafalme wazuri wachache (yaani, Asa na Hezekia), Lakini, hata wao pi hawakumtiii Mungu. Wakaldayo wakatumwa kuvamia, wakawachukua utumwani Babeli; kwa muda wa miaka 70. Hawakuwa na mfalme tena. Baada ya miaka 70 wengine walirudi nchini Israeli chini ya uongozi wa Ezra, Nehemia, Yoshua (kuhani mkuu wakati ule) na Zurubabeli mtawala. kwanza walitawaliwa na Waajemi, kisha Wayunani na mwishowe Warumi. walikuwa chini ya Waroma Yesu alipozaliwa. Kama tokeo la kumkataa Yesu Wayahudi, Mungu alituma Waroma kuungamiza Yerusalemu mnamo mwaka 70 B.K, na hatimaye Wayahudi wote walitolewa katika nchi ya Israeli.

Kwa miaka ya karibuni , Wayahudi wameanza kurudi katika nchi , ni kutimia nusu kwa unabii wa Agano la Kale. Kufufuka kwa Serikali ya Israeli ni ishara ya kweli kuwa Yesu atarudi tena ufalme wa Israeli ukiwa ni ufalme wa Mungu.

**Somo La 5 : Maswali**

1. Ni upi ufuatayo ni muda wa kuwekwa kwa ufalme wa Mungu ?

a) Daima umeisha wekwa

b) Kristo akirudi
c) Siku ya Pentekoste katika karne ya kwanza
d) Mioyoni mwa waaminio wanapoongoka.

2. Je ! Ufalme wa Mungu uliwahi kuwepo zamani ? kama ndivyo kwa namna gani ?

3. Ni lini uliisha ?

4. (Millenia Kikwi) ni nini ?
a) Utawala wa neema mioyoni mwetu
b) Utawala wa miaka 1000 ya waaminio mbinguni
c) Utawala wa miaka 1000 ya shetani duniani
d) Miaka 1000 ya kwanza ya Ufalme wa Mungu ujao duniani

5. Ufalme utakuwa ni wa namna gani ?

6. Waamini waliopo watafanya nini katika (Milenia -Kikwi)
a) Watakuwa juu ya watu waliokufa
b) Watatawala mbinguni
c) Hatujui
d) Wataishi kwenye Sayari nyingine

7. Je ! Ujumbe kuhusu Ufalme wa Mungu ulihubiriwa:
a) Katika Agano Jipya tu
b) Yesu na mitume basi
c) Sehemu zote mbili Agano la Kale na Jipya
d) Katika Agano la Kale peke yake.

# *SOMO LA 6*

# MUNGU NA UBAYA

## 6.1 Mungu Na Ubaya

Madhehebu mengi ya mataifa ya Kikristo, sambamba na dini nyingine nyingi wanaamini kwamba kuna kiumbe au mtu asiye wa kawaida aitwaye Ibilisi au shetani ambaye ni Muasisi wa matatizo yaliyomo ulimwenguni na katika maisha yetu, na ni anayehusika na dhambi tunazotenda. Ni wazi Biblia inafundisha kuwa Mungu ni mwenye nguvu zote. Tumeona somo la 1.4 kuwa Malaika hawatendi dhambi. Ikiwa kweli tunaamini mambo haya, basi haiwezekani kuwa yupo kiumbe asiyewakawaida anayefanya kazi hapa ulimwenguni anayepingana na mwenyezi Mungu. Kama tunaamini kuwa huyu kiumbe yupo, basi tunahoji ukuu wa Mungu mwenyezi. Toleo hili ni la lazima sana ya kuwa kumfahamu vema Ibilisi na shetani inabidi fundisho la muhimu lipimwe; Tumeambiwa kuwa Yesu alimharibu Ibilisi katika Ebra. 2: 14 kwa kifo chake; kwa hiyo tusipomwelewa vema Ibilisi, hatuwezi kuelewa kazi ya Yesu, au Yesu ni nani.

Katika ulimwengu kwa ujumla, hasa unaoitwa ulimwengu wa'Kikristo', lipo wazo la kuwa mambo mema katika maisha yanatoka kwa Mungu na mambo mabaya yanatoka kwa Ibilisi au shetani. Hili sio wazo jipya; sio wazo pekee lililokomea kwenye ukristo uliokengeuka. Kwa mfano, Wakaldayo, waliamini kuwepo Mungu wawili, Mungu wa mema na nuru na Mungu wa uovu na giza, na kwamba walishikana katika kupingana sana. Koreshi, Mfalme mkuu wa Uajemi, naye aliamini hivi. Basi Mungu akamwambia, "Mimi ni BWANA, wala hapana mwingine; zaidi yangu mimi hapana Mungu ….. mimi naumba nuru, na kuumba (kuhuluku ) giza: Mimi nafanya suluhu, na kuhuluku ubaya (uovu) - B.H.N -"balaa": Mimi BWANA, niyatendaye haya yote" (Isa. 45: 5-7, 22). Mungu anafanya amani, na ubaya,au balaa. Mungu ni muumba"Ubaya"Kwa maana hii ipo tofauti kati ya ubaya na dhambi,hivi ni kosa la binadamu; Vimeingia ulimwenguni kama tokeo la binadamu, sio Mungu (Rum. 5:12).

Mungu anawaambia Koreshi na watu wa Babeli kuwa "hayupo Mungu (mwingine) zaidi yangu"Neno la Kiebrania lililotafsiriwa'EL' na kuwa Mungu kwa ukubwa maana yake'nguvu au chanzo cha uweza'. Mungu anasema kwamba hakuna chanzo cha uweza kilichopo mbali ya yeye. Hii ndiyo sababu kwa nini mwamini wa kweli kwa Mungu hawezi kukubali wazo la kuwepo Ibilisi asiyewa kawaida au mapepo.

**MUNGU: MLETA BALAA**

Biblia imejaa mifano jinsi Mungu aletavyo "Ubaya" kwa maisha ya watu na katika ulimwengu huu. Amosi 3:6 anasema kwamba ukiwapo ubaya mjini, ni Mungu amefanya. Kwa mfano, kama likiwepo tetemeko la ardhi katika mji, mara nyingi imedhaniwa kwamba Ibilisi amepanga juu ya mji huo, na kuleta

msiba mkuu. Lakini mwamini wa kweli inampasa afahamu kwamba ni Mungu anayehusika na tukio hili.

Basi Mika 1:2 anasema kwamba "msiba -ubaya umeshuka toka kwa Bwana umefika mpaka lango la Yerusalemu". Katika kitabu cha Ayubu tunasoma jinsi Ayubu, mtu mwenye haki, alivyopoteza vitu alivyokuwa navyo katika maisha yake. kitabu kinafundisha kwamba kupata 'Ubaya' katika maisha ya mtu sio moja kwa moja ni kipimo kwa utii wao au uasi juu ya Mungu. Ayubu aligundua hilo "Bwana alitoa, na Bwana ametwaa" (Ayubu. 1:21). Hasemi Bwana alitoa na shetani ametwaa. Alifafanua kwa mke wake: Je ? tupate me,a mikononi mwa Mungu, nasi (pia) tusipate na mabaya"? (Ayubu. 2:10). Mwishoni mwa kitabu, rafiki zake Ayubu walimfariji kwa habari za huo uovu wote Bwana aliouleta juu yake"(Ayubu. 42: 11; 19: 21; 8: 4). hivyo Mungu ndiye chanzo cha 'Uovu' kwa maana ya kuwa ni wa kwanza kuruhusu matatizo ambayo tunayo katika maisha yetu.

"Maana yeye ambaye Bwana ampenda humrudi ….. kama mkistshimili kurudiwa …. Lakini baadaye huwaleta wao waliozoezwa nayo matunda ya haki yenye amani" (Ebra. 12: 6 - 11). Hii inaonyesha kwamba majaribu ambayo Mungu anatupatia yanatuongoza mwisho kukua kiroho. ni kupinga neno la Mungu juu yake kusema kwamba Ibilisi ni kiumbe anayetulazimisha kutenda dhambi na kutenda yasiyo haki, Wakati huo huo amedhaniwa kuleta matatizo katika maisha yetu ambayo yanatupeleka tupate maendeleo "matunda ya haki yenye amani". Hapa wazo la Orthodox juu ya Ibilisi lakimbilia kwenye matatizo makubwa. Makubwa hasa unapoona maneno kama nimempa shetani watu hao "ili wafundishwe wasimtukane Mungu au" kumtolea shetani mtu

huyo, ili mwili uadhibiwe, na roho iokolewe katika siku ya Bwana Yesu"

(1 Tim. 1:20; 1 Kor. 5: 5). Ikiwa shetani ni kiumbe anayefanya watu watende dhambi na kuwa na matokeo yasiyofaa juu ya watu, ni kwa sababu gani mafungu haya ya maneno yasema'Shetani' kwa nuru ya hakika ? Jibu lipo kwa ukweli kwamba adui,'shetani' au shida katika maisha, mara nyingi inaweza kuleta matokeo ya hakika kiroho katika maisha ya mwamini.

Kama tukikubali kwamba ubaya watoka kwa Mungu, Basi tunaweza kumwomba Mungu afanye jambo lingine kuhusu matatizo ambayo tunayo k. m ayaondoe. Kama hafanyi hivyo, basi, tunajua yametoka kwake Mungu kwa ajili yetu kiroho. Sasa kama tunaamini ya kwamba kuna kiumbe fulani mbaya anayeitwa Ibilisi au shetani anayesababisha matatizo yetu, Basi hakuna namna ya kupatana na mema. Ulemavu, Ugonjwa, Kifo cha ghfla au msiba mkuu uchukuliwe kuwa ni bahati mbaya. Ikiwa Ibilisi ni Malaika mwenye dhambi aliye na nguvu, basi atakuwa ni mwenye nguvu nyingi zaidi yetu, hatutakuwa na kuchagua bali kuteseka mikononi mwake. kwa kuhitilafiana, tunafarijiwa kuwa chini ya uongozi wa Mungu, "mambo yote (katika maisha) hufanya kazi pamoja na wale wampendao katika kuwapatia mema"kwa waamini (Rum. 8:28). Kwa hiyo hakuna kitu kama hiki 'bahati' katika maisha ya mwamini.

**ASILI YA DHAMBI**

Inabidi kusisitiza kwamba dhambi hutoka ndani yetu. Ni kosa letu hata kutenda dhambi. Bila shaka, ingekuwa vema kuamini kuwa halikuwa kosa letu hata tukitenda dhambi. kwa hiyari tungetenda dhambi na halafu kutoa udhuru wenyewe kwa kuwaza kwamba kweli lilikuwa kosa la Ibilisi na ya kuwa lawama kwa dhambi yetu ingewekwa kabisa juu yake. Sio ajabu sana

kwamba katika kesi ya mwenendo mbaya sana, mtu mwenye kosa anaomba msamaha kwa kuwa anasema ya kwamba alishikwa na shetani kwa muda na kwa sababu hii yeye mwenyewe hahusiki. Lakini ni sawa kabisa, udhuru huu dhaifu unahukumiwa kwa sababu hauna msingi kabisa, na mtu anapotishiwa hukumu juu yake.

Tukumbuke kuwa "mshahara wa dhambi ni mauti" (Rum. 6:23); dhambi huleta kifo. Kama sio kosa letu kutenda dhambi, bali ni Ibilisi, Bali Mungu mwenye haki yampasa amwadhibu Ibilisi kuliko sisi. Lakini ukweli ni kwamba tunahukumiwa kwa ajili ya dhambi zetu wenyewe yaonyesha tunahusika kwa dhambi zetu. Wazo la kwamba Ibilisi ni mtu dhahiri aliye nje yetu kuliko kwamba ni jambo la dhambi ndani yetu ni kujaribu kuondoa kuhusika kwa ajili ya dhambi zetu. Lakini huu ni mfano mwingine watu wanapokataa kupatana na Biblia inapofundisha kuhusu mwili wa binadamu: huo kwa asili ni wenye dhambi.

“Hakuna kitu kilicho nje ya mtu ambacho kikimwingia chaweza kumtia unajisi ….. Kwa maana ndani ya mioyo ya watu hutoka mawazo mabaya, Uasherati, wivu, uuaji, uzinzi, tamaa mbaya ….. kiburi, upumbavu: haya yote yaliyo maovu yatoka ndani, nayo yamtia mtu unajisi"(Marko. 7: 15 -23).

Wazo la kwamba kipo kitu fulani nje yetu kinachotuingia na kutusababisha kufanya dhambi halilingani na mafundisho yaliyo wazi ya Yesu hapa. Toka ndani, ya moyo wa mtu, hutoka yote haya mambo mabaya. Hii ndiyo sababu wakati wa gharika, Mungu aliona kwamba "mawazo ya moyo wa mwanadamu ni mabaya tangu ujana wake"(Mwa. 8:21. Yak. 1:14) anatuambia namna tunavyojaribiwa:"Kila mmoja (yaani mwanadamu) hujaribiwa na tamaa yake mwenyewe huku akivutwa na

kudanganywa" Tunajaribiwa kwa tamaa zetu wenyewe, mawazo yetu mabaya; sio kitu kingine chochote nje yetu. "Vita vyatoka wapi, na mapigano yaliyo kati yenu" ?. Yakobo anauliza; "Si humu katika tamaa zenu ?" (Yak. 4:1). Kila mmoja wetu ana majaribu yake binafsi. yanazalishwa na nia zetu mbaya, kwa sababu ni yetu wenyewe. ukweli umesemwa ya kwamba sisi wenyewe ndio adui zaidi mbaya.

Kitabu cha Warumi kwa upana kinahusika na dhambi, asili yake, na jinsi ya kuishinda. Ni muhimu sana kwamba Ibilisi na shetani hawapatikani sehemu walipotajwa katika kitabu hiki; kwa maneno ya kusema kuhusu asili ya dhambi, Paulo hamtaji Ibilisi au shetani. Kwa njia hiyo hiyo'Ibilisi' ni dhana ya Agano Jipya. Kama yupo kiumbe aliye nje anayefanya tutende dhambi, kwa kweli asingetajwa kwa upana katika Agano la Kale ?. Bali upo ukimya wa maana uliokwenda chini kuhusu hili. Taarifa ya kipindi cha waamuzi au Israeli jangwani, zinaonyesha ya kwamba nyakati hizo Israeli walitenda dhambi sana. Lakini Mungu hakuwaonya kuhusu kiumbe mwenye nguvu kuwa atawaingia na kuwafanya watende dhambi. Badala yake, aliwasisitiza kushika neno lake, ili wasivutwe kwenda nje ya mapenzi yake na kuufuata mwili wao (K/Torati 27:9,10; Yoshua 22:5)

Paulo analia:"Ndani ya mwili wangu halikai neno jema …. Kutenda lililo jema sipati ….. Basi kama lile nisilolipenda ndilo nilitendalo, si mimi nafsi yangu nilitendaye, bali ile dhambi ikaayo ndani yangu"(Rum. 7:18 -21). Kutenda kwake dhambi hamlaumu kiumbe aliye nje aitwaye Ibilisi. Anaweka kwenye mwili wake mbaya kuwa ndiko asili ya dhambi:"Sio mimi nafsi yangu, bali ni ile dhambi ikaayo ndani yangu". Basi, nimeona sheria hii (ndani yangu), ya kuwa kwangu mimi nitakaye kutenda lililojema, lipo lililo baya (yaani - ndani) yangu. Hivyo anasema kwamba

kipingamizi cha kuwa kiroho kinatoka kwingine anapoita"dhambi ikaayo ndani yangu". kila mtu mwenye mawazo ya kunia kiroho atafikia kwenye mawazo hayo hayo. Ijulikane ya kwamba hata mkristo mkubwa kama Paulo hakuona badiliko la mwili baada ya kuongoka, wala hakuwekwa kwenye nafasi ambayo hawezi kufanya dhambi.

Makundi ya siku hizi ya "Kiinjili" yanadai kwamba wapo katika nafasi hii ya kutotenda dhambi, kwa hivyo wanamweka Paulo vema ndani ya 'wasiookoka' kwa sababu ya taarifa yake hapa katika Rum. 7: 15 -21. Mistari hii imewaletea shida kubwa kwa madai yao. Daudi, mwingine pasiposhaka mtu mwenye haki, vivyo hivyo alifafanua juu ya mwili wake kabisa mwelekeo wa daima wa dhambi: "Tazama mimi naliumbwa katika hali ya uovu, mama yangu alichukuwa mimba hatiani - dhambini"(Zab. 51:5).

Biblia ipo wazi kabisa kuhusu ukubwa na ubaya wa mwili wa binadamu. Kama hili likikubalika, hakuna haja ya kutafuta mtu wa kufikiriwa aliye nje ya mwanadamu anayehusika na dhambi zetu. Yer. 17: 9 unasema kwamba moyo wa binadamu huwa mdanganyifu kuliko vitu vyote ambapo hauwezi hasa kukubali upana mbaya sana wa dhambi zake. Naye Yesu alitia alama pia mwili wa mwanadamu kwa asili ni mbaya katika Math. 7:11; Mhubiri 9:3 (andiko la Kiebrania) halikuweza kuwa wazi;"Moyo wa wanadamu umejaa uovu", Efe. 4:18 inatoa sababu ya mtu asili ya kutengwa toka kwa Mungu kuwa ni "kwa sababu ya ujinga uliomo ndani yao, kwa sababu ya ugumu wa mioyo yao". Ni kwa sababu ya upofu wa kiroho na ujinga wa mioyo, njia zetu za kufikiri zilizo ndani yetu, ndizo zimetuweka mbali na Mungu. Pamoja na mstari huu, Gal. 5:19 unasema dhambi zetu kuwa ni"Matendo ya mwili"; ni mwili wetu wenyewe, utu wetu kabisa na umbo, ndivyo hutufanya tutende dhambi. Hakuna hata fungu la

maneno linaloeleza asili ya dhambi ndani yetu kuwa zimekuwemo kwa sababu ya Ibilisi aliyeziweka; maelekeo ya dhambi ni mambo mengine ambayo kwa kawaida tunayo tangu kuzaliwa; ni sehemu kubwa ya umbo la mwanadamu.

## 6. 2 Ibilisi Na Shetani

Mara nyingi maneno ya asili ya aya za Biblia yameachwa bila tafsiri. Neno'Shetani' ni neno la Lugha ya Kiebrania ambalo halijabadilishwa, nalo lina maana'adui' wakati 'Ibilisi' - devil ni badiliko la lugha ya Kiyunani - Kigriki 'diabolos', maana yake mwongo, adui au mshitaki. Kama tunaamini ya kwamba shetani na Ibilisi ni kiumbe mwingine aliye nje yetu mwenye kuhusika na dhambi, basi popote atakapotoka upande mmoja hadi mwingine wa maneno haya katika Biblia, yatupasa tuyafanye kumtaja mtu huyu mbaya. Matumizi ya Biblia kwa maneno haya yanaonyesha kuwa yaweza kutumika kama neno linalotaja sifa za kawaida, za kusimulia watu wa kawaida. Ukweli huu unafanya isiwezekane kudhani kwamba Ibilisi na shetani kama yalivyotumika ndani ya Biblia yafanya yenyewe kumtaja mtu mkuu mbaya au kiumbe kilicho nje yetu.

### NENO 'SHETANI' KATIKA BIBLIA

**1 Wafalme 11: 14** imetolewa taarifa ya kwamba "Bwana akamwondokeshea - yaani, aliamsha adui wa Suleimani (neno lile lile la Kiebrania kila mahali limetafsiriwa"Shetani"), Hadadi Mwedomi"."Tena, Mungu akamwondokeshea adui mwingine (Shetani mwingine), Rezoni ….. naye akawa adui (shetani) wa Israeli" (1 Wafal. 11: 23, 25). Hapa haina maana kwamba Mungu aliamsha mtu asiye wa kawaida au Malaika ili awe shetani / adui wa Suleimani; aliwaamsha watu wa kawaida. Math. 16: 22,23

inatoa mfano mwingine. Petro alikuwa anajaribu kumzuia Yesu toka kwenda Yerusalemu kufa msalabani. Yesu aligeuka na kumwambia Petro"Nenda nyuma yangu, shetani ….. huyawazi yaliyo ya Mungu, bali ya wanadamu”. Hivyo Petro aliitwa shetani. Habari ipo wazi kwa kuonekana ya kwamba Kristo alikuwa haongelei Malaika au mtu mbaya sana alipotamka maneno hayo; alikuwa akimsema Petro.

Kwa sababu neno 'Shetani’ lina maana tu adui, mtu mwema, hata Mungu mwenyewe, anawezakuitwa 'shetani’. katika maana hakuna lazima kuwa na dhambi kuhusiana na neno lenyewe. ukubwa wa maana ya dhambi ambalo neno'shetani’ linao kwa sehemu ni kwa ajili ya ukweli kwamba mwili wetu wenyewe ulio na dhambi ni 'shetani’ wetu mkubwa au adui, na kwa sababu pia ya matumizi ya neno katika semi za ulimwengu hutajwa kitu kingine kinachokuwa pamoja na dhambi. Mungu mwenyewe aweza kuwa shetani kwetu kwa njia ya kuleta mitihani katika maisha yetu, au kwa kuchukua hatua kutokana na mwendo mbaya wa matendo tunayoweza kuingia.Lakini ukweli ni kuwa Mungu anaweza kuitwa 'shetani’ haina maana ya kuwa yeye mwenyewe ni mtenda dhambi.

Kitabu cha Samweli na mambo ya Nyakati vina maelezo sambamba yenye matukio aina moja, kama taarifa za Injili zina matukio yale yale lakini zinatumia misemo tofauti. 2 Sam. 24: 1 pameandikwa:"Tena …. Bwana akamtia nia Daudi juu yao - Israeli" ili afanye sensa ya Israeli. Maelezo yaliyo sambamba katika 1 M / Nyakati 21: 1 unasema kwamba"Tena shetani akasimama juu ya Israeli, akamshawishi Daudi kuwahesabu Israeli" Katika fungu moja la maneno Mungu anashawishi, lingine shetani anafanya hivyo. Neno la mwisho ni kwamba Mungu alisimama akiwa 'Shetani’ adui wa Daudi. Alifanya hivyo hivyo

kwa Ayubu kwa kumletea majaribu katika maisha yake, hivyo basi Ayubu alisema kuhusu Mungu:'Umegeuka kuwa mkatili kwangu yaani 'shetani', wanitesa kwa mkono wako wenye nguvu"kimsingi ndivyo asemavyo Ayubu (Ayubu. 30: 21 B. H. N).

## NENO 'IBILISI' KATIKA BIBLIA

Hivyo hata neno 'Ibilisi' vile vile. Yesu akasema, "Sikuwachagueni ninyi kumi na mbili (wanafunzi), na mmoja wenu siye ibilisi ?" Alisema Yuda Iskarioti aliyekuwa mtu wa kawaida. Hakuwa anazungumzia kiumbe binafsi aliye na pembe, au aitwaye 'roho'. Neno 'Ibilisi' hapa anatajwa tu binadamu muovu. 1 Tim. 3: 11 tumepewa mfano mwingine. Wake wa wazee (Mashemasi) wa kanisa hawatakiwi kuwa 'wasingiziaji'; neno la asili la Kigriki hapa ni 'diabolos' ambalo lina maana moja na 'Ibilisi' kila mahali katika Biblia. Paulo alimuasa Tito ya kuwa wanawake wazee katika eklezia wasiwe "wachongezi" au'mashetani' (Tito. 2:3 - B.H.N). Na hivyo hivyo alimwambia Timotheo (2 Tim. 3: 1,3) kuwa "Siku za mwisho …. Watu watakuwa …. Wasingiziaji (Mashetani)". Hii haina maana kuwa watu hawatakuwa watu wa kawaida, bali wataongezeka na kuwa waovu mno. Inabidi yawe wazi kabisa tokana na haya maneno 'Ibilisi' na 'shetani' kutotaja Malaika aliyeanguka toka juu au kiumbe mwenye dhambi nje yetu.

## DHAMBI, SHETANI NA IBILISI

Maneno 'Shetani' na'Ibilisi' hutumika kwa mfano kusimlia maelekeo ya asili yenye dhambi yaliyo ndani yetu tuliyo yasoma katika somo la 6.1. Haya ndiyo 'shetani' wetu mkuu au adui. Pia yamesemwa kana kwamba ni mtu, na kama hivi, yaweza kusemwa kama'Ibilisi' - au adui yetu, msingiziaji kweli. Hivi ndivyo ulivyo 'utu' wetu wa asili - Ibilisi kabisa. Muungano kati ya Ibilisi na nia zetu mbaya - dhambi ndani yetu - vimewekwa wazi

kwenye mafungu kadhaa ya maneno: "Basi, kwa kuwa watoto (sisi wenyewe) wameshiriki mwili na damu, yeye (Yesu) naye vivyo hivyo alishiriki yayo hayo; ili kwa njia ya mauti (yake) amharibu yeye aliyekuwa na nguvu za mauti, yaani, 'Ibilisi' (Ebra. 2: 14). Hapa Ibilisi amesemwa ndiye anayehusika na mauti. Lakini "mshahara wa dhambi ni mauti (Rum. 6:23). Basi, dhambi na Ibilisi inabidi wawe sawa. Yakobo 1: 14 kama hivi anasema kwamba nia zetu mbaya hutujaribu, na kutuongoza kutenda dhambi na hivyo kupata kifo. Mstari huo huo unasema kuwa Yesu alikuwa na mwili wetu ili amharibu Ibilisi. Kutofautiana na, Rum. 8: 3; "Mungu kwa kumtuma mwanae mwenyewe katika mfano wa mwili ulio wa dhambi (mwili wetu wanadamu), na kwa sababu ya dhambi, aliihukumu dhambi katika mwili. Hii inaonyesha kuwa Ibilisi na maelekeo mabaya ya dhambi ambayo kwa kawaida yamo ndani ya mwili wa mwanadamu kwa maana ni mamoja. Ni lazima na muhimu kufahamu kwamba Yesu alijaribiwa kama sisi.

Kutokufahamu vema mafunzo ya Ibilisi maana yake ni kwamba kwa usahihi hatuwezi kuelewa mwili na kazi ya Yesu. Ilikuwa ni kwa sababu tu Yesu alikuwa na mwili wa mwanadamu - Ibilisi ndani yake - hata tumeweza kuwa na tumaini la wokovu (Ebra. 2: 14 -18; 4: 15). Kwa kuzishinda nia za mwili wake mwenyewe, Ibilisi wa Biblia, Yesu aliweza kumharibu Ibilisi juu ya msalaba Ebra. 9:26 unasema kuwa Kristo alifunuliwa "azitangue dhambi kwa dhabihu ya nafsi yake" Ebra. 2:14 unalingana na taarifa ya kuwa Kristo kwa kifo chake amemharibu Ibilisi ndani yake mwenyewe. Kwa kufa kwake Yesu kwa matazamio aliuharibu "mwili ulio wa dhambi"(Rum. 6:6), yaani, mwili wa mwanadamu, dhambi ilifunuliwa katika (umbo la) miili yetu kabisa.
“Atendaye dhambi ni wa Ibilisi" (1 Yoh. 3:8), Kwa sababu dhambi hutoa ruhusa kwa mawazo yetu ya asili (Yak. 1: 14, 15),

kile ambacho Biblia inaita' Ibilisi'."Kwa kusudi hili mwana wa Mungu alidhihirishwa ili azivunje kazi za Ibilisi ni nia zetu, (1 Yoh. 3:8). Kama tupo sahihi kwa kusema kwamba ibilisi ni nia zetu, basi kazi za nia zetu mbaya, yaani, zinazoleta dhambi, tunazo wenyewe. Hizi zimethibitishwa na 1 Yoh. 3:5."Yeye (Yesu) alidhihirishwa ili aziondoe dhambi zetu" Huu unathibitisha kwamba "dhambi zetu" na "kazi za Ibilisi"ni moja. Matendo. 5: 3 huu unatupatia mfano mwingine wa muungano huu kati ya Ibilisi na dhambi zetu. Petro akamwambia Anania:"Kwa nini shetani amekujaza moyo wako ?". Kuwaza jambo fulani baya mioyoni mwetu ni sawa sawa na shetani amejaa mioyoni mwetu. Kama sisi wenyewe tuna jambo baya, k.m. mpango wa dhambi, basi unaanza ndani yetu. Ikiwa mwanamke anazaa watoto, hakai nje yake; mtoto anatoka ndani ya tumbo. Yakobo. 1: 14, 15 anatumia mfano huu kwa kuelezea jinsi tamaa inavyozaa dhambi, ambayo inaleta mauti. Zab. 109: 6 unasawazisha mtu mwenye dhambi na'shetani'; "Uweke mtu mbaya (mkorofi) juu yake: Shetani asimame mkono wake wa kuume"yaani kwa nguvu juu yake (Zab. 110: 1).

**KUTAJA KITU KANA KWAMBA NI MTU**

Ingawa hivyo, kwa haki unaweza kujibu: 'Lakini anasema ibilisi kama mtu !'. Ni kweli kabisa; Ebra. 2: 14 amesemwa "Yeye aliye na nguvu za mauti, yaani, ibilisi". Hata kiasi kidogo cha usomaji wa Biblia chaonyesha kuwa mara nyingi kutaja kitu kama mtu Biblia inatumia sana - kuzungumzia jambo la kuwazika tu kana kwamba ni mtu. Hivyo Mithali 9: 1 hekima anaonekana kama vile ni mtu ameijenga nyumba, na Rum. 6:23 dhambi imelinganisha na Bwana mwenye malipo atoaye mshahara wa mauti. Jambo hili limejadiliwa tena katika kuacha kitambo kilichokuwa kimeandikwa sehemu ya 5. Ibilisi wetu, 'diabolos' mara kwa mara maana yake ni mawazo yetu mabaya.

Hata hivyo huwezi kuwa na Ibilisi wa kuwazika tu; mawazo mabaya ambayo yamo ndani ya moyo wa mtu hayawezi kuwepo kwa kujitenga na mtu; kwa hiyo 'Ibilisi' ametajwa kama vile ni mtu. Mara nyingi dhambi imetajwa kama mtu ambaye ni Bwana (k.m. Rum. 5:21; 6:6, 17; 7:3). Kwa hiyo inaeleweka kuwa'Ibilisi' pia ametajwa kama kiumbe, kwa kuwa vile vile'Ibilisi' inatajwa dhambi. Kwa njia h iyo hiyo, Paulo anasema sisi tuna watu wawili, kama alivyokuwa ndani ya mwili wetu (Rum. 7:5 -12): Utu na mwili,'Ibilisi' anapingana na utu wa Rohoni. Lakini ni wazi hawapo viumbe binafsi wawili wanaopingana ndani yetu. Hii sehemu ya mwili wetu ulio na dhambi imeitwa kama ni mtu "yule mwovu"(Math. 6:13) - Ibilisi wa Biblia. Fungu hilo hilo la maneno katika sentensi ya Kiyunani limetafsiriwa "yule mwovu"kwa usemi wetu limetafsiriwa "yule mbaya"katika 1 Kor. 5:13, yaonyesha kwamba mtu anaporuhusu dhambi, 'yule mwovu' wake yeye mwenyewe - anakuwa ni 'yule mwovu"au 'Ibilisi'.

## 'IBILISI' NA 'SHETANI KATIKA MANENO YA - TAWALA

Maneno haya 'ibilisi' na 'shetani' vile vile yametumika kuelezea uovu, mpangilio wa ulimwengu wenye dhambi tunamoishi. Kijamii, Kisiasa na muungano wa daraja za mamlaka toka chini hadi juu kwa walimwengu wenye dini za uwongo zaweza kuitwa'Ibilisi' kwa maneno. Ibilisi na shetani katika Agano Jipya mara nyingi zinatajwa tawala na nguvu za jamii ya Wayahudi au utaratibu wa Waroma. Tunasoma hivi Ibilisi akiwatupa baadhi ya waaminio gerezani (Uf. 2:10), yatajwa mamlaka ya Waroma ikiwafunga waaminio. Katika maneno haya haya tunasoma habari ya kanisa lililokuwa Pergamo ni kwenye kiti cha shetani, au kiti cha enzi, kilikuwa - yaani mahali pa utawala wa koloni katika Pergamo, Kundi la waaminio. Hatuwezi kusoma shetani

mwenyewe, kama yupo anaishi, binafsi alikuwa na kiti cha enzi Pergamo.

Dhambi ya mtu mmoja mmoja imefafanuliwa kuwa ni kuvunja amri za Mungu (1 Yoh. 3:4). Bali dhambi ikielezwa kwa pamoja kama kisiasa na nguvu ya jamii vikipingana na Mungu ni nguvu yenye uwezo mkubwa kuliko mtu mmoja - mmoja; ni hii nguvu ya pamoja inayoitwa mara nyingine kama vile ni mtu mwenye uwezo mkubwa anayeitwa Ibilisi. Kwa maana hii Irani na mamlaka zingine za Kiislamu zimeita Amerika ni "Shetani mkubwa"- yaani, adui mkubwa kwa lengo lao, Kisiasa na maneno ya dini. Hivi ndivyo maneno 'Ibilisi' na'Shetani' mara nyingi yalivyotumika katika Biblia.

Kwa kumalizia, labda ni kweli kusema kuwa katika jambo hili tunalosema zaidi ya lingine lolote, ni muhimu kuweka fahamu zetu juu ya mtazamo uliowiana wa Biblia nzima, kuliko kujenga mafundisho makubwa kwa mistari michache iliyo na maneno yaliyovuma yanaonekana kutaja imani ya kawaida kuhusu Ibilisi.Somo la 6.1 na sehemu hii kwa makini yanalipa, kwa kuomba kusoma tena. Nafasi ya mafunzo iliyowekwa imeelezea njia pekee ya kuweza kufahamu vema mafungu yote ya maneno yanayotaja vema ibilisi na shetani. Maneno hayo yaweza kutumika kama ni yenye sifa za kawaida, au katika maneno mengine yanataja dhambi ambayo inapatikana ndani ya mwili wake mwanadamu. Baadhi ya mafungu ya maneno ambayo kwa upana zaidi hayaeleweki yaliyonukuliwa kwa kusaidia mawazo ya watu wengi yamepimwa katika sehemu tunayoacha kilichokuwa kinaandikwa inayofuatana na somo hili.

Walio na matatizo ya kukubali maneno yetu wanatakiwa wajiulize wenyewe: (1) Je ! dhambi imeitwa kama vile mtu ?. Ni wazi. (2) Je ! ni kweli kwamba 'shetani' aweza kutumika kama

maneno ya sifa ? Ndiyo. Ni tatizo gani basi, laweza kukubalika kwamba dhambi imeitwa kama mtu kama adui yetu / shetani ?. Ulimwengu mara nyingi umeitwa kama mtu katika nyaraka za Yohana na Injili; ni jina gani bora litumiwe kuliko 'shetani' au'Ibilisi' kwa mtindo huu wa kuita kama mtu ?.

## 6.3 Mapepo - Mashetani

Sehemu mbili zilizotangulia zaeleza sababu zilizotufanya tusiamini kuwa Ibilisi au shetani ni kiumbe binafsi au mtu mkubwa aliye mbaya sana. Kama tunakubali ya kwamba hayupo kiumbe huyu, basi ni kweli kuwa mapepo, ambao wamedhaniwa kuwa ni watumishi wa Ibilisi, vile vile hawapo. Watu wengi wanafikiri ya kuwa Mungu anatupatia mambo mema ya maisha, naye ibilisi na mapepo yake watupatia mambo

mabaya, na wanatunyang'anya mambo mema atupayo Mungu.

Ni wazi Biblia yafundisha kwamba Mungu ndiye chanzo cha nguvu zote (tazama somo la 6.1), na kuwa Yeye ndiye mhusika wa yote mawili mambo mema na mambo mabaya katika maisha yetu: -

"Mimi naumba nuru, na kuhuluku giza. nafanya amani, na kuhuluku ubaya: 'Mimi Bwana ndiye nayafanya yote haya' (Isa. 45: 7);

"Msiba umeshuka toka kwa Bwana, umefika mpaka lango la Yerusalemu" Mika. 1:12;

"Je ! tarumbeta itapigwa mjini, watu wasiogope ? mji utapatikana na hali mbaya, asiyoieleta Bwana?"Amosi. 3:6.

Basi tunapopata majaribu, tufahamu ya kwamba yametoka kwa Mungu, lawama zisipelekwe kwa Ibilisi au mapepo. Ayubu alikuwa ni mtu aliyepoteza vitu vingi vizuri alivyobarikiwa na Mungu, Lakini hakusema, "Mapepo haya yamechukuwa yote aliyonipa Mungu". Hapana; sikiliza alichosema: -

"Bwana alitoa, na Bwana ametwaa; jina la Bwana na libarikiwe"Ayubu. 1:21;

"Je ! tupate mema mkononi mwa Mungu, nasi tusipate mabaya ?"Ayubu 2:10

Mara tukifahamu kuwa mambo yote yatoka kwa Mungu, wakati tuna matatizo katika maisha tunaweza kumwomba Mungu ayaondoe, na kama hafanyi hivyo, twaweza kuwa na hakika ya kuwa anatupatia hayo ili tabia zetu zikue kwa ajili ya faida yetu katika safari ndefu.

"Mwanangu usiyadharau marudia ya Bwana, wala usizimie moyo ukikemewa naye; Maana yeye ambaye Bwana ampenda, humrudi, (sio mapepo). Naye humpiga kila mwana amkubaliye. Ni kwa ajili ya kurudiwa mwastahimili; Mungu awatendea kama wana; maana ni mwana yupi asiyerudiwa na babaye ? Basi kama hamna kurudiwa, ambako ni fungu la wote, ndipo mmekuwa wana wa haramu ninyi, wala si wana wa halali"(Ebra. 12: 5-8).

## MUNGU: CHANZO CHA NGUVU ZOTE

Mungu ndiye chanzo cha nguvu zote: -

“Mimi ni BWANA, zaidi yangu hapana mwingine, hapana Mungu (neno la Kiebrania'Mungu’ maana yake'nguvu au uweza’) zaidi yangu mimi"- Isa. 45: 5

“Je ! yuko Mungu zaidi yangu mimi ? hakika hapana mwamba; mimi sijui mwingine - Isa. 44:8;

“BWANA ndiye Mungu; hapana mwingine ila yeye"- K /Torati 4:35.

Mistari hii inatokea mara nyingi katika Biblia yote. Kwa kuwa Mungu ndiye chanzo cha nguvu zote na Mungu pekee, basi ni Mungu mwenye wivu, kama anavyotukumbusha mara nyingi (k.m Kutoka 20:5; K/torati. 4:24).

Mungu anaingiwa na wivu hapo watu wake wanapoanza kuiamini miungu mingine, kama wakimwambia, ' Wewe ndiye Mungu mkuu, Mungu mwenye nguvu, lakini pia bado naamini wapo miungu wengine mbali na wewe, hata kama si wenye nguvu kama wewe’.Hii ndiyo sababu hatuamini yapo mapepo au Ibilisi yupo sawa na Mungu wa kweli. Hili ni kosa ambalo Israeli walifanya. Mengi yaliyo katika Agano la Kale yametumika kuonyesha jinsi Israeli walivyomchukiza Mungu kwa kuamini Miungu wengine kama yeye. Tutaona toka biblia kuwa "Mapepo"ambayo watu wanayaamini siku hizi ni kiasi kama wale Miungu wa uongo ambao Israeli waliamini kuwa wapo.

## MASHETANI NI SANAMU

Katika 1 Wakorintho, Paulo ameeleza sababu za Wakristo kutotakiwa kujihusisha na ibada za sanamu au kuyaamini mambo haya. Katika nyakati za Biblia watu waliyaamini mapepo kuwa ni

miungu wadogo ambao nao waabuduwe ili wazuie matatizo yasije katika maisha yao. Kwa hiyo walitengeneza aina ya mashetani, ambao walikuwa sawa na sanamu, wakawatumikia. Hii ni kwa nini Paulo anaeleza kwa kutumia maneno "pepo"na "sanamu" kwa kubadilishana katika waraka wake:

"Lakini vitu vile wavitoavyo sadaka watu wa mataifa, wavitoa kwa mashetani, wala si kwa Mungu; nami sipendi ninyi kushirikiana na mashetani ….. lakini mtu akiwaambia, Kitu hiki kimetolewa kiwe sadaka ya sanamu, msile, kwa ajili yake …….." (1Kor. 10:20,28). Hivyo sanamu na mashetani ni maana moja. Tazama jinsi Paulo anavyosema walitoa sadaka "kwa mashetani (sanamu) si kwa Mungu" - Mashetani hawakuwa Mungu, kwa kuwa yupo Mungu mmoja, kinachofuata ni kwamba mashetani hawana uwezo wowote wa kweli kabisa, Si Miungu. Sababu hasa inatoka katika 1Kor. 8:4:-

"Basi …… vitu vilivyotolewa sadaka kwa sanamu; twajua kuwa sanamu si kitu katika huu ulimwengu, na ya kuwa hakuna Mungu ila mmoja" Sanamu, au mashetani hayaishi kabisa. Yupo Mungu mmoja wa kweli tu, au uweza, ulimwenguni. Paulo anaendelea katika (mst. 5,6): -

"Ijapokuwa wako waitwao miungu …….. (kama vile walivyoko miungu mingi na mabwana wengi), (kiasi kama watu wanavyoamini kuwepo aina nyingi za mashetani siku hizi - shetani mmoja asababisha upoteze kazi yako, na mwingine asababishe mkeo au mumeo akuache,n.k) Lakini kwetu (waaminio wa kweli) Mungu ni mmoja tu, aliye Baba, ambaye vitu vyote vimetoka kwake (Vitu vibaya na vizuri, kama tulivyokwisha ona maana zilizotolewa awali)"

Ushahidi zaidi ambao watu wa nyakati za Agano Jipya waliamini mashetani kuwa ni sanamu au ' miungu' unapatikana katika matendo 17: 16 -18: huu unaeleza jinsi Paulo alivyohubiri katika mji wa Anthene, ambo ulikuwa umezungukwa na sanamu, kwa hiyo wakizitumikia sanamu za aina mbalimbali Baada ya kumsikia Paulo akihubiri Injili, watu wakasema,"Aonekana kuwa mtangaza habari za miungu migeni (mashetani): Kwa maana alikuwa akihubiri habari za Yesu na ufufuo. Watu walidhani kwamba "Yesu"na"ufufuo"walikuwa mashetani wapya au sanamu ambazo walielezewa. Kama ukisoma sura yote, utaona Paulo jinsi alivyoendelea kufunza ukweli wetu hawa, na katika mstari 22 anasema, "ninyi ni watu wa kutafakari sana mambo ya dini"(yaani, mnajitoa sana kuwatumikia mashetani), akawaeleza jinsi Mungu asivyokuwamo katika mashetani yao, au sanamu. Kumbuka kwamba Mungu ndiye muasisi wa nguvu zote. Kama hayumo katika mashetani, basi mashetani hawana uwezo wowote kwa sababu hakuna chanzo kingine cha uweza katika ulimwengu huu - yaani, hawaishi.

## 'MASHETANI' WALIO KATIKA AGANO LA KALE ZILIKUWA NI SANAMU

Tukirudi kwenye Agano la Kale, upo ushahidi zaidi kuwa "mashetani"ni mamoja kama sanamu. Katika K/torati 28:22 -28, 59 -61 yalitabiriwa magonjwa ya akili kuwa moja ya adhabu kwa ajili ya kutumikia sanamu /mashetani. Huu unabii waeleza muungano wa mapepo na magonjwa ya akili katika Agano Jipya. Lakini ijulikane ya kwamba msemo wa mashetani au mapepo umeungana na maradhi, sio dhambi. Hatusomi kuwa Kristo alitoa mashetani au mapepo ya husuda, uuaji n.k. Inabidi pia ieleweke kwamba Biblia inapowasema watu wenye pepo / maradhi si

kusema mashetani yaliyosababisha maradhi. Ni muhimu kujua kuwa tafsiri ya kiyunani ya Agano la Kale (Septuagint) neno lililotumika ni 'daimonion' kwa maana ya'Sanamu' katika K/torat. 32: 17 na Zab. 106: 37 hili ndilo neno lililotafsiriwa'pepo' katika Agano Jipya. Zaburi 106: 36 -39 yaelezea makosa ya Israeli na kulinganisha sanamu za Kanaani na mashetani: -

"(Israeli) wakazitumikia sanamu zao; nazo zikawa mtego kwao. Naam, walitoa wana wao na binti zao kuwa sadaka kwa mashetani, wakamwaga damu isiyo na hatia, damu ya wana wao na binti zao, waliwatoa dhabihu kwa sanamu za Kanaani ….. Ndivyo walivyotiwa uchafu kwa kazi zao, wakafanya uasherati kwa matendo yao".

Ni wazi kabisa pepo /mashetani ni jina lingine tu la sanamu. Wao kutumikia mashetani Mungu amesema ni kuabudu"Kazi zao"wenyewe …….. na ni matendo yao kwa sababu imani ya juu ya mashetani ilitokana na fikra za mwanadamu; sanamu zilizoundwa zilikuwa ni'Kazi zao' wenyewe.

Hivyo hao ambao siku hizi wanaamini kuwa yapo mashetani / pepo wanaamini mambo ambayo yamefikiriwa na watu uumbaji wa watu, sivyo ambavyo Mungu alivyofunza.

Kumbukumbu la Torati 32: 15 -24 laeleza ni kiasi gani Mungu anakasirika watu wake wanapoamini mashetani:"Israeli akamdharau mwamba wa Wokovu wake. Wakamtia wivu kwa miungu migeni, wakamkasirisha kwa machukizo. Walitoa sadaka kwa pepo, si Mungu, kwa miungu wasiowajua, kwa miungu mipya iliyotokea siku zilizo karibu, ambayo baba zenu hawakuiogopa …... (Mungu) akasema, Nitawaficha uso wangu …… maana, ni kizazi cha ukaidi mwingi, watoto wasio imani ndani yao.

Wamenitia wivu kwa kisicho Mungu; wamenikasirisha kwa ubatili wao …… nitaweka madhara juu yao chungu chungu".

Hivyo Mungu anasema mashetani ni sanamu, machukizo, na ubatili - mambo ambayo haifai kuyaamini, hayana uhai. Kuamini kwamba mashetani yapo ni kukosa imani ya kusadiki kwa Mungu. Sio rahisi kuamini kuwa Mungu anatoa kila jambo, pande zote mbili, baya na jema, katika maisha. Ni vyepesi kudhani kuwa mambo mabaya yanatoka kwa mwingine, Kwa sababu mara tukisema yanatoka kwa Mungu, basi tutakuwa tumwamini Mungu kwamba mambo mabaya atayaondoa au ni kwamba yatakuwa ni yenye faida kwa hatima yetu.

## MASHETANI / PEPO WALIO KATIKA AGANO JIPYA

Lakini, waweza kusema,"Ni vipi mafungu yote ya maneno yaliyomo katika Agano Jipya ambayo ni dhahiri yasema habari za pepo ?".

Kwa jambo moja yatupasa tuwe wazi: Biblia haiwezi kupingana yenyewe, ni neno la Mungu mwenyezi. Ikiwa ni wazi tumeambiwa kuwa Mungu ndiye aletaye matatizo yetu na kwamba yeye ndiye muasisi wa nguvu za aina zote, basi Biblia vile vile haiwezi kutuambia kuwa pepo - Miungu wadogo washindanao na Mungu - hutuletea mambo haya sisi. Ni jambo la maana kujua kwamba Neno'pepo' linaonekana kutokeza mara nne katika Agano la Kale na daima laelezea kutumikia sanamu, bali limetokea mara nyingi katika taarifa za Injili. Tunadokeza hii ni kwa sababu, wakati Injili zilipokuwa zikiandikwa, ulikuwa ni msemo wa siku zile kuusema ugonjwa wowote ambao haukufahamika ulikuwa ni sababu ya mapepo. Kama kweli pepo wanaishi nao wahusika na kuugua na matatizo yetu, basi

tungesoma habari zake zaidi katika Agano la Kale. Bali hatusomi taarifa zake kabisa fungu hili la maneno katika sentensi humo.

**PEPO KATIKA AGANO JIPYA.**

Kusema kuwa pepo walikemewa na mtu ni kusema ya kwamba maradhi ya akili yaliponywa, au ugonjwa ulipokuwa haueleweki muda huo. Watu walioishi karne ya kwanza kwa kila kitu ambacho hawakukifahamu walielekeza lawama juu ya viumbe wa kuwazika waitwao'pepo'. Maradhi ya akili yakiwa ni shida kuyaelewa kwa usawa wao wa elimu ya Kitabibu, watu waliwasema wale wenye shida kuwa'Walipagawa na pepo'. Kwa nyakati za Agano la Kale, Roho mbaya au mchafu ilikuwa inatajwa hali ya akili iliyotaabika (Amu. 9: 23; 1 Sam. 16:14; 18: 10). Kwa nyakati za Agano Jipya, msemo wa roho chafu / kupagawa na pepo ulifikia kuwasema waliokuwa wanasumbuliwa na maradhi ya akili. Muunganiko kati ya pepo na ugonjwa umeonyeshwa kama ifuatavyo:"Wakamletea (Yesu) wengi wenye pepo: akawatoa pepo kwa neno lake …… ili litimie lile neno lililonenwa na nabii Isaya (Katika Agano la Kale) akisema, mwenyewe aliutwaa udhaifu wetu, na kuchukua magonjwa yetu"(Math. 8: 16, 17). Hivyo udhaifu na magonjwa ya mwanadamu ni mamoja na kupagawa na "pepo"na "Roho wachafu".

Watu walimdhania Yesu alikuwa na wazimu na walisema hii inabidi iwe ni kwa sababu alikuwa na pepo -"Ana pepo huyu, tena ana wsazimu"(Yoh. 10: 20; 7:19, 20; 8: 52). Kwa hiyo waliamini kwamba pepo walileta wazimu.

**KUPONYA UGONJWA**

Walipoponywa, watu "waliokuwa na pepo"wanasemwa walirudi kuwa na "Akili zao timamu" - Marko. 5:15; Luka 8: 35. Hii inadokeza ya kuwa "kupagawa na pepo"ni njia nyingine ya kusema mtu fulani si mzima kiakili - yaani, hana akili timamu.

Wale "waliokuwa na pepo"wamesemwa "waliponywa"au "alikemea"- Mathayo. 4:24; 12: 22; 17: 18 - husema kwamba kuwa na pepo ni njia ya kueleza ugonjwa.

Katika Luka 10:9 Yesu aliwaambia mitume wake 70 kwenda "kuponya wagonjwa", walifanya hivyo walirudi na kusema, mst wa 17,"hata pepo wanatii kwa jina lako"- tena, pepo na magonjwa yamelinganishwa. wakati mwingine mitume walikemea watu kwa jina la Yesu na hapa tuna mfano huu (tazama pia Matendo 3: 6; 9: 34).

## MSEMO WA SIKU ZILE

Basi tunaona kwamba katika Agano Jipya ulikuwa ni msemo wa siku zile wa kusema mtu mwingine kuwa ana pepo ikiwa walikuwa wagonjwa wa akili au walikuwa na ugonjwa ambao hakuna aliyeufahamu. Warumi wa wakati ule na Wayunani malezi ya imani yao ilikuwa kwamba watu waliokuwa na pepo, kwa sababu hii walipata ugonjwa wa akili. Hao "Wakristo" Waaminio kuwepo kwa pepo wana maana ya kusema kwamba imani za kipagani za wakati ule kwa eneo hili zilikuwa sahihi kabisa. Biblia imeandikwa kwa Lugha ambayo watu wanaweza kuielewa. Kwa sababu inatumia msemo wa siku hizo haina maana kwamba yenyewe au Yesu aliamini kuwepo mapepo. Kwa njia hiyo hiyo kwa Kiswahili tuna neno 'kupigwa na mwezi' huwa ni kueleza mtu mwenyewe wazimu wakati mwezi ukiwa mchanga. Miaka ya zamani watu waliamini kwamba mtu akitoka nje wakati wa usiku

nuru ya mbalamwezi ikiwa inang'aa, wanaweza kupigwa na mwezi na kupata ugonjwa wa akili.Tunatumia neno hilo 'kupigwa na mwezi' siku hizi ni kusema mtu aliye na wazimu, lakini haina maana kwamba tunaamini wazimu unasababishwa na mwezi.

Ikiwa maneno haya yaliandikwa na kusomwa tena kwa kipindi cha miaka 2000 - Yesu kama hajarudi - watu watafikiri tuamini kwamba mwezi huleta wazimu, Lakini watakosea kwa sababu tunatumia msemo wa siku zetu tu, kama Yesu alivyofanya miaka 2000 iliyopita.

Ni dhahiri kwamba Yesu hakuzaliwa tarehe 25 Desemba; lakini mwandishi wa sasa bado anatumia neno'Siku ya Krismasi' inaposemwa siku hiyo, ingawa siamini kwamba tusherehekee siku ya kuzaliwa Kristo. Majina ya siku za juma yamewekwa juu ya kuabudu sanamu ya kipagani - k.m.'Jumapili' maana yake'siku iliyotolewa kuabudu jua'; 'Jumamosi' ilikuwa ni siku ambayo sayari ya Saturn ya sita toka kwenye jua ilikuwa iabudiwe, Jumatatu kwa ajili ya mwezi n.k. Kutumia majina haya haina maana kwamba tunashiriki katika imani za kipagani za hao wa kwanza kuvumbua misemo yetu ya sasa. Vile vile 'Influenza au flu' - Makamasi - mafua ni majina yatumiwayo kwa pamoja siku hizi; maana yake 'aliyevutwa na pepo'.Danieli alipoitwa jina lingine'Belteshaza' jina lenye maana ya Mungu wa kipagani, taarifa iliyovuviwa katika Dan. 4: 19 yamwita'Belteshaza' bila kuonyesha kuwa hili jina linaonyesha fikira potofu. Nasema kuhusu'Papa' kama njia ya kumtambulisha mtu, ingawa nadhani ni kosa hasa kuamini kwamba ni 'papa' au baba (Math. 23: 9).

Ilikuwepo hadithi ya uongo katika kipindi cha Ezekieli ya kwamba nchi ya Israeli ilihusika na balaa kwa walio ndani yake. Hii haikuwa kweli, hata hivyo Mungu alihojiana na Israeli,

akitumia wazo lililokuwa wakati ule na watu wengi, "Bwana MUNGU asema hivi; Kwa kuwa watu hukuwaambia, wewe nchi u mwenye kula watu, nawe umekuwa mwenye kufisha watu wa taifa lako; basi (wewe nchi) hutakula watu tena, asema Bwana Mungu"(Ezek. 36: 13, 14). Lilikuwepo wazo la mazoea ya kipagani la kuwa bahari ilikuwa ni mtu mkubwa na mbaya sana atakaye kuimeza dunia. Wakati hii ni dhahiri siyo kweli, mara nyingi Biblia inatumia mfano huu ili kusaidia usomaji wake wa kuanza kupata kuelewa jambo lililoonyeshwa: Ona Ayubu.7: 12; Amosi. 9: 3; Yer. 5: 22; Zab.89: 9; Habakuki 3:10; Math. 14:24; Marko. 4:30 (neno la Kiyunani); Hadithi za Waashuri waliita mnyama huyu mkaidi wa baharini 'Rahabu' na hili ndilo jina hasa alilopewa mnyama wa bahari ya Misri katika Isa. 52: 10.

Kwa kuwa Biblia imevuviwa na Mungu, haiwezekani kwamba Biblia yaeleza tu ushawishi wa kipagani uliokuwa ukitumika kwenye kipindi ilipoandikwa. Inabidi iwe kwamba Mungu alikuwa anafahamu kutaja imani za wakati ule ule, ili kuonyesha kwamba Yeye ni muasisi wa nguvu; ndiye pekee anayemtawala'mnyama mkubwa' wa bahari, kwa matokeo anafanya mapenzi yake. Kwa sababu hii Mungu alisahihisha kosa kubwa la imani za watu hawa, ambazo zilikuwa kwamba zilikuwepo nguvu zingine zikifanya kazi ulimwenguni ambazo haziko chini ya mamlaka ya Mungu, na kwa hiyo kwa kuzisema zilikuwa mbaya. Ingawa hivyo, kwa mfano huu, Biblia haiachi njia yake kujaribu kuondoa upumbavu wa kuamini kwamba kuna mnyama mkubwa anayejificha baharini, au kuwa bahari ni mnyama .

Mfano mwingine ni maelezo ya radi na dhoruba ya mawingu kuwa ni "nyoka aendaye mbio" (Ayu. 26: 13 Isa. 17: 1 ). Kwa uwazi huu alikuwa anataja imani za wapagani wa siku zile kuwa radi na muundo wa wingu litishalo yalikuwa hasa ni maono ya

nyoka mkubwa. Maneno haya hayabainishi ujinga wa wazo hili, au jarabio la kuelezea kisayansi. Mwenendo wa Kristo kwa imani iliyoenea ya pepo kwa sababu hii ulikuwa ule ule; miujiza yake ilibainisha kwamba uweza wa Mungu ulitimilika kabisa, haukufungwa na imani za uongo wa watu kuhusu yaitwayo 'pepo'.

Hao wanaoamini kwamba Agano Jipya limeandika habari za ' pepo' ili kuthibitisha viumbe hawa wanaishi kwa kweli ni kazi inayoelekea kukubali kuwa bahari kweli ni mnyama, na ya kuwa radi ni joka mkubwa hasa. Hii kweli ni maana yenye nguvu; inabidi ijulikane kwamba Biblia inatumia lugha ya siku zile ambayo ilitumika kuandikwa, bila ulazima wa kusaidia imani zinazofanya msingi wa msemo huo. Tumeonyesha matumizi yetu ya lugha kuwa ni mamoja. Biblia yafanya hivi ili kuthibitisha aina ya ukweli wenye msingi tuliouona katika masomo ya 6.1 na 6.2 - ya kwamba Mungu ni mwenye nguvu zote; Anahusika na majaribu yetu; dhambi hutoka ndani yetu - mambo yote haya yanaweza kuleta maana ya kukubali ukuu wa uweza wa Mungu kuokoa. Waitwao 'Watafiti wakuu' daima wanachimbua vitu ardhini vinavyounga kati ya msemo wa maandiko na imani na mawazo ya tamaduni zinazozunguka ambazo Biblia ilivuviwa na kuandikwa taarifa. Hizi zinaeleweka, mara ikieleweka kwa matumizi ya lugha ya Biblia inayoweza kutaja kwa kuandikwa imani ya mahali, lakini yafanya hivyo ili kumaanisha kwamba Yahweh, Mungu wa kweli wa pekee, ni mkuu sana kuliko imani hafifu za watu ambazo zilijulikana kwa wale waliosoma kwanza maneno yaliyovuviwa, mapya toka Kiywani mwa nabii.

Jambo hili likiwa moyoni inastajaabisha kuweza kupata mifano mingi kiasi gani katika Agano Jipya la msemo wa siku zile ulivyotumika bila msemo huo kusahihishwa. Hapa kuna mifano mingine: -

• Mafarisayo walimshutumu Yesu kufanya miujiza kwa nguvu za Mungu wa uongo aitwaye Beelzebuli. Yesu alisema "Na mimi nikitoka pepo kwa Beelzebuli, Je ! wana wenu watoa kwa nani ?"(Math. 12: 27). Kitabu cha 2 Fal. 1:2. kwa kubainisha kinatuambia kwamba Beelzebuli alikuwa ni Mungu potofu wa Wafilisiti. Yesu hakusema, 'Sasa tazama, 2 Wafalme 1: 2 kinasema Baal-zebubu alikuwa mungu wa uongo, hivyo mashutumu yenu hayawezi kuwa ya kweli'. Hapana, alisema kana kwamba Beelzebuli aliishi, kwa sababu alipendezwa kuupata ujumbe wake kwa kupitia kwa watu ambao aliwahubiri habari njema. Basi kwa njia hiyo hiyo Yesu alisema kuhusu kutoa / kukemea pepo - na kuendelea kusema, 'kweli wapo' alihubiri tu injili kwa msemo wa siku zile.

• Matendo 16: 16 -18 ni maneno ya Luka, chini ya kuvuviwa:"kijakazi aliyekuwa na pepo wa uaguzi akatukuta". Mstari huu kama ulivyoelekezwa kwa maelezo machache chini ya kitabu chenye tafsiri ya Diaglott huyu kijakazi katika kufanya uaguzi alikuwa na chatu - huyu nyoka ameitwa Python - nalo lilikuwa ni jina la Mungu wa uongo aliyeaminika kipindi cha karne ya kwanza, yawezekana alikuwa ni sawa na Mungu Apollo. Ni dhahiri chatu - python hakuwa hai, lakini Luka hasemi huyu msichana alikuwa na roho ya python, ambaye ni Mungu wa uongo asiyeishi. Kwa maana hiyo hiyo Injili haisemi kwamba Yesu 'alikemea pepo' ambao wapo, ni Lugha tu ya siku zile kwa ajili ya kutaja ugonjwa.

• Luka. 5: 32 unatoa taarifa Yesu aliwaambia Wayahudi wabaya:"Sikuja kuwaita wenye haki ……." Alikuwa anafahamu kwa kusema'Sikuja kuwaita hao wanaoamini wao ni wenye haki'. Lakini Yesu alizungumza nao kwa maneno yao wenyewe, hata

kama, kwa maneno ya ustadi, alikuwa anatumia yasio kweli. Luka. 19: 20 -23 yaonyesha Yesu akitumia maneno yasio kweli ya mtu mwenye talanta moja katika mahubiri ya mfano ya kuhojiana naye, lakini hasahihishi maneno potofu yaliyotumiwa na huyo mtu.

- Mara nyingi Biblia inasema jua ' lilichwa' na 'mawio'; hii ni njia ya kibinadamu kusema hivyo, lakini kisanyansi sio sahihi. Vivyo hivyo ugonjwa unaosemwa kwa ustadi wa Lugha "isiyosahihi"kutaja 'pepo' Matendo 5: 3 inaema jinsi Anania alivyomdanganya Roho Mtakatifu. Kwa kweli haiwezekani, lakini kile Anania alichofikiria kufanya kimesemwa kama kweli; hata kama haikuwa hivyo.

- Ipo mifano mingi ya Biblia na misemo iliyotumika ambayo ilieleweka wakati ule ilipoandikwa, lakini sasa ni migeni kwetu, kwa mfano,'ngozi kwa ngozi' (Ayubu. 2: 4) mfano huu ulitaja mazoea ya Kale ya biashara ya ngozi ya thamani sawa; kahaba mwanaume ameitwa"Mbwa"katika K/ torati 23: 28. msemo wa pepo ni mfano mwingine.

- Wayahudi wa zama za Kristo walidhani kwamba walikuwa ni wenye haki kwa sababu walikuwa ni watoto wa Abrahamu. Kwa hiyo Yesu aliwahutubia kuwa ni 'wenye haki' (Math. 9: 12,13) na kusema "najua ya kuwa ninyi ni uzao wa Ibrahimu"(Yoh. 8:37). Lakini hakuamini kwamba walikuwa ni wenye haki, kama alivyobainisha hivyo mara nyingi; wazi wazi alionyesha kwa kutoa hoja katika Yh. 8: 39 - 44 ya kuwa hawakuwa uzao wa Ibrahimu. Basi Yesu alichukua imani za watu zilivyo pasipo kuwapinga mara moja, lakini alieleza kwa kuonyesha ukweli badala yake. Tumeonyesha ya kuwa hivi ndivyo mungu alivyokaribiana na kushughulika na imani za kipagani zilizokuwa zimeenea nyakati za Agano la Kale.

Mwenendo wa Kristo kwa pepo wa Agano jipya ulikuwa hivyo hiyvo; miujiza yake aliyopewa na Mungu ilibainisha sana kuwa maradhi yalisababishwa na Mungu. Sio nguvu yoyote ingine kwa kuwa ni Mungu aliyekuwa ni mwenye uweza kuwaponya.

- Paulo aliyanukuu mashairi ya Wayunani, mashuhuri kwa upuuzi wa maneno yasiyo ya Biblia yaliyosukasuka, ili kuwashangaza wale waliyoyaamini mashairi yalichofundisha (Tito 1: 12; Mdo. 17: 28). Tunachodokeza ni maelezo mafupi ya jawabu la paulo alipoiona madhabahu iliyotolewa kumtumikia"Mungu asiyejulikana"yaani, miungu yoyote ya kipagani inayoweza kuwepo, lakini ambayo watu wa Anthene hawakuitazama. Badala ya kuwakaripia kwa ujinga wao wa kuamini hivi, Paulo aliwachukuwa toka walipo na kumfahamu Mungu mmoja wa kweli, ambaye hawakumjua (mdo. 17: 22, 23).

- Efe. 2:2 yataja "Mfalme wa uwezo wa anga" Ni bayana anataja maarifa ya mawazo ya Zoroaster - aina ya kitu ambacho wasomaji wa Paulo mara moja waliwahi kuamini. Paulo anasema kwamba waliishi chini ya"Mfalme wa uwezo wa anga" kwa mstari huo huo Paulo anafafanua kuwa ni"Roho (mwenendo wa akili)yule atendaye kazi"katika mtu wa mwilini. Awali waliamini wazo la kipagani la mfalme - roho wa mbingu, sasa Paulo anaonyesha maana ambayo uweza hasa uliokuwa wa kawaida waliojitiishia chini yake ulikuwa ni wa akili yao mbaya. Wazo hili la kipagani limetajwa kwa kuandikwa na kulisema, bila bayana kulikaripia, wakati ukweli unaonyeshwa kuhusu dhambi.

- Matendo 28: 3- 6 yaeleza jinsi nyoka mwenye sumu alivyojizonga kwenye mkono wa Paulo. Watu waliozunguka waliamua kwa kusema Paulo alikuwa muuaji, "haki haimwachi

kuishi" kufuatia hali hiyo kwao walikuwa wamekosea vibaya, lakini Paulo hakuwaelezea suala hili moja moja; badala yake alifanya muujiza - alimtukusia motoni pasipo kumgonga.

• Miujiza ya Yesu ilifunua mitazamo maalumu, k.m ya pepo, bila kuwasahihisha katika maneno mengi mno. Hivyo katika Luka 5: 21 Wayahudi walitoa taarifa mbili potofu: Yesu alikuwa anakufuru, kwamba Mungu pekee anaweza kusamehe dhambi. Kwa maneno Yesu hakuwasahihisha; badala yake alitenda muujiza uliothibitisha upotofu wa taarifa hizo.

• Ilikuwa ni bayana imani ya Yesu ya kuwa matendo hunena zaidi ya maneno. Ni mara chache alikanusha mawazo yadanganyayo moja kwa moja, hivyo hakukanusha sheria ya Musa kama kuwa haiwezi kutoa wokovu, bali alionyesha kwa matendo, k.m. kuponya siku ya sabato, ndivyo ukweli ulivyokuwa. Aliposhutumiwa kwa makosa ya kuwa alikuwa msamaria, Yesu hakukana (Yoh. 8: 48, 49; 4: 7 -9) hata kama Uyahudi wake, akiwa uzao wa Ibrahimu, ulikuwa wa muhimu kwa mpango wa wokovu wa Mungu (Yoh, 4: 22).

Hata wakati Wayahudi walipoleta maneno mabaya (kwa makusudi ) ya kuwa Yesu alikuwa "anajifanya kuwa sawa na Mungu" (Yoh. 5:18), Yesu hakukana wazi wazi; badala yake kwa nguvu alisisitiza kuwa miujiza yake ilimwonyesha kuwa ni mtu atendaye kwa niaba ya Mungu, na kwamba hakuwa sawa na Mungu. Miujiza ya Yesu vivyo hivyo ilionesha kosa la kusadiki kuwa kuna pepo. Muujiza wa Kristo wa kumponya mlemavu kwenye bwawa ulikuwa ni wa kuonesha ujinga wa hadithi ya Wayahudi ya kuwa wakati wa Pasaka Malaika aliyagusa maji ya bwawa la Bethesaida, na kutoa nguvu humo. Hadithi hii imeandikwa bila kukana moja kwa moja ukweli wake; taarifa ya miujiza ya Kristo ni kuweka wazi ujinga wao (Yoh. 5: 4). 2 Petro

2: 4 kusemwa watu wabaya kutupwa shimoni, ni sawa na kusema kuzimu, inaonekana kama ni nchi nyingine; Petro hasahihishi wazo hilo bali ana litumia kama ishara ya maangamizo kamili na adhabu kwa ajili ya dhambi. Matumizi ya Yesu kwa neno Jehanamu ni mamoja (ona somo la 4.9).

**JE ! NI KWELI PEPO ANALETA UGONJWA ?**

Kila mmoja anayeamini kuwa pepo anaishi inabidi ajiulize wenyewe swali: "Ninapo ugua, je ! ugonjwa umeletwa na pepo ?"Kama unadhani Agano Jipya linapotaja pepo linahusu Miungu wadogo wanaozunguka kutenda mabaya, basi inakubidi useme"ndiyo"kwa suala hilo, utaelezaje ukweli wa kwamba magonjwa yanayolaumiwa kuwa ni pepo sasa yaweza kutibiwa au kudhibitiwa na madawa ?.

Malaria ni mfano bora unaojulikana sana. Watu wengi wa Afrika waliamini mpaka hivi karibu ya kuwa malaria ililetwa na pepo. lakini tunajua kwamba malaria inaweza kutibiwa na kwinini au vidonge vingine. Basi unasema kwamba pepo aonapo vidonge vidogo vya njano vikishuka kooni wanatishika na kuruka na wakakimbia ?. Magonjwa mengine ambayo Yesu aliponya, yanayosemwa ni matokeo ya pepo, yametambulika kama tetenasi au kifafa - yote yanaweza kutulizwa kwa dawa.

Rafiki yangu anatoka kijiji kilicho nje ya Kampala Uganda. Alituambia kwamba watu waliamini Malaria yanaletwa na pepo, lakini mara walipoona dawa jinsi inavyodhibiti kwa urahisi sana, wakaacha kutupia lawama kwa pepo. Ingawa hivyo, wakati mtu mmoja aliposhikwa na malaria ya kichwani (ikisababisha ugonjwa wa akili) bado wakalaumu pepo. Tabibu akaja toka mji ulio jirani na kuwapa dawa yenye nguvu kubwa kuzuia malaria iwe tiba, walikataa kwa sababu walisema walihitaji kitu kingine cha

kupingana na pepo, sio malaria. Daktari alirejea baadaye na kusema, "Nina dawa ya kufukuza pepo”; mgonjwa kwa furaha alichukuwa dawa, naye akapona. Vidonge vya pili vilikuwa vile vile kama vya kwanza. Daktari hakuamini pepo, bali alitumia msemo wa siku hiyo ili kumponya huyo mtu - kiasi kama "Tabibu Mkuu"Bwana Yesu, kwa miaka 2000 iliyopita.

### *Tumeacha kitambo sehemu ya 17: Uchawi*

Sehemu hii imeandikwa kwa upana kwa kuwapatia hao wahitaji walio Afrika na pande zingine za ulimwengu ambako uchawi ni jambo lililoenea kwa maisha ya kila siku. Imejulikana na wasomaji wengi wa Biblia kwamba wanawaendea wachawi, Waganga wa Kiafrika na wengineo hawapatani na kushika kweli. Walakini, nafahamu kuwa waganga wa kienyeji wakiwa rahisi na mara nyingi wanasifika kuliko matabibu wa dawa za kisasa, wameunganisha kufaulu kwao kunakoonekana, kunawafanya wavutiwe. Tunataka kujua tatizo hili, kwa akili timamu, kwa njia ya Biblia. Hii ndiyo njia pekee utapata nguvu ya kupinga majaribu ya kuwatumia watu hawa.

## MADAI YA UCHAWI

Ya kwanza, madai ya uchawi huu hufanya kufanikiwa haja ya kuchambua. Tunaweza kuwa na hakika ya kuwa sifa nyingi zinakwenda katika madai yaliyofanywa kwa mafanikio yao. Tiba zao hazifanywi kwa kuonekana wazi, ili wote waone. Ikiwa kweli zimekuwa na mafanikio basi labda walikuwa wakifanya kazi katika mahospitali, na wangepatikana ulimwenguni pote. Hali hasa ya hao wanaodai kuwaponya pia haieleweki - kiasi gani kweli wanapona haipo wazi.

Ninyi kati yenu mnaokabiliana na majaribu haya mnatakiwa mjiulize wenyewe ikiwa mnaushahidi bayana wa uweza wao - k.m. umewahi kuona (hujawai kusikia kuhusu) mtu aliyekatwa mkono na msumeno amekwenda kwa mchawi na kurudi na mkono mwingine unaofanya kazi sawa sawa ?. Huu ni aina ya ushahidi tunaouhitaji kabla ya kuwapa lolote la kuwasadikisha kabisa. K/Torati 13: 1-3 ni lenye nguvu sana: Israeli waliambiwa kwamba kama mchawi akitoa ishara au ajabu ambayo inaonekana kuwa muujiza, hawakutakiwa bado kumwamini mtu huyo isipokuwa wakinena mafundisho ya kweli kama yaliyodhihirika ndani ya Biblia. Ni bayana kwamba mchawi au mganga wa kienyeji haamini kweli katika neno la Mungu - kwa hiyo tusijaribu kuwasadiki kuwa wana uwezo wa kweli, kwa kuwa uwezo wote watoka kwa Mungu (Rum. 13: 1; 1 Kor. 8: 4-6).

Pili, aina ya magonjwa wanayoshughulikia ni ya maana, imegundulika sasa ya kuwa tunatumia karibu 1% tu ya nguvu ya ubongo wetu. zinazobaki zinaonekana kuwa nje ya nguvu zetu kwa fahamu kutoa nguvu (bila shaka tutafanya hivyo kwenye ufalme). Pasipo kuelewa, fikira zetu zinaweza kuwa karibu na matokeo ya viungo vya miili yetu. Hivyo watafiti wa akili ya binadamu wamejulikana kwa kuponya magonjwa ya damu za watu kwa mkazo wa kupima damu zao vema na jumla ya viungo vya mtu na kufanya kazi kawaida. Madaktari wanakiri kwamba pengine tiba hii inayofanyika ambayo haitegemei juu ya dawa za imani. Vivyo, kuwa na mawazo mengi yaweza kusababisha vidonda vya tumbo na maumivu ya kichwa. Kuipumzisha akili au kufanya mazoezi kwa namna fulani yaweza maumivu kuondoka. Lakini kama, kwa mfano, mkono wetu umekatwa na msumeno, hakuna kiasi cha mazoezi ya akili kinachoweza kurudisha tena. Ni fikira zetu pekee zinazotawala magonjwa ambayo wachawi waonekana kuweza kuyageuza. Kwa sababu hatujui vya kutosha

namna fikira zetu zinavyofanya kazi, hii inaonekana kuwa kwa ajili ya nguvu nyingine za mwili ambazo hawa waganga wa kienyeji wanazo. Lakini hivi sivyo; ni kwa ushawishi wao juu ya fikira za watu unaoleta matokeo haya..

**CHANZO CHA UWEZO**

Kwa kadri yeyote, uweza wote ni wa Mungu, Mambo ya pande mbili mazuri na mabya kama haya magonjwa yaletwa na yeye - sio wachawi. Haya ni mambo yanayosemwa sana katika maandiko: - Isa. 45: 5 -7; Mika. 1: 12; Amosi. 3: 6; Kutoka. 4: 11; K/torat. 32: 39; Ayubu. 5: 18. Yote haya yatoa faida kwa kusoma vema. Kinachofuata ni kwamba ni yeye ambaye tumgeukie kwa maombi kama tukiwa wagonjwa, tukifanya yote ambayo ni ya jinsi ya mwanadamu inapowezekana kwa kutumia dawa zinazokubalika na nchi ili kurekebisha tatizo lakini sio kwenda kwa waganga wa kichawi. Kama tukifuata waganga wa kienyeji, tujue twafuata watu ambao wanadai wana 'nguvu za giza' ambazo zinawawezesha kutufanya tupone. Lakini tunajua ya kwamba hizo nguvu wanaamini kuzitenda hazipo. Mungu ndiye muasisi wa nguvu. Kuwaendea wachawi ni kuamini kwamba Mungu hana nguvu zote, na kwamba siye Mungu anayeleta magonjwa yetu bali nguvu ambazo wachawi hudai wanazivuta.

Kufikiri kama hivyo ni kutompendeza Mungu kabisa, kwa kuwa anajua ya kuwa ameuleta ugonjwa, na ni mwenye uweza wote. Israeli walichagua kumwamini Mungu lakini pia waliamini kwamba zipo nguvu zingine zinzotenda kazi katika maisha yao, ambazo iliwabidi washughulike nazo kwa kuzitumikia na sanamu zilizoundwa na nguvu hizo. Jambo hili lilimkasirisha sana Mungu hata akawaacha kuwa watu wake (K/Torati. 32:16 - 24) kwa Mungu tusipomwamini kikamilifu, kwa kweli tujue hatumwamini kabisa. Kadhia ya kusadiki kwa Mungu wa kweli wa Israeli na

wakati huo huo kuwa na wazo la kuwepo kwa nguvu zilizojitenga na Mungu, na kuruhusu mganga wa kienyeji ajaribu kuvuta hizo nguvu zituache kutenda kosa kabisa kama Israeli walivyofanya zamani. Historia ya muda mrefu ya kuhuzunisha ya Israeli ya kuzitumikia sanamu "imeandikwa ili tujifunze"(Rum. 15: 4). Tusishirikiane kabisa na hao waaminio nguvu hizi.

"Pana shirika gani kati ya nuru na giza ?. Tena pana mapatano gani kati ya hekalu la Mungu na sanamu ?. Kwa maana sisi tu hekalu la Mungu aliyehai …. Kwa hiyo tokeni kati yao mkatengwe nao , asema Bwana …….nitakuwa Baba kwenu nanyi mtakuwa kwangu wanangu wa kiume na wa kike"(2 Kor 6:14 -17).

Kama kweli tunafanya bidii na kujitoa kwa kujitenga toka mambo haya, basi tuna amana yenye utukufu na ya kuwa tu wana wa Mungu mwenyewe. Mzazi wa mwili kwa moyo anamtunza mtoto wake anapoumwa. Je ! ni shida kweli kukusanya imani yetu kwa kumwamini kwamba Baba yetu aliye mbinguni atafanya hivyo hata zaidi ?.

Ukweli ni kwamba uchawi una mvuto tu juu yao wanaoamini. Kwa jinsi hii mtu aliyempoteza mpenzi wake anaweza kwenda kwa mtu anaye dhaniwa kuongea na wafu na kwa mchawi na kutaka kumwona mtu aliye kufa. Huyo mtu atawaambia wafumbe macho yao na wakumbuke sura ya mtu wazi wazi kabisa. Mtu atakaye shauri anaweza kukaza nia yake juu ya picha ya mtu anaweza kumkumbuka bayana. Huyu mwenye kudhaniwa kuongea na roho za watu basi anaweza kusoma nia ya mwenye shida, na kwa kupiga chuku kidogo ananena kuhusu mtu kwa maneno anavyoonekana,Hivyo basi mtu anayetaka shauri anaamini kwamba mlozi amemuona mtu aliyekufa angali hai. ujue kwamba hakuna ushahidi kamili umewahi kutolewa wa kuwa mtu

yu hai. Lakini mtaka shauri au mpigiwa ramri akikataa kuamini au kumtii huyu mwaguzi basi hakuna kinachotokea kabisa.

'Wachawi ambao kwa kawaida walimwambia Farao na Nebukadneza ndoto zao wangefanikiwa na nafasi zao za madaraka ila wangefaulu kwa haki. Bila shaka walitumia ujanja huu wa kusoma akili kwa wingi. Lakini Mungu anajihusisha katika maisha ya mtu aliyejishughulisha naye, kama alivyoingilia katika maisha ya Farao na Nebukadneza, walipoteza nguvu zao wakati ule. Vivyo hivyo Baraki aliamini uwezo wa Balaamu wa kuwalaani watu - alipamatia zawadi kubwa ya fedha kwa huduma yake, huku akisema najua tangu zamani alivyopata kukuona "yeye umbarikiye hubarikiwa, na yeye umlaaniye hulaaniwa"(Hesabu. 22: 6). Lakini Balaamu ambaye alikuwa kwa namna nyingine ni sawa na mganga wa kuagua, alikuta kwamba uwezo wake wa kawaida ulitoka alipokuwa anajishughulisha na watu wa Israeli. Ni bayana, watu hawa hawana nguvu kabisa wanapojishughulisha na watu ambao wameungana na Mungu wa kweli, Wowote umashuhuri unaweza kujipatia kwa kufanikiwa unapojihusisha na watu wengine.

**UCHAWI KATIKA BIBLIA**

Maana ya kufaa ni kwamba kama tunajaribu kwenda kwa mganga wa kienyeji, basi tumwamini kabisa. Hakuna maana ya kuaguliwa na mchawi kama tunatumainia mema; na huenda wao wenyewe watafanya hayo hayo. Kuamini kabisa watu hawa na kuwepo kwa nguvu wanazodai wanamiliki, maana yake hatumwamini Mungu mwenye nguvu zote wa kweli. Kama kweli tunaamini taarifa za Farao, Nebukadneza na Balaki waliotajwa, ndipo na sisi tutakwenda kwa mpiga ramli na imani kwamba watakuwa na matokeo yoyote juu yetu . Mifano tuliyoiona yaonyesha kwamba

uchawi hauna nguvu juu ya watu wa Mungu - tunajua ndivyo tulivyo, kwa sababu ya kuitwa kwetu na kubatizwa.

Uchawi ni bayana umeelezewa na Paulo kuwa ni "Matendo ya mwili", na kwa jinsi hiyo hata'uzushi' (mafundisho ya uongo), Uzinzi / uasherati na uchafu (Gal. 5: 19 -21). Anafafanua: "Nawaambia mapema kama nilivyokwisha kuwaambia (yaani haya yalitiliwa msisitizo katika mafundisho ya Paulo), Ya kwamba watu watendao mambo ya jinsi hiyo, yakufanana na hayo hawataurithi ufalme wa Mungu"Uwiano wa hili chini ya sheri ya Musa, amri ilikuwa kwamba wachawi wote, wote wanaoagua au kupiga ramli (jina lingine la Uchawi) na hao waliopitisha watoto wao chini ya moto waliuliwa mara moja (K/torati. 18: 10,11; Kut. 22: 18). Waliopitisha watoto wao motoni hawakuwa ni wachawi hasa - Wachawi na viongozi wa Ibada ya sanamu walifundisha kwamba ili kujilinda dhidi ya nguvu za uovu, watotot wa hao waliotaka ulinzi waliwapitisha katika moto. Basi tunaona kwamba wote wachawi na hao walioutumia waliuwawa; na kwenye Agano Jipya adhabu kwa wafanyayo hayo ni kutoingia ufalme wa Mungu.

Kutumia uchawi kuwa ndio njia yako nzuri kuboresha maisha ni jambo lingine ambalo Mungu hapendi sisi kufanya kwa kila uamuzi tunakabiliwa na maisha yetu kwa Kristo, inatubidi kwa kusema kweli tujiulize 'Je ! kweli Mungu anataka mimi nifanye hivi ?. Je ! nifanye hivi huku Yesu akiwa karibu yangu ? kwa mtazamo wa hukumu ya Mungu bayana kwa uchawi, nadhani jawabu liwe dhahiri ipasavyo - hapana, Mungu hataki tutumie uchawi umebainishwa na Samweli ni kuhusika na 'uasi' (Kiebrania kinadokeza'kukasirisha') juu ya neno la Mungu (1 Sam. 15: 23). Kumkasirisha mwenyezi kama Israeli walivyofanya kuamini sanamu na uchawai (K/Torati 32: 16 -19), ni hakika hakuwazika. Mungu ana maana kwa kuwaamuru Israeli kwa kuwafukuza

Wakanaani watoke kwa sababu ya kuamini uchawi ambao ulikuwa chukizo mno kwake, lakini badala yake, walijiunga kutenda hayo (K/Torati 18: 9-14).Basi kwa Israeli wapya, waamini waliobatizwa, haitupasi kutenda mambo haya ya ulimwengu mbaya uliotuzunguka, au la sivyo hatutaweza kurithi milele nchi ya ufalme tuliyoahidiwa. Kutoa sababu kwamba ni uchawi pekee unaotumika, sio sisi, sio jambo lenyewe, kama tunatumaini kwamba matokeo ya uchawi yataonekana kwetu, basi kwa kushitusha tuna utumia.

Mungu atubariki sote tunapotembea kwa kufunga siku za giza, ulimwengu wa watu na mataifa kuelekea ufalme wake wenye nuru ya kweli na utukufu.

“Kwa sababu hawakubali kuipenda hiyo kweli, wapate kuokolewa kwa hiyo Mungu awaletea nguvu ya upotevu, Wauaminio uongo; …… Lakini imetupasa sisi kumshukuru Mungu siku zote kwa ajili yenu, ndugu mliopendwa na Bwana ……Basi ndugu simameni imara mkashike mapokeo mliofundishwa ama kwa maneno, ama kwa waraka wetu. Na Bwana wetu Yesu Kristo mwenyewe, na Mungu Baba yetu, aliyetupenda akatupa faraja ya milele na tumaini jema, katika neema, awafariji mioyo yenu, na kuwafanya imara katika kila neno na tendo jema" ( 2 Thes. 2: 10 -17 ).

***Tumeacha kitambo sehemu ya 18: Edeni palitokea nini ?***

Mwanzo 3 mstari 4 -5:"nyoka akamwambia mwanamke, Hakika hamtakufa: Kwa maana Mungu anajua ya kwamba siku mtakayo kula matunda ya mti huo, mtafumbuliwa macho, nanyi mtakuwa kama Miungu, mkijua mema na mabaya”

**TAFSIRI YA WATU WALIO WENGI:**
Imeaaminika kwa ubaya kwamba hapa nyoka ni Malaika aliye asi, ameitwa"Shetani". Akiisha kutupwa toka mbingu kwa sababu ya dhambi zake, akaja duniani na kumjaribu Eva kutenda dhambi.

**FAFANUZI:**

1. Maneno ya shetani yamesema "nyoka" maneno "Shetani"na"Ibilisi" hayamo katika kitabu kizima cha mwanzo. Ukweli ni kwamba nyoka wana mwili kama sisi, wanatambaa kwa matumbo yao, ni ushahidi wa kwmba nyoka katika Edeni alikuwa mnyama halisi. Wanaoamini vingine wanathubutu kufikiri kwamba popote wanapomwona nyoka halisi wanakuwa wamemwona 'shetani' mwenyewe.

2. Kamwe nyoka hajasemwa ni Malaika

3. Kwa hiyo haishangazi kwamba hakuna mstari katika mwanzo kwa yeyote kutupwa toka mbinguni.

4. Dhambi huleta mauti (Ru. 6: 23). Malaika hawezi kufa (Luk. 20: 35 -36), kwa hiyo Malaika hawatendi dhambi. Thawabu ya wenye haki ni kufanywa kuwa sawa na Malaika bila kufa tena (Luka 20:35 -36). Ikiwa Malaika waweza kutenda dhambi, ndipo na wenye haki nao wataweza kufanya dhambi na kwa hiyo watakuwa na uwezekano wa kufa, ina maana kwa kweli hawatakuwa na uzima wa milele.

5. Sifa zinazowatofautisha za wahusika kwa taarifa ya kitabu cha Mwanzo kuhusu kuanguka kwa mtu ni: Mungu, Adamu, Eva na nyoka. Hayupo mwingine aliyetajwa. Hakuna ushahidi kuwa kitu chochote kilimwingia nyoka kumfanya alichotenda.Paulo

anasema nyoka"alimdanganya Hawa kwa hila yake"(2 Kor. 11: 3). Mungu alimwambia nyoka:"Kwa sababu umefanya hayo ….."(Mwa. 3:14). ikiwa "Shetani' alikuwa anamtumia nyoka, ni kwa sababu gani hajatajwa na kwa nini naye hakuadhibiwa ?

6. Adamu alimlaumu Eva dhambi yake:"Huyo mwanamke ndiye aliyenipa matunda ya mti" ( Mwa. 3: 12). Eva alimlaumu nyoka:"Nyoka alinidanganya, nikala" (Mwa. 3: 13). Nyoka hakumlaumu ibilisi - hakutoa udhuru.

7. Kama ikisisitizwa ya kwamba nyoka wa leo hawana uwezo wa kusema au fikira kama nyoka wa Edeni aliokuwa nao, kumbuka kwamba: -

a) Punda aliwahi kufanywa anene na kuhojiana na mtu (Balaamu): "Punda (wa kawaida) asiyeweza kusema, akanena kwa sauti ya kibinadamu, aliuzuia wazimu wa nabii yule (2 Pet. 2, 16) na

b) Nyoka alikuwa mwerevu kuliko wanyama wote (Mwa. 3,1). Laana juu yake iliondoa uwezo wake wa kunena na Adamu na Hawa.

8.Mungu alimwambia nyoka (Mwa. 3, 1) mwingine aitwaye "Shetani"na kugeuka kuwa nyoka, kama tunasadiki hivi basi tuna maana ya kusema mtu fulani anaweza kuingia katika maisha ya mwingine na kumwongoza. Hili ni wazo la kipagani, sio la Biblia tu kama ukitiwa mkazo wa kwamba Mungu asingemuumba nyoka kwa sababu ya dhambi kubwa aliyomshawishi Adamu na Hawa kuitenda, kumbuka dhambi iliingia ulimwenguni kutoka kwa mtu (Rum. 5: 12); kwa hiyo nyoka kuwekwa kujua baya na jema alinena kutokana na kuangalia mwili wake, na kwa hivi hakuwa na la kujibu kwa Mungu na kwa sababu hii hakutenda dhambi.

Wengine wanadokeza kwamba nyoka wa Mwa. 3 amewiana na Maserafi. Walakini, neno la kawaida la Kiebrania"nyoka"ambalo limetumika katika Mwanzo 3, haliwiani kabisa na"Maserafi"Neno la Kiebrania lililotafsiriwa "Maserefi"kimsingi maana yake "Mkali"au wa moto na limetafsiriwa"nyoka za moto"katika Hesabu 21: 6, lakini sio neno lililotafsiriwa"nyoka" kwenye kitabu cha Mwanzo 3. Neno la Kiebrania shaba linakuja toka asili moja kama neno'nyoka' katika mwanzo 3. Shaba inaelezwa au ni mfano wa dhambi (Amu. 16: 21; 2 Sam. 3: 34; 2 Fal. 25: 7; 2 Nyak. 33: 11; 36: 6), mistari hii yote ieleweke kwamba vifungo walivyokuwa wanafungwa navyo ni vya shaba, ukiwa na Biblia Habari njema sehemu zingine utakuta pameandikwa pingu za shaba lakini hii Biblia yetu tuliyoizoea ya Afrika Mashariki sentensi haimaliziwi na neno shaba. Hivyo nyoka aweza kuunganishwa na jambo la dhambi, lakini sio Malaika mwenye dhambi.

**MAELEZO YALIYODOKEZWA** ***kama maana ya mafungu haya ya maneno:***

1. Hakuna sababu ya kuwa na shaka ya kile tulichoambiwa kuhusu uumbaji na kuanguka katika sura za kwanza kitabu cha mwanzo hizo habari zake zieleweke vivyo hivyo."Nyoka"alikuwa ni nyoka halisi. Ukweli tunaona nyoka wa leo kutambaa kwa tumbo ni utimilifu wa laana iliyowekwa juu ya nyoka wa kwanza (Mwa. 3,14), unathibitisha jambo hili. Vivyo hivyo twaona mwaume na mwanamke wakisumbuka kutokana na laana iliyowekwa juu yao wakati ule ule.Tunaweza kufahamu kuwa Adamu na Hawa walikuwa ni mwanaume na mwanamke kama tunavyojua mwanaume na mwanamke wa siku hizi, wakifurahia hali njema ya mwili wanao ishi nao, kwa hiyo nyoka wa kwanza alikuwa ni mnyama halisi, ingawa alikuwa mwerevu sana kuliko nyoka wa leo.

2. Vifuatavyo ni vielelezo vinavyoendelea kuwa sura ya kwanza kwa kitabu cha Mwanzo kisomwe kilivyo: -

• Yesu alitaja taarifa ya uumbaji wa Adamu na Hawa ikiwa ni msingi wa Mafundisho yake juu ya ndoa na talaka (Math. 19: 5-6); hakuna dokezo kuwa aliisoma kwa mfano.

• "Maana Adamu aliumbwa kwanza, kisha Hawa. Adamu hakudanganywa (na nyoka ), bali mwanamke alidanganywa na akaingia hali ya kukosa" (1 Tim. 2: 13 -14) - hivyo Paulo, naye, alisoma kitabu cha Mwanzo bila kukigeuza. Na ya muhimu zaidi aliandika mapema kuhusu namna "nyoka alivyomdanganya Hawa kwa hila yake" (2 Kor. 11: 3) - fahamu kwamba Paulo hamtaji ibilisi akimdanganya Hawa.

• Je ! upo ushahidi wowote kabisa wa kwamba kuna kitu kingine pembeni kwenye taarifa ya uumbaji na kuanguka ambao usomwe kimfano ?. Ulimwenguni uliumbwa kwa siku sita kulingana na Mwanzo 1. Kama hizi zilikuwa ni siku halisi za masaaa 24 zimethibitishwa kwa ukweli wa kwamba vitu mbali mbali viliumbwa kwa siku tofauti zisingefaa kuwepo bila kila moja kwa namna yake zilivyopo kwa zaidi ya siku chache. Tena ni siku, havikuwa ni vipindi vyovyote vya miaka 1000, bali alikufa baada ya siku saba akiwa na umri wa miaka 930 (Mwa.5: 5). Ikiwa siku ya saba ilikuwa ni kipindi cha miaka 1000 basi Adamu angekuwa zaidi ya miaka 1000 alipokufa.

• Ushahidi unaendelea wa siku halisi za uumbaji unaweza kukutwa katika sheria ya Sabato ya Kut 20: 10, 11. Sabato ilikuwa na saa 24 za kupumzika, kwa sababu Mungu alipumzika siku ya saba, akiisha fanya kazi kwa siku sita (kama Israeli

walivyofanya kabla ya kutunza sabato yao). Kama mimea ingechipuka siku ya miaka ingetegemea nyuki n.k walioumbwa siku ya sita.. Kupishana kwa nafasi ndefu kati ya kuumbwa kwao kwa sababu hii haifai kutumika.

3. Kwa sababu nyoka alilaaniwa kwa kufanya atambae kwa tumbo lake (Mwa. 3: 14). Hii inaweza kudokeza kwamba awali alikuwa na miguu, pamoja na uwezo wake bayana na kuhojiana, labda umbo la maisha ya mnyama lilikaribiana na mtu ingawa bado alikuwa ni mnyama - jinsi moja na "Wanyama wa mwitu aliowafanya Bwana Mungu" (Mwa. 3: 1 -14).

4. Labda nyoka alikula matunda ya mti wa ujuzi, ambao ulimweleza hila yake. Hawa "alipoona ule mti … ni mti wa kutamanika kwa maarifa" (Mwa. 3: 6). Ni jinsi gani aliweza kuuona huu, isipokuwa aliona matokeo ya kula matunda katika maisha ya mwingine aliyejifanya hivyo tayari ?. Yawezekana vema kwamba Hawa alifanya mazungumzo na nyoka kabla ya taarifa moja iliyo katika Mwa. 3.Taarifa ya maneno ya kwanza yaliyoandikwa ya nyoka kwa Eva ni,"Ati ! hivi ndivyo alivyosema Mungu ….." (Mwa. 3: 1) - neno 'Ati' inawezekana kwamba linadokeza hili lilikuwa ni endelezo la mazungumzo yaliyotangulia ambayo hayajaandikwa.

***Tumeacha kitambo sehemu ya 19: Lusifa***

Kabla ya yote hili ni jina la mtu, lakini msomaji hutokuta linapatikana ndani ya Biblia zenu za kiswahili isipokuwa Biblia zingine za Kiingereza. ukifungua Biblia yako utaona nyota ya alfajiri sio Lusifa. Maneno yenyewe yameandikwa hivi: -

Isaya 14 mstari 12 -14: "Jinsi alivyoanguka kutoka mbinguni Ewe lusifa, mwana wa asubuhi. jinsi alivyokatwa kabisa, Ewe uliyewaangusha mataifa: Nawe ulisema moyoni mwako nitapanda mpaka mbinguni, nitakiinua kiti changu juu kuliko nyota za Mungu; Nami nitaketi juu ya mlima wa mkutano, katika pande za mwisho za Kasikazini: Nitapaa kupita vimo vya mawingu, Nitafanana na yeye aliye juu".

**TAFSIRI YA WATU WALIO WENGI**

Amesadikika kwamba Lusifa aliwahi kuwa Malaika mwenye nguvu aliyekosa wakati wa Adamu, kwa hiyo alitupwa chini duniani, ambako anawasumbua watu wa Mungu.

**FAFANUZI: -**

1. Maneno hayo"Ibilisi", "Shetani"na "Malaika"hayamo katika sura hii. Hii ni sehemu pekee katika maandiko ambayo neno "Lusifa" limeonekana - lakini sio katika Biblia yetu ya Kiswahili.

2. Haupo ushahidi wowote katika Isaya 14 unaoelezea jambo lolote lililotokea kwenye Bustani ya Edeni; kama upo, basi ni kwa sababu gani tumeachwa miaka 3000 toka wakati wa Mwanzo kabla ya kuambiwa sababu ya kweli iliyotokea pale ?

3. Lusifa amesemwa amefunikwa na funza (mst. 11) na kudhihakiwa na watu (mst. 16) kwa sababu hana uwezo tena baada ya kutupwa toka mbinguni (mst. 5 -8); basi hakuna haki ya kudhani kwamba Lusifa sasa yupo duniani kuwapotosha waaminio.

4. Ni kwa sababu gani Lusifa ameadhibiwa kwa ajili ya kusema kwamba "Nitapanda mpaka mbinguni" (mst. 13) ikiwa tayari aliwahi kuwapo kule ?

5. Lusifa anaoza kaburini:"Fahari yako imeshushwa hata kuzimu ….., funza wametandazwa chini yako na vidudu vinakufunika"(mst. 11). Malaika hawawezi kufa (Luk. 20: 35 -36), kwa hiyo Lusifa hawezi kuwa Malaika; msemo umefaa sana kwa binadamu.

6. Mstari wa 13 na 14 ina muungano na 2 Thes. 2: 3-4, ambayo inamuhusu "mtu wa kuasi"- huyu Lusifa anaonyesha mbele kwa mtu mwingine, sio Malaika.

**MAELEZO YALIYOTOLEWA: -**

1. Tafsiri yetu ya Biblia imeanza andiko la Isaya sura za 13 - 23 kuwa ni mfululizo wa "Ufunuo"juu ya mataifa mbalimbali, k.m. Babeli, Tiro na Misri. Isa. 14:4 inaanza kueleza fungu dogo la maneno ya mistari tunayoipima: "Utatunga mithali hii (mfano) juu ya mfalme wa Babeli …… ? Basi, unabii unamhusu mfalme mwanadamu wa Babeli, ambaye amesemwa ni "Lusifa”. Kwa kuanguka kwake:"wao wakuonao …… watakuangalia sana, wakisema, Je ! huyu ndiye aliyeitetemesha dunia …. ?"(mst. 16). Kwa hivi Lusifa amebainishwa kuwa ni mtu.

2. Kwa sababu Lusifa alikuwa mwanadamu mfalme,"Walio wakuu wote wa dunia …. Hao wote watakujibu na kukuambia, Je ! wewe nawe umekuwa dhaifu kama sisi ? wewe nawe umekuwa kama sisi ?" (Mst. 9 -10). Kwa hiyo Lusifa alikuwa mfalme kama mfalme yeyote mwingine.

3. Mstari wa 20 unasema kwamba uzao wa Lusifa utaangamizwa. Mstari wa 22 unasema ya kuwa uzao wa Babeli utaharibiwa, hivi wao wanasawazishwa.

4. Ukumbuke kwamba hii ni "Mithali juu ya mfalme wa Babeli"(mst. 4)"Lusifa" maana yake "nyota ya Asubuhi"ambayo inang'aa zaidi ya nyota zingine. Katika mfano, nyota hii kwa kiburi inaamua kupanda (kupaa) kwenda mbinguni …. Nitakiinua kiti changu juuu ya nyota zingine za Mungu" (mst. 13)Kwa sababu hii nyota inatupwa chini duniani. Nyota ni mfalme wa Babeli. Danieli mlango wa 4 unaeleza jinsi gani Nebukadreza mfalme wa Babeli kwa kiburi aliuchunguza ufalme mkuu alioujenga, akafikiri kwamba aliyashinda mataifa mengine kwa uwezo wake, Kuliko kutambua ya kwamba Mungu ndiye aliyempa mafanikio. "Ukuu wako umekuwa na kufika mpaka mbinguni"(mst. 22). Kwa sababu hii"alifukuzwa mbali na wanadamu, akala majani kama ng'ombe, mwili wake ulilowa maji kwa umande wa mbinguni, hata nywele zake zikakua, zikawa kama manyoya ya tai, na kucha zake kama kucha za ndege"(mst. 33). Kutwezwa huku ghafla kwa mmoja wa watu wa ulimwengu wenye nguvu sana na kutiwa wazimu lilikuwa ni tukio lisilotazamiwa ikahitajika mithali ya kuhusu kuanguka kwa nyota ya Asubuhi toka mbinguni kuja chini. Nyota ni mfano wa watu wenye nguvu, k.m. Mwa. 37:9; Isa. 13:10 (kuhusu viongozi wa Babeli); Ezek. 32: 7 (kuhusu kiongozi wa Misri); Dan. 8: 10, 24. Kupaa mbinguni na kuanguka toka mbinguni ni maneno yasiyotumika isivyokawaida mara nyingi yametumika kwa kuongezeka katika kiburi na kwa maana ya kushushwa - tazama Ayubu 20: 6; Yer. 51: 53 (kuhusu Babeli); Omb. 2: 1; Math. 11:23 (kuhusu Kapernaumu):"Nawe Kapernaumu, Je ! utakuzwa mbinguni ? utashushwa mpaka kuzimu"(kaburi).

5. Mstari wa 17 analaumiwa Lusifa kwa kuufanya "Ulimwengu ukiwa, ( kuuharibu) miji yake; asiyewafungua

wafungwa wake waende kwao …..". Haya yote ni maelezo ya utaratibu wa jeshi la Babeli - likiteketeza eneo lote (kama walivyofanya kwenye mji wa Yerusalemu), wakiwahamisha mateka kwenda maeneo mengine bila kuwaruhusu warejee nchi zao (kama walivyowafanyia Wayahudi), Wakijenga miji mipya na kutwaa kodi ya dhahabu toka mataifa yaliyokandamizwa. Kwa hivi upo mkazo juu ya ukweli kwamba Lusifa hakupata maziko kama wafalme wengine walivyokuwa nayo (Mst. 18 -19), Ukidokeza kuwa alikuwa ni mfalme mwanadamu tu kama wao, kuona mwili wake ulihitajika kuzikwa.

6. Mstari wa 12 unasema kwamba Lusifa alikuwa "akatwe kabisa"unadokezwa kuwa alikuwa mti. Huu unatoa muunganiko unaoendelea na Danieli 4: 8 -16, ambapo Nebukadreza na Babeli wamelinganishwa na mti ukikatwa kabisa.

7. Babeli na Ashuri mara nyingi wanabadilishana maneno katika manabii; hivi akiisha kusema kifo cha mfalme wa Babeli, Msta. 25 unasema "Nitamvunja huyo mwashuri ……" Unabii kuhusu Babeli katika Isa. 47 umerudiwa kuhusu Waashuri kwa Nahumu 3: 5, 4, 18 na Sefania 2: 13,15; na Nyaka. 33: 11 kusema kwamba mfalme wa Ashuri (alimchukua) alimtwaa manase utumwani Babeli - ni kuonyesha kubadilishana kwa kuita maneno. Amosi. 5: 27 unasema kwamba Israeli walikuwa wanakwenda utumwani "mbali kupita Dameski"yaani Ashuru, lakini Stefano ananukuu mstari huu kuwa"mbali kupita Babeli" (Matendo. 7: 43). Ezra 6:1 ni maelezo ya Dario mfalme wa Babeli akitoa amri ya kujenga tena hekalu. Wayahudi walimtukuza Mungu kuugeuza"Moyo wa mfalme wa Ashuru" (Ezera. 6: 22), tena inaonyesha kwamba ni maneno yanayobadilishana. Unabii wa Isaya 14, pamoja na mwingi mwingine kwa Isaya, unapatana vema kwa maneno ya uvamizi wa Sennakeribu kipindi cha Hezekia, huo mst. 25 unaeleza kuvunjwa kwa mwashuri. Msta.

wa 13 ni mwepesi kuufahamu ikiwa unazungumzia kuhusu maneno ya kufuru ya kuuhusuru Yerusalemu Waashuri, walitaka kuingia Yerusalemu na kuteka hekalu kwa ajili ya miungu yao. Awali mfalme wa Ashuru, Tiglath -pileseri, pengine alitaka kufanya yale yale (2 Nyak. 28: 20, 21); Isa. 14: 13 "Maana umesema moyoni mwako, nitapanda mpaka mbinguni ….. (ya mfano wa hekalu na sanduku la agano - 1 Fal. 8: 30; 2 Nyak. 30: 27; Zab. 20: 2, 6; 11: 4 Ebra. 7: 26). Nami nitaketi juu ya mlima wa makutano (mlima sayuni lilipokuwa hekalu) katika pande za mwisho za Kaskazini"(Yerusalemu - Zab. 48: 1, 2).

***Tumeacha kitambo sehemu ya 20: Majaribu ya Yesu***

Mathayo 4: 1 -11:"Kisha Yesu akapandishwa na Roho nyikani, ili ajaribiwe na Ibilisi. Akafunga siku arobaini mchana na usiku, mwishowe akaona njaa. Mjaribu akamjia akamwambia; Ukiwa ndiwe mwana wa Mungu, amuru kwamba mawe haya yawe mikate. Naye akajibu akasema, Imeandikwa, Mtu hataishi kwa mkate tu, ila kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu. Kiisha Ibilisi akamchukua mpaka mji mtakatifu, akamweka juu ya kinara cha hekalu, akamwambia; Ukiwa ndiwe mwana wa Mungu jitupe chini; kwa maana imeandikwa, Atakuagizia Malaika zake; na mikononi watakuchukua usije ukavunjika mguu wako katika jiwe. Yesu akawaambia, tena imeandikwa, Usimjaribu Bwana Mungu wako. Kisha Ibilisi akamchukua mpaka mlima mrefu mno, akamwonyesha miliki zote za ulimwengu, na fahari yake, akamwambia haya yote nitakupa, ukianguka kunisujudia. Ndipo Yesu alipomwambia, nenda zako, shetani; kwa maana imeandikwa, Msujudie Bwana Mungu wako,

Umwabudu yeye peke yake. Kisha Ibilisi akamwambia na tazama, wakaja Malaika wakamtumikia".

**TAFSIRI YA WATU WALIO WENGI**

Maneno haya yanasomwa kuwa na maana ya kuwa kiumbe aitwaye"Ibilisi alimjaribu Yesu kutenda dhambi kwa kutoa shauri la mambo fulani kwake na kumwongoza katika sehemu za kumjaribu.

**UFAFANUZI**

1. Yesu "alijaribiwa sawa sawa na sisi kwa mambo yote, bila kufanya dhambi" (Ebra. 4:15), na "kila mmoja hujaribiwa na tamaa yake mwenyewe huku akivutwa na kudanganywa"(Yak. 1: 14). Tunajaribiwa na"Ibilisi"wa tamaa yetu wenyewe au nia mbaya, ndivyo hata Yesu. Hatujaribiwi na kiumbe mbaya asimamaye ghafla karibu yetu akitushurutisha kutenda dhambi - dhambi na majaribu huja"toka ndani"ya moyo wa mtu"(Marko. 7:21).

2. Ni wazi majaribu hayawezi kuchukuliwa kwa jinsi ya maana hasa ya maneno: -

• Mathayo 4: 8 anadokeza ya kwamba Yesu alichukuliwa mpaka mlima mrefu ili kuona miliki zote za ulimwengu na fahari ijayo"kwa dakika moja"(Luk. 4:5). Haupo mlima mrefu wa kutosha kuuona ulimwengu wote. Ni kwa sababu gani urefu wa mlima ulimwezesha Yesu kuona ulimwengu utakavyokuwa baadae ?. Dunia ikiwa duara, hakuna maana toka uso wake mtu akaweza kuona pande za ulimwengu kwa dakika moja.

• Mlinganisho wa Math. 4 na Luk. 4 unaonyesha kwamba majaribu yameelezwa kwa mpangilio unaohitilafiana. Marko 1: 13

anasema Yesu alikuwa"Jangwani siku arobaini, akijaribiwa na shetani", Wakati Math. 4: 2-3 anasema ya kuwa 'alipofunga siku arobaini …... mjaribu (shetani) akamjia ……".Kwa sababu maandiko hayawezi kujipinga yenyewe, tunaweza kusema kwamba majaribu yale yale yalikaa yakirudiwa -rudiwa yenyewe. Jaribu la kubadili mawe kuwa mkate ni mfano bayana. Kwa uzuri huu utafaa ikiwa haya majaribu yalitokea ndani ya moyo wa Yesu. Akiwa na mwili wetu, kukosa chakula kulimdhuru kiakili na kimwili, na hivyo moyo wake kwa urahisi ulianza kuwaza mambo. Kukaa siku chache bila kula kwa wengine wanaweza kuweweseka au kuzimia (1 Sam. 30: 12). Hali iliyo sawa kati ya mkate na mawe umetajwa na Yesu kwa Mathayo 7:9, hapana shaka mifano hiyo mara nyingi iliungana na mawazo yake yaliyoumia vibaya - ingawa siku zote upesi uliyatawala kwa kuamuru yarudi nyuma kwa Neno.

- Inaweza kuwa Yesu aliwaambia waandishi wa Injili habari ya majaribu yake, na kukiri kwa maneno yaliyokuwa ya nguvu aliyoyapata, inawezekana alitumia mfano ulioufikia ulionekana kwa Math. 4 na Luk. 4.

Anaonekana namna tofauti ibilisi aliyemwongoza Yesu kupita jangwani na mitaa ya Yerusalemu kisha walipanda kinara cha hekalu pamoja, wote kwa mtazamo wa udadisi wa Wayahudi. Josephus hatoi taarifa yoyote ya kutokea hii - kwa kuthubutu kungesababisha vurugu kubwa. Kwa hali moja, ikiwa haya majaribu yalitokea mara kadhaa ndani ya siku arobaini sawa na mwisho wa kipindi hicho (ambacho yalifanya karibu mara mbili, kwa kuwa Mathayo na Luka wanayo kwa mpangilio unaotofautiana ), ni jinsi gani Yesu alikuwa na muda wa kutembea (n.b ibilisi"akampandisha"pale) kwenye mlima mrefu ulio karibu (ambao wanaweza kuwa ulikuwa Hermoni upande wa mbali

Kaskazini mwa Israeli), kupanda hata kileleni na kushuka chini tena, kurudi jangwani na kisha kurudia zoezi ? Majaribu yake yote yalitokea jangwani - alikuwepo kule kwa siku arobaini, akajaribiwa muda wote na ibilisi (ambaye alimwacha mwishowe - Math. 4: 11). Ikiwa Yesu alijaribiwa na ibilisi kila siku, na majaribu yalitokea jangwani tu, basi ni kwamba Yesu hakuondoka jangwani kwenda Yerusalemu au kusafiri ili kupanda mlima mrefu. Kwa hiyo mambo haya hayakuweza kutukia kwa jinsi ya maana ya maneno yalivyo.

- Kama ibilisi ni mtu aliye na mwili ambaye haheshimu Neno la Mungu naye anapenda kuwakosesha watu, basi ni kwa nini Yesu alinukuu Maandiko ili kushinda ? Kulingana na mtazamo wa walio wengi, hii isingemwondoa Ibilisi. Fahamu kuwa Yesu alinukuu fungu la maneno ya Biblia kwa kila wakati. Ikiwa ibilisi yalikuwa ni mawazo mabaya ndani ya moyo wa Yesu, basi inaeleweka kwamba kwa tendo la kuwa na Neno la Mungu ndani ya moyo wake na kujikumbusha mwenyewe, aliweza kuyashinda mawazo haya mabaya. Zab. 119: 11 ni ya muhimu ambapo labda ni bayana alikuwa anatoa unabii wa yaliyompata Kristo jangwani:"Moyoni mwangu nimeliweka neno lako, nisije nikakutenda dhambi".

- Math. 4: 1 unasema kwamba Yesu "alipandishwa na roho jangwani (ukipenda nyikani), ili ajaribiwe na ibilisi". Huyu alikuwa ni Roho kustaajabisha Roho wa Mungu kumpeleka Yesu jangwani ili akajaribiwe na kiumbe anayemzidi mwanadamu kwa maarifa aishiye kwa kupingana na Mungu.

**MAELEZO YAMEDOKEZWA: -**

1. Yesu alipobatizwa mto Yordani na Yohana, alipokea nguvu za Roho Mtakatifu (Math. 3: 16). Mara alipotoka majini, alipelekwa kwenda nyikani kujaribiwa. Akiisha kuwa na uweza wa roho kugeuza mawe kuwa mkate, kuruka jengo bila kudhurika n.k, majaribu haya ilibidi yatamani vitu moyoni mwake. Ikiwa ni mtu alikuwa adokeza mambo haya kwa Yesu naye akijua mtu huyo ni mtenda dhambi, basi majaribu yalikuwa magumu kidogo kuliko kama yaliyotoka ndani ya moyo wa Yesu.

2. Jaribu la kuutwaa ufalme wake lilikuwa na nguvu mno ikiwa lilitoka ndani ya Kristo. Moyo wa Yesu ulikuwa umejaa Maandiko, na kwa hali ya kuumia moyo, Kulikosababishwa na aumu, ilimjaribu atumie vibaya maneno ili kumwezesha kujihesabia haki ya kuchukua njia rahisi ya kujiepusha na mazingira aliyokuwemo. Kusimama juu ya mlima mrefu kunakumbusha Ezekieli akiisha kuonyeshwa ufalme utakavyokuwa toka mlima mrefu (Ezek. 40: 2), na Yohana akiuangalia"Mji mtakatifu wa Yerusalemu"toka "mlima mrefu mkubwa"(Uf. 21: 10). Yesu aliuona ufalme wa ulimwengu kama utakavyokuwa wakati ujao (Luk. 4: 5), yaani, akiwa katika ufalme, hapo "Falme za ulimwengu huu unakuwa ufalme wa Bwana wetu na wa Kristo wake"(uf. 11:15).

Inawezekana aliwaza Musa mwishoni mwa miaka 40 ya kuzunguka jangwani (siku zake 40) akitazama nchi ya Ahadi (Ufalme) toka mlima Nebo. Mkazo umewekwa kwa ( Dan. 4:17, 25, 32; 5: 21) kwamba "aliye juu hutawala katika falme za wanadamu, naye humpa amtakaye" Yesu aliishajua kuwa, ni Mungu pekee, sio mtu mwingine, atampa ufalme. Kwa hiyo lisingekuwa jaribu sana kama ni mtu mbaya ndiye aliyedai kuweza kumpatia Yesu ufalme, lingebidi litolewe shauri na 'iblisi' ndani ya Yesu kwamba ataweza kuuchukua huo ufalme mara moja. Isitoshe, aliweza kujihoji, Mungu amenipa Mamlaka kwa

matazamio (Yoh. 5: 26, 27), kwa upana ambao pande mbili zote alikuwa na uwezo kutoa uhai wake na kuutwaa tena (Yoh. 10: 18), ingawa hatimaye uweza wote alipewa baada ya kifo na kufufuka kwake tu (Math. 28: 18).

3. Kwa uzoefu wake wa Maandiko, Kristo aliona hali moja kati yake mwenyewe na Eliya, moyo wake ulikata tamaa baada ya siku 40 jangwani (1 Fal. 19: 8) na Musa, ambaye alipoteza urithi wake haraka wa nchi mwishoni mwa miaka 40 ya kuzunguka jangwani. Yesu, mwishoni wa siku 40, alikuwa na hali ya nafasi moja nao - akikabiliwa na uwezekano wa ukweli wa kushindwa Eliya na Musa walishindwa kwa sababu ya udhaifu wa mwanadamu - sio kwa sababu ya mtu aitwaye "Ibilisi". Ulikuwa ni huu udhaifu wa mwanadamu,"shetani" au adui, ndiyo ulikuwa unamjaribu Yesu.

"Ibilisi akamwambia, Ukiwa ndiwe mwana wa Mungu, ……."(Luk. 4: 3). ilibidi majaribu yawe yakidumu bila kubadilika ndani ya nia ya Yesu kuhoji ikiwa kwa kweli alikuwa Mwana wa Mungu, kwa kuwa kila mmoja aliwaza ni mtoto wa Yusufu (Math. 1: 1, 6; Luk. 3: 23, palipo na neno"akidhaniwa"maana yake'alihesabiwa kwa sheria'). Alikuwa ni mtu wa pekee kutokuwa na Baba mwanadamu. Wafilipi 2: 8 unashauri la kwamba Yesu alikubali kuwa ni kweli alikuwa binadamu kama sisi, kwa kujua sababu yake alikuwa akijaribiwa kutoamini alikuwa ni Mwana wa Mungu, au kutouelewa mwili wake mwenyewe.

Majaribu yalitawaliwa na Mungu kwa elimu ya kiroho ya Kristo. Maneno aliyonukuu Yesu kujipa moyo mwenyewe dhidi ya mawazo yake mabaya ("Ibilisi") yote yapo sehemu ile ile

kumbukumbu la Torati, kuhusu yaliyowapata Israeli Jangwani. ni wazi Yesu aliuona usawa kati ya yaliyomsibu yeye na wao:-

| KUM. 8 | Math. 4 /Luka 4 |
|---|---|
| **mst. 2**<br>"Bwana Mungu wako alikuongoza miaka arobaini katika jangwa, ili akutweze, Kukujaribu kuyajua yaliyo moyoni mwako, kwamba utashika amri zake, au sivyo" | "Yesu alipandishwa na roho""siku arobaini""Jangwani"Yesu alitwezwa kwa majaribu. Yesu aliyashinda kwa kunukuu Maandiko yaliyo kuwa moyoni mwake. **(Zab. 119: 11)**. |
| **mst.3.**<br>"Akakutweza, akakuacha uone njaa, akakulisha kwa mana…apate kukujulisha ya kuwa mwanadamu imetafsiriwa na haishi kwa mkate tu, bali huishi kwa kila litokalo katika kinywa cha Bwana | "Mwisho akaona njaa"Katika Yohana 6 mana Yesu kuwa ni Neno la Mungu ambalo Yesu aliishi kwa hilo jangwani. Yesu alijifunza kwamba kiroho alikuwa akiishi"Akawaambia ……. Imeandikwa, mtu hataishi kwa mkate tu, bali kwa kila neno la Mungu" |
| **mst. 5.**<br>"Nawe fikiri moyoni mwako, ya kuwa kama vile Baba amrudiavyo mwanaye, ndivyo Bwana, Mungu wako, akurudivyo" | Bila shaka Yesu aliwaza kwa yaliyompata.Mungu alimrudi mwanawe, Yesu **2 Sam.7: 14; Zab. 89:32**. |

Hivyo Yesu ametuonyesha jinsi ya kusoma na kujifunza neno - aliwaza yeye mwenyewe nafasi ya Israeli walipokuwa jangwani,

kwa hiyo alichukua masomo ya kujifunza toka yaliyowapata mwenyewe kwa majaribu yake katika jangwa.

*Tumeacha kitambo sehemu ya 21: Vita Mbinguni*

Ufunuo 12: 7 -9 "Kulikuwa na vita mbinguni, Mikaeli na Malaika zake wakapigana na yule joka, yule joka naye akapigana nao pamoja na Malaika zake; Nao hawakushinda, wala mahali pao hapa kuonekana tena mbinguni. Yule joka akatupwa, yule mkubwa, nyoka wa zamani, aitwaye Ibilisi na shetani, audanganyaye ulimwengu wote; akatupwa hata nchi, na Malaika zake wa katupwa pamoja naye".

**TAFSIRI YA WALIO WENGI: -**

Hii ni sura mojawapo ambayo watu wengi wameitumia kutoa shauri kuwa ulikuwepo uasi mbinguni miongoni mwa Malaika, uasi ukasababisha ibilisi na Malaika zake kutupwa duniani toka mbinguni, ambapo akiwa na namna ya nyoka, wakaanza kufanya matatizo na kuleta vurugu duniani.

**FAFANUZI: -**

1. Yote tuliyojifunza mpaka hapa katika somo hili inabidi yaletwe na kuchukuliwa juu ya fungu hili la maneno. Tumekwisha ona ya kuwa Malaika hawawezi kutenda dhambi na ya kuwa uasi hauwezi kuwepo mbinguni. Hivyo hili fungu la maneno ambalo ni la aina yake pekee - inabidi litafsiriwe kwa njia ambayo haiwahusishi Malaika kutenda dhambi au kuwepo Malaika wenye dhambi wanaowafanya watu kufanya dhambi duniani, kwa kuwa

dhambi inakuja toka ndani yetu sio nje yetu sisi (Marko. 7: 20 -23)

2. Kutupwa nyoka - joka toka mbinguni, inadokezwa asili alikuwa huko - Lakini nyoka halisi wa Edeni aliumbwa na Mungu toka mavumbi ya ardhi (Mwa. 1: 24 -25). Hakuna kidokezo kwamba ibilisi alishushwa toka mbinguni na kumwingia nyoka ndani yake.

3. Fahamu kwa makini kwamba hakuna ushahidi wowote hapa wa Malaika akifanya dhambi au akifanya uasi juu ya Mungu, ni vita iliyokuwa mbinguni. Uwezekano hakuna wa mtu yeyote akipigana na Mungu mbinguni: "Wala hapana awezaye kuokoa katika mkono wangu"(Kum. 32: 39).

4. Baada ya mfululizo wa mambo yaliyo katika mstari wa 7 - 9, mst. 10 unasema kwamba "kukawa na sauti kuu mbinguni, ikisema, Sasa kumekuwa wokovu wa nguvu, na ufalme wa Mungu wetu, na Mamlaka ya Kristo wake: kwa maana mshitaki wa ndugu zetu ametupwa chini, Yeye awashitakiye mbele za Mungu wetu, mchana na usiku”. Ikiwa mst. 7 -9 mambo yake yalitokea mwanzo wa ulimwengu, kabla wakati wa Adamu na Hawa, ni jinsi gani imesemwa kuwa baada ya kutupwa shetani ukaja wokovu na ufalme wa Mungu ? Baada ya dhambi ya Adamu, walimwengu wameanza historia yao mbaya ya utumwa wa dhambi na hali ya kushindwa kufanya kitu - hali ya shida kuieleza kuwa"Wokovu"na ufalme wa Mungu. Kuna furaha ya kuwa ibilisi - mshitaki - ametupwa chini hadi duniani. kwa sababu gani kuwe na furaha ikiwa kuja kwake duniani kulikuwa ni mwanzo wa dhambi na msiba kwa binadamu ?. Basi, kuanguka toka mbinguni kuja duniani kukieleweka kwa maneno ya mfano sio kwa maneno yenyewe hasa, kuwa maana ya kuanguka toka kwenye mamalaka (kama ushahidi wa Isa. 14: 12; Yer. 51: 53; Omb. 2:1;Math 11: 23),

unavyosema, zaidi mno maana inaweza kufanywa ka yote haya. Kama yote haya yalitokea kabla ya kipindi cha Adamu, au kabla ya kuanguka kwa mtu, ni jinsi gani ibilisi alikuwa anawashitaki "ndugu zetu"kuona hawa kuwepo wakati ule ?.

5. Hakuna ishara inayoonyesha yote haya yaliyotokea kwenye Bustani ya Edeni. Kipengele cha muhimu kipo kwa Uf. 1: 1 na 4: 1 - kwamba ufunuo ni unabii wa"Mambo ambayo hayanabudi kuwako upesi". Sio maelezo basi ya kile kilichotokea katika Edeni, bali ni unabii wa mambo yaliyokuwa yanatokea wakati mwingine baada ya karne ya kwanza, hapo ufunuo ulipotelewa na Yesu. Yeyeto ambaye kweli ni mnyenyekevu wa Neno ataona kwamba haya mabishano ya maneno pekee yanazuia kabisa hata kutowezekana majaribio yote ya kutaja ufunuo 12. kwenye bustani ya Edeni. Swali linabidi lijibiwe kama ni kwa sababu gani ibilisi yule yule na habari kuhusu kile kilichotokea Edeni itunzwe mpaka mwisho wa Biblia kabla ya kubainishwa.

6. "Joka kuu yule …… nyoka wa zamani" (Uf. 12: 9). Joka alikuwa na "Vichwa saba na pembe kumi" (mst. 3), kwa hiyo hakuwa nyoka halisi. Kuitwa "nyoka wa zamani"yaonyesha kwamba alikuwa na tabia ya yule nyoka wa zamani aliyekuwa Edeni, kwa maana ya kuwa mdanganyifu kama nyoka aliyekuwa. Hali moja, "Uchungu wa mauti ni dhambi" (1 Kor. 15: 56), Lakini hiyo haina maana ya kuwa mauti ni nyoka yule. Anatabia ya nyoka, kwa kuunganika na dhambi.

7. Ibilisi alitupwa duniani na kwa ukali alianzisha ugomvi "akijua ana wakati mchache tu"(mst. 12). Ibilisi kama alitupwa katika Edeni, alikuwa na nafasi ya kumtesa binadamu wakati wake wote wa historia ndefu - ambayo ni vigumu kwa kuwa na" Wakati mchache"tu wa kufanya maangamizi makuu.

8. Ni jinsi gani Ibilisi amemdanganya "ulimwengu wote"(mst. 9) kabla ya kutupwa mbinguni, kwa kuwa hapa kuwepo mtu yeyote ulimwenguni kabla ya Adamu ?.

9. Mst. 4 unasema kwamba joka akakokota theluthi ya nyota za mbinguni kuja chini kwa mkia wake. Ikiwa huu unasomwa kwa jinsi ya maneno yalivyo - Ufunuo 12. unabidi usomwe kwa maneno yalivyo ili kusaidia tafsiri ya watu walio wengi - ukubwa kamili wa joka ni mkubwa sana - theluthi ya ulimwengu wote (au karibu mfumo wa sayari) aliweza kuwemo kwa mkia wake. Hakuna jinsi ya sayari dunia kuwa kubwa kiasi cha kutosha kuenea kiumbe huyu mkubwa akitambaa juu yake. Nyota nyingi ni kubwa kuliko dunia yetu - inakuwaje theluthi yake kuanguka juu ya dunia ?. Imekadiriwa kwamba theluthi ya nyota zitaenea kwa karibu maili trilioni tano. Hivi ndivyo urefu wa mkia wa joka inabidi uwe !. Kumbuka kwamba haya yote yametokea, au yatatokea, baada ya karne ya kwanza B.K. wakati unabii huu ulipotolewa

10. Kwa mtazamo huu na mwingi wa mambo mengine katika Uf. 12 (na unabii wote) ambao hauwezekani kwa kutumia kwake kokote, sio ajabu tumeambiwa kabla ya yote (Uf. 1: 1) ni kwamba ujumbe huu umeandikwa kwa "ishara"yaani, kwa msemo wa kuashiria, au kwa mfano. Kana kwamba kutia mkazo huu kwa maneno yenyewe ya Uf. 12, Ufunuo 12: 1 unaeleza tendo lililofuata kuwa "Ishara kuu".

11. Kwa kusoma anachofanya Ibilisi anapokuwa duniani, hakuna maelezo yake yeye akiwafanya watu watende dhambi; kweli mstari wa 12 - 16 inaonyesha ya kwamba ibilisi

hakufaulu kwa majaribio yake kusababisha matatizo duniani mara alipofika hapa. Taarifa hii inapingana na tafsiri ya watu wengi.

12. Maana moja ya maswali ni kuelewa endapo fungu hili la maneno lasaidia wazo la kuwepo vita mbinguni kwenyewe, iwapo "Mbingu" zilizosemwa hapa ni za maneno halisi au za maneno ya mfano. Tulieleza awali kwamba "mbingu"zaweza kwa maneno ya msemo wa mfano kutaja eneo la mamlaka. Ufunuo kikiwa ni kitabu cha mifano, tulitegemea jambo hili hapa.

Mwanamke wa mstari wa 1 "amevikwa jua, na mwezi upo chini ya miguu yake, na juu ya kichwa chake taji za nyota kumi na mbili" Mkusanyiko huu wa mbinguni, vile vile na mwanamke, ni dhahiri walining'inia mbinguni, maneno hayawezi kuwa na maana hiyo. Mwanamke hawezi kuvikwa jua, au nyota kubwa kama dunia kuwa juu ya kichwa chake.

Ishara nyingine inaonekana mbinguni mst. 3 - joka jekundu. Mstari huu umechukuliwa ulivyo kwa kawaida, Lakini kwa nini iwe hivyo, Kwa kuwa mbingu ni zile zile zilizotajwa katika mst. 1, ni wazi huu ni maneno ya mfano? mstari wa 4 unamwonyesha joka akiziangusha nyota katika nchi toka mbinguni. Tumeona kwamba kwa sababu ya ukubwa wa nyota na dunia, Basi hauwezi kutaja nyota tulizonazo angani au mbinguni. Ufalme wa Mungu utawekwa duniani (Dan. 2: 44; Math. 5: 5), ambao hautaweza kusimikwa kama dunia itaangamizwa kwa kuangukiwa na nyota juu yake.

Mwanamke "akazaa mtoto wake mbinguni", yyeye atakaye wachunga ….. mtoto akanyakuliwa kwa Mungu na kwa kiti cha enzi"(mst. 5). Kiti cha enzi cha Mungu kiko mbinguni. Kama tayari mwanamke alikuwa mbinguni, ni kwa sababu gani mtoto

wake "akanyakuliwa"kwenda mbinguni. Mwanamke alikuwa mfano wa kitu kingine duniani, ingawa kwa maneno ya kimfano"mbinguni"alikuwa. Kisha akakimbilia"jangwani"(mst. 6). Kama alikuwa katika mbingu halisi, hii ina maana ya kwamba jangwa lipo mbinguni. Inafaa zaidi mwanamke alikuwa eneo la kimbingu, na kisha kukimbilia kwenye jangwa la mfano duniani.

Ndipo tukafika mst. 7 -"kulikuwa na vita mbinguni" ushahidi mwingine toka kwa "mbingu"za Uf. 12 ukiisha kuwa ni maneno ya mfano, inaonekana tu hii vita ilikuwa katika mbingu za mfano. Suala hili linabidi liwe hivyo, kwa sababu uasi haupo au dhambi katika mbingu halisi tunazo ziona (Math. 6: 10; Zab. 5: 4, 5; Hab. 1: 13). Mtazamo wa wengi, madai ni kwamba Malaika wamefungwa kuzimu; Lakini hapa wako mbinguni. Basi sivyo Malaika halisi.

Mwandishi aliyepo mara nyingine anawauliza waaminio wazo la orthodox la Ibilisi kwa swali lifuatalo: Je ! unaweza kunipa historia fupi ya Ibilisi wa Biblia, kulingana na tafsiri yenu kwa maneno ya Biblia ?

Jawabu linapingana mno. Kulingana na hoja ya orthodox, kujibu kunakuwa kama hivi: -

a) Ibilisi alikuwa Malaika mbinguni aliyetupwa kwenye bustani ya Edeni. Alitupwa duniani katika Mwa. 1.

b) Amedhaniwa alikuja duniani na akaoa katika Mwa. 6.

c) Kwenye kipindi cha Ayubu amesemwa alikuwa anapita sehemu zote mbili mbinguni na duniani.

d) Wakati wa Isaya 14 alitupwa toka mbinguni hadi duniani.

e) Katika Zekaria 3 yuko mbinguni tena.

f) Yupo duniani kwa Math. 4"Alitupwa nje"kwenye kipindi cha Yesu kulingana na wazo la wengi "mkuu wa ulimwengu huu" akiisha "tupwa nje"kipindi kile.

g) Upo unabii wa Ibilisi "wa kutupwa"katika Uf. 12.

h) Ibilisi amefungwa "mnyororo" katika Uf. 20, bali Malaika zake walifungwa minyororo katika Mwanzo, kufutana na kawaida ya kutazama Yuda mst. 6. Kama alifungwa na "minyororo ya milele" basi, ni jinsi gani ameitwa kwa kufungwa minyororo tena katika Uf. 20.

Kutokana na hili itakuwadhahiri kwamba mtazamo wa watu wengi wa kuwa ibilisi alitupwa toka mbinguni kwa kutenda dhambi sio kweli, kwa kuwa amesemwa bado yuko mbinguni baada ya kila kutokea na'Kutupwa'. Ni muhimu kuelewa pande zote mbili 'mbingu' na ibilisi kwa maana ya maneno ya mifano.

**MAELEZO YALIYODOKEZWA: -**

1. Kujaribu na kutoa maelezo ya sura hii wazi kabisa ni nje ya upeo wetu s sasa. Maelezo yote ya mistari hii inatakiwa ufahamu wote wa kitabu kizima cha ufunuo ili kupata maneno yake.

2. Matata katika mbingu za mfano - yaani, sehemu ya madaraka ilikuwa basi kati ya makundi ya Mamlaka mbili, kila moja likiwa na wafuasi wake, au malaika.Kumbuka kwamba tumeonyesha ya kwamba ibilisi na shetani mara nyingi wameshirikishwa na mfumo wa Waroma ama Wayahudi.

3. Kama ibilisi - joka maana yake aina nyingine ya Mamlaka ya kisiasa ilivyoonyeshwa na kuwa na 'taji juu ya vichwa vyake' (mst. 3); Ufu. 17: 9,10 pia hufafanua juu ya joka huyu:"Hapa ndipo penye akili zenye hekima"- yaani - usijaribu kuelewa mnyama huyu kuwa ni kiumbe halisi - Vichwa saba ni milima saba …. Ambao ni wafalme saba" na mwingine hajaja bado "naye atakapokuja imempasa kukaa muda mchache"labda anaunganika na Ibilisi - joka mwenye "wakati mchache"wa Ufunuo 12: 12.

**Somo La 6: Maswali**

1. Ni nani wa mwisho anayehusika na matatizo na majaribu yetu ?
a) Mungu b) Tukio
b) Kiumbe mwenye dhambi aitwaye shetani
c) Viumbe watenda dhambi wanaoitwa mashetani au pepo.
2. Ni nani anahusika na majaribu yetu kutenda dhambi ?
a) Mwili wetu wenyewe wanadamu
b) Mungu
c) Roho wachafu
d) Kiumbe mtenda dhambi aitwaye shetani
3. Neno 'Ibilisi' maana yeke nini ?
a) Dhambi b) Nyoka
c) Mshitaki / mchongeaji d) Lusifa.
4. Neno 'Shetani' lina maana gani ?
a) Mtenda dhambi b) Adui
c) Mnyama d) Mfalme wa pepo
5. Je ! neno "Shetani" laweza kutumika kwa watu wema ?
6. 'Shetani' na'Ibilisi' kwa maneno ya mifano yaweza kutaja kitu gani ?
7. Tunaelewa kwa jinsi gani 'pepo' kama walivyotajwa kwenye Agano Jipya
a) Malaika watenda dhambi
b) Magonjwa
c) Msemo wa siku zile wa magonjwa, ambayo watu walidhani yalisababishwa na'pepo'
d) Viumbe wa roho.
8. Unamwelewa vipi nyoka wa kwenye bustani ya Edeni ?

## 7.1 Unabii unaomhusu Yesu kwenye Agano la Kale

Somo la 3 limeeleza jinsi gani lengo la Mungu kuwaokoa watu liliwekwa katikati kumzunguka pande zote Yesu Kristo. Ahadi alizotoa kwa Hawa, Ibrahimu na Daudi zote zilimsema Yesu kuwa ni mtoto wao halisi. Kwa kweli, Agano lote la Kale lilionyesha mbele na kutabiri kumhusu Kristo. Sheria ya Musa, ambayo Israeli iliwapasa waitii kabla ya wakati wa Kristo, mara nyingi ilionyesha mbele kuja kwa Yesu:"Torati ilikuwa ni kiongozi kutuleta kwa Kristo,"(Gal. 3:24).Basi kwenye siku kuu ya Pasaka, mwana kondoo asiye na kasoro ilibidi achinjwe (Kut. 12: 3-6); hii inamaanisha dhabihu ya Yesu,"mwana kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu"(Yn. 1: 29; 1 Kor.5:7). Hali ya kutokuwa na doa ambayo ilitakiwa kwa wanyama wote wanaotolewa kuwa dhabihu ilitabiri jambo lililokuwa mbele la sifa njema kamili ya Yesu (Kut. 12:5; 1Pet. 1: 19).

Zaburi zote na vitabu vya manabii vya Agano la Kale kuna unabii usiohesabika kumhusu Masihi atakavyokuwa. Hasa walilenga kwa kuelezea jinsi atakavyo kufa. Wayahudi kukataa kukubali wazo la Masihi anaye kufa laweza tu kwa sababu ya wao kutoangalia unabii huu, baadhi yake sasa unatolewa:

| Unabii ulio katika Agano la Kale | Umetimilika kwa Kristo |
|---|---|
| “Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha ?"**(Zaburi 22: 1)** | Haya yalikuwa kabisa ni maneno ya Yesu palemsalabani **(Math. 27: 46).** |
| “Laumu ya wanadamu na mzaha wa watu. wote wanionao hunicheka sana, Hunifyonya, | Israeli walimdharau Yesunao walimdhihaki **(Luk. 23:35 8:53);** walitikisa vichwa vyao |

| | |
|---|---|
| wakatikisa vichwa vyao; Husema, umtegemee (yaani, alimtegemea) Bwana; na amponye; na amwokoe sasa, maana apendezwa naye"**(Zaburi 22: 6 -8).** | **(Math.27:39),** walisema haya maneno alipokuwa msalabani **(Math. 27:43).** |
| "…. Ulimi wangu waambatana na taya zangu; wamenizuia mikono na miguu"**(Zab. 22:15,16)** | Huu ulitimia Kristo)alipokuwa na kiu msalabani **(Yn.19:28).** Kuzuiwa mikono na miguu ni tendo la kusulubiwa ambalo limetajwa. |
| "Wanagawanya nguo zangu, na vazi langu wanalipigia kura"**(Zab. 22: 18)** | Utimilifu kabisa wa huu unapatikana katika **Mathayo. 27:35.** |
| Ujue ya kwamba **Zaburi 22: 22** ni bayana imenukuliwa kumhusu Yesu katika **Waebrania 2:12.** | |
| "Nimekuwa mgeni kwa ndugu zangu, namsikwao kwa wana wa mama yangu Maana wivu wa nyumba yako umenila"**(Zab. 69: 8,9)** | Huu vema unaelezea mawazo.ya Kristo kuvunjwa urafiki toka kwa Wayahudi ndugu zake na jamaa yake mwnyewe **(Yn. 7:3 -5; Math12: 47 -49)**. Huu umenukuliwa **Yn. 2:17**. |
| "Wakanipa uchungu kuwa chakula changu; nami nilipokuwa na kiu wakaninywesha siki"**(Zab. 69:21).** | Jambo hili lilitokea wakati Kristo akiwa msalabani **(Math. 27:34)**. |
| Sura nzima ya **Isaya 53** ni unabii wa kustaajabisha wa kifo cha Kristo na ufufuo, kila msitari ulikuwa unatimia bila kosa. Mifano miwili tu inatolewa: - | |
| "Kama mwana-Kondoo apelekwaye machinjoni…. | "Kama mwana-Kondoo apelekwaye machinjoni…. |

| | |
|---|---|
| Mbele yao wakatao manyoya yake; Naam hakufunua kinywa chake"**(Isa. 53:9)** | Mbele yao wakatao manyoya yake; Naam hakufunua kinywa chake"**(Isa. 53:9)** |
| Wakamfanyia kaburi pamoja na wabaya, na pamoja na matajiri katika kufa kwake"**(Isa. 53:9)** | Yesu alisulubiwa pamoja na wahalifu **(Math. 27:38),** bali alizikwa ndani ya kaburi la mtu tajiri **(Math. 27:57-60)** |

Ni ajabu ndogo ya kwamba Agano Jipya linatukumbusha ya kuwa"Torati na Manabii"wa Agano la Kale ndio msingi wetu kumweka Kristo (Mdo. 26:22; 28: 23; Rum 1: 2,3; 16: 25,26). Yesu mwenyewe alitahadhalisha kwamba kama hatumwelewi vema"Musa na Manabii", hatuwezi kumfahamu (Luk. 16:31; Yn. 5:46, 47).

Ikiwa Torati ya Musa ilionyesha mbele kwa Kristo, nao manabii walitabiri habari zake, unakuwa ni ushahidi wa kutosha kwamba Yesu kuishi katika mwili kabla ya kuzaliwa. Mafundisho potofu ya kwamba"aliishi akiwa na mwili Kristo kabla ya kuzaliwa yanafanya ahadi zilizorudiwa -rudiwa kwamba atakuwa mzao (mtoto) wa Hawa, Abrahamu, na Daudi ni upuuzi. Kama alikuwa tayari anaishi mbinguni wakati hizi ahadi zinatolewa, Mungu angekuwa amekosea kuwaahidi watu hawa kupata mtoto atakayekuwa masihi. Ukoo wa Yesu, ulioandikwa kwa Mathayo 1 na Luka 3, unaonyesha jinsi Yesu alikuwa na mfuatano wa mababu ambao mlolongo wao unarudi nyuma hadi kwa wote ambao Mungu alifanya nao ahadi.

Ahadi aliyoahidiwa Daudi kuhusu Kristo inakanusha kuishi na mwili wake wakati ahadi ilipofanywa:"Nitainua mzao wako nyuma

yako, atakayetoka viunoni mwako ….Mimi nitakuwa Baba yake, naye atakuwa mwanangu"(2 Sam. 7: 12,14), Fahamu wakati ujao ulivyotumika hapa. Kwa kuwa Mungu atakuwa Baba ya Kristo, haiwezekani kwamba mwana wa Mungu tayari alikuwa akiishi wakati ule hapo ahadi zilipokuwa zinafanywa. Ikiwa mzao wako"atatoka viunoni mwako"inaonyesha ya kuwa alikuwa mtoto halisi mwenye mwili wa Daudi."Bwana amemwapia Daudi neno la kweli …. Baadhi ya wazao wa mwili wako nitawaweka katika kiti chako cha enzi"(Zab. 132:11).

Sulemani alikuwa wa kwanza kutimiza ahadi, lakini tayari kwa kuwa alikuwa akiishi wakati hizi ahadi zinatolewa (2 Sam. 5: 14), utimizwaji mkuu wa ahadi hii kuhusu Daudi kuwa na mzao wa mwili atakaye kuwa ni mwana wa Mungu, anatajwa Kristo

(Luk. 1: 31-33)."Nitamchipushia Daudi chipukizi la haki"(Yer. 23:5) - yaani, Masihi.

Kama huu msemo wa kutaja wakati ujao katika unabii mwingine kuhusu Kristo umetumika."Mimi nitawaondokeshea (Israeli) nabii miongoni mwa ndugu zao mfano wako wewe (Musa)"(Kum. 3:22,23, ambao unabainisha "nabii"kuwa ni Yesu."Bikira (Mariamu) atachukua mimba, atazaa mtoto mwanamume, naye atamwita jina lake"Emmanueli"(Isa. 7:14). Huu kwa utimilifu ni wazi Kristo alipozaliwa. (Math. 1: 23).

## 7.2 Kuzaliwa na Bikira

Habari iliyoandikwa ya mtungo wa mimba na kuzaliwa hairuhusu shauri la kwamba aliishi kwa mwili kabla ya kuzaliwa. Hao wanaoshika mafundisho ya uongo ambayo ni'Utatu' wanapelekwa kwenye dhana ya kwamba wakati fulani walikuwa watu watatu mbinguni, kisha mmoja wao alitoweka na kwa njia

nyingine alibadilika kuwa kitoto kidogo katika tumbo la Mariamu, akawaacha wawili tu mbinguni. Tumeona katika Maandiko kwamba kuwako yote - yakijumuishwa haya ya Mungu - anaishi kwa kuonekana, kwa umbo la mwili. Kwa hiyo tumeachwa tuone toka imani ya'kuishi kabla ya kuja' Kristo ya kwamba kwa njia isiyoeleweka akiwa na mwili wa kuonekana alishuka toka mbinguni akaingia ndani ya tumbo la Mariamu. Elimu yote hii ya dini inayotatiza kuielewa ipo nje kabisa ya mafundisho ya Maandiko. Taarifa ya mwanzo wa Kristo haitoi sababu yoyote ya kufikiri kwamba akiwa na mwili wa kuonekana aliondoka mbinguni na halafu akaingia kwa Mariamu. Kwa hili ni kukosa shabaha kubwa ya ungano katika mafunzo ya utatu.

Malaika Gabrieli akamtokea Mariamu na ujumbe kuwa"tazama, utachukua mimba na kuzaa mtoto mwanamume; na jina lake utamwita Yesu. Huyu atakuwa Mkuu, ataitwa mwana wa Aliye juu ……. Mariamu akamwambia Malaika, Litakuwaje neno hili, maana sijuimume ? (Yaani, alikuwa bikira). Malaika akajibu akamwambia, Roho Mtakatifu atakujilia juu yako, na nguvu zake aliye juu zitakufunika kama kivuli; kwa sababu hiyo hicho kitakachozaliwa kitaitwa kitakatifu, Mwana wa Mungu"(Luk. 1: 31 -35)

Mara mbili mkazo umetiwa kwamba Yesu atakuwa Mwana wa Mungu kwa kuzaliwa kwake; ni dhahiri Mwana wa Mungu hakuwahi kuishi kabla ya kuzaliwa. Tena, viarifa vingi vya wakati ujao vyahitajika kuangaliwa - k.m."atakuwa Mkuu". Ikiwa Yesu alikuwako na mwili kama Malaika alivyosema maneno na Mariamu, tayari angekuwa Mkuu. Yesu alikuwa ni"Shina na mzao wa Daudi"(Uf. 22: 16), neno la Kigriki'genos' linadokeza kwamba Yesu'alizaliwa toka' kwa Daudi.

## MTUNGO WA MIMBA YA YESU

Kwa njia ya Roho Mtakatifu (Pumzi ya Mungu /uweza) akitenda kazi juu yake, Mariamu aliweza kupata mimba ya Yesu pasipo kukutana na mwanamume. Hivyo Yusufu hakuwa Baba wa kweli wa Yesu. Inabidi ieleweke ya kwamba Roho Mtakatifu si mtu (tazama somo la 2); Yesu ni mwana wa Mungu, siye Roho Mtakatifu. Mungu kwa kutumia Roho yake juu ya Mariamu,"kwa sababu hiyo hicho kitakatifu"kilichozaliwa naye,"ameitwa mwana wa Mungu"(Luk. 1:35). Kutumia neno"kwa sababu hiyo"linatoa shauri kwamba pasipo Roho Mtakatifu kutenda kazi katika tumbo la Mariamu, Yesu, mwana wa Mungu asingekuja kuishi.

Ikiwa Yesu alikuwa'mimba' ndani ya tumbo la Mariamu (Lk. 1:31) ni ushahidi kwamba hakuwahi kuishi kimwili kabla ya wakati huu. Kama'tunafikiria' wazo, linaanza ndani yetu. Vivyo hivyo Yesu alichukuliwa mimba ndani ya tumbo la Mariamu - alianza humo akiwa yai, kadri kama binadamu yeyote mwingine. Yohana 3:16 mstari maarufu sana wa Biblia, unatoa habari kwamba Yesu alikuwa"Mwana wa pekee wa Mungu".Mamilion ya watu wanaosimlia mstari huu wanashindwa kutafakari unachodokeza. Ikiwa Yesu alikuwa "mwanawe wa pekee", basi"alianza"kuzaliwa alipochukuliwa mimba ndani ya tumbo la Mariamu. Ikiwa Yesu alikuwa mwanwe Mungu na akiwa na Baba yake, huu ni ushahidi wazi kuwa Baba yake ni mkubwa kuliko yeye - Mungu hana mwanzo (Zab. 90: 2) na kwa sababu hiyo Yesu hawezi kuwa ni Mungu mwenyewe (somo la 8 linaeleza kwa upana maana hii).

Ni muhimu kuwa Yesu"alizaliwa"na Mungu kuliko kuwa aliumbwa, kama Adamu anavyofanywa awali. Jambo hili linaeleza ukaribu wa muungano wa Mungu na Yesu -"Mungu alikuwa ndani ya Kristo akiupatanisha ulimwengu na nafsi yake"(2 Kor. 5:19) Kristo akiisha zaliwa na Mungu, kuliko kuumbwa toka mavumbi

ya ardhi, inasaidia vile vile kueleza wepesi wake aliozaliwa nao kwa ajili ya njia za Mungu Baba yake.

Isa. 49: 5,6 ina unabii kumhusu Kristo kuwa ni nuru ya ulimwengu, ambao aliutimiza (Yn. 8: 12). Amesemwa kuwa anafanya upatanisho"kwa bwana aliyemuumba tangu tumboni ili awe mtumishi wake". Kwa hiyo Kristo"aliumbwa"na Mungu ndani ya tumbo la Mariamu, kwa uweza wa Roho yake Mtakatifu. Tumbo la Mariamu lilikuwa ni mahala palipokuwa dhahiri pa asili pa mwili wa Kristo.

Tumeanza katika somo la 7. 1 kuwa zaburi 22 inatabiri mawazo ya Kristo pale msalabani. Aliwaza kwamba Mungu"ndiwe uliyenitoa tumboni …….. nalitupwa tangu tumboni: toka tumboni mwa mama yangu ndiwe Mungu wangu"(Zab. 22: 9,10). Wakati wake wa kufa, Kristo alitazama nyuma kwenye asili yake - katika tumbo la Mariamu mama yake, alipoumbwa kwa nguvu ya Mungu. Maelezo kabisa ya Mariamu katika Injili kuwa ni"Mama"yake Kristo yenyewe yanaondoa wazo la kuwa aliishi kabla ya kuzaliwa na Mariamu.

Mariamu alikuwa binadamu wa kawaida, mwenye desturi ya wazazi wanadamu. Imethibitishwa na ukweli kwamba alikuwa na binamu aliyemzaa Yohana mbatizaji, mtu wa kawaida (Lk. 1:36). Wazo la kanisa Katoliki la Roma la kuwa Mariamu hakuwa mwanadamu wenye mwili wa kawaida maana yake ni kwamba Kristo kwa pande mbili hakuwa ni"mwana wa Adamu" na"mwana wa Mungu". Haya ni majina yake mara kwa mara katika Agano Jipya lote. Alikuwa"mwana wa Adamu"kwa sababu ya kuwa na mama mwanadamu kabisa, na"mwana wa Mungu"kwa kuwa tendo la Mungu juu ya Mariamu lilifanya kazi kwa roho Mtakatifu (Lk. 1:35), inamaanisha kwamba Mungu alikuwa Baba yake. Mpangilio

huu mzuri unafuatwa ikiwa Mariamu hakuwa mwanamke mwenye desturi ya kawaida.

"Ni nani awezaye kutoa kitu kilicho safi kitoke katika kitu kichafu ? Hapana awezaye. Mwnadamu ni kitu gani hata akawa safi ? huyo aliyezaliwa na mwanamke, hata akawa na haki ? ……… au awezaje kuwa safi aliyezaliwa na mwanamke ?"(Ay. 14:4; 15:14; 25:4). Hii imekomesha ili pasiwepo na utata kwa jambo lolote la kuweza kutungwa mimba pasipo mawaa, aidha kwa Mariamu au Yesu.

Mariamu akiwa "amezaliwa na mwanamke”, mwenye wazazi wanadamu wa kawaida, ilibidi alikuwa na uchafu wetu, Mwili wa mwanadamu, ambao naye Yesu akazaliwa nao,"amezaliwa na mwanamke"(Gal 4:4). Lugha ya kusema"amezaliwa"kwa njia ya Mariamu ni ushahidi tena kuwa hakuwahi kuishi kimwili bila yeye kuzaliwa.

Mara nyingi taarifa ya Injili inaonyesha Mariamu asili yake ya binadamu. Kristo ilimbidi amkaripie mara tatu kwa kukosa kuona kiroho (Luk. 2:49; Yohana 2:4); alishindwa kuelewa misemo yake yote (Luk. 2:50). Hivi ndivyo hasa tungetegemea mwanamke mwenye mwili wa mwanadamu, mwanawe alikuwa mwana wa Mungu, na kwa sababu hiyo mwenye kuona kwa kiroho zaidi kuliko yeye - Mariamu, ingawa Kristo, naye, alishiriki damu na mwili. Yusufu alishiriki na Mariamu baada ya kuzaliwa Kristo (Math. 1:25), hakuna sababu ya kufikiri kwamba hawakuwa na uhusiano wa ndoa ya kawaida tangu hapo na kuendelea.

Kutajwa"mama na ndugu zake"Kristo katika Math. 12:46,47 kwa sababu hiyo kulidokeza ya kwamba Mariamu alikuwa na watoto wengine baada ya Yesu. Yesu alikuwa wa pekee"Mzaliwa wake wa kwanza”. Mafunzo ya katoliki ya kuwa Mariamu alibakia

kuwa Bikira na kisha alipazaliwa mbinguni basi Biblia haisemi lolote kabisa. Kama binadamu mwenye mwili unaopatwa na mauti, Mariamu alizeeka na hatimae kufa; mbali na hivi tunasoma katika Yohana 3:13 "hakuna mtu aliyepaa mbinguni"ukweli kwamba Kristo alikuwa na mwili wa mwanadamu (ona Ebra. 2: 14 -18; Rum 8:3) maana yake ni kwamba mama yake nae alikuwa nao, tunaona Baba yake hakuwa nao.

### 7.3 Nafasi ya Kristo katika mpango wa Mungu

Mungu hafanyi Uamuzi wa mipango yake bila kufikiri, akivumbua sehemu za ziada kwa kusudi lake kama historia ya mwanadamu inavyofunua. Mungu alikuwa na mpanngo kamili ulioelezwa kwa taratibu tangu mwanzo wa uumbaji (Yn. 1:1). Nia yake kuwa na mwana katika mpango wake basi ulikuwa toka mwanzo. Agano la Kale linadhihirisha maelekeo tofauti - tofauti ya Mungu kwenye mpango wake wa wokovu katika Kristo.

Mara nyingi tumeonyesha kwa kueleza kuwa katika ahadi, unabii wa utabiri, na mifano ya torati ya Musa, Agano la Kale daima linafunua kusudi la Mungu kwa Kristo. Ilikuwa ni kwa sababu ya maarifa ya Mungu hata akawa na mwana, ndipo uumbaji Mungu akaufanya uwepo (Ebra. 1: 1, 2, neno dogo la kiyunani;"kwa"katika U.V. ni bora ingetafsiriwa"sababu ya”). Ilikuwa sababu Kristo hata enzi za historia ya mwanadamu ziliruhusiwa na Mungu (Ebra.1: 2 (kiyunani). Kinachofuata ni kwamba ufunuo wa Mungu kwa mwanadamu kushuka chini katika miaka, kama taarifa ilivyoandikwa katika Agano la Kale, ina ushahidi tele wa Kristo.

Ubora wa Kristo na ukubwa wake mno na umuhimu wa asili kwa Mungu ni vigumu kwetu kufahamu kabisa. Basi ni kweli kusema kwamba Kristo alikuwamo ndani ya fikira za Mungu na kusudi tangu mwanzo, ingawa alikuja kuishi tu kimwili alipozaliwa na Mariamu. Waebrania 1: 4, 7, 13,14 inasisitiza kwamba Kristo hakuwa Malaika wakati akiwa na mwili unaopatikana na mauti alikuwa mdogo punde kuliko Malaika (Ebra. 2:7), alikuja inuliwa kuwa na heshima kubwa kuliko wao sababu alikuwa ni"Mwana wa pekee wa Mungu"(Yn. 3: 16). Awali tumeonyesha ya kwamba namna pekee ya kuwako ambako Maandiko yamefundisha ni kuishi kwa umbo la mwili, kwa hiyo Kristo hakuishi akiwa'Roho' kabla ya kuzaliwa. 1 Pet. 1: 20 unaisema nafasi kwa machache; Kristo"alijulikana tangu zamani, kabla haijawekwa misingi ya dunia, lakini alifunuliwa mwisho wa zamani hizi". Yesu alikuwa kiini kikuu cha Injili, ambacho Mungu'aliahidi kabla kwa kinywa cha manabii wake katika maandiko Matakatifu, yaani, habari za mwanawe, …….. Yesu Kristo Bwana wetu, aliyezaliwa katika ukoo wa Daudi kwa jinsi ya mwili; na kudhihirishwa kwa uweza kuwa Mwana wa Mungu, kwa jinsi ya roho ya Utakatifu, kwa ufufuo wa wafu' (Rum. 1:1 -4).

**Hivi unaeleza Muhutasari wa historia ya Kristo: -**

1. Aliahidiwa katika Agano la Kale - yaani, katika mpango wa Mungu

2. Aliumbwa akiwa mtu aliye na mwili kwa kuzaliwa na bikira, akiwa ni mzao wa Daudi;

3. Kwa ajili ya tabia timilifu ("roho ya Utakatifu"), iliyoonekana wakati wa maisha ya mwili unaopatikana na mauti.

4. Alifufuliwa, na tena hadharani alielezewa kuwa ni Mwana wa Mungu na mitume waliopewa kipawa cha roho ya kuhubiri.

**MAARIFA YA MUNGU**

Tutakuwa tumesaidiwa mno kufahamu jinsi gani Kristo alikuwa ndani ya Moyo wa Mungu hapo mwanzo, ambapo kwa mwili hakuwapo, kama tukiukubali ukweli kwamba Mungu anajua mambo yote ambayo yatatokea'wakati ujao'; Ana maarifa ya kujua jambo kabla halijatokea. Kwa sababu hiyo Mungu anaweza kusema na kufikiri kuhusu mambo ambayo hayapo, kana kwamba yapo. Haya ndiyo maarifa yake kabisa ya wakati unaokuja. Mungu'anataja mambo yasiyokuwepo kana vile yapo' (Rum. 4:17). Kwa sababu hiyo anaweza kueleza"Mwisho tangu mwanzo, na tangu zamani za kale mambo yasiyotendeka bado; nikisema, shauri langu litasimama, nami nitatenda mapenzi yangu yote"(Isa. 46: 10).Kwa sababu hii, Mungu anaweza kutangaza wafu kama kwamba wapo hai, na anaweza kuwasema watu kama wapo hai kabla ya kuzaliwa.

"Shauri", au neno la Mungu, lilimtabiri Kristo tangu mwanzo; alikuwa siku zote katika kusudi la Mungu au"mapenzi". Basi ilikuwa yakini kwmba wakati fulani Kristo kwa mwili atazaliwa; Mungu atatimiza kusudi lake alilolisema katika Kristo. Uhakiki wa maarifa ya Mungu kujua mambo kabla, umeletwa ndani ya neno lake lililo la kweli. Biblia ya kiebrania ina kiarifa cha'utimilifu wa unabii', (1 Nyak. 22: 1), wakati bado hekalu lilikuwa limeahidiwa tu na Mungu. Hiyo ilikuwa imani yake kwa neno hilo la ahadi ambayo Daudi alitumia wakati aliokuwapo kutangaza mambo ya wakati ujao. Maandiko yana mifano tele ya Maarifa ya Mungu kujua mambo kabla. Mungu alikuwa na hakika mno kwamba atatimiza ahadi kwa Ibrahimu, ambayo alimwambia:"Uzao wako nimewapa nchi hii …."(Mwa. 15:18) wakati Ibrahimu hata mtoto

hakuwa naye. Wakati wa kipindi kile kile kabla ya uzao (Isaka / Krsito) haujazaliwa, tena Mungu akamwahidi:"Nimekuweka uwe Baba wa mataifa mengi"(Mwa. 17: 5). Kweli,Mungu"hutaja hayo mambo yasiyokuwapo kana kwamba yapo”

Kristo alisema hivyo wakati wa utumishi wake jinsi Mungu'amempa vyote mikononi mwake (Kristo)"(Yn. 3:35), ingawa suala hili wakati ule halikuwa hivyo."umeweka vitu vyote chini ya nyayo zake (Kristo) ….. lakini sasa hatujaona vitu vyote kutiwa chini yake"(Ebra. 2: 8).

Mungu alitangaza mpango wake wa wokovu kupitia kwa Kristo"kama alivyosema tangu mwanzo kwa kinywa cha manabii wake watakatifu"(Luk. 1: 70). Kwa sababu walijumuika kwa karibu sana na mpango wa Mungu, watu hawa wamesemwa kana kwamba wenyewe waliishi mwanzo, ingawa suala si hivyo. Badala yake, tunaweza kusema manabii walikuwa katika mpango wa Mungu tangu mwanzo. Yeremia ni mfano mkuu. Mungu alimwambia:"Kabla sijakuumba katika tumbo nalikujua; na kabla hujatoka tumboni, nalikutakasa; nimekuweka kuwa nabii wa mataifa"(Yer. 1:5). Hivyo Mungu alijua kila kitu kumhusu Yeremia hata kabla ya uumbaji. Kwa namna hiyo Mungu aliweza kusema kuhusu mfalme wa Uajemi, Koreshi, kabla ya kuzaliwa kwake, akitumia msemo unaodokeza wakati ule alikuwako (Isa. 45: 1 -5). Waebrania 7: 9-10 ni mfano mwingine wa msemo huu wa kuwako kiumbe umetumika kumhusu mtu ambaye wakati ule alikuwa hajazaliwa.

Kwa njia iyo hiyo kama Yeremia na manabii wamesemwa kama wanaishi hata kabla ya uumbaji, kwa ajili ya wao kushiriki katika mpango wa Mungu, hivyo waamini wa kweli wamesemwa kuwa wanaishi wakati ule. Ni dhairi kwamba kimwili hatukuishi

wakati ule isipokuwa katika fikira za Mungu. Mungu"alituokoa akatuita kwa wito mtakatifu ……… bali kwa makusudi yake yeye na neema yake. Neema hiyo tulipewa katika Kristo Yesu tangu milele"(2 Tim.1:9). Mungu"alivyotuchagua katika yeye (Kristo) kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu …. Kwa kuwa alitangulia kutuchagua …. Sawa sawa na uradhi wa mapenzi yake"(Efe. 1: 4,5). Wazo zima kwa kila mmoja kutangulia kujulikana na Mungu tangu mwanzo, na kwisha kuchaguliwa kwa wokovu, inaonyesha kwamba walikuwemo katika fikira za Mungu hapo mwanzo (Rum. 8: 27; 9:23).

Kwa mwangaza wa yote haya, Sio ajabu kwamba Kristo, kama kujumlisha kusudi la Mungu, anaweza kusemwa kama amekuwapo tangu mwanzo katika mawazo ya Mungu na mpango, ingawa kwa mwili hakufanya hivyo. Alikuwa ni"Mwana-kondoo aliyechinjwa tangu kuwekwa msingi wa ulimwengu"(Uf. 13: 8). Yesu mwenyewe hakufa wakati ule; alikuwa ni"Mwana-kondoo wa Mungu"aliyetolewa kuwa sadaka karibu miaka 4,000 baadaye Msalabani (Yn. 1:29; 1 Kor. 5:7). Kwa njia hiyo hiyo kama Yesu alivyochaguliwa tangu mwanzo (1 Pet 1:20), hivyo na waaminio (Efe. 1: 4; kwa Kiyunani ni neno moja"kuchaguliwa"limetumika katika mistari hii). Shida yetu kwa kufahamu yote haya ni kwa sababu hatuwezi kwa urahisi kufikiri jinsi Mungu anavyoshughulika nje ya wazo la wakati.'Imani' ndio uwezo wa kutazama mambo toka mtazamo wa maana ya Mungu, pasipo sharti la muda.

## 7.4 "Hapo Mwanzo Kulikuwako Neno" Yohana 1: 1-3.

Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Huyo mwanzo alikuwako kwa Mungu. Vyote vilifanyika kwa huyo"(Yn. 1: 1-3).

Mistari hii, inapoeleweka vema, huthibitisha na kufunua mawazo ambayo yamefikiwa katika sehemu ya mwisho. Ingawa hivyo, fungu hili la maneno ni mojawapo lisiloeleweka zaidi sana kuwa linafundisha ya kwamba Yesu alikuwako mbinguni kabla ya kuzaliwa. Kuelewa kwa usahihi mistari hii kunahusiana na kukubali nini maana ya"Neno"lenyewe. Halimtaji mtu moja kwa moja, kwa sababu mtu hawezi kuwa"na Mungu"halafu awe ni Mungu wakati huo huo. Neno la Kiyunani'Logos' ambalo limetafsiriwa hapa"neno"ndani yake lenyewe halina maana'Yesu' Aghalabu limetafsiriwa kuwa"neno", lakini vile vile kuwa ni: -

**Maelezo** **Kusudi**
**Kupasha habari** **Elimu au Mafundisho**
**Nia** **Kuhutubu**
**Hoja** **Methali**
**Habari**

"Neno"halina maana kumtaja Yesu, ingawa'Logos' ni la kiume katika Lugha ya Kiyunani. Kwa Kiingereza ni'he'. Tafsiri ya Kijerumani (Luther) husemwa"das Wort"(si kiume wala kike); tafsiri ya Kifaransa (segond) inasema"la parole"ya upande wa kike, inaonyesha kwamba"Neno"halina lazima ya kujulisha mtu mume.

**"HAPO MWANZO"**

'Logos' kwa nguvu laweza kutaja wazo la moyoni ambalo limeelezwa kwa upande wa nje kwa maneno na kupashana habari kwingine. Hapa mwanzo'Logos' alikuwa nayo Mungu. Nia hii isiyokuwa ya kawaida kiini kilikuwa kwa Kristo. Tumeonyesha jinsi Roho ya Mungu inavyoweka mawazo yake yatende kazi, hapa ni muungano kati ya Roho yake na Neno lake (tazama sehemu ya 2.2). Roho ya Mungu ilipotimiza mpango wake kwa watu na

kuvuviwa neno lake liandikwe tangu mwanzo, kwa hiyo lilipasha wazo la habari ya Kristo katika kutenda kazi yake na maneno. Kristo alikuwa'Logos' wa Mungu, basi Roho ya Mungu ilieleza mpango wa Mungu wa Kristo kwa shughuli zote. Hizi zinaeleza sababu za matukio mengi yaliyo katika Agano la Kale ni ya mfano hasa wa Kristo. Walakini, haliwezi kukaziwa zaidi kwamba Kristo kwa utu hakuwa"neno"; lilikuwa ni mpango wa Mungu wa wokovu kwa njia ya Kristo ambaye alikuwa"neno".'Logos' ("Neno") mara nyingi sana limetumika kuhusu Injili inayomhusu Kristo. k.m"neno la Kristo"(Kol.3: 16; Math. 13:19; Yn.. 5:24; Mdo. 19: 10; 1 Thes 1: 8 n.k). Fahamu kuwa'Logos' linamhusu Kristo, kuliko yeye mwenyewe binafsi. Kristo alipozaliwa, hili"neno"liligeuka na kuwa umbo lenye mwili na damu -"neno alifanywa mwili"(Yn.. 1: 14). Yesu binafsi alikuwa ni neno lililofanywa mwili kuliko kuwa"neno"; yeye binafsi alikuwa"neno"kwa kuzaliwa na Mariamu, sio alikuwa vingine wakati wowote wa kwanza.

Mpango, au ujumbe, unamhusu Kristo ulikuwa na Mungu tangu mwanzo, lakini uliwekwa wazi katika utu wa Kristo, na kuhubiri Injili inayomuhusu yeye kwenye karne ya kwanza. Hivyo Mungu alitangaza neno lake kwetu kwa njia ya Kristo (Ebra. 1: 1, 2). Wakati mwingine tena umetiwa mkazo wa kwamba Kristo alitangaza neno la Mungu na alitenda miujiza kwa amri ya neno la Mungu ili kumfunua Mungu kwetu (Yn.. 2: 22; 3: 34; 7: 16; 10: 32, 38; 14 10,24).

Paulo alitii agizo la Kristo kuhutubu Injili inayomhusu yeye"kwa mataifa yote"."Kwa kuhubiriwa kwake Yesu Kristo, sawa sawa na ufunuo wa ile siri iliyositirika tangu zamani za milele, ikadhihirika wakati huu kwa maandiko ya manabii, ikajulikana na mataifa yote kama alivyoamuru Mungu"(Rum. 16: 25,26; 1 Kor. 2: 7).

Uzima wa milele umewezeshwa tu kwa mtu, kwa njia ya kazi ya Kristo (Yn.. 3: 16; 6: 53); lakini hapo mwanzo Mungu alikuwa na mpango huu wa kumpa mwanadamu uzima wa milele, akijua kama alivyofanya dhabihu ambayo Yesu aliifanya. Ufunuo timilifu wa toleo lile ulikuja tu baada ya kuzaliwa na kifo cha Yesu:"Uzima wa milele ambao Mungu …… alifunua neno lake (la uzima) katika ujumbe"(Tito.1: 2, 3) Tumeona jinsi manabii wa Mungu wanavyosemwa kuwa wanaishi siku zote (Luk. 1: 70) katika maana ya kwamba"neno"walilolitangaza lilikuwako na Mungu tangu mwanzo.

Mahubiri ya mifano mingi yalifunua mambo haya; kwa hiyo alitimiza unabii unaomhusu yeye mwenyewe,"Nitafumbua kinywa changu kwa mifano; Nitayatamka yaliyosotirika tangu awali - yaani tangu mwanzo wa ulimwengu"(Math. 13: 35). Ilikuwa ni kwa maana hii ya kuwa"neno alikuwa na Mungu ……. Hapo mwanzo"ili"lifanyike mwili"Kristo akazaliwa.

**"NENO ALIKUWA MUNGU"**

Sasa tupo katika nafasi ya kupima ni kwa namna gani "neno alikuwa Mungu". Mipango yetu na mawazo kwa sehemu ya muhimu ni yetu.'Ninakwenda Uingereza ni'neno' au kupasha habari inayoeleza kusudi langu, kwa sababu ni nia yangu. Vivyo hivyo mpango wa Mungu kwa Kristo unaweza kueleweka hivi."Maana (mtu) aonavyo nafsini mwake ndivyo alivyo"(Mithali 23: 7), naye Mungu aonavyo, ndivyo alivyo. Basi neno la Mungu au fikira ni Mungu:"neno lilikuwa na Mungu". Kwa sababu hii upo muungano ulio karibu sanan kati ya Mungu na neno lake: kama usambamba wa Zaburi 29: 8 ni mmoja:"Sauti ya Bwana yalitetemesha jangwani; Bwana alitetemesha jangwa la Kadeshi".Taarifa kama"ninyi hamkunisikiliza, asema Bwana"(Yer. 25: 7) ni ya

kawaida katika manabii. Kwa matokeo ya Mungu ana maana"ninyi hamjasikiliza neno langu lililonenwa na manabii"Daudi alichukuwa neno la Mungu kuwa taa yake na mwanga (Zab. 119: 105), lakini pia alisema:"Wewe u taa yangu, Ee Bwana: Na Bwana ataniangazia giza langu"(2 Sam. 22: 29), usambamba kati ya Mungu na neno lake unaonekana. Kwa sababu hii, linaeleweka kuwa neno la Mungu limeitwa kama vile ni mtu yeye mwenyewe, yaani, limesemwa kana kwamba ni mtu ingawa sivyo (tazama sehemu inayoitwa kuacha kitambo kilichokuwa kinaandikwa sehemu ya 5'Jambo la kuita kitu kama vile ni mtu').

Mungu ni kweli yenyewe (Yn. 3: 33; 8: 26; 1Yoh. 5: 10), na kwa sababu hii neno la Mungu ni kweli pia (Yn. 17: 17). Kwa jinsi hii Yesu mwenyewe anajitambulisha kwa maneno yake yanayokaribiana sana hata neno lake analitamka kama vile ni mtu:"Yeye anikataaye mimi, asiyeyakubali maneno yangu, anaye amhukumuye; neno hilo nililonena ndilo litakalo mhukumu siku ya mwisho"(Yn. 12: 48). Yesu anatamka neno lake kama ni mtu hasa, yaani, mwenyewe. Maneno yake yameitwa kama kwamba ni mtu, kwa sababu yalijumuika kwa karibu na Yesu.

Vile vile neno la Mungu limetamkwa kana kwamba ni mtu, yaani, Mungu mwenyewe, kwa Yohana 1: 1-3. Tumeambiwa kuhusu Neno hivi,"Vyote vilifanyika kuwa huyo"(Yn. 1: 3). Ingawa hivyo"Mungu aliumba"vyote kwa neno lake alililoamuru (Mwa. 1: 1). Kwa sababu hii, Neno la Mungu limesemwa kama vile ni Mungu mwenyewe. Kutokana na jambo hili la maana ya Ibada, inatakiwa kujua kwamba kwa njia ya neno lake kuwamo mioyoni mwetu, Mungu anaweza kutukaribia sana.

Ni bayana toka Mwanzo 1 ya kuwa Mungu aliumba, kwa kutumia neno lake, sio Kristo binafsi. Lilikuwa neno ambalo

limesemwa limefanya vyote, kuliko Kristo mwenyewe (Yn. 1: 1 - 3)."Kwa neno la Bwana mbingu zilifanyika; na jeshi lake lote (yaani, nyota) kwa pumzi ya kinywa chake …….. maana yeye alisema, ikawa"(Zab. 33: 6,9). Hata sasa ni kwa neno lake hata viumbe vya asili vinatenda kazi:"Huipeleka amri yake juu ya nchi: Neno lake lapiga mbio sana. Ndiye atoaye theluji kama sufu ……. Hulituma neno lake ….. maji yakatiririka"(Zab. 147:15 -18).

Neno la Mungu likiwa nguvu yake kuumba, alilitumia kumzaa Yesu toka tumbo la Mariamu. Neno, mpango wa Mungu limewekwa katika shughuli maalumu kwa Roho yake Mtakatifu (Luk. 1: 35), likafanya itunge mimba ya Kristo. Mariamu alitambua hili kwa kuitikia kwake habari kuhusu kutungwa mimba ya Kristo iliyokuwa inakuja:"Na iwe kwangu kama ulivyosema neno lako"(Luk. 1: 38).

Tumeona kwamba Neno /Roho ya Mungu imeleta kusudi lake, ambalo lilitangazwa kwenye Agano la Kale lote. Kiwango ambacho hii ni kweli kimeonyeshwa katika Matendo 13: 27, mahali ambapo Yesu amesemwa anasawazishwa na maneno ya manabii wa Agano la Kale:"(Wayahudi) hawakumjua yeye, wala maneno ya manabii"Kristo alipozaliwa, Neno /Roho yote ya Mungu ilielezwa na mtu Yesu Kristo. Kwa kuvuviwa, mtume Yohana alifurahi mno jinsi gani mpango wa Mungu wa uzima wa milele ulivyoelezwa na Kristo, ambaye wanafunzi waliweza wao wenyewe kupapasa na kuona. Basi, alitambua ya kuwa walikuwa wanalipapasa Neno la Mungu, mpango mzima wa wokovu unaopatikana kwa Kristo (1 Yoh. 1: 1-3) Wakati sisi wenyewe hatuwezi kumwona Kristo, nasi vile vile, tunaweza kufurahi kwamba kwa kumfahamu hakika yeye, tunaweza kufahamu kusudi lake Mungu kwetu na kwa sababu hiyo kuwa na uhakika wa uzima wa milele (1 Pet. 1: 8,9). Imetupasa tujiulize swali sisi wenyewe:'Je ! ni kweli namjua Kristo ?.

Kukubali tu kwamba mtu mzuri aitwaye Yesu aliwahi kuishi hakutoshi. Kwa kudumu, kuomba dua na kujifunza Biblia, inawezekana kwa haraka kumfahamu kuwa ni mwokozi wako na kujihusisha wewe mwenyewe naye kwa kubatizwa.

Maelezo mafupi chini ya ukurasa:"Hapo mwanzo kulikuwako Neno"huenda linafafanushwa wazo la Wayahudi kuwa Torati (Vitabu vitano vya Musa) vilikuwako kabla ya uumbaji. Yohana 1: 1-3 inasema ya kwamba jambo la muhimu kuelewa ni kuwa maneno hayo ya Mungu yalitabiri kumhusu Yesu; mpango wa Mungu kumhusu yeye ulikuwako kabla ya uumbaji (Luk. 1: 70).

### *Tumeacha kitambo sehemu ya 22: Yesu wa Historia*

Ikiwa, kama wengine wanavyodai, hakuna ushaidi wa kwamba Yesu wa Nazareti aliwahi kuishi, basi kuwepo kabisa Ukristo ni vigumu kueleza. Ni kuuliza jumla ya vitu vyote vikubwa kwa kutegemea mtu yeyote aamini kwamba mamilioni ya watu zaidi ya miaka 2,000 iliyopita wameweka imani zao kwa mtu fulani ambaye hakuwako, na kuwa na mkazo wa imani hii kwake hata wakakusudia kueneza imani yao kuhusu yeye ulimwenguni pote, aghalabu kwa hatari ya mateso na mauti. Wakristo na Wayahudi kwa ujumla hawana shida kukubali kuwa Mohamedi aliwahi kuwapo, ingawa wanakataa kazi yake na mafundisho. Kwa kweli tunakubali kuwa watu mashuhuri sana wa historia walikuwako bila kuhitaji kutazama tena kwa kuchunguza ushahidi. Mara nyingi uchambuzi umefanywa kwa upana wa matokeo yanayofahamika ya historia, k.m. ile vita ya Hastings ambayo ilifanyika mwaka 1066, ushahidi madhubuti umepatikana kwa kadiri ya ugumu kuupata kwa bahati.

Ni jambo la hakika kwamba kwa nguvu wanakana hivi kabisa kuwahi kuwako Yesu wa Nazareti hapana shaka ni kuuliza maswali ya jambo la uhakika kupita hali iliyotendwa, kutaka kutafuta udhuru wa kufaa kutokubali sababu zake kuwako na kufahamu kazi yake Masihi. Hili hasa linaonekana kweli inapofahamika kwamba wao wenyewe Wayahudi wa kwanza walikubali kuwa mtu aitwaye Yesu aliwahi kuishi katika karne ya kwanza. Ushahidi ufuatao wa historia ya kuwahi kuwako Yesu wa Nazareti unaonyesha kwamba hauwezi kuondoshwa kama theologia ya uvumbuzi wa watu. Taarifa nyingi za kusaidia katika sehemu hii ni habari zilizopatikana toka kwa Gary Hebermas,'Ushahidi wa Kale wa maisha ya Yesu'.

1). Ticitus alikuwa mwana -historia wa Roma ambaye vitabu vyake vikubwa viwili kuhusu karne ya kwanza ("Annals"- taarifa ya uvumbuzi ulioandikwa mwaka kwa mwaka, na"Histories"- masimulizi ya historia) vyote viwili vinamtaja Yesu na Ukristo. Aliandika katika"Annals"(karibu mwaka 115 B.K.).

"Kundi la watu waliochukiwa kwa machukizo yao, walioitwa Wakristo na watu wa vivi hivi. Kristo ni jina limetokana na Christus asili yake, alipata adhabu kubwa mno wakati wa kipindi cha utawala wa Tiberio kwenye mikono ya mmoja wa maliwali wetu, Pontio Pilato".

Mfalme Tiberio alitawala toka mwaka wa 14 - 37 B.K., wakati ambao ni kipindi Kristo aliuwawa, kulingana na taarifa. Ticitus vile vile anaeleza jinsi imani ya kundi hili"Ilivyotokea sio katika Uyahudi pekee, chanzo cha kwanza (mambo haya), bali hata katika Rumi", anaendelea kueleza jinsi Wakristo walivyochukiwa sana, nao wengi wao waliuwawa katika mji wa Roma. Taarifa yote hii ya Yesu inalingana na taarifa ya Agano Jipya, Wafuasi na mitume wa

kwanza walieneza mafundisho yao kwanza Uyahudi, na kisha katika ulimwengu wote wa Roma, pamoja na mji wa Rumi, kwa upinzani mkubwa kwao.

2.) Suetonius, mwandishi wa historia mwingine wa Kirumi, alitoa maelezo juu ya utawala wa Klaudio (41- 54 B K): "Kwa kuwa Wayahudi katika mji wa Roma walisababisha ghasia zilizoendelea kwa kuanzishwa Ukristo, yeye (Klaudio) aliwafukuza toka kwenye mji". Kwa kutokea, Matendo ya mitume 18: 2 yametolewa maelezo jinsi Wayahudi wawili Akila na Prisila iliwabidi waondoke Roma kwa sababu ya mateso ya Wayahudi. Suetorius alitoa maelezo baadaye kuhusu adha iliyowapata Wakristo kwenye kipindi cha Nero: Baada ya moto mkubwa kwenye mji wa Roma …….. vile vile Wakristo waliadhibiwa kwa kupigwa, jamii ya watu wanaokiri dini yenye imani mpya yenye kugombanisha". Ushahidi huu wa kuwako kundi la watu walioitwa"Wakristo"kwenye karne ya kwanza unadokeza kwamba mtu aliyeitwa"Kristo"aliwahi kuishi mapema katika hiyo karne.

3.) F.F. Bruce ("Mwanzo wa Ukristo"uk. wa 29, 30) unavuta macho kuangalia ukweli kwamba kuna ushahidi wa historia ya Mashariki mwa Bahari ya Mediterania iliyoandikwa na mwandishi wa mambo ya kale aliyeitwa Thallus kuhusu mwaka 52 B K. Bruce anaonyesha kila mahali ("Hati za Agano Jipya", uk. 113) ya kuwa mwanafunzi aliyeitwa jina Julius Africanus alinukuu toka kwa Thallus, akifanya mzaha maelezo yake ya giza Yesu aliposulubiwa ilikuwa sababu ya kupatwa kwa jua. Haya yanadokeza kwamba Thallus aliandika maelezo ya kusulubiwa Yesu kulikotokea miaka mingine kabla hajaandika historia yake mnamo mwaka 52 B.K.

4.) Pliny, afisa wa serikali ya Kirumi, ametajwa kwa kirefu kuwahi kuwako kwa kundi tendaji la watu walioitwa Wakaristo

kwa miaka iliyofuata ya karne ya Kwanza. Kushika kwao ibada ya kumbukumbu yeye ameitaja:"Walikuwa na desturi ya kukutana siku halisi iliyopangwa kabla, ilipokuwa nuru, wakaimba mistari miwili ya wimbo wa kumsifu Kristo"("Nyaraka za Pliny", zilitafsiriwa na W. Melmoth, Vol. 2, x: 96). Watawala wa Kirumi Trajani na Hadriani wote wawili wametaja matatizo ya kushughulika na Wakristo. Kwa Ushahidi wa hili, tazama"Nyaraka za Pliny", Vol.2,x:97 na Eusebio' Historia ya Ukasisi, IV: IX - moja - moja. Kuwako kwa kundi hili tangu karne ya kwanza na mshikamano wao wa ajabu wakati wa mateso ulidokeza kuwa walikuwa wafuasi wa tabia ya mtu wa historia ya kweli aliyeishi katika karne ya kwanza.

5.) Talmud, kitabu kitakatifu cha Wayahudi, katika Sanhedrin 43a kifo cha Yesu kimetajwa. Kimekubalika ya kwamba sehemu hii ya Talmud tarehe zake toka kipindi cha kwanza cha kitabu hicho kutungwa (yaani, mwaka 70 - 200 B.K)

"Siku kabla ya sikukuu ya Pasaka Yeshu (Yesu) alitundikwa msalabani. Kwa muda w a siku arobaini kabla ya kuuawa, habari ilitolewa ya kusema,'Atapigwa kwa mawe kwa sababu amefanya uchawi na kuvuta Israeli kukengeuka. Yeyote anayeweza kusema lolote kwa kumsaidida, aje mbele kwa niaba yake'. Lakini tangu hakuna chochote kilicholetwa mbele kwa kumsaidida akatundikwa kabla ya siku kuu ya Pasaka"

"Kuangikwa"linaweza kuwa ni namna ya neno la kusema kusulubiwa limetumika kama hivyo katika Agano Jipya (Gal. 3: 13; Luk. 23: 39). Fungu hili la maneno linaeleza Wayahudi wakitaka Yesu apigwe mawe (kulingana na sheria ya Musa, labda ?), bali yametajwa kuwa alitundikwa katika Agano Jipya jinsi gani Wayahudi iliwabidi watumie sheria za Kirumi kutoa kifo cha Yesu - ambacho cha kutundikwa.

Sanhedrin 43a vile vile inaeleza jinsi wanafunzi watano wa Yesu walihukumiwa na kupewa adhabu ya kifo, tena inaonyesha kwamba kwa mafundisho yaliyotokea zamani Wayahudi waliamini kuwahi kuwako Yesu wa historia. Hata Sanhedrin 106b yasema ya kuwa Yesu alikuwa na umri wa miaka 33 alipokufa; kikamilifu kama Agano  Jipya lilivyodai. Maier ("Siku kuu ya kwanza ya kufufuka", uk. 117, 118) ananukuu toka hati ya Wayahudi karne ya kwanza"Toledoth Jesu", yenye kadhia ya kwamba wanafunzi walijaribu kuuiba mwili wa Yesu baada ya kufa, lakini mtunza bustani aliyeitwa Yuda aliposikia mipango yao aliuhamisha mwili wa Yesu na kuupeleka mahala pengine, akaukabidhi baadae kwa Wayahudi. Justin Martyr akiandika mnamo mwaka 150 B.K ameandika kwamba Wayahudi walituma wajumbe maalumu ili waseme ya kuwa mwili wa Yesu uliibiwa ("Dialogue with Trypho", 108), na Tertullian ("On Spectacles", 30) ana maelezo mamoja wakati alipoandika katika mwaka 200 B. K.

Kati yao ushahidi huu  unaoendelea wa historia unaonyesha kwamba Wayahudi wa karne ya kwanza B.K waliamini aliwahi kuwako Yesu wa historia na alipata kifo cha nguvu.

6.) Mtunga hadithi wa Kiyunani, Luciana, akiandika katika karne ya kwanza, anawafanyia mzaha Wakristo ambao"wanamwabudu mtu hata leo (ambaye) alisulubiwa"(Lucian, The Death of Peregrine - yaani kifo cha mwendo usio mkunjufu, uk. 11-13, in"The works of Lucian"- katika kazi ya Lucian, Vol 4, iliyofasiriwa na Fowler wa Foweler).

7.) Josephus ni mwandishi wa historia anayejulikana vizuri sana wa karne ya kwanza. Katika"Antiquities"- yaani mambao ya Kale, aliyoandika mwaka 90 -95 B K, anamtaja Yakobo,"ndugu

yake Yesu, aliyeitwa Kristo". Vile vile anasema katika sehemu nyingine ya kitabu hicho hicho kwa maneno ambayo ni wazi yanathibitisha picha ya Yesu katika Agano Jipya:"Mara hiyo ulikuwa karibu muda huu Yesu mtu mwenye busara ….. Maana alikuwa ndiye aliyefanya matendo magumu ya kustaajabisha ….. Alikuwa Kristo ….. aliwatokea akiwa yu hai siku ya tatu, kama manabii wa Mungu walivyotabiri hivi mambo ya ajabu mengine kumi elfu yanayo muhusu yeye".

Maneno haya yameonyesha hivyo kama wengine walivyodai kwamba ni nyongeza katika kitabu. Kama bado ipo sababu ya kutumia maneno haya kusaidia shauri la kwamba alikuwepo mtu aliyeitwa Yesu wa Nazareti aliyeishi katika karne ya kwanza yametokelewa mambo ambayo lazima yakumbukwe ifuatavyo:

- Eusebio (Historia ya Kanisa la Kikristo, 1: XI) anainukuu sehemu hii ya Josephus.

- Wanafunzi walioheshimika wanasaidia somo hili la kwanza kuwa ni la asili, laweza kuonyesha kwamba sehemu hii imeandikwa kwa mtindo ule ule unaofungamana na kazi ya Josephus ( tazama kanuni za Danieli,"Ukimya wa Yesu, wa wakati ule ule"Uk. 21; J.N.D. Anderson,"Ukristo: Ushahidi wa Historia"uk. 20; F.F. Bruce,"Hati za Agano Jipya"uk. 108, 109)

- Kwa haya haupo ushahidi wa maneno ya kitabu kuwa nyongeza kwenye kitabu.

- Profesa Schlomo Pines amedai kwamba toleo kwa lugha ya Kiarabu la kazi ya Josephus limevumbuliwa ambalo karibu lilikuwa lenyewe ni la mwanzo. Maneno yaliyotajwa juu yanatokea humo, Lakini bila taarifa ya mafundisho ya wazi kuhusu ufufuo na

Yesu kuwa Masihi ambayo yalifanywa kwa kunakiliwa. Haya yanaonekana ni ya maana, kwa kuwa Josephus alikuwa Myahudi: Pines aliyoyapata ya kwanza aliyaweka katika majarida ya"The New York Times", Februari 12. 1972, ndani yake ananukuu mabishano wa maneno ya Josephus kuhusu Yesu toka toleo la Kiarabu"Kwenye kipindi hiki alipokuwepo mtu mwenye busara aliyeitwa Yesu > Mwenendo wake ulikuwa mzuri na alikuwa mwema. Watu wengi miongoni mwa Wayahudi na wa mataifa mengine wakawa wafuasi wake. Pilato alimuhukumu asulubiwe na kufa. Nao wale waliokuja kuwa wafuasi wake hawakuacha kumfuata. Walitoa taarifa ya kwamba aliwatokea siku tatu baada ya kusulubiwa na ya kuwa alikuwa yu hai; kwa kulingana, labda alikuwa ni Masihi ambaye Manabii wamesimulia maajabu"

Kwa ubora maelezo haya yanalaiki kwa yale ya Agano Jipya.

## *Tumeacha kitambo sehemu ya 23: Nimeshuka kutoka Mbinguni*

"Maana mkate wa Mungu ni yule ashukaye kutoka mbinguni na aupaye ulimwengu uhai ..... kwani nimeshuka kutoka mbinguni"(Yn. 6: 33, 38 B.H. N). Tafsiri toka Biblia Habari njema sio U.V.

Maneno haya, na mengine kama hayo, yametumika vibaya kusaidia wazo potofu kwamba Yesu alikuwako mbinguni kabla ya yeye kuzaliwa. Ingawa hivyo vipengele vifuatavyo inabidi vitazamwe:

1) Wanao amini katika Utatu na Mungu wanachukua maneno haya kuwa ni halisi ili kuthibitisha maana yao. Lakini, kama tutaelewa kwa maneno jinsi yalivyo, basi hii ina maana kwamba kwa njia isiyoeleweka Yesu mwenyewe alielea na kushuka kutoka

angani kuja chini. Sio tu kwamba Biblia imekuwa kimya kuhusu jambo hili, bali msemo wa kuwa Yesu alizaliwa mtoto mchanga katika tumbo la Mariamu unafanywa kuwa hauna maana. Yohana 6: 60 unaeleza mafundisha yanayohusu mana kuwa ni neno"gumu, ni nani awezaye kufahamu"(tafsiri ya Moffatt): yaani, tunahitaji kuelewa kuwa ni lugha ya kimfano iliyotumika.

2) Katika Yohana 6, Yesu anaeleza jinsi gani mana ilikuwa ni mfano wake mwenyewe. Mana ilitoka kwa Mungu katika maana ya kuwa Mungu ndiye aliyehusika kuiumba duniani; katika umbile haikupeperuka toka juu kwa Mungu mbinguni na kufika chini. Basi Kristo kuja toka mbinguni ieleweke vivyo hivyo; aliumbwa duniani, kwa uwezo wa Roho Mtakatifu ndani ya tumbo la Mariamu (Luk. 1: 35).

3) Yesu anasema kwamba"chakula (mkate) nitakachotoa ni mwili wangu"(Yn.6: 51) Makundi yanayoamini Utatu yanadai kwamba ilikuwa ni sehemu ya'Mungu' huyu Yesu aliyekuja toka mbinguni. Lakini Yesu anasema kwamba ulikuwa"Mwili"wake uliokuwa chakula kilichoshuka toka mbinguni. Vivyo hivyo Yesu anajumuisha chakula toka mbinguni na mwili wake mwenyewe kuwa'Mwana wa Adamu"(Yn. 6: 62), Sio'Mungu Mwana'.

4) Katika fungu hili la maneno kwa Yohana 6 kuna ushahidi mwingi wa kwamba Yesu hakuwa sawa na Mungu."Kama vile Baba aliye hai alivyonituma mimi"(Yn. 6: 57) mstari unaonyeshaYesu na Mungu hawashiriki usawa wa pamoja; ukweli ni kwamba "nami ni hai kwa Baba"(Yn. 6: 57) ni shida kuishi pamoja milele ambako hao wafundishao utatu husema.

5) Inabidi kuuliza, Ni lini na jinsi gani Yesu'alishuka' toka mbinguni? Wanaofundisha wazo la utatu hutumia mstari huu katika Yohana 6 ili"Kuthibitisha"kwamba Yesu alikuja toka mbinguni

alipozaliwa. Lakini Yesu anajisema mwenyewe kuwa"kile kishukacho kutoka mbinguni"(mstari 33, 50) kana kwamba ni jambo linaloendelea. Akizungumzia Yesu ni kipawa cha Mungu, Kristo alisema"Baba yangu anawapa ninyi chakula"cha kweli kutoka mbinguni (mst. 32 U.V). Wakati Yesu akisema maneno haya, tayari alikuwa'amekuja' kwa maana halisi kwa kuwa alikuwa ametumwa na Mungu. Kwa sababu hii, vile vile aliweza kusema kwa tendo lililopita tayari - yaani lilikwisha fanyika wakati uliopita:"Mimi ndimi chakula chenye uzima kilichushuka kutoka mbinguni"(mst. 51). Bali pia anasema kuhusu'kushuka' akiwa chakula kutoka mbinguni kwa namna ya kifo chake msalabani:"Na chakula nitakachotoa mimi ni mwili wangu, kwa ajili ya uzima wa ulimwengu"(mst. 51). Basi tunaye hapa Yesu akisema tayari'ameshuka' toka mbinguni, na anaendelea kushuka, bado inambidi ashuke kwenda chini kwa kifo chake msalabani. Ukweli huu pekee uthibitishe kwamba'Kushuka' kunamtaja Mungu akijifunua mwenyewe, kuliko kutaja tu kuzaliwa kwa Kristo. Kwa nguvu hili linathibitisha yote ya Agano la Kale yamtajayo Mungu'kushuka' yakiwa na maana moja tu. Hivyo Mungu akaona mateso ya watu wake katika nchi ya Misri, naye'akashuka' kuwaokoa kwa mkono wa Musa. Ameuona utumwa wetu wa dhambi basi'ameshuka' au amejidhihirisha yeye mwenyewe, kwa kumtuma Yesu mwenye maana kama Musa ili atuongoze toka utumwani.

## *Tumeacha kitambo sehemu ya 24: Je ? Yesu aliumba Dunia*

"Mzaliwa wa kwanza wa viumbe vyote: kwa kuwa katika yeye (Yesu) vitu vyote viliumbwa, vilivyo mbinguni na vilivyo juu ya nchi,vinavyoonekana na visivyoonekana ikiwa ni viti vya enzi, au Usultani, au enzi,au mamlaka; vyote viliumbwa kwa njia yake, na kwa ajili yake. Naye amekuwako kabla ya vitu vyote, na vitu vyote

hushikamana katika yeye. Naye ndiye kichwa cha mwili, yaani cha Kanisa; naye ni mwanzo, ni mzaliwa wa kwanza katika wafu ………"(Kol. 1: 15 -18). Maneno hayo ni mfano huu mmoja unaoweza kutoa fikira za kwamba Yesu hasa aliumba nchi.

1. Ikiwa huu mfano ulikuwa kweli, basi maneno mengine mengi yamepingana yanayofundisha kwamba Yesu hakuwahi kuwepo kabla ya kuzaliwa. Ni wazi taarifa iliyo katika kitabu cha Mwanzo inafundisha kuwa Mungu aliumba. Aidha Yesu au Mungu walikuwa waumbaji; kama tukisema kwamba Yesu alikuwa muumba ambapo Mwanzo inasema ni Mungu, moja kwa moja tunasema kwamba muumba Yesu alikuwa sawa na Mungu. Katika Suala hili haiwezekani kuielezea mistari mingi inayoonyesha tofauti zilizopo kati ya Mungu na Yesu  (Ona Somo la 8.2 kwa mifano hii).

2. Yesu alikuwa"Mzaliwa wa kwanza"ambaye anadokezwa kuanza. Hakuna ushahidi wa kwamba Yesu alikuwa ni"Mzaliwa wa kwanza"kabla ya uumbaji wa dunia yenyewe. Mafungu ya Maneno kama yaliyo kwa 2 Sam. 7: 14 na Zab. 89: 27 yalitabiri kwamba mtoto halisi wa Daudi atakuwa mzaliwa wa kwanza wa Mungu. Ni wazi hakuwahi kuwapo wakati maneno haya yakiandikwa, na kwa sababu hiyo sio wakati wa uumbaji wa mwanzo. Yesu alidhihirishwa"kwa uweza kuwa Mwana wa Mungu”, kwa ufufuo wa wafu (Rum. 1: 4) Mungu kwa kutimiza ahadi iliyomfufua Yesu kama ilivyoandikwa katika zaburi ya pili; Yesu akawa mzaliwa wa kwanza kwa kufufuliwa kwake. Ujue vilevile kuwa mwana aliyesimama  mkono wa kuume wa Baba yake ameungwa pamoja na kuwa mzaliwa wa kwanza (Mwa. 48: 13 -16), naye Kristo aliinuliwa mkono wa kuume wa Mungu baada ya kufufuliwa kwake (Matendo.2: 33; Ebra. 1:3).

3. Ni kwa maana hii ambayo Yesu amesemwa ya kuwa ni mzaliwa wa kwamza kutoka wafu (Kol. 1: 18), msemo uliosambamba na"mzaliwa wa kwanza wa viumbe vyote (Kol. 1: 15). Kwa hiyo anajisema mwenyewe kuwa ni"mzaliwa wa kwanza wa waliokufa …. Mwanzo wa kuumba kwa Mungu"(Uf. 1: 5, 3: 14). Yesu alikuwa ni wa kwanza kwa uumbaji mpya wa watu wasiokufa wanaume na wanawake,ambao ufufuo wao na kuzaliwa kabisa wakiwa ni wana wa Mungu wasiokufa umewezeshwa na kifo chake Yesu na ufufuo wake (Efe.2:10; 4:23,24; 2 Kor.5:17)"Katika Kristo wote (waamini wa kweli) watahuishwa. Lakini kila mmoja mahala pake; limbuko - wa kwanza ni Kristo, baadaye walio wake Kristo, atakapokuja"(1 Kor. 15: 22, 23). Hili ni jambo moja na Kol. 1: Yesu alikuwa ni mtu wa kwanza kufufuka kutoka wafu na kupewa kutokufa, alikuwa wa kwanza kwa uumbaji mpya, nao waamini wa kweli watafuata mfano wake mzuri akirudi.

4. Basi uuumbaji uliosemwa katika Kol.1 unatajwa uumbaji mpya, sio huo ulio kwenye kitabu cha mwanzo. Kwa njia ya kazi ya Yesu"Vitu vyote viliumbwa …… ikiwa ni viti vya enzi …au mamlaka"n.k. Paulo hasemi kwamba Yesu aliumba vitu vyote na kisha akatoa mifano ya mito, milima, ndege n.k. Vitu vya huu uumbaji mpya zinatajwa hizo thawabu ambazo tutazipata kwenye Ufalme wa Mungu."Viti vya enzi ….. Mamlaka n.k. wanatajwa waamini watakao fufuliwa jinsi watakavyokuwa"Wafalme na Makuhani, nasi tutakuwa na mamlaka juu ya nchi"(Uf. 5: 10) Vitu hivi viliwezeshwa kwa kazi ya Yesu."Katika yeye vitu vyote viliumbwa, vilivyo mbinguni ……"(Kol. 1: 16). Katika Efe. 2: 6 tunawasomo waamini walio katika Kristo wamekaa katika ulimwengu wa roho - yaani "wameketi sehemu za kimbingu”. Hivyo mistari hii inafundisha kwamba nafasi ya kupandishwa kiroho ambayo sasa tunaweza kuwa nayo, sawa na ile tutakayo kuwa nayo wakati ujao, yote imewezeshwa na Kristo."Mbingu na

nchi"zina "Mambo yote ambayo yalihitajika kuyafanyia upatanisho kwa damu ya Kristo msalabani"(Kol. 1: 16, 20), yanaonyesha kwamba"Vitu vyote …. Vilivyo mbinguni"wanatajwa waaminio ambao sasa wanaketi katika ulimwengu wa roho -"nafasi za kimbingu katika yeye Kristo Yesu"Sio vitu vyote vya kimaumbile vinavyotuzunguka.

## *Tumeacha kitambo sehemu ya 25:"Kabla ya Ibrahimu, Nalikuwepo"(Yn. 8: 58 )*

Maneno haya mara nyingi yametumiwa vibaya ya kwamba Yesu alikuwako kabla ya Abrahamu kuwepo. Ingawa hivyo, uchunguzi wa karibu unadhihirisha ukweli upo kinyume.

1. Yesu hasemi"Yeye Abrahamu asijakuwako, mimi nilikuwepo"Alikuwa ni mtoto aliyeahidiwa Abrahamu; ikiwa tunasema ya kwamba kimaumbile Yesu alikuwepo kabla ya wakati wa Abrahamu, ahadi alizoahidiwa Abrahamu tunazifanya zisiwe na maana.

2. Maneno yenyewe kwa Yohana 8: 58 ni mazungumzo ya Kristo na hao Wayahudi kuhusu Abrahamu. Kwa kadiri walivyohusika, Abrahamu alikuwa mtu mkuu ambaye ataishi. Yesu anasema"Mimi hivi sasa, kama ninavyosimama hapa, ni wa muhimu zaidi kuliko Abrahamu". Kama walivyosimama pale, Yesu alikuwa ni mtu wa kuheshimiwa kuliko Abrahamu. Anasema'Mimi ni wa muhimu sasa zaidi kuliko alivyo Abrahamu' Inawezekana kuelewa neno"kabla"lililo katika Yohana 8:58 pamoja na kutaja wakati mwingine, katika maana ya kwamba kabla ya kuwapo Abrahamu, Kristo alikuwemo ndani ya mpango wa Mungu tangu mwanzo kabisa wa ulimwengu. Ilikuwa ni sababu ya Yesu

kuwapo"kabla"ya Abrahamu katika maana hii ya kwamba alikuwepo"kabla"yake kwa umuhimu wake.

3. Neno la kuthibitisha linapatikana katika Yohana 8: 56;"Ibrahimu baba yenu, alishangilia kwa vile alivyoiona siku yangu, naye akaiona, akafurahi”. Muda pekee ambao Ibrahimu amesemwa alicheka na kufurahi moyoni ni pale alipopewa ahadi ya kuwa kwake atazaliwa mtoto; alifahamu kwamba mwishowe hiyo ahadi ilikuwa inamtaja Yesu (Mwa. 17: 17). Ibrahimu"aliona"mbele kwa Kristo alivyoahidiwa ahadi kumhusu Yesu. Katika maana isiyoeleweka kirahisi alitoa ufafanuzi kuhusu dhabihu ya Yesu kwa wakati uliokuwa unakuja:"Katika mlima wa Bwana itapatikana"(Mwa. 22: 14). Ilikuwa ni katika maana hii ambayo Yesu anamsema Ibrahimu kama alimwona. Ni kwa maneno haya ya kuzungumzia kuhusu ahadi ambayo Yesu aliweza kusema "Kabla ya Ibrahimu kuwako, mimi niko”. Alielewa kama tulivyokwisha eleza katika sehemu ya 3. 1 ya kuwa ahadi ambazo Mungu alimwahidi Ibrahimu zilikuwa zinafunua mpango kumhusu Yesu ambao Mungu alijua tangu mwanzo wa ulimwengu. Shabaha hiyo, iliyokuwepo"Kabla ya kuwako Ibrahimu”, ilifunuliwa kwa Ibrahimu kwa ahadi alizoahidiwa, na sasa zilitimilika machoni pa Wayahudi wa karne ya Kwanza, waliposimama makutano kumzunguka Yesu,"neno (la ahadi) lililofanywa mwili”.

4. Mara nyingi imedaiwa Yesu anataja katika kusema Jina la Mungu anaposema"Mimi niko”. Tulieleza katika Tumeacha tulichokuwa tunaandika sehemu ya 3 ya kuwa Yesu na watu wa kawaida kweli wanaweza kuchukua Jina la Mungu, pasipo maana hii ya kwamba wao ni Mungu mwenyewe katika mtu. Walakini, inaweza kuwa kwamba Yesu anatumia kiarifa cha wakati uliopo'kuwa'. Muundo wa maneno mamoja kwa Kiyunani unatokea katika Yn. 9: 9 mistari michache inayofuata. Majirani wa yule mtu

kipofu aliyeponywa waliulizana ikiwa kweli alikuwa mtu yule aliyekuwa akikaa na kuomba:"Wengine walisema, huyu ndiye: wengine walisema, Amefanana naye: Lakini yeye mwenyewe alisema, Mimi (ndiye). Hivyo mtu kipofu anasema"Mimi", kiasi kama Yesu aliposema"mimi niko"anathibitisha kwamba yeye ni Mungu kabisa, Basi inatubidi tuseme kwamba naye kipofu pia alikuwa"Mungu kabisa". Lakini, inafaa kujua kwamba Yahweh - au Kiswahili YAHU Jina la Mungu, kwa kweli maana yake ni"Mimi nitakuwa ambaye mimi nitakuwa"(Kut. 3:14 - kwenye pambizo la Biblia ya Kiingereza ya R.S.V. na R.V) kuliko kuwa "Mimi niko".

## *Tumeacha kitambo sehemu ya 26: Melkizedeki*

Mwanafunzi wa Biblia amesema kwa ukunjufu mwingi'Ameni' kwa maneno ya mtume Paulo alipoandika:"……. Ndugu yetu mpenzi Paulo …… katika nyaraka zake zote ….. katika nyaraka hizo yamo mambo ambayo ni vigumu kuelewa nayo; na mambo hayo watu wasio na Elimu, wasio imara, huyapotoa, kama vile wayapatavyo na maandiko mengine kwa uvunjifu wao wenyewe"(2 Pet. 3: 15, 16). Hakika huu unatumika juu ya ufafanuzi wa Paulo kwa Melkizedeki ulioandikwa kwa Waebrania; yeye mwenyewe alikiri aliingia ndani sana ya maandiko, akinena mambo ambayo yaweza kueleweka tu na waamini waliokomaa sana kwenye maandiko (Ebra. 5: 10, 11, 14). Basi sio kwa ajili ya kuweka elimu ya msingi juu ya mafunzo ya mistari hii; wala maneno ya Melkizedeki yasiyoonekane kwa upana kwenye fikira za hao ambao bado wanajifunza mafundisho ya msingi wa Maandiko.

“Kwa maana Melkizedeki huyo, mfalme wa selemu (Yerusalemu), kuhani wa Mungu aliye juu, aliyekutana na Ibrahimu alipokuwa akirudi katika kuwapiga hao wafalme, akambariki”; amesemwa kuwa"hana baba, hana mama, hana wazazi (kizazi), hana mwanzo wa siku zake, wala mwisho wa uhai wake; bali amefananishwa na mwana wa Mungu"(Ebra. 7: 1,3). Yesu alikuwako hasa kabla ya kuzaliwa, na kwa sababu hiyo hakuwa na wazazi wanadamu.

Yesu alikuwa na Baba (Mungu) na mama (Mariamu) na ukoo (tazama Math. 1, Luk. 3 na Yoh.7: 27). Kwa sababu hii'Melkizedeki’ hawezi kutajwa yeye mwenyewe. Isitoshe, Melkizedeki"alifananishwa na Mwana wa Mungu"(Ebra. 7: 3); hakuwa ni yeye mwenyewe Yesu, bali alikuwa na mfano mmoja halisi naye ambao umetumika na mwandishi kwa kusudi la kufundishia."Ametokea kuhani mwingine mithili ya Melkizedeki”, Yesu (Ebra. 7: 15) naye amefanywa kuhani mkuu'kwa mfano wa Melkizedeki"(Ebra. 5: 5,6).

Lugha ya Waebrania kumhusu Melkizedeki haiwezi kuchukuliwa tu kwa maneno jinsi yalivyo. Ikiwa Melkizedeki kwa maneno halisi hakuwa na Baba wala mama, basi mtu pekee anaweza kuwa ni Mungu mwenyewe; ni mtu wa pekee asiye na mwanzo ( 1 Tim. 6: 16; Zab.90: 2). Lakini taarifa hii haikubaliani na Ebra 7: 4:"Angalieni jinsi mtu huyo alivyokuwa mkuu"na vile vile kwa ukweli wa kwamba watu walimuona (ambapo Mungu hawezi kuonwa) na alimtolea dhabihu Mungu. Ikiwa ameitwa mtu huyo, basi huyo ilimpasa kuwa na wazazi halisi. Yeye kuwa,“hana Baba, wala Mama, na wazazi"kwa hiyo inabidi kutaja ukweli kwamba ukoo wa babu na wazazi wake taarifa zao hazikuandikwa. Taarifa za wazazi wa Malikia Esta hazikuandikwa, kwa hiyo maisha yake ya nyuma yameelezewa kwa namna hii.

Mordekai"alimlea …..Esta, binti wa mjomba wake: kwa kuwa hana Baba wala Mama …… nao walipokufa Baba na Mama yake, yule Mordeklai alimtwaa kuwa binti yake yeye"(Esta 2: 7).

Kitabu cha Mwanzo mara kwa mara kinatutambulisha kwa kirefu maisha ya mwanzo wa jamii na sifa zetu ambazo kitabu kinatuonyesha. Bali Melkizedeki anatokea bila kutamkwa, bila taarifa za wazazi wake, na kupotea kwenye maelezo kulingana kusiko tazamiwa. Hata hivyo hapawezi kuwepo shaka kwani alistahili heshima kubwa kabisa; hata Ibrahimu alipokuwa akirudi katika kuwapiga hao Wafalme, akambariki, ambaye Ibrahimu alimgawia sehemu ya kumi ya vitu vyote, jambo hili linaonyesha wazi ubora wa Melkizedeki kumpita Ibrahimu (Ebra. 7:2, 7).

Paulo sio anafanya tu mazoezi ya akili na Maandiko. Lilikuwepo tatizo kweli kabisa katika karne ya kwanza ambalo mashindano ya maneno ya kuweza kutatuliwa kuhusu Melkizedeki. Wayahudi wanahoji:'Ninyi Wakristo tuambieni kama huyu Yesu sasa anaweza kuwa kuhani wetu mkuu, mwenye kutoa maombi yetu na matendo yetu kwa Mungu. Lakini kuhani inampasa ukoo wake ujulikane, akithibitishwa katoka kabila ya Lawi. Na kwa vyovyote, ninyi wenyewe mnakiri Yesu alitoka kabila ya Yuda (Ebra. 7: 14). Tunasikitika, kwetu sisi Ibrahimu ndiye Kiongozi wetu mkuu na mfano (wa kuufuata) (Yn. 8: 33, 39), hatutamheshimu huyu Yesu'.

Kwa hiyo Paulo anajibu:

'Lakini mkumbukeni Melkizedeki. Taarifa ya kitabu cha Mwanzo imetengenezwa ili kuonyesha kwamba kuhani huyu mkuu hakuwa na ukoo wa babu yeyote; naye Masihi kwa pande zote mbili anakuwa mfalme na kuhani, ambaye ukuhani wake ni wa

kufuata mfano mzuri wa Melkizedeki (Ebra. 5: 6; Zab. 110: 4). Ibrahimu alikuwa na cheo kidogo kuliko Melkizedeki,hivyo mpindue mkazo wenu utoke kwa Ibrahimu hadi kwa Yesu, na muache kuleta maswali ya nasaba - ukoo kuwa ni ya lazima (tazama 1 Tim. 1: 4). Ikiwa mnatafakari ni kiasi gani Melkizedeki yeye ni mfano wa Yesu (yaani, habari zake moja moja zililenga mbele kwake), ndipo mngekuwa na ufahamu mkubwa wa kazi za Kristo'.

Na sisi wenyewe hili liwe somo letu.

**Somo La 7 : Maswali**

1. Andika orodha mbili za unabii ulio kwenye Agano la Kale unaomhusu Yesu.
2. Je ! Kimwili Yesu aliwahi kuwako kabla hajazaliwa ?
3. Ni katika maana gani Yesu anaweza kusemwa alikuwako kabla ya kuzaliwa kwake?

a) Akiwa ni Malaika
b) Akiwa ni sehemu ya Utatu
c) Akiwa Roho
d) Ni katika nia na kusudi la Mungu.

4. Ni taarifa zipi za kweli kumhusu Mariamu ?

a) Alikuwa mkamilifu, Mwanamke asiye na dhambi
b) Alikuwa ni Mwanamke wa kawaida
c) Alipata mimba ya Yesu kwa uwezo Roho Mtakatifu
d) Kwa sasa anatoa maombi yetu kwa Yesu.

5. Je ! Yesu aliumba nchi ?
6. Yohana 1:1-3 unaielewaje ?"Hapo Mwanzo kulikowako neno"kwa nini haimaanishi
7. Kwa sababu gani unadhani ni muhimu kuwa na hakika kumhusu Yesu endapo alikuwako kimwili kabla hajazaliwa ?

## 8:1 Asili Ya Yesu: Dibaji

Inabidi iwe ni moja ya fikira kubwa zaidi za kuhuzunisha katika ukristo ya kuwa Yesu Kristo hajapata heshima na kuinuliwa vinavyomstahili kwa sababu ya kushinda dhambi, kwa kuendeleza tabia kamilifu. Fundisho lililoenea la watu linamfanya Yesu ni Mungu mwenyewe. Kwa kuwa Mungu hajaribiwi (Yakobo 1:13) na wala hawezi kufanya dhambi. Kwa hiyo maisha yake hapa duniani yatakuwa ya kujisingizia, akiishi nje ya yale yanayowakabili wanadamu, lakini bila ya hisia za kiroho na kwa mwili kuchagua kati ya mambo mawili yanayowakabili watu, kwa kuwa yeye mwenyewe hakudhurika nayo.

Mawazo yao kwa mbali, makundi kama wamormoni na mashahidi wa Yehova kwa uzuri wanashidwa kufahamu ajabu ya Kristo ya kuwa ni Mwana pekee wa Mungu. Kwa hivi asingekuwa Malaika au mwana wa kawaida wa Yusufu? Watu wengine wamedokeza kwamba wakati wa maisha yake mwili wa Kristo ulikuwa kama ule wa Adamu kabla ya kuanguka. Mbali ya kukosa ushahidi kutoka kwenye Biblia kwa mtazamo huu, kufahamu ya kwamba Adamu aliumbwa na Mungu toka katika mavumbi kunakosekana, wakati Yesu 'aliumbwa' kwa kuzaliwa na Mungu ndani ya tumbo la Mariamu. Basi, ingawa Yesu hakuwa na baba binadamu, mimba yake ilitungwa na kuzaliwa kama sisi kwa jinsi zote. Watu wengi hawakubali ya kuwa mtu mwenye mwili wa dhambi ulio wetu aliweza kuwa na tabia timilfu. Ni ukweli ambao ni kizuizi cha kumwamini Kristo katika imani ya kweli.

Kuamini ya kuwa Yesu alikuwa na mwili kama wetu, bali hakuwa na dhambi kwa tabia yake, sio rahisi daima kushinda majaribu haya. Taarifa za maisha yake kikamilifu zimeandikwa kwa kirefu, zimeungana pamoja na maneno mengi ya Biblia yanayokana kuwa Yesu alikuwa Mungu, kwa kuthibitisha ufahamu na imani katika Kristo wa kweli. Ni vyepesi mno kudhani kwamba

alikuwa Mungu mwenyewe, na kwa sababu hii alikuwa mkamilifu mwenyewe bila sharti. Hata hivyo mtazamo huu unahitaji ushindi mkuu ambao Yesu alishinda dhambi na mwili wa kibinadamu.

Alikuwa na mwili wa kibinadmu; alishiriki kila moja ya mienendo yetu ya kutaka kufanya dhambi (Ebra 4:15), hata hivyo alishinda kwa kujiweka kwenye njia ya Mungu na kutafuta msaada toka kwake ili kushinda dhambi. Kwa hiari Mungu alimtoa, kwa upana na kwamba"Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu na nafsi yake"kwa njia ya mwanae mwenyewe kabisa (2 Kor 5:19)

### 8.2 Tofauti zilizopo kati ya Mungu na Yesu

Upo uwiano mzuri wa kuupokea kati ya maneno hayo yanayotia mkazo kiwango ambacho"Mungu alikuwa ndani ya Kristo", na hayo yatokezayo ubinadamu wake, fungu la maneno ya sasa yanamfanya Yesu asiweze kuwa Mungu mwenyewe kwa kuthibitisha kwa Biblia jambo hilo,"Mungu kabisa ambaye ni Mungu"kama mafundisho ya utatu kwa makosa yanavyosema.(Msemo huu:"Mungu kabisa ambaye ni Mungu"ulitumiwa kwenye baraza la Nicea katika mwaka wa 325 BK, ambako wazo la Mungu kuwa na 'nafsi tatu' lilitangazwa kwa mara ya kwanza, halikujulikana kwa wakristo wa kwanza) Neno 'utatu' halipatikani katika Biblia. Somo la 9 linachimba zaidi katika ushindi wa Kristo juu ya dhambi kabisa na sehemu ya Mungu ndani yake. Tunapoanza masomo haya, tukumbuke ya kuwa wokovu kuja kuupata unahitaji kumfahamu vyema Yesu Kristo wa kweli (Yohana 3:36; 6:53; 17:3). Mara moja tukifahamu

ukweli wa yeye kushinda dhambi na mauti, tunaweza kubatizwa katika jina lake ili tushiriki wokovu huu.

Moja ya maelezo mafupi yaliyo wazi ya uhusiano kati ya Mungu na Yesu yanapatikana katika 1Tim 2:5;"Mungu ni mmoja na mpatanishi kati ya Mungu na wanadamu ni mmoja, mwanadamu, Kristo Yesu ; Fikira juu ya maneno yaliyojitokeza sana yanatuongoza kwenye dhana inayojitokeza baada ya kufikiri sana ifuatavyo:-

Kuwepo Mungu mmoja tu, basi haiwezekani Yesu awe ni Mungu; ikiwa Baba ni Mungu na Yesu naye ni Mungu, basi wapo Miungu wawili."Lakini kwetu sisi Mungu ni mmoja tu, aliye Baba'(1Kor 8:6) 'Mungu Baba' kwa sabau hii ni Mungu pekee. Basi haiwezekani kwamba kunaweza kuwapo Mungu aliyejitenga aitwae 'Mungu mwana' kama mafundisho potufu ya utatu yasemavyo. Vivyo hivyo Agano la kale linatoa maelezo ya kumhusu YAHU, Mungu mmoja akiwa ni Baba (mfano Isaya 63:16; 63:8)

Nyongeza kwa Mungu huyu mmoja, kuna mpatanishi mwanadamu Kristo Yesu"-……… na mpatanishi mmoja……"Hili neno 'na' linaonyesha tofauti iliyopo kati ya Mungu na Kristo.

- Kristo kuwa"mpatanishi"maana yake ni kwamba yeye husimama kati ya- hivyo yeye ni mjumbe. Mpatanishi kati ya binadamu mwenye dhambi na Mungu asiye na dhambi hawezi kuwa na dhambi Mungu mwenyewe; ilibidi awe mtu asiye na waa, aliye na mwili ulio na dhambi wa mwanadamu."Mwanadamu Kristo Yesu"tunaachwa bila shaka kwenye usahihi wa maelezo haya. Hata kama alikuwa akiandika baada ya kupaa kwa Yesu, Paulo hamsemi"Mungu Kristo Yesu".

Mara kadha tumekumbushwa kuwa"Mungu si mwanadamu"(Hes 23:19; Hosea 11:9); lakini ni wazi Kristo alikuwa ni"mwana wa Adamu”, kama alivyoitwa mara nyingi katika Agano Jipya,"mwanadamu Kristo Yesu’’. Alikuwa ni"mwana wa aliye juu"(Luka 1:32). Mungu akiwa ‘Juu’ inaonyesha ana kipeo cha juu; Yesu kuwa"mwana aliye juu”inamaana hakuwa Mungu mwenyewe katika utu. Lugha kabisa ya Baba na Mwana ambayo imetumika kumhusu Mungu na Yesu, ni dhahirri haiwafanyi kuwa wapo sawa. Ingawa mwana anaweza kuwa na mifano halisi na baba yake, haiwezi kuwa ni mmoja yule yule, wala kuwa mzee kama baba yake.

Kwa kukubaliana na hii habari, kuna hesabu dhahiri iliyo tofauti kati ya Mungu na Yesu’ ambayo ni wazi inaonyesha ya kuwa Yesu hakuwa Mungu mwenyezi

| MUNGU | YESU |
|---|---|
| “Mungu hawezi kujaribiwa (Yakobo 1:13) | Kristo"alijaribiwa sawasawa na sisi kaika mambo yote (Ebr 4:15) |
| Watu hawawezi kumwona Mungu 1 Tim 6:16 Kut. 33:23) | Watu walimwona Yesu na walimpapasa (Yohana 1:1 huu ni mkazo |
| Mungu hawezi kufa - Hapatikani na mauti (Zab 90:2; ! Tim 6:16) | Kristo alikufa kwa siku tatu (Math 12:40; 16:21). |

Tujaribiwapo, tunasukumwa na tendo la kuchagua kati ya kutenda dhambi na kumtii Mungu. Aghalabu tunachagua kumwasi Mungu naye Kristo alikuwa na uamuzi ule ule, bali daima alichagua kuwa mtii. Kwa sababu hii alikuwa na uwezekano wa kutenda dhambi, ingawa hakutenda kwa kweli. Mungu hadhaniwi kwamba anauwezekano wowote wa kufanya dhambi. Tumeonyeshwa kuwa mzao wa Daudi aliyeahidiwa kwa 2 Sam 7: 12-16 ni dhahiri alikuwa Kristo. Mstari wa 14 unasema uwezekano wa Kristo kufanya dhambi ;"Akitenda dhambi nitamwadhibu”.

## 8.3 Asili Ya Yesu

Neno ‘hali ya tabia’ inatajwa kwa tabia ya kawaida sehemu muhimu ilivyo. Tumeonyesha katika somo la 1 ya kwamba Biblia inazungumzia hali ya tabia mbili - hiyo ya Mungu na hiyo ya binadamu. Kwa hali ya Mungu hawezi kufa, kujaribiwa n.k. Ni dhahiri kwamba Kristo hakuwa na mwili wa Mungu wakati wa maisha yake.Kwa hiyo Yesu alikuwa mwenye mwili wa mwanadamu kabisa. Kutokana na maelezo yetu ya neno ‘hali ya tabia’ itakuwa dhahiri kwamba Yesu hakuweza kuwa na miili miwili wakati ule ule. Ni muhimu kuelewa kuwa Kristo alijaribiwa kama sisi (Ebr 4;16) ili kwamba kwa kushinda kikamilifu majaribu aweze kuupata msamaha kwa ajili yetu. Mawazo mabaya ambayo ni msingi wa majaribio yetu yanakuja toka ndani ya mioyo yetu (Marko 7:15-23) toka ndani ya miili yetu wanadamu (Yakobo 1:13-15). Basi,ilikuwa ni lazima, kwamba Kristo awe na mwili wa binadanu ili kwamba aweze kuonja na kuyashinda haya majaribu.

**Waebrania 2:14-18 yamewekwa yote haya kwa maneno mengi:-**

“Basi, kwa kuwa watoto (sisi) wameshiriki damu na mwili (mwili wa kibinadamu) naye vivyo hivyo alishiriki yayo hayo (yaani hali ya tabia ile ile) ili kwa njia ya mauti amharibu….. ibilisi……. Maana ni hakika, hatwai asili ya Malaika bali anatwaa asili (hali ya tabia) ya mzao wa Ibrahimu. Hivyo ilimpasa kufananishwa na ndugu zake katika mambo yote, apate kuwa kuhani mkuu mwenye rehema,….ili afanye suluhu(upatanisho) kwa dhambi za watu wake. Na kwa kuwa mwenyewe aliteswa alipojaribiwa, aweza kuwasaidia wao wanaojaribiwa”.

Maneno haya yanaweka mkazo wa ajabu juu ya ukweli wa kwamba Yesu alikuwa wa asili ya mwanadamu:"Yeye naye vivyo hivyo"alishiriki yayo hayo (Ebra 2:14). Fungu hili linatumia maneno matatu yote yenye maana moja, kuleta maana alihsiriki asili"ile ile”; taarifa ingesema ‘alishiriki tu’, bali inasisitiza"alishiriki yayo hayo"Mstari wa 16 Waebrania mlango wa 2 kwa mfano mmoja unatoa maana ya kuwa Kristo hakuwa na asili ya malaika, kwa kuwa alikuwa mzao wa Ibrahimu, aliyekuja kuleta wokovu wa mkutano wa waaminio ambao wamekua wazao wa Ibrahimu. Kwa sababu hii, ilikuwa ni muhimu kwa Kristo awe na asili ya binadamu. Kwa namna yoyote ilimpasa kufananishwa na ndugu zake (Ebra 2:17) ili kwamba Mungu aweze kutupatia msamaha kwa njia ya dhabihu ya Kristo. Kusema kwamba Yesu hakuwa na mwili wa kibinadamu kabisa basi ni kutojua misingi kabisa ya habari njema za Kristo.

Popote waamini waliobatizwa wakitenda dhambi, wanaweza kumjia Mungu kwa kuungama dhambi zao kwa sala kupitia Kristo (1Yoh 1:9); Mungu anajua kwamba Kristo alijaribiwa kutenda dhambi hasa kama wao, bali alibaki kuwa mkamilifu, akashinda kabisa lile jaribu linalowashinda. Kwa sababu hii Mungu kwa ajili ya Kristo anaweza kutusamehe (Efeso 4:32). Basi, ni lazima tufahamu ni jinsi gani Kristo alijaribiwa kama sisi, na ilihitajika

awe na mwili kama wetu kuwezesha hili. Waebrania 2:14 ni dhahiri inasema kwamba Kristo alikuwa na mwili na damu kuwezesha hili."Mungu ni Roho"(Yn. 4:24) kwa asili, na ingawa ana mwili wenye kuonekana, ukiwa ni 'Roho' hana mwili wa nyama na damu. Kristo akiwa na mwili wa"nyama"maana yake ni kwamba kwa vyovyote hakuwa na asili ya Mungu wakati wa maisha yake.

Majaribio yaliyotangulia ya watu kushika neno la Mungu, yaani kushinda jaribu kabisa yote yalishindikana. Kwa sababu hiyo"Mungu kwa kumtuma mwanawe mwenyewe katika mfano wa mwili ulio na dhambi na kuwa dhabihu ya dhambi, aliihukumu dhambi katika mwili (Rum 8:3).

"Dhambi"ni kutaja uelekeo wa kuvunja sheria ambapo ni tabia yetu ya asili. Hii tayari tumeipa kipaumbele na tutaendelea kufanya hivo"kisha mshahara wa dhambi ni mauti". Ili kujiondoa kwenye hatari hii, binadamu anahitaji msaada toka nje. Yeye mwenyewe aonekana kutoweza kukamilika; kujikomboa hakukumo na hukumu ndani ya nyama za mwili. Basi, Mungu ameingila kati na kutupa mwanawe mwenyewe ambaye alikuwa na 'mwili wa nyama ulio na dhambi ambao sisi tunao'pamoja na mvuto wa kuelekea kutenda dhambi kama sisi tulivyo wepesi kufanya dhambi. Tofauti na binadamu yoyote Kristo alishinda kila jaribu, ingawa alikuwa na uwezekano wa kuvunja sheria kama tulivyo. Rum 8:3 hueleza jinsi Kristo alivyo na mwili wa kibinadamu ni"mwili ulio na dhambi". Mistari michache iliyotangulia Paulo alisema jinsi gani ndani ya mwili"halikai neno jema", na namna kwa asili mwili unavyopinga kumtii Mungu (Rum 7:18-23). Katika maneno haya yote yanastahajabisha zaidi kusoma ya kuwa Kristo alikuwa na"mwili ulio wa dhambi"katika Rum 8:3.Ilikuwa sababu hii na huko kushinda mwili wake, hata tunayo njia ya kuuepuka mwili wetu;

kwa nguvu Yesu alijua hali ya dhambi ya asili ndani ya mwili wake kidokezao cha kwamba alikuwa"mwema"na mkamilifu wa tabia ya asili alijibu:"Kwanini kuniita mwema? Hakuna aliye mwema ila mmoja, ndiye Mungu"(Marko 10:17,18)

Wakati mwingine watu walianza kushuhudia ukuu wa Kristo kwa sababu ya mfululizo wa miujiza ya kuonekana dhahiri aliyoifanya. Haya hayakumpatia faida"kwa kuwa yeye aliwajua wote, na kwa sababu hakuwa na haja na mtu kumshuhudia habari za wanadamu"(Yn. 2:23-25). Kwa sababu ya elimu yake ya kujua mwili wa mwanadamu (alijua yote kuhusu huu), Kristo hakutaka watu wamsifu yeye mwenyewe kwa haki yake mwenyewe, kwa kuwa alijua ni kiasi gani uovu ulivyokuwamo ndani ya mwili wake mwenyewe wa kibinadamu.

### 8.4 Ubinadamu Wa Yesu

Taarifa zilizo katika injili zinatoa mifano mingi jinsi Yesu alivyo kuwa na mwili wa mwanadamu kikamilifu. Habari imetolewa ya kwamba alichoka akaketi vivi hivyi kisimani (Yn 4:6)"Yesu alilia", Lazaro alipokufa (Yn 11:35). Kwa ukubwa sana, taarifa ya mateso yake ya mwisho yamekuwa ni ushahidi wa kutosha wa ubinadamu wake:"Sasa roho yangu imefadhaika", alikiri alipomwomba Mungu amuokoe toka kwenye kifo chake cha msalaba (Yn 12:27)."Aliomba akisema, Baba yangu ikiwezekana kikombe hiki kiniepuke (cha mateso na mauti); walakini si kama nitakavyo mimi, bali kama utakavyo wewe"(Math 26:39). Mstari huu unaonyesha kwamba kwa namna nyingine nia ya Kristo, au matakwa, yalikuwa tofauti na nia ya Mungu.

Wakati wa maisha yake yote Kristo alitoa mapenzi yake kwa kuyaelekeza kwa yale ya Mungu akijitayarisha kwa ajili ya

majaribio ya mwisho msalabani. Mimi siwezi kufanya neno mwenyewe; kama nisikiavyo ndivyo nihukumuvyo; na hukumu yangu ni ya haki; kwa sababu siyafuati mapenzi yangu mimi; bali mapenzi yake aliyenituma"(Yn 5:30). Tofauti hii kati ya mapenzi ya Kristo na ya Mungu ni ushahidi wa kutosha kwamba Yesu hakuwa Mungu.

Katika maisha yetu tunategemewa kukua katika maarifa ya kumjua Mungu, tukijifu- nza kutokana na majaribu tunayopata katika maisha. Kwa hili, Yesu alikuwa ni mfano wetu mkuu. Hakuwa na majaribu kamili ya Mungu yaliongizwa ndani yake zaidi kuliko tuliyonayo. Tangu utoto,"Yesu akazidi kuendelea katika hekima na kimo (yaani, kukua kiroho mfano Efe 4:13), alimpendeza Mungu na wanadamu (Lk 2:52)."Yule mtoto, akakua akaongezeka nguvu (akakua) katika roho"(Luka 2:40). Mistari hii miwili inaonyesha ukuaji wa mwili wa Kristo ikiwa sambamba na kukuwa kwake kiroho; maendeleo ya ukuaji ulitoka ndani yake pande mbili kwa kawaida na kwa kiroho. Ikiwa"mwana ni Mungu", kama imani ya Athanasi isemavyo kuhusu 'utatu', hii isengewezekana. Hata mwisho wa maisha yake, Kristo alikiri kwamba hakujua hasa ni lini atarudi mara ya pili, ingawa Baba alijua (Marko 13:32).

Kutii mapenzi ya Mungu ni jambo lingine yanatupa sote kujifunza kwa kipindi chote cha wakati. Naye Kristo ilimpasa kupitia njia ya kujifunza kumtii Baba yake, kama ipasavyo mwana yeyote."Na ingawa ni mwana, alijifunza kutii (yaani kumtii Mungu) kwa mateso hayo yaliyompata; naye alipokukwisha kukamilishwa (yaani, akiisha kua ki- roho), akawa sababu ya wokovu wa milele."Kwa matokeo yake kamili ya kukua kiroho (Ebr 5:8,9), Wafilipi 2:7,8 (zaidi limefafanuliwa katika somo la kuacha kitambo kilichoandikwa sehemu ya 27) imetoa taarifa ya hii

njia moja ya kukua Yesu kiroho, na kuishia kwenye mauti ya msalabani."Alijifanya hana utukufu, akatwaa namna ya mtumwa (yaani kwa mwenendo)……. alijinyenyekeza akawa mtii….. mauti ya msalaba."Msemo uliotumika hapa unaeleza jinsi gani kwa fahamu Yesu hakugeuka katika maendeleo ya kiroho, mwenyewe akijinyenyekeza zaidi na zaidi, kwa sababu hiyo"akawa mtii"kufanya mapenzi ya Mungu ili afe msalabani, Hivyo basi"akakamiliswa"kwa kuitikia kwa usahihi mateso yake.

Ni dhahiri kutokana na hii Yesu ilimpasa kuwa na fahamu, bidii yake mwenyewe kuwa mwenye haki; hakulazimishwa kuwa hivyo na Mungu, tendo ambalo lingemfanya yeye kuwa ni wa bandia tu. Kwa kweli Yesu alitupenda, aliutoa uhai wake msalabani toka kuendesha hivi. Mkazo ule ule juu ya upendo wa Kristo kwetu ingekuwa sio kweli ikiwa Mungu ndiye aliye mshurutisha kufa msalabani (Efe. 5:2,25; Uf 1:5; Gal2:20). Ikiwa Yesu alikuwa ni Mungu,basi asingekuwa na uchaguzi bali kuwa mkamilifu, ndipo afe juu msalabani. Kama Yesu alikuwa na chaguzi hizi, zatufanya tufahamu upendo wake, ili tutengeneze uhusiano wetu naye.

Ilikuwa sababu ya hiari ya Kristo kujitoa uhai wake hata Mungu akapendezwa naye: Ndiposa"Baba anipenda, kwa sababu nautoa uhai wangu ili ni utwae tena. Hakuna mtu aniondoleye bali mimi nautoa uhai mwenyewe."(Yn. 10:17,18). Mungu akiwa amependezwa mno na utiifu wa hiari wa Kristo ni vigumu kuelewa ikiwa Yesu alikuwa Mungu, akiishi toka maisha ya kibinadamu kama kwa namna nyingine ya ushahidi wa kuwa pamoja na mwanadamu aliye wa dhambi (Math 3:17; 12:18;17:5). Taarifa hizi za Baba kufurahia utii wa mwanawe, ni ushahidi wa kutosha kuwa Kristo alikuwa na uwezekano wa kuasi, bali akiwa anasikia mwenyewe nafsini alichagua kutii.

**KRISTO KUTAKA WOKOVU.**

Kwa sababu ya asili yake ya mwanadamu, Yesu alipata ugonjwa mdogo uchovu n.k kama sisi tupatavyo. Kwa hiyo kinachotokea ni kwamba asingalikufa msalabani, angekufa kwa namna yeyote kama kwa uzee. Kwa mtazamo huu Yesu alihitaji kuokolewa na Mungu toka kwenye mauti. Kwa mkazo akitambua hili, Yesu"alimtolea yule awezaye kumwokoa na kumtoa katika mauti; maombi na dua pamoja na kulia sana machozi, akasikilizwa kwa jinsi alivyokuwa mcha Mungu"(Ebra 5:7). Jambo la hakika ni kwamba Kristo alimwomba Mungu kusudi amwokoe kutoka katika mauti halielezwi lolote la yeye kuwa Mungu ndani ya mtu. Baada ya ufufuo wa Kristo, mauti"haimtawali tena"(Ram 6:9), ukidokeza ya kuwa hapo awali alikuwa na mwili uliotawaliwa na mauti.

Zaburi nyingi ni za kutabiriwa kwa Yesu; wakati aya zingine kutoka zaburi zikinukuliwa kumhusu Kristo katika Agano jipya, inafaa kusadiki ya kwamba mistari mingine katika Zaburi yamhusu yeye vile vile. Kuna idadi ya sababu ambazo zimekaziwa kwa kuonyesha ya kuwa Kristo anahitaji wokovu toka kwa Mungu.

- Zab 91:11,12 imenukuliwa kumhusu Yesu katika Math 4:6. Zaburi 91:16 inatoa utabiri jinsi gani Mungu alimpa Yesu wokovu"Kwa siku nyingi (yaani uzima-wa milele) nitamshibisha, nami nitamuonyesha wokovu wangu”. Zab.
- : 69:21 kusulubiwa kwa Kristo (Math 27:34); Zaburi, nzima yatoa mawazo ya Kristo juu ya msalaba;"Ee Mungu uniokoe….Uikaribie nafsi yangu, uikomboe Mungu wokovu wako utaniinua"(Mst 1,18,29.).
- Zab. 89 ni ufafanuzi juu ya ahadi ya Mungu kwa Daudi kumuhusu Kristo. Kuhusu Yesu, Zaburi 89:26 ilitabiri"Yeye ataniita (Mungu), wewe Baba yangu. Mungu wangu na mwamba wa wokovu wangu”.
-

Maombi ya Kristo kwa Mungu ili kupata wokovu yalisikiwa; alisikiwa kwa ajili ya yeye kuwa kiroho, sio kwa sababu ya nafsi yake katika 'utatu'(Ebra 5:7) Ya kwamba Mungu alimfufua Yesu na kumtukuza na mwili usiopatikana na mauti ni msemo mkuu kwenye Agano Jipya.

- "Mungu …….alimfufua Yesu……. Mtu huyo Mungu amemtukuza kwa mkono wake wa kiume, awe Mkuu na Mwokozi"(Mdo 5:30,31).
- "Mungu…..amemtukuza mtumishi wake Yesu,….. ambaye Mungu amemfufua katika wafu"(Mdo 3:13,15).
- "Yesu huyo Mungu alimfufua"(Mdo 2:24,32,33).
- "Yesu mwenyewe alitambua yote haya alipomuomba Mungu amtukuze (Yohana 17:5; 13:32; 8:54).

Ikiwa Yesu alikuwa ni Mungu mwenyewe, basi mkazo wote huu ungekuwa nje ya maana iliyoongelewa, kwa kuwa Mungu hawezi kufa. Yesu asingekuwa na haja ya kuokolewa ikiwa alikuwa ni Mungu. Kama alikuwa ni Mungu aliyemtukuza Yesu yanatolewa maelezo ya ubora wa Mungu zaidi yake, na utofauti wa Mungu na Yesu. Kristo hakuwa"Mungu wa milee kabisa (mwenye) miili miwili……mwili wa uungu na wa kibinadamu", kama nakala 39 za kwanza za Kanisa la Uingereza zisemavyo. Kwa maana kabisa ya neno, kiumbe anaweza kuwa na asili moja tu. Ushahidi tunauweka ni wa kuvunja kuwa Kristo alikuwa na asili yetu wanadamu.

### 8.5 Uhusiano Wa Mungu Na Yesu

Kupima ni jinsi gani Mungu alimfufua Yesu kunatuongoza tufikirie uhusiano kati ya Mungu na Yesu. Ikiwa wote wawili ni wa"usawa pamoja"…… milele pamoja; kama fundisho la utatu pamoja linavyosema, basi tungetegemea uhusiano wao kuwa huo

wa uwiano ulio sawa. Tayari tumeona ushahidi mkubwa wa kuwa hili haliko hivyo. Uhusiano kati ya Mungu na Kristo ni hali moja kati ya mume na mke;"kichwa cha kila mwanaume ni Kristo;na kichwa cha mwanamke ni mwanamume; na kichwa cha Kristo ni Mungu"(1Kor 11:3). Mwanamume akiwa ni kichwa cha mke, basi Mungu ni kichwa cha Kristo, ingawa wana kusudi lile la umoja kama linavyokuwepo kati ya mke na mme. Hivyo"Kristo ni wa Mungu"(1Kor 3:23), kama mke anavyomhusu mwanamume

Mungu Baba mara nyingi ameelezewa kwa maneno kuwa Kristo ni wa Mungu. Uhakika wa kwamba Mungu amesemwa kuwa ni"Mungu ni Baba wa bwana wetu Yesu Kristo"(1Petro 1:3; Efe 1:17) hata baada ya Kristo kupaa kwenda mbinguni, kunaonyesha ya kuwa huu sasa ni uhusiano wao, kama ulivyokuwapo wakati wa maisha ya mwili hapa duniani. Mara nyingi mkazo umetiwa na hao waminio katika utatu pamoja ya kwamba Kristo amesemwa tu kuwa chini- mdogo kuliko Mungu ni wakati wa maisha yake duniani. Nyaraka katika Agano jipya ziliandikwa miaka mingine baadaye Kristo alipopaa kueleke mbinguni, lakini bado Mungu amesemwa kuwa Kristo ni wa Mungu na Baba. Bado Yesu anasema Baba ni Mungu wake

Ufunuo, kitabu cha mwisho cha Agano Jipya, kiliandikwa karibu miaka 30 baada ya Kristo kutukuzwa na kupaa, lakini kinasema Mungu ni"Mungu na baba yake (Kristo)" (Uf 1:6 U.V) katika kitabu hiki Kristo aliyefufuliwa na kutukuzwa alitoa ujumbe kwa waminio. Analitaja"hekalu la Mungu wangu…. Jina la Mungu wangu…… mji wa Mungu wangu"(Uf 3:12). Hivi inathibitisha ya kwamba hata sasa anadhani Baba kuwa ni Mungu wake na kwa sababu hii yeye (Yesu) sio Mungu.

Wakati wa maisha yake ya mwili wa kufa,Yesu alimtaja Baba yake kwa njia hii. Alisema napaa kwenda kwa "Baba yangu na

Baba yenu; na kwa Mungu wangu na Mungu wenu"(Yohana 20:17). Msalabani Yesu alionyesha ubinadamu kabisa : Mungu wangu, Mungu wangu, kwa nini umeniacha? (Math 27:46). Maneno haya hayawezi kueleweka ikiwa yanasemwa na Mungu mwenyewe. Uhakika wa kwamba Yesu alimtolea dua Mungu"na kulia sana na machozi”ndani yake wenyewe inaonyesha hali ya kweli ya uhusiano wao (Ebra 5:7; Luka 6:12).ni bayana Mungu hawezi kujiombea mwenyewe. Hata sasa, Kristo anamuomba Mungu kwa ajili yetu (Rum 8:26,27; 2Kor 3:18 U.V).

Sasa tumeonyesha kwa maelezo ya kwamba uhusiano wa Mungu na Kristo wakati wa maisha yake duniani haukuwekwa kimsingi tofauti na sasa ulivyo. Kristo amesimulia kuwa Mungu ni Baba yake na Mungu wake, naye alimwomba Yeye; nafasi iyo hiyo inapatikana sasa, baada ya ufufuo na kupaa kwa Kristo. Wakati wa maisha yake duniani, Kristo alikuwa mtumishi wa Mungu (Mdo 3:13,26; Isaya 42:1; 53:11). Mtumishi hufanya mapenzi ya Bwana wake, na kwa njia yeyote hawi sawa na bwana wake (Yohana 31:16). Kristo alitia mkazo wa kwamba uwezo na mamlaka aliyokuwa nayo vilitoka kwa Mungu, sio kutoka kwake mwenyewe;"Mimi siwezi kufanya neno mwenyewe…. Sitafuti…… bali mapenzi yake aliyenituma … Mwana hawezi kutenda neno mwenyewe….."(Yn.5:30,19).

### *Tumeacha kitambo sehemu ya 27: “Akiwa Yuna na namna ya Mungu”*

“……Yesu alikuwa yuna namna ya Mungu, naye hakuona kule kuwa sawa na Mungu kuwa kitu cha kushikamana nacho; bali alijifanya hana utukufu, akatwaa namna ya mtumwa"(Flp 2:5-11). Aya hizi zimechukuliwa kuwa na maana ya kwambaYesu alikuwa

ni Mungu, lakini alipozaliwa akawa binadamu. Ikiwa jambo hili ni kweli, basi kila kipengele kilicho katika masomo ya 7na 8 inabidi yaelezewe mbali vile vile. Imekubalika kwamba aya moja hairuhusiwi kuachana na maana yeyote ya mafundisho ya Biblia. Ni jambo la maana kwamba hili ndilo fungu pekee la maneno ambalo laweza kuwekwa mbele ili kueleza mtengano wa ‘kukosekana kiungo’ katika wazo la wanaoamini katika utatu pamoja - ni jinsi gani Yesu alihama toka kuwa ni Mungu katika Mbingu na kuwa kitoto kichanga ndani ya tumbo la Mariamu. Uchambuzi ufuatao unataka kuonyesha kwa maneno maana ya fungu hili hasa lilivyo.

1. Kuna idadi ya maneno ambayo karibu yanatoka ndani ya fungu hili ambayo yanaachana kabisa na wazo la wanaoamini katika utatu:

a) "Kwa hiyo tena Mungu alimwadhimisha mno”, Yesu,"akamkirimia yaani alimpa jina"(mst 9) yaonyesha kwamba Yesu hakujiadhimisha mwenyewe- ni Mungu aliyefanya hivyo. Imetokea kuwa hakuwa kwenye hali ya kuadhimishwa kabla Mungu hajamfanyia hivi, kwenye ufufuo wake.

b) Muunganiko mzima wa mfululizo wa matendo ya kujinyenyekeza Kristo mwenyewe na baadaye kuadhimishwa na Mungu yote yalikuwa kwa ajili ya utukufu wa"Mungu Baba"(Mst 11). Mungu Baba kwa sababu hii hana uwiano ulio sawa na Mwanae.

2. Maneno yenyewe ya fungu hili inabidi yapimwe kwa uangalifu. Paulo haanzi tu kusema kuhusu Yesu ‘nje ya utaratibu’. Anataja moyo wa Yesu katika Wafilipi1:8. Tukirudi katika Wafilipi 1:27 Paulo anaanza kusema umuhimu wa hali yetu ya moyo. Hii imekuzwa katika aya za awali za sura ya 2;"Mwe na nia moja….. roho- moyo mmoja…… mkinia mamoja….. kila mtu

asiangalie mambo yake mwenyewe, bali kila mtu aangalie mambo ya wengine. Iweni na nia moyo uo huo ndani yenu, ambayo ilikuwamo pia ndani ya Kristo Yesu…"(Wafilipi 2:2-5).Basi Paulo anazungumzia umuhimu wa kuwa na moyo, nia kama wa Yesu, alijitoa kuwatumikia wengine kwa upole. Aya zinazofuata kwa sababu hii zinaainisha juu ya ubinadamu wa moyo ambao Yesu alionyesha, si kuzungumzia badiliko lolote la mwili.

3. Yesu alikuwa,"Yuna namna ya Mungu"Tumeonyesha katika somo la 8:3 ya kuwa Yesu alikuwa wa asili ya mwanadamu na kwa hiyo huu hauwezi kumtaja Kristo akiwa na mwili wa Uungu. Biblia habari njema B.H.N fungu hili la maneno lina upotoshaji mkubwa hapa. Kwa kupita, ijulikane ya kuwa matoleo mengine ya siku hizi yamepanga ‘usomaji rahisi’, yameelekea kurahisisha juu ya maana halisi ya maneno ya Kiyunani, nayo yamelekea kutoa ufafanuzi kuliko kutafsiri kwa maneno ya hakika. Wafilipi 2:5-8 huu ni mfano uliojulikana tangu zamani. Walakini, huu sio kuvunja sifa yao katika kutumia kwa namna nyingine.

“Namna"(Kiyunani ‘morphe’) haiwezi kutajwa asili ya mwili imethibitishwa na Flp 2:7 akinenwa Kristo akitwaa ‘namna ya mtumwa’. Alikuwa yuna namna ya Mungu, lakini akatwaa namna ya mtumwa. Mwili wa asili wa mtumwa hauna tofauti na ule wa binadamu yeyote mwingine. Kwa mapatano na maneno yenyewe, tunaweza kwa usalama kufasiri huu kuwa na maana ya kuwa ingawa Yesu alikuwa mkamilifu alikuwa na nia kama ya Mungu kabisa, lakini akapenda kutwaa mwenendo wa mtumwa. Aya zingine zilizofuata Paulo anatutia moyo"tufanane na kufa kwake (Kristo)"(Wafilipi 3:10). Tushiriki ‘morphe’, namna ya Kristo aliyotuonyesha kwa kifo chake. Hii haina maana hatuwezi kushiriki mwili wake aliokuwa nao wakati ule, kwa kuwa tayari tuna mwili wa kibinadamu. Tusijibadilishe wenyewe mwili huu, bali tunahitaji

kubadili mwendo wa kuwaza, ili kwamba tuweze kuwa na morphe au mfano wa akili aliyokuwa nayo Kristo kwa kufa kwake.

Neno la Kiyunani ‘morphe’ maana yake ni mfano chapa au kufanana. Wanadamu wamesemwa wana"mfano(morphe) wa utauwa"(2Tim 3:5). Gal 4:19 yamsema"Kristo aumbike-awe Morphe ndani yenu”waaminio. Kwa kuwa alikuwa na tabia timilifu, mwendo wa ukamilifu kama Mungu kwa kuwaza, Yesu alikuwa"yuna namna ya Mungu”.Kwa sababu hii hakuona kule kuwaza au kujua ya kwamba kwa maana hii alikuwa mmoja pamoja na Mungu. B.H.N. inatoa tafsiri tofauti kwa fungu hili la maneno ikisema lakini hakufikiri kwa kule kuwa sawa na Mungu ni"kitu cha kung’ang’ania kwa nguvu". Ikiwa tafsiri hii ni sahihi (ambayo vile vile inasaidiwa na U.V kwa sehemu)basi hii inatia kosa, kabisa wazo la kwamba Yesu alikuwa ni Mungu. Kulingana na B.H.N tafsiri yake, Yesu kwa muda hakushiriki wazo la kuwa sawa na Mungu alijua kwamba alikuwa chini ya Mungu, na sio uwiano sawa Naye.

4. Kristo"akajifanya kuwa hana utukufu”, Ukitamka unabii wa kusulubiwa kwake katika Isaya 53:12:"Alimwaga nafsi yake hata kufa”, Yeye mwenyewe akatwaa namna (mwenendo) ya- wa mtumwa”. Kwa msimamo wake wa kuwa kama mtumwa kwa wafuasi wake (Yn. 13:14), ulijionyesha kwa ukuu na kufa kwake msalabani (Math.20:28). Isaya 52:14 ulitabiri kuhusu mateso ya Kristo ya kwamba juu ya msalaba"uso wake ulikuwa umeharibiwa sana zaidi mtu yeyote, na umbo lake zaidi ya mwanadamu”. Uendelevu huu wa kujinyenyekeza mwenyewe"hata mauti, naam mauti ya msalaba"ulikuwa ni jambo lingine lililotokea wakati wa maisha yake na kufa, sio wakati wa kuzaliwa kwake. Tumeonyesha maneno ya fungu hili yakitaja nia ya Yesu, unyenyekevu ulioshikwa kwa ajili yetu ukiwa ni mfano wa kuiga. Aya hizi

yapasa basi kusema maisha ya Yesu alipokuwa hapa duniani, katika mwili wetu wanadamu, na jinsi gani alijinyenyekeza mwenyewe, mbali ya kuwa na moyo unaolingana na Mungu, kupima haja zetu.

5. Ikiwa Kristo alikuwa Mungu kwa asili na kisha aliacha nyuma akatwaa asili ya mwananadamu, kama wanaoamini katika utatu pamoja na wanavyo jaribu kutafsiri fungu hili la maneno, basi Yesu hakuwa 'Mungu kabisa' wakati akiwa duniani: lakini waaminio katika utatu husema hivyo. Yote haya yanaonyesha kuachana kunako fanywa na wanao kubali kutoa pamoja ufafanuzi uliofanywa kama huu wa utatu.

6. Hatimaye, maana inayohusu maneno"ambaye yeye mwanzo alikuwa yuna namna ya Mungu". Hapa yeye mwazo haina maana ya kwamba asili alikuwa ni wa milele. Kristo kuwa"yuna namna ya Mungu" basi ina maana ya kwamba alikuwa na mfano na Mungu (kiakili) mstari huu haudokezi kuwa tangu mwanzo wa wakati alikuwa namna hiyo.

**Somo La 8 : Maswali**

1. Je! Biblia inafundisha kwamba Mungu ni utatu pamoja?
2. Orodhesha tofauti tatu kati ya Mungu na Yesu.
3. Ni kwa njia zipi zifuatazo Yesu alikuwa tofauti nasi?
a)Kamwe hakutenda dhambi b)Alikuwa ni mwana pekee wa Mungu
c)Hakuweza kamwe kutenda dhambi d)Alilazimishwa na Mungu kuwa mwenye haki
4 Ni kwa nji zipi zifuatazo Yesu alikuwa pamoja na Mungu
a)Alikuwa na asili ya Mungu wakati wa maisha yake duniani b)Alikuwa na tabia timilifu kama ya Mungu c)Alijua sana kama Mungu d) Alikuwa moja kwa moja sawa na Mungu
5. Ni kwa njia zipi zifuatazo Yesu alikuwa kama sisi?
a)Alikuwa na majaribu yetu yote na yapatikanayo na wanadamu

b)Alitenda dhambi wakati akiwa kijana
c)Alihitaji wokovu.
d)Alikuwa na asili ya mwanadamu.

6. Ni taarifa zipi zifuatazo ni za kweli?
a)Yesu alikuwa mwili mkamilifu na tabia kamilifu
b)Yesu alikuwa na mwili wa dhambi lakini tabia kamilifu.
c)Pande mbili Yesu alikuwa Mungu kabisa na Mwanadamu kabisa
d)Yesu alikuwa na asili ya Adamu kabla ya kutenda dhambi

7. Je; Yesu alikuwa na uwezekano wa kutenda dhambi?

### 9.1 Ushindi Wa Yesu

Somo lilotangulia limeonyesha kwa maneno jinsi gani Yesu alikuwa na asili yetu wanadamu, alijaribiwa kutenda dhambi kama sisi tu. Tofauti iliyopo kati yetu na yeye ni kwamba alishinda dhambi kabisa; wakati ana mwili ulio na dhambi, alionyesha tabia iliyo kamilifu ya kumpendeza Mungu. Ajabu ya hii isikome kutufunua tunapoongeza kuielewa. Upo mkazo ulio rudiwa rudiwa katia Agano Jipya kuhusu tabia kamilifu ya Kristo:

-Yeye "alijaribiwa sawa sawa na sisi katika mambo yote, bila kutenda dhambi" (Ebr.4:15).

-Yeye "asiyejua dhambi alimfanya …." "Dhambi haimo ndani yake" (2Kor. 5:21; 1Yoh.3:5).

-"Yeye hakutenda dhambi, wala hila haikuonekana kiywani mwake"(1Petro 2:22).

"Mtakatifu, asiye na uovu, asiye na waa lolote, aliyetengwa na wakosaji" (Ebr 7:26)

Taarifa za Injili zinaonyesha kwa maneno jinsi gani watu, ndugu zake walivyotambua ukamilifu uliotirika kutoka kwenye tabia yake, ulijionyesha katika maneno yake na matendo . Mke wa Pilato alitambua ya kwamba alikuwa ni " mtu mwenye haki" (Math 27:19) asiyesitahili kuadhibiwa: askari wa Kirumu aliyetazama mwenendo wa Kristo wakati ametundikwa juu ya msalaba ilibidi atoe maelezo, "Hakika yake, mtu huyu alikuwa mwenye haki" (Luka 23:37). Awali katika maisha yake, Yesu aliwauliza Wayahudi swali: "Ni nani miongoni mwenu anishuhudiae ya kuwa nina dhambi?" (Yohana 8:46). Kwa hili hawakuwa na jibu.

Kwa ajili ya tabia yake kamilifu Yesu alikuwa udhihirisho wa Mungu katika mwili(1 Tim 3:16); Alitenda na kunena kama Mungu alivyotaka afanye binadamu. Kwa sababu hii alikuwa anarudisha nuru kamili ya Mungu."mfano wa Mungu asiyeonekana" (Kol.1:15). Kwa sababu hii hakuna haja kwa watu wanaopatikana na mauti kumwona Mungu kwa mwili wake.Kama vile Yesu alivyoeleza "aliyeniona mimi amemuona Baba"; basi unasemaje! wewe,Tuonyeshe Baba (kimwili)?" (Yohana 14:9). Akiishi katika ulimwengu wa dhambi, na kusumbuliwa na dhambi katika mwili wetu kabisa, ni vigumu kwetu kufahamu ujumla na ukubwa wa Kristo kiroho na ukuu wake; ya kwamba mtu aliye na mwili wetu afunue kabisa haki ya Mungu katika tabia yake. Kuamini jambo hili inatakiwa imani ya kweli zaidi kuliko kukubali tu nadharia ya wazo la kwamba Kristo alikuwa Mungu mwenyewe; inaeleweka ya kuwa mafundisho potofu ya utatu wa Mungu na "Uungu wa Kristo yana watu wengi mno kwa kuwa ni rahisi kuyakubali."

Kwa kuwa alikuwa ni wa asili yetu, Kristo inambidi afe. Alikuwa mtoto wa Adamu kwa kuzaliwa na Mariamu, na watoto wote wa Adamu inabidi wafe (1Kor 15:22). Inawapasa wazao wote watokanao na Adamu kufa kwa sababu ya dhambi yake, bila kutazama haki zao: "Walakini mauti inatawala…. Ikiwa kwa kukuosa kwake yule mmoja (Adamu) wengi walikufa….. Uamuzi-hukumu ilikuja kwa njia ya mtu mmoja (Adamu) ikaleta adhabu (kifo) …. Kwa maana ikiwa kwa kukuosa mtu mmoja watu wengi waliingizwa katika hali ya wenye dhambi; na kwa sababu hii inawapasa kufa (Rum 5:14-19; 6:23). Akiwa mzao wa Adamu Kristo ,'alifanywa' kuwa 'mwenye dhambi' na kwa hiyo ilimbidi afe, kama watoto wote wa Adamu walivyoainishwa kuwa watenda dhambi nao wamestahili mauti kwa sababu ya dhambi. Mungu hakubadili jambo hili, Aliliacha likamdhuru Kristo naye pia.

Mungu "alimfanya kuwa dhambi kwa ajili yetu, yeye asiyejua dhambi" (2Kor 5:21)

Mbali ya Yesu, wazao wote wa Adamu wamestahili kupata adhabu hii, kwa maana sisi sote tumekosa. Yesu ilimpasa kufa kwa sababu alikuwa na maumbile yetu, akishiriki laana iliyokuja juu ya watoto wa Adamu. Lakini kwa kuwa yeye hakufanya chochote kinachostahili afe "Mungu akamfufua kutoka katika wafu, akaufungua uchungu wa mauti, kwa sababu haikuwezekana ashikwe nao"(Matendo 2:24 U.V).Kristo alidhihirishwa kwa uweza kuwa mwana wa Mungu, kwa jinsi ya roho ya utakatifu, kwa ufufuo wa wafu" (Rum 1:4). Hiyo ilikuwa sababu ya tabia kamilifu ya Kristo, "roho yake ya utakatifu", hata akafufuliwa kwa utukufu.

Kristo sio tu alikufa msalabani kwa sababu alikuwa na mwili wa kibinadamu. Kwa hiari yake aliutoa uhai wake kamili kuwa kipawa kwetu; alionyesha upendo wake kwetu na kufa "kwa ajili ya dhambi zetu" (1 Kor 15:3) akijua ya kwamba kwa njia ya mauti atatupatia wokovu toka dhambi na mauti (Efe. 5:2, 25; Ufunuo 1:5; Gal 2:20). Kwa kuwa Yesu alikuwa mkamilifu kitabia aliweza kushinda matokeo ya dhambi kwa sababu ya kuwa wa kwanza kufufuka toka wafu na kupewa uzima wa milele. Wale wote ambao wana jishirikisha na njia ya Kristo kwa njia ya ubatizo na kuishi kama Kristo wanatumaini la ufufuo huu na kupewa thawabu.

Ndani ya jambo hili imelala maana yenye utukufu wa ufufuo wa Kristo. Ni "Uhakikisho" wa kwamba tutafufuliwa na kufanyiwa uamuzi kwa yale tuliyotenda katika mwili (Mdo 17:31), na kama kweli tumeishi kama yeye tutashiriki thawabu yake ya uzima wa milele, "tukijua ya kwamba yeye aliyemfufua Bwana wetu Yesu atatufufua sisi nasi pamoja na Yesu" (2Kor 4:14; 6:14; Rum 6:3-5). Jinsi tulivyo wakosaji tumestahili mauti ya milele (Rum. 6:23).

Lakini, kwa sababu ya maisha kamilifu ya Kristo, utiifu hata katika mauti yake na kufufuliwa kwake, Mungu anaweza kutupatia kipawa cha uzima wa milele, kulingana kabisa na mambo yake yote makuu.

Kwa kuhamisha matokeo ya dhambi zetu, Mungu "atatuhesabia kuwa na haki" (Rum. 4:6) kwa njia ya imani katika ahadi zake za wokovu. Tunajua ya kwamba dhambi huleta mauti, kwa hiyo kama kweli tunaamini ya kwamba Mungu atatuokoa nayo, yatupasa tuamini ya kwamba atatuhesabu kana kwamba sisi ni wenye haki, ingawa sivyo. Kristo alikuwa mkamilifu; kwa tendo kweli la kuwa ndani ya Kristo, Mungu anaweza kutuhesabu kana kwamba sisi tuwakamilifu, ingawa sisi wenyewe hatupo hivyo. Mungu alimfanya Kristo "kuwa dhambi kwa ajili yetu, yeye asiyejua dhambi; ili tuweze kufanywa wenye haki na Mungu kwa yeye (Yesu)" (2Kor. 5:21) yaani, kwa tendo la kuwa ndani ya Kristo kwa njia ya kubatizwa na kuishi kama Kristo. Hivyo kwa wale walio "katika Kristo",….. alifanywa kwetu… haki, na utukufu na ukombozi" (1Kor. 1:30,31); aya zifuatazo basi zinatutia moyo kumtukuza Kristo kwa mambo makuu aliyotenda; "Kwa maana Habari Njema inaonyesha wazi jinsi Mungu anavyowakubali watu kuwa waadilifu, jambo hili hufanyika kwa imani"(Rom 1:17 B.H.N). Basi kuelewa mambo haya ni sehemu muhimu ya kujua Injili ya kweli

Yote haya yamewezeshwa kwa kufufuka kwake Kristo. Yeye alikuwa "limbuko" la mavuno yote ya wanadamu watakao pewa uzima wa milele kwa kufaulu kwake(1Kor. 15:20), "mzaliwa wa kwanza"wa jamaa mpya wa kiroho watakaopewa mwili wa Uungu (1Kor :18; Efe 3:15). Basi, ufufuo wa Kristo umemwezesha Mungu awahesabu wamino katika Kristo kana kwamba ni wenye haki, kwa kuwa wamefunikwa na kuzungukwa na haki yake. Kristo

“alitolewa kwa njia ya makosa yetu na kufufuliwa ili tupate kuhesabiwa haki” (Rum 4:25). Inachukua fikira zetu, kuamua kuamini mambo haya ili kwa kweli kusadikishwa ya kwamba tunaweza kweli kuhesabiwa na Mungu kana kwamba sisi ni wakamilifu. Kristo anaweza kutulinda kwenye kiti cha hukumu “bila mawaa mbele ya utukufu wake” “watakatifu wasio na mawaa wala lawama” (Yuda mst: 24, Kolos 1:22; Efes 5:27). Kuwa na mwili ulio na dhambi na kushindwa daima kiroho, kwa kweli kuamini jambo hili kunahitaji imani thabiti. Kuweka mkono wetu juu tu kwenye mafundisho yaliopangwa hayahusiani na aina hii ya imani. Kwa kufahamu vema ufufuo wa Kristo kunako leta kusudi la imani yetu: “… Mungu, aliyemfufua katika wafu…. hata imani yenu na tumaini lenu (kama hili la ufufuo) liwe kwa Mungu” (Petro 1:21).

Ni kwa kubatizwa vyema katika Kristo ndipo tunaweza kuwa “ndani ya Kristo” na kwa sababu hii kuzungukwa na haki yake. Kwa ubatizo sisi wenyewe tunashiriki mauti yake na ufufuo (Rum 6:3-5), ambao ni njia yetu kukombolewa toka dhambi, ‘kwa kuhesabiwa haki”(Rum 4:25)

Mambo ya kustaajabisha ambayo tumeona sehemu hii yapo nje kabisa na fahamu zetu ila tukibatizwa. Kwenye ubatizo wenyewe tunashiriki damu ya Kristo iliyomwagika msalabani; waaminio hufua “mavazi yao, na kuyafanya meupe katika damu ya mwana kondoo” (Ufu. 7:14). Katika mfano, basi wanakuwa wamevikwa mavazi meupe maana yake ni haki ya Kristo ambayo wamehesabiwa haki (Ufu 19:8). Inawezekana kuzitia uchafu hizi nguo kutokana na dhambi zetu (Yuda mst 23); tukifanya hivi baada ya kubatizwa, yatupasa tena kutumia damu ya Kristo kuziosha ziwe safi kwa kumuomba Mungu atusamehe kwa njia ya Kristo.

Kinachofuata baada ya kubatizwa ni bado tunatakiwa kujitahidi kubaki ndani ya nafasi ambayo wakati huo tumeingia. Ipo haja ya kawaida, siku zote kujihoji kujipima nafsi kwa dakika chache kila siku, kwa kusali daima na kumuomba msamaha. Kwa kufanya hivi siku zote kwa unyenyekevu tutakuwa na ujasiri wa kwamba, kwa ajili ya kufanikiwa na haki ya Kristo, kwa kweli tutakuwepo kwenye ufalme wa Mungu. Yatupasa tutake kukutwa tukiwa ndani ya Kristo siku ya kufa kwetu na Kristo ajapo, "tusiwe na haki (yetu) wenyewe….bali ile ipatikanayo kwa imani iliyo katika Kristo, haki ile itokayo kwa Mungu, kwa imani.(Filip 3:9).

Mkazo ulirudiwa-rudiwa ni kuwa na imani kunakosababisha kuhesabiwa haki, kunaonyesha kwamba kwa vyovyote hatuwezi kupata wokovu kwa matendo yetu; kupata wokovu ni kwa neema: "mmeokolewa kwa neema kwa kuwa na imani ;sio kwa nafsi zenu ni kipawa cha Mungu sio kwa matendo" (Efes 2:8:9). Ikiwa kuhesabiwa haki ni 'kipawa' (Rum 5:17), nao wokovu vilevile. Makusudi yetu katika kufanya matendo yoyote ya utumishi wa Kikristo basi uwe ule wa kushukuru kwa kile alichotendea Mungu kutuhesabia haki kwa njia ya Kristo, na kwa sababu hii kutupatia njia ya wokovu. Ni jambo la kutisha kufikiri tukitenda matendo ndio tutaokoka. Hatutafanikiwa kuwa katika kupata wokovu kama tu tukifikiria hivi: ni kipawa ambacho hatutapata kwa upendo tu wa kuitika kwa kushukuru kwa undani, ambako hautaonekana katika matendo yetu. Imani ya kweli huzaa matendo kama haizai imekufa (Yakobo 2:17).

### 9.2 Damu Ya Yesu

Mara nyingi imesemwa katika Agano Jipya ya kwamba kuhesabiwa kwetu haki na kupata wokovu ni kwa damu ya Yesu (

K.m 1Yoh 1:7; Ufu 6:9; 12:11; Rum 5:9). Kufahamu maana ya damu ya Kristo, yatupasa tuelewe ya kuwa ni neno la awali la Biblia kwamba “uhai wa wanyama wote ni katika hiyo damu yake” (Law 17:14). Pasipo damu mwili hauwezi kuishi; kwa hiyo ni mfano wa uhai. Hii yaeleza uzuri wa maneno ya Kristo, “Msipo ula mwili wake mwana wa Adamu, na kuinywa damu yake, hamna uzima ndani yenu”. (Yoh 6:53).

Dhambi huleta mauti (Rum 6:23), yaani, kumwaga damu ambayo hushika uhai uzima. Kwa sababu hii wana wa Israel walitazamiwa kumwaga damu kila wakati walipotenda dhambi, ili kuwakumbusha kuwa dhambi inaleta mauti. Na katika torati (ya Musa) karibu vitu vyote husafishwa kwa damu, na pasipo kumwaga damu hakuna ondoleo (la dhambi Ebra 9:22). Kwa sababu hii, Adamu na Hawa walipojifunika wenyewe na majani ya mtini hayakukubalika; badala yake, Mungu alimchinja mwanakondoo na kuwagawia ngozi za kujifunika dhambi zao (Mwanzo 3:7,21). Vivyo hivyo, dhabihu za wanyama wa Abeli ilikubalika zaidi kuliko matoleo ya mboga ya Kaini, kwa kuwa alielewa jambo hili ya kwamba pasipo kumwaga damu ingekuwa vigumu kusamehewa na kukubalika kumkaribia Mungu (Mwanzo 4:3-5)

Matukio haya yanalenga mbele kwenye umuhimu mkubwa wa damu ya Kristo. Hasa haya kivuli chake ni kwenye Pasaka, ambako watu wa Mungu iliwabidi kupaka damu ya mwana kondoo juu ya miimo ya nyumba yao ili kuokolewa kutokana na mauti. Hii damu ilikuwa inaonyesha mbele kwa ile ya Yesu, ambayo yatupasa sisi tufunikwe. Kabla ya wakati wa Kristo wayahudi iliwabidi kutoa dhabihu za wanyama kwa ajili ya dhambi zao, kufuata sheria ya Mungu kwa mkono wa Musa. Walakini, huku kumwaga damu ya mnyama ilikuwa kwa madhumuni ya kufundisha. Dhambi

inaadhibiwa kwa mauti(Rum 6:23); haiwezekani kwamba wanadamu waweze kuua mnyama kuwa badala ya mauti yake yeye mwenyewe. Mnyama aliyekuwa anamtoa hakufahamu jema na baya; hakuwa mwakilishi wake kabisa: "Maana haiwezekani damu ya mafahali na mbuzi kuondoa dhambi". (Ebr. 10:4)

Basi swali linajitokeza, ni kwa sababu gani Wayahudi inawabidi kutoa sadaka za wanyama walipotenda dhambi? Paulo anajumlisha majibu mbali mbali kwa swali hili katika Gal. 3:24; "Torati ilikuwa kiongozi kutuleta kwa Kristo". Wanyama walio waua kuwa matoleo ya dhambi ilibidi wawe hawana doa - bila waa (Kut 12:5; Law 1:3, 10 n.k). Hizi zililenga mbele kwa Kristo, "Mwana kondoo asie na ila" (1Petr. 1:19). Damu za hao wanyama zilikuwa zipo badala ya ile ya Kristo. Zilikubaliwa kama dhabihu kwa ajili  ya dhambi kwa kuwa zililenga mbele kwenye sadaka kamili ya Kristo, ambayo Mungu alijua ataifanya. Kwa sababu hii Mungu aliweza kusamehe dhambi za watu wake walioishi kabla ya kuja Kristo. Mauti ya Kristo "ilifanyika kwa kukomboa makosa yaliyokuwa chini ya Agano la kwanza" (Ebr 9:15) , Yaani, Torati ya Musa (Ebr 8:5-9). Dhabihu zote zilizotolewa chini ya Musa zililenga mbele kwa Kristo sadaka kamili kwa ajili ya dhambi, yeye, "azitangue dhambi kwa dhabibu ya nafsi yake" (Ebr 9:26; 13:11'12; Rum 8:3; 2Kor 5:21).

Tulielezwa katika sehemu ya 7.3 jinsi gani Agano la kale lote, hasa Torati ya Musa, ilionyesha mbele kwenye ujio wa Kristo. Chini ya Torati njia ya kumkaribia Mungu ilkuwa kwa kuwakilishwa na Kuhani Mkuu alikuwa mpatanishi kati ya Mungu na wanadamu chini ya Agano la Kale kama ilivyo chini ya Agano jipya (Ebra 9:15). "Torati yawaweka wanadamu walio wanyonge kuwa makuhani wakuu;  bali hilo  nenola kiapo….. limemweka Mwana, aliyekamilika hata milele" (Ebr 7:28). Kwa kuwa wao

wenyewe walikuwa wakosaji, watu hawa hawakuwa katika nafasi ya kuwapatia watu msamaha wa kweli. Wanyama waliowatoa kwa ajili ya dhambi kwa kweli hawakuwa wawakilishi wa kweli wa wakosaji. Sadaka iliyotakiwa ni mwanadamu mkamilifu, ambaye kwa vyovyote ni mwakilishi wa mwanadamu mkosaji, ambaye anatoa dhabihu inayokubaliwa kwa ajili ya dhambi ambayo watu wanaweza kufaidika kutokana na kujiunga na dhabihu hiyo wao wenyewe. Kwa namna hii, Kuhani mkuu mkamilifu alitakiwa ambaye aweza kuwasaidia wenye dhambi ambao huwafanyia suluhu, na kwa kuwa mwenyewe aliteswa alipojaribiwa, aweza kuwasaidia wao wanaojaribiwa (Ebra 2:14-18).

Yesu kwa matakwa haya kwa ukamilifu anafaa. “Maana ilitupasa sisi tuwe na kuhani mkuu wa namna hii aliye mtakatifu”, asiye na uovu, asiyekuwa na waa lolote” (Ebra 7:26). Haina haja daima ya kutoa daima dhabihu ya dhambi zake mwenyewe wala kustahili kifo tena (Ebra 7:23,27). Kwa mwangaza huu maandiko yanatoa ufafanuzi juu ya Kristo kuwa ni kuhani wetu mkuu;” Naye kwa sababu hii, aweza kuwaokoa kabisa wao wamjiao Mungu kwa kupitia kwake; maana yu hai siku zote ili awaombee” (7:25). Kwa sababu alikuwa na asili ya mwanadamu, Kristo, akiwa ni kuhani wetu mkuu asiye na kombo lolote, “aweza kuwachukulia kwa upole wao wasiojua na wenye kupotea; kwa kuwa yeye mwenyewe yu (alikuwa) katika hali ya udhaifu” (Ebra 5:2). Kulingana na Kristo taarifa hii inarudia ya kwamba, “yeye naye vivyo hivyo alishiriki yayo hayo” alitwaa mwili wetu (Ebra. 2:14).

Ikiwa kuhani mkuu wa kiyahudi alifanya upatanisho kwa watu wa Mungu pekee. Israel, basi Kristo ni kuhani pekee wa Israel wa roho, waliobatizwa katika Kristo, wakiisha ifahamu Injili ya kweli. Yeye ni kuhani “mkuu wa Nyumba ya Mungu” (Ebra 10;21), ambayo ina wale waliozaliwa tena kwa kubatizwa (1Petro 2:2-5),

wakiwa na tumaini la kweli la Injili (Ebra 3:6). Tukifahamu faida za ajabu za ukuhani wa Kristo basi zaweza kututia moyo tubabatizwe katika jina lake; bila hizi hawezi kutuombea.

Tukiisha batizwa katika Kristo, kwa bidii tutautumia vya kutosha ukuhani wa Kristo, kweli, tuna wajibu halisi kulingana na unavyotupasa kuutendea kazi. "Basi , "Kwa njia yake yeye, na tumpe Mungu dhabihu ya sifa daima (Ebra 13:15). Mpango wa Mungu kutupatia Kristo kuwa kuhani wetu ilikuwa kwamba tumtukuze; kwa hiyo tutumie siku zote njia yetu kuelekea kwake Mungu katika Kristo ili tumtukuze. Ebra 10:21-25 inaorodhesha idadi ya majukumu ambayo tunayo kwa sababu ya Kristo kuwa kuhani wetu: "Akiwa ni kuhani mkuu juu ya nyumba ya Mungu.

1. Na tumkaribie (Mungu) wenye moyo wa kweli, kwa utimilifu wa imani, hali tumenyunyiziwa mioyo tuache dhamiri mbaya; tumeoshwa miili kwa maji safi". Kuuelewa ukuhani wa Kristo maana yake ni kwamba tubatizwe kwa yeye ("miili yetu ioshwe"), kamwe tusiendeleze dhamiri mbaya mioyoni mwetu. Kama tukiamini upatanisho wa Kristo, tunakuwa kwenye umoja na Mungu (KUWA- PAMOJA-NA MUNGU) kwa dhabihu yake Kristo.

2. "Na tushike sana ungamo la tumaini letu, lisigeuke". Tusiende upande toka kwenye mafundisho ya kweli yaliotufanya tuulewe ukuhani wa Kristo.

3. " Tuangaliane sisi kwa sisi na kuhimizana katika upendo na kazi nzuri; wala tusiache kukusanyika pamoja". Kwa upendo tujifunge pamoja na wengine wanaoelewa na kufaidika kutokana na ukuhani wa Kristo; tendo hili hasa ni kwa kukusanyika pamoja katika ibada ya ushirika, kwa hiyo tunakumbuka dhabihu ya Kristo (tazama sehemu ya 11.3.5)

Kufahamu mambo haya yatatujaza ujasiri wa unyenyekevu ambao kwa kweli yatatufikisha kwenye wokovu, kama tukibatizwa na kudumu ndani ya Kristo. “Basi na tukikaribie kiti cha neema kwa ujasiri; ili tupewe rehema na kupata neema ya kutusaidia wakati wa mahitaji”((Ebra. 4:16).

## 9.3 Kutoa Dhabihu Kwa Ajili Yetu Na Kwa Ajili YaNafsi Yake Mwenyewe

Kuhani mkuu wa wayahudi ilimpasa kutoa dhabihu ya kwanza kwa ajili ya dhambi zake mwenyewe, na halafu kwa ajili ya hao watu (Ebra 5:1-3). Dhabihu ya Kristo ilikuwa na muundo u huu mara dufu. Ingawa yeye mwenyewe hakuwa na dhambi yeyote, bado Yesu alikuwa na mwili wa kibinadamu, alihitaji wokovu toka mauti. Wokovu huu ulitolewa na Mungu, kwa sababu ya dhabihu yake mwenyewe Kristo; hivyo kwa pande mbili Yesu alikufa ili apate wokovu wake mwenyewe, na kuuwezesha wa kwetu vile vile. Maneno mengi yanataja hii.

Sehemu hii ni orodha ya aya zinazothibitisha kuwa dhabihu ya Kristo ilikuwa kwa faida yake mwenyewe sambamba na sisi. Ni mbali kuliko kuthibitisha maana hii; lakini ina maana kuwa jambo hili tunalolizungumzia ni la muhimu kufahamu ikiwa ubinadamu wa Bwana wetu uweze kueleweka vizuri. Kwa kumalizia kitabu hiki unaweza wakati mwingine utakaofuata ukataka kufikiri kuhusu mambo haya kwa undani, kwa hiyo mambo haya yamejumuishwa.

 Kuhani Mkuu “imempasa, kama kwa ajili ya watu, vivyo hivyo kwa ajili ya nafsi yake mwenyewe; kutoa dhabihu kwa ajili ya dhambi….. vivyo hivyo Kristo” alitimiza mfano wa kuhani mkuu wa kipindi cha Musa kwa kuangalia hili (Ebra. 5:3,5). Neno

la kiyunani “imempasa” kwa namna yake maalum maana yake kuwa na deni la fedha- likiwa linataja Bwana wetu ananunua ukombozi wake mwenyewe vile vile na wa kwetu. Ulikuwa ni “kwa sababu ya” ubinadamu wake (Ebra 5:3) ambao inambidi kufanya hivi. Hapa haina maana kwamba alikuwa na dhambi yake yoyote ambayo alihitaji kuilipia. Jambo hili haliwezi kukaziwa mno. Tulikombolewa kwa damu yake ya dhabihu -basi na yeye pia.

 Kristo “hana haja kila siku, mfano wa wale makuhani wakuu wengine, kwanza kutoa dhabihu kwa ajili ya dhambi zake mwenyewe, kisha kwa ajili ya dhambi za hao watu; maana yake alifanya hivi  mara moja, alipojitoa nafsi yake” (Ebra 7:27). Hakuna shaka ya kwamba Paulo anakazia hali ya kufanana ya matokeo ya kuhani kwa vitu viwili kati yake na Kristo. Anafanya hivyo tena katika Ebra 9:7 (mst 12,25). Tofauti ilikuwa kwa Kristo kufanya hivyo mara moja, bali kuhani mkuu kila mwaka. Ikiwa tofauti ilikuwa kwamba Kristo alitoa tu dhabihu kwa ajili ya watu, basi hii ingejitokeza. Fahamu kwamba dhabihu ya Kristo ilikuwa kwa ajili ya “dhambi” zake mwenyewe ambazo zilitofautiana na za watu - ‘dhambi’ zake hazikuwa zetu alizichukua. Kwa sababu kwa mfano alitoa dhabihu iliyojitenga kwa ajili yetu. Kwa kuwa Yesu alikuwa mkamilifu, tabia isiyo na dhambi, hapa ‘dhambi’ ni namna nyingine ya kuueleza mwili wa dhambi ya mwanadamu. Sababu (mwili ulio na dhambi) umesemwa kama ni tokeo. Lakini bado inahitajika kukazia ya kwamba Bwana wetu alikuwa mkamilifu, hawezi kuthibitishwa kuwa ana dhambi.

 Mungu “akamleta tena kutoka kwa wafu mchungaji Mkuu wa kondoo, kwa damu ya Agano la milele, yeye Bwana wetu Yesu” (Ebra 13:20), yaani damu yake mwenyewe. Basi, kwa pande mbili Bwana wetu alikuwa mchungaji, kwa kuwa alikwenda mwenyewe kwa mchinjaji, na kwa damu yake Mungu akamfufua; na kwa jinsi iyo hiyo kwa pande zote mbili alikuwa anatoa dhabihu na ni kuhani.

 Katika Biblia ya Kingereza A.V kwa Zekaria 9:9 unasema vizuri kwenye pambizo: “Mfalume wako (Yesu) anakuja kwako; ni mwenye haki, anajiokoa mwenyewe, (UV ‘naye ana wokovu’)” . Hizi tafsri mbili za kufaa zimedokeza kwamba kwa kujiokoa mwenyewe Bwana wetu ametuletea wakovu. Kwa dhabihu yake msalabani, yaani alilipia mwili wake mwenyewe ili kwamba afanikishe ukombozi wetu. Sio busara kufikiri mauti yake nje ya maneno yenyewe kwa kusudi lake la kutaka kutuokoa

 Inabidi ifahamike kuwa ushahidi wote wa kumwaga damu ya mnyama kuwa dhabihu chini ya torati kwa namna nyingine yahusu dhabihu yenyewe ya Kristo. Madhabahu, alama ya Kristo,ilifanyiwa upatanisho mara moja kila mwaka kwa damu (Kut 30:10), ikionyesha ni jinsi gani Kristo alijitakasa mwenyewe kwa kutoa dhabihu yake. Hakika ile hema nzima ya kukutania jangwani ilimwakilisha Kristo, ilibidi isafishwe kwa damu (Ebra 9:23). Vyombo vya mle ndani ya maskani havikutenda dhambi yeyote, ingawa vilitakiwa vitakaswe kwa sababu ya kushirikishwa na dhambi. Ndivyo na Bwana wetu.

Kuhani Mkuu mwenyewe ilimpasa kuanza utumishi wake kwa kunyunyuziwa damu, naye Kristo alihitaji dhabihu yake mwenyewe ili aanze utumishi wake kwa ajili yetu Mbinguni (Law 8:23).

Ya kwamba Yesu alijipatanisha mwenyewe haina maana kuwa alikuwa na dhambi zake mwenyewe. Kutoa dhabihu yake kwa dhambi siku zote haina maana kuwa mtoaji dhabihu amekosa (Yaani; Law 12 mwanamke ilimbidi afanye hivi baada ya kuzaa).

## 9.4 Yesu Ni Mwakilishi Wetu.

Tumeona kwamba dhabihu za wanyama hazikuwawakilisha kikamilifu watu wenye dhambi. Yesu alikuwa mjumbe wetu, kwa mambo yote "akafananishwa na ndugu zake" (Ebr 2:17). "Alionja mauti kwa ajili ya kila mtu" (Ebra 2:9). Tunapofanya kosa kama - tukiwa na hasira - Mungu aweza kutusamehe sisi "katika Kristo" (Efe 4:32). Hivi ni kwa sababu Mungu aweza kutulinganisha na Kristo mwanadamu aliyekuwa kama sisi alipojaribiwa kufanya dhambi - kama kukasirika - bali alishinda kila jaribu. Kwa hiyo Mungu aweza kutusamehe dhambi yetu- ya hasira kwa kule kuwa ndani ya Kristo, tukiwa tumefunikwa na haki yake. Kristo akiwa mwakilishi wetu, basi amekuwa na njia ambayo Mungu anaweza kutuonyesha neema yake, wakati tukithibitisha mambo ya haki yake mwenyewe.

Ikiwa Yesu alikuwa ni Mungu na siye mtu aliye na mwili wa Adamu tu, asingekuwa mwakilishi wetu. Huu ni mfano mwingine wa wazo moja potofu linalokwenda kwenye lingine. Kwa sababu hii, watu wa dini wameendeleza njia nyingi zilizo ngumu kufahamika kueleza mauti ya Kristo. Mtazamo wa madhehebu mengi ya Kikristo yaliyo kengeuka ni kwamba dhambi za mwanadamu zimemfanya awe na deni kwa Mungu ambalo yeye mwenyewe hakuweza kulipa. Ndipo Kristo akalipa deni la kila mwamini kwa damu yake, iliyomwagika msalabani. Wahubiri wengi wa kwenye baraza la Injili wameeleza namna hii; "Ilikuwa kana kwamba tulikuwa tumepangwa kwenye ukuta, karibu kupigwa risasi na ibilisi. Wakati huo Yesu akakimbilia ndani kwa haraka; badala yetu ibilisi akampiga, sisi tupo huru".

Maelezo ya mawazo haya hayana uthibitisho wowote imara wa Biblia. Yameachana wazi ikiwa kama Kristo alikufa badala yetu,

wakati huo tusife. Kama bado tuna mwili wa Adamu, bado yatupasa kufa; wokovu toka dhambi na mauti mwishoni utafunuliwa kwenye hukumu ( tutakapopewa kutoharibika). Huu hatukupokea wakati wa kufa Kristo. Mauti ya Kristo yalimharibu ibilisi (Ebr 2:14) na sio Ibilisi alimwangamiza yeye.

Biblia inafundisha ya kwamba wokovu umepatikana kwa njia ya mauti ya Kristo NA ufufuo, na sio kwa mauti yake. Kristo "alikufa kwa ajili yetu" mara moja. Wazo la kuwa badala ya mwingine lina maana ya kwamba yeye mwenyewe ilimpasa kufa kwa ajili ya kila mmoja wetu.

Ikiwa Kristo alilipa deni kwa damu yake, wokovu wetu unakuwa ni jambo lingine ambalo tunaweza tegemea kama ni haki. Ukweli ni kwamba wokovu ni zawadi (kipawa), kimeletwa kwa neema na msamaha wa Mungu, unapotea machoni ikiwa tunaelewa dhabihu ya Kristo kuwa ni malipo ya deni. Vile vile inadaiwa kwamba hasira ya Mungu ilitulizwa mara alipoiona damu yake Yesu. Lakini kile ambacho Mungu anaona tunapotubu ni mwanae kama ni mwakilishi wetu, ambaye tunajaribu kuiga mwenendo wake, sio tunajiunga na damu ya Kristo kama kitu cha kutupa bahati njema. Utenzi na nyimbo nyingi za 'Kikristo' zina kiasi cha kushangaza mafundisho potofu katika eneo hili. Mafunzo potofu zaidi yameingia mioyoni mwa watu kwa njia ya miziki, kuliko kwa busara, mafundisho ya Biblia. Siku zote yatupasa kujihadhari na aina hii ya msukumo wa kukataa mafundisho ya kweli kwa kupokea yaliyo ya upotoshaji.

Kwa huzuni sana, maneno rahisi "Kristo alikufa kwa ajili yetu" (Rum 5:8) yameelekwa vibaya sana kwa maana ya kuwa Kristo alikufa badala yetu. Kama idadi ya miunganiko kati ya Warumi 5 na 1 Wakorintho 15 (k.m mst 12=1Kor 15:21 mst 17=

Kor 15:22). “Kristo alikufa kwa ajili yetu” (Rum 5:8) umelingana na “Kristo alikufa kwa sababu ya dhambi zetu” (1Kor 15:3). Kifo chake kilikuwa kikifanya njia ya kutuwezesha tupate msamaha wa dhambi zetu, ilikuwa namna hii ya kusema ya kwamba “Kristo alikufa kwa ajili yetu”. Neno ‘kwa’ halina sharti la maana ya ‘badala ya’; Kristo alikufa “kwa ajili ya dhambi zetu”, sio badala yao. Kwa sababu hii, Kristo anaweza “kutuombea” tukimjia Mungu (Ebra 7:25), sio ‘badala yetu’. Wala “kwa” halina maana ya ‘badala ya’ katika Ebra 10:12 na Gal 1:4.

### 9.5 Yesu Na Torati Ya Musa

Yesu akiwa ni dhabihu timilifu kwa dhambi na Kuhani Mkuu asiye na kasoro yoyote ambaye kweli anaweza kutupati msamaha, utaratibu wa zamani wa kutoa dhabihu za wanyama na makuhani wakuu uliondolewa baada ya kifo chake (Ebra 10:5-14). “Maana ukuhani ule ukibadilika, (toka kwa walawi kwenda kwa Kristo), hapana budi sheria nayo ibadilike” (Ebra 7:12). Yeye hakufanywa Kuhani kwa sheria na maagizo ya kibinadamu (yaani kwa sababu ya mtu lazima atoke kwa kabla la Lawi ndipo awe kuhani), bali kwa nguvu ya uhai ambao hauna mwisho”, ambao alipewa kwa sababu  ya dhabihu yake timilifu (Ebra 7:16 B.H.N). basi ile amri ya zamani yaani torati ya Musa ilifutwa kwa sababu ilikuwa hafifu na isiyo kitu. Maana sheria ya Musa haikuweza kukamilisha jambo lolote. Lakini sasa mahali peke pamewekwa tumaini lilo bora zaidi (kwa njia ya Kristo) ambalo kwalo tunaweza kumkaribia Mungu. (Ebra 7”18.19 B.H.N).

Ni dhahiri kutokana na jambo hili ya kwamba sheria ya Musa ilifikia mwisho kwa dhabihu ya Kristo. Kuuamini ukuhani wa kibinadamu au kuendelea katoa dhabihu za wanyama maana yake hatukubali utimilifu wa ushindi wa Kristo. Kuwa na imani hizi ni kwamba sisi hatufahamu kuwa sadaka ya Kristo ni yenye ushindi uliokamilifu, na ya kuwa tunaona kufanya kazi hii ni ya lazima kutuletea kuhesabiwa haki, kuliko kumwamini Kristo pekee. “Ni dhahiri ya kwamba hakuna mtu ahesabiwaye haki mbele za Mungu katika sheria; kwa sababu mwenye (kuhesabiwa) haki ataishi kwa imani” (Gal 3:11 ml Hab 2:4).

Juhudi ya mapenzi yetu wenyewe kuwa imara kutii andiko la sheria ya Mungu haitatuletea kuhesabiwa haki; kwa kweli kila msomaji wa maneno haya tayari ameziasi sheria hizo.

Kama tunashika Torati ya Musa, yatupasa kujaribu kuyashika yote. Kutotii moja tu ya sehemu yake maana yake ni kwamba wote walio chini yake wamehukumiwa; “Kwa maana wale wote walio wa matendo ya sheria, wako chini ya laana; maana imeandikwa, Amelaaniwa kila mtu asiyedumu katika yote yalioandikwa katika kitabu cha torati;ayafanye” (Gal 3:10).

Kutokana na udhaifu wa mwili wetu wanadmu hatuwezi kutunza kwa ukamilifu torati ya Musa, lakini kwa kuwa Kristo alitii yote kabisa, tumeachwa huru toka sharti lolota la kuishika. Wokovu wetu ni kipawa cha Mungu kwa ajili ya Kristo, kuliko,matendo yote ya kutii. “Maana yake yasiowezekana kwa sheria, kwa vile ilivyokuwa dhaifu kwa sababu ya mwili, Mungu kwa kumtuma mwanae mwenyewe katika mfano wa mwili ulio na dhambi, na kwa sababu ya dhambi (Yaani, kutoa dhabihu ya dhambi. Kama unayo Biblia iitwayo Biblia Habari Njema aya hii inaeleweka vizuru zaidi), aliihukumu dhambi katika mwili” (Rum

8:3). Hivyo basi. Kristo alitukomboa katika laana ya torati, kwa kuwa alifanywa laana kwa ajili yetu" (Gal 3:13).

Kwa hiyo hatutakiwi tena kutunza sehemu yoyote ya torati ya Musa. Tuliona katika somo la 3.4 kuwa Agano Jipya kwa Kristo liliingia mahali pa Agano la Kale la torati ya Musa (Ebra 8:13). Kwa kufa kwake Kristo aliifuta ile hati iliyoandikwa ya kutushitaki kwa hukumu zake ( kwa kutoweza sisi kushika vizuri torati)….. akaiondoa isiwepo tena, akaipigilia misumari msalabani……. Basi, mtu asiwahukumu nyinyi katika chakula au vinywaji (kutoa dhabihu), au kwa sababu ya sikukuu ya mwandamo wa mwezi; au sabato mambo haya ni kivuli cha mambo yajayo; Ukweli wenyewe ndiye Kristo" (Kolos 2:14-17 U.V na B.H.N). Hapa ni wazi kabisa - kwa sababu ya Kristo kufa msalabani, Torati "aliiondoa" ili kwamba tusishindane na mkazo wowote uliowekwa yetu kwa kushika sehemu yake k.m sikukuu za sabato. Kama shera yote, lengo la mambo haya lilikuwa laonyesha mbele kuja kwa Kristo ile mara ya kwanza. Baada ya kufa kwake maana ya mifano yake ilitimia, hapakuwa na haja zaidi kuendelea kuifuata.

Kanisa la awali la Kristo kwenye karne ya kwanza daima lilikuwa chini ya mkazo uliotoka kwa wayahudi wenye msimamo mkali kufuata sehemu ya sheria. Katika Agano hilo lipo onyo lililorudiwa la kuzuia haya mashauri. Usoni pa yote haya, ni ajabu ya kwamba yapo madhehebu baadhi yanayoshauri kutii sheria. Awali tumeonyeshwa ya kwamba jaribio lolote la kupata wokovu kutokana na kutii torati inabidi shabaha iwe kutunza Torati yote, upande mwingine sisi wenyewe tunakuwa tumehukumiwa kwa kuiasi hiyo Torati (Gal 3:10)

Kuna jambo ndani ya mwili wa mwanadamu linaloelekea kwenye wazo la kuhesabiwa haki kwa matendo; tunapenda kuona

kwamba tunafanya jambo fulani la kuuelekea wokovu wetu. Kwa sababu hii, kutoa sehemu ya kumi (fungu la kumi) kwa lazima, kuvaa msalaba, kusemasema orodha ya sala, kusali kwa mkao fulani n.k. yote haya ni sehemu wafanyayo watu wengi wa dini, za Kikristo na wengineo.Wokovu kwa kumuamini Kristo peke yake ni mafundisho karibu ya kipekee kwa Ukiristo wa kweli msingi ukiwa ni Biblia.

Maonyo juu ya kushika sehemu iwayo yote ya Torati ya Musa ili kuupata wokovu, yametapakaa katika Agano Jipya. Wengine walifundisha ya kuwa wakristo watahiriwe kulingana na sheria za Musa, na “kuitunza Torati”. Yakobo alilaumu wazo hili kwa niaba ya waamini wa kweli: “sisi hatukuwaagiza” (Mdo 15:24). Petro aliwasema wale waliofundisha ni lazima kutii Torati ya kuwa ni kuweka “ kongwa juu ya shingo za wanafunzi ambalo baba zetu wala sisi hatukuweza kulichukua. Bali tunaamini kwamba tunaokoka kwa neema(ni kinyume na matendo yao ya kutii sheria) ya Bwana Yesu vile vile kama wao” (Mdo 15 10:11) Akivuviwa, Paulo akisema ilivyo sawa mambo yalivyo, anasisitiza jambo lilo hilo mara kwa mara: “ Mwanadamu hahesabiwi haki kwa matendo ya sheria bali kwa imani ya Kristo Yesu …. Ni dhahiri ya kwamba hakuna mtu ahesabiwaye haki mbele za Mungu katika sheria……. Na kwa yeye (Kristo) kila amwaminiye huhesabiwa haki katika mambo yale yote asiiyoweza kuhesabiwa haki toka kwa torati ya Musa” Gal 2:16; 3:11; Mdo 13:36).

Ni ishara ya hakika jinsi Ukristo wa wengi ulivyogeuka hata mengi ya mazoea yao yapo juu ya mambo ya Torati ya Musa - mbali ya mafunzo yaliyo wazi na kutendewa kazi yaliyopimwa hapo juu ya kuwa Wakristo wasiishike sheria, kwa kuwa katika Kristo imeondolewa. Sasa tutaona njia zilizowazi ambazo ndani yake Torati ya Musa ndio msingi wa mazoea ya ‘Ukristo’ uliopo.

**Makuhani**

Makanisa ya Katoliki na Anglikani yanatumia utaratibu ulio wazi mno wa ukuhani wa mwanadamu. Wakatoliki wa Roma wanamuona Papa wao kuwa yupo sawa na Kuhani wa Wayahudi. Yupo "Mpatanishi mmoja kati ya Mungu na wanadamu, Mwanadamu Kristo Yesu" (Tim 2:5) Basi. Haiwezekani kwamba Papa au makuhani wengine kuwa wapatanishi wetu kama Makuhani walivyokuwa chini ya Agano la Kale. Sasa Kristo ni Kuhani wetu pekee aliyekwenda mbiguni, akitoa maombi yetu kwa Mungu.

Haupo ushahidi kabisa wa Biblia wa kwamba mamlaka waliyokuwa nayo wazee waliopewa kipawa cha Roho karne ya kwanza - k.m Petro - waliwapa vizazi vilivyofuata au hasa kwa Papa. Hata kama uwezekano huu uliingizwa, hakuna njia iliyothibitisha kwamba Papa na Makuhani wenyewe ndio hao juu yao ambao vazi la kiroho la wazee wa kwanza liliwaungikia.

Vipawa vya Roho viliondolewa, Wote wanaoamini wana ruhusa iliyo sawa ya kutumia Roho- Neno lilo ndani ya Biblia (tazama masomo ya 2.2 na 2.4) Kwa sababu hii wote ni ndugu, hakuna awaye yote aliye na nafasi ya juu kiroho kuliko mwingine. Kweli, waaminio wote wa kweli ni washiriki wa ukuhani mpya kwa sababu ya wao kubatizwa katika Kristo, kwa maana ya kwamba wanaionyesha nje nuru ya Mungu katika ulimwengu wenye giza (1Petro 2:9). Kwa hiyo watakuwa wafalme - Makuhani wa Ufalme, utakapo wekwa duniani Kristo akirudi tena (ufunuo 5:10).

Mazoea ya Katholiki kuwaita makuhani wao 'Baba' (vile vile 'Papa' maana yake ni 'baba.) yanapingana kabisa na maneno

bayana ya Kristo" "Msimwite mtu baba duniani maana baba yenu ni mmoja. Aliye wa mbinguni"(Math 23:9). Kweli, Yesu alionya kumpa mtu - ndugu awaye yote heshima ya kiroho inayotakiwa na makuhani wa siku hizi: Ninyi msiitwe Rabi (mwalimu): maana mwalimu wenu ni mmoja, ndiye Kristo; nanyi nyote ni ndugu" (Math 23:8).

Mavazi yanayovaliwa na makuhani yenye mapambo sana, maaskofu na mapadri yana msingi wake katika vazi maalum lililovaliwa na makuhani katika kipindi cha Musa na Kuhani Mkuu. Uvaaji huu ulionyesha mbele kwenye tabia kamilifu ya Kristo, na kama pamoja na sheria yote, kusudi lake sasa limetimilika. Hakika ni ya Kuvunja Moyo, ya kuwa uvaaji ulilenga kuutukuza sana utukufu wa Kristo, na siku hizi uvaaji umesogeza utukufu wa wanadamu wanaovaa- wengine wanakiri ya kwamba hawakubali kuwa Kristo alifufuka hata uwepo wa Mungu.

Wazo la katholiki kwamba Mariamu ni kuhani ni kosa kubwa. Maombi yetu ni katika jina la KRISTO, sio Mariamu (Yon. 14:14,14; 15:16; 16:23-26). Kristo pekee ndiye kuhani wetu mkuu, sio Mariamu. Yesu aliwahi kumkemea Mariamu alipomjaribu awafanyie mambo wengine (Yn 2:2-4). Mungu sio Mariamu, huwaleta watu kwa Kristo (Yn 6:44).

**FUNGU LA KUMI**

Hii nayo ilikuwa sehemu ya Torati ya Musa(Hesabu 18:21), ambapo Wayahudi walitoa Fungu la kumi katika vitu vyao na kuwapa kabila ya Lawi ya ukuhani. Kwa kuwa sasa hakuna ukuhani wa kibinadamu, shurutisho haliwezi kuwapo tena la kutoa fungu la kumi kwa mzee awaye yote wa kanisa. Wazo potofu tena (katika suala hili la kuhusu makuhani) limewaongoza kwenye lingine (yaani, la kutoa fungu la kumi). Mungu mwenyewe hana

haja ya matoleo yetu ya sadaka, kwa kuwa vitu vyote ni vyake (Zab. 50:8-13). Tunamrudishia Mungu tu kile ambacho ametupatia sisi (1 Nyak 29:14). Hatuwezi kupata wokovu kama tokeo la kutoa vitu vyetu viwe sadaka, kama katika masharti ya fedha. Katika kushukuru zawadi kubwa ya Mungu aliyotupatia, hatutoi tu sehemu ya fungu la kumi bali tunato maisha yetu yote. Katika haya , Paulo ameweka mfano, kweli akitendea kazi kile alichokihubiri: "Iitoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu, ya kumpendeza Mungu, ndiyo ibada yenu yenye maana" (Rum 12:1).

**CHAKULA**

Sheri ya wayahudi iliweka sheria fulani ya vyakula kuwa ni najisi- tabia iliyochukuliwa na madhehebu mengine, hasa ya nguruwe. Kwa sababu ya Kristo kuiondoa sheria juu ya msalaba, "Basi mtu asiwahukumu nyinyi katika vyakula, au vinywaji" (Kolos 2:14-16). Hivyo maagizo ya Musa kuhusu mambo haya yameondolewa na Kristo, kwa kuwa sasa amekuja. Alikuwa ni yeye ambaye 'vyakula safi' vilitabiri kuja kwake.

Ni wazi alieleza ya kuwa hakuna kitu anachokula mtu halafu kikamtia unajisi kiroho; ni kile kimtokacho ndani ya moyo ndicho hufanya hivi (Marko 7:15-23). " Kwa kusema hivi, Yesu alieleza kuwa vyakula vyote ni 'safi'" (Marko 7:19). Petro alifundisha somo lile lile (Mdo 10:14,15), kama alivyofanya Paulo: "Najua tena nimehakikisha sana katika Bwana Yesu, ya kuwa hakuna kitu kilicho najisi kwa asili yake" (Rum 14:14). Awali Paulo alitoa hoja ya kwamba kukataa vyakula fulani ilikuwa ishara ya udhahifu wa kiroho (Rum 14:2). Msimamo wetu wa vyakula "hakituhudhulishi mbele ya Mungu" (1Kor 8:8). Kwa yote yanayotia hatia zaidi ni onyo ambalo Wakristo wenye kuacha imani watafundisha watu, "kujiepusha na vyakula, ambavyo Mungu aliviumba vipokelewe

kwa shukurani na walio na imani wenye kuijua hiyo kweli" (1 Tim 4:3).

## 9.6 Sabato

Moja ya mifululizo iliyoenea zaidi katika 'Ukristo' wa leo kwa matendo yao na Torati ya Musa yameonekana katika wazo la kwamba yatupasa kuishika sabato. Makundi mengine yanadai kwamba tuishike sabato ya Wayahudi hasa kama ilvyoainishwa katika sheria; wengi wengine wanaona kwamba Wakristo wawe na siku moja ya juma iwe siku ya kuabudu, ambayo mara nyingi wanaiainisha kama Jumapili. Kwa kudhihirisha jambo la kwanza ni kuwa Sabato ilikuwa siku ya mwisho ya juma, Mungu alipumzika baada ya siku sita za uumbaji (Kut 20:10,11). Jumapili ikiwa ni siku ya kwanza ya juma, haiwi sahihi kuitunza siku hii kuwa ni sabato. Kwa namna sahihi Sabato ilikuwa ni "ishara kati yangu mimi (Mungu) na Israel wapate kujua ya kwamba mimi, BWANA, ndimi niwatakasae"{Ezek 20:12). Kama hivi, kamwe haikusudiwi kuwafunga watu wa mataifa (wasio Wayahudi).

Tumeona ya kwamba kwa kufa kwake Yesu Kristo Msalabani, Torati ya Musa iliondolewa, kwa hiyo sasa haupo ulazima wa kuitunzu Sabato, au kweli, sikukuu yoyote kama siku ya kifo cha Kristo (Kolos 2:14-17). Wakristo wa kwanza waliorudia kuishika sehemu ya Torati ya Musa kama Sabato wamesemwa na Paulo ni kurudia "mafundisho manyonge, yenye upungufu ambayo mnataka tena kuyatumikia. Mnashika siku (kama Sabato), na miezi, nyakati na miaka (yaani sikuu za wayahudi). Nawachelea (nina wasiwasi), isiwe nimejitaabisha bure kwa ajili yenu" (Gal 4:9-11). Ni jambo la kufikiri kujaribu kuishika Sabato kuwa ni njia ya Wokovu. "Mtu afanya tofauti kati ya siku na siku (katika umuhimu wa kiroho)

mwingine aona siku zote kuwa ni sawa sawa. Kila mtu athibitike katika akili zake mwenyewe. Yeye aadhimishae siku, huiadhimisha kwa Bwana; naye alaye, hula kwa Bwana, kwa maana amshukuru Mungu"…. (Warumi 14:5,6).

Kwa sababu hii, inaeleweka ya kuwa hatusomi taarifa ya kwanza ya Waamini wa kwanza wakiitunza Sabato. Hakika imeandikwa kwamba wao walikutana "siku ya kwanza ya juma", yaani, Jumapili; "Hata siku ya kwanza ya juma, tulipokutana ili kumega mkate……" (Mdo 20:7). Kama haya yalikuwa ni mazoea yaliyoenea pote yameonyeshwa na Paulo akiwashauri Waamini wa Korintho wachukue michango "siku ya kwanza ya juma" (1Kor 16:2), yaani katika mikutano yao ya kawaida kwa siku hiyo. Wote wanaoamini wamesema kuwa ni Makuhani (1Petro 2:9)- waliosamehewa kuishika Sabato (Math 12:5).

Kama tunatunza Sabato, yatupasa kufanya hivyo kwa uzuri; awali tumeoneswa ni jambo la kufisha kushika Torati ya Musa nusu-nusu, kwa kuwa hii itasababisha tokeo la hukumu yetu(Gal 3:10; Yakobo 2:!0). Wokovu ni wakutunza sheria ya Kristo kuliko ya Musa. Israel hawakuruhusiwa kutenda kazi yeyote ya utumishi siku ya sabato: "Mtu awaye yote atakaye fanya kazi yoyote siku hiyo atauawa". Vilevile waliamriwa: " Hamtawasha moto katika nyumba zenu kwa siku ya Sabato", na kwa sababu hiyo walikatazwa kuadaa chakula siku hiyo (Kut 35:2,3: 16:23). Mtu aliyekusanya kuni kwenye sabato, labda ili kuwasha moto, adhabu yake ilikuwa kifo kwa kufanya hivyo (Hesabu 15:32-36).

Hayo madhehebu yanayofundisha kwamba kuitunza Sabato kunahitajika kwa washirika wao basi hao washirika wanapoivunja waadhibiwe kifo. Usiwepo upishi wa chakula au matumizi ya moto kwa namna yoyote- kama kuendesha magari, kutumia mfumo

wa kuchoma au kupasha joto n.k. Wayahudi wenye msimamo mkali wa siku hizi wameweka mfano wa aina ya mwenendo unaotakiwa na Sabato: wanabaki ndani ya Nyumba siku nzima isipokuwa kwa sababu ya dini, wao hawajihusishi na upishi, kusafiri n.k. Wengi wa 'Wakristo' hao wanaodai kuitunza Sabato wanashindwa mno kwenye jambo hili.

Imesisitizwa ya kwamba kuitunza Sabato ilikuwa moja ya amri kumi alizopewa Musa, na ya kuwa, Sheria iliyobaki ya Musa iliondolewa, ulazima umesalia wa kushika amri zote kumi. Seventh Day Adventists (S.D.A) wanatofautisha kati ya 'sheria ya uadilifu' ya amri kumi na iitwayo 'Sheria ya mambo ya ibada kulingana na mwili', ambayo wanaamini iliondolewa na Kristo. Huku kutofautisha hakujafundishwa na maandiko. Tangu awali tumeeleza kwa kuandika kwamba Agano la Kale linataja mambo ya Torati ya Musa, iliyobadilishwa msalabani na Agano Jipya. Inaonyesha kwamba amri kumi, ukijumlisha ile inayohusu Sabato, yote ilikuwa ni sehemu ya Agano la kale ambayo iliondolewa na Kristo:-

- Mungu "akawahubiri ninyi (Israel) agano lake, aliwamuru (Israel) kulitenda, yaani, zile amri kumi; akaziandika juu ya mbao mbili za mawe" (Km 4:13).
- Tena ilielekea ya kwamba agano hili, msingi wake ulikuwa juu ya amri kumi, lilifanywa kati ya Mungu na Israel, sio watu wa mataifa walikuwepo siku hiyo.
- Musa alikwea Mlima Horebu kupokea mbao za mawe ambazo Mungu aliandika juu yake Amri kumi. Kuhusu hii Musa alifafanua baadae."BWANA, Mungu wetu, alifanya agano nasi katika Horebu"(Km 5:2) yaani, kwa amri hizo kumi.
- Kwa wakati huu Mungu "aliandaka maneno ya agano juu ya mbao, amri kumi (Kut 34:28). Agano lili hili lilikuwa na hiyo inayoitwa ' sheria ya ibada kulingana na mwili' (Kut. 34:27). Kama

tukitia mkazo kushika ibada kama ilivyofanywa katika amri kumi ni lazima, yatupasa vile vile kufuata kila kipengele cha sheria nzima, kwa kuwa yote haya ni sehemu ya agano moja. Kwa kuweka wazi ni vigumu kufanya hivi.

- Ebra 9:4 yazungumzia ‘mbao za agano’. Amri kumi ziliandikwa juu ya mbao za mawe, ambazo zilikuwa za “agano la kale”.
- Paulo analitaja agano hili kuwa “liliandikwa na kuchorwa katika mawe”, yaani, juu ya mbao za mawe. Analiita “huduma ya mauti….. huduma ya adhabu…….. iliyobatilika (iliyoondolewa)” 2 Kor 3:7-11. Agano lilokuwa pamoja na amri kumi ni dhahiri haliwezi kutoa tumaini lolote la wokovu.
- Kristo aliifuta “ hati iliyoandikwa ya kutushitaki kwa hukumu zake, iliyokuwa na uadui kwetu” (Kol. 2:14) msalabani. Hii inatajwa hati ya Mungu ya amri kumi juu ya mbao za mawe. Vivyo hivyo Paulo anaisema ‘torati’….katika hali ya zamani, ya andiko” (Rum. 7:6) hali inayodhihirisha kutaja maandiko ya amri kumi yalioandikwa juu ya mbao za mawe.
- Ni moja tu ya amri kumi inayoitwa “amri” katika Rumi 7:8: “Amri…. ilisema, usitamani”. Aya zinazotangulia katika Rum 7:1-7 zinasisitiza jinsi “torati” ilivyobatilishwa kwa kufa Kristo; kwa hiyo ‘torati’ ina amri kumi.

Yote haya yanaweka wazi ya kwamba Agano la kale na ‘torati’ ndani yake ilikuwa na amri kumi. Kama zilivyobatilishwa na Agano Jipya, kwa sababu hiyo amri kumi ziliondolewa. Ingawa hivyo, tisa kati ya amri kumi zimethibitishwa tena, iwayo yote katika roho, kwenye Agano Jipya. Kitabu cha hesabu 3,5,6,7,8,na 9 zaweza kupatikana kwa 1Tim.1 peke yake, na Hesabu 1,2 na 10 kwa 1 Kor. 5. Bali amri ya nne inayohusu Sabato kurudiwa katika Agano Jipya haijawa lazima kwetu kushika.

Orodha ya maneno ya hati zifuatazo zinakuza jinsi gani nyingine tisa zimethibitishwa tena Agano Jipya:-

Ya 1-Efe 4:6; 1 Yoh 5:21; Math 4:10
Ya 2- 1Kor 10:!4; Rum 1:25
Ya 2 -1 Kor 10:14; Rum 1:25
Ya3- Yak 5:12; Math 5 :34,35
Ya 5-Efe 6:1,2; Kol 3:20
Ya 6- 1 Yoh 3:15; Math 5:21
Ya 7- Ebra 13:4; Math 5:27,28
Ya 8- Rum 2:21; Efe 4:28
Ya 9- Kol 3:9; Efe 4:25; 2 Tim 3:3
Ya 10- Efe 5:3; Kol 3:5

**Tumeacha kitambo sehemu ya 28: Sanamu ndogo ya Yesu Msalabani**

Kwa upana imeaminika kwa Wakristo ya kwamba Yesu Kristo aliuwawa msalabani. Walakini neno la Kiyunani 'stauros', ambalo kwa kawaida limetafsiriwa 'msalaba' katika Biblia, maana yake hasa ni mti ambao umesimikwa ardhini kama nguzo au mti wa kuchonga. Hakika, alama ya sanamu ya Yesu Kristo amepigiliwa msalabani imeelekea kuwa chanzo chake ni kwenye upagani. Inafaa ya kwamba Kristo na mikono yake na viganja viliinuliwa juu ya kichwa chake kuliko kwamba aliitandaza kwa mfano wa Yesu msalabani, kwa kuwa mikono iliyonyooshwa kuelekea juu ni ishara ya ahadi ya Mungu imethibitishwa (Ezek. 10:5,6,13; 36:7; 47:14), pamoja na sala (Omb 2:19;1 Tim 2:8; 2 Nyak 6 12,13; Zab 28:2), ambayo Kristo alijirikisha msalabani (Ebra 5:7). Alisema kama vile nyoka wa shaba alivyoinuliwa kwenye mti Israel

walipokuwa jagwani, basi atainuliwa wazi mbele za watu muda wake wa kufa; hivyo alijumuisha 'msalaba' na mti (Yohana 3:14).

Kanisa Katholiki limefungasha fumbo kubwa lenye ushawishi kuelekea msalabani. Wazo hili halina usaidizi kabisa na Biblia; limesababisha sanamu ya Yesu msalabani kuwa wazo la bahati njema, ishara ya kuonekana kwamba Mungu yu pamoja nasi. Watu wamefikiri ya kwamba kuvaa msalaba shingoni au kila mara kuonyesha alama ya msalaba, Mungu atakuwa pamoja nao. Hii ni ishara tupu; nguvu ya kweli ya msalaba ni kwetu sisi kuungana na mauti ya Kristo kwa kuamini na kubatizwa, kuliko kurudia mfano wa kuonekana na msalaba. Kwa kweli ni vyepesi kufanya la pili kuliko la kwanza.

**Tumeacha kitambo sehemu ya 29: Je? Yesu alizaliwa December 25?**

Kosa lingine kubwa la ukristo wa watu wengi ni kuhusu siku ya kuzaliwa Yesu. Wachungaji walikuwa wamelala kondeni na mifugo yao wakati wa kuzaliwa Kristo (Luka 2:8); hawakufanya hivi wakati wa Krismasi, majira ya kipupwe. Kristo aliishi miaka 331/2 na kisha alikufa kwenye sikukuu ya Paska, ambao ni wakati wa kufufuka. Basi inapasa kuwa alizaliwa miezi sita upande mwingine wa Pasaka, yaani karibu mwezi wa September/October.

Tarehe 25 Disemba ilikuwa ni sikukuu ya Kipagani huko Ulaya kabla ya Ukristo kuingia. Taarifa ya matendo ya Mitume inayo habari jinsi gani Wakristo wa kweli waliteswa vibaya mno na wapagani kwa sababu ya imani zao. Mara kwa mara mitume walionya kuwa kwa sababu hii, Wakristo wengine walitafuta imani

za kipagani, ili kuwezesha dini yao iwe ya kupendeza zaidi mbele ya wapagani waliowazunguka (k.m Mdo 20:30, 1 Yoh. 2:18; 2Thes 2:3; 2Pet 2:2-3). Kuichagua tarehe 25 Disemba kuwa sikukuu ya Kikristo huu ni mfano mkubwa. Miti ya Krisimasi n.k yote yaweza kufuatiliwa kurudi nyuma hadi kwenye kanuni za ibada ya kipagani zilizotendwa tarehe 25 Disemba.

Kwa sababu hii Wakristo wa kweli wasisherekee kuzaliwa kwa Kristo tarehe 25 Disemba. Kwa matendo, waamini wa kweli watatumia siku za mapumziko ya watu wote, k.m krisimasi, kuabudu pamoja popote iwezekanavyo.

**Somo La 9 : Maswali**

1. Ni kwa sababu gani kifo cha Yesu, kuliko cha mtu mwingine awaye yote, kilitakiwa kwa wokovu wetu?

2. Ni kwa sababu gani dhabihu za Wanyama kwenye Torati ya Musa hazikutosha kuondoa dhambi?

3. Je! Yesu alikuwa ni mwakilishi wetu au alipokufa alifanya hivyo badala yetu?

4. Ni ipi kati ya taarifa zifuatazo ni kweli?
   a) Kristo alikufa badala yetu
   b) Kristo alituwakilisha, hivyo Mungu anaweza kutusamehe kwa ajili yake
   c) Kristo alikuwa kama sisi lakini hatuwakilishi

d) Kristo kwa kufa kwake maana yake ni kwamba Mungu hatamhesabia mwanadamu awaye yote kwa ukosaji wa dhambi

5. Je! Yesu alifaidika kutokana na mauti yake mwenyewe?

6. Kristo alipokufa msalabani, je! ali….

a) Komesha amri ndogo za Torati ya Musa lakini sio amri kumi

b) Komesha Torati ya Musa pamoja na amri kumi

c) Komesha Torati ya Musa isipokuwa sikukuu za Wayahudi

d) Kuwa na tokeo kwenye nafasi ya Torati ya Musa?

7. Je! tushike Sabato sasa?

8. Toa sababu ya jibu lako kwa swali la 7.

## 10.1 Maana Muhimu Sana Ya Ubatizo

Mara kadhaa katika masomo yaliotangulia tumetaja maana muhimu sana ya ubatizo; ni hatua ya kwanza ya utii kwa ujumbe wa Injili. Ebra 6:2 unazungumzia ubatizo kuwa ni moja ya mafunzo ya msingi sana. Tumeacha tafakari yake hata hatua hii ya mwisho kwa sababu ubatizo wa kweli unaweza kutokea tu baada ya kufahamu kwa usahihi ukweli wa kina ambao ndani yake kuna Injili. Kwa haya sasa tumekamilisha somo letu; ikiwa unataka kweli kuungana na tumaini kubwa ambalo Biblia inatoa kwa Yesu Kristo, basi ubatizo ni wa muhimu kabisa.

"Wokovu watoka kwa Wayahudi" (Yohana 4:22) kwa maana ya kwamba ahadi zote kuhusu wokovu zilifanywa kwa Abrahamu pekee na uzao wake. Tunaweza kuwa na ahadi hizo tu zilizofanywa kwetu kama tukiwa ndani ya mzao, kwa kubatizwa katika Kristo (Gal. 3:22-29).

Basi ni wazi Yesu aliwaagiza wafuasi wake: "Enendeni ulimwenguni pote, mkahubiri Injili (ambayo ndani yake kuna ahadi za Abrahamu - Gal 3:8) wa kila kiumbe. Aaminiye na kubatizwa ataokoka" (Marko 16:16). Wazo juu ya neno hili "na" linadhihirisha kuamini Injili kwa weza kutuokoa; Ubatizo sio tu ni ziada ya hiari kwa maisha ya Mkristo, ni sharti la muhimu sana kwa wokovu. Hivi sio kusema kwamba tendo la ubatizo pekee litatuokoa; linabidi lifuatwe kwa maisha yote ya kuendelea kutii neno la Mungu. Yesu alikazia hili: "Amini amini, nakuambia, Mtu asipozaliwa kwa maji na kwa roho, hawezi kuingia Ufalme wa Mungu" (Yn. 3:5).

Huku kuzaliwa “kwa (Kiyunani ‘kutoka’) maji” anatajwa mtu anatoka ndani ya maji ya ubatizo kuja nje; baada ya kufanya hivi, yampasa azaliwe tena kwa roho. Hili ni jambo linaloendele katika maisha: “kuzaliwa mara ya pili….kwa Neno la Mungu” (1 Petr 1:23) Hivi ni kwa kuitikia kwetu kunako endelea mtu anaposikia na kutii Roho neno ndipo tunazaliwa kwa roho (ona somo la 22 ).

Tuna “batizwa katika Kristo” (Gal 3:27), katika jina lake (Mdo 19:5; 8:16; Math 28:19). Elewa ya kwamba unabatizwa katika Kristo- sio katika Wakristadelfiani au jumuia iwayo yote ya kibinadamu. Bila kubatizwa hatuwi “katika Kristo”, na kwa sababu hii hatuwi tumefunikwa na kazi yake inayookoa (Mdo 4:12). Petro anatoa mfano wa nguvu kuzunguka ukweli huu, anailinganisha na Safina wakati wa Nuhu na Kristo, ikiwa Safina iliwaokoa Nuhu na jamaa yake toka hukumu iliyowajia watenda dhambi, basi kubatizwa katika Kristo kutawaokoa waaminio toka mauti ya milele (1 Petr 3:21). Jinsi Nuhu alivyoingia katika Safina tendo hilo limelinganishwa na namna nasi tunavyoingia katika Kristo kwa kubatizwa. Wale wote waliokuwa nje ya Safina waliangamizwa na gharika; kusimama karibu na Safina au kuwa rafiki wa karibu wa Nuhu hakukusaidia kabisa. Njia ya pekee ni kuwa ndani ya Kristo/ Safina. Ni bayana ya kuwa kuja mara ya pili, ambayo gharika ile ilikuwa ni mfanowe (Lk 17:26,27), kumekaribia sana (tazama Habari iliyo mwisho wa kitabu sehemu ya 3).Kuingia katika Kristo/Safina kwa njia ya kubatizwa basi ni muhimu zaidi. Maneno ya kibinadamu kweli yameshidwa kuleta maana ya umuhimu huu; huu mfano wa Biblia wa kuingia katika safina wakati wa Nuhu ni wenye nguvu zaidi.

Wakristo wa kwanza walitii agizo la Kristo kwenda ulimwenguni pote kuhubiri Injili na kubatiza; kitabu cha Matendo kinazo taarifa hizi. Ushahidi mkubwa wa muhimu kubatizwa

unapatikana kwa namna ambayo taarifa inavyokazia jinsi gani watu mara wakabatizwa baada ya kupokea Injili (k.m. Mdo 8:12, 36-39; 9:18; 10:47; 16:15). Mkazo huu unafahamika mara moja ukikubalika kwamba bila ubatizo kujifunza kwetu Injili ni bure; Ubatizo ni hatua muhimu sana kutembea katika barabara ya kupata wokovu. Kwa masuala mengine taarifa iliyovuviwa inaonekana kujitokeza jinsi gani, mbali ya sababu nyingine wanadamu kuchelewesha ubatizo, na shida nyingi katika kulifanya tendo hili, ni muhimu sana watu wafanye kila jitihada kuyashinda yote haya, kwa msaada wa Mungu.

Mlinzi wa jela pale Filipi alitumbukia katika wakati muhimu sana wa maisha yake kwa tetemeko kubwa la ardhi lililobomoa gereza lake la ulinzi wa hali ya juu. Wafungwa walikuwa na nafasi kubwa ya kutoroka- jambo ambalo lingemgarimu maisha yake. Wakati ule imani yake kwa Injili ikawa kweli, kwa kadiri hiyo hata "Saa ile ile ya usiku….. akabatizwa….. wakati uo huo" (Mdo 16:33). Ikiwa awaye yote alikuwa na udhuru wa kuchelewesha ubatizo alikuwa ni yeye. Hivyo aliyashinda matatizo ya karibu sana ya tetemeko lilomzunguka kusongwa na ajira yake ya kila siku na mkazo wa maumivu ya mshituko alijikuta ndani mwenyewe - akabatizwa- . Wengi wenye wasi wasi atakaye ubatizo anaweza kuchukua uvuvia wa kweli toka kwa mtu huyo. Kama aliweza kufanya tendo hili la imani ni ushahidi wa kutosha kwamba tayari alikuwa na maarifa ya Injili iliyoelezwa, kwa kuwa imani hii ya kweli huja tu toka kusikia neno la Mungu (Rum 10:17; Matendo 17:11).

Matendo 8:26-40 inatoa taarifa ni jinsi gani Afisa wa Kushi alikuwa akisoma Biblia yake huku akisafiri na gari katika jangwa. Akakutana na Filipo ambaye kwa upana alimweleza Injili, pamoja na matakwa ya ubatizo. Kunena kibinadamu hapana budi

ilionekana kutowezekana kutii agizo la kubatizwa katika jangwa hilo lisilo na maji. Lakini Mungu asingetoa agizo ambalo anajua watu wengine hawawezi kutii. “Walipokuwa wakiendelea mbele njiani, wakafika mahali penye maji”, yaani chemi chem ya penye miti jangwani, mahali ambapo ubatizo uliwezekana (Mdo 8:36). Tukio hili linatoa jibu kwenye mapendekezo yasiyo na msingi ya kuwa ubatizo wa kuzamishwa kabisa ndani ya maji mengi ulifanyika tu katika maeneo yenye kufikiwa kwa urahisi mahali pa maji mengi. Siku zote Mungu atatoa njia iliyo ya kweli ya kutii maagizo yake.

Mtume Paulo alipata maono ya namna ya pekee toka kwa Kristo yalioichoma dhamiri yake hata mara hiyo ilipowezekana …“akasimama, akabatizwa” (Mdo 9:18). Lingekuwa ni jaribu tena kwake yeye kuchelewesha ubatizo wake, akifikiria umaarufu wake katika jamii na namna ya maisha ya kupata riziki yaliyotengezwa katika dini ya Kiyahudi. Lakini kuchomoza nyota ya ulimwengu wa Wayahudi alifanya uamuzi sahihi na wa mara moja kubatizwa na kutupilia mbali mtindo wa maisha yake ya awali. Baadae alitafakari uchaguzi wake kubatizwa; “Lakini mambo yote yaliyokuwa faida kwangu, naliyahesabu kuwa ni hasara kwa ajili ya uzuri usio kuwa na kiasi wa kumjua Kristo….. nimepata hasara ya mambo yote (yaani, mambo yaliyokuwa mara ya kwanza ni ‘faida’ kwake), nikiyahesabu huwa kama mavi ili nimpate Kristo…. Nikiyasahau yaliyo nyuma (‘Mambo” ya maisha yake ya kwanza katika maisha ya Kiyahudi), nikiyachuchumilia yaliyo mbele, niifikilie mede ya thahabu ya mwito mkuu”( Flp 3:7,8,13,14).

Huu ni msemo wa mpiga mbio akijinyoosha kwa mbele kukata utepe. Huku kuongeza nguvu za akili na juhudi ya mwili iwe tabia yetu baada ya ubatizo. Inabidi ieleweke ya kwamba ubatizo ni mwanzo wa shindano la mbio kuelekea ufalme wa Mungu; sio kwa ishara tu ya kubadili makanisa na imani, wala kuwa ni kushindishwa kwa furaha katika maisha ya kustarehe ya ufuasi wa kwenda kirahisi kwenye yale machache yasiyoeleweka mambo yaliyosemwa na Ukristo. Ubatizo unatuunga pamoja katika maana inayoendelea kwa kusulubiwa na ufufuo wa Yesu (Rum 6:3-5) mambo yote ya mwisho yenye nguvu kwa kila njia.

Akiwa amechoka mzee mwenye furaha kiroho kwa sababu ya kushinda Paulo aliweza kukumbuka: "Sikuyaasi yale maono ya Mbinguni" (Mdo 26:19). Kama ilivyokuwa kweli kwa Paulo hivyo ndivyo kwa wote waliobatizwa kwa usahihi.Ubatizo ni uamuzi mtu hata jutia. Maisha yetu yote yatafahamu ya kwamba tulifanya uchaguzi ulio sahihi. Maamuzi machache ya mwanadamu tumewahi kuwa na hakika mno. Swali linapasa lijibiwe bila kucheka: 'Ni kwa sababu gani nisibatizwe?'

### 10.2 Tubatizwe Jinsi Gani?

Kuna mtazamo umeshikiliwa wa kwamba ubatizo unaweza kufanywa, hata kwa watoto wadogo, kwa kuwanyunyuzia maji kwenye vipaji vya nyuso zao (yaani, kuwabatiza). Huu ni tofauti kabisa na ubatizo unaotakiwa na Biblia.

Neno la Kiyunani 'baptizo, ambalo limetafsiriwa 'batiza' katika Biblia za kiswahili halina maana ya kunyunyuzia; lina

maana kamili kuosha na kutumbukiza ndani ya maji (tazama kwenye mfuatano wa maneno -concordances- ulioandikwa na Robert young na James Strong). Neno hili limetumika katika daraja bora la waandishi wa Kiyunani kuhusu meli ikizama ni kuwa 'imebatizwa' (Yaani, imetota) katika maji. Vile vile limetumika katika kutaja kipande cha nguo kutiwa rangi kwa kuchovya katika maji yenye rangi na kuwa rangi nyingine. Kubadili rangi ya nguo, ni bayana ya kwamba imetumbukizwa kabisa ndani ya maji, kuliko kuwa kugeuka rangi iliyo nyunyuziwa juu yake. Ikiwa kuzamisha kweli ni namna sahihi ya ubatizo inakubalika kwa aya zifuatazo.

- "Yohana naye alikuwa akibatiza huko Ainoni, karibu na Salimu, kwa sababu huko kulikuwa na maji tele; na watu wakamwendea wakabatizwa" (Yohana 3:23). Hapa inaonyesha ya kwamba "maji tele" yalikuwa kwa ajili ya ubatizo; kama ulifanyika kwa kunyunyuziwa matone kadhaa ya maji, wakati ule, ndoo moja tu ya maji ingalitosha katika mamia ya watu. Watu walikuja mahali penyewe kwenye kingo za mto Yordani kwa ajili ya kubatizwa, sio Yohana aliwazungukia akiwa na chupa ya maji.

- Yesu naye, alibatizwa na Yohana katika mto Yordani: "Naye Yesu alipokwisha kubatizwa mara akapanda kutoka majini" (Math 3:13-16). Ubatizo wa Yesu ni dhahiri ulikuwa wa kuzamishwa ndani ya maji mengi- "aliinuka… toka majini" baada ya kubatizwa. Moja kati ya sababu za Yesu kubatizwa ilikuwa ni kuweka mfano, hivyo kwamba hakuna mtu ataweza kudai bila mzaha ya kwamba anamfuata Yesu pasipo kuiga mfano wake wa kubatizwa katika maji mengi.

- - Kwa desturi ya mfano mmoja, Filipo na afisa wa Ethiopia "waliteremka wote wawili majini…… naye akambatiza. Kisha walipopanda kutoka majini…" (Mdo 8:38,39). Kumbuka kwamba,

afisa aliomba ubatizo alipoona maji: “Tazama maji haya, ni nini kinachonizuia nisibatizwe?” (Mdo 8:36). Ni hakika ya kwamba huyo mtu asingefanya safari jangwani bila kuwa na kiasi cha maji ya kunywa kama katika chupa. Ikiwa ubatizo ilikuwa ni kwa kunyunyuziwa, basi ungeweza kufanyika pasipokuwa na haja ya maji ya chemi chem ya jangwani.

• Ubatizo ni kuzikwa (Kolos 2:12), ambao unadokeza kufunikwa kabisa.

• Ubatizo umeitwa ni ‘kuosha’ dhambi (Mdo 22:16). Maana ya kweli ya kuongoka imelinganishwa na ‘kuoshwa’ katika Uf 1:5; Tito 3:5; 2Petro 2:22; Ebra 10:22n.k. Huu msemo wa kuoshwa ni wa maana mno kwa ubatizo wa kuzamishwa kuliko kunyunyuziwa.

Kama vielekezo kadhaa kwenye Agano la kale ambavyo vinakubali kumkaribia Mungu ilikuwa kwa namna nyingine ya kuoshwa au kuoga.

Makuhani iliwapasa kuoga kabisa ndani ya bafu liloitwa ‘birika’ kabla ya kumkaribia Mungu kumtumikia (Law 8:6; Kut 40:32). Israel iliwabidi kuoga wenyewe ili wawe safi kutokana na unajisi fulani (K.m  Kumb 23:11), ambao ulikuwa ni mfano wa dhambi.

Mtu alieitwa Naamani alikuwa mtu wa mataifa mwenye ukoma aliyetafuta kuponywa na Mungu wa Israel. Kama hivi alikuwa anaonyesha mwanadamu aliyetaabika na dhambi, kwa maana anatembea katika mauti hai kwa sababu ya dhambi. Tiba yake ilikuwa kujichovya ndani ya mto Yordani. Kwa kuanza tendo hili jepesi ilikuwa vigumu kwake kukubali, akidhani ya kwamba Mungu angemtaka afanye jambo fulani kwa ghafla, au kujichovya

katika mto mkubwa unaojulikana, k.m Abana. Kwa namna mmoja, tunaweza kuona wokovu wetu. Yanapendeza sana kudhania kwamba matendo yetu wenyewe kwa kujiunga na kanisa kubwa, linalojulikana vyema na watu wengi (kama mto Abana) kuweza kutuokoa, kuliko tendo hili rahisi la kujiunga na tumaini la kweli la Israel. Baada ya kujichovya katika mto Yordani mwili wa Naamani "ukarudi ukawa kama wa mtoto mchanga, akawa safi" (2Fal. 5:9-14)

Sasa hakuna shaka ya kwamba 'ubatizo' unahusisha kabisa kujichovya ndani ya maji baada ya kuelewa kwanza ujumbe wa msingi wa Injili. Ufafanuzi huu wa Biblia kuhusu ubatizo hautoi ushahidi wowote wa cheo cha mtu ambaye hasa anafanya ubatizo. Ubatizo ukiwa wa kuzamishwa ndani ya maji baada ya kuamini Injili; kwa nadharia mtu anaweza kujibatiza mwenyewe. Lakini, kwa kuwa kubatizwa ni ubatizo tu kwa sababu ya mafunzo sahihi ambayo mtu ameshika wakati wa kuzamishwa, kwa kuweka wazi inafaa kubatizwa na mtu mwingine aaminiye mafundisho ya kweli, ambaye awali ya yote anampima kiwango cha elimu ya mtu aliyonayo kabla ya kuzamishwa ndani ya maji hasa.

Basi pamekuwepo mafundisho tokea zamani miongoni mwa wa -Kristadelfiani ya kufanya mjadala wa kina na mtaka ubatizo yeyote kabla ya kuzamishwa majini. Orodha ya maswali kama hayo yanayopatika mwishoni mwa kila somo katika kitabu hiki yaweza kuwa msingi wa mjadala huu. Wa- kristadelfiani wamesafiri maili maelfu ili kumsaidia mtu mmoja tu kuja kwenye tumaini la kweli la uzima wa milele, ni kwamba kwa kuanza hatuhusiki na uwingi wa wanaoongoka. Ni ubora, wala sio idadi ndiyo lengo letu la kumwendea.

## 10.3 Maana Ya Ubatizo.

Moja ya sababu za ubatizo wa maji mengi ni kwamba kuzama ndani ya maji kunaashiria kuzikwa kwetu kaburini- tunajiunga na mauti ya Kristo, na kuonyesha 'kufa' kwetu kwenye maisha ya kwanza ya dhambi na ujinga. Kuinuka toka ndani ya maji kunatuunga na ufufuo wa Kristo, tunasimuliwa tumaini la ufufuo wa uzima wa milele akirudi, na sasa hivi kuishi maisha mapya, ushindi kiroho juu ya dhambi kwa sababu ya ushindi wa Kristo aliofaulu kwa kufa na kufufuliwa.

"Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake. Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende (yaani, tuishi kila siku) katika upya wa uzima. Kwa maana kama mlivyounganika naye katika mfano wa mauti yake (kwa Ubatizo), kadhalika mtaunganika kwa njia ya kufufuka kwake" (Rum 6:3-5)

Kwa kuwa wokovu umewezeshwa tu kwa kifo cha Kristo na ufufuo, ni muhimu kwamba tujiunge wenyewe na mambo haya ili tuokolewe. Mfano wa kufa na kufufuka na Kristo, ambao ubatizo unatupatia, ndio njia pekee ya kufanya hivi. Ieleweke ya kuwa kunyunyuzia maji hakutimizi ishara hii. Kwenye ubatizo, "utu wetu wa kale (mtindo wa maisha) umesulubiwa" pamoja na Kriso msalabani (Rum 6:6); Mungu "ametuhuisha pamoja na Kristo" wakati wa kubatizwa (Efe. 2:5). Ingawa hivyo bado tunao mwili wa kibinadamu baada ya ubatizo, na kwa sababu hiyo mtindo wa maisha ya mwilini utaendelea kujiinua. Basi 'kusulubisha' mwili

wetu ni jambo linaloendelea ambalo lilianza pia kwenye ubatizo, ndivyo alimweleza aaminiye aubebe msalaba wake kila siku na amfuate, kama ilivyokuwa katika maandamano ya kuelekea Kalvari (Lk 9:23; 14:27). Wakati maisha ya kweli ya kusulubiwa na Kristo sio rahisi, kuna faraja na furaha isiyosemeka kwa kuungana pamoja na ufufuo wa Kristo.

Kristo ameleta “amani kwa damu ya msalaba wake” (Kolos 1:20); “amani ya Mungu ipitayo akili zote” (Flp 4:7). Kuhusu hii Yesu aliahidi, “Amani nawaachieni; amani yangu nawapa: niwapavyo mimi sio kama ulimwengu utoavyo (amani)” (Yn. 14:27). Hii amani na furaha kweli ni zaidi ya kusawazisha toka uchungu na shida zilizo wazi kwa kuungana wenyewe na Kristo msulubiwa: “Kwa kuwa kama vile mateso ya Kristo yanavyozidi kwetu vivyo hivyo faraja inazidi kwa njia ya Kristo” (2 Kor 1:5). Tena upo uhuru unaokuja katika kujua ya kwamba nafsi yetu ya asili kwa kweli imekufa, kwa hiyo Yesu anaishi nasi kabisa kwa kila jaribu letu. Mtume mkuu Paulo alizungumzia mengi yote haya yaliyompata kwenye maisha yake: “Nimesulubiwa pamoja na Kristo; lakini ni hai; wala si mimi tena, bali Kristo yu hai ndani yangu; na uhai nilionao sasa katika mwili, ninao katika imani ya mwana wa Mungu, ambaye alinipenda (Gal. 2:20).

“….. ni ubatizo, unaowaokoa ninyi pia siku hizi …… kwa kufufuka kwake Yesu Kristo” (1Petro 3:21) kwa sababu ya kuunganika kwetu na Kristo ufufuo wake kwa uzima wa milele unatupa njia ile ile akirudi. Ni kwa kushiriki ufufuo huu, wakati huo hatimaye tutaokolewa. Yesu alisema kuhusu jambo hili kwa maneno rahisi sana: “Na kwa sababu mimi ni hai, ninyi nanyi mtakuwa hai” (Yohana 14:19). Vivyo hivyo Paulo: “Tulipatanishwa na Mungu kwa mauti ya mwana wake,….. tutaokolewa katika uzima wake” (Ufufuo; Rum. 5:10).

Mara kwa mara imesisitizwa ya kwamba kujiunga wenyewe na mauti ya Kristo na mateso kwa kubatizwa, na mtindo wetu wa maisha ya baadaye, hakika tutashiriki ufufuo wake wenye utukufu:-

• "Kama tukifa pamoja naye (Kristo) tutaishi pamoja naye: kama tukistahimili, tutamiliki pamoja"(2Tim 2:11,12).

• "Siku zote twachukua katika mwili kunawa kwake Yesu, ili uzima wa Yesu nao udhihirishwe katika miili yetu…. Tukijua ya kwamba yeye aliyemfufua Bwana Yesu atatufufua sisi nasi pamoja na Yesu" (2Kor 4:10,11,14).

• Paulo alishiriki "mateso yake (Kristo) ni kifananishwa (maisha magumu yaliyompata) na kufa kwake; ili nipate kwa njia yoyote kufikia kiama ya wafu kwa uzima wa milele kama Kristo alivyopata" (Flp 3:10,11 linganisha na Gal 6:14).

### 10.4 Ubatizo Na Wokovu

Ubatizo unatuunganisha na mauti ya Kristo maana yake ni kwamba ni kwa kubatizwa tu ndipo tunaweza kupata msamaha. "Tumezikwa na Kristo kwa kubatizwa, na katika huo mkafufuliwa pamoja naye kwa….. na ninyi mlikuwa mmekufa kwa sababu ya makosa yenu…… aliwafanya hai pamoja naye, akiisha kutusamehe makosa yote" (Kolos. 2:12,13). "tumeoshwa…… katika jina la Bwana Yesu Kristo" (1 Kor 6:11) -yaani kubatizwa katika jini la Yesu ndiyo njia ambayo dhambi zetu huoshwa.

Huu mfano ulionyeshwa nyuma katika Hesabu 19:13, mahali ambapo wale waliokuwa nje ya maji ya utakaso ilibidi wafe. Tumeonyesha kwa kuandika katika Somo la 10.2 jinsi ubatizo ni kuziosha dhambi (linganisha Mdo. 12:16). Maelezo ya waaminio ya kuwa wameoshwa dhambi zao katika katika damu ya Kristo basi yanashuhudia kutenda kwo kwa njia ya kubatizwa (Uf 1:5; 7:14; Tito 3:5) kusema hivi ni kama "kuoshwa kwa kuzaliwa tena", tunahitajiwa

"kuzaliwa kwa maji" wakati wa kubatizwa(Yohana 3:5).

Kwa mwangaza wa yote haya, inafahamika ya kwamba jibu la Petro kwa swali, "Tutendaje?" (ili tuokoke) lilikuwa, "Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu" (Matendo 2:37,38). Kubatizwa katika jina la Kristo ni kwa ajili ya kusamehewa dhambi,; bila kufanya hiyo hapawezi kuwepo msamaha wa dhambi, na asiyebatizwa basi itambidi apate mshahara wa dhambi -mauti (Rum 6:23). Hakuna wokovu isipokuwa ni kwa jina la Yesu(Mdo 4:12), tunaweza kushiriki tu jina hilo kwa kubatizwa ndani yake. Huu ni uhakika ya kwamba dini zisizokuwa za Wakristo haziwezi kutuongoza kupata wokovu. Hakuna mwamini wa kweli wa Biblia anayeweza kukubali zinatoa njia ya wokovu; ni uhakika wa kwamba Ukatoliki na upana wa muungano wa Wakristo kwa mashauri ya watu matendo yao nao kufanya hivyo, ni wazo la kusikitisha juu ya msimamo wao kwenye Maandiko Matakatifu.

Ufufuo wa Kristo kwa uzima wa milele ulikuwa ni ishara ya ushindi wake juu ya dhambi. Sisi nasi kwa kubatizwa tunajiunga na huu, na kwa sababu hii tumesemwa kuwa tumefufuliwa pamoja na Kristo, dhambi haina nguvu tena juu yetu, kama ilivyokuwa haina nguvu juu yake. Kwa kubatizwa basi "tunawekwa huru mbali na dhambi….maana dhambi haitawatawala ninyi" baada ya ubatizo

(Rum 6:18,14). Walakini, baada ya ubatizo bado tunakosa (1Yoh 1:8,9); dhambi bado ipo katika nafasi ya kututumikisha tena kama tukigeukia mbali na Kristo. Kwa hiyo tukishiriki katika mauti ya Kristo na mateso, ingawa ubatizo unatuonyesha jinsi gani nasi pia tumejiunga na ufufuo wa Kristo, tunalo tumaini kushiriki akirudi.

Tena kwa mtazamo tunakuwa mbali na dhambi. "Aaminiye na kubatizwa ataokoka" (Marko 16:16) Kristo ajapo mara ya pili. Wokovu wa mwisho hautokei mara baada ya kubatizwa, bali mbele ya kiti cha hukumu (1Kor 3:15). Kwa kweli hakuna haja ya mafundisho kuhusu hukumu ikiwa tunapata wokovu wakati wa kubatizwa wala itatupasa kufa. "Mwenye kuvumilia hata mwisho, ndiye atakaye okoka" (Math 10:22).

Hata baada ya ubatizo wake, Paulo (na Wakristo wote) iliwapasa kujitahidi kuelekea kwenye wokovu (Flp 3:10-13; 1Kor 9:27); alilitaja tumaini la uzima wa milele (Tito 1:2; 3:7; 1Thes 5:8; Rum 8:24) nasi kuwa "warithi wa wokovu" (Ebra 1:14). Mbele ya kiti cha hukumu, wenye haki wataingia katika uzima wa milele (Math 25:46). Wazo lililovuviwa ajabu na Paulo linang'aa katika Warumi 13:11 - alihoji ya kwamba baada ya ubatizo tunaweza kujua ya kuwa kila siku tunayoishi na kustahimili ni siku moja iliyokaribu kwa ujio wa mara ya pili Kristo, hivyo basi tunaweza kufurahi yakuwa "Sasa wokovu wetu umekaribia kuliko tulipoanza kuamini". Kwa hiyo sasa hatunao wokovu wetu. Wokovu ni kwa sharti: tutaokoka kama tukishika sana imani ya kweli (Ebra 3:12-14), kama tukikumbuka mafunzo ya msingi yanayofanya Injili (1 Tim4:16; 1Kor 15:1,2), na kama tukifanya mambo yale yaliyo ndani ya tumaini hili kuu (2 Petro 1:10)

Kiarifa cha Kiyunani kilichotafsiriwa "okolewa" basi wakati mwingine kimetumika kwa wakati unaoendelea, kuonyesha ya

kwamba wokovu ni jambo linaloendelea linalotokea ndani yetu kwa sababu ya utii wetu ulioendelezwa kwenye Injili. Hivyo waaminio wamesemwa kuwa “wameokolewa” kwa kuitikia injili (Kor 1:18;.mifano mingine jambo hili tunaloandika lenye kuendelea inapatikana katika Matendo 2:47 na 2Kor 2:15). Neno hili la Kiyunani “Okolewa” limetumika tu kwa wakati uliopita kuhusu wokovu mkuu aliouwezesha msalabani, tunaoweza nasi kujiunga na kubatizwa (2 Tim 1:9; Tito 3:5).

Yote haya yameonyeshwa kwa mifano Mungu akishughulika na Israel wa mwili yanayofanya msingi wa uhusiano wake na Israel wa roho, yaani, waaminio. Israel waliondoka Misri, mfano wa ulimwengu na dini za uongo tulikokuwa awali kabla ya kubatizwa. Walipita bahari ya shamu na kisha walisafiri katika jangwa la Sinai kuelekea nchi ya ahadi, mahali ambapo walisimikwa kabisa kuwa Ufalme wa Mungu. Kuvuka kwao bahari ya shamu ni mfano wa kubatizwa kwetu (1Kor 10:1,2); Safari ya Jangwani ni maisha yetu yaliyopo, na Kanaani ni kuingia Ufalme wa Mungu. Yuda mstari wa 5 unaelezea ni wangapi kati yao waliangamia wakati wa kusafiri jangwani: “Bwana, akiisha kuwaokoa watu katika nchi ya Misri, aliwaangamiza baadaye wale wasioamini” Basi Israel “aliokolewa” toka Misri, kama hao wote ambao wanaobatizwa leo“wameokolewa” katika dhambi. Ikiwa mmoja wa hao Israel aliulizwa, Je! Umeokolewa?’ jibu lao lingalikuwa ‘ndiyo’, lakini hii isingalikuwa na maana ya kwamba mwishowe wangeokolewa.

Kwa njia iyo hiyo kiasi kwamba Israel aligeuka nyuma kurudi Misri kwa mioyo yao (Matendo 7:39) na kurudia hali ya kwanza kwenye maisha ya kuufuata mwili na mafunzo potofu, hivyo hao walio “okolewa” toka dhambi kwa ubatizo wanaweza vivyo hivyo kugeuka toka kwenye nafasi yenye baraka ambayo wanasimama. Uwezekano wetu kufanya yale yale kama Israel wa mwili jangwani

umetokeza katika 1 Kor 10:1-12; Ebra 4:1,2 na Rum 11:17-21. Ipo mifano mingi katika maandiko ya wale walio wahi "kuokolewa" kutoka dhambi kwa ubatizo, na baadaye kuangukia kwenye nafasi ambayo inamaana watahukumiwa Kristo akirudi (k.m Ebra 3:12-14; 6:4-6;10:20-29). "Walio wahi kuokolewa siku zote wameokoka" juhudi ya mafunzo ya wahubiri wa Injili imefunua ilivyo kwa maneno haya yaliyo kwenye mafungu- fikira za kudanganya kuufuata mwili kabisa.

Kama na mambo yote, akili sahihi ya matokeo ya mwisho yanatakiwa katika kutafuta kupata kujua upana gani "tumeokolewa" kwa ubatizo. Tendo lisionekane kama linatupatia nafasi ya wokovu- ni bora kadiri iwezekanavyo kuliko bila kubatizwa. Na kuwa "katika Kristo" kwa ubatizo, tunaokolewa kwa matarajio; kwa kweli tunalo tumaini la uhakika kuwamo kwenye Ufalme wa Mungu kama tukiendelea kuwa ndani ya Kristo kama tulivyo wakati tunatoka kwenye maji ya ubatizo wetu tuweze kuwa wanyenyekevu wa ujasiri wa kwamba bila shaka tutakubaliwa kuingia Ufalme wa Kristo akirudi. Hatuwezi kuwa na hakika hata mwisho, kwa sababu tunaweza kukengeuka siku inayofuata; hatujui wakati wetu wenyewe ujao kiroho katika maisha haya.

Yatupasa tufanye yote tuwezayo ili kudumisha dhamiri njema tuliyo nayo na Mungu kwenye ubatizo. Ubatizo ni "patano la dhamiri njema" (1 Pet 3:21 Kiyunani); Mtaka ubatizo anapatana(ahidi) kuitunza hiyo dhamiri iliyowazi mbele za Mungu.

Wakati ubatizo una umuhimu mkubwa kutupatia njia kuelekea wokovu mkuu unaopatikana kwa Kristo, yatupasa tuwe waangalifu tusiwaze ya kwamba kwa kazi moja au "tendo" la kubatizwa pekee tutaokolewa. Awali tumeonyesha jinsi gani ambavyo maisha yanayodumu kushiriki mateso ya Kristo ni muhimu. "Mtu

asipozaliwa kwa maji na kwa Roho, hawezi kuingia Ufalme wa Mungu" (Yn. 3:5). Uwiano huu na 1 Petro 1:23 unaonyesha ya kwamba kuzaliwa kwa Roho kunakotokea baada ya kubatizwa sharti tuongozwe pole pole kiroho na Roho/Neno. Wokovu sio tu kwa sababu ya kubatizwa; ni matokeo ya neema (Efe 2:8) imani (Rum 1:5) na tumaini (Rum 8:24), miongoni mwa mambo mengine. Shauri limesikika mara nyingi kuwa wokovu si kwa kuamini peke yake, na kwa hiyo "tendo" kama ubatizo halina umuhimu. Walakini, Yakobo 2:17-24 inaweka wazi kuwa kuwaza huku kunaweka tofauti potofu kati ya imani na matendo; imani ya kweli, k.m katika Injili imeonyeshwa kwa kuandika kuwa imani ya kweli kwa matendo ni yenye kuwa na matokeo, si kwa imani peke yake" (Yakobo 2:24). Kwa masuala kadhaa ya ubatizo, mwamini aliuliza imempasa 'afanye' nini aokoke; siku zote jibu limehusisha ubatizo (Mdo 2:37;9:6; 10:6; 16:30). "Kufanya" halafu "tendo" la kubatizwa kwa hiyo ni kionyesho cha lazima kwa jinsi tulivyoiamini Injili ya wokovu. Tendo la kutuokoa mwishoni limefanywa na Mungu na Kristo lakini tunahitajika kufanya "matendo yanayopatana na kutubu" na kuamini hili (Matendo ya Mitume 26:20 linganisha na Marko 16:15,16).

Awali tumeonyesha kwamba msemo wa kuoshwa dhambi unatajwa msamaha wa Mungu kwetu kwa sababu yetu kubatizwa katika Kristo. Kwa maneno mengine tumesemwa ya kuwa tumeoshwa dhambi zetu kwa imani yetu na kutubu (Mdo 22:16; Uf 7:14; Yer 4:14; Isaya 1:16); kwa mengine Mungu ameonekana kuwa yeye atuoshae dhambi zetu (Ezek 16:9; Zab 51: 2,7; 1Kor 6:11). Kwa uhalisi haya yanaonyesha jinsi gani kwamba kama tukifanya kwa upande wetu kubatizwa katika Kristo, wakati huo Mungu ataondoa dhambi zetu. Hivyo 'kazi' au tendo la ubatizo ni hatua muhimu katika kushika habari njema za neema ya Mungu ('upendeleo usiostahili'), tuliokwisha pewa katika Neno lake.

### *Tumeacha kitambo sehemu ya 30: Kubatizwa tena*

Watu wengi wanahisi kutofanya lolote kabisa kubatizwa baada ya kuwa tayari walifanya kile kinachodhaniwa kuwa ulikuwa ni "ubatizo" wa namna fulani aidha kwa kunyunyuziwa maji akiwa mtoto mchanga, au kuzamishwa kwenye maji mengi katika kanisa lingine. Ingawa hivyo, kabla ya ubatizo inabidi pawepo toba na imani sahihi ya Injili ya kweli (Mdo 2:38; Marko 16:15,16). Ubatizo basi ni ubatizo kwa sababu ya mambo haya yakiwa katika mpango kabla ya kuzamishwa kwenye maji. Mathayo 28:19,20 unaunganisha ubatizo na kusikia kwanza mafunzo ya Kristo aliyoeleza.

Mtoto mdogo hawezi kutubu au kufahamu Injili; kwa vyovyote, kunyunyuziwa si ubatizo. Mpiga mbizi akiogelea katika bwawa aweza kuzama katika maji lakini huo si ubatizo, kwa kuwa mtu hajui kuitikia Injili ya kweli. Vivyo hivyo ni kweli kwa hao wanaobatizwa katika maji mengi wakati wakiamini mafundisho potofu; wamezamishwa katika maji lakini hawajabatizwa.

Ila kuna "imani moja", yaani orodha ya mafundisho yanayofanya kuwa Injili ya Kweli, na kwa sababu hii tu "ubatizo mmoja" - ubatizo unaotokea baada ya kusadiki "imani moja". Kuna mwili mmoja (yaani kanisa moja la kweli)…… kama na mlivyoitwa katika tumaini moja la wito wenu. "Bwana mmoja, imani moja, ubatizo mmoja, Mungu mmoja"(Efe 4:4-6). Hakuna matumaini mawili, kama ilivyoaminika na hao wasemao kwama hayo ni mamoja ikiwa twaamini thawabu yetu itakuwa mbinguni au duniani. Yupo "Mungu" mmoja tu -basi Yesu si Mungu. Kwa

sababu hiyo kama, wakati tulipobatizwa, tulishidwa kufahamu mafundisho ya msingi kama Ufalme wa Mungu, sifa na tabia ya Mungu na Yesu, n.k basi ‘ubatizo’ wetu wa kwanza haukuwa wa msingi.

Yohana mbatizaji aliwazamisha katika maji watu, akiwataka watubu na kuwafunza mambo hakika ya kuhusu Yesu (Marko 1:4; Luka 1:77). Lakini, huu haukutosha. Matendo 19:1-5 taarifa imetolewa kuwa wengine ambao Yohana aliwabatiza ikawabidi wabatizwe tena kwa kuwa hawakukamilika kushika mafunzo ya hakika. Kama wale ambao Yohana alibatiza, tunaweza kuona ya kwambva kwenye kuzamishwa kwetu kwa kuanza tulifanya toba halisi na kuanza upya. Huu waweza kuwa kweli lakini hauondoi haja ya kupokea “ubatizo mmoja (wa kweli) unaoweza kutokea tu baada ya kushika mambo ya “imani moja”.

***Tumeacha kitambo sehemu ya 31: Kiwango cha elimu itakiwayo kabla ya kubatizwa***

Wasomaji wengi watakuwa wamewahi kukabiliwa na hao walio katika makanisa ya ‘Kiinjili’ wanao hoji ya kwamba mafundisho hayana umuhimu katika wokovu, na ya kwamba maneno tu ya kuungama kuwa ‘Nina amini, Yesu Kristo ni mwana wa Mungu’ ni sharti la msingi kupata wokovu. Kwa kijuu juu hii inaonekana kuwa kweli kwa sababu ya jinsi waongofu walivyoandikwa katika matendo, huku pia wakitaka mambo ya ‘upendo’ na ‘uvumilivu’ vyote vikiwa ni roho ya kipindi chetu.

Somo hili linatoa uchanganuzi mmoja-mmoja zaidi umuhimu wa mafunzo.

**NI UPESI SANA KWA NINI?**

Hapawezi kuwapo shaka ya kwamba usomaji upesi wa Matendo ya Mitume kunatoa wazo la kuwa ubatizo mwingi ulitumia mafundisho kidogo yenye thamani katika misingi ya Injili, na pamoja na kuungama kifupi tu kuwa Kristo ni mwana wa Mungu. Kwa kusema maneno matatu: 'Mimi namwamini Kristo' ni wazi sio namna yenye maana kwa wokovu- na idadi kubwa ya madhehebu ya 'Wainjilisti' watakubali ya kwamba pawepo maarifa mengine baadhi au ufahamu moyoni mwa mtu awaambiaye maneno hayo kuwa ni yenye maana.

Hii maana haiwi ngumu kuiweka. Ni shida basi, kupinga ya kwamba maneno yanayotoa taarifa ya maungano ya kuamini Kristo kuwa ni mwana wa Mungu yanathibitisha msemo huu wa maneno kwamba ndiyo yanayohitajika kabisa. Karibu ni maana ya kawaida kuwa kusema tu kwa kifupi hiyo sentensi, bila kujali mawazo ya mtu mwingine na imani, hakuwezi kumweka kwenye njia ya wokovu. Vipengele vifuatavyo vitaweza kusaidia katika kueleza huku kuongoka kunakoonekana upesi:

- Taarifa iliyo katika Matendo ya Mitume - kama katika maandiko mengi - ni kwa lazima habari imefupishwa sana. Inafanya mazoezi ya kuvutia kusoma kwa sauti baaadhi ya hotuba zilizoandikwa katika Matendo na kujua muda inayochukua kufanya hivyo; ni hakika kidogo zingechukua muda mfupi kwa kweli, ukijumuisha nyingi ambazo hazijaandikwa. Mifano kadhaa:

Utetezi wa Paulo katika mji wa Yerusalemu umechukua dakika nne kusoma (Mdo 22); hata mbele ya Feliki dakika moja;

mbele ya Agripa dakika nne; Akiwahubiri watu Petro siku ya Pentekoste alichukua dakika nne tu; hata kwa Kornelio dakika tatu; Hotuba ya Bwana baada ya kulisha watu 5,000 (Yn. 6) dakika 6, mahubiri mlimani dakika 18. Petro alihubiri katika Matendo 3:12-26 alichukua karibu dakika mbili kusoma kwa sauti; lakini kwa kweli ulikuwa ni muda wa kutosha kwa habari iliyomo katika mahubiri yake kupelekwa hadi kwa “makuhani, na akida wa Hekalu na Masudukayo” na wao kuwatokea (Mdo 4:2).

Hivyo ukweli wa kwamba ‘mafunzo’, yaliongelewa kwa kirefu zaidi kwa atakaye kubatizwa muda haujaelezwa na si kwamba ushahidi hautatokea. Mjadala kuwa kimya si wa hakika sana kwa suala hili.

 Kuwa na “kipawa cha maarifa (kufanya miujiza)…. Kuchunguza roho (mioyo)” kuliwawezesha wahubiri wa kwanza kuisoma mioyo ya watu kwa usahihi ya wale waliowahubiri, basi kufanya maulizo- mahojiano ya mafundisho, kama tunavyohitaji, si lazima.

 Ipo sababu ya kuamini kuwa ubatizo wa watu wengi ambao ni Wayahudi wa Yerusalemu mwanzoni mwa Ukristo lilikuwa ni suala mahususi. Hakuna ushahidi ya kwamba utaratibu huu ni uwingi wa ubatizo uliofanywa baadae katika karne ya kwanza. Ikiwa waongofu wangeendelea kwa kiwango kile, basi Yerusalemu yote ingejawa na Ukristo ndani ya miaka michache. Watu hawa wakiwa ni Wayahudi kulikuwa na maana ya kwamba walikuwa na elimu nzuri ya Agano la kale na njia ya Mungu. Kina cha waraka wa Paulo kwa Waebrania na Petro (kwa Wayahudi vilevile) unaonyesha kwamba wasomaji wake walikuwa na uwezo wa kufahamu misemo iliyosemwa mingi katika Agano la Kale. Inashangaza kwamba Paulo anaelezea anachosema kuhusu

Melkizedeki kuwa ni maziwa ya neno, kwa sababu yao kutokukua kiroho (Ebra 5:11,12). Hali hiyo akiwaagiza kwa kutokukua sana tangu wakati ule. Inaonekana kwamba nyaraka hizo kimsingi ziliandikwa kwa ajili ya Iklezia lililokuwepo Yerusalemu, wengi wao walikuwa wamebatizwa siku za kwanza zilizoandikwa mwanzoni mwa Matendo ya Mitume.

□ Tunatumaini kuonyesha ya kwamba kuhubiri jina la Kristo na kuungama ambako kumeelezewa katika Matendo ilikuwa sawa na kuelewa kabisa mafunzo yote yaliyonenwa.

□ Ilionekana toka 1 Kor 1:17 ya kwamba Paulo (na mitume wengine?) alishughulika katika kazi za siku zote pamoja na ya maana inayofuata ya waalimu na wanaobatizwa, hivyo basi alitumia kadiri ya muda mfupi tu kwa kila mahali alipohubiri.

**JINA LA YESU**

Jina la Mungu lina mafunzo mengi kumhusu Yeye na njia zake- Majina ya Mungu na vyeo vinaeleza tabia yake na nia. Jina la Yesu Kristo pia si utaratibu tu wa kupeana majina bali maneno yenyewe ni yenye mafunzo ya kina. Kuamini jina la Yesu kumelinganishwa na kubatizwa (Yn. 3:5,18,23). Gal 3:26,27 yafanya imani kwa Kristo kutoepukika imeungwa na ubatizo katika yeye: "Ninyi nyote ni wana wa Mungu kwa imani iliyo kwa Kristo Yesu. MAANA ninyi nyote mliobatizwa katika Kristo mmemvaa Kristo. Mifano zaidi ya huku kuungwa kati ya kusadiki na kubatizwa kunapatikana katika Matendo 19:4; 10:42 linganisha na 48; 2:37,38; Lk 24:47. Apolo "aliujua" ubatizo wa Yohana (Mdo 18:25) ikionyesha kwamba ubatizo sio tu ni tendo, bali kunahusisha kujua mafundisho hakika.

" Filipo….. akawahubiri Injili" (Mdo 8:5) yaonekana kana kwamba alisema tu 'Mumwamini Yesu'; lakini "Kristo"

amefafanuliwa katika Matendo 8:12: " Lakini walipomwamini Filipo, akihubiri habari njema (Injili) za ya Ufalme wa Mungu, na jina lake Yesu Kristo, wakabatizwa wanaume na wanawake. Elewa kwamba "mambo" yapo katika uwingi; si taarifa fupi tu kuhusu Kristo; na 'kuwahubiri Kristo' vile vile kulikuwa ndani yake mafunzo ya ubatizo. Yohana 6:40 unatuambia ya kwamba ni mapenzi ya Mungu "ya kwamba kila amtazamaye (amfaamuye) Mwana na kumwamini yeye, awe na uzima wa milele", ambapo baadaye Yesu anasema kuwa "Mtu akipenda kuyatenda mapenzi yake (Mungu), atajua habari ya yale mafunzo" (Yohana 7:17). Basi kujua mafunzo ni sawa na 'kumtazama' Mwana. Maneno ya Kristo "Umelitunza neno langu, wala hakulikana jina langu" (Ufunuo 3:8) vile vile laonyesha ya kwamba neno la Kristo ni sawasawa na jina lake. Kristo akivuviwa ananukuu Isaya 42:4, "Visiwa vitaingojea sheria yake (Kristo)" kama "katika jina lake Mataifa watalitumainia"(Math. 12:21), tena jina lake linalingana na Injili kumhusu yeye. Waraka wa pili na wa tatu wa Yohana una ushahidi wa wahubiri wakisafiri "Walioshuhudia upendo wako mbele ya kanisa; utafanya vizuri ukiwasafirisha kama ipasavyo kwa Mungu, kwa ajili ya jina hilo, walitoka" (3 Yoh 6,7). Hii yaonesha kutaja siku za nyuma kazi waliyopewa kwa Marko 16:15,16, kwenda ulimwenguni kote na kuhubiri Injili, hivyo jina la Kristo na Injili yake vinalingana. "Kumwamini Kristo" kibiblia jambo la kubatizwa limejumuishwa: "Ninyi nyote ni watoto wa Mungu katika imani iliyo kwa Kristo Yesu. Maana (yaani, kwa sababu) nyote mliobatizwa katika Kristo mmemvaa Kristo"(Gal. 3:26,27). Paulo anasema kana kwamba wao kumwamini Kristo kwa kawaida yalikuwepo maelezo yao ya hiyo imni ya ubatizo. Basi kumwamini Kristo ni mambo yanayoendelea kufuatana na utii, si kwa maneno tu ya haraka kuungama 'Ninamwamini Kristo'. Hili limesemwa kutoka kwa Yohana 6:35: "Yeye ajaye kwangu hataona njaa kabisa, naye aaminiye na kubatizwa hataona kiu kamwe" ambalo ni

sawa na kumwamini Kristo na KUJA kwake - laonyesha kwamba imani ni jambo la maendeleo.

Kuhubiri "Kristo" kwa hiyo yalikuwamo mfululizo wa mafundisho. Vivyo Luka 9:11 unamtaja Kristo akihubiri ufalme wa Mungu (ulinganishe Mthayo 4:23), wakati habari iliyo sambamba katika Marko 6:34 inamtaja akiwafundisha "mambo mengi". Injili ina "mambo mengi" - sio taarifa fupi tu kuhusu Kristo ambayo inaweza kusemwa kwa dakika. Hivyo tunasoma mafungu ya maneno kama, "Hata walipokwisha kuhubiri Injili katika mji ule, na kufundisha mambo mengi…." (Mdo 14:21 A.V), ni sawa sawa kuhubiri na kufundisha. Kusema hivi kungekua si muhimu kama Injili ilikuwa na taarifa moja pekee rahisi. Kuhubiri Paulo kule Beroya kulisababisha watu wakachunguza Maandiko kila siku (kwa nakala za Agano la Kale katika Sinagogi?) ili waone kwamba mambo hayo alioyafundisha Paulo msingi wake ulikuwa katika Agano la kale lote. Na ilikuwa kwa sababu ya watu maendeleo ya kuisoma Biblia baada ya kumsikia hata wakaamini - "Basi watu wengi miongoni mwao wakaamini" (Mdo 17:12). Tunaposhughulika na watu walio na maarifa kidogo ya Biblila ya wasio chunguza mara kwa mara Biblia mara baada ya majadiliano, si ajabu ya kwamba wakati mafunzo unachukua muda mrefu kuliko katika Karne ya kwanza. "Kila mtu aaminiye kwamba Yesu amezaliwa na Mungu" (1Yoh 5:1) ni wazi aya hii inafanana na mistari kama "Kwa kupenda kwake alituzaa sisi kwa neno la kweli" (Yakobo 1:18)."Kwa kuwa mmezaliwa mara ya pili … kwa neno la Mungu….. neno hilo ni neno lile jema lilohubiriwa kwenu" (1 Petro 1:23,25). Hii yaonyesha ya kwamba kuamini kuwa Kristo ni mwana wa Mungu ni maelezo mafupi yenye ukweli wa kwamba mtu ameielewe Injili ambayo ndani ina neno la Mungu.

**MFALME WA UFALME**

Mkazo wa “kumwamini Kristo” unakuwa na maana zaidi mara ukifahamika ya kwamba cheo ‘Kristo’ kinaweza kusomwa kwa maana ile ile katika lugha moja ya maneno mengine ya Ufalme wa Kristo. Hivyo Bwana wetu aliwambia Mafarisayo ya kwamba hawakuwa na haja ya kwenda kuzunguka wakitarajia kuja kwa Masihi, kwa kuwa alikuwa tayari amesimama miongoni mwao. Ameeleza hivi kwa maneno “…Ufalme wa Mungu huko kati yenu(B.H.N)” (Lk. 17:21), waonyesha kwamba “Ufalme” utalingana na Mfalme wa Ufalme. Mahubiri ya Yohana ya kwamba Ufalme wa Mungu umekaribia basi alikuwa anatoa habari ya kudhihirika kwa Kristo. Jiwe linaloponda sanamu ya ndoto ya Nebukadneza lasimama badala ya Ufalme wa Mungu (Dan 2:44); ni jiwe/Ufalme “ utakaovunja falme zote hizi vipande vipande na kuziharibu”, habari yaaonyesha kwamba jiwe ni Ufalme utakaovunja sanamu, vile vile’ baada ya kuziharibu. Katika uzi wa mfano mmoja wa Ezekieli na mzabibu kimeelezewa “kitawi chororo” vijiti vyake vimekatwa na kupandikizwa, hata ukawa ni mti mkubwa, “ na chini yake watakaa ndege wa kila namna ya mbawa” (Ezekiel 17:22,23). Unapaswa huu mfano kuwa unamtaja Kristo, “mche mwororo” wa Isaya 53:2; hata hivyo upo muungano dhahiri wa mfano wake wa mbegu ya haradali, ambapo Ufalme wa Mungu umelinganishwa na punje ndogo ya mbegu ikakuwa hata ikawa mti mkubwa, chini yake ndege wa aina mbalimbali wakaweka viota vyao. Muungano huu kati ya neno la Ufalme na Yesu mwenyewe nafsi yake inaonyesha kwamba alijiona mwenyewe kuwa ni neno lililohai la Ufalme. Kwa mwanga huu unaelekea kwamba ‘kumwamini Kristo na kuiamini Injili yote ya Ufalme wa Mungu vyote ni mamoja.

**INJILI NI NINI?**

Sasa tunajadili kwa maelezo zaidi yale yaliyodhaniwa kuwa ni maunzo ya muhimu miongoni mwa waaminio katika karne ya kwanza. Inabidi itambulike ya kwamba palikuwepo muundo mkuu katika Nyakati za Agano Jipya ambao kwa karibu sana ulikuwa sawa na "Habari ya Imani" yetu. Kigawanyo kingine muhimu kumbuka walikuwepo ndugu wenye kipawa cha unabii -'utabiri ulionyooka wa ufunuo toka kwa Mungu chini ya kuvuviwa. Ipo sababu ya kuamini kuwa pamoja na muda mwingine wa kunena usemi ulipovuviwa uliongezeka kwenye muundo mkuu wa mafundisho.

**MUUNDO MKUU WA MAFUNZO**

Paulo aliweza kusema ya kuwa kwenye iklezia la Ruma karibu "walitii kwa mioyo yao ile namna ya elimu ambayo mliwekwa chini yake" (Rum 6:17) kabla ya kubatizwa kwao. Kwa kiyunani "namna" imetafsriwa "Mfano" na "Mfano mzuri " - kana kwamba ilitaja mafundisho ambayo yaliigwa kila mahali. Ushuhuda wa Paulo kwa huu unaonyesha umuhimu wa muundo mkuu ulioainishwa na mafunzo yanayopaswa kueleweka kabla ya ubatizo, na vile vile hazikuwa ni habari chache fupi ambazo zilitajwa kabla ya ubatizo. Wengine ndani ya Iklezi walikuwa na "mfano wa utauwa, huku wakikana nguvu zake" (2Tim 3:5), labda imedokezwa ya kwmba walishika mafunzo ya msingi wa imani lakini bila ya kutambua nguvu halisi ya KWELI katika maisha yao ya kila siku. Paulo aliweza kuwakumbuka Wagalatia ya kwamba "Yesu Kristo aliwekwa wazi mbele ya macho yenu ya kuwa amesulubiwa" (Gal 3:1). Kwa Kiyunani "kuwekwa" maana yake halisi "iliandikwa picha kwa maneno yaliyoandikwa, kana kwamba maagizo ya kwanza yalikuwa kwa njia nyingine - mfano ulioandikwa wa maagizo ya mafundisho.

Akifafanua mafunzo ya ufufuo, Paulo aliweza kusema “Naliwatolea ninyi…. yale niliyoyapokea mimi mwenyewe, ya kuwa Kristo alikufa…..” (1Kor 15:3), yaonyesha jinsi gani alipokea ufunuo kuhusu mambo haya, naye akawatolea wao kama mafunzo yanayowapasa kukubalika kuwa ya muhimu. 2 Petro 2:21,22 kwa uzuri unaangukia hapa: “Ingelikuwa heri kwao kama wasingalijua njia ya haki: ….. kuiacha ile amri takatifu waliyopewa. Lakini…… aliyeoshwa (kwa ubatizo) amerudi kugaa-gaa matopeni”.

Hapa “njia” na “amri takatifu” ambavyo “aliwatolea” kwao vyote viwili vimeungwa na kuoshwa kwa ubatizo; basi “amri” katika umoja yaweza kudokeza ya kwamba ulikuwepo muundo mkuu wa mafunzo ulioainishwa wazi wazi kabisa ambao ilibidi ufahamike kabla ya kubatizwa. Yapo mafungu kadhaa ya maneno yasemayo ‘kupokea’ mafunzo yahusuyo Elimu na “Injili”: Gal 1:9,12; Flp 4:9; Kol2:6; 1The 1:6; 2:13;4:1. Hii inathibitisha ya kwamba ‘Injili’ ilikuwa na muundo wa namna yake maalum wa mafundisho ambayo ‘yalipokelewa’ ya kwanza na mitume na kisha kwa wale ambao walihubiriwa.

**“IMANI”**

Yuda nae anazungumzia “imani waliyokabidhiwa watakatifu (wote) mara moja tu” (Yuda 3). Kwa hivi "imani” ni sawa sawa na “ile imani ya elimu” iliyokabidhiwa kwao kabla ya kubatizwa, yalikuwa ni maneno mengine katika msamiati wa karne ya kwanza uliotaja muundo mkuu wa mafundisho. Onyo la Paulo “kushika sana ungamo la tumaini (imani) yetu” (Ebra 10:23) laweza kuwa linataja nyuma ungamo lao mbele ya watu imani katika “tumaini” kabla ya ubatizo wao. Kulishika lile “neno la imani” (Tito 1:9) mara ya kwanza inatajwa kuitengeneza hii ‘habari ya imani’ ambayo awali ilifundishwa. “Imani tuishirikiyo” (Tito 1:4)

yaonyesha jinsi gani huu muundo wa mafundisho walishirikiana wote waaminio; ili kuwepo “imani moja” tu (Efe 4:5). “Imani” na jina la Kristo ni jina lingine kwa fundisho lile lile lililomo ndani ya “Imani”. Kwa mambo yote mawili ya mazoea (1Tim 6:10) na mafundisho (1Tim 4:1) Paulo alitahadharisha ya kwamba wengine“watajijenga na Imani”. Hatua ya kwanza katika huko kukengeuka ilikuwa ni kusema ya kuwa “imani” haikuwezekana kuiainisha.

**MAMBO YA MAZOEA**

Mambo ya desturi vilevile yalikuwa sehemu ya muundo huu wa mafundisho. “Kumwamini Kristo” kulijumlisha hoja ya kuhusu “haki, kuwa na kiasi na hukumu itakayokuja” (Mdo 24:24,25). Paulo anazungumzia maagizo yanayohusu kumega mkate kama anavyofanya mafunzo juu ya ufufuo. “mimi nalipokea kwa Bwana niliyowapa nanyi” (1Kor 11:23). Hapo yaonekana lilikuwepo kundi lenye desturi ya mambo haya, ambayo baadaye Paulo aliyapanua kwa kuongeza mafunzo juu ya nafasi ya wa dada katika Iklezia: “Nanyi mmeshika yale mapokeo vile vile kama nilivyowatolea. Lakini nataka mjue ya kuwa…… kichwa cha mwanamke ni mwanamume….”(1Kor 11:2,3). Haya yanaonekana kuwa maelezo ya mambo yawe kabla ya kubatizwa, nayo yalikuwa sehemu ya muundo mkuu uliosisitizwa kwenye karne ya kwanza. Kwa Kiyunani “amri” pia ni neno lililotafsiriwa “mapokeo” katika 2 Thes 3:16 na 2:15: “Jitengeni ….. na kila ndugu aendaye….. si kwa kufuata mapokeo mliyopokea kwetu…… simameni imara, mkayashike mapokeo mliofundishwa, ama kwa (kuvuviwa, Unabii) wa maneno, au kwa waraka wetu”.

Haya yaonyesha umuhimu mkubwa wa kushika muundo huu mkuu wa mafunzo, na haja ya kujitenga toka kwa hao wasio wa utii: “Kwa kushika lile neno la imani (namna nyingine ya maelezo

ya u huu mkusanyiko wa muundo wa mafundisho) vile vile kama alivyofundishwa, apate kuwaonya watu kwa mafundisho yenye uzima, na kuwashinda wenye kupinga" (Tito 1:9).

Tunajua walikuwepo "manabii wa uongo"katika Iklezia ya kwanza, wakidai kuwa na mafunuo toka kwa Mungu juu ya mafundisho ambayo yaliongezwa ili muundo wa mafunzo ukubalike. Basi Paulo anakazia "neno la kuaminiwa" la ufunuo wa elimu iliovuviwa (Tito 1:9; 3:8; 2Tim 2:11; 1Tim 4:9), ambalo "linastahili kukubalika" (1Tim 1:15; 4:9) - yaani, katika muundo mkuu wa mafundisho yanayofanya "imani". Hii ndiyo sababu Yohana alitoa tahadhari "….msiiamini kila roho" inayodai imevuviwa (1 Yohana 4:1).

**HABARI YA MAMBO MOJA MOJA DHAHIRI**

Ifuatavyo ni baadhi tu ya mifano iliyowazi mahali mafunzo mengine kuliko "kumwamini Kristo" tu ilifundishwa kama sehemu ya msingi wa injili ambayo ilieleweka kabla ya kubatizwa.

-"Mungu atazihukumu siri za wanadamu, sawa sawa na Injili yangu" (yaani, ile moja aliyoihubiri Paulo; Rum 2:16). Mafunzo ya kiti cha hukumu na kuhusika kwa sababu hiyo yamepimwa kuwa ni 'jambo la kwanza' tazama pia Matendo ya Mitume 24:25, Ebra. 6:1,2.

-Wazo la tohara kwamba lilikuwa la muhimu kwa wokovu lilielezwa na Paulo kuwa ni "Injili nyingine" (Gal 1:6) Hivyo kujua ya kwamba tusishike torati ya Musa, k.m Sabato, ni sehemu ya kuwa sasa tunafahamu Injili.

-"Injili ya Ufalme" sio tu ni kuhusu Kristo bali pia ni juu ya Ufalme wake unaokuja; Isaya 52:7 (linganisha na Rum 10:15)

anasema mhubiri wa Injili anayetaja kipindi hapo itakapoweza kusemwa Sayuni “Mfalme wako anatawala “- yaani katika Ufalme.

-Kuelewa vema ‘maana nzuri’ jinsi Kristo alivyokuwa lilikuwa ni jambo la ushirika (2Yn. 7-10); kwa sababu hii Injili ilihusu “mambo” ya uwingi, juu ya Kristo (Mdo 8:12). Tena, kusema tu ninamuamini Kristo haitoshi.

-Umuhimu wa ahadi kuhusu Ufalme ni sehemu kuu ya Injili; ilikuwa na kwa ahadi hata Injili ilihubiriwa kwa Abrahamu (Gal 3:8) na Israeli (Ebra 4:2). Hivyo Paulo alinena katika kuhubiri kwake juu ya ahadi zilizofanywa kwa Daudi kuwa ni “neno la wokovu” (Mdo 13:23,26). Kwa hiyo zilikuwa ni sehemu muhimu ya ujumbe wa wokovu. Hivyo anasema “Na sisi tunawahubiri habari njema ya ahadi ile waliyopewa mababa” (Mdo 13:32). Vivyo hivyo Rum 1:1-4: “ Injili ya Mungu yaani, habari za mwanawe, aliyezaliwa katika ukoo wa Daudi kwa jinsi ya mwili ….. Yesu Kristo”.

-Ili kuelewa ahadi unatakiwa kufahamu hakika historia ya Israeli. Somo la mahubiri ya Paulo pale Antiokia katika Matendo 13 linamwonyesha akieleza habari ya historia ya Israeli na mkazo maalum juu ya ahadi akasisitiza jinsi gani zilitimilika kwa Yesu. Hivyo mahubiri yake msingi ulikuwa juu ya historia ya Israeli, nayo ilikuwa tunayoweza kuiita

‘uwazi’ akimaliza kwa kuonya matokeo ya hukumu kwa kutoitika neno alilokuwa anahubiri (Mdo 13:40,41). Katika mahubiri yetu yawe namna hii.

**MWISHO**

Ukubwa wa yote haya hauwezi kukaziwa zaidi. Ila “Jitunze nafsi yako, na mafundisho yako; Dumu katika mambo hayo; maana

kwa kufanya hivyo utajiokoa nafsi yako na wale wakusiao pia" (1Tim 4:13-16). Orodha ya mafundisho makubwa kama haya yaliyotolewa mwishoni mwa kitabu sehemu ya 1 ya kitabu hiki kwa udhahiri hayakuvuviwa, bali katika wazo la mwandishi unaonekana ni muhustasari mzuri wa mambo mengi ya namna yake maalum yaliyotajwa kwenye mafungu ya maneno ya Biblia yanayozungumzia mambo ambayo ni ya sehemu ya "imani", "mapokeo" n.k . Kwa matumaini somo hili limeonyesha kwamba ipo haja halisi ya kuwa na muundo mkuu wa mafundisho ambayo sote tunaukubali na kutokuwa wavivu kuthibitisha utii wetu utupasao kwake. Yaliyomo katika muundo huu mkuu wa mafundisho yawe ni maagizo yetu kwa watakao ubatizo., tena ni vizuri kwao kuchunguza kwa kujadiliana kabla ya kutumbukizwa kwao ili wafahamu kabisa mambo waliyofundishwa. Mara nyingi waaminio walitiwa moyo waambatane na "Imani" katika wakati wa shida. "Msingi wa Mungu ulio imara umesimama". Mazoea yetu kwa mambo makuu ya kwanza, na njia ya ajabu ya kusudi la Mungu kushikamana pamoja, ndani yake yenyewe yatutie moyo. Kwa kuhubiri kwetu kabisa kila mara au kujifunza tena na tena mambo haya hii itakuwa faida na maana ya kina ya matumaini yetu, hivyo kama Paulo katika saa yake ya giza na upweke tunaweza kusema "….. mwendo nimeumaliza, imani nimeilinda…. Maana namjua yeye niliyemwamini, na kusadiki ya kwamba aweza kukilinda kile nilichokiweka amana kwake (maisha yetu, utu wetu wote) hata siku ile" (2 Tim 4:7; 1:12).

## MAELEZO YALIYO CHINI YA UKURASA: KUMKIRI BWANA YESU

"Kwa sababu, ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kumuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka" (Rum 10:9).

Vipengele vifuatavyo vinahitaji kufanywa:

 Tumeonyesha kwamba ‘Bwana Yesu’ ni neno lililoelekea kuwa na maana ile ile na jingine katika Lugha moja ya Muundo mzima wa mafunzo makuu yaliyo na “mambo yanayohusu Ufalme wa Mungu na jina lake Yesu Kristo”, pamoja na ubatizo (Mdo 8:5 linganisha mst. wa 12). ‘Kukiri’ anakosema Paulo vema kunaweza kuwa kwenye ubatizo. Kwa suala hili alikuwa anataja kwa kusema Marko 16:16 “Aaaminiye (linganisha, kukiri kwa kinywa) na kubatizwa (linganisha, kufufuka na Kristo toka kwa wafu) ataokoka”.

-Kuelewa ufufuo wa Kristo kunahusisha kufahamu fundisho la Biblia jinsi mwanadamu alivyo.

-Rum. 10:8,9 yaonekana kuwa sawa na mst wa 13: “Kwa kuwa, kila atakaye liitia

(yeye mwenyewe, kwa Kiyunani) Jina la Bwana ataokoka.” Paulo anasemwa kama amebatizwa na hivyo akiliitia mwenyewe jina la Bwana (Mdo 22:16); Ubatizo tu unatupatia kuingia katika jina la Bwana (Math 28:19).

-Umuhimu wa kubatizwa ukishatiliwa mkazo katika sura chache awali Warumi 6, haiwezekani kwamba Paulo angefundisha sasa ya kuwa haukuwa na ulazima kwa ajili ya wokovu katika sura ya 10.

-Rum 10:9 umetanguliwa na mst 6-8: “Usiseme moyoni kwako, Ni nani atayepanda kwenda mbinguni ….. Ni nani atayeshuka kwenda kuzimu? …lakini yanenaje? Lile neno li karibu nawe, katika kinywa chako na katika moyo wako: yaani, ni lile neno la imani tulihubirilo”. Neno (lile) la imani” basi lilikuwa

lenye kuwapasa kulikiri, sawa sawa na "Bwana Yesu" katika mst wa 9. Tumeona ya kwamba "Imani" inatoa maelezo ya muundo mzima wa mafundisho yaliyo na Injili. Paulo ananukuu toka Kum. 30:11-14: "Maagizo haya nikuagizayo leo, …. si mbinguni wala si ng'mbo ya pili ya bahari (kilindini)…. lakini neno li karibu nawe sana". Anaonekana akitafsiri "neno" …. "maagizo haya" kama kumtaja Kristo. Kwa njia iyo hiyo ikiwa kama Israeli wangelitunza neno wangelibarikiwa (Kum 30:16), hivyo kama Israel wapya waliamini neno kuhusu Kristo wangaliokolewa. Basi kumkiri Kristo kwa kinywa kunalingana na kukubali fundisho juu ya Kristo. "ukiwa utaifuata sauti ya BWANA" (Kum 30:10) ni sawa na Rum 10:9: "Kwa sababu, ukimkiri Yesu kwa kinywa chako". Huku kuwa sawa sawa tena inaonyesha kwamba "Bwana Yesu" ni jina lenye maelezo mafupi yenye fundisho la msingi wa neno la Mungu.

### *Tumeacha kitambo sehemu ya 32: Mnyang'anyi Msalabani*

Mnyang'anyi "alimwambia Yesu, Bwana nikumbuke utakapoingia katika ufalme wako. Yesu akamwambia, Amini, nakuambia, Leo hii utakuwa pamoja nami peponi" (Lk. 23:42,43). Aya hizi zimechukuliwa kuwa na maana moja ya kuwa ubatizo si wa muhimu kwa wokovu, na ya kwamba mara baada ya kufa tunakwenda mbinguni. Mbali toka ushahidi wote mwingine kutofautiana, kusoma fungu la maneno kwa karibu linadhihirisha yafuatayo:

1. Agizo la kubatizwa katika mauti ya Kristo na ufufuo lilitolewa baada ya kufufuka kwa Kristo (Marko 16:15,16). Yule mnyang.anyi alikuwa bado anaishi chini ya Torati ya Musa Kristo aliponena naye.

2. Ubatizo wa kweli ni katika mauti na ufufuo wa Yesu. Kwa kuwa Yesu alipozungumza na mnyang'anyi wala matukio hayo hayakutokea, kubatizwa katika Kristo haukuwezekana.

3. Ubatizo unaashiria kufa kwetu na Kristo (Rum 6:3-5). Mnyang'anyi ndiye pekee aliyefanya hivi.

4. Inawezekana kabisa ya kwamba yule mnyang'anyi alikuwa ni mmoja wa wale waliowahi kubatizwa na Yohana mbatizaji. Wengi waongofu wake zamani walikuwa na tabia isiyonyoofu (Math 21:32).Kusema mnyanganyi hakubatizwa ni kuleta sababu za kupinga kutokana na ukimya; ambalo ni jambo kamili tu juu ya kutoa udhuru sisi wenyewe kutoka agizo la kubatizwa. Vivyo hivyo fungu lipo kimya kuhusu maneno 'nafsi' na 'mbinguni'

5. Mnyang'anyi alimwomba Yesu amkumbuke kwa mema hapo Yesu akirudi "katika" Ufalme wake (R.S.V). Kwa hiyo mnyang'anyi hakuwa mjinga wa kutojua Injili ya Ufalme wa Munngu aliyokuwa Yesu anahubiri(Math 4:23). Alijua ya kwamba itakuwepo siku ya hukumu wakati wa kuanzishwa kwa Ufalme huo, na kwa sababu hii alimwomba Yesu, aliyemjua atafufuka katika wafu na hatimaye kufanya hukumu siku hiyo, amkumbuke kwa wema. Bila shaka yule mnyang'anyi hakuwa mtu asiyejua; alitambua ya kwamba wokovu katika siku ya ufufuo na hukumu utatamkwa toka midomo ya Kristo.`

6. Yesu alijibu ya kwamba mnyang'anyi atakuwa naye "peponi"(Kiyunani ni Paradiso)- neno hili siku zote linataja hali timilifu duniani. Limetumika kuhusu kurudia Bustani ya Edeni itakoyoonekana katika Ufalme ujao wa Mungu duniani (Uf. 2:7). Wakati wa Ufalme wa Mungu, ulimwengu utarudi kwenye hali ya Paradiso ya Bustani ya Adeni (Isa 51:3; Ezek 36:35), laana itakapo

kuwa imeondolewa (Uf. 22:3). Kwa kiswahili tuna neno ‘peponi’ kuwa na maana sehemu yenye raha, hivyo imedhaniwa ni mbinguni kutokana na uongo kama wa ‘Kupotea Paradiso ya Milton’. Ahadi ya Yesu kwa mnyang’anyi kuwa na sehemu katika paradiso ilikuwa ni haja yake kuwa katika Ufalme wa Kristo. Tumeonyesha katika somo la 5 kuwa Ufalme utakuwa duniani; ‘peponi’ kwa hiyo patakuwepo vile vile.

7. Njia ambayo mstari wa 43 kwa kawaida umetafsiriwa unafanya uonekane kana kwamba Kristo na mnyang’anyi walikwenda siku ile ile ‘peponi’ Lakini ni dhahiri Ufalme haukuwa umeanzishwa duniani. Hawakwenda katika Ufalme siku ile. Yesu alikwenda kaburini (Mdo 2:32); kama alivyotabiri, alikuwa “siku tatu mchana na usiku katika moyo wa nchi”.(Math 12:40 linganisha 16:21) baada ya kufa kwake msalabalani . Hata baada ya kufufuka alisema “Usinishike; kwa maana sijapaa kwenda kwa Baba”(Yn. 20:17). Basi Yesu hakwenda mbiguni siku alipokufa.

Lakini Yesu anaonekana akimwahidi mnyang,anyi “Leo utakuwa nami peponi”. Jibu kwa utofauti hii inayoonekana inapatikana kwa ukweli wa kwamba katika Kiebrania na Kiyunani asilia aya za Biblia, hakuna kutenga maneno au aya kwa vituo vifaavyo herufi kubwa. Inawezekana kutenga tena maneno kwa vituo na kuweza kusoma “Amini nakuambia leo hivi, utakuwa pamoja nami peponi” (Luka 23:43).Mnyang’anyi alikuwa anamwomba Yesu amkumbuke kwa wema kwenye siku ya hukumu; alijua ya kwamba alihusika kuhukumiwa, naye atatakiwa pale. Lakini Yesu alimpa uhakika wa kushangaza - ‘Naweza kukuambia saa hivi! Usisubiri mpaka wakati huo wa hukumu yangu juu yako- utakuwa pamoja nami katika Ufalme!.

8.Kutokana na vipengele kujulikana hapo juu, yawezekana kutoa orodha ya mafunzo ambayo mnyang’anyi ni dhahiri aliyafahamu:

- Ufalme wa Mungu
- Kuja mara ya pili
- Ufufuo na hukumu
- Wajibu
- Wokovu kwa njia ya Imani iliyo kwa Kristo.
- Ufufuo wa Kristo
- Ukamilifu wa Kristo ("mtu huyu hajafanya lolote baya")
- Haja ya kumfuata Kristo (alimwita "Bwana ")
- Hali ya dhambi ya mwanadamu ("kweli inayo tustahili")

Basi hakuna maana kumtumia mtu huyu kuwa ni udhuru wa kudhania ya kuwa mtu yeyote anaweza kuokoka kama akionyesha kidogo mapenzi kwenye Ukristo; inabidi pawepo msingi wa aina ya mafundisho aliyokuwa nayo. Bila hivi, asingekuwa na uwezo wa kuinuka kufikia imani aliyokuwa nayo. Kristo hakumpa tumaini lolote la wokovu yule mnyang'anyi mwingine, ambaye msimamo wake ulikuwa "Ukiwa ndiwe Kristo jiokoe mwenyewe na sisi". Huyu alikuwa ni mtu aliyesema, "Kama kuna shughuli yoyote kwa huyu Yesu, sioni kwa nini nisipate jambo lingine". Ni kwa sababu alikosa ufahamu wa mafundisho ambayo mnyang'anyi wa pili alikuwa nayo ambapo hakuweza kupata wokovu wa kweli mwishoni mwa siku zake, ijapokuwa mapenzi yake yalikuwa yakipita kwa Kristo.

***Tumeacha kitambo sehemu ya 33: Mfano wa huduma ya Ubatizo***

Ili kutoa wazo lingine la jinsi gani ubatizo unaweza kufanywa vema, ifuatayo ni habari ya huduma ya kubatiza iliyofanywa na Wakristadelfiani wa mjini Hartlepool, Uingereza siku ya Jumapili

mchana Novemba 1990. Walakini, inabidi ieleweke ya kuwa kimsingi ubatizo ni wa kutumbukizwa katika maji kufuatia toba ya kweli na kuiamini Injili. 'Huduma' ni ya hiari sana kutoa maana inayostahili ya umuhimu wa jambo. Mpangilio wa mambo ulikuwa kama ifuatavyo:-

Sala ya kufungua
Somo toka Warumi mlango wa 6

Hotuba fupi ya ubatizo (Yaliochapishwa chini; majina halisi yamebadilishwa)

Sala

Kuzamishwa kwa mtu katika bwawa la kuogelea

sala

**HOTUBA YA UBATIZO**

Hapana shaka kuwa leo ni siku muhimu sana katika maisha ya Deve; kwa muda mchache ataingia ndani ya maji na kusimama mzima "katika Kristo", mzao wa Abrahamu na kuwa na hizo ahadi zenye utukufu ambazo zinafanya Injili aliyoahidiwa.

Mwisho wa jambo hili lililo rahisi kufanywa, laweza kuwa lakudanganya lakini Dave na sisi wote hapa tunaamini ya kwamba huku kutumbukia ndani ya maji kutamuunganisha na mauti na ufufuo wa Yesu, kama tulivyosoma katika warumi mlango wa 6 mst 3-5:

"Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliyobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake? Basi tulizikwa naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, Kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi

tuenende katika Upya wa uzima. Kwa maana kama tulivyounganika naye katika mfano wa mauti yake, kadhalika tutaunganika kwa mfano wa kufufuka kwake".

Kwa muda mfupi hebu tujaribu kufikiri tukio la ufufuo wa Yesu, kwa kuwa tumeona ya kwamba Dave alipopanda juu toka majini ataungana na kufufuka kwa Yesu toka kwa wafu.

Tunaweza kuwaza uzuri na utulivu wa hewa ya usiku, na hisia zenye utukufu wa maisha mapya ndani ya Yesu. Aliweza kuona taa za Yerusalemu zikimeta-meta kwa mbali;watu wa hapo hawakujua kabisa jambo la kushangaza lililokuwa linatokea karibu sana nao-la kwamba mtu alikuwa anafufuka kwa upya wa uzima. Kama Dave anavyotoka katika maji, ulimwengu unaotuzunguka haufahamu jambo lenye utukufu linalotokea; yote wanayoweza kuona, kama wakijali kutazama, ni kundi dogo la wanaume na wanawake wakitembea kuelekea katika bwawa la kuogelea na mtu mmoja akimzamisha mwingine. Lakini kama vile malaika walivyofurahi Yesu alipofufuliwa, basi sasa hatuwaoni, lakini Malaika wanafurahi kwa mtu mmoja anayetubu.

Tumesoma kwa Wrumi 6 ya kwamba tunatakiwa "tutembee katika maisha mapya" -Furaha ambayo Dave atakuwa nayo atakwenda nayo atembeapo kuelekea mbele katika maisha. Kama tulivyosoma hatakuwa mtumwa wa dhambi tena, bali wa Mungu, akifanya mapenzi yake kama yalivyodhihirika katika Biblia. Ni kujitia jaribuni kufikiri kwamba tutataka uhuru wetu wenyewe, lakini kwa kujitumikia wenyewe hatuwi huru, tunakuwa watumwa wa dhambi. Sasa Dave anabadili mambo, kumtumikia Mungu. Kwa wakati itaonekana kwamba vikwazo vinavyoonekana kuishi maisha mapya vinawekwa juu yetu ni vingi mno kuchukua, tunajaribu

kuwa huru navyo. Lakini tukifanya hivyo, hatutakuwa huru, tutakuwa tunatumikia dhambi tena.

Paulo ameeleza katika 1 Kor 10:1,2 ya kwamba kupita kwetu katika maji ya ubatizo ni sawa na Israeli walipopita katika maji ya Bahari ya Shamu. Aina ya mfano unaweza kukuzwa toka huu, pamoja na masomo mengi kwa ajili yetu. Israeli walikuwa watumwa Misri, kuishi maisha yasiyo na maana, wakifanya kazi ngumu katika utumwa wao na kuzitumikia sanamu za Misri. Kwa maisha waliyoyapata wakamlilia Mungu aweze kuwaokoa, ingawa huenda hawakujua ni jinsi gani angewajibu.

Kwa kuwajibu Mungu alimtumia Musa kuwatoa Misri, kupitia Bahari ya shamu na kisha kupita Jangwani, na kuingia nchi ya ahadi. Israel nchini Misri walikuwa kama Dave na wote wanaokuja kwenye ubatizo; sasa Dave ameongozwa kama ilivyokuwa, ufukoni mwa Bahari ya Shamu. Mara akipita katika maji, hatakuwa mara moja katika nchi yenye Ahadi ya Ufalme, ataungana na sisi hapa katika kutembea Jangwani na Malaika, Ambaye daima alikuwa nao mchana na usiku. Basi na sisi, kila mmoja wetu ana Malaika anayetuzunguka, akituongoza katika maisha yetu kuuelekea wokovu (Zaburi 34:7;Ebra 1:14).

Israel walilishwa kila siku kwa mana, ambayo Yesu ameifafanua katika Yohana 6 kuwa ni Neno la Mungu. Kama wasingalikula wangekufa mapema katika Jangwa hilo - hapakuwepo chakula kingine cha kula. Kwa sababu hii kwa nguvu ya kutosha tutaweza kukukabidhi “Mwenza wa Biblia” jedwali la kusoma, ambapo unasoma Biblia kila siku, na kupata habari yote ya maneno unaposoma ndani. Ni muhimu kutenga muda wa taratibu ya kila siku, kwa hiari muda uo huo kila siku, ili kusoma hizo sura na kuzitafakari.

Kwa kupita, Israeli waliambiwa wsijaribu kukusanya mana nyingi kwa siku moja, bali wafanye bidii ya kwenda kuikota kwa kila siku. Kujilisha kwetu Neno inatakiwa kila siku. Na kiasi kama tusivyoweza kusahu kula chakula chetu cha mwili, hivyo kwa Moyo tufanye bidii kujilisha Neno la Mungu; kweli; Ayubu aliweza kusema ya kwamba alithamini maneno ya Mungu "kuliko chakula changu cha kawaida".

Vile vile Israel walikunywa maji ya kijito kilichotiririka toka mwamba uliopigwa:1Kor 10 tumeambiwa kuwa ulikuwa badala ya "Kristo"

Basi tujishibe na kunywa katika mfano wa Yesu, ambao tunaweza kufanya kwa ibada ya kumbukumbu kila juma. Kusema mikutano, iwe ni nia yetu ya kawaida kukutana na wengine wanaoshiriki tumaini letu. Msafiri kwenye jangwa halisi atachukua fursa yoyote ili akutane na msafiri mwingine kwa kujadili matatizo ambayo yapo mbele, na kushiriki yatupatayo. Hivyo sisi katika jangwa la maisha ya ulimwengu huu mbaya tufanye kila juhudi kukutana na kila mmoja wetu. Mara nyingi mikutano hii haiwezekani katika mwili kama tunavyopenda sana, lakini tuchukue kila nafasi ya kuwasiliana kwa kuandikiana waraka, kusoma magazeti ya Biblia n.k

Tumenena juu ya majukumu ya maisha mapya, lakini itakuwa ni kuwaza vibaya ya kwamba kama tukifanya mambo fulani, kama haya ya kusoma Biblia kila siku, ndipo Mungu itambidi atupe thawabu. Ni mapenzi ya Mungu, nia yake, kutupatia Ufalme kama kipawa, na si kama mshahara kwa matendo yetu (Rum 6:23). Itakuwa ni kosa kwetu kudhani ya kwamba ubatizo ni jambo jema kwa kuwa sasa tuna nafasi nzuri ya kuingia Ufalme. Ukweli na

upendo wa Mungu, ushindi wa Kristo, haya yote mawili ndiyo yanayofanya hakika zaidi kuliko hivyo. Mungu kwa kweli anamtaka Dave na sisi sote hapa kuwamo katika Ufalme. Ukweli huu ni wenye utukufu mno ambao yatupasa tujikumbeshe wenyewe mara kwa mara ya kwamba hakika ni kweli katika mwangaza wake tuwe tunafanya aina nyingine ya kuitikia upendo wa Mungu.

Israeli walipovuka Bahari ya Shamu ilikuwepo furaha kubwa. Musa aliimba wimbo wake na watu wote wakafurahi Zaburi 105:35-41 yaeleza vizuri tukio hili, ikionyesha jinsi gani Mungu aligawa kila kitu kilichokuwa lazima kwa ajili ya Safari:-

“(BWANA) akaila miche ya nchi yao ya (Misri). Wakayala matunda ya ardhi yao. Akawapiga wazaliwa wa kwanza katika nchi, malimbuko ya nguvu zao.Akawatoa (Israeli) hali wana fedha na dhahabu, katika kabila zao asiwepo mwenye kukwaa. Misri walifurahi walipoondoka, maana kwa ajili ya hofu imewaangukia. Alitandaza wingu liwe kifuniko, na moto utoe nuru usiku. Walipotaka akaleta kware akawashibisha chakula cha mbinguni. Akaufunua mwamba, kukabubujika maji, yakapita pakavu kama mto”

Furaha ile ni furaha yetu, ndugu na dada zako wa wakati ujao, ambao wapo hapa kushuhudia kubatizwa kwako. Ni furaha ya Mungu, ya Yesu na Malaika ambao kwa mkazo wanatutazama wakati huu. Sisi kila mmoja tuweze kushika Tumaini hili, na kushangilia huku “kwa uthabiti mpaka mwisho”, hata tuweze kutembea pamoja katika ufalme.

***Sasa tunaingia kwenye vyumba vyetu vya kubadilishia nguo, na kisha kuingia katika bwawa la kuogelea…***

**Somo La 10 : Maswali**

1. Je! tunaweza kuokolewa pasipo kubatizwa?

2. Neno ‘ubatizo’ lina maana gani?
   a)Kujitoa
   b)Kunyuziwa maji
   c)Imani
   d)Kutumbukizwa/kuzama katika maji

3. Maana yake nini Ubatizo ulioelezwa kwa Warumi 6:3-5?
4. Ni lini yatupasa tubatizwe?
   a)Baada ya kujifunza Injili ya kweli na kutubu
   b) Tukiwa watoto wadogo
   c) Baada ya kupendezwa/kuvutiwa na Biblia
   d) Tunapotaka kujiunga na kanisa
5. Tunabatizwa katika nini?
   a)Kanisa linalobatiza
   b)Neno la Mungu
   c)Kristo
   d)Roho mtakatifu
6. Jambo gani linalofuata baada ya ubatizo?
   a)Tunakuwa sehemu ya uzao wa Abrahamu
   b)Hatuta tenda dhambi tena
   c)Kwa maana dhahiri tunaokolewa muda wote
   d)Dhambi zetu zinasamehewa
7. Je! ubatizo peke yake unatuokoa?
8. Je! tutapokea vipawa vya miujiza ya Roho Mtakatifu baada ya kubatizwa?

## 11.1 Dibaji

Ubatizo unatupa tumaini la uhakika kuwa na uzima wa milele katika Ufalme wa Mungu. Tunapoamini zaidi na kufahamu uhakika wa tumaini hili, kadri linapokuwa wazi zaidi yanakuwepo majukumu juu yetu. Haya yanazunguka kuishi maisha pande zote ambayo yanafaa mtu aliye na tumaini la kupewa mwili na Uungu (2 Petro 1:4), hasa wa kushiriki Jina lake (Uf 3:12) akiisha kamilishwa kwa kila njia.

Tumekwisha eleza katika Somo la 10:3 ya kuwa baada ya kubatizwa tumejipa sharti la maisha ya kusulubisha daima mawazo mabaya ya mwili wetu (Rum 6:6). Tusipopenda kujaribu kufanya hivi, basi ubatizo hauwi na maana. Yatafanyika tu mara mtu akiwa yu tayari kupokea majukumu ya maisha mapya yatakiwayo kufuata.

Katika Ubatizo tunakufa kwa haya ya kale, njia ya maisha ya asili, na katika mfano tumefufuka na Kristo. "Basi ikiwa mmefufuka pamoja na Kristo (kwa ubatizo), yatafuteni yaliyojuu, Kristo aliko ameketi mkono wa kuume wa Mungu. Yafikirini mambo ya juu, siyo yaliyo katika nchi. Kwa maana mlikufa….. Basi, vifisheni(ueni) ……. uasherati, uchafu, tamaa" (Kolos 3:1-5). Baada ya kubatizwa tunajiweka wenyewe kwenye maisha ya kuangalia mambo yatokanayo na uhusiano wa mbinguni, tukifikiria ya mbinguni (yaani ya kiroho) hayo mambo, tukibadili tamaa yetu ya ulimwengu kwa tamaa ya kutaka kushinda maelekeo ya mwili wetu wa nyama na damu na kwa hiyo kuuingia Ufalme wa Mungu.

Maelekeo ya tabia ya mwanadamu ni kuonyesha shauku ya kumtii Mungu kwa kushika na kuacha. Mara nyingi Mungu

anaonya juu ya tabia hii. Kwa habari ya amri na hukumu Mungu anasema “ambazo mwanadamu ataishi kwazo kama akizitenda” (Ezek 20:21). Kama tukijua amri za Mungu, na kuanza kuzitii katika Ubatizo, tutajiweka maisha yote kuishi kwa utii wa hizo.

### 11.2 Utakatifu

“Mtakatifu, mtakatifu,mtakatifu, ni BWANA” (Isaya 6:3). Mkazo wa tatu pamoja kwa aya hii ni moja ya mafungu mengi ya maneno yanayokaza utakatifu wa Mungu. Kimsingi ‘utakatifu’maana yake ‘kutenga’ pande mbili kujitenga ili kufuata mambo ya Kiroho. Tumetakiwa “kumfuata Mungu,” kama watoto wanaopendwa (Efe 5:1). Kwa hiyo “aliyewaita alivyo mtakatifu ninyi nanyi iweni watakatifu katika mwenendo wenu wote (yaani mwenendo wa maisha); kwa maana imeandikwa, Iweni watakatifu kwa kuwa mimi ni mtakatifu” (1 Petro 1:15-16; Law 11:44).

Israeli wa asili waliitwa toka Misri kwa kubatizwa kwao Bahari ya Shamu na kuwa “taifa takatifu” (Kut 19:6). Baada ya ubatizo wetu, vivyo hivyo washiriki Israeli kiroho wanapokea “mwito mtakatifu” (2 Tim 1:9). Baada ya kubatizwa “tunafanywa watumwa wa ……. Utakatifu” (Rum 6:19,22 na hudhihirisha maana yake).

Utakatifu ni hii sehemu muhimu ya Ukuu wa Mungu, hivyo linabidi liwe jambo kubwa kwa wote wanaojaribu kuwa “wanamfuata Mungu”. Kama tukifanya hivi, tutakuwa “washiriki wa utakatifu wake” tutakapopewa mwili wake (Ebra 12:10; 2 Petro

1:4). Kwa sababu hii pasipo utakatifu katika maisha haya, aaminiye hawezi "kumwona Bwana" (Ebra 12:14)- yaani, hataweza hasa kweli kumwona Mungu na kuungana naye kwa uwiano wake mwenyewe katika Ufalme kama hajaonyesha utakatifu kwa maisha haya.

Huku kupewa tumaini hili kuu maana yake ni kwamba tujitenge toka ulimwengu unaotuzunguka usio na tumaini hili, tukiisha tengwa kwa uzima wa milele wa kushiriki mwili wa Uungu. Basi ' kujitenga' kwetu kusiwe ni jambo fulani tunaloona tumelazimishwa kufanya; kwa ajili ya kujitenga kwetu kwa huu mwito wa juu sana na tumaini, itakuwa ni kawaida tu tunapoona tumetengeka toka mambo ya ulimwengu, unaotawaliwa na mambo ya kimwili.

Sasa tutapima baadhi ya mambo ambayo tuone tumetengeka kwayo, na ndipo katika somo la 11.3 tutajifunza yapi tumetengeka kwa maneno na matendo.

**MATUMIZI YA NGUVU**

Tunaishi katika ulimwengu wenye kutawaliwa na dhambi. Tuliona katika sehemu 6.1 ya kwamba serikali ya wanadamu zinaweza kuitwa 'Ibilisi' kwa kuwa zimetengezwa kuzunguka pande zote matakwa ya mwili, 'Ibilisi' wa Biblia.

Ujumbe wa Biblia uliorudiwa ni kwamba, kwa kifupi, dhambi na uzao wa Nyoka utaonekana kuwa na Ushindi, ambapo baada ya mateso ya kitambo kidogo kwa namna mbalimbali, uzao wa mwanamke hatima yake utahesabiwa kuwa na haki. Kwa sababu hii mwamini ameamriwa daima "Kutoshindana na uovu" (Math 5:39; Rum 12!&; 1Thes 5:15; 1 Petro 3:9).

Tumeona kwamba ubaya mwishoni umeruhusiwa na kuletwa na Mungu (Isaya 45:7; Amosi 3:6 linganisha Somo la 6.1). Kwa kutumika ili kushindana na uovu basi ni kupingana na Mungu. Kwa sababu hii Yesu aliamuru ya kuwa sisi kimwili tusishindane na nguvu ya uovu: "lakini akupigayeshavu la kuume mgeuzie na la pili. Na mtu atakaye kukushitaki, na kuitwaa kanzu yako, mwachie na joho pia" (Mathayo 5:39,40). Kwa jambo hili Kristo ni mfano "Naliwatolea wapigao mgongo wangu…." (Isaya 50:6).

Maneno ya Kristo yanaunga pamoja atakaye kukushitaki na shughuli za ulimwengu zinapopingana na aaminiye. Kufanya hivi ni mfano mkubwa wa kupinga uovu, nao hautafanywa na awaye yote aliye na imani thabiti katika ahadi ya Mungu ya kwamba "Kisasi ni juu yangu; mimi nitalipa anena Bwana" (Rum 12:19). "Usiseme, mimi nitalipa mabaya; Mngojee Bwana, naye atakuokoa" (Mithali 20:22 linganisha Kum 32:35). Kwa sababu hii Paulo aliwakaripia wazi Wakoritho kwa kuwapeleka wengine kwenye sheria (1 Kor 6:1-7).

Kwa mtazamo wa ukuu wa tumaini letu, hatutajihusisha sana na maisha ya sasa yasiyo na haki: "Je! mtu wa kwenu akiwa ana daawa juu ya mwenzake athubutu kushitaki mbele ya wasio na haki …… Au hamjui ya kwamba watakatifu watahukumu ulimwengu?" (1 Kor 6:1,2). Kuwapeleka wengine kuwashitaki, ikiwa ni kugombea kiwanja au mambo ya talaka, basi liwe ni tendo lisilokuja akilini kwa mwamini wa kweli.

Ili kukomesha nguvu za ubaya, sawa sawa (katika masuala mengine) kwa kuweka watu wabaya katika uweza, jeshi na nguvu za polisi zinatumika na serikali za wanadamu. Hizi ni desturi zilizowekwa kupinga uovu, kwa hiyo mwamini wa kweli asizishiriki hizo. "Wote washikao upanga, wataangamia kwa huo

upanga (Math 26:52). Hili ni jambo la Mungu la awali kabisa linalorudia "Atakayemwaga damu ya mwanadamu (kwa kusudi), damu yake huyo itamwagwa na mwanadamu: maana kwa mfano wake Mungu alimfanya mwanadamu" (Mwanzo 9:6). Jeuri yoyote ya makusudi juu ya ndugu yetu mwanadamu ni kumfanyia jeuri Mungu, ila akiruhusu.

Chini ya utumishi wa Kristo, tumeambiwa, "Wapendeni adui zenu, waoombeeni wanaowaudhi, watendeeni mema wale ambao wawachukia ninyi" (Math 5:44; Lk 6:27). Nguvu za kijeshi na Polisi zinashughulika na kupingana moja kwa moja na mambo haya na kwa hiyo mwamini wa kweli atajiepusha yote kujiunga nao. Hata kama si moja kwa moja kuhusika katika kutenda jeuri, kufanya kazi katika Taasisi hizi au kujihusisha katika ajira zilizoungana nazo, ni dhahiri haushauriwi; hakika, ajira yeyote inayofuatana na kutoa kiapo cha kutii mamlaka hizi, hutuondolea uhuru wa dhamiri ya kutii amri za mwenyezi Mungu. Waamini wa kweli basi siku zote ni wenye bidii kufanya vyema yote yapasayo kukataa shughuli za jeshi na kutumikia Polisi kwa namna yeyote , ingawa siku zote wanapenda kutumia ajira ya hiari katika nyakati shida za taifa ambazo zitawafaidisha kupata vitu ndugu zao wanadamu.

**SIASA**

Kufahamu wazi, na kuwa na imani thabiti katika Ufalme wa Mungu ujao maana yake ni kwamba tutatambua ya kwamba serikali ya mwanadamu haiwezi kuleta ukamilifu. Kujihusisha kokote katika siasa za wanadamu basi hakuelekeani na tumaini la Ufalme. Yesu alitabiri ya kwamba mambo yataharibika toka kwenye ubaya hadi ubaya zaidi katika "siku za mwisho" kabla ya kuja kwake (Luka 21:9-11,25-27). Haiwezekani kuamini maneno yake na wakati uo huo kujaribu kustawisha nafasi ya ulimwengu

kupitia tawala za wanadamu au kusaidia matokeo. Maono ya Msamaria mwema unaonyesha jinsi gani Mkristo atasaidia mazingira ya ulimwengu - kutenda mema kwa watu wote kadri tupatavyo nafasi (Gal. 6:10).

Taarifa ya waamini wa kwanza inawaonyesha walijitoa kuishi maisha ya kiroho katika kutazamia kurudi kwa Kristo, zaidi wakidhihirisha kuhusika kwao na mazingira ya ulimwengu kwa kuhubiri kwao. Hakuna taarifa ya kuhutubia kwao jamii, uchumi na matatizo ya utawala wa ulimwengu uliowazunguka.

“Kuelekeza hatua zake si katika uwezo wa mwanadamu” (Yer 10:23); kufahamu ubaya mkubwa na uovu wa mwili wa mwanadamu maana yake ni kwamba tutatambua ya kuwa uongozi wa mwanadamu haufai kwa watu wa Mungu. Kwa hiyo kupiga kura hakupatani na huu ufahamu. Aliye juu ndiye anayemiliki katika Ufalme wa mwanadamu, naye humpa amtakaye, awaye yote” (Dan 4:32). Hawa watawala wamepewa uwezo wa mwisho na Mungu (Rum 13:1); basi kupiga kura katika mfumo wa kidemokrasia kunafuatana na upigaji kura juu ya mtu ambaye Mungu amemchagua kuwa katika mamlaka. Hivyo imetolewa taarifa ya kwamba Mungu alimpa mataifa fulani yawe katika mkono wa Nebukadreza mfalme wa Babel (Yeremia 27:5,6).

Kwa sababu ya kutambua kwetu ya kuwa Mungu ametia mataifa mikononi mwa viongozi wao, tuwe waangalifu sana na kuwa raia walio kama mfano, tukikaa na kuheshimu sheria za nchi tunamoishi, ila zikihitilafiana na sheria za Kristo. “Kila mtu na atii mamlaka iliyo kuu… na ile iliyopo imeamriwa na Mungu….. kwa sababu hiyo lipeni kodi…. Wapeni wote haki zao; mtu wa kodi, kodi…. Astailiye heshima, heshima” (Rum 13:1-7)

Kujihusisha kwa jumuiya zinazoitwa za Kikristo katika mifano ya makatazo ya kisiasa na kususia kulipa kodi basi ni ishara inayoonyesha kusoma kwao kwa kutoangalia mambo haya yenye msingi wa Biblia. Lakini, mfano wa Petro kuendela kumhubiri Kristo alipokatazwa na mamlaka kufanya hivyo, ni kuonyesha ni jinsi gani tunaweza tu kutii amri za mwanadamu zisipoleta utata na amri za Kristo: "Kwamba ni haki mbele za Mungu kuwasikiliza ninyi kuliko Mungu, hukumuni ninyi wenyewe" (Matendo 4:17-20; 5:28,29).

Msimamo wa Kristadelfiani kwa lazima ya kutotumikia jeshi katika miaka ya karibu huu ni mfano mwingine.

**ANASA ZA ULIMWENGU**

Kwa ajili ya kukosa uhusiano wa kweli na Mungu na tumaini la kweli la kipindi kijacho, ulimwengu umevumbua mifano isiyohesabika ya kutafuta kujifurahisha. Wale watafutao kuupendeza mwili waepukwe na wale wanaojaribu kuendeleza nia ya roho. "Mwili hutamani ukishindni na roho, na Roho hushindana na mwili" (Gal 5:17). Kwa sababu ya upinzani huu mkubwa, haiwezekani kufikiri kwamba tunaweza kwa halali kuruhusu mwili na vile vile kudai kuifuta Roho.

Ulimwengu umeundwa kuzunguka pande zote kwa "tamaa za mwili, tamaa ya macho, na kiburi cha uzima" (1 Yoh 2:16). "Basi yeyote ajifanyae kuwa rafiki wa ulimwengu huwa adui wa Mungu" (Yak 4:4). Kuwa na marafiki wa ulimwengu, kutazama picha za filamu za ulimwengu n.k. ni kuwa "rafiki wa ulimwengu". Matakwa ya ulimwengu yatapita mapema, na wale ambao wamejiweka upande wa ulimwengu katika maisha haya watapita na dunia (1 Yoh 2:15-17). "Dunia au ulimwengu (yaani, jamii) ya waovu" itaangamia kwa kuja mara ya pili (2 Petro 2:5), kwa kuwa

“dunia yote hukaa katika uovu” (1 Yoh 5:19). Ikiwa tunataka kuepuka uharibifu huo, yatupasa “tusiwe wa ulimwengu” (Yn. 17:16 linganisha Uf 18:4).

Njia nyingi za ulimwengu za kuufurahisha mwili zafuatana na kufanya hivyo kwenye gharama za afya ya mwili; uvutaji tumbaku, madawa ya kulevya na kunywa pombe kiasi kikubwa hii ni mifano. Afya yetu ya mwili, pesa zetu, hakika yote tuliyonayo kwa kweli ni mali ya Mungu. Kwa sababu hii hatuna uhuru wa kutumia mambo haya kama tutakavyo, bali yatupasa kutenda kazi ya uwakili wa kile alichotupatia Mungu. Tutatakiwa kutoa hesabu ya jinsi tulivyotumia hivyo vitu kwenye kiti cha hukumu (Luka. 19:12-26). Haya mazoea kama uvutaji sigara na unywaji pombe ni matumizi mabaya kwa pande mbili, fedha zetu na afya . “Hamjui ya kuwa ninyi mmekuwa hekalu la Mungu, na ya kuwa Roho wa Mungu anakaa ndani yenu?. Kama mtu akiliharibu hekalu la Mungu, Mungu atamharibu mtu huyo….. maana mlinunuliwa kwa thamani: sasa basi, mtukuzeni Mungu katika miili yenu” (1 Kor 3:16,17; 6:19,20). Matumizi mabaya ya mwili kwa mazoea kama uvutaji kwa sababu hii ni jambo si la mchezo.

Walakini, inaeleweka ya kuwa ikiwa mazoea haya yalifanywa kabla ya kuongoka, itakuwa vigumu kuyaacha mara moja. Kinachotegemewa ni kutambua ubaya wa tabia hii, na juhudi ya kweli kuiacha. Mkazo wa maisha kuongezeka unatakiwa ukabiliwe kwa kukimbilia Neno la Mungu na sala, kuliko kulegezwa na namna yoyote ya mwanadamu.

## 11.3 Maisha ya kikristo yenye Matendo

### KUJIFUNZA BIBLIA

Baada ya kubatizwa, tuishi maisha ya kuzaa "tunda la utakatifu", tukiishi maisha yanayoongozwa na Roho kuliko mwili (Rum 6:22; 8:1; Gal 5:16,17). Ni kwa kukaa neno la Mungu ndani yetu ndipo tunazaa tunda la Roho (Yon. 15:7,8). Tumeona kwamba tumeongozwa na Roho katika maana ya kwamba Roho ya Mungu imo katika Neno lake. Katika maisha yetu yote yatupasa kuwa karibu na Neno hilo kwa kujifunza na kusoma Biblia kila mara.

Kujifunza kwa kuwaza Neno la Mungu matokeo ni mtu kutambua haja ya kubatizwa na kwa sababu hiyo akionyesha tendo hilo. Hii njia ya kuruhusu Neno livute matendo yetu na kuongoza maisha yetu iendelee; lakini ubatizo ni hatua ya kwanza katika maisha yetu ya kutii Neno la Mungu. Kweli kuna hatari sana kuwa na mazoea na Biblia pamoja na mafunzo ya msingi wa Injili, ya kutupeleka kwenye hali ambayo, ndani yake Neno haliwi na ushawishi kwetu tena: tunaweza kusoma nayo yakawa hayana matokeo ya maana juu yetu (tazama yaliyotiwa mwishoni mwa kitabu sehemu ya 2).Kwa sababu hii ni busara kuomba sala fupi kabla ya kila somo la kila Maandiko: "Unifumbue macho yangu niyatazame maajabu yatokayo katika sheria yako" (Zab 119:18).

Neno la Mungu liwe chakula chetu cha kila siku kwa kweli, utegemezi wetu juu yake, na kulitamani, nia yetu iwe kubwa kuliko silika yetu ya hamu ya chakula cha mwili: "Nimeyatunza maneno ya kinywa chake zaidi ya riziki yangu" ilikuwa hisia ya Ayubu (Ayubu 23:12). Vivyo hivyo Yeremia: Maneno yako yalionekana nami nikayala: na maneno yako yalikuwa ni furaha kwangu, na shangwe ya moyo wangu" (Yer 15:16). Kutenga muda wakati wa kila siku kwa ajili ya utaratibu wa kusoma Biblia ni jambo la

muhimu, basi kutengeza katika maisha yetu ya kila siku ni mfano mzuri wa kuigwa. Dakika 30 za bila kukatiza kujifunza biblia likiwa ni jambo la kwanza asubuhi linaelekea kutuanzisha kila siku katika mwendo sahihi wa kiroho. Imani hii inayofanya mazoea itakuwa yenye thamani kwa uzito wao wa dhahabu katika siku ya hukumu.

Kwa kuepuka maelekeo ya mwili kwa kusoma sehemu hizo za Maandiko ambazo kwa kawaida zinatuvuta macho, Kristadelfiani wamevumbua mpangilio wa kusoma uitwao "Mwenza wa Biblia" (hupatikana kwa wachapishaji wa kitabu hiki). Huu mpangilio unatupata idadi ya sura za kusoma kwa kila siku, ukisababisha kusoma katika Agano Jipya mara mbili na Agano la kale mara moja katika mwendo wa mwaka. Tunaposoma sura siku kwa siku, tunaweza kujipa moyo toka wazo ambalo maelfu ya waamini wengine wanasoma sura zizo hizo. Popote tunapokutana, basi tuna kiungo cha karibu sana; sura ambazo tumekuwa tukisoma kwa karibu ndizo zinafanya msingi wa mazungumzo yetu.

**SALA**

Mazoezi mengine muhimu kukuza ni hayo ya sala. Tukiisha kumbushwa ya kwamba yupo "mpatanishi mmoja kati ya Mungu na wanadamu, mwanadamu Kristo Yesu; aliyejitoa mwenyewe kuwa fidia kwa wote" Paulo anaagiza sana kwa kina kufahamu kazi ya Kristo: "Basi, nataka wanaume wasalishe kila mahali…… pasipo hasira wala majadiliano" (1 Tim 2:5-8). "Kwa kuwa hatuna kuhani mkuu asiyeweza kuchukuliana nasi katika mambo yetu ya udhaifu, bali yeye alijaribiwa sawasawa na sisi katika mambo yote, bila kufanya dhambi. Basi natukikaribie kiti cha neema kwa ujasiri, ili tupewe rehema, na kupata neema ya kutusaidia wakati wa mahitaji" (Ebr 4:15,16).

Tukifahamu ukweli wa kwamba Kristo ni kuhani mkuu wetu wenyewe wa kutoa maombi yetu yenye nguvu mbele za Mungu, huu unatuvuvia kwa desturi kuomba kwa imani. Ingawa hivyo, ombi lisiwe tu na 'orodha ya mahitaji' ya kumpa Mungu; kutoa shukrani kwa ajili ya chakula kabla ya milo, kwa ajili ya kulindwa safarini n.k haya yatafanywa kuwa sehemu muhimu ya maombi yetu.

Kuweka shida zetu mbele za Bwana katika sala iwe ndani yake yenyewe, inatoa maana kubwa ya amani: "Katika kila neno (hakuna lilo dogo mno kuombea) kwa kusali…. na kushukuru, haja zenu na zijulikane na Mungu. Na amani ya Mungu, ipitayo akili zote, itawahifadhi mioyo yenu na nia zenu" (Wafilip 4:6,7).

Ikiwa maombi yetu yanakuwa sawa na mapenzi ya Mungu, hakika kweli yatajibiwa (1 Yoh 5:14). Tunaweza kujua nia ya Mungu tunapojifunza kwa kusoma Neno lake, linalofunua Roho/nia yake kwetu. Kwa hiyo somo letu la Biblia litufundishe sehemu mbili, jinsi ya kuomba na jambo gani liombewe, yafanywe hivi maombi yetu ya nguvu. Basi "…. Maneno yangu yakikaa ndani yenu, ombeni mtakalo lote nanyi mtatendewa" (Yoh 15:7). Kuna mifano mingi ya kuomba sawa sawa katika maandiko (Zab 119:164; Dan 6:10). Asubuhi na jioni, kwa maombi machache mafupi ya kutoa shukrani wakati wa mchana yataonekana kama yanafunua kidogo sana.

**KUHUBIRI**

Moja ya majaribu makubwa yanayozuka toka kumjua Mungu wa kweli ni kuwa mbinafsi kiroho. Tunaweza kutosheka mno na uhusiano wetu tulionao na Mungu, kujishughulisha sana katika kusoma kwetu wenyewe Biblia na kwa kiroho, hata tunaweza

kuacha kushirikiana mambo haya na wengine-pande mbili ndugu waaminio na ulimwengu unaotuzunguka. Neno la Mungu na Injili ya kweli inayopatikana ndani yake, imelinganishwa na nuru au taa iwakayo gizani (Zab 119:105; Mithali 4:18). Yesu alieleza wazi kwamba hakuna mtu aliye na nuru hii halafu akaiweka chini ya kiango bali huionyesha kwa watu wote (Math 5:15). "Ninyi ni nuru ya ulimwengu" kwa sababu ya kubatizwa katika Kristo, "aliye nuru ya ulimwengu" (Math 5:14; Yoh 8:12). "Mji hauwezi kusitirika ukiwa juu ya mlima" Yesu aliongea (Mathayo 5:14).

Kama kweli tunaishi maisha ya kulingana na Injili ya kweli tunayoifahamu, 'utakatifu' wetu utakuwa dhahiri kwa hayo tuishiyo. Hatutaweza kuugeuza ukweli ambao umetufanya 'tujitenge' kwa ajili ya tumaini la Ufalme, na vile vile 'tumejitenga toka' njia za watu wa ulimwengu.

Kwa njia yenye busara, tutataka kushirikiana maarifa yetu ya kweli ya Mungu na wale wote tunaokutana nao: mazungumzo yakigeukia kuzunguka mambo ya Kiroho; kujadili mafundisho ya washirika wa makanisa mengine, tukigawa vitabu kidogo vyenye mafunzo ya dini, na hata kuweka matangazo madogo kwenye magazeti ya mahali maalum, haya yote ni njia ya kutuwezesha nuru yetu iangaze. Hatuta waza ya kwamba tunaweza kuiacha kazi ya kushuhudia kwa waamini wengine; sisi kila mmoja anao wajibu wa kufanya kazi ya kushuhudia neno. Kwa kulinganisha, Kristadelfiani wametunga hatua za kwanza chache zenye kipimo kikubwa cha kuhubiri mbali kabisa na makundi mengine. Sisi sote kila mtu mmoja mmoja, anaweza kufanya anacho weza, zaidi kwa gharama zetu wenyewe.

Moja ya njia zenye mafanikio zaidi katika kuhubiri ni kwa kueleza imani yetu kwenye jamii yetu na hao ambao kwa karibu

sana tunakutana nao. Hao walio na mapenzi wasio katika imani ni wazi wataeleza imani yao kwao, ingawa mara hii kazi ikiisha fanywa sio busara kuendelea kuzusha hizi habari au kutoa mkazo wowote juu yao. Waongofu waliosongwa si ambao Mungu awataka. Jukumu letu ni kuishuhudia kweli pasipo jambo la kuchelewa kuhusu idadi ya wanaoitikia. Tuna wajibu mkubwa wa kushuhudia huku (Ezek 3:17-21); kama Kristo anakuja wakati tukiwa na uhai wetu "watu wawili watakuwa shambani; mmoja atatwaliwa, mmoja ataachwa" (Luka 17:36). Hakika itakuwa ajabu ikiwa hatukusema mbele ya jamii yetu na wafanyakazi wenzetu juu ya kuja mara ya pili Bwana wetu linapokea hili.

**UHAI WA IKLEZIA**

Mpaka hapa katika Somo hili tumenena majukumu yetu wenyewe kiroho. Lakini, tunao wajibu wa kukutana pamoja na wengine wanaoshiriki tumaini letu. Tena, hili liwe ni jambo lingine ambalo yatupasa kufanya. Tumeeleza ya kwamba baada ya kubatizwa tumeingia kuanza safari ya Jangwani kuelekea kwenye Ufalme. Basi ni jambo la kawaida ya kwamba tutataka kukutana na wasafiri wenzetu. Tunaishi siku za mwisho kabla ya kuja Kristo; ili kuyashinda majaribu yenye sehemu nyingi na kutatiza yanayotusumbua nyakati hizi, tunahitajika kushirikiana na hao walio katika maono yayo hayo: "Tusiache kukusanyika pamoja …… bali tuonyane: kwa kadiri mwonavyo siku ile kuwa inakaribia (ya kuja mara ya pili)" (Ebra 10:25 linganisha na Mal. 3:16). Kwa hiyo waamini watafanya kila juhudi ili kukutana na kila mwingine kwa nyaraka na kusafiri ili kukutana na mwingine kushiriki kujifunza Biblia, ibada ya ushirika, na shughuli za kuhubiri.

Sisi sote kila mtu 'tumeitwa kutoka' ulimwenguni tuingie katika tumaini kuu la Ufalme. Neno 'mtakatifu' maana yake 'mtu aliyeitwa atoke', wanaweza kutajwa wote waamini wa kweli kuliko

waamini wachache tu walio mashuhuri wa zamani. Neno la Kiyunani ambalo limetafsiriwa ‘kanisa’ katika Biblia ya kiswahili ni ‘Iklezia’, maana yake ‘kusanyiko la walioitwa au alikwa’, yaani, waaminio. Kwa hiyo ‘Kanisa’ linatajwa kundi la waaminio, wala si jengo ambalo wanakutana humo. Kuepuka kutolewa tumizi la neno hili, Kristadelfiani wamelekea kutaja ‘makanisa’ yao kuwa ni ‘ma-Ikelezia’. Popote palipo na idadi ya waaminio katika eneo la mji fulani, ni jambo la maana kama wakipata eneo la kukutania mara kwa mara. Sehemu hii inaweza kuwa ndani ya nyumba ya aaminiye au katika ukumbi wa kukodi. Maklezia ya Kristadelfiani wanakutana ulimwenguni pote katika maeneo kama ya vituo vya jamii, vyumba vya mikutano katika hotel, kumbi za kujenga wenyewe au katika nyumba binafsi. Shabaha ya Ikelezia ni kujenga washiriki wake kwa watu kukusanyika pamoja kujifunza Biblia, vile vile kwa watu wote pamoja kuushuhudia ulimwengu kwa kuifanya nuru yao iangaze kwa kuhubiri. Taarifa ya mfano wa Iklezia la Kristdelfiani yaweza kuwa na jambo fulani kama hivi :-

| | | |
|---|---|---|
| JUMAPILI | saa 5 Asubuhi | Ibada ya kumega mkate |
| | saa 11 Jioni | Kazi ya watu wote kuhubiri. |
| JUMATANO | saa 10 Jioni | Kujifunza Biblia. |

Iklezia ni sehemu ya jamaa ya Mungu. Kwa jumuiya yoyote iliyoungana karibu, kila mshirika anahitajika kuwa msikivu na mtiifu kwa wengine; Kristo mwenyewe alikuwa mfano mkubwa kwa jambo hili. Mbali ya ukuu wake dhahiri kiroho alitenda kazi kama “mtumishi wa wote”, akawatawadha wafuasi wake miguu wakati waliposhindana miongoni mwao kama ni nani alikuwa mkubwa kati yao. Katika jambo hili Yesu ametuagiza kufuata mfano wake (Yn. 13:14,15; Math 20:25-28).

Sasa kama vipawa vya miujiza ya Roho Mtakatifu viliondolewa, hakuna mahali pa 'wazee' kama ilivyokuwa katika kanisa la kwanza; "maana mwalimu wenu ni mmoja, nanyi nyote ni ndugu" (Math 23:8). Basi, Kristadelfiani wanaitana kila mtu na mwenzake "ndugu (kaka)au dada" bila kujali kuwa katika kuitana kwa kwanza kunako tofautisha nafasi zao kwa maisha haya kusema hivi, ni dhahiri kwamba kutakuwa na heshima kwa wamino waliomjua Mungu wa kweli kwa miaka mingi, au ambao wamepevuka kwa upesi katika mambo ya kiroho kwa kujiweka kwao katika Neno la Mungu. Ushauri wa waamini kama hivi utathaminiwa mno na wale watafutao kufuata Neno la Mungu. Ingawa hivyo, watachukua ushauri tu wa waumini wengine kwa upana huo kama ilivyo tafakari ya Neno la Mungu.

Fundisho linalotolewa katika Iklezia ni bayana msingi wake uwe juu ya neno la Mungu. Wale ambao wananena wazi ndani ya Iklezia kwa hiyo wanarudisha nuru ya Mungu, wakisema kwa niaba yake. Kwa kuwa Mungu ni wa kiume, kwa sababu hiyo ni ndugu pekee watafanya kazi ya kufundisha wazi toka neno la Mungu. Waraka wa 1 Kor 14:34 uko wazi; "Wanawake na wanyamaze katika Kanisa; maana hawana ruhusa kunena". Waraka wa 1 Tim 2:11-15 unafuatilia sababu hii kurudi nyuma hadi katika bustani ya Edeni; kwa kuwa Hawa - Eva alimfunza Adamu kutenda dhambi, sasa mwanamke asimfundishe mwanamume. Ni kweli Mungu alimuumba Adamu kabla ya Hawa ikiwa ni ishara ya kuwa "kichwa cha mwanamke ni mwanamume" (1 Kor 11:3), kwa hiyo mwanamume amwongoze mwanamke kiroho vile vile.

Kwa sababu ya mambo yote haya, "Mwanamke na ajifunze katika utulivu akitii kwa kila namna. Simpi mwanamke ruhusa ya kufundisha, wala kumtawala mwanamume, bali awe katika utulivu. Kwa maana Adamu ndiye aliyeumbwa kwanza, na Hawa baadaye.

Wala Adamu hakudanganywa,ila mwanamke alidanganywa kabisa akaingia katika hali ya kukosa. Ijapokuwa ataokolewa katika (Kiyunani 'kwa') uzazi wake kama wakidumu katika imani na upendo na utakaso, pamoja na moyo wa kiasi" (1 Tim 2:11-15)

Kutokana na hii ni dhahiri kwamba Biblia inaweka wazi kazi fulani zilizotengeka kwa wanaume na wanawake waaminio. Wanawake wakiwa wameamuriwa katika masuala fulani "kuolewa, kuzaa watoto, wawe na madaraka nyumbani" (1 Tim 5:14), yaonyesha kwamba shughuli zao za kujitahidi kiroho ni hizo za nyumbani. Kwa hiyo kazi ya wazi katika Iklezia ameachiwa mwanamume. Hii inapingana vikali kwa mawazo ya kibinadamu ya usawa kwa mwanamke na mwanamume, kwa maisha anayoishi mwanamke anaweza kudai usawa na mumewe kwa kila namna, kutokana na kusimamia habari za gharama kwa jamaa hadi nguo za kuvaa wote. Kuzaa watoto kumeonekana kutumika isivyofaa, ambapo imeonekana kama lazima kwa kulinda mawazo mengine ya akili timamu katika anasa kabisa na uchoyo wa ulimwengu. Waumini wa kweli watajiepusha na roho ya kipindi hiki, ingawa, kama siku zote, kupambanisha baina ya vitu viwili ni kwa lazima.

Mume haimpasi kuwa mtawala mkuu juu ya mkewe, bali kumpenda kama Kristo alivyotupenda (Efe. 5:25).

"Waume, kaeni na wake zenu kwa akili (yaani, mtendee mke kwa busara kulingana na jinsi ulivyoelimika katika Neno la Mungu); na kumpa mke heshima, kama chombo kisicho na nguvu; na kama warithi pamoja wa neema ya uzima" (1 Petro 3:7)

Kwa maneno ya kiroho, kubatizwa katika Kristo kunamfanya mwanaume na mwanamke kuwa sawa (Gal 3:27,28 linganisha 1 Kor.11:11). Lakini hii haidhuru, jambo kuu bayana ni kwamba

‘Mume ni kichwa cha mwanamke’ (1 Kor 11:3) katika maana na mambo ya kiroho, pande zote mbili ndani ya jamaa na Iklezia.

Ili kuonyesha kutambua jambo hili, muumini aliye mwanamke atavaa kitu cha kufunika kichwa popote ndugu akifundisha Neno la Mungu. Hii ina maana kwa desturi ya kwamba kofia au kitambaa cha kichwani kivaliwe wakati wote wa mikutano ya Ikelezia. Tofauti ipasayo kati ya mwanaume na mwanamke utatiwa mkazo kwa namna wanaume na wanawake walivyo na nywele (1Kor. 11:14,15). “Kila mwanamke asalipo, au….. bila kufunika kichwa, yuaibisha kichwa chake (yaani, mumewe mst 3) kwa maana ni sawa sawa na yule aliyenyolewa. Maana mwanamke asipofunikwa na akatwe nywele; au ikiwa ni aibu mwanamke kukatwa nywele zake au kunyolewa, na afunikwe…. Kwa hiyo imempasa mwanamke awe na dalili ya kumilikiwa kichwani” (1 Kor 11:5,6,10).

Akiwa na kichwa “kisichofunikwa” ni “kana kwamba amenyolewa”, yaonyesha ya kwamba kichwa kisicho funikwa ni kichwa kisicho na nywele. Kwa hiyo kichwa “kilichofunikwa” si kilicho na nywele bali ni kile ambacho kwa kufahamu kina mfuniko juu yake. Pasipo kufunikwa kichwa mwanamke hawezi kutegemea kufunikwa na nywele zake za asili; kufanya hivi ni kana kwamba hana nywele mbele za Mungu. Ni kosa kwa mwanaume kufunika kichwa (1 Kor 11:7); hii haitaji kuwa na nywele, bali kufunikwa kichwa kwa namna yake maalum.

Katika malezi ya mazingira ya nyakati za Agano Jipya, nyakati pekee mwanamke aliponyolewa nywele zake zilikuwa kama alidhihirika kuwa mzinzi au muasherati, au kama alikuwa amefiwa na mumewe. Maana mwanamke akinyolewa ataonyesha amempoteza au amemkana mumewe -yaani, Kristo, kimfano.

Mwanamke anawakilisha Ikelezia, wakati mwanamume anamwakilisha Kristo. Kama itupasavyo kufanya uamuzi wa akili ili dhambi zetu zifunikwe na Kristo, basi mwanamke yampasa kufanya uamuzi wa kufunika kichwa chake. Kutumaini kufunikwa na nywele zake za asili ni sawa sawa na kutumaini haki yetu wenyewe kujiokoa kama inavyopingana na hiyo ya Kristo.

Kwa kuwa nywele ndefu za mwanamke "ni utukufu wake (aliopewa na Mungu); kwa sababu amepewa zile nywele ndefu ili ziwe badala ya mavazi (1 Kor 11:15), mwanamke atafuga nywele zake kwa jinsi mkazo uliotiwa ili kutofautisha kati ya mwanaume na mwanamke. Tofauti kati ya mtindo wa nywele za kiume na kike utumike na mwanamke kama nafasi inayojitokeza kuonyesha wajibu wake.

Kwa mambo haya ya mwanamke kuwa na nywele ndefu na kufunika kichwa, yatupasa kuwa makini kwa kutofanya mambo haya kama watu wa ishara tupu. Ikiwa dada kweli yu kiroho na ana mwenedo wa utii (linganisha 1 Petro 3:5), atajitiisha chini ya kaka kama waamini walivyo kwa Kristo, atafurahi kuonyesha ya kwamba ni mtiifu kwa kila hali, ikijumuisha kufunika kichwa. Ikiwa hoja ya amri hizi imeeleweka, kama maagizo yote ya Mungu, ndipo hatutakuwa na kutotaka kuzikubali.

Siku zote ipo kazi kwa ajili ya dada ndani ya Ikelezia - kufundisha shule ya Jumapili (Sunday school), na mwenye wajibu wakukaribisha wageni usiohusisha kufundisha watu au kunena, k.m. kutunza mahesabu. Wanawake waliopevuka kiroho wanaweza kutiwa moyo na kuendesha baraza la wanawake, vijana (Tito 2:3,4 linganisha Miriamu akiongoza wanawake wa Israeli Kut. 15:20).

**KUMEGA MKATE**

Pamoja na kusali, kusoma Biblia, desturi ya kutii amri ya Kristo ya kumega mkate na kunywa divai kwa kukumbuka dhabihu yake ni muhimu. " Fanyeni hivi kwa ukumbusho wangu" Yesu aliagiza (Luka 22:19). Ilikuwa ni nia yake kuwa wafuasi wake watafanya hivi mara kwa mara hata ajapo mara ya pili, Yesu atakaposhiriki mkate na kunywa divai pamoja nao (1 kor. 11:26; Luka 22:16-18).

Mkate ni mfano wa mwili wa Kristo uliotolewa msalabani, na divai ni damu yake (1 Kor 11:23-27). Waumini wa kwanza wanaonekana walishika ibada hii mara nyingi (Mdo. 2:42,46), mara moja kwa wiki (Mdo. 20:7). Kama kweli tunampenda Kristo, tutatii maagizo yake (Yoh.15:11-14). Ikiwa tuna uhusiano wa kweli naye, itakuwapo haja ya kukumbuka dhabihu yake kama alivyotaka, na kwa sababu hiyo tutajitia nguvu wenyewe sisi kwenye wokovu aliotimiza kwa ajili yetu. Kipindi cha kutulia wakati wa kuwaza juu ya mateso yake msalabani kitafanya majaribu yetu wenyewe yafifie na kuwa hayana maana yanapolinganishwa na hayo ya Bwana wetu.

Kimsingi kumega mkate ni ibada ya ukumbusho, hakuna muujiza unaotokea kwa matokeo ya kuifanya hii ibada. Ni sawa sawa na Pasaka iliyofanywa chini ya Torati ya Musa (Lk 22:15; 1 Kor 5:7,8). Hii ilikuwa ni njia ya kukumbuka wokovu mkuu wa kutoka Misri ambao Mungu aliutenda kwa mkono wa Musa penye Bahari ya Shamu. Ibada ya kumega mkate inatukumbusha wokovu kutoka katika dhambi kwa njia ya Kristo, ambao umefanikishwa msalabani na uliotuunganisha na Ubatizo. Basi kushika amri hii kwa kawaida iwe ni desturi kufanya ukumbusho.

Kutwaa mkate na divai, kimwili kunafanya upendo wa Kristo kwetu na kwa kweli mambo yote yanayohusu wokovu wetu, huja vivi hivi kuwa ya kweli mara nyingine tena. Kumega mkate kwa karibu mara moja kwa juma basi ni dalili ya kuwa na hali ya afya kiroho. Ikiwa mtu hawezi kuhudhuria ibada hii na waumini ndugu wa Kweli, ifanywe hata akiwa pekee yake. Hakuna udhuru unaoruhusiwa kutuzuia kutunza/ kutimiza amri hii. Tufanye kila jitihada kuwa na mkate na divai kwa ajili ya ibada, ingawa katika mambo mbalimbali hata vikikosekana vitu hivi hatutazuiwa toka kumkumbuka Kristo kwa njia iliyowekwa kwa kadri tuwezavyo. Yesu alitumia "tunda la mzabibu" (Luka 22:18), basi nasi tutumie divai ya zabibu nyekundu.

Kuchukua vitu ambavyo ni mfano wa mateso ya Kristo na dhabihu ni heshima ya juu zaidi ambayo mwanamme au mwanamke aweza kuwa nayo. Kuvishiriki isivyostahili kwa namna inavyoonyesha ni sawa na kukufuru, kwa "maana kila mlapo mkate huu na kukinywea kikombe mwaitangaza mauti ya Bwana….. kila aulaye mkate huo, au kukinywea kikombe hicho cha Bwana isivyostahili, atakuwa amejipatia hatia ya mwili na damu ya Bwana" (! Kor 11:26,27). Ibada ya kumega mkate kwa sababu hii itafanywa wakati na mahali ambapo hapata kuwapo na kuvutwa mawazo kwenda pengine na kudakizwa na mtiririko wa mawazo ya mtu. Hii yaweza kufanywa mapema asubuhi au mchana ukishapita, ndani chumbani au mahali pengine panapofaa. Tunashauriwa zaidi,

" Lakini mtu ajihoji mwenyewe, na hivyo (katika hiyo roho ya unyenyekevu ya kujipima nafsi) aule mkate, na kukinywea kikombe", (1 Kor 11:28). Kwa hiyo tutaweka mioyo yetu juu ya dhabihu ya Kristo, labda kwa kutazama taarifa za Injili kuhusu kusulubiwa kwake, kabla ya kutwaa mifano. Kwa kufanya hivyo

vema, bila kuepuka tutajihoji dhamiri zetu wenyewe kumweleke Kristo, zaidi.

Kanuni inayofaa kwa ibada ya kumega mkate ni kama ifuatavyo:-

1. Sala - ya kumuomba Mungu abariki mkutano:

Afumbue macho yetu kuelekea Neno lake; kukumbuka mahitaji ya waumini wengune; kumtukuza kwa upendo wake, hasa ulioonyeshwa kwa Kristo, na kuomba kwa habari za matokeo mengine dhahiri.

2. Kusoma masomo ya Biblia kwa siku kama yalivyotajwa katika "Mwenzi wa Biblia"
3. Kutafakari juu ya masomo ya kufundisha, kusoma 'Maonyo'- kujifunza Biblia juu ya sura hizo zinazotuongoza kuelekea kwenye lengo la ibada yetu - ukumbusho wa Kristo.
4. Somo 1 Kor 11:23-29
5. Kipindi cha kukaa kimya cha kujihoji mwenyewe
6. Sala kwa ajili ya mkate
7. Mega mkate, kula kipande chake kidogo.
8. Sala kwa ajili ya divai
9. Kunywa tone la divai
10. Sala ya kumalizia

Ibada nzima ichukue saa moja tu.

## 11.4 Ndoa

Tutaanza sehemu hii kwa kupima hali yao ambao hawajaoa wakati wa kubatizwa. Tumezungumzia katika somo la 5.3 juu ya haja ya kuoa au kuolewa na waumini waliobatizwa tu. Yapo mafungu ya maneno machache, yaliotiwa pamoja na mifano ya Yesu, Paulo na wengineo yanawatia nguvu wao wasio na wake kukumbuka hiari iwayo yote ya kubaki bila kuoa hivyo kama kujitoa wenyewe kabisa kufanya kazi ya Bwana (1 Kor. 7:7-9, 32-38 linganisha na 2 Tim 2:4; Math. 19:11,12,29; Mhubiri 9:9). “Lakini kama ukioa huna hatia” (1 Kor 7:28). Mitume wengi walioa (1 Kor 9:5), ndoa kama Mungu alivyoikusudia imepangwa ili kuleta faida nyingi za mwili na kiroho. “Ndoa iheshimiwe na watu wote, na (matumizi ya ) malazi/kitanda yawe safi” (Ebra 13:4).

“Si vema huyu mtu awe peke yake” ila akiweza kuongoza hali ya juu katika mambo ya kujitoa kwenye mambo ya  kiroho, na kwa sababu hiyo Mungu aliweka ndoa (Mwanzo 2:18-24). Kwa hiyo, “Apataye mke apata kitu chema; naye ajipatia kibali kwa Bwana……. Mke mwenye busara mtu hupewa na Bwana” (Mithali 18:22; 19:14).

Tumepewa maelezo mafupi yaliyosawazishwa ya hali ilivyo katika 1 Kor 7:1,2: “Ni heri mwanamume asimguse mwanamke. Lakini kwa sababu ya zinaa (yaani, ili kuepuka uzinzi), kila mwanamume na awe na mke wake mwenyewe, na kila mwanamke awe na mume wake mwenyewe” (linganisha mst 9).

Kidokezo cha aya hii ni kwamba kujifurahisha kwa tamaa za ngono nje ya ndoa ni uasherati. Maonyo juu ya kufanya uasherati (ngono baina ya watu wasiooana), uzinzi (ngono ambayo mmoja au watu wawili wameoana tayari na wenza wengine) na namna yeyote ya vitendo viovu ni mengi katika Agano Jipya lote; karibu kila

waraka yapo ndani. Maonyo yafuatayo ni baadhi: Matendo 15:20; Rum 1:29; 1Kor 6:9-18; 10:8; 2Kor 12:21; Gal 5:19; Efe 5:3; Kol 3:5; 1The 4:3; Yuda 7; 1 Petro 4:3; Uf 2:21.

Katika mwangaza wa mkazo huu uliorudiwa, kutotii mapenzi ya Mungu yaliyoelezwa wazi ni kosa kubwa sana. Wakati dhambi za udhaifu wa mara moja kama zikitubiwa, Mungu anapenda kusamehe(k.m. uzinzi wa Daudi na Bathsheba), kuishi namna ya maisha ambayo kwa kawaida ni ya kufanya matendo haya yanaweza kusababisha hukumu tu. Huu, Paulo aliunena: “Uzinzi, uasherati…. Na mambo kama hayo: katika hayo nawaambia mapema (kiti cha hukumu), kama nilivyokwisha kuwaambia, ya kwamba watu watendao (daima) mambo ya jinsi hiyo hawataurithi Ufalme wa Mungu” (Gal 5:19,21), kwa hiyo “Ikimbieni zinaa (linganisha na 2 Tim 2:22). Kila dhambi atendayo mwanadamu ni nje ya mwili wake; ila yeye afanyae zinaa hutenda dhambi juu ya mwili wake mwenyewe” (1 Kor 6:18).

Imekuja kukubalika karibu ulimwenguni pote ya kwamba mume na mke vijana waweza kuishi pamoja kabla ya ndoa halali, wakifurahia maisha kamili ya uhusiano wa ngono. Kutumia neno ‘ndoa ya sheria ya kawaida’ kueleza hivi ni maelezo yaliyo sahihi kabisa ya neno. Ndoa kwa waumini inabidi iwe ndoa inayolingana na Mungu alivyofafanua; hatuwezi kuruhusu elezo la ndoa iliyofanywa na ulimwengu unaotuzunguka wenye kuupendeza mwili kuwa juu zaidi ya taarifa za Mungu wala si mwanadamu. Kwa Biblia ndoa inafanywa karibu na mambo matatu :-

1. Lakini namna nyingine ya sherehe ya ndoa ni rahisi. Taarifa ya Boazi akimuoa Ruthu katika Ruthu 3:9-4:13 yaonyesha ya kwamba ndoa si uhusiano unaoingizwa tu; inabidi uwepo muda dhahiri wakati mtu anaolewa/oa kabisa. Kristo amelinganishwa na bwana arusi na waumini bi arusi, ambaye atamwoa ajapo mara ya pili. Itakuwepo “karamu ya arusi ya Mwana kondoo” itakayo

sherekewa (Uf 19:7-9). Uhusiano kati ya mme na mke ni mfano uliopo kati ya Kristo na waumini (Efe 5:25-30); kama inavyokuwapo maana halisi ya ndoa kati yetu, basi itakuwepo arusi kati ya waaminio inayoanza ndoa yao, ikionyesha mfano wa kuungana Kristo na sisi wenyewe kwenye kiti cha hukumu.

2. Ndoa ya Mungu kwa Israeli ilihusisha kuingia katika mapenzi ya agano la uaminifu

3. kiroho kwa wao na mwingine (Ezek 16:8), na hili liwe ni jambo la kuangaliwa katika ndoa ya waaminio.

4. Ushirika wa mume na mke ni wa lazima ili kukamilisha ndoa (Kum 21:13; Mwa 24:67; 1Falm 11:2). Kwa sababu hii 1 Kor 6:15,16 inaeleza kwa nini ushirika ukifanywa nje ya walioona ni vibaya mno. Ushirika unamaanisha kwa maneno ya kimwili ni jinsi gani Mungu alivyowaunga pamoja wanandoa (Mwa 2:24). Kuungwa na kuwa "mwili mmoja" ni uhusiano wa kitambo basi ni vibaya kutumia miili aliyotupa Mungu isiyotakiwa. Ameipanga kwa utaratibu ili kuweza kukamilisha katika mapatano ya kimwili alivyoiunga pamoja katika ndoa.

Kutokana na hili, kwa sababu hiyo watu wawili 'wanaoishi pamoja' kabla ya harusi kwa kweli wanaishi katika dhambi. Isipokuwa wakitengeneza uhusiano wao kwa kuoana vyema - au kutengana - hakuna maana kwao wakiwa wamebatizwa. Tatizo linazuka kwenye tamaduni zingine katika nchi zinazoendelea ambapo hakuna wazo la sherehe au mkataba kwa watu wa kawaida. Watu wawili wanaweza kuishi kwa miaka mingi pamoja bila mambo haya, wakijiona wenyewe kama wameoana. Ni ushauri wa mwandishi wa wakati huu wa kwamba katika masuala haya hao wabatizao waeleze hali ya huyo atakaye Ubatizo, wawakutanishe

na wenza wao ili watie saini kwenye fomu ya mapatano ya ndoa. Kisha uhusiano uorodheshwe na mamlaka muhimu ya Serikali haraka iwezekanavyo.

Hao waliobatizwa, muda wenza wao wakiwa bado, kwa namna iwayo yote wasiachane nao (1 Kor 7:13-15), bali wafanye kila juhudi kuwapenda, na hivyo kuonyesha mwenendo wa maisha wa kwamba wana imani halisi kwa Mungu wa kweli, kuliko kuwa ni dini ambayo imebadilishwa. Waraka 1 Petro 3:1-6 unawatia moyo walio kwenye hali hii kwamba kufanya hivi kunaweza, ndani yake, kuwa njia ya kumuongoa mwenzi asiyeamini.

Mambo yanayotawala ndoa yamewekwa kwa ufupi katika taarifa ya Mungu kwa habari zake: "Mwanamume atamwacha baba yake na mama yake, naye ataambatana na mkewe: "nao watakuwa mwili mmoja" (Mwz 2:24). Jitihada hii ya umoja kati ya mume na mke kwa namna nyingine kama iwezekanavyo ni ya kulinganika na juhudi yetu ambayo inaendelea kwenye umoja na Kristo, kwa kushinda msingi wa dhambi na uchoyo wa mwili wetu. Kujitahidi huku ni juu yetu wenyewe kuliko juu ya Kristo au mwenza wetu. Zaidi tunapofaulu kwa hili, uhusiano wetu utakuwa wenye furaha na kutimilika zaidi.

Lakini tunaishi katika ulimwengu wenye dhambi kweli na kushindwa, usioweza kusimama kabisa kwenye viwango vya hali ya juu vya utakaso tuliowekewa katika Biblia na katika mfano wa upendo wa Mungu na Kristo. Desturi isiyo na upungufu iliyowekwa katika Mwanzo 2:24 ya mwanamume na mwanamke mmoja, waishi pamoja kwa umoja wa maisha kabisa.

Waumini yawapasa wawe tayari kukubali kwamba mara nyingine desturi hii haitafikiwa pande mbili katika maisha yao

wenyewe na kwa hayo ya waamini wengine. Waume kwa wake waweza kushindana kwa maneno na kupoteza umoja huo wa roho ambao watakuwa nao; haitawezekana kwa mwili kukamilisha ndoa; mwanamume aweza kuwa na wake kadhaa, aliowachukua kabla ya ubatizo, kama amekuwa akiishi katika jamii mahali ndoa ya mitara imeruhusiwa. Katika suala hilo atabaki na hao wake, lakini asiongeze tena. Mtume Paulo mwenye mchanganyiko wa kupenda kuongoza wengine huruma ya mwanadamu na mwaminifu na kufuata mambo ya Mungu, kwa hiyo alishauri kwamba kutengana kuliwezekana katika kipeo cha masuala yasiyopatakana: "Mke asiachane na mmewe; lakini ikiwa ameachana naye, na akaye asiolewe" (1 Kor 7:10:11).

Huku kueleza kwa maneno ya desturi isiyo na upungufu,bali nia ya kukubali desturi ya chini maadamu haidhihaki msingi wa jambo la Mungu (k.m huo uzinzi ni mbaya), ni sura ya Andiko inayotokea kabisa. Ushauri wa Paulo kwa 1 Kor 7:10-11 ni sawa na 1 Kor 7:27,28: "…. Umefunguliwa?usitafute mke (yaani, ubaki pekee yako) "Lakini kama ukioa huna hatia". Ingawa hivyo, kuachana kwa makusudi ni kudharau mpango uliowekwa na Mungu wa kwamba mwanaume na mwanamke watambueya kuwa amewaunga kuwa mwili mmoja, hata kama juu ya matokeo ya kufaa haya wanakuta ni shida kujizoeza. Maneno ya Kristo ni ya kujitahidi kuwa sawa.

"Tangu mwanzo wa kuumbwa ulimwengu Mungu aliwafanya mume na mke. Kwa sababu hiyo mtu atamwacha babaye na mamaye, ataambatana na mkewe; na hao wawili watakuwa mwili mmoja: (Yesu anatia mkazo) hata wamekuwa si wawili tena, bali mwili mmojas. Basi alichokiunganisha Mungu, mwanadamu asikitenganishe (kwa kuachana kutoa hati ya talaka")….. "Kila mtu atakaye mwacha mkewe na kuoa mwingine azini juu yake. Na mke

atakeye mwacha mumewe na kuolewa na mtu mwingine, azini" (Marko 10:6-12)

Kwa hili eneo zima la mahusiano ya ngono, mwili ni mkono unaogusa mapendekezo na kuachilia kujihesabia haki katika tamaa za asili za kuupendeza mwili. Hao wanaojikuta wenyewe wamo katika mazingira hasa ya kujaribiwa watapata nguvu za uwezo wanaouhitaji kutoka tafakari inayorudiwa juu ya aya zinazonukuliwa katika sehemu hii. Wengine wametafuta kuhesabia haki vitendo vya kulawiti na vitendo vya mwanamke na mwanamke kuwa ni halali, kwa matakwa ya mwili. Walakini, hapana shaka ya kwamba mazoea haya yote ni machukizo mbele za Mungu.

Jambo la msingi lililo katika Mwanzo 2:24 linafafanua dhambi ya kulawiti; nia ya Mungu ni kwamba mwanamume na mwanamke waoane na kuambatana. Mungu aliumba mwanamke kumsaidia Adamu, wala si mwanamume. Mahusiani ya ngono baina ya wanaume Biblia imerudia kutoa lawama. Hii ilikuwa ni moja ya dhambi zilizofanya Sodoma iliangamizwa (Mwanzo mlango wa 18,19): Mtume Paulo anaweka wazi sana jambo hili kuendelea kufanya mazoea haya watapata hasira ya Mungu, na kutokuingia katika Ufalme wake (Rum 1:18-32; 1Kor 6:9,10).

Ukweli wa kuwahi kujiingiza katika matendo haya hautatufanya hatuwezi kupata msaada wa Mungu. Kuna msamaha wa Mungu, kama wakipenda kwa unyenyekevu na wale wanaopata msamaha wake (Zab 130:4). Iklezia ya Korintho lilikuwa na ushirika wa haki yake kwa waliotubu: "Baadhi yenu mlikuwa wotu wa namna hii: lakini8 mlioshwa (kwa kubatizwa), lakini mlitakaswa, lakini mlihesabiwa haki (kwa kubatizwa) katika jina la Bwana Yesu Kristo" (1 Kor 6:9-11).

Malalamiko ya kwamba mtu hana mvuto wa mwili kuelekea jinsia tofauti ni ya maana ya kumlaumu Mungu kwamba hana haki kutukataza kufira, au kulawiti, bali anatuwekea majaribu ya kutuzidi nguvu. Mungu hatatuacha tujaribiwe kupita tuwezavyo; lakini pamoja na lile jaribu atafanya na mlango wa kutokea (1 Kor 10:13). Kwa kuufurahisha kupita kiasi mwelekeo wowote wa mwili, mtu anaweza kufikia kilele ambavyo hivi ndivyo kwa kawaida apendavyo mtu. Hivyo, mtumiaji kileo au madawa ya kulevya hawezi kuishi bila desturi ya kujidunga madawa fulani; lakini anatakiwa kubadili mwelekeo wa akili yake, na pamoja na tiba ya kurudisha namna ya kuishi sawa sawa.

Ufiraji/kulawiti inabidi uende kwa njia hii. Mungu ataimarisha juhudi ya mwanamme kwa haya; kama wao wenyewe huendekeza tamaa za mwili, Mungu atawatendea kama Israeli zamani:

"Hivyo Mungu aliwaacha wafuate tamaa zao za aibu: hata wanawake wakabadili matumizi ya asili kwa matumizi yasiyo ya asili: wanaume nao vivyo hivyo waliacha matumizi ya mke ya asili, wakawakiana tamaa; wanaume wakiyatenda yasiyopasa, wakapata nafsini mwao malipo (yaani, katika miili yao) ya upotevu wao yaliyo haki haki yao" (Warumi 1:26,27)

Kwa upofu wa makusudi mtu anaweza kushindwa kuona dhahiri jambo hili la unabii wa **UKIMWI**, na zao lingine kubwa linalotokana na magojwa ya zinaa ambayo ulimwengu wetu ulioharibika unavuna sasa.

## 11.5 Ushirika

Maneno ya Kiyunani yaliyofasiriwa 'ushirika', kimsingi yanaelezea hali ya kuwa na kitu fulani kwa ushirikiano. 'Ushirika' ni neno linalohusisha 'kushiriki kanuni na imani ile ile - hivyo kuwasiliana. Kwa sababu ya kujua na kujizoeza njia ya Mungu, tunaushirika naye na wote wengine wafanyayo yale yale kwa kuwa "katika Kristo". Ni vyepesi kuacha majukumu ambayo tunayo ya kuwa na ushirika na wengine: "kutenda mema na kushirikiana, msisahau (Ebr 13:16). Flp 1:5 umezungumzia ushirika wetu katika kuieneza Injili; basi msingi wa ushirika wetu ni mafundisho yaliyo na Injili ya kweli. Kwa sababu hii ushirika unaofurahiwa na waumini wa kweli ni mkubwa mno kuliko jumuia yoyote nyingine au kanisa. Kwa ajili ya Ushirikiano huu wanasafiri umbali mrefu ili kuwa na mwingine na kuwatembelea waumini walio pekee, na atatumia vema posta na simu kwa kuwasiliana mahali panapowezekana. Paulo anausema "ushirika wa Roho" (Flp 2:1), yaani, ushirika ambao kama ilivyofunuliwa katika Roho yake/neno.

Moja ya maelezo makubwa ya ushirika wetu ni kufanya ibada ya kumega mkate pamoja. Waumini wa kwanza "walidumu katika fundisho la mitume, na katika ushirika, na katika kumega mkate, na katika kusali….. wakimega mkate ……. Kwa furaha na kwa "moyo mweupe" (Mdo 2:42,46). Mifano inayokuwa mbele yetu mezani yaonyesha kiini kikuu cha tumaini letu, tunavyovigawana pamoja vitatuunga pamoja katika "moyo mweupe". "Kikombe kile cha baraka tukibarikicho, Je! si ushirika wa damu ya Kristo? Mkate ulio tu umegao, Si ushirika wa mwili wa Kristo?. Kwa kuwa mkate ni mmoja, sisi tuliotulio wengi tu mwili mmoja; kwa maana sisi sote twapokea sehemu ya ule mkate mmoja"; yaani Kristo (1 Kor 10:16,17) kwa hiyo tunawajibu wa kugawana mifano ya dhabihu ya Kristo na wote wale wanaofaidika kutokana na kazi yake, ambao

“wanashiriki kugawana sehemu ya huo mkate mmoja”. Wale tu waliobatizwa vema katika Kristo, baada ya kujua ukweli, wamo hali hii, ni kufanyia mzaha mifano kwa kugawana na aweye yote mbali ya hawa.

Paulo anakumbuka ni jinsi gani alishiriki Injili ya uzima wa milele na wengine “ili nanyi pia mpate kushirikiana nasi; na ushirika wetu ni pamoja na Baba, na pamoja na Mwana wake Yesu Kristo” (1 Yoh 1:2,3). Hivi yaonyesha ya kwamba ushirika umelala kuzunguka desturi ya kufahamu Injili ya kweli, na kwamba hii inatuleta katika ushirika wa pande mbili na waumini wa kweli wengine, vile vile Mungu na Yesu juu ya usawa wenyeywe. Tunapotumia zaidi Injili katika maisha yetu, tukiyashinda maelekeo yetu ya dhambi, na kwa kina tunapoendelea katika kufahamu kwetu Neno la Mungu, ndipo kwa kina zaidi ushirika wetu utakuwa na Mungu pamoja Kristo.

Ushirika wetu na Mungu na Kristo na waamini wengine hautegemei tu juu ya desturi yetu ya kukubaliana na kweli zenye mafunzo ambayo yana “imani moja”. Mwenendo wetu wa maisha inabidi ulingane na mambo yalioelezwa humu ndani. “Mungu ni nuru, wala giza lolote hamna ndani yake. Tukisema ya kwamba twashirikiane naye, tena tukienenda gizani, twasema uongo, wala hatuifanyi iliyo kweli: bali tukienenda nuruni twashirikiana sisi kwa sisi, na damu yake Yesu, Mwana wake, yatusafisha dhambi yote” (1 Yoh 1:5-7)

‘Kuenenda gizani’ inabidi kuwa unatajwa mwenendo wa maisha ambao siku zote ni wa kutumikia na watu wote walio mbali mbali na Neno la Mungu (Zab 119:105; Mithali 4:18); haitajwi udhaifu wetu wa dhambi za mara kwa mara, maana aya inayofuata inaendelea. “Tukisema kwamba hatuna dhambi twajidanganya

wenyewe, wala kweli haimo mwetu (yaani Neno la Mungu (Yn. 17:17; 3:21 Waefeso (5:13) linakuwa halimo mioyoni mwetu".

Kutokana na hivi itakuwa dhahiri kwamba ushirika unakoma hapo muumini akianza kufuata mafunzo au mwenendo wa maisha, ambao upo wazi ukipingana na fundisho lilowazi la Biblia: "Msishirikiane na matendo yasiyo zaa ya giza, bali myakemee" (Efe 5:11). Kila juhudi ifanywe kuwarudisha kwa kufuata mfano mzuri wa mchungaji mwema amtafutae kondoo aliyepotea (Lk 15:1-7). Ikiwa ndugu au dada anaendelea katika elimu ya uongo au tabia mbaya kabisa, ni lazima kupanga ukomo wa ushirika uliotokea (Mathayo 18:15-17). Kwa desturi hivi hufanywa kwa usaili wa washirika wanaohusika na Iklezia, na kutangaza ukweli katika gazeti la Kristadelfiani. Lakini habari isitiliwe mkazo sana ya kuwa njia hii itatumika kwa kuchukua njia ya mkato ya kushika masuala ya elimu potofu au kuendelea katika mwenendo wa maisha yasiyo ya Kiroho. Inabidi mtu awe na hakika ya kwamba kuna desturi kidogo mno baina yetu, kwa ajili ya kupotoka toka msingi wa mafundisho ya Biblia, hata kuvunja utaratibu wa ushirika ni lazima.

Moja ya maneno yaliyo wazi sana kuhusu ushirika yanapatikana katika 2Kor 6:14-18: "Msifungwe nira pamoja na wasioamini": kwa maana pana urafiki gani kati ya haki na uasi? Tena pana shirika gani kati ya nuru na giza….. Kwa hiyo tokeni kati yao, mkatengwe nao, asema Bwana,….. nami nitawakaribisha, nitakuwa Baba kwenu, nanyi mtakuwa kwangu wanangu wa kiume na wa kike, asema Bwana mwenyezi".

Tumeonyesha ni kiasi gani kwamba Neno la Mungu ni nuru. Aya hizi zaeleza ni kwa sababu gani tusifanye ushirika na makanisa yafundishayo elimu iliyopotoka; kwa sababu gani tusioane na hao

wasiojua kweli, na kuepuka mienendo ya ulimwengu. Kwa sababu ya kujitenga kwetu toka ulimwengu tuna heshima kubwa sana ya kuwa wana kabisa wa Mungu na binti, sehemu ya jamaa iliyoenea duniani pote ya wengine walio na uhusiano u huu - ndugu zetu na dada. Upo "mwili mmoja" tu, yaani, kanisa la kweli (Efe 1:23), ambalo msingi wake upo juu ya hao washikao tumaini moja Mungu mmoja, ubatizo mmoja na "imani moja", yaani orodha moja ya kweli yenye mafundisho yaliyo na imani moja (Efe 4:4-6). Haiwezekani kuwa sehemu ya huu "mwili mmoja" na vile vile kushirikiana na jumuia za dini nyingine zisizo shika imani ya kweli. Kwa kuwa nuru haishirikiani na giza, twajitangaza sisi wenyewe kuwa tumo gizani kama tukichagua kushirikiana na giza.

Ikiwa kweli tunaufahamu muundo mzima wa elimu ya kweli iliyofunuliwa katika Andiko, tutaona ya kwamba hao waaminio elimu iliyopotoka katika jina la Ukristo hawana ushirika tena na Mungu zaidi ya wao kuwa hamwamini Mungu kuwa yupo.

Kama umefuatilia masomo haya kwa makini, itakuwa dhahiri ya kuwa sasa hapatakuwapo hali ya mwenendo nusu katika ushirika wetu na Mungu. Aidha tunakuwamo katika Kristo kwa ubatizo ndani yake. Aidha katika nuru kwa sababu ya kushika kwetu elimu ya kweli ya kupenda kuitii au katika giza. Mtu hawezi kuwa na unyayo katika kambi mbili.

Elimu juu ya mambo haya inatupatia kiwango fulani cha kuwajibika mbele za Mungu. Sasa hatutembei mitaani au kwenda kuzungusha maisha yetu kama wastani wa mwanadamu wa ulimwengu. Kwa nguvu anatazama kuitika kwetu. Pande zote mbili Mungu, Bwana Yesu na waumini wa kweli karibu 'watapenda' wewe ufanye uamuzi sahihi. Bali mengi kama Mungu, Kristo sisi wenyewe tutafanya yote tuwezayo kukusaidia - hata kwa suala la

Mungu kwenye upana wa kuwa amemtoa mwana wake wa pekee kufa kwa ajili yetu - wokovu hutegemea juu ya hiari yako mwenyewe kuamua kushika tumaini kuu ambalo sasa limetolewa kwako.

**Somo La 11: Maswali**

1.Ni mabadiliko ya aina gani yatatokea katika maisha yetu wakati wa ubatizo?

2. ‘Utakaso’ una maana gani?
a) Kutogusana na wasio amini
b) Kujitenga toka dhambi na kufuata mambo ya Mungu
c) Kwenda kanisani
d) Kutenda mema kwa wengine

3. Aina zipi za shughuli hazimfai Mkristo wa kweli?

4. Maneno ‘mtakatifu’ na ‘Iklezia’ yana maana gani?

5. Habari zipi zifuatazo ni za kweli kuhusu kuumega mkate?
a) Tutafanya karibu kila juma
b) Tutafanya mara moja kwa mwaka wakati wa Pasaka
c) Mkate na divai hugeuka kuwa mwili halisi na damu ya Yesu
d) Mkate na divai huwa mfano wa mwili na damu ya Yesu

6. Ni taarifa zipi zifuatazo ni za kweli kuhusu ndoa?
a) Tuoane na waumini wa kweli tu

b) Kutoa hati ya talaka inaruhusiwa kwa waumini

c) Muumini aliyeoa aliye na mwenza asiyeamini wajaribu kukaa nao

d) Katika ndoa, mwanamume ni mfano wa Kristo na mwanamke ni waumini

7. Je! wanawake wana ruhusa kufundisha katika Iklezia?

8. Ikiwa umebatizwa baada ya kujua ukweli, je! utabaki kushirikiana na makanisa yasiyofundisha ukweli kabisa?

## MWISHONI MWA KITABU 1: MAELEZO MAFUPI YA MSINGI WA MAFUNZO YA BIBLIA.

### 1. MUNGU

1.1 Yupo mtu mmoja aitwaye Mungu
1.2 aliye na mahali maalum katika mbingu
1.3 aliye hai mwenye mwili halisi
1.4 ambaye tumechukuwa sura yake
1.5 Malaika ni wajumbe wake
1.6 ambao hawatendi dhambi,
1.7 wakishiriki tabia ya Mungu.
1.8 Lipo umbo moja tu la kuwapo hai limefundishwa na Biblia - uwepo katika umbo la mwili. Mungu na Malaika wanaishi katika umbo la kimwili.
1.9 Tumaini la Mkristo ni kupewa tabia ya Mungu katika umbo la kimwili Kristo akirudi.

### 2. ROHO YA MUNGU

2.1 Inapotajwa Roho ya Mungu ni uweza wake, pumzi na akili,

2.2 ambayo kwayo anatimiliza mambo yote

2.3 na kuwepo kila mahali.

2.4 Roho Mtakatifu anatajwa uwezo huu uliotumika kutimiza miishi fulani.

2.5 Kwenye nyakati mbalimbali zamani, watu wamekirimiwa kuwa na vipawa vyenye miujiza ya Roho.

2.6 Hivi vimeondolewa,

2.7 Uweza wa Mungu sasa umefunuliwa kwetu katika neno Lake.

2.8 Roho Mtakatifu hawashurutishi watu kuwa wa kiroho kinyume na mapenzi yao wenyewe.

2.9 Biblia ilivuviwa na Roho wa Mungu kabisa.

2.10 Biblia tu ndio yenye mamlaka yetu katika uhusiano wetu na Mungu.

**3. AHADI ZA MUNGU**

3.1 Injili ilihubiriwa kwa namna ya ahadi zilizofanywa kwa mababa wa Kiyahudi.

3.2 Uzao wa mwanamke katika Mwa 3:15 unataja Kristo na wenye haki, "waliochubuliwa" na wanachubuliwa kwa muda na dhambi, uzao wa nyoka.

3.3 Kwa kutimilika ahadi za Mungu, sayari duniani haitaharibiwa.

3.4 Uzao wa Abrahamu na Daudi alikuwa ni Kristo;

3.5 twaweza kuwa ndani ya Kristo kwa kuamini na ubatizo,

3.6 kwa hiyo basi ahadi hizi zinawahusu waamini wa kweli.

## 4. MUNGU NA MAUTI

4.1 Kwa tabia mwanadamu ni mfu, mwenye kuelekea kutenda dhambi, na

4.2 amelaaniwa kwa matokeo ya kosa la Adamu.

4.3 Kristo alikuwa na huu mwili wa kibinadamu.

4.4 Nafsi hutajwa 'sisi', mwili wetu, mawazo au mtu.

4.5 Roho ni kutaja nguvu za uhai wetu/pumzi na silika.

4.6 Hakuna mtu awezaye kuishi akiwa na roho pasipo mwili.

4.7 Mauti ni hali ya kutokuwa na fahamu.

4.8 Atakaporudi Kristo kutakuwa na ufufuo wa mwili kwa wale tu wenye kuijua Injili ya kweli.

4.9 Maarifa na kufahamu Neno la Mungu vitakuwa msingi wa hukumu.

4.10 Kupewa kabisa kutokufa kutatokea kwenye kiti cha hukumu.

4.11 Adhabu ya waovu wahusika itakuwa mauti ya milele.

4.12 'Kuzimu' ni kaburi.

4.13 'Jehanamu' lilikuwa eneo nje ya Yerusalemu mahali pa takataka na walipochomwa wavunja sheria.

## 5. UFALME WA MUNGU

5.1 Watu wa Israeli walikuwa Ufalme wa Mungu zamani.

5.2 Huu uliisha sasa, lakini utaanzishwa tena Kristo akirudi, kwa namna

5.3 ya kuwa wa kuenea pote Ufalme wa Mungu duniani, ukitawaliwa na Kristo kwa niaba ya Mungu.

5.4 Miaka 1000 ya kwanza (au 'Kikwi') ya huu Ufalme itaona waamini wa kweli wa zama zote watakuwa hai Kristo akirudi.

5.5 Kwa hiyo sasa Ufalme kiutawala haujaanzishwa.

5.6 Tunaokolewa kwa neema kwa njia ya imani yetu, wala si kwa matendo yetu.

## 6. MUNGU NA UBAYA

6.1 'Ibilisi' kwa maana ya neno ni 'mshitaki' au 'msingiziaji'

6.2 'Shetani' kwa maana ya neno ni 'adui',

6.3 laweza kutumika kutaja watu wa pande mbili wema na wabaya.

6.4 Kwa mfano ibilisi na shetani yaweza kutajwa dhambi na mwili wa nyama.

6.5 Nyoka wa Edeni alikuwa mnyama halisi;

6.6 taarifa ya kitabu cha Mwanzo ya uumbaji wa mtu na kuanguka ieleweke ilivyo si kwa maneno ya kimfano.

6.7 'Mashetani' kama roho iliyojaa dhambi, roho waliotoka au nguvu ya dhambi hawapo.

6.8 Kristo 'kuwatoa pepo' yaweza kufahamika kama sehemu ya lugha ambayo kwa namna yake inamaana ya kuwa aliponya magonjwa.

6.9 Lusifa hatajwi Malaika aliyejaa dhambi.

6.10 Mungu ni mwenye nguvu zote; hashirikiani uweza wake na kiumbe awaye yote mwenye dhambi apingaye njia zake.

6.11 Majaribu katika maisha ya aaminiye mwisho huja toka kwa Mungu wala sio kwa matokeo ya 'bahati mbaya' au kwa kiumbe mwenye dhambi sana aitwaye Ibilisi.

## 7. YESU KRISTO

7.1 'Utatu' kama kwa upana unavyofahamika katika Ufalme wa Kikristo ni elimu ambayo haijafundishwa katika Biblia.

7.2 Kristo alizaliwa na bikira Mariamu

7.3 aliyekuwa mwanamke wa kawaida mwenye mwili wa kibinadamu.

7.4 Yesu alikuwa na mwili wa kibinadamu,

7.5 ila alikuwa na tabia timilifu isiyo na dhambi,

7.6 ingawa Mungu hakumshurutisha kutofanya dhambi; Yesu alikufa kwa hiari yake mwenyewe akiwa dhabihu timilifu kwa dhambi.

7.7 Yesu alifufuliwa baada ya mauti yake msalabani.

7.8 Kabla ya kuzaliwa Yesu hakuwahi kuishi,

7.9 ingawa alikuwa katika nia/ kusudi la Mungu tangu mwanzo.

7.10 Yesu alikufa akiwa sadaka kwa ajili ya dhambi zetu

7.11 ili kupata wokovu kwa ajili yetu na yeye mwenyewe.

7.12 Yesu alikufa akiwa mwakilishi wetu.

7.13 Sio badala yetu kama kwa upana inavyoaminika na ufalme wa Kikristo.

7.14 Kwa kifo cha Kristo Torati ya Musa ilikoma,

7.15 Kwa sababu hiyo haitupasi kuitunza sasa, pamoja na Sabato.

## 8. UBATIZO

8.1 Bila ubatizo, hakuna tumaini la wokovu;

8.2 kuamini na kubatizwa kunatuingiza kushiriki ahadi za Abrahamu,

8.3 na kwa kupata msamaha wa dhambi

8.4 Ubatizo ni kwa kuzamishwa ndani kabisa ya maji

8.5 mtu mzima aliyeijua Injili.

8.6 Hao waliozamishwa pasipo kuwa na elimu ya kutosha kwa Injili hawana budi kubatizwa tena. Kwa uzuri.

8.7 Kufahamu Injili ya kweli unahitaji ubatizo kuwa thabiti.

## 9. MAISHA KATIKA KRISTO

9.1 Baada ya ubatizo, mwamini hanabudi kufanya bidii yenye akili kujitenga katika njia zilizojaa dhambi za ulimwengu,

9.2 na kuendeleza tabia yenye sifa kama Kristo.

9.3 Kujishirikisha katika shughuli za anasa zitakazopeleka kuvunja maagizo ya Mungu, k.m kutumia nguvu na unywaji pombe kupita kiasi, haiwezi kupatana kwa kweli na maisha ya Kristo.

9.4 Waamini waliobatizwa wana wajibu kukutana na kushirikiana, popote wakati wowote kibinadamu ikiwezekana.

9.5 Waamini waliobatizwa kila mara wamege mkate na kunywa divai kwa ukumbusho wa dhabihu ya Kristo.

9.6 Sala ya kila mara na kusoma Biblia ni muhimu kwa mwamini aliyebatizwa.

9.7 Mwamini aliyebatizwa tu ana ushirika na wale ambao wanashika mafundisho ya kweli na kujaribu kwa hali ilivyo kutenda kazi.

9.8 Kwa hiyo ambaye anakoma kuamini au kuitendea kazi ile Kweli anakoma kuwa mshirika wa mwili wa waumini.

**Angalia:** ***Taarifa ya Imani moja ya utaratibu ambao umekuwa ukitumika zaidi ya miaka 100 unapatikana kwa wachapishaji.***

## MWISHONI MWA KITABU 2: TABIA YETU KUJIFUNZA BIBLIA

Yawezekana kabisa kujifunza mafunzo ya msingi wote wa Biblia lakini akashindwa kufahamu hali ya kweli yenyewe kwa ujumbe wake. Ukweli huu unaweza kuwa wakuleta huzuni sana kwa wale ambao hutumia kitabu cha mafundisho kama hiki na maelezo kwa wengine ambao wakati huo wanaonekana kushindwa kushika mambo yaliyozungumziwa.

Watu waliitikia kwa kweli kwenye mahubiri ya Injili katika karne ya kwanza. Watu "walilipokea neno" la Injili wakabatizwa (Mdo 2:41). Bila kuguswa na ujumbe moyoni - "imani yenye moyo wa kupenda", kama Robert Roberts mara nyingi alivyoielezea - hakuna maana ya kubatizwa. Wale ambao wapokea ujumbe tu kwa sababu ya kusongwa na wenza wao au wazazi hawaelekei kusimama kwenye mwendo. Kwa kuwa tunavutiwa na kuwaleta watu kwenye wokovu kuliko kuwa na idadi ya wanaobatizwa, inafaa kuchukua muda wa kuhubiri kwetu Injili na kuhakikisha kwamba waongofu wetu wanaujia ubatizo na msimamo ulionyooka.

Wale Waberoya "walilipokea lile neno kwa uelekevu wa moyo wakayachunguza maandiko kila siku" kuchunguza kile alichohubiri Paulo (Mdo 17:11). Kitabu hiki cha mafundisho - kwa kweli vitabu vyovyote vya mwanadamu vyenye ufasaha - ni jaribio tu la

kufikiri kwa usahihi fundisho la Biblia. Kwa maana ili pawepo uitikiaji wa kweli wa Injili, inabidi iwepo akili nyepesi kusikia Neno, kwa kweli ukitamani kuchunguza maandiko kwa usawa wake. Hili ndilo jambo fulani ambalo muhubiri wa Injili kwa ulazima hawezi kulileta; tunaweza tu kuvuta macho kuangalia mafungu ya Biblia yanayohusu jambo lenyewe. Waumini wa pale Rumi "walitii kwa mioyo yao ile namna ya elimu ambayo waliipokea" kabla ya wao kubatizwa (Rum 6:17).

Wale ambao kwa ukaidi wanadumu katika njia za mwili kamwe hawata weza kufahamu vema ujumbe wa kweli ya Injili; wataishi wakiwa "wenye mfano wa utauwa, huku wakikana nguvu zake……. Wakijifunza siku zote, lakini wasiweze kabisa kuufikia ujuzi wa kweli" (2 Tim 3:1-7). Kamwe hatufahamu kile tusichotaka. Kama hatuipendi hasa haki, hakuna haja kweli ya kuleta maisha yetu chini ya uongozi wa Mungu, kamwe hatutaweza "kufikia ujuzi wa kweli", pamoja na kusoma kwetu Biblia; kujifunza kwetu kutakuwa ni kufanya mazoezi tu ya kujizoeza kusoma bila maana.

Kuna mifano kadhaa ya watu wakisoma Maandiko, lakini si kwa namna ya kuyasoma. Huu ni ugonjwa ambao sote sisi tunaelekea. Wayahudi wakati wa Kristo walionekana kuwa na juhudi kubwa kwa ajili ya neno la Mungu; waliyaamini maandishi ya Agano la Kale kuwa yalivuviwa (Yn. 5:45; Mdo 6"11); walijua ya kwamba kwa kusoma Maandiko haya wanaweza kuwa na tumaini la uzima wa milele (Yohana 5:39), na kila juma walisoma mbele ya watu (15:21). Kwa nyongeza, baadhi yao kwa karibu walisoma mafungu haya ya maneno wakati wa juma. Walakini, walishidwa kabisa kufahamu maana halisi ya Maandiko haya, kwa kuwa yalilenga mbele kwa Kristo. Yesu aliwaambia wazi wazi: "Mwayachunguza Maandiko……… kwa maana kama

mngalimwamini Musa, mngeniamini mimi: kwa sababu yeye aliandika habari zangu. Lakini msipoyaamini maandiko yake, mtayaamini wapi maneno yangu? Msipowasikia Musa na manabii" (Yohana 5:46,47; Luka 16:29-31).

Tunaweza kufikiri uchungu wa Wayahudi: 'Lakini tunafanya kuisoma Biblia! Tunafanya kuiamini! Ila, kwa sababu ya tabia yao ya karibu, kwa namna ya kipekee hawakufanya hivyo - wanasoma, ila hawakuielewa; walitazama, lakini hawakuona. Kwa kweli hakuna walio vipofu kama hao wasiotaka kuangalia. Katika hatua zote kwa maendeleo yetu ya kiroho yatupasa kujilinda sana juu ya jambo hili.

## MWISHONI MWA KITABU 3: KRISTO AMEKARIBIA KURUDI.

Maneno ya Kristo katika Math 24:36 yanaweka wazi kuwa hatujua kamwe wakati hasa wa kuja tena mara ya pili: "Walakini habari ya siku ile na saa ile hakuna ajuaye, hata malaika walio mbinguni, wala Mwana, ila Baba peke yake" (linganisha Mdo 1:7). Ingawa hivyo, wafuasi walipomwuliza Yesu, "Nayo ni nini dalili ya kuja kwako?" (Math 24:3), hakuwajibu kwamba swali lao lilikuwa gumu kulijibu. Hakika aliwapa ishara ambazo zitaonekana katika ulimwengu kabla ya kurudi. Yesu asingaliwapa hizi isipokuwa alikusudia kizazi kinachoishi kabla ya kurudi kiweze kwa upana kutambua ya kuwa kwa kweli kinaishi katika "siku za mwisho". Ipo sababu nzuri ya kutumaini na kuamini ya kwamba tumo kwenye siku hizo za mwisho sana.

## DALILI ZINAONYESHA KURUDI TENA KRISTO

Katika Mathayo 24 na Luka 21, Yesu alinena wakati hapo

1) Kutakuwa na manabii waongo wakidai kuwa ni Kristo
2) Vita na vurugu vitaenea duniani
3) "Kutakuwa na njaa, magonjwa na matetemeko"
4) Kukengeuka toka kwenye kweli kutakuwepo.
5) Watu watavunjika mioyo kwa hofu ya hali itakayakuwapo duniani, "kwa kutazamia yatakayo upata ulimwengu" (Luka 21:26).

Ni kweli kwamba siku zote ulimwengu umekabiliwa na matatizo yanayongezeka ya aina hii. Ni bayana Yesu alijua ukweli huu; kwa hiyo ni halali kusadiki kuwa alikuwa anataja kwa wakati hapo shida hizi zitakapokuwa kubwa mno hata kutishia kuiharibu sayari. Hapawezi kuwepo shaka, kwa mtazamaji wa makini ulimwengu, kwa kweli hii ndiyo hali iliyopo. Matumaini ya ajabu ya hali ya mwanadamu na kutopenda kwake kufikiri vilivyopo kukabili nafasi yetu, kunafanya iwe shida kwetu kufahamu hii hali ilivyo.

Ifuatayo ni sehemu ndogo tu ya ushahidi unaopatikana ambao unaonyesha jinsi maneno ya Kristo sasa yanatimilika:

1). Kwa karibu kila bara kuna mkondo usiogeuka wa watu waongo wenye kadhia ya kuwa na ufunuo na maarifa maalum na madhehebu yanayosema yanauwezo wa kuponya na ya kuwa yana vipawa ambayo yanawavuta watu kuwafuata.

2). Ifuatayo ni habari ya hesabu inayoonyesha jinsi matatizo yasiyotazamiwa ya vita yakiongezeka - mbali ya juhudi za wanadamu pamoja kama kuyazuia:

| Karne | Vita na majeruhi, waliouawa (mamilioni) | Idadi ya vita kuu |
|---|---|---|
| ya 17 | 3.3 | ? |
| ya 18 | 5.0 | ? |
| ya 19 | 5.5. | ? |
| 1900-1945 | 40.5 | 19 |
| 1945-1975 | 50.7 | 119 |

(Mtoa taarifa: Kitivo cha Uangalizi wa mapigano, Chuo kikuu cha London)

3) Shida kubwa ya njaa na magonjwa ya kuambukiza yanajulikana vema kwetu sote. **UKIMWI** kwa ukubwa na maradhi yanayo ambukiza kwa kuenea ulimwengu pote ambao umejulikana. Mbali na maneno ya Yesu katika Mathayo 24 na Luka 21, kuna mafungu kadhaa mengine ya maneno yanayo jumuisha matetemeko ya ardhi na kurudi Kristo: Isaya 2:19-22; Ezek . 38:20; Yoel 3:16; Hagai 2:7; Zek 14:3,4. Kwa kadri ya kuangalia matetemeko ya hivi karibuni yakitokea kwenye maeneo yasiyotegemewa pamoja na hasara isiyotazamiwa ya matokeo ya hasara ya maisha, yaweza kudokeza ya kwamba tunaanza kuona utimilifu wa dalili ya tetemeko vilevile. Habari ya idadi ifuatayo kuhusu matetemeko, iliyotolewa na idara ya ndani ya Serikali ya Amerika vilevile ni ya maana:

| **Mwaka** | **Taarifa ya Idadi ya Mitetemeko** |
|---|---|
| 1948 | 620 |
| 1949 | 1152 |

| | |
|---|---|
| 1950 | 2023 |
| 1964 | 5154 |
| 1965 | 6686 |
| 1976 | 7180 |

4) Kupungua mkazo juu ya umuhimu wa ukubwa kufuata Biblia ili kupata mafunzo ya kweli umesababisha ukengeufu mkubwa toka kweli ya Biblia. Umoja wa elimu ya binadamu kwa gharama yote ambayo sasa imeenea katika jamii imeongeza kasi katika maendeleo haya.

5) Mazoea yanayoongeza kasi ya kutoangalia hali ya kweli na kupenda anasa yanayoonekana katika kila jamii ya sasa ni ushahidi wa kutosha wa hofu ya mwanadamu kwa ajili ya wakati ujao. Wanasayansi, wachumi na wataalam wa mimea na wanyama na mazingira yao wote wanakubali ya kuwa ulimwengu hauwezi kuendelea kama ulivyo sasa. Kuondoa na kuharibu mali za asili, uchafuzi wa hewa, bahari na utando wa ozoni angani, pamoja na vitisho vya mambukizo na maangamizi ya nyuklia yote yanaonyesha uangamizo wa ulimwengu wa sasa. (ona Tumeacha kitambo kidogo tuchokiandika sehemu ya 9). Kwa kutunza hiyo ahadi, Mungu itampasa kumtuma Yesu kubadili upesi na kueleweka hii sayari kwa kusimamisha Ufalme wa Mungu juu yake.

## KUANZISHWA TENA TAIFA LA ISRAELI

Yesu alikamilisha kwa kutosheleza vema orodha yake ya ishara ya maelezo dhahiri: “Hapo ndipo watakapomwona Mwana wa Adamu akija katika wingu pamoja na nguvu na utukufu

mwingi” (Lk 21:27). Aya inayofuata inawapatia faraja pekee wale ambao wamekwisha batizwa nao wanaishi katika dhamiri njema mbele za Mungu: “Basi mambo hayo yaanzapo kutokea (sasa!), changamkeni, mkaviinue vichwa vyenu; kwa kuwa ukombozi wenu umekaribia” (Lk 21:28).

Kisha Yesu aliongeza habari ya ziada kwa unabii huu wa kuja mara ya pili, kwa namna ya mfano wenye kuongoa unaohusu mtini: “Utazameni mtini na miti mingine yote; wakati iishapo kuchipuka, mwaona na kutambua wenyewe ya kwamba majira ya mavuno yameisha kuwa karibu, nanyi kadhalika, mwonapo hayo yaanzapo kutokea, tambueni ya kwamba Ufalme wa Mungu u karibu (na kwa hiyo kuja mara ya pili. Amini nawaambieni, kizazi hiki hakitapita mpaka hayo yote yatimie” (Lk 21:29-32). Kwa uchunguzi wetu kuchipuka kwa mimea, tuna akili ya ujuzi wa kujua kiangazi na kipupwe au kubadilika majira kunakuja; vivyo “mtini” uanzapo kuchipuka, tuwe na fahamu ya jinsi hii ya kuwa kizazi chetu kitaona kuja kwa pili Bwana. Mtini ni ishara ya Biblia inayotaja taifa la Israeli (Yoeli 1:7; Hosea 9:10; Yeremia 24:2 linganisha Ezek. 36:8). Hii ishara maalum ya kurudi Kristo mara ya pili inataja basi kuanzishwa tena taifa la Israeli (‘kuchipuka’) kwa njia nyingine. Matukio ya upesi yaliyo pamoja na kukua kwa Israeli tangu kuanzishwa tena kuwa taifa katika mwaka 1948 hakika inabidi kuwa ya maana katika fungu hili la maneno.

## WAKATI UJAO ISRAELI KUVAMIWA

Unabii mwingi wa Biblia unatoa maelezo ya kuvamiwa Israeli, uvamizi mkubwa utakao tokea wakati wa kurudi Kristo. Zaburi 83 inatoa habari ya mataifa yakiizingira Israeli na kuwa muungano wa pamoja dhidi yake yakisema “Njoni, tuwakatilie mbali wasiwe taifa, na jina la Israeli halitakumbukwa tena”……. Na tutamlaki

makao ya Mungu" (Zab. 83:4,5,12). Tambua ya kuwa huu ni uvamizi wa siku za mwisho kwa Israeli likiwa taifa. Kuanzishwa kwake kuliopo lilivyo taifa ni muhimu basi kama utangulizi wa uvamizi huu wa mwisho juu ya taifa. Wasomaji wa Biblia walikuwa wakitabiri kuanzishwa tena taifa miaka mingi kabla ya kutokea (tazama kwa mfano, John Thomas Elps Israeli, kitabu ambacho kilichapishwa kwanza mwaka 1848. Kazi inayochapishwa tena inapatikana kwa wachapishaji). Msimamo wa wavamizi wa Israeli umeelezwa katika Zab. 83 hasa ni mashindano ya waarabu, majirani wa Israeli wa leo. Siku zote wanaeleza uchungu wa chuki yao isiyotulizika kwa Israeli, wakidai mji wa Yerusalemu ni wao mji wa Uislamu. Zaburi inaendelea kueleza jinsi shambulio lao litakavyoisha kwa haraka Mungu atakapo ingilia kati, na matokeo yakiwa kusimikwa Ufalme wake utakao enea ulimwenguni pote (Zab 83: 13-18).

Unabii mwingine unatoa maelezo ya mfululizo wa matokeo yaya haya: kuvamiwa Israeli na Waarabu, na toka jeshi la Kaskazini na maadui wengine, na kusababisha Mungu kuingilia kati kwa njia ya Kristo akiwa amerudi kusimamisha ufalme (k.m Ezekiel mlango wa 38-40; Dan. 11:40-45). Kusoma kwa kina unabii kama huu unafanya sehemu muhimu ya makuzi yetu kiroho haraka baada ya ubatizo. Zekaria 14:2-4 ni kati ya ulowazi sana: "Nitakusanya mataifa yote walete vita juu ya Yerusalemu, na huo mji utapigwa (linganisha Lk :21:24), nazo nyumba zitatekwa, nao wanawake watatendwa jeuri…… hapo ndipo atakapotokea BWANA, naye atapigana na mataifa hayo, kama vile alipopigana zamani siku ya vita (Yaani, kwa ajabu ataingilia kati mambo ya ulimwengu kama alivyowahi kufanya zamani ). Na siku hiyo miguu yake itasimama juu ya mlima wa Mizeituni, unaoelekea Yerusalemu upande wa Mashariki"

Uvamizi huu mkubwa kwa Israeli unaweza kutokea muda wote sasa, zana za vita zinaongezeka kwa kasi na matendo ya kisiasa. Sio dhana njema kuwaza kuwa tutangojea hadi uvamizi ndipo tuitikie Injili, tukikumbuka maneno ya Paulo: "wasemapo kuna amani na salama, ndipo uharibifu uwajiapo kwa ghafla…." (1 Thes 5:1-3). Kamwe hatutaweza kujua siku hasa atakaporudi Kristo, tunachojua tu ni kwamba siku imejumuishwa na uvamizi kwa Israeli toka Kasakzini, na ya kwamba uvamizi huu unaonekana kana kwamba utatokea mapema. Yawezekana utakuwepo uvamizi mwingine juu ya Israeli kabla ya huo ulionenwa kwenye unabii ambao tumeona; lakini wasomi wa Biblia wataendelea kuangalia kwa makini nafasi ya Israeli. Tunajua ya kwamba hatimaye Mungu ataingilia kwa njia ya Kristo miguu yake kusimama juu ya mlima wa Mizeituni. Ilikuwa toka mlima u huu ambao Kristo alipaa mbinguni, na kwa huo atarudi. "Huyu Yesu aliyechukuliwa kutoka kwenu kwenda juu mbinguni, atakuja jinsi iyo hiyo mlivyomuona akienda zake mbinguni", Malaika waliwaambia wanafunzi waliposimama juu ya mlima huo, wakikaza macho Bwana wao akipaa juu (Mdo 1:9-12).

Fahamu zetu inabidi tuziwianishe kwa jinsi Kristo alivyokaribia kurudi. Unabii kuhusu matukio ya ulimwengu karibu kurudi kwake umetolewa kwa upana ili kuimarisha imani ya hao ambao tayari wamejitia wenyewe katika Kristo kwa kubatizwa. Ingawa hivyo, ulinganifu dhahiri kati yao na hali ya ulimwengu uliopo ni hakika hauna budi kuwa zaidi kuliko kuvutia kwa hao ambao bado kuchukua hatua, na vile vile unabii utasaidia imani yetu katika Neno la Mungu la kutegemewa lenye kuvuviwa. Utii wetu haupaswi kusukumwa na akili ya uoga wa kuwa kuja kwa pili kumekaribia. Wale tu wapendao kweli "kufunuliwa kwake" (2 Tim 4:8) watapokea thawabu. Hata hivyo, ni nafasi yetu ya kuangalia upesi, tunaishi ukingoni kabisa mwa wakati na yatakayotokea kwa

wanadamu kama tujuavyo, kamwe isikome kukazwa kwetu kila siku ambayo tunaishi.

## MWISHONI MWA KITABU 4:- HAKI YA MUNGU

Kufundisha wanafunzi wa Biblia kumedhihirisha kuwa idadi ya maswali yanayohusiana mara nyingi hutokea wakati wa kusoma kukikamilika. Yote haya yanalenga karibu haki ya Mungu. Mifano ina:

Je! sio kweli kila mmoja anaitwa na Mungu aijue Injili.

Ni kwa sababu gani Mungu aliruhusu Adamu na Hawa kutenda dhambi, na hivyo kuleta masumbufu na shida katika maisha ya watoto wao mabilioni.

'Kwa nini Mungu alichagua Israeli tu kuwa watu wake katika Agano la Kale, kuliko kumpa kila mmoja nafasi?

Shida hizi zitatokea kwetu sisi sote,hatua iwayo yote kwenye uhusiano wetu na Mungu. Mambo haya kupata kuwa magumu kuyaelewa yenyewe isiwe sababu ya kuchelewa kuitikia mwito wa Mungu. Upande huu wa kundi la Kristo, hatutaweza kamwe kufikia cheo cha mwisho wa maarifa kuhusu hayo. Miaka elfu mbili iliyopita, mtu "alipaza sauti aksema kwa machozi, Bwana naamini nisaidie kutoamini kwangu" (Marko 9:24). Sote tuna utu huu uliogawanyika; nusu tunaamini, lakini upande mwingine umetiwa katika daraja ya "wasio na imani" wakihitaji mno msaada wa Bwana kunyamazisha. Katika masiku au juma kabla ya ubatizo, hili ni wazo linaloonekana kwa kawaida, na kwa kiwango kingine itatokea tena siku zetu zote.

'Kutoamini' kwetu mara nyingi kunachukua mfano wa aina ya mifano ya maswali kwa Mungu yaliorodheshwa hapo juu. Jambo la

msingi kwa macho ni kwmaba haidhaiwi ya kwamba tutamlaumu Mungu kuwa hana haki au si kweli. Kama tukifanya hivyo tunamhukumu Mwenyezi Mungu kwa maneno ya kuona kwetu. Tunasema ya kuwa kama tungekuwa ni Mungu, tungetenda kwa namna tofauti kwa jinsi gani Mungu anafanya. Ni moja ya makosa makubwa ya mwanadamu kutofahamu ni jinsi gani binadamu alivyojaa dhambi, na haki ya Mungu ya mwisho. Kama Mungu hayupo sawa mwisho, basi hakuna jambo la uadilifu linalopima ubora wa uwepo wote. Kwa hiyo hakuna dhana kweli ya sawa au kosa. Wazo zima la dini (kufungamana tena) na Mungu kwa hiyo halina maana. Kama watoto wanaweza kuwa na akili ya kuwafahamu watu wazima kwa upeo wao wa kuona na mfano wa kufikiri, ndivyo ilivyo mtu kwa Mungu. Yeremia alihoji njia ya Mungu, lakini katika juhudi kumfahamu kwa kina zaidi Mungu ndipo mwisho alikubali kuwa Mungu yupo sawa: “Wewe u mwenye haki, Ee BWANA, nitetapo nawe, lakini nitasema nawe katika habari ya haki (Yer 12:1; linganisha Zab 89:19,34,49,52).

Kidokezo cha kwamba Mungu hana haki kinatoa wazo la kwamba sisi tuna haki fulani, ambazo kwa njia isiyoeleweka Mungu anaharibu. Ukweli kwamba Mungu ndiye muumba wetu na ndiye mwenye kutufanya hai siku zote maana yake hatuna haki. Daima tunaishi katika huruma yake sio tu tunapokosa. ‘Haki za binadamu’ ni wazo la kibinadamu, limeundwa na wanadamu kwa kujihesabia haki mwenyewe. Tulikuja ulimwenguni bila kitu, na tutaondoka bila kitu. Yote tulionayo ni kipawa, tumepewa kwa kitambo kidodo kuona ni jinsi gani tutaitika. Ikiwa Mungu anatuita sisi kwenye uhusiano wa karibu naye, kwa furaha tuitikie. Kukataa kufanya hivyo kwa sababu wengine hawajaitwa kufanya hivi, ni kumhuzunisha Mungu katika moja ya njia ziwezazo kutia uchungu zaidi.

Kwa umbile sisi sote ni wanyama (Mhubiri 3:18-20). Tunaweza kusema, 'ni kwa sababu gani mwanadamu alichaguliwa kuwa na uhusiano na Mungu, kuliko mnyama mwingine yeyote?' Sababu hasa hatuwezi kufahamu hata kama tungeambiwa. Moja ya kweli na taarifa ya uumbaji katika kitabu cha Mwanzo. Maelezo ya kisayansi ya jinsi gani Mungu aliumba vitu vya kuonekana na kuratibu katika ajabu isiyo na kikomo ya ulimwengu ni nje ya uwezekano wa sayansi ya binadamu kufahamu. Kwa hiyo Mungu alieleza matendo yake ya uumbaji katika lugha ambayo mwenye hali kama mtoto aweza kukubali. Yayo hayo kwa uadilifu wa kuchagua katika mambo mawili ambayo tuliorodheshewa mwanzoni mwa maneno haya ya ziada mwishoni mwa kitabu. Kitabu hiki kimeeleza fundisho la Biblia kuhusu mambo haya. Kwa kawaida akili zetu hazinyenyekei katika neno la Mungu; tutakuwa na shida ya kufahamu na kukubali baadhi ya mambo katika njia ambayo Biblia inayaelezea. Lakini tunatakiwa kutambua ya kuwa tatizo ni letu, na sio Mungu. Kwa upana tunakosa maarifa binafsi yanayotakiwa kukubali kwamba kimsingi fikira zetu zina kasoro na makosa. Yatupasa tuelewe ukweli wa kwamba akili zetu tumeharibika mno zipotofauti na Mungu. Njia yetu ya kufikiri sio tu ni hatua kushuka chini toka kwa Mungu; kwa ukubwa ni wazo tofauti katika maendeleo na yake. Kwa sababu hii tumetakiwa kuwa na akili ya Kristo, kujifunza katika neno la Mungu kufahamu njia yake ya kufikiri, na kujaribu kufanya iwe yetu.

Sisi sote tutakiri kuwa kuna vitu vingi vya uumbaji wa Mungu ambavyo ni wazi ni vizuri sana; ni bayana kuna wazo lingine la haki linalotoka kwa muumba wetu, na liko wazi katika uumbaji wake. Tatizo ni, kuna mambo mengi tunayoyaona wanadamu ambayo mengine ni wazi maovu na yasiyofaa. Ni haya yanayosababisha machafuko mengine kama kuhoji haki ya Mungu. Kwa huzuni, wakati huo wengi wanaendelea kuionea shaka haki ya

Mungu, na hata ikiwa yupo. Lakini sio bora zaidi kusema kuwa tunaamini ukuu wa wema wa Mungu na haki, kama anavyodai katika neno lake, lakini tuna shida kufahamu mahali pa ubaya katika uumbaji wake?

“Mambo ya siri ni ya Bwana, Mungu wetu: lakini mambo yaliyofunuliwa ni yetu sisi” (Kum 29:29). Injili imeitwa “mambo ya Mungu yanayojulikana” (Rum 1:19), inadokeza kuna mengi mengine ambayo bado kujulikana. Kuna mambo ya kweli makuu ambayo ni wazi tunaweza kuona katika Neno la Mungu; pia kuna sifa nyingine za Mungu zinazoendelea . Lakini mengine yasiohesabika yapo “mambo ya siri” yanahusu njia za Mungu, ambazo hatuwezi kuzipita kwa kuzifikia katika maisha haya. Hivyo Paulo aliweza kusema kuwa katika maana moja alimjua Kristo na Mungu, kama tuwezavyo sisi (2 Tim 1:12; 2Kor 5:16; Gal 4:9; Ebra 10:30; 1Yoh 2:13), hasa kwa kuona wenyewe upendo wa Mungu na kuitikia (1 Yoh 4:7,8); ila kwa maana nyingine “alijua kwa sehemu” (1 Kor 13:9,12), kutamani kurudi Kristo, “ili (wakati huo) nimjue yeye, na uweza wa kufufuka kwake” (Flp 3:10).

Kama tunavyoogezeka kufunukiwa na haki ya Mungu kwa njia ya kujifunza neno lake, tutaongezeka kutamani kuwa Ufalme wake uje wakati hatimaye sifa zake zenye haki zitakuwa dhahiri, kwa mwili zitafunuliwa kwa namna ambayo watu wake wote kwa furaha watafahamu na kupenda.Kipindi hicho wataona ufumbuzi wa mwisho wa shida zote ambazo sasa zinawatesa watoto wa Mungu - kiakili, kwa mema na mabaya na kwa mwili. “Maana wakati wa sasa tunaona kwa kioo, kwa jinsi ya fumbo, wakati ule tutaona uso wa uso, wakati wa sasa nafahamu kwa sehemu; wakati ule nitajua sana kama nami ninavyojuliwa sana “ (1 Kor 13:12,13).